**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

# RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
4 Barabara ya Ukaguzi,
S.L. P 950,
41104 Tambukareli,
Dodoma.
Simu: 255(026)2161200,
Nukushi: 255(026)2117527,
Barua Pepe: ocag@nao.go.tz,
Tovuti: www.nao.go.tz

Machi 2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi,S.L. P 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: 255(026)2161200, Nukushi: 255(026)2117527, Barua Pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

**Kumb. No. CGA.319/421/01-A/6** **28 Machi 2021**

Mheshimiwa, Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
11400 Chamwino,
S. L. P. 1102,
40400 DODOMA

**YAH: KUWASILISHA RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI JUU YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020**

Kulingana na Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kadhaa), Kifungu Na. 34 (1) (c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 pamoja na Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009, ninawasilisha kwako ripoti yangu ya ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020.

Naomba kuwasilisha,

**Charles E. Kichere,**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**Mamlaka**

Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa mara kwa mara) na kufafanuliwa zaidi na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009.

**Dira ya Ofisi**

Kuwa Taasisi ya Hali ya Juu katika ukaguzi wa Sekta ya Umma.

**Dhamira**

Kutoa Huduma za Ukaguzi wa Sekta ya Umma Zenye ubora wa Hali ya Juu Zinazoimarisha Utendaji, Uwajibikaji na Uwazi Katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma.

**Misingi ya Maadili**

| | |
|---|---|
| Uadilifu | Sisi ni taasisi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo. |
| Ubora | Sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi. |
| Uaminifu | Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia Utawala wa sheria. |
| Kuwalenga Watu | Tunamakinikia zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi |
| Ubunifu | Tunamakinikia zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi. |
| Kujielekeza kwenye matokeo | Sisi ni taasisi inayojikita kwenye mafanikio kulingana na malengo tuliyojiwekea |
| Kufanya Kazi kwa Kushirikiana | Tunafanya kazi pamoja kama timu, kujadiliana kitaalamu na kubadilishana maarifa |

**YALIYOMO**

YALIYOMO.................................................................III

ORODHA YA MAJEDWALI .......................................................V

ORODHA YA VIELELEZO ...................................................... XII

ORODHA YA VIAMBATISHO.................................................. XIV

VIFUPISHO ................................................................ XVI

DIBAJI .................................................................XVIII

SHUKRANI ................................................................. XX

MUHTASARI ................................................................ XXI

SURA YA KWANZA...........................................................1

MAELEZO YA AWALI.......................................................1

SURA YA PILI...............................................................8

HATI ZA UKAGUZI .........................................................8

SURA YA TATU ............................................................ 16

UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA. 16

SURA YA NNE .............................................................. 24

UANDAAJI NA UTEKELEZWAJI WA BAJETI.................................. 24

SURA YA TANO ............................................................ 44

HESABU ZA TAIFA ........................................................ 44

SURA YA SITA.............................................................. 72

TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI NA UTAWALA BORA ...... 72

SURA YA SABA.............................................................. 93

UKAGUZI WA RASILIMALI WATU NA USIMAMIZI WA MISHAHARA........... 93

SURA YA NANE ............................................................110

UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI, MIFUKO MAALUMU YA FEDHA, BODI ZA MABONDE YA MAJI, HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA NA TAASISI NYINGINE.................................................................110

SURA YA TISA .......... 155
UNUNUZI NA USIMAMIZI WA MIKATABA .......... 155
SURA YA KUMI .......... 196
USIMAMIZI WA MATUMIZI .......... 196
SURA YA KUMI NA MOJA .......... 221
USIMAMIZI WA MALI NA MADENI .......... 221
SURA YA KUMI NA MBILI .......... 241
UKAGUZI WA VYAMA VYA SIASA .......... 241
SURA YA KUMI NA TATU .......... 252
KAGUZI MAALUMU .......... 252
VIAMBATISHO .......... 283

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Orodha ya Taasisi Zilizoandaa Taarifa za Fedha kwa Mara ya Kwanza kwa Mwaka 2019/20....................................................4

Jedwali Na. 2: Orodha ya Kaguzi Maalumu Zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/20........................................................................6

Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi ................................ 11

Jedwali Na. 4: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Miaka Mitatu Mfululizo13

Jedwali Na. 5: Baadhi ya Taasisi Ambazo Zina Mapungufu katika Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma.................................... 15

Jedwali Na. 6: Tafsiri ya Maneno Yaliyotumika katika Kutathmini Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo.................................................. 16

Jedwali Na. 7: Idadi ya Mapendekezo kwa kila Taasisi ...................... 17

Jedwali Na. 8: Mwenendo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Mitatu ........................................................................ 19

Jedwali Na. 9: Hali ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) katika Kutekeleza Mapendekezo yangu kwa Mwaka 2018/19 ...................................... 20

Jedwali Na. 10: Mwenendo wa Mlipaji Mkuu wa Serikali katika Kutekeleza Mapendekezo yangu kwa Kipindi cha Miaka Mitatu........................... 21

Jedwali Na. 11: Mwenendo wa Maagizo ya Kamati ya PAC kwa Kipindi cha Miaka Mitatu ........................................................................ 22

Jedwali Na. 12: Vyanzo vya Makusanyo na Asilimia za Kuchangia.......... 25

Jedwali Na. 13: Marejeo ya Bajeti ya Matumizi.............................. 27

Jedwali Na. 14: Mwenendo wa Makusanyo Ikilinganishwa na Makadirio... 28

Jedwali Na. 15: Usuluhishi wa Makusanyo ya Jumla na Makusanyo Yaliyotambuliwa Mfuko Mkuu wa Hazina....................................... 35

Jedwali Na. 16: Makusanyo na Malipo katika Mfuko Mkuu wa Hazina...... 35

Jedwali Na. 17: Mgawanyo wa Matumizi ikilinganishwa na Bajeti ......... 36

Jedwali Na. 18: Malipo ya Ukaguzi ambayo Hayakukusanywa na Wizara ya Afya katika Bandari ya Dar es Salaam Kitengo cha Afya .................... 40

Jedwali Na. 19: Bakaa ya Fedha zilizo katika Akaunti ya Fedha za Mali Zilizotaifishwa na Kurejeshwa Serikalini ........................................ 41

Jedwali Na. 20: Fedha zilizokaa Muda Mrefu katika Akaunti ya Amana bila kurejeshwa Mfuko Mkuu ........................................................ 42

Jedwali Na. 21: Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Iliyopita kwenye Makusanyo ya Mapato................................. 45

Jedwali Na. 22: Ukusanyaji wa Mapato kwa Idara (Tanzania Bara na Zanzibari)................................................................................. 46

Jedwali Na. 23: Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka 2015/16 hadi 2019/20......... 48

Jedwali Na. 24: Ulinganifu wa Uwiano wa Kodi Dhidi ya Pato la Ndani kwa Nchi za Afrika Mashariki ....................................................... 48

Jedwali Na. 25: Kesi zilizokuwapo katika Mamlaka za Rufaa za Kodi hadi tarehe 30 Juni 2020 .......................................................... 49

Jedwali Na. 26: Mwenendo wa Deni la Ndani kwa Miaka Mitatu (Deni Halisi) ....................................................................................... 56

Jedwali Na. 27: Mwenendo wa Ukopaji wa Ndani kwa Miaka Mitatu (Thamani halisi) .............................................................. 57

Jedwali Na. 28: Mwenendo wa Deni la Nje kwa Miaka Mitatu .............. 57

Jedwali Na. 29: Mwenendo wa Ukopaji wa Nje kwa Miaka Mitatu ......... 58

Jedwali Na. 30: Mafao Yaliyokokotolewa Kimakosa .......................... 62

Jedwali Na. 31: Majalada Yaliyocheleweshwa Kuandaliwa na Kuwasilishwa kwa Ukaguzi wa Awali ....................................................... 63

Jedwali Na. 32: Kutoondolewa kwa Miamala ya Amana za Kudumu Inayohusiana na Taasisi za Serikali ............................................ 67

Jedwali Na. 33: Kutokuwepo kwa Usuluhishi wa Mali za Kudumu Zilizonunuliwa na Kuripotiwa kwenye Mtiririko wa Fedha Chini ya Shughuli za Uwekezaji Dhidi ya Ongezeko la Kifedha Sh.Bilioni 635.9 ............... 70

Jedwali Na. 34: Tathmini ya Ubadhirifu ....................................... 74

Jedwali Na. 35: Rekodi za Kiasi kilichowekwa na kutolewa na Mtunza Fedha.................................................................................. 76

Jedwali Na. 36: Kushindwa Kuwatangaza Wataalamu kwenye Gazeti la Serikali ........ 80

Jedwali Na. 37: Ukosefu wa Miongozo ya uandaaji wa Taarifa za Fedha . 81

Jedwali Na. 38: Mapungufu Yaliyojitokeza wakati wa Kuiendesha Akaunti ya Benki ya Masufuru ........ 82

Jedwali Na. 39: Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani ........ 84

Jedwali Na. 40: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi ........ 85

Jedwali Na. 41: Tathmini katika Usimamizi wa Vihatarishi ........ 87

Jedwali Na. 42: Kulinganisha Tathmini ya mazingira ya Habari na Teknolojia ya Mawasiliano (TEHAMA) ........ 89

Jedwali Na. 43: Hakuna Usuluhisho wa mapato yanayokusanywa na kuripotiwa kwenye Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT-HOMIS) na mfumo wa malipo ya serikali (GePG) ........ 91

Jedwali Na. 44: Upungufu wa Watumishi katika Taasisi za Serikali. ........ 95

Jedwali Na. 45: Makato yaliyocheleweshwa kuwasilishwa na Taasisi. ..... 97

Jedwali Na. 46: Fedha kwa Ajili ya Makato Zilizocheleweshwa Kutumwa 98

Jedwali Na. 47: Mishahara ambayo Haijarejeshwa ........ 101

Jedwali Na. 48: Malipo ya Mishahara kwa Watumishi Waliokoma Utumishi wa Umma ........ 102

Jedwali Na. 49: Taasisi zenye Watumishi Wanaokaimu Zaidi ya Miezi Sita ........ 103

Jedwali Na. 50: Taasisi ambazo Hazikupima Utendaji wa Watumishi .... 104

Jedwali Na. 51: Orodha ya Taasisi zenye Watumishi wenye Makato Makubwa ........ 105

Jedwali Na. 52: Malipo ya Kukaimu bila Idhini ........ 106

Jedwali Na. 53: Malipo kwa Watumishi wasiokuwa na Mikataba ........ 107

Jedwali Na. 54: Taasisi ambazo Hazikuandaa Mpango wa Mafunzo ....... 108

Jedwali Na. 55: Uthibitishaji wa Tiketi za Abiria Nje ya Mfumo ........ 116

Jedwali Na. 56: Mikataba Aliyopatiwa Mzabuni Ambaye Hajakidhi Vigezo ........ 122

Jedwali Na. 57: Miradi Iliyotelekezwa........................................ 123

Jedwali Na. 58: Gharama za Usambazaji wa Mahindi Ambazo Hazijalipwa na Waziri Mkuu............................................................ 126

Jedwali Na. 59: Malimbikizo Yasiyolipwa ya Ada za Uchunguzi wa Kimaabara ............................................................ 127

Jedwali Na. 60: Malipo Yaliyochelewa Kulipwa ya Wakandarasi, Washauri na Wasambazaji ............................................................ 128

Jedwali Na. 61: Wakala ambao Fedha Zao Zimetaifishwa na TRA ........ 129

Jedwali Na. 62: Wakala Ambao Zinatekeleza Miradi Bila ya Dhamana ... 131

Jedwali Na. 63: Wakala wenye Makusanyo ya Mapato ya Nndani Yasiyoridhisha............................................................ 132

Jedwali Na. 64: Malipo yaliyofanywa kwa walengwa ambayo hayajathibitishwa ............................................................ 140

Jedwali Na. 65: Gharama Iliyoingiwa na TWPF kwa Uwekezaji Ambao Haujaendelezwa............................................................ 142

Jedwali Na. 66: Majimbo yenye Kiasi Kikubwa ambacho Hakijatumika .. 143

Jedwali Na. 67: Fedha za CDCF Zilizotumika kwa Nje ya Kusudio ........ 144

Jedwali Na. 68: Fedha zilizokopwa na Wizara .............................. 145

Jedwali Na. 69: Ucheleweshaji wa Ujenzi wa Majengo ya Hospitali...... 147

Jedwali Na. 70: Malipo Yenye Shaka.......................................... 151

Jedwali Na. 71: Taasisi zenye Malipo yenye Nyaraka Pungufu............. 153

Jedwali Na. 72: Taasisi Zilizofanya Malipo Nje ya Bajeti ................... 154

Jedwali Na. 73: Taasisi Zilizofanya Ununuzi Nje ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka............................................................ 158

Jedwali Na. 74: Ununuzi Uliofanyika Bila Ushindanishi ..................... 160

Jedwali Na. 75: Vifaa Vilivyonunuliwa bila Kufanyiwa Ukaguzi............ 162

Jedwali Na. 76: Orodha ya Taasisi Zilizonunua Vifaa na Mafuta Bila Kuingizia kwenye Rejista za Stoo ............................................ 164

Jedwali Na. 77: Ununuzi Uliofanyika Bila ya Kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni............................................................ 165

Jedwali Na. 78: Vifaa na Mali Zilizolipiwa Lakini Hazikupokelewa........ 167

Jedwali Na. 79: Wilaya zilizofanyiwa Ukaguzi wa Kina wa Usimamizi wa Mikataba ........................................................................ 171

Jedwali Na. 80: Mikataba yenye Hati za Dhamana na Malipo ya Awali yenye Mapungufu ........................................................................ 173

Jedwali Na. 81: Mikataba Iliyotekelezwa Bila Dhamana za Utendaji ..... 174

Jedwali Na. 82: Mikataba ambayo Dhamana Zake za Utendaji zina Mapungufu ........................................................................ 175

Jedwali Na. 83: Mikataba Iliyotekelezwa Bila Kuwekewa Bima ........... 178

Jedwali Na. 84: Kazi Zilizotekelezwa na Kulipwa Bila Kuthibitishwa ..... 180

Jedwali Na. 85: Mikataba yenye Ununuzi na Tofauti Zisizoidhinishwa na Bodi ya Zabuni ........................................................................ 182

Jedwali Na. 86: Mikataba ambayo Malipo Yalichelewa Kufanyika au Kutolipwa Kabisa ........................................................................ 184

Jedwali Na. 87: Miradi Iliyochelewa Kutekelezwa na Kukamilika ......... 186

Jedwali Na. 88: Miradi Iliyotelekezwa na Wakandarasi kwa Zaidi ya Miezi Sita ........................................................................ 191

Jedwali Na. 89: Mikataba ambayo Haikutozwa Fidia ya Ucheleweshaji Miradi ........................................................................ 192

Jedwali Na. 90: Mikataba iliyositishwa na kurekebishwa bila kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ................................................ 194

Jedwali Na. 91: Mikoa ambayo Halmashauri Hazijarejesha Fedha Tume ya Taifa ya Uchaguzi ........................................................................ 197

Jedwali Na. 92: Malipo Yasiyo na Tija ........................................ 198

Jedwali Na. 93: Hati za Malipo Ambazo Hazikuwasilishwa Wakati wa Ukaguzi ........................................................................ 199

Jedwali Na. 94: Malipo yenye Nyaraka Pungufu kwa Miaka Mitano ....... 199

Jedwali Na. 95: Matumizi Nje ya Bajeti........................................ 202

Jedwali Na. 96: Matumizi Yaliyofanywa Nje ya Bajeti kwa Miaka Mitano 202

Jedwali Na. 97: Malipo yenye Mapungufu .................................... 203
Jedwali Na. 98: Malipo Yaliyofanywa kwenye Vifungu Visivyohusika ..... 204
Jedwali Na. 99: Taasisi Zilizofanya Malipo bila kudai Risiti za Kielekitroniki ........................................................................ 206
Jedwali Na. 100: Orodha ya Taasisi ambazo Hazikukata Kodi ya Zuio .... 208
Jedwali Na. 101: Mtiririko wa Mabadiliko Kiasilimia kwa miaka mitano . 208
Jedwali Na. 102: Masurufu ambayo Hayajarejeshwa ........................ 209
Jedwali Na. 103: Taasisi ambazo Masurufu Yalichelewa Kurejeshwa ..... 210
Jedwali Na. 104: Mtiririko wa Masurufu Yasiyorejeshwa kwa miaka mitano ........................................................................ 210
Jedwali Na. 105: Taasisi zenye Dosari kwenye Kuidhinisha Malipo ....... 211
Jedwali Na. 106: Halmashauri Zilizobadili Matumizi ya Fedha za Uchaguzi ........................................................................ 212
Jedwali Na. 107: Taasisi Zilizofanya Malipo yenye Nyaraka Pungufu ..... 214
Jedwali Na. 108: Hati za Malipo ambazo Hazikuwasilishwa ................ 215
Jedwali Na. 109: Taasisi zilizofanya Malipo Nje ya Bajeti .................. 216
Jedwali Na. 110: Taasisi zilizofanya Malipo bila Kudai Risiti za Kielekitroniki ............................................................. 217
Jedwali Na. 111: Halmashauri Ambazo zina Masurufu Yasiyorejeshwa ... 218
Jedwali Na. 112: Halmashauri Zilizofanya Ununuzi kwa Kutumia Masurufu Sh 149,944,500 ............................................................ 219
Jedwali Na. 113: Orodha ya Taasisi zenye Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika ....................................................... 223
Jedwali Na. 114: Orodha ya Taasisi Zisizo na nNyaraka za Umiliki wa Ardhi ........................................................................ 227
Jedwali Na. 115: Orodha ya Taasisi zisizo na Mpango wa ukarabati na utunzaji wa kumbukumbu. ................................................. 230
Jedwali Na. 116: Orodha ya taasisi zenye mali zisizo na namba ya utambulisho ............................................................. 231

Jedwali Na. 117: Orodha ya Taasisi Zisizofanya Tathimi ya Mali na Muda wa Matumizi .......... 233

Jedwali Na. 118: Orodha ya Taasisi Zilizonunua Mali na Kujenga Majengo Bila Kutumika. .......... 234

Jedwali Na. 119: Orodha ya Taasisi zenye Kesi Mahakamani .......... 236

Jedwali Na. 120: Muelekeo wa madeni ya Hospitali za India .......... 239

Jedwali Na. 121: Matumizi ya Vyama vya Siasa .......... 245

Jedwali Na. 122: Orodha ya Vyama vya Siasa Vilivyochelewa Kuwasilisha Taarifa za Fedha .......... 246

Jedwali Na. 123: Orodha ya vyama vya siasa vilivyoandaa taarifa za fedha bila ya kufuata mfumo wa IPSAS .......... 247

Jedwali Na. 124: Kiasi cha fedha ambacho hakijawekwa benki na vyama vinane vya Siasa .......... 248

Jedwali Na. 125: Orodha ya Kaguzi Maalumu .......... 252

Jedwali Na. 126: Orodha ya Kaguzi Maalumu Zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/20 .......... 253

## ORODHA YA VIELELEZO


Kielelezo Na. 1: Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita kwa Taasisi za Serikali Kuu .......... 18

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Jumla ya Mapendekezo kwa Miaka Mitatu Mfululizo .......... 19

Kielelezo Na. 3: Hali ilivyo ya Utekelezaji wa Maagizo ya PAC kwa Mwaka 2018/19 .......... 22

Kielelezo Na. 4: Mgawanyo wa Makadirio ya Matumizi kwa asilimia ...... 26

Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Makadirio na Makusanyo kwa Miaka Mitano (Kiasi katika Sh. bilioni) .......... 29

Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa ufadhili wa kibajeti kwa kipindi cha ..... 30

Kielelezo Na. 7: Uwiano wa Bajeti na Makusanyo ya kila chanzo.......... 33

Kielelezo Na. 8: Makadirio, Fedha Zilizotolewa na Matumizi Halisi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa kipindi cha Miaka Mitano (Kiasi katika Sh. billioni) .......... 37

Kielelezo Na. 9: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi ya Fedha za maendeleo kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh. billioni) .......... 39

Kielelezo Na. 10: Ulinganifu wa uchangiaji wa makusanyo halisi kwa Idara 2019/20 na 2018/19.......... 47

Kielelezo Na. 11: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali kwa Miaka Mitatu .......... 56

Kielelezo Na. 12: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi .......... 86

Kielelezo Na. 13: Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi .......... 87

Kielelezo Na. 14: Tathmini ya Mwenendo wa Mifumo ya TEHAMA......... 89

Kielelezo Na. 15: Uchambuzi wa ajira zilizopangwa, zilizoombwa na zilizotolewa na Serikali .......... 95

Kielelezo Na. 16: Mtiririko wa Malipo Yaliyofanywa kwenye Vifungu Visivyohusika .......... 205

Kielelezo Na. 17: Mtiririko wa Malipo Yasiyokuwa na Risiti za Kielekitroniki .......... 207

Kielelezo Na. 18: Mwenendo wa Mali zisizotumika kwa Muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa. ........................................ 226

Kielelezo Na. 19: Uwiano wa Mapato Yasiyolipwa ........................ 235

Kielelezo Na. 20: Mwenendo wa Madeni Tarajiwa ........................ 236

Kielelezo Na. 21: Uwiano wa Matumizi Yasiyolipwa ...................... 238

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Orodha ya Hati za Ukaguzi Zilizotolewa ............... 283

Kiambatisho Na. II: Taasisi Zilizopata Hati Zenye Shaka.................... 305

Kiambatisho Na. III: Taasisi Zilizopata Hati Mbaya .......................... 311

Kiambatisho Na. IV: Taasisi ambazo Hazikupata Maoni ..................... 313

Kiambatisho Na. V: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mwaka Uliopita ........................................................................................ 316

Kiambatisho Na. VI: Hali ya Utekelezwaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Maalum ya kwa Miaka Mitatu ................................................... 396

Kiambatisho Na. VII: Makadirio, Fedha Zilizotolewa na Matumizi Halisi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa kipindi cha Miaka Mitano............. 417

Kiambatisho Na. VIII: Makadirio, Fedha Zilizotolewa na Matumizi ya Fedha za Maendeleo kwa Miaka Mitano ............................................... 423

Kiambatisho Na. IX: Tarakimu ambazo Hazijathibitishwa Kuondolewa Zinazohusiana na Madai ya Kawaida, Madai ya Mikopo na Malipo kati ya Taasisi za Serikali.......................................................... 428

Kiambatisho Na. X: Taarifa ambazo Hazikupatanishwa katika Shughuli za Uendeshaji kwenye Taarifa ya Mzunguko wa Fedha......................... 434

Kiambatisho Na. XI: Taasisi zenye Upungufu kwenye Ukaguzi wa Ndani . 437

Kiambatisho Na. XII: Taasisi Zenye Mapungufu ya Kamati ya Ukaguzi .... 439

Kiambatisho Na. XIII: Tathmini ya Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi . 441

Kiambatisho Na. XIV: Tathmini ya Mifumo ya TEHAMA...................... 442

Kiambatisho Na. XV: Upungufu wa Watumishi wa Umma................... 445

Kiambatisho Na. XVI: Madai ya Watumishi wa Umma ambayo Hayajalipwa kwa Muda Mrefu .......................................................... 447

Kiambatisho Na. XVII: Watumishi Wanaokaimu Zaidi ya Miezi Sita........ 451

Kiambatisho Na. XVIII: Mapungufu Yaliyobainika kwenye Hospitali za Rufaa na Maalumu ............................................................ 453

Kiambatisho Na. XIX: Kuchelewa Kukamilika kwa Kazi za Ujenzi, Ununuzi wa Bidhaa na Utoaji wa Huduma............................................. 454

Kiambatisho Na. XX: Halmashauri ambazo Hazikurejesha Fedha Tume ya Taifa ya Uchaguzi ........................................................... 456

Kiambatisho Na. XXI: Taasisi Zilizofanya Malipo bila Kuwa na Nyaraka Stahiki na Toshelezi ........................................................... 459

Kiambatisho Na. XXII: Orodha ya Taasisi zenye Mali ambazo Hazitumiki kwa Muda Mrefu bila Kufanyiwa Matengenezo au Kuuzwa. ...................... 460

Kiambatisho Na. XXIII: Orodha ya Taasisi zenye Mali za Serikali Zilizotelekezwa, majengo Yaliyochakaa, Yasiyomaliziwa Kujengwa, Viwanja visivyoendelezwa kwa Muda Mrefu na Ujenzi wa Kasi Ndogo.... 462

Kiambatisho Na. XXIV: Orodha ya Taasisi zenye Mapato Yasiyopokelewa 464

Kiambatisho Na. XXV: Orodha ya Taasisi zenye Matumizi Yasiyolipwa ... 466

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AAFP | Alliance for African Farmers Party |
| ACT -Wazalendo | Alliance for Change and Transparency |
| ADA (TADEA) | African Democratic Alliance Party |
| ADC | Alliance for Democratic Change |
| ATCL | Shirika la Ndege Tanzania |
| BRELA | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| CBCTC | Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Jamii |
| CCK | Chama Cha Kijamii |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CDA | Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma |
| CHADEMA | Chama Cha Demokrasia na Maendeleo |
| CHAUMMA | Chama Cha Ukombozi wa Umma |
| CIMS | Mfumo wa Kusimamia Vifaa vya ofisi |
| CRDB | Benki ya CRDB |
| CRS | Mfumo wa Usajili wa Kiraia |
| CWT | Chama cha Walimu Tanzania |
| DFP | Miradi ya Wafadhili |
| EFD | Kifaa cha malipo ya fedha cha kielektroniki |
| eGA | Mamlaka ya Serikali Mtandao |
| EISA | Athari za Mazingira na Tathmini ya Jamii |
| FRP | Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi |
| GCC | Masharti ya Jumla ya Mkataba |
| GePG | Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato |
| GN | Tangazo la Serikali |
| ICT | TEHAMA |
| IFMS | Mfumo wa kusimamia fedha |
| IPSAS | Uandaaji wa Hesabu za Sekta ya Umma Kwa Viwango vya Kimataifa |
| MDAs | Wizara, Idara na Wakala |
| MOHCDGEC | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto |
| MSD | Bohari Kuu ya Dawa |
| Na. | Namba |
| NCCR-Mageuzi | National Convention for Construction and Reform |
| NHIF | Mfuko wa Bima ya Afya |
| NIDA | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa |
| NLD | National League for Democracy |
| NRA | National Reconstruction Alliance |
| OR -TAMISEMI | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PAC | Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali |
| PFA | Sheria ya Fedha za Umma |

| | |
|---|---|
| PFR | Kanuni za Uzimamizi wa Fedha za Umma |
| PMG | Mlipaji mkuu wa Serikali |
| POS | Mashine ya Mauzo |
| PPA | Sheria ya Ununuzi wa Umma |
| PPR | Kanuni za Ununuzi wa Umma |
| PURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli |
| RF | Mfuko wa Barabara |
| RITA | Wakala wa Usajili,Ufilisi na Udhamini |
| RRH | Hospitali za Rufaa za Mikoa |
| RUWASA | Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini |
| SAU | Sauti ya Umma |
| Sh. | Shilingi |
| STK na STL | Serikali ya Tanzania |
| TAA | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege |
| TAGLA | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TANePS | Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki Serikalini |
| TANROADS | Wakala wa Barababra Tanzania |
| TARURA | Wakala wa Barabara Vijijini |
| TEMESA | Wakala wa Ufundi na Umeme |
| TGFA | Wakala wa ndege za Serikali |
| TLP | Tanzania Labour Party |
| TPDF | Jeshi la Wananchi wa Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| UDP | United Democratic Party |
| UMD | Union for Multiparty Democracy |
| UNESCO | Tume ya Taifa katika Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni |
| UPDP | United Peoples Democratic Party |
| UWT | Umoja wa Wanawake |
| VAT | Kodi ya ongezeko la thamani |
| WMA | Wakala wa Vipimo |

**DIBAJI**



Kwa heshima kubwa ninayo furaha kuwasilisha Ripoti Kuu ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha ya Serikali Kuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka ulioshia Juni 30,2020.Hii ni kwa Mujibu wa Matakwa ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka, 1977(iliyorekebishwa).

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Bunge kuhusiana na usimamizi wa Fedha za Umma ili kuleta uwajibikaji na uwazi katika sekta ya Umma.

Nimefanya ukaguzi katika Taasisi nyingi za serikali Kuu ikijumuisha; Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mifuko Maalumu ya fedha, Mabonde ya Maji, Vyama vya Siasa, pamoja na Taasisi nyingine za Serikali. Hata hivyo, sikuweza kufanya ukaguzi katika ofisi 43 za balozi za Tanzania zilizopo nje ya Nchi kutokana na vizuizi vya usafiri vilivyowekwa ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID 19).

Ripoti hii imejumuisha Masuala muhimu yaliyobainika kupitia ukaguzi niliofanya katika Taasisi 263 za Serikali Kuu katika maeneo ya mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu na michakato ya ununuzi, utayarishaji wa taarifa za fedha na nyaraka zilizoambatishwa, pia uzingatiaji wa Sheria na Kanuni zilizowekwa. Aidha, nimeonesha matokeo ya ukaguzi maalumu uliofanywa kipindi cha Mwaka wa fedha 2019/20 na hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka ya nyuma na utekelezwaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Nilifanya Ukaguzi huu kwa kuzingatia Viwango kubalifu vya kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) ambazo zinahusu ukaguzi wa Sekta za Umma. Nimetoa Hati za Ukaguzi kwa kuzingatia Taarifa za Fedha nilizokagua na kuzitolea ripoti ya ukaguzi kwa kila taasisi ambayo ilikaguliwa. Pia, nilitoa barua za ukaguzi zinazoonesha Mapungufu yaliyobainika kwa kila taasisi iliyokaguliwa na mapendekezo ya

kutekeleza ili kuboresha na kuondoa mapungufu kama hayo siku za mbeleni.

Nimefanikiwa kufanya tathmini huru juu ya jinsi rasilimali za umma zinavyosimamiwa kwa uwajibikaji na kwa ufanisi kufikia matokeo yaliyokusudiwa, kwa kufanya hivyo, Serikali inaweza kufikia uwajibikaji na uadilifu, kuboresha utendaji, na kukuza imani kwa wananchi na wadau wengine.

**Charles E Kichere**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

## SHUKRANI

Kwa niaba ya ofisi yangu, ninapenda kutambua na kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suhulu Hassan kwa kuendelea kuamini ofisi yangu.

Aidha, ninaongeza shukrani zangu kwa ushirikiano mzuri unaoendelea kati ya ofisi yangu, Bunge na Kamati za Usimamizi wa fedha za Bunge hususan Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC) kwa kuendelea kuzifanyia kazi ripoti ninazozitoa pamoja na kuhakikisha Serikali inatekeleza Mapendekezo yaliyopo kwenye ripoti hizo.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuendelea kushirikiana na kutenga rasilimali kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Ninawashukuru pia washirika wa maendeleo kwa juhudi na rasilimali zao wanazoelekeza katika uboreshaji wa ofisi hii ili kuniwezesha kutimiza wajibu wangu.

Zaidi, natambua na kuheshimu michango ya Taasisi zote za serikali Kuu na umma kwa jumla katika kuniwezesha kwa namna moja au nyingine kuandaa ripoti hii. Vile vile, ninatambua ushirikiano unaotolewa na wale waliopewa dhamana ya usimamizi wa Taasisi nilizokagua katika kuhakikisha kuwa ninatekeleza majukumu yangu vizuri na mwishowe kuweza kutoa ripoti hii.

Mwisho, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kujitolea kwao na kuhakikisha kuwa ninatimiza jukumu hili la Kikatiba. Ninawasihi waendelee kudumisha nia hii katika kuweka juhudi zote pamoja ili tuendelee kutoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu ambazo zinaboresha utendaji wa sekta ya umma, uwajibikaji, na uwazi katika kusimamia rasilimali za umma.

Ninashukuru kwa dhati,

**Charles E. Kichere**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

## MUHTASARI

Ripoti ya jumla inatoa matokeo ya ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 ambayo yanahusu Wizara na Idara za Serikali 66, Wakala wa Serikali 34, Mifuko Maalumu 14, taasisi nyingine 53, vyama vya Siasa 19, Sekretarieti za Mikoa 26, Bodi za Mabonde ya Maji 15, Hospitali za Rufaa na hospitali maalum 32. Inajumuisha pia ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Akaunti za Mfuko Mkuu, ukaguzi wa awali wa mafaili ya mafao ya wastaafu na kaguzi maalumu 14. Ukaguzi wa Balozi 43 haukufanyika kwa sababu ya Janga la COVID- 19.

**Hati za Ukaguzi**

Kwa jumla, nimebaini Taasisi zilizokaguliwa zimeonesha utendaji mzuri kutokana na kuongezeka kwa Taasisi zilizopewa hati zinazoridhisha kutoka 218 hadi 239, ikiashiria ongezeko la Taasisi 21 (10%). Aidha, Hati zenye kasoro (modified opinions) zimepungua kutoka Taasisi 35 mwaka 2018/19 hadi Taasisi 21 mwaka 2019/20, ambayo inaashiria kupungua kwa Taasisi 14 (40%).

Kati ya vyama 19 vya siasa vilivyokaguliwa, ni vyama vinne tu vya siasa vilivyoweza kuandaa Taarifa za fedha kwa kufuata mfumo wa kimataifa wa uandaaji Taarifa za fedha za Umma (IPSAS) na kupata hati zinazoridhisha. Vvyama vinne vilipata hati mbaya (Adverse Opinions) na nilishindwa kutoa maoni (Disclaimer of Opinions) kwa vyama tisa kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, vyama viwili vilivyokaguliwa havikuandaa hesabu. Maelezo zaidi yametolewa katika sura ya pili ya ripoti hii.

**Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita**

Kwenye sura hii, nimewasilisha hali ya utekelezaji wa mpango kazi ulioandaliwa na Serikali kupitia Maafisa Masuuli juu ya mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa Wizara, Idara, Wakala, Tawala za Mikoa, Mifuko Maalumu na Taasisi mbalimbali. Pia, nimezingatia majibu ya Serikali yaliyotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) na utekelezaji wa Maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), ili kuboresha na kuimarisha usimamizi na udhibiti wa fedha za umma.

Kwa mwaka 2018/19, jumla ya mapendekezo 5,892 yakijumuishwa na maagizo ya PAC, yalitolewa kwenda kwa Maafisa Masuuli na Ofisi ya PMG. Kati ya mapendekezo hayo, mapendekezo 5,483 yalitolewa kwa Maafisa Masuuli kupitia Barua za Mapungufu kwa Menejimenti za mwaka 2018/19,

Mapendekezo 135 yalitolewa kwa PMG kupitia Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha iliyotolewa Machi 2020, mapendekezo 15 yalihusu Taarifa za ukaguzi maalumu zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2018/19, na mapendekezo 259 yaliyobaki yalitolewa kama Maagizo ya PAC kwa Maafisa Masuuli husika.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo hapo juu inaonesha kuwa, Mapendekezo 1,638 (sawa na asilimia 28) yametekelezwa kikamilifu, Mapendekezo 2,197 (sawa na asilimia 37) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, Mapendekezo 1,279 (sawa na asilimia 21) hayajatekelezwa, Mapendekezo 508 (sawa na asilimia 9) yamerudiwa, na Mapendekezo 270 (sawa na asilimia 5) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati. Aidha, katika uchambuzi wangu wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo, nimebaini kuwa Serikali imefanya jitihada katika kutekeleza mapendekezo, ingawa bado idadi kubwa ya mapendekezo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mapendekezo**
Natambua juhudi za Serikali kupitia Maafisa Masuuli na Ofisi ya PMG kwa kutekeleza asilimia 28 ya mapendekezo yangu na maagizo yaliyotolewa na PAC. Pamoja na juhudi hizo, ninapendekeza Serikali kuongeza jitihada za makusudi ili kukamilisha mapendekezo yaliyosalia ambayo ni sawa na asilimia 72 ya mapendekezo yote. Hii itasaidia kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani itakayosaidia kuepusha kujirudia kwa hoja za ukaguzi pamoja na kuzingatia umuhimu wa uwajibikaji na utawala bora.

**Uandaaji na Utekelezwaji wa Bajeti**
Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali ilikadiria kukusanya mapato ya Sh. Bilioni 33,105.41. Hata hivyo, jumla ya kiasi cha Sh. Bilioni 31,519.49 (95%) kilikusanywa, hivyo kiasi cha Sh. Bilioni 1,585.92 (5%) hakikukusanywa. Ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2018/19 (Bilioni 25,817.45), kumekuwa na ongezeko la Sh. Bilioni 5,702.04 (22.09%). Jumla ya mapato yaliyokusanywa yanajumuisha Sh. Bilioni 20,514.52 (65%) zinazotokana na vyanzo vya ndani na Sh.Bilioni 11,004.97 (35%) zilizotokana na misaada ya wahisani na mikopo ya nje na ndani.

Aidha, nilibaini kuendelea kuwapo kwa makusanyo yasiyohesabiwa Mfuko Mkuu. Hii ni pamoja na Makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Sh. bilioni 132.08 na Sh. Bilioni 2,025.67 zilizopelekwa moja kwa moja kwenye

miradi ya Maendeleo. Hali hii inasababishwa na kutotambuliwa kwa makusanyo na matumizi yasiyo taslimu (Dummy transaction) katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2019/20 Makusanyo yaliyopokelewa katika Mfuko Mkuu wa Serikali yalikuwa Sh. Bilioni 29,348.90. Serikali ilitoa kiasi cha Sh. Bilioni 28,416.89 kwenye Mfuko Mkuu kwa ajili ya matumizi ya Serikali, ikijumuisha Sh. Bilioni 19.87 zilizozuiliwa. Mgawanyo wa Fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya Serikali ulikuwa: Sh. bilioni 3,198.93 (11.26%) kwa matumizi ya mengineyo, Sh. Bilioni 7,289.66 (25.65%) kwa ajili ya Mishahara, Sh. bilioni 9,718.52 (34.20%) kulipa Deni la Taifa na huduma za jumla wakati Sh bilioni 8,189.9 (28.82%) zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo.

Kwa upande wa makusanyo, nilibaini ukiukwaji wa Sheria na Miongozo inayohusiana na usimamizi wa Makusanyo. Hii inajumuisha: Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliyokusanya mapato yasiyotokana na Kodi ya Sh. bilioni 1.236 Nje ya Mfumo (GePG), Wizara ya Afya kupitia kitengo cha Afya Bandari ya Dar es Salaam kushindwa kukusanya ada ya Ukaguzi wa vyombo na mashua za kimataifa pamoja na majahazi ya kitaifa Sh. bilioni 0.201, Sh. bilioni 1.609 zilizokaa kwa zaidi ya miaka mitano katika Akaunti za Amana bila kurudishwa mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na fedha zilizokaa muda mrefu bila kutumika katika Akaunti za fedha za mali zilizotaifishwa na kurejeshwa Serikalini (Forfeiture, Recovery Account and Plea Bargain) kupitia Mkurugenzi wa Mashitaka Sh bilioni 51.522 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020. Hali hii inasababishwa na kukosekana kwa sheria elekezi na udhibiti unaosimamia mgawanyo na matumizi ya fedha hizo.

**Mapendekezo**

Ninaishauri Serikali kutafiti vyanzo vipya vya mapato na kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari ili kuhakikisha makusanyo yanaendana na matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, taarifa za makusanyo na matumizi zinapaswa kufanyiwa usuluhisho kwa wakati, kuhesabiwa na kutotumika kabla ya kuwasilisha taarifa Mfuko Mkuu wa Serikali. Sheria na kanuni zinapaswa kutungwa ili kudhibiti matumizi ya makusanyo katika akaunti ya fedha za mali zilizotaifishwa na kurejeshwa Serikalini.

Maelezo ya Hoja na mapendekezo yamefafanuliwa zaidi katika Sura ya Nne.

**Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato**

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya Sh. trilioni 17.92 dhidi ya makisio yaliyowekwa ya Sh. trilioni 19.41. Hali

hii inaakisi upungufu wa makusanyo kwa Sh. trilioni 1.48, sawa na asilimia nane ya jumla ya makisio ya makusanyo. Taarifa ya jumla ya makusanyo haikujumuisha Sh. bilioni 9.02 ambayo ni vocha za misamaha ya kodi kutoka serikalini. Hivyo, makusanyo halisi ya mapato kwa mwaka wa fedha 2019/20 yakijumuisha vocha za misamaha kutoka serikalini ni Sh. trilioni 17.93.

**Kodi Zilizoshikiliwa na Kesi Zilizopo katika Mamlaka za Rufaa za Kodi**
Ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2019/20 umebaini kuwa Mamlaka ya Mapato ilikuwa na kesi 1,097 zenye thamani ya Sh. trilioni 360.08 na Dola za Marekani milioni 181.43 (sawa na jumla ya Sh. trilioni 360.49). Fedha hizi zinasubiri maamuzi mbalimbali ya kikodi katika Mamlaka za Rufaa za Kodi. Hii inafanya punguzo la kiasi cha Sh. trilioni 5.53 (sawa na asilimia mbili) ikilinganishwa na kiasi cha Sh. trilioni 366.03 kwa kesi 950 katika mwaka wa fedha 2018/19. Sambamba na hilo, nimebaini kuongozeka kwa idadi ya kesi kutoka 950 mwaka 2018/19 hadi kesi 1,097 mwaka 2019/20.

**Ushughulikiaji na Utatuzi wa Mapingamizi ya Kodi**
Ukaguzi wangu umebaini kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ilithibitisha kupokea mapingamizi ya kodi yenye thamani ya jumla ya Sh. 38,780,078,621 yaliyofanywa na walipa kodi ambayo bado yalikuwa hayajashughulikiwa, kinyume na muda uliowekwa kwenye Mkataba wa Huduma na Mlipakodi wa mwezi wa Julai 2017. Kuchelewa kushughulikia mapingamizi ya kodi kunaathiri malengo ya ukusanyaji wa kodi, kwani mapingamizi haya yanashikilia kiasi kikubwa cha kodi.

**Usimamizi wa Malimbikizo ya Madai ya Kodi**
Vilevile, nilibaini kutokuwapo taarifa muhimu katika malimbikizo ya madai ya kodi kama namba za utambuzi wa tathmini ya kodi kwenye makusanyo na marekebisho yaliyofanyika na mapendekezo ya kufuta madai ya kodi mikoa 13 niliyokagua ikiwa na kiasi cha Sh. 270,601,656,589 ambayo imepelekea ugumu kwangu katika kuhakiki uhalali wa taarifa hizo kwenye orodha ya malimbikizo ya madeni. Pia, nilibaini madai ya kiasi cha jumla ya Sh. 13,244,425,721 kwenye mikoa miwili ambacho kilikuwa kimesemwa kama hakikusanyiki bila sababu kubainishwa, Sh. 8,425,526,719 kilikuwa kwenye mapingamizi wakati kiasi cha Sh. 4,734,851,900 kilichobakia kilikuwa cha walipakodi ambao wanalipa kodi hivyo kinatakiwa kukusanywa. Kiasi cha Sh. 84,047,102.02 Mamlaka haikuthibitisha sababu ya kuzibainisha kama hazikusanyiki.

**Usimamizi wa Ukusanyaji wa Kodi**

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha wa 2019/20 nimebaini mapungufu mbalimbali kwenye ukusanyaji wa Mapato. Nayo ni haya yafuatayo:

(a) Kutokukusanywa kwa tozo na ada za forodha ya Sh. 408,723,375 kwenye lita 3,887,849 za mafuta yaliyoagizwa kutoka nje kwa ajili ya matumizi ya migodini. Hali hii ilitokana na udhaifu kwenye usimamizi wa ufanyaji wa tathmini za tozo na ada za forodha.

(b) Makadirio ya chini ya kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. 8,895,045,787 yaliyofanywa na walipakodi kutokana na matamko ya chini ya mauzo yao kwenye ritani za kodi ya ongezeko la thamani wanazofanya kila mwezi ikilinganishwa na taarifa zao za mauzo walizotoa kwenye taarifa za mwaka za mahesabu yao. Hii imechangiwa na uhakiki na uchambuzi usiotosheleza wa taarifa mbalimbali za matamko ya walipakodi wanazotoa kama vile ritani za kodi ya ongezeko la thamani za kila mwezi, mauzo kwenye za kielekitroniki, pamoja na mahesabu ya mwaka.

**Mapendekezo**

Serikali itengeneze mpango mkakati wa kuwahamasisha na kuwavutia wawekezaji wapya wa ndani na nje ili kuongeza wigo wa kodi.

Pia, Serikali iboreshe utendaji na ufanisi wa Mamlaka za rufaa za kodi kwa kuzipa fedha za kutosha na rasilimali zingine zinazohitajika kwenye kuziendesha Mamlaka hizo ili kusaidia usikilizaji na umalizaji wa kesi kwa wakati na kuimarisha upatikanaji wa haki.

Kadhalika, Serikali iongeze idadi ya wataalamu wanaoshughulikia mapingamizi ya kodi na kuimarisha uwezo wa kitengo cha mapingamizi ya kodi ndani ya mamlaka ya mapato ili kusaidia utatuzi wa mapingamizi ya kodi kwa haraka. Pia, kuhakiki madeni yanayoripotiwa ili kupata usahihi wa madeni yanayotakiwa kukusanywa.

Sambamba na hayo, Serikali iimarishe mifumo kwenye usimamizi wa mafuta yanayotumika kwenye shughuli za uchimbaji wa madini kuhakikisha ushuru na tozo ambazo hazijapewa misamaha zinatathminiwa na kukusanywa kwa wakati.

Mwisho, Serikali iboreshe mifumo ya ukusanyaji wa Mapato ili kuwezesha kufanyika ulinganifu na uthibitishaji wa taarifa za walipa kodi kusaidia ukusanyaji mkubwa wa Mapato ya kodi kwa ustawi wa taifa letu.

**Usimamizi wa Deni la Taifa**
Deni la Taifa linajumuisha madeni yote inayodaiwa serikali ndani na nje ya nchi kupitia Serikali Kuu na wakala zake, Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na mashirika ya serikali na tanzu (Subsidiaries) ambazo wana umiliki wa pamoja na sekta binafsi.

Deni la ndani linajumuisha mikopo ya muda mrefu na muda mfupi. Mikopo ya muda mrefu ni hati fungani, hisa za serikali na hati fungani maalum. Mikopo ya muda mfupi ni dhamana za serikali za muda mfupi na nakisi ya serikali kwenye akaunti za benki kuu (*Government overdraft*). Mikopo ya muda mfupi hutumika kulipia dhamana za serikali zilizoiva na mikopo ya muda mrefu hutumika kugharamia miradi. Deni la nje linajumuisha ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kutoka taasisi za kimataifa, nchi marafiki, benki za kibiashara, pamoja na wakopeshaji wa kibiashara

Katika ukaguzi wangu nilibaini deni la Taifa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 lilikuwa Sh. bilioni 56,757, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 3,652 (sawa na asilimia saba), ikilinganishwa na deni la Sh. bilioni 53,105 lililoripotiwa mwaka wa fedha 2018/19. Kuongezeka kwa deni la serikali kunasababishwa na malimbikizo ya riba, mabadiliko ya thamani ya Sh. na mikopo halisi (Net disbursements) ambayo inajumuisha mapokezi ya fedha za mikopo, ulipaji wa mtaji na malipo ya riba za dhamana za Serikali za muda mfupi.

**Mapungufu Niliyobaini katika Usimamizi wa Deni la Serikali ni kama Ifuatavyo**
Katika ukaguzi wangu wa muundo mpya wa Wizara ya Fedha na Mipango ulioidhinishwa mwaka 2018, nilibaini kuwa Wizara ilianzisha idara kwa ajili ya kusimamia shughuli zote zinazohusiana na madeni ya serikali. Idara ina vitengo vitatu ambavyo ni uhamasishaji wa rasilimali, usimamizi wa viashiria hatarishi na usimamizi wa kanzidata. Hata hivyo, nimebaini kuwapo kwa mwingiliano wa majukumu baina ya vitengo. Mathalani, nimebaini kuna mwingiliano wa majukumu baina ya kitengo cha usimamizi wa kanzidata na kitengo cha uhamasishaji wa rasilimali kwenye utekelezaji wa jukumu la utunzaji wa mikataba ya madeni ya nje. Pia,

nimebaini kutokuwapo kwa kitengo kinachohusika na mahesabu, yaani uhasibu.

Pia, nilibaini Wizara ya Fedha na Mipango ilipanga kuunda kanzidata ya pamoja ya taifa ili kusimamia taarifa za Miradi (NPMIS) tangu mwaka 2010. Hata hivyo, hadi kufikia Juni 2020 mfumo huo ulikuwa haujaanza kutumika kikamilfu. Sambamba na hilo, nilibaini taarifa za maendeleo ya miradi zimegawanyika katika idara mbalimbali za wizara ya Fedha na Mipango; na taarifa za maendeleo ya miradi hiyo zinapatikana kwa watekelezaji wa miradi pekee, kinyume na matakwa ya kanuni 14(c) ya kanuni za mikopo, ruzuku na dhamana za serikali ya mwaka 2003.

**Mapendekezo**

Ninaishauri serikali irekebishe muundo wa Wizara ya Fedha na Mipango ili kuwe na kitengo kinachoshughulikia masuala ya uhasibu katika idara na kuzuia mwingiliano wa majukumu ili kuimarisha uwajibikaji. Pia, iandae mpango kazi utakaowezesha kukamilisha utengenezaji na kutumika kikamilifu kwa mfumo mmoja wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi kwa wadau wote.

**Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao ya Watumishi Waliomaliza Muda wao Kazini.**

Katika mwaka wa fedha husika, ofisi yangu imekagua majalada **2,502** ya watumishi waliomaliza muda wao kazini. Majalada **2,328** kati ya hayo, yenye jumla ya Sh. **154.27** bilioni, yalikaguliwa na kuidhinishwa kwa ajili ya malipo. Majalada **174** yalihojiwa na kurejeshwa kwa Maafisa Masuuli husika kwa ajili ya marekebisho ya makosa yaliyobainishwa. Jumla ya Majalada **184** yalikuwa bado katika ukaguzi wakati wa kufunga mwaka wa fedha tarehe 30 Juni 2020.

Kadhalika, ukaguzi wangu wa mafao kwenye majalada 2328 ulibaini majalada 372 yalikokotolewa kimakosa na Maafisa Masuuli husika. Kati ya hayo, majalada 211 yalikokotolewa zaidi ya kiwango stahiki ambacho kingepelekea serikali kupoteza jumla ya Sh. milioni 652.59. Majalada 161 yalikokotolewa kwa kiwango pungufu ambacho kingesababisha mapunjo ya jumla ya Sh. milioni 430.04 kwenye mafao kama ukaguzi wangu wa awali usingefanyika.

Vilevile, nilibaini ucheleweshaji uliohusisha hadi miaka 30 kwa baadhi ya majalada kati ya 750 niliyokagua. Ucheleweshaji huo ulifanywa na waajiri

katika maandalizi na uwasilishaji wa majalada hayo kwangu kwa ajili ya ukaguzi wa awali.

**Mapendekezo**

Naishauri serikali kuhakikisha:

(a) Maafisa Masuuli wanazingatia kanuni ya kikokotoo cha mafao na sheria husika. Kadhalika, majalada ya watumishi waliomaliza muda wao kazini yawasilishwe ofisini kwangu kwa wakati yakiambatishwa na nyaraka sahihi kwa ajili ya ukaguzi wangu wa awali; na

(b) Inashughulikia kwa wakati majalada ya watumishi waliomaliza muda wao kazini ambayo nimebainisha makosa mbalimbali ili kuepuka ucheleweshaji wa malipo na kuimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti ili kuepuka makosa kwenye mafao.

**Tathmini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani na Utawala Bora**

Nilifanya tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani na utawala bora pamoja na mfumo wa ukaguzi wa ndani, kamati ya ukaguzi, tathmini ya ubadhirifu, TEHAMA na usimamizi wa vihatarishi. Tathmini yangu ya mifumo ya udhibiti wa ndani ilibaini kuwa kuna taasisi 28 zenye mapungufu ambayo yalitokea katika mfumo wa ukaguzi wa ndani. Katika tathmini ya Kazi ya Kamati ya Ukaguzi, ilibaini Taasisi 24 zenye mapungufu. Pia, tathmini ya usimamizi wa vihatarishi ilibaini Taasisi 9 zenye mapungufu.

Tathmini ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inaonesha kuwa kuna taasisi 23 zenye mapungufu katika mfumo. Tathmini yangu ya kuhusu viashiria vya ubadhirifu ilibaini kuwa, Taasisi 6 zilikuwa na mapungufu katika masuala ya ubadhirifu. Matokeo ya kina yanaoneshwa katika Sura ya Sita.

**Mapendekezo**

Ili Kusimamia vyema rasilimali za umma, napendekeza kuimarishwa kwa udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha sheria na taratibu zilizowekwa zinafuatwa. Pia, kuhakikisha usimamizi wa vihatarishi. Kadhalika, kuhakikisha kuwa mifumo ya utawala ipo na inafanya kazi ipasavyo.

**Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara**

Usimamizi wa rasilimali watu na mishahara ni eneo muhimu sana Serikalini. Eneo hili linahitaji umakini na uboreshaji wa mara kwa mara ili kuzidisha ufanisi katika shughuli na utendaji wa Serikali za kila siku.

Kwa mtazamo wa hapo juu, nimebaini mapungufu mbalimbali ambayo yanahitaji kuboreshwa na Taasisi za Serikali na nimeyaelezea kwa kirefu zaidi kwenye sura ya saba ya taarifa hii. Aidha, kuna mapungufu ambayo nimebaini ni muhimu yaelezwe kwenye muhtasari huu kama yanavyoonekana kwenye aya zifuatazo:

Mapungufu ambayo yameonekana kwenye ukaguzi wa mwaka huu wa fedha na hayakuwapo kwenye taarifa yangu ya mwaka uliopita ni: Mosi ni ucheleweshaji wa kuwasilisha makato ya kisheria kiasi cha Sh. 1,557,988,754.82 kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Bima ya Afya na Mamlaka ya Mapato Tanzania uliofanywa na Taasisi mbalimbali za Serikali. Pili, ni madai ya watumishi yenye thamani ya Sh. 331,518,426,304.13 yaliyotokana na mishahara ambayo haikulipwa baada ya watumishi kupandishwa vyeo au ajira mpya na malipo ya posho mbalimbali. Tatu, ni Taasisi mbili ambazo hazikurejesha Wizara ya Fedha na Mipango mishahara ambayo haikulipwa kwa sababu mbalimbali kiasi cha Sh. 222,683,585.95.

Kwa mapungufu yaliyowasilishwa kwenye taarifa yangu ya mwaka uliopita, nimebaini kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa Umma. Upungufu huo unasababishwa na Serikali kutoa vibali vichache ikilinganishwa na maombi ya vibali vya ajira mpya kama nilivyoona kwenye Taasisi 52 ambazo zina upungufu wa watumishi 7,889, malipo ya mishahara yenye thamani ya Sh. 59,158,470 yaliyolipwa kwa watumishi waliokoma utumishi wa Umma, pamoja na watumishi wanaokaimu nafasi mbalimbali za juu kwa muda mrefu bila kuthibitishwa kwenye nafasi hizo.

**Mapendekezo**

Kutokana na mapungufu ya hapo juu, napendekeza Maafisa Masuuli wa Taasisi za Serikali kwa kushirikiana na OR-UTUMISHI kufanya tathmini ya watumishi kwa lengo la kubaini upungufu na mahitaji ya watumishi kwenye Taasisi zao ili kujaza nafasi hizo. Aidha, napendekeza kwa Taasisi kuboresha mfumo wa udhibiti wa ndani utakaosaidia uwasilishaji wa makato ya watumishi kwa muda kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Pia, napendekeza Serikali kuhakikisha inalipa madai ya watumishi kwa wakati, kuthibitisha watumishi wanaokaimu nafasi za juu kwa wakati na kuboresha Mfumo wa usimamizi wa Watumishi wa Umma ambao utasaidia kupunguza hatari ya kufanya malipo kwa watumishi wasiostahili, kama vile waliokoma utumishi wa Umma.

**Wakala wa Serikali, Mifuko Maalumu na Taasisi Nyingine**

Katika ukaguzi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), nilibaini kuwa Wakala wa Majengo Tanzania ilikuwa imecheleweshа ujenzi wa majengo mbalimbali ya serikali katika mkoa wa Dodoma yenye thamani ya Sh. 46,628,482,327.13. Ucheleweshaji huu unaathiri malengo ya Serikali ya kuhakikisha Serikali nzima inahamia kwenye makao makuu mapya ya nchi Dodoma.

Katika ukaguzi wa Wakala wa Ndege wa Serikali (TGFA), nimebaini kuwa TGFA iliikodishia ndege nane ATCL kwa makubaliano kuwa ATCL itatakiwa kulipa tozo ya kodi ya ndege hizo na gharama ya akiba ya matengenezo. Hata hivyo, nimebaini kuwa TGFA ilimtoza ATCL kiasi cha Sh. 79,626,383,417, ikiwa ni gharama ya kukodi ndege na fedha ya akiba ya matengenezo. Hata hivyo, TGFA ilipokea jumla ya Sh. 8,143,504,800 kutoka ATCL, huku jumla ya Sh. 71,482,878,617 ikiwa haijalipwa mpaka tarehe 30 Juni 2020. Aidha, nimebaini kuwa TGFA ilitumia kiasi cha Sh. Bilioni 3.9 kufanya matengenezo ya ndege iliyoundwa mwaka 1978 (miaka 40 iliyopita); hatahivyo, nimebaini ndege hiyo bado imetelekezwa na haifanyi kazi licha ya matengenezo yaliyofanyika.

Katika ukaguzi wa TANROADS nimebaini yafuatayo: TANROADS haikukata tozo ya ucheleweshaji wa mradi ya Sh. 5,459,428,648.81 kwenye mkataba wa ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta (Sanzate) (50 km). Pia, nilibaini TANROADS ilianza ujenzi wa daraja la Kigogo – Busisi bila ya kuwapo kwa Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira. Aidha, nimebaini kasi ndogo ya utekelezaji wa huduma ya ushauri juu ya hatua za kuzuia mafuriko katika bonde la Jangwani.

Ukaguzi wangu wa shughuli za TARURA ulibaini kuwa TARURA ilimpatia mzabuni mikataba yenye thamani ya Sh. 1,179,910,730 aliyeshindwa kukidhi vigezo vya uhalali wa zabuni na hakuwasilisha nyaraka muhimu za kuwezesha kufanyika tathmini ya zabuni. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 204 (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013. Aidha, nimebaini kuwa miradi ya ujenzi wa barabara yenye thamani ya Sh. 1,959,810,460 imetelekezwa na wakandarasi mbalimbali kabla ya kukamilika.

Katika ukaguzi wa NFRA, nimebaini kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu haijalipa gharama ya mahindi yenye thamani ya Sh. 167,376,994,882.48 yaliyotolewa na NFRA ili kukabiliana na baa la njaa na majanga

yaliyotokea katika maeneo tofauti ya nchi kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 12.

Nimebaini mapungufu yafuatayo yanayohusisha Wakala mbalimbali: Mosi, ni kutokulipwa kwa madai ya wakandarasi, wahandisi washauri, na watoa huduma yenye thamani ya Sh. 783,392,176,735.35. Pili, ni Mamlaka ya Mapato Tanzania kutaifisha fedha za wakala kiasi cha Sh. 66,834,646,659.16. Kiasi hiki kimetaifishwa kutokana na malimbikizo ya kodi. Tatu, ni usimamizi usioridhisha wa dhamana za mikataba zenye thamani ya Sh. 35,145,710,896.75. Nne, nilibaini Wakala 12 ambazo zinaendeshwa kibiashara lakini makusanyo ya mapato ya ndani yalikuwa chini sana kwa kiwango cha kuanzia asilimia 21 mpaka 83 ikilinganishwa na kiwango cha bajeti.

Ukaguzi wangu wa NIDA ulibaini kuwa NIDA ilikuwa na kadi 426,757 zenye thamani ya Sh. 3,399,973,019 ambazo zimeharibika na hazifai kwa matumizi ya kutengeneza vitambulisho vya taifa, huku muda wa mkataba wa mtoa huduma wa kadi hizo zenye kasoro ulikwa umeisha tokea miaka mitatu nyuma (14 Machi 2018).

Katika ukaguzi wa shughuli za REA zinazohusu usambazaji wa umeme vijijini nimebaini kuwa nguzo za umeme 2,612 zenye thamani ya Sh. 1,065,696,000 ambazo ziliwekwa mkoani Lindi zilikuwa na mipasuko, huku mkandarasi husika akiwa bado hajabadilIsha nguzo hizo zenye kasoro.
Kwenye ukaguzi wa Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori (TWPF) nilibaini kuwa, TWPF ililipa jumla ya Sh. 4,511,552,869 kwa mshauri elekezi baada ya kuwasilisha ripoti ya usanifu wa jengo la Kakakuona Dar es Salaam. Hata hivyo, nimebaini shughuli za ujenzi wa jengo hilo hazijaanza kwa miaka minane tangu kuwasilishwa kwa ripoti ya usanifu wa jengo hilo mnamo Mei 2012.

Katika ukaguzi wa Hospitali za Mkoa za Rufaa, nimebaini kuwapo kwa madai yenye thamani ya Sh. 2,179,268,577.86 yaliyokataliwa na NHIF kutokana na mapungufu katika kujaza taarifa za wagonjwa na mfumo duni wa kuhifadhi taarifa za wagonjwa. Aidha, nimebaini kuwapo kwa madawa yaliyoisha muda wake wa kutumika yenye thamani ya Sh. 238,708,163 ambapo madawa hayo bado hayajeteketezwa na hospitali husika. Maelezo zaidi yametolewa kwenye sura ya nane ya ripoti hii.

**Mapendekezo**

Mbali na pendekezo la kawaida la kuanzisha na kusimamia mfumo wa udhibiti wa ndani, ninapendekeza vyombo vya uchunguzi vya serikali kuchunguza mapungufu makubwa yaliyooneshwa katika ripoti hii na kuchukua hatua za kisheria na za kiutawala.

**Ununuzi na Usimamizi wa Mikataba**

Serikali ya Tanzania inatambua umuhimu wa usimamizi bora wa ununuzi wa Umma na Mikataba kama jambo la msingi la kuhakikisha rasilimali za Umma zinatumika kwa ufanisi na uwajibikaji. Kutokana na umuhimu huo, Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) pamoja na Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) zilitungwa. Sheria hizi zinaweka utaratibu wa kisheria, usimamizi wa taasisi za ununuzi pamoja na michakato ya ununuzi katika sekta ya umma.

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2019/2020, nilibaini mapungufu katika kufuatisha Sheria tajwa hapo juu kwa Taasisi za Serikali Kuu ambayo nimeyabainisha katika Sura ya Tisa ya ripoti hii. Mapungufu makubwa yaliyobainika katika ukaguzi wa ununuzi na usimamizi wa Mikataba ni haya yafuatayo:

- Ukaguzi ulibaini Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (**Fungu Na. 19**) ilifanya ununuzi wa dharura wa huduma za Kisheria kwa kiasi cha Sh. 2,757,322,034 bila ya kufuata taratibu za ununuzi wa dharura;
- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (**Fungu Na. 57**) ilishindwa kutekeleza majukumu yake ya Mkataba na Kampuni ya ZTE Corporation ya Nchini China kwa ajili ya Ujenzi wa Mradi wa Mfumo Salama wa Mawasiliano (Independent Mobile Secured Networks-IMSN) kwa gharama ya Sh 129,555,020,000;
- Wakati wa Ukaguzi nilibaini kukosekana kwa Makubaliano (Concession Agreement) baina ya Wizara ya Ujenzi na Mfuko wa Pensheni wa NSSF katika ukusanyaji wa mapato katika Daraja la Nyerere (Kigamboni), ambapo kiasi cha Sh. 9,602,000,000 kinakusanywa kwa mwaka;
- Kuwapo kwa manunuzi ya Sh. 15,959,992,081 nje ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka, Ununuzi wa bidhaa na huduma bila ya ushindanishi Sh 1,448,432,377;
- Kuongezeka kwa gharama za Mkandarasi Mshauri kwa kiasi cha Sh 13,262,485,816 kutokana na kuchelewa kukamilika kwa Miradi ya Maji.
- Ununuzi wa vifaa visivyokaguliwa kwa kiasi cha Sh 1,485,976,283;

- Ununuzi wa vifaa bila ya kuingizwa kwenye vitabu vya stoo vyenye thamani ya Sh 1,034,263,676;
- Ununuzi wenye thamani ya Sh 1,560,986,067 bila idhini ya Bodi ya Zabuni;
- Kuwapo kwa vifaa na Mali zilizolipiwa lakini hazikupokelewa kiasi cha Sh. 6,878,038,989;
- Ununuzi bidhaa na huduma nje ya Mfumo wa Kielekitroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) Sh. 227,490,940;
- Kuchelewa kukamilika kwa kazi za ujenzi, ununuzi wa bidhaa na utoaji wa huduma wa kiasi cha Sh. 70,536,032,862;
- Mapungufu yaliyobainika katika Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi Kikombo-Dodoma Sh. 30,246,348,255; na
- Mapungufu yaliyobainika katika usimamizi wa ujenzi wa Majengo mbalimbali ya Mahakama Sh. 40,950,961,181.

Halikadhalika, nilifanya ukaguzi wa kina wa usimamizi wa Mikataba katika Ofisi 36 za Wilaya za RUWASA katika Mikoa 19. Lengo kuu lilikuwa kupima kama kulikuwa na mifumo madhubuti katika kusimamia Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Maji kwa Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ili kupata matumizi bora ya rasilimali zilizotengwa na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Maelezo zaidi yapo kwenye Sura ya Tisa ya ripoti hii.

**Mapendekezo**

Kutokana na mapungufu yaliyobainika hapo juu katika ukaguzi wa ununuzi, natoa ushauri kwa menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu kuhakikisha zinazingatia kikamilifu Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) pamoja na Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016), hususani katika maeneo ya: kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali katika ununuzi wa dharura, usimamizi bora wa mikataba ili kuepuka tozo, pamoja na riba zitokanazo na kusitisha mikataba.

Vilevile, Taasisi za ununuzi zizingatie: Mpango wa ununuzi wa Mwaka, ununuzi wa bidhaa na huduma kuidhinishwa na bodi ya Zabuni na ununuzi kupitia mfumo wa kielekitroniki katika ununuzi wa Umma. Pia, nasisitiza Menejimenti za Wizara, Idara na Sekretarieti ya Mikoa husika kuzingatia ushindanishi katika ununuzi ili kuweza kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi. Pia, Menejimenti za Taasisi husika kuzingatia matakwa ya

Mikataba na kuhakikisha Wakandarasi wanaochelewesha kazi wanatozwa tozo ya ucheleweshaji.

**Usimamizi wa Matumizi**

Usimamizi wa matumizi ni eneo muhimu kwenye utendaji wa kila siku wa Serikali, hivyo ni jambo la muhimu sana kwenye ukaguzi wangu. Hakuna tofauti kubwa sana ikilinganishwa na ripoti zangu za miaka iliyopita, ambapo nimekuwa nikibaini dosari mbalimbali zinazopaswa kufanyiwa kazi na menejimenti husika ili kuboresha usimamizi wa rasilimali kama walivyopewa dhamana na walipa kodi. Ninawasilisha muhtasari wa mapungufu niliyobaini kwenye ukaguzi wangu wa mwaka huu, maelezo zaidi yanapatikana sura ya kumi ya ripoti yangu.

Ukaguzi wangu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ulibaini kuwa fedha kiasi cha Sh.43,263,677,359 zilitumwa mikoa yote 26 pamoja na Zanzibar kwa ajili ya kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura. Nilibaini kuwa, kuna bakaa kiasi cha Sh. 716,706,995 katika Halmashauri 70 kwenye mikoa 19 ambazo hazijarejeshwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya matumizi husika kukamilika. Nilishindwa kubaini kiasi ambacho kilitumika na kilichobaki katika Halmashauri za Kasulu na Uvinza ambazo zilipelekewa kiasi cha Sh. 262,059,500 na Sh. 219,632,000, mtawalia. Hii ni kwa sababu Wakurugenzi wa Halmashauri walishindwa kunipa nyaraka husika. Kutokurejesha fedha ambazo hazijatumika kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha hizo.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, Wizara mbili zilifanya matumizi kiasi cha Sh. 453,782,820.35 ambazo naona hayana tija, wakati fedha hizo zingeweza kutumika kwenye shughuli zingine. Bila ya kuwa na mfumo madhubuti wa udhibiti wa fedha, Serikali itaendelea kupata hasara kutokana na maamuzi yanayofanyika, ambayo yanapelekea matumizi yasiyo na tija.

Nilibaini kuwa, taasisi 36 zilifanya malipo ya Sh. 7,320,136,708 bila kuwa na nyaraka stahiki na toshelezi katika mwaka huu wa ukaguzi, wakati hati za malipo kiasi cha Sh. 2,638,372,956.12 yaliyofanywa na taasisi nne hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hivyo, sikuweza kujiridhisha na uhalali wa malipo hayo.

Pia, ukaguzi wangu ulibaini kuwa, taasisi sita zilifanya matumizi kiasi cha Sh. 24,408,396,381 ambayo hayakuwa kwenye bajeti, kinyume na sheria

ya bajeti ya mwaka 2015. Matumizi kinyume na bajeti huathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali, hivyo kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Zaidi ya hayo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 13 zilifanya malipo kiasi cha Sh. 593,801,192 kupitia vifungu visivyohusika, kinyume na kanuni 46(2) ya Kanuni za Fedha.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa taasisi 21 zililipa jumla ya Sh. 1,547,458,579.29 kwa wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za kielekitroniki. Zaidi ya hapo, taasisi tano zilishindwa kukata na kuwasilisha kodi ya zuio kiasi cha Sh. 60,035,534 kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania kinyume na Sheria ya Kodi ya Mapato.

**Mapendekezo**

Kutokana na hayo, ninashauri Maafisa Masuuli kuendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti kwenye usimamizi wa matumizi ili kupunguza hatari ya matumizi mabaya ya fedha. Ili kutekeleza hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iweke mfumo madhubuti utakaowezesha usimamizi wa matumizi ya fedha zinazotumwa Halmashauri, na kuhakikisha fedha ambazo hazijatumika zinarejeshwa. Vilevile, nyaraka za malipo ziwe zinapatikana zinapohitajika kwa ajili ya ukaguzi zikiwa stahiki na toshelezi. Pia, kuhakikisha kuwa sheria za kodi na ununuzi zinazingatiwa kwa kudai risiti za kielekitroniki pamoja na kukata kodi zuio na kuziwasilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**Ukaguzi wa Matumizi ya Fedha za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa**

Nilifanya ukaguzi wa matumizi yaliyofanywa na OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika tarehe 24 Novemba 2019.

Nilibaini kuwa, OR–TAMISEMI na Halmashauri 46 zilifanya matumizi ya Sh. 1,628,589,360.53, kinyume na shughuli za uchaguzi bila kibali. Pia, nilibaini kuwa OR-TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 zilifanya malipo ya Sh. 2,141,019,933 bila ya kuwa na nyaraka stahiki na toshelezi, ilhali malipo yenye thamani ya Sh. 389,160,384.31 hayakuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo sikuweza kujiridhisha kuhusu uhalali wake.

Pia, nilibaini uradidi wa ununuzi wa vidau vya wino na wino wa mihuri vyenye thamani ya Sh. 199,991,209. Hivi vilinunuliwa na OR-TAMISEMI wakati Halmashauri zilipewa maelekezo ya kufanya ununuzi wa vitu hivyo hivyo. Hadi namaliza ukaguzi wangu, vidau pamoja na wino vilikuwa

havijatumika. Pia, nilibaini kuwa, Halmashauri 14 zilifanya matumizi nje ya bajeti kiasi cha Sh. 244,778,685.68.

Kwenye ununuzi, nilibaini kuwa Halmashauri tano zilifanya ununuzi wa Sh. 149,406,000 kwa fedha taslimu, kinyume na kiwango kinachoruhusiwa kwa mujibu wa sheria ya ununuzi.

**Mapendekezo**
Kutokana na dosari hapo juu, ninashauri Maafisa Masuuli husika: (a) Kuhakikisha malipo yanayofanyika yanakuwa na nyaraka stahiki na toshelezi; (b) Kuhakikisha wanazingatia bajeti iliyoidhinishwa; (c) Kuwasilisha hati za malipo kwa ukaguzi zinapohitajika kwa ajili ya ukaguzi; na (d) Kuzingatia sheria za ununuzi kwa kutokufanya ununuzi kwa fedha taslimu zaidi ya ukomo uliowekwa kisheria.

**Udhibiti wa Mali na Madeni**
Katika mwaka wa fedha 2019/20, nimepitia Usimamizi na Udhibiti wa Mali na Madeni na kubaini mapungufu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na: udhibiti usioridhisha wa usajili wa magari ya Serikali unaofanyika chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), utunzaji hafifu wa daftari la Mali za Kudumu za Serikali, pamoja na Mali za Serikali ambazo zimetelekezwa kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa.
Aidha, nilibaini kuwapo kwa taasisi 22 ambazo hazina hati ya umiliki wa Ardhi. Pia, nimebaini Taasisi 16 zilikuwa na mali zilizotelekezwa, zilizochakaa, ujenzi usiokamilika, viwanja visivyo endelezwa kwa muda mrefu.

Mbali na hayo, nimebaini kuwapo kwa Taasisi 16 zenye mali ambazo hazijasajiliwa na kupewa namba ya utambulisho. Zaidi, ukaguzi wangu ulibaini nyumba zilizojengwa na kukamilika bila kutumika kwa muda mrefu.

**Mapato Yasiyokusanywa na Matumizi Yasiyolipwa (Receivables and Payables)**
Katika ukaguzi wa mwaka 2019/20, nilibaini Taasisi 78 ambazo zilikuwa na madai yenye thamani ya Sh. 1,032,851,584,396, ikiwa ni ongezeko la Sh. 991,353,737,153 ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 41,497,847,243 kilichoripotiwa mwaka wa fedha 2018/19. Mwenendo huu wa kuongezeka kwa madai unasababishwa na udhibiti wa ndani usioridhisha juu ya

usimamizi wa mapato. Aidha, nilibaini kuwa Taasisi kama vile Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, Wakala wa Ndege za Serikali na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, zilikuwa na kiasi kikubwa cha madai. Hivyo, taasisi hizi zinahitaji umakini na juhudi zaidi katika usimamizi wa mapato.

Katika ukaguzi wa mwaka 2019/20, nilibaini Taasisi za Serikali 122 zilikuwa na madeni yenye thamani ya Sh. 3,126,442,872,063 ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 2,687,140,232,434 kilichoripotiwa kwenye taarifa yangu ya mwaka uliopita 2018/19 ikiwa ni sawa na ongezeko la kiasi cha Sh. 439,302,639,629. Hii inaashiria udhibiti usioridhisha katika usimamizi wa matumizi yasiyolipwa.

Aidha, katika kuangalia madeni tarajiwa, nimebaini taasisi 23 zenye kesi dhidi ya makampuni na watu mbalimbali zenye thamani ya Sh. 314,321,747,130, zikiwa bado zinasubiri maamuzi ya mahakama. Hata hivyo, ni maoni yangu kuwa kuwapo kwa kiasi kikubwa cha madeni tarajiwa kinaweza kuziathiri taasisi kifedha ikiwa maamuzi ya mahakama yataegemea upande wa wadai.

**Mapendekezo**

Pamoja na Mapendekezo niliyotoa miaka iliyopita kuhusu usimamizi wa Mali na Madeni, bado naendelea kusisitiza Maafisa Masuuli kuimarisha udhibiti katika kusimamia mali. Udhibiti huo unajumuisha kutunza kumbukumbu zinazofaa, kulinda mali, kufuata sheria na kanuni na kutenga fedha za kutosha ili kuwezesha ujenzi na ukarabati wa majengo. Pia, ninapendekeza Serikali ibuni na kuanzisha mfumo dhabiti wa kusajili na kufuatilia Magari katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta Ujenzi)

Kuhusiana na madai na madeni kwa muda mrefu, ninatoa ushauri kwa Wizara, Idara, na Wakala wafuatilie kwa karibu na kukusanya mapato ili kuepuka upotezaji wa fedha za umma pale yanaposhindikana kukusanywa. Pia, ninashauri Serikali itoe fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa kuweza kuwalipa watoa huduma na wakandarasi kwa wakati.

**Ukaguzi wa Vyama vya Siasa**

Kwa mwaka huu wa fedha 2019/20, nimepokea taarifa za fedha za vyama vya siasa 17 kati ya vyama 19 vilivyosajiliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa. Chama cha Democratic Party (DP) na Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) havikuwasilisha taarifa zao za fedha. Hata hivyo, nimekagua mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuthibitisha ubora wake katika kulinda mali za wanachama. Ukaguzi wangu umebaini masuala yafuatayo:

- Masurufu ya jumla ya Sh. 30,364,440 yalitolewa kwa wafanyakazi saba (7) bila ya kurejesha masurufu ya nyuma yaliyotolewa;
- Masurufu ya jumla ya Sh.41,101,150 yalicheleweshwa kurejeshwa na Watumishi sita (6) kwa kipindi kati ya siku 80 hadi 475;
- Masurufu ya jumla ya Sh. 173,249,334 kwa watumishi 55 ambayo hayajarejeshwa hadi kipindi changu cha ukaguzi, mwezi Februari 2021;
- Ofisi ya CCM Mkoa wa Mwanza haikukusanya malipo ya kodi za pango Sh.348,465,790 kutoka kwa wapangaji 149 wa kiwanja cha CCM Kirumba na Ofisi ya CCM ya Mkoa wa Mwanza.
- Ofisi ya CCM Lumumba, Dar es Salaam ilitumia Sh. 27,095,000 kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma bila ya kufuata taratibu za ushindani za ununuzi;
- Ofisi ya CCM Zanzibar ilinunua bidhaa za jumla ya Sh. 75,056,000 na kulipa taslimu kwa wazabuni badala ya kuhamisha malipo hayo kwenye akaunti zao za benki;
- Bidhaa za jumla ya Sh. 247,718,400 zilinunuliwa na CCM bila ya kuandikishwa kwenye Daftari la utunzaji mali;
- Chama cha Wananchi (CUF) kilituma kiasi cha Sh. 72,981,268 kwa mmoja wa wanachama wake kwa ajili ya ununuzi wa magari mawili kutoka kwa mojawapo wa Wazabuni waliopo Japani. Mwanachama huyo alinunua magari hayo, na yalisajiliwa kwa majina binafsi badala ya jina la Baraza la Wadhamini la CUF;
- Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilinunua magari matano yenye thamani ya Sh. 227,430,000 na nyumba moja yenye thamani ya Sh. 50,000,000 iliyopo Serengeti bila ya idhini ya Baraza Kuu la Chama. Pia, Sh.100,000,000 zilitumika kwenye matumizi ya kawaida ya Chama bila ya idhini ya Baraza Kuu la chama;
- Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilifanya malipo yasiyokuwa na tija Sh. 19,800,000 kulipa bakaa ya mkopo wa

mmojawapo wa viongozi wa Chama hicho aliyeacha uanachama wa CHADEMA;
- Vyama vya siasa 11 vilitumia jumla ya Sh. 347,521,794 bila ya kuwa na nyaraka toshelezi. Hivyo, sikuweza kuhakiki sababu, uhalali na uhalisia wa malipo yaliyofanyika;
- Vyama vya siasa vitano vilichelewa kuwasilisha taarifa zao za fedha kwa ajili ya ukaguzi kwa kipindi kati ya siku 42 hadi 126;
- Vyama vya siasa kumi viliandaa taarifa zao za fedha bila ya kufuata kwa mfumo wa kimataifa wa uandaaji wa taarifa za fedha (IPSAS) kama ilivyoanishwa kwenye Kanuni Na. 3(1) ya Kanuni za vyama vya Siasa (uhasibu wa fedha) za mwaka 2019;
- Vyama vya siasa vinane vilitumia mapato yake yaliyopokelewa ya jumla ya Sh. 244,583,800 bila ya kuwekwa benki kinyume na Kanuni Na. 15(1) ya Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019;
- Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) na Chama cha Tanzania Labour Party (TLP) havikuandaa tamko la mali na kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kinyume na Kifungu Na. 14(1)(ii) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorekebishwa mwaka 2019;
- Chama cha UMD, Chama cha UDP, Chama cha NCCR-Mageuzi na Chama cha Demokrasia Makini havikuhuisha rejista za wanachama na viongozi wake, kinyume na Kifungu Na. 8C cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019; na
- Chama na Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) hakikuwasilisha ritani ya mwaka ya wajumbe wa Baraza la Wadhamini toka mwaka 2006, kinyume na Kifungu Na. 16(3) cha Sheria ya Usajili wa Udhamini Sura ya 318.

Ufafanuzi wa kina kuhusu mapungufu haya nimeutoa katika Sura ya 12 ya ripoti hii.

**Mapendekezo**

a) Kufuatia kiwango cha juu cha kutokuzingatia Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019, ninapendekeza kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa afuatilie na kusimamia uzingatiaji wa Sheria ya vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorekebishwa mwaka 2019. Pale penye ulazima, Msajili wa Vyama vya Siasa atoe adhabu kwa vyama vyote vya siasa vitakavyoshindwa kuzingatia sheria hiyo;

b) Maafisa Masuuli wa vyama vya Siasa kuhakikisha vinaandikisha mali zote zinazopokelewa kwa misaada au kununuliwa kwa jina la Baraza la Wadhamini la Chama ili kuepuka migogoro inayojitokeza ambayo inapunguza kasi ya vyama vya siasa katika kufikia malengo yake; na
c) Ninahimiza Maafisa Masuuli wa Vyama vya Siasa kuweka mifumo imara ya udhibiti wa ndani kwenye matumizi, masufuru, ununuzi na usimamizi wa mapato ili kupunguza hatari ya wizi na ubadhirifu wa fedha za wanachama.

**Kaguzi Maalumu Zilizofanyika Kwenye Wizara, Idara, Wakala na Mifuko Maalumu**

Mbali na kufanya ukaguzi wa kifedha wa kila mwaka, Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kinaipa Ofisi yangu mamlaka ya kufanya Kaguzi Maalumu. Katika mwaka huu, nimefanya kaguzi maalumu 15 kwenye Wizara, Idara, Mifuko Maalumu na Wakala. Katika kaguzi hizo 15, TAKUKURU waliomba kaguzi 7 ambazo matokeo yake ya ukaguzi na mapendekezo yamewasilishwa TAKUKURU kwa hatua zaidi za kisheria. Ukaguzi wangu umebaini masuala yafuatayo:

**Ukaguzi Maalumu wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii, Tamasha la Urithi na Uanzishwaji wa Chaneli ya Tanzania Safari na Studio ya Kutangaza Utalii**

- Tozo za Maendeleo ya utalii za jumla ya Sh. 37,237,508,966.72 zilipokelewa na kutumiwa na idara ya Utalii iliyopo Wizara ya Maliasili na Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania, na Makumbusho ya Taifa. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi ulioonesha kuwa Kamati ya Ushauri wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii na Afisa Masuuli wa Wizara walitoa idhini ya kutolewa kwa fedha kwenye Akaunti ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii. Matumizi ya jumla ya Sh. 6,875,458,200.34 yalilipwa bila ya idhini ya Afisa Masuuli. Matumizi ya jumla ya Sh. 16,363,437,737.11 yalilipwa bila ya kuwa na Hati za malipo na matumizi ya jumla ya Sh. 11,156,910,952.25 bila ya kuwa na nyaraka toshelezi. Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) ililipa Sh. 500,000,000 kwenye Bodi ya Utalii bila kuwekwa kwenye akaunti za benki za Tozo ya Maendeleo ya Utalii, kinyume na Kanuni Na. 9(1) na (2) ya Kanuni za Tozo za Maendeleo ya Utalii za mwaka 2013 na Makumbusho ya Taifa ilitumia Sh. 89,343,421.10 kwa shughuli zisizoendana na Utalii;
- Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya

Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Mfuko wa Tozo za Maendeleo ya Utalii zilichangia Sh. 1,569,924,204 kufadhili Tamasha la Urithi bila ya kuwapo kwenye bajeti zao za mwaka 2018/2019;

- Kituo cha Televisheni cha Clouds na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) hawakupatikana kwa njia za taratibu za ununuzi zenye ushindani na usawa kwenye utangazaji wa Tamasha la Urithi na zilipokea malipo ya Sh. 629,700,014 na Sh. 201,463,784 mtawalia bila ya kutoa risiti za kielekitroniki; na Serikali haikukusanya kodi ya zuio ya Sh. 31,485,000.70 na Sh. 10,073189.20 kutoka Clouds na TBC, mtawalia;
- Taasisi Saba zilipokea Sh. 487,258,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Tamasha la Urithi. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka za matumizi zilizowasilishwa. Mhasibu wa Mfuko wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii alilipa Sh. 585,515,000 kutoka kwenye Mfuko wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii kwa ajili ya shughuli za Tamasha la Urithi bila kuwa na nyaraka toshelezi;
- Kampuni ya Wasafi ililipwa Sh. 140,000,000 kwa ajili ya shughuli za Tamasha la Urithi bila ya kuwa na Mkataba. Nilibaini kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii aliidhinisha malipo kwa Kampuni ya Wasafi bila ya kufuata taratibu za malipo ya Serikali;
- Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) zilitumia Sh. 171,998,045 kufadhili tamasha la upandaji Mlima Kilimanjaro bila ya fedha hizo kuwa kwenye bajeti; na
- Matumizi ya Ofisi ya Waziri Sh. 148,229,045 yalilipwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kupitia maelekezo ya katibu wa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**Ukaguzi Maalumu wa Matumizi ya Fedha za Utekelezaji Miradi ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi Yaliyofanywa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Nilibaini mapungufu mbalimbali kwenye utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), ikiwamo udanganyifu wa idadi za siku zilizolipwa kwa washiriki, kughushi mihuri ya wenyeviti wa vijiji na watendaji kata. Pia, niligundua udanganyifu kwenye tarakimu zilizorekodiwa kwenye Hati za malipo, udanganyifu wa tarakimu, na kuingizwa kwa washiriki wasiostahili, kughushi risiti za ununuzi na risiti za nyumba za kulala wageni na Watumishi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na kujipatia kiudanganyifu Sh. 342,351,415.46.

**Ukaguzi Maalumu wa Mali za CUF na ACT-Wazalendo**

Nilibaini kuwa Chama cha Wananchi (CUF) kinamiliki magari tisa na pikipiki 27 ambazo zina majina ya watu binafsi badala ya jina la Baraza la Wadhamini la CUF. Chama cha Wananchi (CUF) kilidai kumiliki magari 24 na pikipiki 24 ambazo zilikuwa zikitumika Zanzibar. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha umiliki huo. Nilibaini utata kwenye umiliki wa magari sita na aliyekuwa Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi kutokana na hoja zifuatazo: Sikuweza kuhakiki Chanzo cha Dola za Marekani 85,637 zilizotumika kwenye ununuzi wa gari hizo.

Nilibaini kuwa magari hayo yalinunuliwa na Mkurugenzi huyo wa Fedha na Uchumi na kuyakabidhi kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) licha ya kukana saini yake. Nilibaini kuwa magari hayo yalisajiliwa kwa majina ya watu binafsi.

**Ukaguzi Maalumu wa Matumizi Yaliyofanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) katika Fedha za Ruzuku Zilizotolewa na Mfuko wa Uwezeshaji Sekta ya Fedha (FSDT)**

Nilibaini kuwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) iliingia makubaliano ya ruzuku na Mfuko wa uwezeshaji Sekta ya Fedha (FSDT) wa jumla ya Dola za Marekani 3,000,000. Makubaliano hayo yalilenga kuisadia NIDA kuzalisha Namba za Utambuzi takribani 20,000,000 kwa kutumia taarifa za wapiga kura za mwaka 2015. Hata hivyo, nilibaini kuwa NIDA ilitumia jumla ya Dola za Marekani 1,153,588 kati ya Dola za Marekani 3,000,000 iliyoahidi. Hata hivyo, hakukuwa na Namba za Utambuzi (NIN) zozote zilizozalishwa na NIDA.

Niligundua kuwa ununuzi wa leseni, usafishaji kanzidata, utunzaji wa mfumo wenye gharama ya Dola za Marekani 220,000 (sawa na Sh. 495,450,000) ulifanywa bila ya Bodi ya Zabuni na Idara ya Ununuzi kushirikishwa. Pia, nilibaini kuwa wafanyakazi wawili (2) walipitisha ununuzi huo na wakamuidhinisha mkandarasi kufanya mabadiliko kwenye kanzidata ya NIDA.

**Ukaguzi Maalumu wa Fedha za Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) Zilizotumiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

Nilibaini kuwa wafanyakazi wa Idara ya Ustawi wa Jamii wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto walilipa posho ya kujikimu ya jumla ya Sh. 15,020,000 kwa washiriki 78 kwa Kiwango kilichozidi posho ya Serikali. Wafanyakazi tisa (9) walidanganya idadi ya siku walizozitumia na kujipatia Sh. 20,480,000 kwa udanganyifu. Nilibaini kuwa wawezeshaji wa nje watano (5) walilipwa Sh. 12,375,000 bila ya kuwa na mikataba. Wafanyakazi watano (5) walidanganya majina ya washiriki na kujipatia Sh. 4,311,000 kwa udanganyifu. Pia, nilibaini kuwa idara ya Ustawi wa Jamii (DWS) haikukata Sh. 41,963,500 kutoka kwenye malipo ya chai na chakula cha mchana kwenye shughuli 20 za UNICEF na kuisababishia Serikali hasara.

Pia, nilibaini kuwa watumishi wawili wa Idara ya Ustawi wa Jamii waliwasilisha nyaraka za masurufu ambazo hazikuwa na nyaraka toshelezi; hivyo nilishindwa kuthibitisha ukweli wa matumizi ya Sh. 6,679,000. Pia, nilibaini kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii ilifungiwa kupokea fedha za UNICEF kwa kipindi cha miezi 10 kwa sababu ya kuchelewesha marejesho ya shughuli 23 zenye gharama ya Sh. 562,427,000. Pia, nilibaini kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii ilitumia Sh. 200, 851,061 kwenye ununuzi wa bidhaa mbalimbali bila ya kufuata taratibu za ununuzi kama ilivyobainishwa kwenye Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016).

**Ukaguzi Maalumu wa Mfumo wa Usajili wa Vyeti vya Kuzaliwa na Vifo Uliofanyika Ofisi ya RITA DODOMA**

Nilibaini kuwa vyeti ya kuzaliwa 6,180 vyenye thamani ya Sh. 84,586,000 vilichapishwa kutoka kwenye Mfumo wa Usajili wa Kiraia (CRS) ambavyo sikuweza kuvithibitisha kwenye Mfumo wa Kielekitroniki wa malipo Serikalini (GePG) kuanzia mwezi Juni 2018 hadi Juni 2020. Vilevile, vyeti ya kuzaliwa 3,861 vyenye thamani ya Sh. 14,694,500 vilichapishwa kutoka kwenye Mfumo wa Usajili wa Mozilla ambavyo sikuweza kuvithibitisha kwenye taarifa za mapato yaliyokusanywa kwa kutumia Stakabadhi kutoka Serikalini (ERV). Pia, nilibaini kuwa wafanyakazi saba (7) wa Ofisi ya RITA walihusika kwenye ubadhirifu huu. Mifumo ya Kielekitroniki ya malipo Serikalini GePG na CRS haijaunganishwa; hivyo, taarifa za mapato zinazopatikana kwenye mfumo wa Usajili (CRS) sio za kuaminika.

Nilibaini vyeti vya vifo 289 vyenye thamani ya Sh. 2,222,500 vilichapishwa kutoka kwenye mfumo wa Usajili wa CRS bila ya kuandikishwa kwenye Mfumo wa kielekitroniki wa malipo Serikalini (GePG) kuanzia Juni 2018 hadi Juni 2020. Nilibaini wafanyakazi watatu (3) wa Ofisi ya Wilaya ya Dodoma walifanya udanganyifu wa kuchapisha vyeti vya vifo 20 vyenye thamani ya Sh. 77,500 kutoka kwenye Mfumo wa Usajili wa Mozilla bila ya kuvihandikisha kwenye taarifa ya makusanyo ya stakabadhi za Serikali (ERV).

Nilibaini kuwa karatasi za vyeti 15,125 vyenye thamani ya Sh. 6,050,000 vilinunuliwa kutoka mmojawapo wa Wazabuni na vimeachwa bila ya kutumika kwenye Ofisi ya RITA ya Wilaya ya Dodoma kwa kukosa namba za utambuzi. Pia, nilibaini kuwa vyeti vya kuzaliwa 368 vya watoto vilitolewa na kuandikishwa kwenye rejista ya maombi na utoaji wa vyeti lakini havikuonekana kuchapishwa kwenye Mfumo wa Usajili wa CRS. Sikuweza kuhakiki nakala 50 za vyeti vya ndoa vyenye thamani ya Sh. 2,500,000 na vitabu vya ndoa 16 vyenye thamani ya Sh. 12,380,000 vilivyotolewa kwa Msajili wa Wilaya Dodoma kuanzia mwezi Januari 2018 hadi Aprili 2020.

**Ukaguzi Maalumu juu ya Tuhuma za Ubadhirifu wa Kodi ya Zuio Iliyokusanywa na Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA)**

Nilibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA) ilikokotoa kimakosa kodi ya zuio ya Sh.11,217,209.93. Pia, nilibaini kuwa Kodi ya zuio kwa Kamishna wa Kodi za Ndani wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) jumla ya Sh. 709,152,607.07 zilichukuliwa na Mtunza fedha wa TEMESA kwa kushirikiana na wafanyakazi wa mojawapo ya benki ya kibiashara.

Wahusika hawa walighushi saini za watoa fedha na kubadilisha hundi iliyofungwa kuwa wazi na kuchukua fedha taslimu kutoka akaunti ya benki ya Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA). TEMESA ilikusanya Sh. 866,160,442.04 ambayo haikuwasilishwa kwa Kamishna wa Kodi za Ndani wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ikiwamo Sh. 709,152,607.07 zilizochukuliwa kwa njia ya udanganyifu na Mtunza fedha wa TEMESA na Hundi 53 kwa Kamishna wa Kodi za Ndani wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zenye thamani ya Sh. 157,007,834.97 ambazo TEMESA haikuwasilisha kipindi cha uchunguzi.

**Ukaguzi Maalumu wa Fedha za Ruzuku na Mali za Chama cha NCCR-Mageuzi**

Msajili wa Vyama vya Siasa hakuthibitisha ruzuku ya Sh, 230,518,993.31 ambayo NCCR Mageuzi ilidai kuwa imepokea kama ruzuku toka serikalini. Pia, nilibaini kuwa mapato ya jumla ya Sh. 326,411,508 yaliyokusanywa na Chama cha NCCR-Mageuzi hayakuwekwa benki kinyume na Kifungu Na. 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019. Pia, nilibaini mapato ya Sh. 10,700,000 ambayo Chama cha NCCR-Mageuzi kiliyapokea bila ya kutoa Stakabadhi. Pia, nilibaini viwanja vitatu vinavyomilikiwa na Chama cha NCCR-Mageuzi ambavyo taarifa katika Ofisi za Ardhi zinaonesha kumilikiwa na watu binafsi; na havina Hatimiliki.

Pia, nilibaini viwanja saba ambavyo Baraza la Wadhamani la Chama cha NCCR-Mageuzi halikutunza nyaraka zake; na sasa Chama cha NCCR-Mageuzi kimepoteza haki ya umiliki. Pia, nilibaini nyumba mbili zilizopo Bunju B Kinondoni, Dar es Salaam na viwanja vilivyopo Zanzibar na Kigoma vilivyonunuliwa na Chama cha NCCR-Mageuzi kati ya mwaka 2002 hadi 2015 ambavyo taarifa zake hazikuandikishwa kwenye rejista za mali za Chama.

Chama cha NCRR-Mageuzi hakikuwasilisha matamko ya mali za chama kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuanzia mwaka 1992/93 hadi 2015/16, kinyume na Kifungu Na. 14(1) (a) ya Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019. Nilibaini bakaa ya mikopo ya jumla ya Sh. 190,925,500 kutoka kwa wanachama wanne na Taasisi moja ambayo Chama cha NCCR-Mageuzi hakikuwasilisha rejista ya mikopo, mikataba na mihtasari ya Kamati Kuu iliyoidhinisha kupokelewa kwa mikopo hiyo. Hakukuwa na ushahidi ulioonesha kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi kilipokea mikopo hiyo. Hivyo, sikuweza kuthibitisha uhalali wa mikopo iliyotajwa.

Pia, nilibaini kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi kililipa mkopo wa Sh. 86,000,000 wa mmojawapo wa wanachama wake licha ya kutoa mkopo wa Sh. 65,000,000 kwa Chama. Nilibaini malipo ya jumla ya Sh. 45,637,500 kutoka kwa wanachama watatu na Sh. 4,500,000 kwa Taasisi moja ikisemekana ni marejesho ya mkopo licha ya kutokuwapo kwa ushahidi wa kupokelewa kwa mikopo hiyo. Nilibaini kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi kiliuza nyumba yake iliopo mjini Tarime bila ya kufuata taratibu za uuzaji

zilizobainishwa kwenye Katiba ya Chama cha NCCR-Mageuzi ya mwaka 2014. Nilibaini kuwa aliyekuwa Katibu Mkuu alijipatia kiudanganyifu Sh. 10,000,000 za uuzaji wa nyumba ya chama huko Tarime.

Nilibaini kuwa mmojawapo wa viongozi wa Chama ilijimilikisha nyumba za Chama na kuzigawa kwa rafiki yake. Aidha, nilibaini utata wa umiliki wa shamba la hekari 56 lililopo Kijiji cha Kiromo, Bagamoyo kati ya Chama cha NCCR-Mageuzi na Kiongozi huyo. Kiongozi huyo aliuza hekari 47 kwa Sh. 164,500,000 kwa Kampuni moja. Hata hivyo, kiongozi huyo hakuwasilisha nyaraka za kuonesha ushahidi wa umiliki wa shamba hilo. Hivyo, ni ukweli kuwa Kiongozi huyo si mmiliki wa Shamba hilo licha ya nyumba hiyo pia kutomilikiwa na Chama cha NCCR-Mageuzi. Rejea Sura ya 12 ya ripoti hii kwa maelezo ya Kina.

**Mapendekezo**

a) Ninapendekeza mifumo ya udhibiti wa ndani wa Wizara, Idara, Wakala na Mifuko Maalumu iimarishwe pamoja na watumishi kubadilishiwa majukumu yao mara kwa mara ili kuepukana na vitendo vya wizi na ubadhirifu wa fedha za umma;
b) Ninapendekeza hatua stahili za nidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika kwenye ubadhirifu wa fedha za umma na pale penye ulazima, wahusika hao warejeshe kiasi husika na kiwekwe kwenye mfuko mkuu wa Serikali; na
c) Ninawahimiza Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara, Wakala na Mifuko Maalumu kusimamia na kufatilia kwa ukaribu miradi ya ujenzi ili kupunguza hasara zinazojitokeza na zisizokuwa na ulazima ambazo huwaumiza walipa kodi.

# SURA YA KWANZA

# MAELEZO YA AWALI

## 1.1 Utangulizi

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) inayofahamika pia kama Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania ni Taasisi ya juu ya ukaguzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi hii ina wajibu wa kukagua taasisi katika sekta ya umma. Pia, ina jukumu la kutoa ripoti yenye tija, ushauri kwa serikali na kulihakikishia Bunge, Watanzania, Washirika wa maendeleo na wadau wengine kwamba usimamizi wa fedha za umma na rasilimali nyingine umezingatia ipasavyo, sheria na kanuni zinazohusika. Ofisi hii inaongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

### 1.1.1 Mamlaka

Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanatokana na Ibara ya 143 (2) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa); ambapo pamoja na mambo mengine, inamtaka CAG, kukagua akaunti za Serikali, za Bunge na za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania angalau mara moja kila mwaka na kuwasilisha kwa Rais kila ripoti ya ukaguzi. Baada ya kupokea ripoti ya ukaguzi Rais atamuelekeza mtu husika kuwasilisha ripoti hizo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kwa namna Katiba inavyoongoza.

Mamlaka yangu ya kikatiba yananiruhusu kutekeleza majukumu yangu bila kuingiliwa na mtu wala taasisi yoyote. Kifungu cha 15 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kimenipa uhuru usiozuilika wa kupata taarifa au nyaraka toka kwa watu, kompyuta na mifumo mingine ya taarifa kwa kiwango kinachofaa ili kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi na uweledi. Kifungu cha 17 cha Sheria hiyo hiyo kimenipa mamlaka ya kuamua mawanda na kiwango cha ukaguzi kitakachozingatiwa katika utekelezaji wa majukumu yangu kikatiba.

Hali kadhalika, Kifungu cha 48 (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinanitaka kujumuisha katika ripoti zangu, taarifa ya namna taasisi za Umma zilivyozingatia sheria na kanuni za ununuzi wa umma

baada ya kufanya tathmini ya taratibu na michakato ya manunuzi katika taasisi hizo.
Kama Mkuu wa Taasisi ya Juu ya Ukaguzi nchini, ninayakubali na kuyatekeleza majukumu na mamlaka yangu kwa mujibu wa sheria kwa kuhakikisha natoa ripoti za ukaguzi zenye ubora wa hali ya juu ili kuiwezesha Serikali na Taasisi zake kuwajibika kwa umma.

### 1.1.2 Madhumuni ya Ukaguzi

Nimefanya ukaguzi ili niweze kutoa maoni huru kwa taarifa za fedha za taasisi za serikali iwapo zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya Uhasibu vinavyotumika katika Sekta ya Umma ambavyo havizingatii fedha taslimu (IPSAS Accrual Basis). Pia, nimefanya ukaguzi ili kupata uhakika kuhusu taarifa za fedha kama hazina dosari kutokana na udanganyifu au makosa katika kuandaa taarifa hizo.

Kutoa uhakika kwa ubora wa hesabu (reasonable assurance) ni kiwango cha juu cha uhakika iwapo hesabu zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango, taratibu na sheria. Hata hivyo hii haina maana kwamba ukaguzi uliofanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya ukaguzi vinavyotumika na Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAIs) utabaini dosari zote ikiwa dosari hizo zipo. Dosari zinaweza kutokea kwa sababu ya udanganyifu au makosa, ambayo kwa ujumla wake yanaweza kuathiri maamuzi muhimu kwa watumiaji wa taarifa za fedha. Kwa hiyo, hatari ya kutokugundua dosari kutokana na udanganyifu ni kubwa kuliko ilivyo kwa dosari zilizotokana na makosa, kwani udanganyifu unaweza kuhusisha ushirika, uwongo, upungufu wa makusudi, taarifa zisizo sahihi au upuuzwaji wa udhibiti wa ndani.

Aidha, ukaguzi wangu ulilenga kutathmini endapo sheria na kanuni zinazotumika zimezingatiwa. Zaidi, ulilenga kutathmini kama Maafisa Masuuli wamebuni na kutekeleza udhibiti wa ndani ulio madhubuti utakaoweza kuzuia dosari au kuzibaini mara tu zinapotokea.

## 1.2 Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika

Nilifanya ukaguzi wangu kulingana na Viwango kubalifu vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za juu za Ukaguzi (INTOSAI) na taratibu zingine ambazo niliona ni muhimu katika kufanya ukaguzi. Viwango hivi vinanihitaji nizingatie

mahitaji ya kimaadili ya upangaji na utekelezaji wa ukaguzi ili kupata uhakika uliojitosheleza kama taarifa za fedha nilizokagua hazina dosari.

## 1.3 Mbinu za Ukaguzi

Utaratibu wa ukaguzi umejumuisha ukaguzi wa taarifa za kihasibu na taratibu zingine ili kukidhi malengo ya ukaguzi. Taratibu hizo ni pamoja na zifuatazo:

- Kupanga ukaguzi ili kubaini na kutathmini hatari za dosari za taarifa za fedha, iwe ni kutokana na udanganyifu au makosa, kwa msingi wa uelewa wa taasisi na mazingira yake, pamoja na udhibiti wa ndani wa taasisi;
- Kupata ushahidi wa kutosha kuhusu kuwapo kwa dosari katika taarifa za fedha; na hii ni kwa kubuni na kutekeleza mwitikio wa udhibiti wa vihatarishi;
- Kutoa maoni juu ya taarifa za fedha kulingana na hitimisho lililotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana; na
- Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotokana na kaguzi za miaka iliyopita pamoja na maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ili kuhakikisha kuwa hatua sahihi zimechukuliwa kwa masuala yote yaliyoainishwa.

## 1.4 Mawanda ya Ukaguzi

Wigo wa ukaguzi wangu unajumuisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kihasibu na udhibiti wa mfumo wa ndani katika shughuli za taasisi husika. Pia, unahusisha ukaguzi na uhakiki wa hesabu, na taratibu nyingine za kikaguzi ambazo nitaziona ni muhimu katika kukamilisha ukaguzi.

Ukaguzi wangu ulifanyika kwa njia ya sampuli. Hivyo, matokeo yake yamewekwa kwa kiwango ambacho kumbukumbu, nyaraka na taarifa nilizoomba kwa madhumuni ya ukaguzi ziliwasilishwa kwangu. Matokeo ya ukaguzi na maoni yametokana na mapitio ya nyaraka za uhasibu, tathmini ya shughuli hizo pamoja na kutathmini Mfumo wa Udhibiti wa Ndani ambao unahitaji uangalizi na usimamizi. Matokeo hayo yameanishwa katika ripoti ya Mapungufu iliyotolewa kwa uongozi wa kila Taasisi husika.

Jukumu la kugundua na kuzuia udanganyifu na makosa ni wajibu wa Uongozi wa taasisi. Kama Mkaguzi, sio wajibu wangu kutafuta udanganyifu; na kwa hivyo, ukaguzi wangu hauwezi kutegemewa kufichua mambo yote

ya udanganyifu. Hata hivyo, niliupanga ukaguzi wangu kwa namna ambayo ningegundua dosari zilizotokana na makosa au udanganyifu.
Kwa hivyo, matokeo yaliyomo katika ripoti Kuu ya Ukaguzi ya mwaka yasichukuliwe kama yanawakilisha mapungufu yote yaliyopo katika mifumo ya kifedha na usimamizi, au katika kubainisha maboresho yote ambayo yanaweza kufanyika katika mifumo na taratibu zilizopo.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya Taasisi 306 za Serikali Kuu zilipaswa kuwasilisha taarifa zao za fedha kwa ajili ya ukaguzi kama inavyotakiwa na Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001 na kanuni ya 71 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009. Kati ya hizo, Taasisi 263 zilikaguliwa na kutengeneza msingi wa ripoti hii. Tofauti ya Taasisi 43 kati ya zilizopaswa kukaguliwa dhidi ya zilizokaguliwa imetokana na kwamba nilishindwa kukagua Balozi na Misheni 42 kutokana na janga la ugonjwa wa Covid-19 uliosababisha kuzuia safari za kimataifa na taasisi moja[1] ambayo ukaguzi wake ulikuwa unaendelea wakati wa maandalizi ya Ripoti hii.

Idadi ya Taasisi zilizopaswa kukaguliwa zimeongezeka kutoka Taasisi 299 katika mwaka 2018/19 hadi 306 katika mwaka 2019/20. Ongezeko hilo linatokana na kuwapo kwa Taasisi mpya 11 na kuondolewa kwa Taasisi tatu zilizositisha utendaji wake pamoja na Taasisi moja ambayo kwa mwaka wa fedha 2019/20 ilikaguliwa na kuripotiwa chini ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma. Orodha ya Taasisi mpya zilizoanzishwa na kuripotiwa na katika Ripoti ya Serikali Kuu ni kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 1** hapa Chini;

**Jedwali Na. 1: Orodha ya Taasisi Zilizoandaa Taarifa za Fedha kwa Mara ya Kwanza kwa Mwaka 2019/20**

| Na | Taasisi | Aina |
|---|---|---|
| **1.** | Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini | Wakala |
| 2. | Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka- Mafinga | Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka |
| **3.** | Hospitali ya Rufaa ya Kanda-Mbeya | Hospitali ya Rufaa ya Kanda |
| **4.** | Hospitali Maalumu ya Benjamin Mkapa | Hospitali Maalumu |
| 5. | Hospitali Maalumu ya Magonjwa ya Kuambukiza | Hospitali Maalumu |

[1] *Mfuko wa Maendeleo ya Vijana*

| Na | Taasisi | Aina |
|---|---|---|
| | Kibong'oto | |
| **6.** | Hospitali Maalumu ya Mirembe | Hospitali Maalumu |
| **7.** | Chuo cha Ardhi Tabora | Taasisi Nyingine |
| 8. | Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora | Taasisi Nyingine |
| **9.** | Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) | Taasisi Nyingine |
| 10. | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) | Taasisi Nyingine |
| 11. | Kituo cha Jemolojia Tanzania | Taasisi Nyingine |

*Chanzo: Ripoti za Ukaguzi za CAG mwaka 2019/20*

Licha ya ukaguzi wa taarifa za hesabu, Ibara ya 143(2) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 5(a) cha Sheria ya ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 vinamtaka CAG kuidhinisha utumiaji wa fedha zinazolipwa kutoka Mfuko Mkuu akiwa ameridhika kuwa Ibara ya 136 ya Katiba imefuatwa au kutimizwa. Kwa matakwa hayo, ripoti hii imejumuisha matokeo ya kaguzi zifuatazo:

Katika mwaka wa ukaguzi, majalada 2686 ya pensheni yaliwasilishwa kwa ukaguzi, kati ya hayo majalada 2502 yalifanyiwa ukaguzi wa awali. Kati ya hayo niliidhinisha, majalada 2328 kwa malipo. Maelezo ya kina ya ukaguzi huu yanapatikana katika Sura ya Tano ya ripoti hii.

Kifungu cha tisa cha Sheria ya Mfuko wa Mendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009 kinanitaka kukagua na kutoa ripoti kuhusu fedha zilizopokelewa kwenye Mfuko wa Jimbo wa Miradi ya Maendeleo. Nilitimiza majukumu yangu ya ukaguzi wa shughuli za mfuko huo kwa upande wa Zanzibar kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni,2020. Sura ya nane ya ripoti hii inaonyesha matokeo ya ukaguzi kwa majimbo 11 ya Zanzibar.

Michakato bora ya manunuzi na usimamizi imara wa mikataba ni muhimu katika kupata matokeo bora yaliyokusudiwa na serikali kupitia utumiaji wa rasilimali za umma. Mbali na ukaguzi wa kawaida wa tathmini ya taratibu za manunuzi ya umma katika taasisi zote za serikali, nilifanya ukaguzi wa kina wa michakato ya Manunuzi na usimamizi wa mikataba katika Ofisi za RUWASA katika wilaya 36 kwenye mikoa 19 ili kutathmini kwa kina ufanisi wa mifumo katika usimamizi wa miradi ya maji katika kutekeleza matumizi bora ya rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya malengo

yaliyokusudiwa. Matokeo ya kina ya kaguzi hizi yamejumuishwa katika Sura ya tisa ya ripoti hii.

Zaidi, ikumbukwe kwamba tarehe 24 Novemba 2019, uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulifanyika katika ngazi anuwai nchini. Nilifanya ukaguzi juu ya uwajibikaji na matumizi ya fedha zilizotumiwa katika chaguzi hizo na matokeo ya kina ya ukaguzi huo yamejumuishwa katika Sura ya Kumi ya ripoti hii.

Aidha, Kifungu cha 29 cha Sheria ya ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na kanuni ya 79 (1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 inampa mamlaka CAG kufanya ukaguzi maalumu kutokana na ombi lililoletwa kwa maandishi kutoka kwa Afisa Masuuli, au mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara inayojitegemea, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa au chombo kingine chochote. Kwa kuongezea, kwa mujibu wa kanuni ya 78 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009, CAG anaweza kufanya ukaguzi maalumu wa taasisi yoyote ya Umma pale anapoona inafaa. Taarifa hii pia imejumuisha matokeo ya kaguzi maalumu 8 zilizoombwa na wadau mbalimbali na zile zilizoanzishwa na ofisi yangu. Hata hivyo, ripoti hii haijabainisha matokeo ya kaguzi 7 zilizoombwa na TAKUKURU. Orodha ya kaguzi maalumu zilizofanyika ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.** Matokeo ya kina ya kaguzi hizi yameainishwa katika sura ya 12 ya ripoti hii.

**Jedwali Na. 2: Orodha ya Kaguzi Maalumu Zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/20**

| Na | Jina la Ukaguzi Maalumu | Taasisi iliyoomba ukaguzi |
|---|---|---|
| 1. | Ukaguzi maalumu kuhusu Tozo ya Maendeleo ya Utalii, Tamasha la Urithi na Uanzishwaji wa chaneli ya Tanzania Safari na Kituo cha Kurusha Masafa ya Kidigitali | CAG |
| 2. | Ukaguzi Maalumu wa ujenzi wa uzio wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba | TAKUKURU |
| 3. | Ukaguzi maalumu kuhusu matumizi ya Fedha za kutekeleza miradi ya upangaji wa matumizi ya ardhi | CAG |
| 4. | Ukaguzi Maalumu wa ujenzi wa Shule ya Msingi Tumaini Bukoba | TAKUKURU |
| 5. | Ukaguzi maalumu unaohusu ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mazoezi ya Patandi iliyopo Chuo Cha Ualimu Elimu Maalumu | TAKUKURU |

| Na | Jina la Ukaguzi Maalumu | Taasisi iliyoomba ukaguzi |
|---|---|---|
| | Patandi Mkoa wa Arusha. | |
| 6. | Ukaguzi Maalumu wa mali za Chama cha Wananchi CUF na ACT-WAZALENDO | Msajili wa Vyama vya Siasa |
| 7. | Ukaguzi maalumu juu ya Matumizi yaliyofanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kutoka kwenye Ruzuku Iliyotolewa na Dhamana ya Kuimarisha Sekta ya Fedha (FSDT) | NIDA |
| 8. | Ukaguzi Maalumu kuhusu matumizi mabaya ya fedha za UNICEF kwenye idara ya Ustawi wa Jamii katika Wizara ya Afya, maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. | UNICEF |
| 9. | Ukaguzi maalumu kwenye Mfumo wa Usajili wa Raia uliofanyika katika Ofisi ya RITA Dodoma | CAG |
| 10. | Ukaguzi Maalumu katika ununuzi wa Dawa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya | TAKUKURU |
| 11. | Ukaguzi Maalumu kwenye mikataba inayohusiana na Huduma za Kiushauri katika Usanifu wa Kina na Usimamizi wa Upanuzi wa Bomba la Maji linaoelekea katika Miji ya Tabora, Nzega na Igunga(Awamu ya kwanza na pili) chini ya Wizara ya Maji | TAKUKURU |
| 12. | Ukaguzi Maalumu wa tuhuma zinazohusiana na upotevu wa kodi ya zuio iliyokusanywa na TEMESA kuanzia Mwezi Julai, 2015 mpaka Juni 2020 | Waziri Mkuu |
| 13. | Ukaguzi Maalumu wa fedha za ruzuku na Mali zinazomilikiwa na Chama cha NCCR- MAGEUZI | Msajili wa Vyama vya Siasa |
| 14. | Ukaguzi Maalumu wa Malipo ya Fidia kwa Moja ya Familia Iliyopo Tegeta-Ununio,Dar Es Salaam Yaliyolipwa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi | TAKUKURU |
| 15. | Ukaguzi Maalumu wa Mradi wa Ukarabati wa Majengo, Mifumo ya maji na majitaka, Miundombinu Ya Tehama Na Mifumo Ya Umeme Chuo Cha Ualimu Ilonga, Kilosa Mkoani Morogoro | TAKUKURU |

***Chanzo:****Ripoti za kaguzi maalumu.*

# SURA YA PILI

## HATI ZA UKAGUZI

### 2.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Viwango vya Ukaguzi wa Umma vya Kimataifa vinavyozingatiwa na Taasisi za Juu za Ukaguzi, hususani (ISSAI 1700), inataja kuwa lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maoni huru kwa kupitia Hati za Ukaguzi kuwa taarifa za fedha zilizoandaliwa zimeonesha usahihi wa hali ya Taasisi iliyokaguliwa katika mwaka wa fedha husika.Aidha, inatoa hakikisho kwa watumiaji kuwa taarifa hizo zimetayarishwa kulingana na viwango kubalifu vya kitaaluma.

Hati za Ukaguzi huchukuliwa kama taarifa muhimu wakati wa kutoa hakikisho la usahihi wa taarifa za fedha kwa watumiaji. Katika sekta ya umma, hulenga kulishauri Bunge na wadau wengine kuwa, Hesabu na Taarifa za Fedha zilizokaguliwa zimeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma kwa msingi usio wa fedha taslimu (IPSAS Accrual), na kwa kuzingatia kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2004).

### 2.2 Aina za Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne za Hati ya Ukaguzi na kila moja hutolewa kulingana na ushahidi uliokusanywa wakati wa ukaguzi.

#### 2.2.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa na Mkaguzi pale anaporidhika kuwa Taarifa za Fedha alizokagua zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango kubalifu vya kimatiafa vinanyohusu uandaaji wa Taarifa za Fedha.

### 2.2.2 Kundi la Hati Zenye Kasoro[2]

Hati za Ukaguzi zilizopo kwenye kundi hili zinatolewa pale ambapo mkaguzi ameshidwa kutoa Hati inayoridhisha. Hati zilizopo kwenye kundi hili zimegawanywa katika aina tatu kama ilivyoonyeshwa hapa chini;

#### 2.2.2.1 Hati Yenye Shaka

Hati Yenye Shaka hutolewa pale ambapo mkaguzi amepata vielelezo vya kutosha na kuhitimisha kwamba Taarifa za Fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa kuzingatia mahitaji ya viwango na miongozo husika isipokuwa kwa athari ya baadhi ya masuala yaliyobainika na ambayo litafafanuliwa kwenye taarifa husika. Pia, Hati yenye shaka hutolewa pale ambapo Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ameshindwa kupata vielelezo/ushahidi wa kuthibitisha usahihi wa Taarifa za Fedha zilizoandaliwa na amejiridhisha kuwa madhara yanayoweza kutokana na kukosekana kwa vielelezo/ushahidi huo yanaweza kuathiri usahihi wa taarifa hizo za fedha.

#### 2.2.2.2 Hati Mbaya (Adverse Opinion)

Hati isiyoridhisha hutolewa pale ambapo Mkaguzi amepata ushahidi na vielelezo vya kutosha kuwa dosari zilizobainika wakati wa ukaguzi kwa ujumla wake zina mapungufu makubwa na ya msingi katika usahihi wa Taarifa za fedha husika.

#### 2.2.2.3 Kushindwa Kutoa Maoni (Disclaimer of Opinion)

Hati hii hutolewa pale ambapo mkaguzi anaposhindwa kupata ushahidi na vielelezo vinavyo jitosheleza vinavyohusiana na Taarifa za Fedha zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hati ya aina hii inapotolewa inamaanisha kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameshindwa kutoa maoni yake kutokana na dosari hizo.

[2] Mwaka huu majina ya hati za Ukaguzi yamebadilika. Kwa miaka iliyopita, **"Adverse Opinion"** illiitwa **"Hati Isiyoridhisha"** na **"Disclaimer of Opinion"** iliitwa **"Hati Mbaya".** Kwa mwaka huu, **"Adverse Opinion"** imeitwa **"Hati Mbaya"** na **"Disclaimer of Opinion"** imeitwa **"Kushindwa kutoa Maoni".** Mabadiliko haya yametokea kwa kuzingatia kuwa majina mapya yanaakisi zaidi maana halisi ya hati zilizotolewa.

## 2.3 Masuala yenye Msisitizo (Emphasis of Matter) na Mambo Mengineyo (Other Matter)

Pale inapofaa, ripoti ya mkaguzi juu ya taarifa za kifedha inaweza kujumuisha aya yenye maswala yenye msisitizo. Aya hizo, hazibadilishi hati (Hati zenye kasoro) na hazibadilishi maoni zaidi (kwa maoni yaliyobadilishwa) aidha pia Aya hiyo haibadilisho maoni yaliyotolewa juu ya Taarifa za fedha zilizoandaliwa.

### 2.3.1 Aya ya Masuala yenye Msisitizo (Emphasis of Matter)

Aya hii inajumuishwa katika ripoti ya ukaguzi ikirejelea maswala yaliyowasilishwa ipasavyo au kufichuliwa katika taarifa za kifedha kwamba, kwa maoni ya kitaalam ukaguzi umeona umuhimu wa kuwaeleza watumiaji wa taarifa za kifedha. Aya hii imejumuishwa katika ripoti ya ukaguzi kwa kichwa cha Habari kijulikanacho kama **'masuala yenye msisitizo'**

### 2.3.2 Mambo Mengineyo (Other Matter)

Aya hii inajumuishwa katika ripoti ya ukaguzi ili kuweka mkazo kwenye masuala mengine nje ya yale yaliyofafanuliwa katika taarifa za Fedha ikiwemo maoni ya kitaalamu pale ambapo ukaguzi uliofanyika umeona kuna umuhimu wa kuwafahamisha watumiaji wa Taarifa za fedha. Aya hii imejumuishwa katika ripoti ya ukaguzi ikiwa na kichwa cha Habari **'Mambo mengineyo'**

## 2.4 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilikamilisha kaguzi za Taasisi 263 za Serikali Kuu na kutoa Hati za ukaguzi kwa Taasisi zote 260. Sikutoa hati ya ukaguzi kwa Taasisi tatu ikijumuisha Vyama viwili vya siasa na Wizara Moja. Sikuweza kutoa hati ya Ukaguzi kwa vyama hivyo vya siasa kwa sababu vilishidwa kuandaa na kuwasilisha Taarifa za Fedha, hivyo ukaguzi wangu uliangalia mifumo ya udhibiti wa ndani pekee, aidha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mahariki (Fungu 34) haikuweza kupewa Hati ya Ukaguzi kwasababu ya Mlipuko wa ugojwa wa COVID 19 ambapo nchi nyingi zilizuia safari na kufunga mipaka yake. Sehemu kubwa ya Taarifa ya Fedha inajumuisha taarifa ya fedha ya Balozi 43 ambazo hazikukaguliwa katika Mwaka huu wa Fedha.

Kati ya Taasisi 260 nilizokagua taarifa zake za fedha, Taasisi 239 zilipata Hati Inayoridhisha, Taasisi 10 zilipata Hati Yenye Shaka, mbili zilipata Hati

Mbaya na hazikupata maoni ya ukaguzi. Aidha, kati ya Hati 239 zinazo ridhisha, Hati 22 zina Masuala Yenye Msisitizo.

Orodha ya Taasisi zilizokaguliwa pamoja na Hati za ukaguzi zilizotolewa zimmeoneshwa katika **Kiambatisho Na. I** wakati sababu zilizopelekea kutolewa kwa Hati Zenye Shaka, Hati Mbaya na Kushindwa Kutoa Hati kwenye **Kiambatisho Na. II, Kiambatisho Na. III na Kiambatisho Na. IV mtawalia.**

## 2.5 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Taasisi zilizopo katika Serikali Kuu kwa kipindi cha miaka mitatu toka mwaka 2017/2018 mpaka 2019/2020 unaonyeshwa katika **Jedwali Na. 3**

**Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi**

| ***Hati*** | ***Inayoridhisha*** | | | ***Yenye Shaka*** | | | ***Mbaya*** | | | ***Kushindwa Kutoa Maoni*** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Mwaka*** | ***2019/20*** | ***2018/19*** | ***2017/18*** | ***2019/20*** | ***2018/19*** | ***2017/18*** | ***2019/20*** | ***2018/19*** | ***2017/18*** | ***2019/20*** | ***2018/19*** | ***2017/18*** |
| *Wizara na Idara* | 64 | 61 | 61 | 0 | 4 | 4 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| *Sekretarieti za Mikoa* | 26 | 26 | 26 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| *Wakala* | 31 | 32 | 32 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| *Mifuko Maalumu* | 14 | 16 | 16 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Bodi za Mabonde Maji | 15 | 14 | 14 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| *Hospitali za Rufaa* | 28 | 22 | 0 | 3 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| *Vyama vya Siasa* | 4 | 3 | 3 | 4 | 1 | 4 | 0 | 3 | 2 | 9 | 12 | 5 |
| *Taasisi Nyingine* | 53 | 42 | 41 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |

| Hati | Inayoridhisha | | | Yenye Shaka | | | Mbaya | | | Kushindwa Kutoa Maoni | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
| Hesabu Jumuifu za Taifa | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| *TRA* | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ***Jumla*** | **239** | **218** | **197** | **10** | **19** | **9** | **2** | **4** | **2** | **9** | **12** | **6** |

*Chanzo*: *Ripoti za Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2017/18 mpaka 2019/20*

Kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 3** hapo juu, kwa ujumla utendaji wa Taasisi zilizokaguliwa umeonesha mwelekeo mzuri kutokana na kuongezeka kwa Hati zenye kuridhisha kutoka Hati 218 zilizotolewa mwaka uliopita hadi Hati 239 zilizotolewa mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la Taasisi 21 (10%). Pia, idadi ya Taasisi zilizopata Hati zenye kasoro (modified opinion) zimepungua kutoka hati 35 hadi 21 ikilinganishwa na Mwaka uliopita.

## 2.6 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Vyama vya Siasa

Vyama vya Siasa vimeendelea kuonesha mapungufu na kutofuata taratibu za uandaaji wa hesabu zinazokubalika. Kati ya vyama vya siasa 19, vyama 17 vilikaguliwa na kupata Hati ya Ukaguzi. Vyama vinne[3] pekee viliweza kuandaa na kuwasilisha hesabu kulingana na viwango kubalifu vya kimataifa vya uhasibu wa Sekta ya Umma (IPSAS-Accrual), hivyo kupata hati zinazoridhisha ikilinganishwa na hati tatu za mwaka uliopita. Vyama vyote 13 vilivyobaki vilipata hati zenye kasoro kwa viwango mbali mbali.

Vyama vinne vilipata Hati Yenye Shaka ikilinganishwa na chama kimoja kwa mwaka uliopita. Hakuna Chama kilichopata Hati Mbaya, ikilinganishwa

[3] ACT Wazalendo, CCM, CHADEMA na NCCR Mageuzi

na hati tatu za mwaka uliopita, Pia, sikutoa maoni ya Ukaguzi kwa Vyama tisa, ikilinganishwa na vyama 12 kwa mwaka uliopita.

Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Vyama vya Siasa kwa miaka mitatu mfululizo toka mwaka 2017/18 mpaka 2019/20 unaoneshwa katika **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Miaka Mitatu Mfululizo**

| Na | Jina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ACT WAZALENDO | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka |
| 2 | African Democratic Alliance (ADA-TADEA) | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni |
| 3 | Alliance For African Farmers Party (AAFP) | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni |
| 4 | Alliance for Democratic Change (ADC) | Siktutoa Maoni | Sikutoa Maoni | Hati Inayoridhisha |
| 5 | Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka |
| 6 | Chama Cha Kijamii (CCK) | Hati Yenye Shaka | Hati Yenye Shaka | Hati Yenye Shaka |
| 7 | Chama Cha Mapinduzi(CCM) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 8 | Chama cha Sauti ya Umma (SAU) | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni |
| 9 | Chama Cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) | - | Sikutoa Maoni | Hati Mbaya |
| 10 | Civic United Front (CUF) | Hati Yenye Shaka | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni |
| 11 | Demokrasia Makini | Sikutoa Maoni | Hati Mbaya | Hati Mbaya |
| 12 | Democratic Party (DP) | - | Sikutoa Maoni | Hati Inayoridhisha |
| 13 | National League for Democracy (NLD) | Hati Yenye Shaka | Hati Mbaya | Hati Mbaya |
| 14 | National Reconstruction Alliance (NRA) | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni |
| 15 | NCCR- Mageuzi | Hati Inayoridhisha | Hati Mbaya | Hati Yenye Shaka |
| 16 | Tanzania Labour Party (TLP) | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni | Hati Inayoridhisha |
| 17 | Union for Multi-Party Democracy (UMD) | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni | Sikutoa Maoni |
| 18 | United Democratic | Hati Yenye | Sikutoa Maoni | Hati |

| Na | Jina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|
| | Party (UDP) | Shaka | | Inayoridhisha |
| **19** | United Peoples' Democratic Party (UPDP) | Sikutoa Maoni | Hati Mbaya | Hakikukaguliwa |

*Chanzo*: Ripoti za Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2017/18 mpaka 2019/20

Ukaguzi wangu umebaini mambo kadhaa yanayosababisha Vyama vya Siasa kushidwa kuandaa hesabu kwa mujibu wa viwango kubalifu vya uandaaji wa hesabu. Nazo zinajumuisha;

- Upungufu katika udhibiti wa utunzaji nyaraka na taarifa sahihi za kifedha. Hii hupelekea ugumu wakati wa ukaguzi kuweza kuthibitisha uhalali wa taarifa zilizoripotiwa katika hesabu. Kwa hivyo, sikuweza kupata ushahidi sahihi na toshelezi ili kutoa msingi wa maoni ya ukaguzi juu ya hesabu hizi; na
- Vyama vya Siasa kukosa wafanyakazi wenye uwezo, ujuzi na taaluma ya kuandaa hesabu. Ndio maana, kwa mara nyingine ukaguzi wangu ulibaini mapungufu katika uandaaji wa taarifa za fedha zenye dosari nyingi na zisizofaa kutumiwa na Umma.

**Napendekeza Viongozi wa Vyama vya Siasa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha taratibu za utunzaji wa nyaraka na taarifa muhimu za masuala ya fedha zinaboreshwa. Pia, narudia pendekezo langu nililolitoa mwaka uliopita kwamba Viongozi wa vyama vya Siasa waajiri/kushirikisha watu wenye taaluma na sifa stahiki kwenye uandaaji wa hesabu kulingana na Miongozo kubalifu ya uandaaji wa hesabu hizo.**

## 2.7 Ripoti ya Uzingatiwaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma.

Pamoja na Ukaguzi wa hesabu, ukaguzi wangu pia uliangazia tathmini ya uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za ununuzi ya umma pamoja na ufanisi wa Mifumo ya udhibiti wa ndani kama Kiwango cha Kimataifa cha Taasisi za Ukaguzi za Juu (ISSAI) Na. 4200 kinavyotaka. Pia, Kifungu Na. 48(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.7 ya mwaka 2011 kinanihitaji kueleza katika ripoti yangu ya ukaguzi ya kila mwaka kama Taasisi niliyoikagua imezingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake.

Kulingana na ukaguzi nilioufanya kwa mwaka wa fedha 2019/20 nilibaini mapungufu katika kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi. Baadhi ya

Taasisi zenye mapungufu zimeorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 5** hapa chini.

**Jedwali Na. 5: Baadhi ya Taasisi Ambazo Zina Mapungufu katika Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma**

| Na | Aina | Taasisi |
|---|---|---|
| 1. | 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki |
| 2. | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania (TPDF) |
| 3. | 46 | Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi |
| 4. | 57 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa |
| 5. | 99 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi- Mifugo |
| 6. | Wakala | Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini (GPSA) |
| 7. | Wakala | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) |
| 8. | Wakala | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi Tanzania (TEMESA) |
| 9. | Wakala | Chuo cha Maji |
| 10. | Mfuko Maalumu | Mfuko wa Misitu Tanzania |
| 11. | Hospitali ya Mkoa ya Rufaa | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa- Amana |
| 12. | Hospitali ya Mkoa ya Rufaa | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa- Singida |
| 13. | Hospitali ya Mkoa ya Rufaa | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa- Songwe |
| 14. | Hospitali ya Kanda ya Rufaa | Hospitali ya Rufaa ya Kanda- Mbeya |
| 15. | Taasisi Nyingine | Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) |
| 16. | Taasisi Nyingine | SUMA JKT -Idara ya Ujenzi |

*Chanzo: Ripoti za Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20*

Maelezo zaidi juu ya kutofuata masharti ya sheria ya ununuzi yametolewa katika Sura ya Tisa ya ripoti hii.

## SURA YA TATU

## UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA

### 3.1 Utangulizi

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yangu ya miaka iliyopita katika kaguzi za hesabu, kaguzi maalum, majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kulingana na Kifungu Na. 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka, 2008, (na marekebisho yake ya mwaka 2013) na utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka wa fedha uliopita 2018/19, imebaini hatua mbalimbali za utekelezaji zilizochukuliwa na serikali ambazo zinawasilishwa katika sura hii.

Nimebaini kuwapo kwa kasi ndogo ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya Kamati ya PAC katika Taasisi zilizokaguliwa. Kutotekelezwa kwa mapendekezo yangu na maagizo ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa wakati kunaweza kusababisha kuendelea kujitokeza kwa mapungufu ya usimamizi wa mapato ya Serikali na matumizi ya mali ya Umma.

Aidha, vigezo vilivyotumika katika kutathmini hali ya utekelezaji wa mapendekezo na maagizo ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ya miaka iliyopita vimefafanuliwa katika **Jedwali Na. 6**;

**Jedwali Na. 6: Tafsiri ya Maneno Yaliyotumika katika Kutathmini Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo**

| Hali halisi | Maelezo |
|---|---|
| **Mapendekezo yaliyotekelezwa** | Mkaguliwa ametimiza kikamilifu mapendekezo na maelekezo, kama ilivyoelezewa katika Ripoti. |
| **Utekelezaji unaendelea** | Mkaguliwa ana mipango mahususi ya kuanza, au ameanza, kutekeleza pendekezo au ametimiza kiasi cha pendekezo na maagizo yaliyotolewa |
| **Mapendekezo hayajatekelezwa** | Mkaguliwa hajatimiza pendekezo hilo wala hajaonesha kuwa atafanya hivyo. |
| **Pendekezo limefutwa kutokana na kupitwa na wakati** | Mkaguliwa amejitahidi kwa kiasi kikubwa kwamba udhaifu wa zamani haufanyiki katika miaka iliyofuata au mapendekezo na maagizo hayana umuhimu tena kwa |

| Hali halisi | Maelezo |
|---|---|
| | utekelezaji kwa sababu ya muda kupita au utekelezaji wake hauwezekani sababu ya mabadiliko ya sheria, Vipaumbele vya Serikali na maagizo ya kisera |
| **Pendekezo limerudiwa** | Mkaguliwa hajatimiza pendekezo la zamani ambalo katika mwaka huu pendekezo hilo hilo lilitolewa kwa kuzingatia ukweli kwamba pendekezo hilo lina haja ya kurudiwa. Kwa hivyo, ili kuweka msisitizo, pendekezo limetolewa tena. |

## 3.2 Hali ya sasa ya Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka Uliopita kuhusu Wizara, Idara na Wakala.

Katika mwaka wa ukaguzi uliopita mwaka 2018/19, nimefuatilia hali ya utekelezaji wa mapendekezo yangu ya miaka iliyopita kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali 263 ambapo nilitoa jumla ya mapendekezo 5,483. Idadi ya mapendekezo kwa kila Taasisi imeonyeshwa kwa muhtasari katika **Jedwali Na. 7**

**Jedwali Na. 7: Idadi ya Mapendekezo kwa kila Taasisi**

| Taasisi | Idadi ya Taasisi | Idadi ya Mapendekezo |
|---|---|---|
| Wakala | 34 | 898 |
| Mifuko ya Fedha (Funds) | 14 | 115 |
| Taasisi Nyingine | 53 | 812 |
| Vyama vya Siasa | 19 | 286 |
| Hospitali Maalum na za Rufaa za Mikoa | 32 | 487 |
| Mafungu (Votes) | 66 | 1198 |
| Hesabu za Taifa | 4 | 586 |
| Sekretarieti za Mikoa | 26 | 854 |
| Ofisi za Mabonde ya Maji | 15 | 247 |
| **Jumla** | **263** | 5,483 |

*Chanzo: Ripoti za Taasisi Mwaka 2019/20*

Kupitia ufuatiliaji na tathmini juu ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita, nilibaini kuwa kati ya mapendekezo 5,483; mapendekezo 1,508 (27%) yalitekelezwa, mapendekezo 2,003 (37%) utekelezaji wake unaendelea, mapendekezo 1,211 (22%) hayakutekelezwa,mapendekezo 502 (9%) yamerudiwa na mapendekezo 259 (5%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati. Hali ya utekelezaji wa

mapendekezo yangu kwa miaka ya nyuma kwenye ripoti za Wizara, Idara na Taasisi za Serikali yamefupishwa katika **Kielelezo Na. 1**

**Kielelezo Na. 1: Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita kwa Taasisi za Serikali Kuu**




### 3.2.1 Mwenendo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Wizara, Idara na Wakala

Mapitio ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya miaka ya nyuma kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo yalibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2016/17 mapendekezo 4,282 yalisalia, mwaka 2017/18 mapendekezo 4,736 yalisalia, wakati katika mwaka wa fedha 2018/19 mapendekezo 5,483 yalisalia. Mwenendo wa mapendekezo kwa ujumla kwa miaka mitatu mfululizo yameonyeshwa kwenye **Kielelezo Na. 2**

**Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Jumla ya Mapendekezo kwa Miaka Mitatu Mfululizo**




Kama inavyoonyeshwa katika takwimu hapo juu, idadi ya mapendekezo yaliyotolewa inaongezeka kila mwaka. Hata hivyo, kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo haya hakiridhishi kwani ni mapendekezo 1,508 tu sawa na (28%) yaliyotekelezwa kwa mwaka 2018/19 wakati mapendekezo 1,474 sawa na (31%) na 1,459 sawa na (34%) tu yakitekelezwa mwaka 2017/18 na 2016/17, mtawalia. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka mitatu mfululizo imeonyeshwa katika **Jedwali Na. 8** hapa chini

**Jedwali Na. 8: Mwenendo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Mitatu**

| Hali halisi/Mwaka | 2018/19 | 2017/18 | 2016/17 |
|---|---|---|---|
| Mapendekezo yaliyotekelezwa | 1,508 | 1,474 | 1,459 |
| Mapendekezo yaliyo katika hali ya Utekelezaji | 2,003 | 1,588 | 1,626 |
| Mapendekezo Yasiyotekelezwa | 1,211 | 1,080 | 752 |
| Mapendekezo yaliyopitwa na wakati | 259 | 286 | 445 |
| Mapendekezo Yaliyorudiwa | 502 | 308 | - |
| **Jumla** | **5,483** | **4,736** | **4,282** |

## 3.3 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)

Kanuni ya 38 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 inamtaka Waziri mwenye dhamana kuandaa mpango wa hatua za utekelezaji wa

mapendekezo ya ukaguzi na kuuwasilisha kwa maandishi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea mapendekezo hayo.

Kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2013), kinawataka Maafisa Masuuli kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kwa ujumuishaji. Baadaye, hali ya utekelezaji ijumuishwe kwenye ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Ili kutekeleza kanuni tajwa hapo juu, Serikali kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG), iliwasilisha majibu ya mapendekezo yaliyotolewa na ripoti ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2019. Majibu ya mapendekezo yaliwasilishwa kwa barua yenye Kumb. Namba CHA.116 / 474/01/57 ya tarehe 2 Julai 2020. Majibu yaliyotolewa na Serikali kupitia ripoti ya Jumla ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019 inaonesha hatua mbalimbali za utekelezaji kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 9 na Kiambatisho Na. V**

**Jedwali Na. 9: Hali ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) katika Kutekeleza Mapendekezo yangu kwa Mwaka 2018/19**

| Hali Halisi | Idadi ya Mapendekezo | Asilimia % |
|---|---|---|
| Mapendekezo yaliyo katika hali ya utekelezaji | 78 | 58 |
| Mapendekezo Yasiyotekelezwa | 51 | 38 |
| Mapendekezo Yaliyorudiwa | 6 | 4 |
| **Jumla** | **135** | **100** |

*Chanzo: Majibu ya PMG kwa mwaka 2018/19*

### Uchambuzi wa Mwenendo wa Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kwa Mapendekezo ya Ukaguzi.

Uchambuzi wa mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo kulingana na majibu ya taarifa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kwa miaka mitatu iliyopita (2018/19, 2017/18 na 2016/17) umeonesha kuwa mapendekezo mengi yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Uchambuzi wa mwenendo huo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 10** hapa chini.

**Jedwali Na. 10: Mwenendo wa Mlipaji Mkuu wa Serikali katika Kutekeleza Mapendekezo yangu kwa Kipindi cha Miaka Mitatu**

| **Hali Halisi** | **2018/19** | **2017/18** | **2016/17** |
|---|---|---|---|
| Mapendekezo Yaliyotekelezwa | 0 | 8 | 2 |
| Mapendekezo yaliyo katika hali ya utekelezaji | 78 | 37 | 17 |
| Mapendekezo Yasiyotekelezwa | 51 | 20 | 4 |
| Mapendekezo Yaliyorudiwa | 6 | 0 | 0 |
| Mapendekezo yaliyopitwa na wakati | 0 | 15 | 68 |
| **Jumla** | **135** | **80** | **91** |

## 3.4 Hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC)

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ndio chombo cha juu zaidi cha uangalizi kwa Taasisi, Wizara na Idara za Serikali kuu (MDAs), kulingana na Kanuni ya 14 ya kanuni za Kudumu za Bunge toleo lililorekebishwa Januari 2020. Majukumu ya Kamati yameelezewa kwa usahihi chini ya kanuni ya 14 ya toleo la nane la kanuni za Kudumu za Bunge.Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinaripoti maoni muhimu kwa Kamati ya PAC.

Maagizo ya Kamati ya PAC yanapaswa kuchukuliwa kwa umuhimu na Maafisa Masuuli. Utekelezaji wa maagizo ya PAC ni muhimu ili kuhakikisha kuwa shughuli na utendaji ndani ya Serikali na Taasisi zake zinatekelezwa kwa utaratibu, maadili na ufanisi. Ni muhimu mambo yote yaliyoibuliwa na Kamati ya PAC yashughulikiwe na maagizo yote yatekelezwe ipasavyo.

Tathmini yangu juu ya Ripoti za ukaguzi wa Serikali na Taasisi zake inaonyesha kuwa wakati wa kikao cha Kamati ya PAC kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020, Kamati ilikuwa imetoa jumla ya maagizo 259 kwa Serikali na Taasisi zake ambayo yalikuwa katika hali tofauti ya utekelezaji. Katika maagizo ya jumla ya PAC yaliyotolewa, 130 (50%) yalitekelezwa, 101 (39%) yalikuwa katika utekelezaji, na 17 (7%) hayakutekelezwa, wakati maagizo 11 (4%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati. Muhtasari huu umeonyeshwa katika **Kielelezo Na. 3**: Hali ilivyo ya Utekelezaji wa Maagizo ya PAC kwa Mwaka 2018/19

**Kielelezo Na. 3: Hali ilivyo ya Utekelezaji wa Maagizo ya PAC kwa Mwaka 2018/19**




### 3.4.1 Ulinganisho wa hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya PAC kati ya Mwaka 2018/19 na Miaka Iliyopita

Tathmini yangu ilibaini kwamba kulikuwa na jumla ya maagizo 259 ya Kamati ya PAC kwa mwaka wa fedha 2018/19 ikilinganishwa na maagizo ya 295 na 272 kwa miaka 2017/18 na 2016/17 mtawalia. Kati ya mapendekezo haya, mapendekezo 130 (50%) mwaka 2018/19 yalitekelezwa wakati mapendekezo 92 (31%) na 82 (30%) yalitekelezwa kwa miaka 2017/18 na 2016/17, mtawalia. Mwelekeo wa Utekelezaji wa Maagizo ya PAC kwa Miaka Mitatu Mfululizo Umeonyeshwa Kwenye **Jedwali Na. 11.**

**Jedwali Na. 11: Mwenendo wa Maagizo ya Kamati ya PAC kwa Kipindi cha Miaka Mitatu**

| Hali Halisi | 2018/19 | 2017/18 | 2016/17 |
|---|---|---|---|
| Mapendekezo Yaliyotekelezwa | 130 | 92 | 82 |
| Mapendekezo Yaliyo katika Hali ya Utekelezaji | 101 | 79 | 163 |
| Mapendekezo Yasiyotekelezwa | 17 | 105 | 19 |
| Mapendekezo Yaliyopitwa na Wakati | 11 | 19 | 8 |
| **Jumla** | **259** | **295** | **272** |

### 3.5 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi Maalumu

Kifungu cha 29 (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, kinaeleza kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), akiombwa na mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka za Umma, Wizara, Idara, Wakala, mamlaka za Serikali za Mitaa na vyombo vingine, anaweza kutekeleza ukaguzi maalum. Pia, katika Kanuni ya 79 (1) ya Kanuni ya ukaguzi wa Umma ya mwaka, 2009 CAG hatalazimika kukubali ombi kama hilo,na Kanuni ya 80 (2) inamruhusu kurekebisha mawanda ya ukaguzi kama atakavyoona inafaa.

Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2018/19, 2017/18 na 2016/17), nimetoa jumla ya mapendekezo 48 katika kaguzi maalumu 21 nilizofanya. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo hayo ulibaini kwamba mapendekezo yote 48 yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.Maelezo ya kina ya hali ya utekelezaji ni kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. VI**

**Hivyo nasisitiza kuwa Wizara, Idara, Wakala, Vyama vya Siasa pamoja na Mlipaji Mkuu wa Serikali, kuweka juhudi zaidi katika kuhakikisha kwamba Maagizo yote yaliyotekelezwa kwa sehemu, yanakamilishwa kulingana na mpango wa utekelezaji uliokubaliwa ili kuhakikisha kuwa mapendekezo ya CAG na maagizo ya PAC yanakuwa na faida kwa Serikali.**

## SURA YA NNE

## UANDAAJI NA UTEKELEZWAJI WA BAJETI

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia masuala yanayohusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, Sera zilizopitishwa ili kuongeza Mapato, usimamizi wa Matumizi na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti. Bajeti ya 2019/20 ililenga kujenga uchumi wa viwanda, kuchochea ajira na kuwezesha ustawi wa jamii endelevu kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo[4]:

**Viwanda na Kilimo**

Lengo lilikuwa kusaidia Viwanda ambavyo vinatumia Malighafi zinazopatikana ndani ya Nchi ili kuzalisha bidhaa kwa Soko la ndani na nje. Kipaumbele hiki kilitekelezwa kwa kutenga fedha ili kusaidia kilimo, kutoa misamaha ya Kodi, kuanzisha viwanda vidogo vya kuongeza thamani ya mazao na kuimarisha Bodi za Mazao ya Kilimo na vitu vingine.

**Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu**

Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za Afya, Elimu na ujuzi, chakula na lishe bora, huduma ya maji safi na salama pamoja na kuweka msukumo katika kuongeza ubora wa nguvu kazi ili iendane na mahitaji ya Soko la Ajira.

**Uboreshaji wa Mazingira ya Uendeshaji Biashara na Uwekezaji**

Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa Miundombinu hususani Reli, Bandari, Nishati, Barabara, Madaraja na Viwanja vya Ndege, kupitia na kuimarisha mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi, pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama ili kushawishi na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa Miradi ya maendeleo katika ngazi zote. Vilevile, kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato ya kodi na yasiyo ya Kodi bila kuathiri Biashara.

---

[4]Kwa maelezo ni Bajeti iliyowasilishwa Bungeni Juni, 2019; https://www.mof.go.tz

## 4.2 Sera na Mikakati ya Bajeti

Ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Bajeti, serikali iliweka hatua kadhaa za kiutawala, Sera, mikakati na mageuzi ya Kodi. Marekebisho yaliyofanywa ni pamoja na marekebisho ya Sheria za Kodi na maboresho katika hatua nyingine za kiutawala kama vile kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya ndani kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani (IDRAS), kupanua wigo wa Kodi kwa kuanzisha vyanzo vipya vya mapato kama vile uvuvi wa Bahari Kuu. Udhibiti mwingine ni kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa uhamishwaji wa Bei (transfer price), kuimarisha usimamizi wa misamaha ya Kodi na kuhakikisha ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi kupitia Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Elektroniki (GePG).

Sera na hatua juu ya usimamizi wa matumizi ni pamoja na; nidhamu katika matumizi ya fedha za Umma, kuhakikisha nakisi ya bajeti haizidi asilimia 2.3 ya Pato la Taifa, kuelekeza rasilimali fedha kwa sekta zinazosaidia ukuaji wa uchumi na zinazoongeza tija ili kuchochea ukuaji wa Uchumi na udhibiti wa malimbikizo ya Madeni. Aidha, Serikali iliendelea kulipa malimbikizo yaliyothibitishwa kuwa halali bila ya kuchelewa. Pia, iliendelea kutoa kandarasi kwa wakati baada ya idhini ya fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali na pale inapohitajika kuweka hatua za kisheria, kiutawala na kinidhamu kwa Sheria na Kanuni zinazokiukwa.

## 4.3 Muundo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

### 4.3.1 Makadirio ya Makusanyo

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali ilitarajia kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 33,105.41, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 629.46 sawa na asilimia mbili ikilinganishwa na makadirio ya Sh. bilioni 32,475.95 zilizoripotiwa kwa mwaka wa fedha 2018/19. Mgawanyo wa ukusanyaji na asilimia ya michango kutoka katika kila chanzo kilichobainishwa ni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali hapa chini;

**Jedwali Na. 12: Vyanzo vya Makusanyo na Asilimia za Kuchangia**

| Maelezo | | Kiasi katika Sh bilioni | % |
|---|---|---|---|
| **Makusanyo ya vyanzo vya Ndani** | Kodi | 19,100.93 | 58 |
| | Makusanyo yasiyotokana na Kodi | 3,178.92 | 9 |
| | Makusanyo Kutoka Mamlaka ya Serikali | 765.48 | 2 |

| Maelezo | | Kiasi katika Sh bilioni | % |
|---|---|---|---|
| | za Mitaa | | |
| **Misaada na Mikopo** | Misaada | 1,208.52 | 4 |
| | Mikopo ya Ndani | 4,959.99 | 15 |
| | Mikopo ya Nje | 3,891.56 | 12 |
| **Jumla** | | **33,105.41** | **100** |

*Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Mwaka 2019/20*

### 4.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Serikali

Bajeti ya Sh.bilioni 33,105.41 ilipitishwa kwa matumizi mbalimbali, yaliyobainishwa katika Matumizi ya Maendeleo Sh. bilioni 12,248.60 na matumizi ya kawaida Sh. bilioni 20,856.81. Mgawanyo wa matumizi kwa asilimia ni kama inavyoonekana katika kielelezo cha hapa chini:

**Kielelezo Na. 4: Mgawanyo wa Makadirio ya Matumizi kwa asilimia**




## 4.4 Marejeo (Reallocation) ya Bajeti ya Matumizi ya Serikali

Katika mwaka wa Fedha 2019/20 Marejeo ya Bajeti ya matumizi Na.1 ya 2019/20 ya kiasi cha Sh biloni 48.308 yalipitishwa na Bunge ili kubadilisha matumizi ya Mafungu mbalimbali, hivyo kupelekea ongezeko la matumizi ya Maendeleo kwa asilimia 0.39 na kupungua kwa matumizi ya kawaida kwa asilimia 0.23. Makadirio ya matumizi ya maendeleo na kawaida baada ya Marejeo ya Bajeti yalikuwa Sh. bilioni 12,296.91 na Sh. bilioni 20,808.50 mtawalia, kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 13: Marejeo ya Bajeti ya Matumizi**

| Maelezo | Matumizi ya Maendeleo Sh.bilioni | Matumizi ya kawaida Sh.bilioni |
|---|---|---|
| Makadirio ya matumizi kama yalivyopitishwa na Bunge | 12,248.60 | 20,856.81 |
| Kiasi kilichorejewa | (+)48.308 | (-)48.308 |
| Bajeti iliyorekebishwa na Kikao cha Bunge | 12,296.91 | 20,808.50 |

*Chanzo: Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha, 2019/20, Sheria ya Matumizi ya 2019 na Marejeo ya Bajeti ya matumizi Na.1 la 2019/20*

## 4.5 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

### 4.5.1 Mwenendo wa Makusanyo

Serikali ilikusanya kiasi cha Sh. bilioni 31,519.49 sawa na 95% ikilinganishwa na Makadirio ya Sh. bilioni 33,105.41, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 1,585.92 (5%) hakikukusanywa. Ikilinganishwa na makusanyo ya 2018/19 ya (Sh. bilioni 25,817.45), nilibaini ongezeko la makusanyo kwa kiasi cha Sh. bilioni 5,702.04 (22.09%).

### 4.5.2 Mwenendo wa Makusanyo Ikilinganishwa na Makadirio

Katika kupitia mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano nimebaini kuwapo kwa ongezeko la makusanyo dhidi ya makadirio yaliyoidhinishwa. Kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 14** hapa chini. Hali hii inawezesha Serikali kutoa huduma bora za kijamii, kujenga Miundombinu, na kuwezesha utekelezwaji wa Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, katika kila mwaka wa fedha ulioripotiwa, makusanyo yamekuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa hali inayonipa mashaka. Mwenendo wa makadirio na makusanyo ni kama ilivyoonyeshwa katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 14: Mwenendo wa Makusanyo Ikilinganishwa na Makadirio**

| Mwaka | 2019/20 (Sh. Bilioni) | 2018/19 (Sh. Bilioni) | 2017/18 (Sh. Bilioni) | 2016/17 (Sh. Bilioni) | 2015/16 (Sh. Bilioni) |
|---|---|---|---|---|---|
| Makadirio | 33,105.41 | 32,475.95 | 31,711.99 | 29,539.00 | 22,495.00 |
| Makusanyo | 31,519.49 | 25,817.45 | 27,695.97 | 25,307.00 | 21,109.00 |
| Mwenendo wa changizo katika % asilimia | | | | | |
| Kodi | 57% | 60% | 55% | 57% | 59% |
| Makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa | 8% | 9% | 5% | 8% | 8% |
| Mikopo ya Ndani | 16% | 15% | 21% | 23% | 25% |
| Misaada na mikopo ya Nje | 19% | 16% | 19% | 12% | 8% |

*Chanzo: Ukaguzi mfuko Mkuu*

Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Makadirio na Makusanyo kwa Miaka Mitano (Kiasi katika Sh. bilioni)



### 4.5.3 Ufadhili wa Kibajeti

Makusanyo yanayotokana na Kodi, makusanyo yasiyotokana na kodi, na makusanyo ya kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa yalikuwa Sh. bilioni 20,514.52, wakati Sh.bilioni 11,004.97 zilitokana na mikopo ya ndani, nje na misaada. Uchambuzi unaonyesha kuwa Mapato ya ndani yanayotokana na (Kodi, Makusanyo yasiyotokana na Kodi, pamoja na makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanaweza kufadhili Matumizi ya Serikali kwa 65%, wakati 35% iliyobaki ilitokana na Misaada na Mikopo.

Ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka uliopita ya Sh.bilioni 8,023, nilibaini kuongezeka kwa Misaada na mikopo ya Sh.bilioni 2,981.97 sawa na 37%. Bajeti ya Mikopo na Misaada imekuwa ikiongezeka kwa kipindi cha miaka mitano isipokuwa kupungua katika mwaka wa fedha 2018/19. Hali hiyo inamaanisha kuongezeka kwa utegemezi wa kibajeti katika mikopo na Misaada.

Mwenendo wa ufadhili wa Kibajeti kwa kipindi cha miaka mitano ni kama inavyoonekana katika kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa ufadhili wa kibajeti kwa kipindi cha miaka Mitano**



**Mapendekezo yangu kwa Serikali na Mamlaka husika ni kuwa, Wizara/Idara na Sekretarieti za mikoa zitafiti vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza wigo wa makusanyo ya ndani na kupunguza utegemezi wa Misaada na Mikopo ya Wahisani.**

### 4.5.4 Tathmini Juu ya Mwenendo wa Ukusanyaji kutoka kila Chanzo Kilichotambuliwa

**Makusanyo ya Kodi**
Makusanyo ya Kodi Tanzania Bara ni Sh. bilioni 17,933.20 sawa na 94% ya makadirio ya Sh. bilioni 19,100.9; hivyo Serikali haikukusanya kiasi cha Sh. bilioni 1,167.73.

Ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2019/20 ya (Sh. bilioni 17,933.20) na makusanyo ya mwaka 2018/19 ya (Sh. bilioni 15,474.33), nimebaini ongezeko la makusanyo la Sh. bilioni 2,458.87 sawa na 16%.

**Makusanyo Yasiyotokana na Kodi**
Makusanyo yasiyotokana na kodi yanajumuisha Makusanyo yanayokusanywa na Wizara, Idara za Serikali kuu, Balozi, Sekretarieti za Mikoa na Taasisi nyingine.

Katika kupitia taarifa za Fedha na makusanyo yaliyowasilishwa nilibaini kiasi cha Sh. bilioni 1,868.12 sawa na 59% ya makadirio ya Sh. bilioni 3,178.92 zilikusanywa, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 1,310.80 hakikukusanywa.

Ikilinganishwa na makusanyo ya 2019/20 ya (Sh. bilioni 1,868.12) na Makusanyo ya 2018/19 ya (Sh. bilioni 1,661.28) nimebaini ongezeko la makusanyo kwa Sh. bilioni 206.84 sawa na 12.5%. Hali hii inaonyesha uboreshaji wa usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato.

**Makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa**
Makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalikuwa Sh. bilioni 713.19 sawa na 93% ikilinganishwa na makadirio ya Sh. bilioni 765.48, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 52.29 (7%) hakikukusanywa.

Ikilinganishwa na makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka wa fedha 2018/19 ya Sh. bilioni 659.10, nimebaini kuwapo kwa ongezeko la Makusanyo kwa kiasi cha Sh. bilioni 54.09 (8.21%).

**Misaada**
Misaada iliyopokelewa kutoka kwa wadau wa maendeleo ni Sh. bilioni 1,119.68 sawa na 93% ikilinganishwa na makadirio ya Sh. bilioni 1,208.52; hivyo, misaada ya Sh. bilioni 88.85 haikupokelewa. Mikopo iliyopokelewa katika mwaka huu wa fedha inajumuisha msaada wa kibajeti, na fedha za Miradi ya Maendeleo.

Kumekuwa na ongezeko la misaada ya Sh. bilioni 476.68 sawa na 74.13% ikilinganishwa na Sh. bilioni 643 zilizopokelewa mwaka 2018/19.

**Mikopo ya Ndani**
Makusanyo yanayotokana na mikopo ya ndani yanajumuisha: Hati fungani za muda mfupi na muda mrefu, Sh. bilioni 4,959.99 za mikopo ya Ndani zilipokelewa na Serikali sawa na 100% ya Makadirio ya Sh. bilioni 4,959.99. Nilibaini kuimarika kwa ongezeko la mikopo ya ndani kwa kiasi cha Sh. bilioni 1,008.95 sawa na 25.54% ikilinganishwa na mikopo ya Sh. bilioni 3,951.04 iliyopokelewa mwaka 2018/19.

**Mikopo ya Nje yenye Masharti Nafuu**
Mikopo ya nje yenye masharti nafuu iliyopokelewa katika mwaka wa Fedha ilikuwa Sh. bilioni 2,535.92, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya makadirio ya Sh. bilioni 1,575.15 kwa Sh. bilioni 961 sawa na 61%. Nilibaini kuongezeka kwa mikopo ya Nje yenye masharti nafuu kwa kiasi cha Sh. bilioni 813.52 sawa na 47.23% ikilinganishwa na mikopo kama hiyo ya Sh. bilioni 1,722.40 iliyopokelewa mwaka 2018/19.

**Mikopo ya Nje isiyo na Masharti Nafuu**
Mikopo ya nje isiyo na masharti nafuu iliyopokelewa na Serikali ilifikia Sh. bilioni 2,389.39 ikiwa ni zaidi ya Makadirio ya Sh. bilioni 2,316.40 kwa Sh. bilioni 73 (3.15%). Ikilinganishwa na mwaka uliopita nilibaini ongezeko la kiasi cha Sh. bilioni 683.09 (40.03%) kinachotokana na Mikopo kutoka Sh. bilioni 1,706.3 zilizoripotiwa 2018/19.

Kwa ujumla, utendaji wa makusanyo kwa kila chanzo kilichotambuliwa ni zaidi ya 50% ya makadirio, jambo linaloonyesha utendaji mzuri wa ukusanyaji; Hata hivyo, juhudi zaidi inahitajika ili kuongeza makusanyo yasiyotokana na Kodi ambayo hayakufanya vizuri ikilinganishwa na vyanzo vingine. **Kielelezo Na. 7** kinaonyesha uwiano wa makusanyo na makadirio kwa kila chanzo.

**Kielelezo Na. 7: Uwiano wa Bajeti na Makusanyo ya kila chanzo**




| Chanzo | Kodi | Makusanyo yasiyotokana na Kodi | Makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | Misaada | Mikopo ya Ndani | Mikopo ya Nje |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bajeti | 19,100.93 | 3,178.92 | 765.48 | 1,208.52 | 4,959.99 | 3,891.56 |
| Makusanyo | 17,933.20 | 1,868.12 | 713.19 | 1,119.68 | 4,959.99 | 4,925.30 |

### 4.5.5 Makusanyo katika Mfuko Mkuu wa Serikali

Nilipitia mwenendo wa uwasilishwaji wa Makusanyo katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kubaini kuwapo kwa Matumizi ya Makusanyo kabla ya kuwasilisha taarifa katika Mfuko Mkuu wa Jumhuri ya Muungano, kinyume na Kifungu Na. 135 (1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 (kama inavyorekebishwa mara kwa mara) ambacho kinataka makusanyo yote kwa Matumizi ya Serikali kuwasilishwa Mfuko Maalumu unaojulikana kama "Mfuko Mkuu wa Jumhuri ya Muungano". Makusanyo yenye hoja ni haya yaliyoelezwa hapa chini:

#### 4.5.5.1 Kutowasilishwa kwa Makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Mfuko Mkuu wa Hazina Sh. bilioni 132.08

Mamlaka za Serikali za Mitaa hukusanya Mapato kutoka katika vyanzo vyake na kuyatumia. Mamlaka za Serikali za Mitaa hupaswa kutoa taarifa Mfuko Mkuu kupitia ripoti za Makusanyo ili kuyatambua kama Mapato na Matumizi.

Ukaguzi ulibaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya jumla ya Sh bilioni 132.08 na kuzitumia bila kuwasilisha taarifa Mfuko Mkuu. Ikilinganishwa na kiasi cha Sh bilioni 553.378 zilizoripotiwa mwaka 2018/19 kumekuwa na kupungua kwa makusanyo ya Serikali za Mitaa yanayotumika bila kutolewa taarifa Mfuko Mkuu kwa 76%.

**Nakazia pendekezo langu la awali juu ya kufanyika kwa usuluhishi wa taarifa za makusanyo kati ya Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Wizara ya Fedha na Mipango. Pia, ninapendekeza uimarishaji wa mfumo wa udhibiti wa ndani katika kuongeza uwazi katika Makusanyo ikiwa ni pamoja na ufahamu wa umuhimu na uwajibikaji katika kutoa taarifa za Makusanyo.**

#### 4.5.5.2 Fedha Zilizopelekwa moja kwa moja Kwenye Miradi bila kutoa Taarifa Mfuko Mkuu Sh.bilioni 2,025.67

Ukaguzi wa Fungu Na. 22-Madeni ya Taifa na Huduma za Jumla ulibaini kuongezeka kwa fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye Miradi ya maendeleo kwa kiasi cha Sh. bilioni 853.76 (73%) kutoka Sh. bilioni 1,171.91 zilizoripotiwa mwaka 2018/19 hadi Sh bilioni 2,025.67 zilizoripotiwa mwaka 2019/20. Kuongezeka kwa fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi ya mendeleo bila kutolewa taarifa Mfuko Mkuu kunachangiwa na ushirikiano duni wa Maafisa Masuuli wanaowajibika kuwasilisha ombi la kupatiwa risiti za mapokezi ya fedha na kibali cha matumizi ya fedha zilizopokelewa moja kwa moja bila kupitia Mfuko Mkuu (Dummy receipt and exchequer).

**Bado narudia pendekezo langu juu ya usuluhisho wa taarifa za fedha kwa wakati na uimarishwaji wa Mfumo wa udhibiti wa ndani kwa fedha zinazokwenda moja kwa moja kwenye Miradi ya maendeleo. Zaidi, nasisitiza juu ya matumizi ya mfumo wa D-fund pale fedha zinapotolewa na wadau wa maendeleo.**

Kutokana na uchambuzi wa makusanyo uliofanywa hapo juu, ninahitimisha kwamba, tofauti ya Sh. bilioni 2,170.59 kati ya makusanyo ya Sh. bilioni 31,519.49 zilizo kusanywa kutoka kila chanzo na Sh. bilioni 29,348.90 zilizopokelewa Mfuko Mkuu inasababishwa na sababu ambazo zimebainishwa katika **Jedwali Na. 15 ;**

**Jedwali Na. 15: Usuluhishi wa Makusanyo ya Jumla na Makusanyo Yaliyotambuliwa Mfuko Mkuu wa Hazina**

| Maelezo ya usuluhisho | Kiasi katika Sh. Bilioni |
|---|---|
| Makusanyo ya Jumla | 31,519.49 |
| Makusanyo kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na Fedha zilizo pelekwa moja kwa moja kwenye Miradi na kutumiwa bila kuhesabiwa katika Mfuko Mkuu | (2,157.76) |
| Marejesho ya Kodi (Tax refund) yaliyopunguzwa katika makusanyo ya jumla ya TRA. | (246.51) |
| Kuwasilishwa kwa Bakaa ya mwaka uliopita Mfuko Mkuu kutoka amana maalum na Makusanyo ya REA, RFB, Mfuko wa Maji na Mfuko wa maendeleo ya Reli. | 53.54 |
| Makusanyo yanayotokana na fedha zilizokaa muda mrefu katika Akaunti za amana bila kutumiwa. | 180.13 |
| Makusanyo yaliyotambuliwa Mfuko Mkuu | 29,348.89 |

### 4.5.6 Makusanyo na Matumizi katika Mfuko Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

Jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 29,348.90 zilipokelewa Mfuko Mkuu wakati jumla ya fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida na maendeleo katika mwaka wa fedha 2019/20 ni Sh. bilioni 28,397.01 hivyo kupelekea kuwapo kwa bakaa ya Sh. bilioni 1,173.75 katika Mfuko Mkuu hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020. Maelezo ya Makusanyo na fedha zilizotoka Mfuko mkuu ni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 16: Makusanyo na Malipo katika Mfuko Mkuu wa Hazina**

| Chanzo cha Mkusanyo na Matumizi | Kiasi katika Sh. bilioni |
|---|---|
| Makusanyo | |
| Kodi[5] | 17,740.24 |
| Makusanyo yasiyotokana na Kodi | 1,868.12 |
| Mkusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | 581.11 |
| Misaada | 1,119.68 |
| Mikopo ya Ndani | 4,959.99 |
| Mikopo ya Nje | 2,899.63 |
| Makusanyo mengine | 180.13 |
| Jumla ya Makusanyo | 29,348.90 |
| Jumla ya Fedha zilizotolewa[6] | (28,416.89) |

[5] Kiasi cha kodi kilichopokelewa Mfuko mkuu kinaondoa Marejesho ya Kodi Sh. bilioni 246.51 na kujumuisha bakaa ya makusanyo ya Sh. bilioni 53.54 za mwaka 2018/19 ambazo hazikuwasilishwa Mfuko Mkuu

| Chanzo cha Mkusanyo na Matumizi | Kiasi katika Sh. bilioni |
|---|---|
| Fedha zilizobaki Mfuko Mkuu | 932.01 |
| Fedha zilizorudishwa kwa Mlipaji Mkuu | 241.74 |
| Jumla ya fedha zilizobaki Mfuko Mkuu | 1,173.75 |

*Chanzo: Taarifa ya Mapato na Matumizi Mfuko mkuu*

Kati ya fedha zilizotolewa Mfuko Mkuu (ukiondoa Sh. bilion 2,157.75 zilizopelekwa moja kwa moja kwenye miradi na makusanyo ya Mamlaka za serikali za Mitaa yaliyotumiwa bila kuwasilisha Taarifa Mfuko Mkuu) Mgawanyo wa Matumizi ikilinganishwa na Bajeti ulikuwa kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 17: Mgawanyo wa Matumizi ikilinganishwa na Bajeti**

| Maelezo | Bajeti | Asilimia | Matumizi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| | Sh. bilioni | | Sh. bilioni | |
| Matumizi ya Maendeleo | 12,248.60 | 37 | 8,189.90 | 29 |
| Kulipa Deni la Taifa | 9,721.13 | 29 | 9,718.52 | 34 |
| Mishahara | 7,558.97 | 23 | 7,289.66 | 26 |
| Matumizi mengineyo | 3,576.71 | 11 | 3,198.93 | 11 |
| **Jumla** | **33,105.41** | **100** | **28,397.01** | **100** |

### 4.6 Uchambuzi wa Makadirio, Fedha Zilizotolewa kwa Matumizi na Matumizi Halisi katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa

Jumla ya Sh. bilioni 23,455.61 zilielekezwa katika matumizi ya Serikali Kuu, ikijumuisha Wizara na Wakala, Idara, na Sekretarieti za Mikoa. Kiasi kilichobaki kilielekezwa kwa matumizi ya serikali za Mitaa.

#### 4.6.1 Makadirio na Fedha Zilizotolewa kwa Matumizi ya Kawaida

Mapitio ya Taarifa za Fedha kwa Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa yanaonesha Kiasi cha Sh. bilioni 16,104.54 sawa na 98% ya makadirio ya Sh. bilioni 16,415.66 zilitolewa kwa matumizi ya Kawaida. Ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka 2018/19 kiasi cha Sh. bilioni 15,140.56, nimebaini kuongezeka kwa Fedha za matumizi ya kawaida kwa Sh bilioni 963.97 (6%) kutoka Sh. bilioni 16,104.54 za mwaka 2019/20.

[6] Fedha zilizopelekwa kwenye Mafungu ni (Sh bilioni 28,397.01) na (Sh bilioni 19.87) zilizuiliwa.

### 4.6.2 Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Kawaida na Matumizi halisi Yaliyofanyika

Matumizi ya kawaida katika Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa yaligharimu Sh. bilioni 16,063.20 sawa na 99.7% kati ya Fedha zilizotolewa Sh. bilioni 16,104.54. Hivyo, kiasi cha Sh. bilioni 41.33 hakikutumika na kurudishwa kwa Mlipaji mkuu wa Serikali (PMG).

Ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ya mwaka wa fedha 2018/19, ya Sh. bilioni 15,109.63, nimebaini kuongezeka kwa matumizi ya kawaida kwa Sh 953.57 (6%) ikilinganishwa na Sh. bilioni 16,063.20 zilizoripotiwa mwaka 2019/20. Ni maoni yangu kuwa, kuwapo kwa bakaa ya fedha zisizotumika kunamaanisha kutotekelezwa ama utekelezaji hafifu wa shughuli zilizokusudiwa au uwezo hafifu wa Taasisi katika kutumia pesa zilizotolewa kwa wakati. Maelezo zaidi ya makadirio, fedha zilizotolewa, pamoja na matumizi halisi yaliyofanyika kwa kila Taasisi iliyokaguliwa zimeoneshwa katika kielelezo kifuatacho na **Kiambatisho Na. VII**

**Kielelezo Na. 8: Makadirio, Fedha Zilizotolewa na Matumizi Halisi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa kipindi cha Miaka Mitano (Kiasi katika Sh. billioni)**




| | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 | 2016/17 | 2015/16 |
|---|---|---|---|---|---|
| Fedha zilizotolewa | 16,104.54 | 15,140.56 | 15,408.03 | 13,159.74 | 12,065.22 |
| Matumizi Halisi | 16,063.20 | 15,109.63 | 15,328.66 | 13,413.69 | 12,045.94 |
| Makisio | 16,415.66 | 16,104.39 | 15,725.16 | 13,882.04 | 12,904.75 |

*Chanzo: Taarifa za Ukaguzi za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa*

**Ninapendekeza maafisa masuuli kuhakikisha kwamba Fedha zilizotolewa zinatumika kwa wakati katika kutekeleza Shughuli zilizopangwa**

### 4.6.3 Uwiano wa Makadirio na Fedha Zilizotolewa kwa Shughuli za Maendeleo

Mapitio ya Taarifa za Fedha katika Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zinaonesha kiasi cha Sh. bilioni 7,351.07 sawa na 66% zilitolewa kwa matumizi ya maendeleo ikilinganishwa na makadirio ya Sh. bilioni 11,147.24.

Ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka 2018/19 za kiasi cha Sh. bilioni 7,144.46 , nilibaini kuongezeka kwa fedha za maendeleo kwa kiasi cha Sh. bilioni 206.61 (3%) ikilinganishwa na Sh. bilioni 7,351.07 zilizotolewa mwaka 2019/20.

### 4.6.4 Uwiano wa Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Maendeleo na Matumizi halisi Yaliyofanyika

Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa yalikuwa Sh. bilioni 7,191.42 sawa na 98% ya Fedha zilizotolewa za Sh. bilioni 7,351.07, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 159.65 hakikutumika.

Ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo ya mwaka 2018/19 ya Sh. bilioni 7,131.24, nimebaini kuongezeka kwa matumizi ya maendeleo kwa Sh bilioni 60.18 (2%) kutoka katika Sh. bilioni 7,191.42 zilizoripotiwa 2019/20.

Ni maoni yangu kuwa, kutotumika kwa fedha za maendeleo zilizotolewa kunamaanisha uwezo mdogo wa Taasisi katika kutumia fedha za maendeleo zilizotolewa, hivyo kuathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.Maelezo zaidi ya Makadirio, Fedha zilizotolewa na matumizi halisi kwa Wizara/Idara, na Sekretarieti za Mikoa yameoneshwa kwenye Kielelezo Na. 9 na Kiambatisho Na. VIII.

**Kielelezo Na. 9: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi ya Fedha za maendeleo kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh. billioni)**




| | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 | 2016/17 | 2015/16 |
|---|---|---|---|---|---|
| Fedha zilizotolewa | 7,351.07 | 7,144.46 | 7,219.26 | 6,939.00 | 3,768.59 |
| Matumizi Halisi | 7,191.42 | 7,131.24 | 7,100.42 | 6,045.81 | 3,729.72 |
| Makisio | 11,147.24 | 10,467.21 | 10,142.72 | 10,235.41 | 4,968.86 |

*Chanzo; Taarifa za Ukaguzi za Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa*

**Napendekeza Fedha za maendeleo zitolewe kwa wakati pia Maafisa Masuuli wa mafungu husika waongeze juhudi katika kuhakikisha Miradi ya maendeleo iliyopangwa inatekelezwa ndani ya kipindi kilichopangwa.**

## 4.7 Usimamizi wa Mapato katika Wizara/Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi

Nilipitia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali zinazosimamia ukusanyaji wa mapato katika mwaka wa fedha 2019/20 nakubaini mapungufu yafuatayo:

### 4.7.1 Wizara ya Afya Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (MOHCDGEC) Kutokukusanya Mapato Yanayotokana na Ukaguzi katika Bandari ya Dar es salaam Kitengo cha Afya Sh. 200,860,138

Kifungu cha 42 cha Sheria ya Afya ya Umma ya mwaka 2009 kinahitaji mmiliki wa chombo au Ndege au wakala kulipa ada ya ukaguzi au ada nyingine zinazohusiana na huduma za ukaguzi zinazotolewa na Kitengo cha Afya katika Bandari.

Ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria hii, aya ya 4.1 na Kiambatisho Na. 1 cha Mwongozo wa ukaguzi uliotolewa Januari 2016, kila Chombo cha Kimataifa hutakiwa kulipa Dola za Marekani 100 na Sh. 10,000 kwa Boti za kitaifa na majahazi zitakazokaguliwa.

Nilipitia taarifa za ukaguzi uliofanywa katika bandari ya Dar es Salaam Kitengo cha Afya na kubaini Vyombo 804 vya Kimataifa na Mashua 1625 zilikaguliwa na kupewa Hati za Usafi bila kutozwa tozo ya ukaguzi ya jumla ya Sh 200,860,138.40 kama ilivyoelezewa katika **Jedwali Na. 18** hapa chini:

**Jedwali Na. 18: Malipo ya Ukaguzi ambayo Hayakukusanywa na Wizara ya Afya katika Bandari ya Dar es Salaam Kitengo cha Afya**

| Maelezo ya Ukaguzi | Idadi ya vyombo | Kiasi katika Sh. |
|---|---|---|
| **Ukaguzi wa Vyombo vya Kimataifa** | Vyombo 804@Dola 100 x2,296.14* | 184,610,138.40 |
| **Ukaguzi wa Mashua ya Kitaifa na Majahazi** | Boti 1625 @Sh 10,000 | 16,250,000.00 |
| **Jumla** | | **200,860,138.40** |

***Kiwango cha kubadilisha fedha Tarehe 30 Juni, 2020 -Sh 2,296.14/Dola**

Kutokutoza ada katika chanzo hiki kilichobainishwa kunainyima Serikali Mapato yaliyokusudiwa hivyo kusababisha upotevu wa mapato ambayo yangeweza kugharamia matumizi ya Serikali.

**Ninapendekeza kuwa, Wizara inayohusika iimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa mapato katika kitengo cha afya katika Bandari ili kupunguza upotezaji wa mapato ya Serikali wakati wa ukaguzi wa vyombo bandarini.**

### 4.7.2 Kutokutumiwa kwa Fedha Zinazotokana na Mali Zilizotaifishwa na Kurejeshwa Serikalini Sh. 51,521,605,271.53

Nilipitia uendeshwaji wa Akaunti ya fedha zinazotokana na mali zilizotaifishwa na kurejeshwa Serikalini zilizo chini ya Mkurugenzi wa Mashtaka hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020. Nilibaini kuwapo kwa bakaa ya fedha Sh. 51,521,605,271.53 kutokana na kesi zilizomalizika katika mahakama mbaimbali kwa kipindi cha miaka 6 na zaidi kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 19** hapa chini.

**Jedwali Na. 19: Bakaa ya Fedha zilizo katika Akaunti ya Fedha za Mali Zilizotaifishwa na Kurejeshwa Serikalini**

| Namba ya Akaunti | Jina la Akaunti | Bakaa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 |
|---|---|---|
| 9921161271 | Akaunti ya Fedha za Mali zilizo taifishwa na kurejeshwa serikalini | 15,264,026,469.22 |
| 9921169817 | Mkurugenzi wa Mashtaka | 18,567,255,515.53 |
| 9931209531 | Akaunti ya Fedha za Mali zilizo taifishwa na kurejeshwa serikalini Dola za Marekani 7,741,633.92 @Sh 2,285.0891 kwa kiwango cha kubadilisha fedha tarehe 30 Juni 2020 | 17,690,323,286.78 |
| **Jumla** | | **51,521,605,271.53** |

*Chanzo: Taarifa za Benki*

Kutotumiwa kwa Bakaa ya fedha katika akaunti kunasababishwa na kutokuwapo kwa sheria na kanuni za kudhibiti matumizi ya fedha itokanayo na mali zilizotaifishwa na kurejeshwa serikalini.

Ni maoni yangu kuwa, kuwapo wa fedha zisizotumiwa kwa sababu ya kukosekana kwa Muongozo au mfumo wa kisheria kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya Fedha za umma na ucheleweshaji wa maendeleo ya umma.

**Ninapendekeza kuwa, Serikali kutunga sheria ya ugawaji na matumizi ya Fedha katika akaunti ya unyakuzi na uokoaji.**

### 4.7.3 Kutorudishwa Mfuko Mkuu Fedha Zilizokaa Muda Mrefu katika Akaunti za Amana Sh.1,608,692,098

Katika ukaguzi wa mwaka 2019/20 nilibaini kuwapo wa bakaa ya fedha kiasi cha Sh. 1,608,692,098 ambazo hazijawasilishwa Mfuko Mkuu kwa zaidi ya miaka mitano kutoka kwa Wizara tatu. Ikilinganishwa na mwaka 2018/19 (Sh. 1,850,209,909.34) kutoka kwa Wizara mbili. Aidha, nimebaini kupungua kwa fedha zinazokaa katika akaunti za Amana kwa zaidi ya miaka mitano bila kuwasilishwa Mfuko Mkuu kwa kiasi cha Sh 241,517,811 (15%). Ambapo ni kinyume na Kanuni Na. 133 ya usimamizi wa fedha ya mwaka 2001 (iliyoboreshwa 2004) inayotaka fedha zote ambazo hazijatumika katika akaunti ya Amana kwa zaidi ya miaka mitano zirudishwe mfuko mkuu kwa kibali cha Mhasibu Mkuu.

**Jedwali Na. 20: Fedha zilizokaa Muda Mrefu katika Akaunti ya Amana bila kurejeshwa Mfuko Mkuu**

| Fungu Na. | Jina la Taasisi | Muda (Miaka) | Kiasi katika Sh. |
|---|---|---|---|
| 40 | Mahakama ya Tanzania | 5 na zaidi | 3,603,492 |
| 69 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 6 hadi 8 | 105,088,606 |
| 58 | Wizara ya Nishati | 8 | 1,500,000,000 |
| **Jumla** | | | **1,608,692,098** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi*

Ni maoni yangu kuwa, fedha kukaa muda mrefu katika akaunti za Amana humaanisha kutofanyika kwa mapitio ya taarifa za fedha zilizowekwa katika akaunti ya amana kulingana na muda ili kutambua fedha zilizokaa muda mrefu bila kutumika, hivyo kupelekea fedha kutunzwa bila kutumika.

**Ninapendekeza uongozi wa Wizara husika itumie fedha zilizowekwa katika Akaunti ya Amana kulingana na lengo lililokusudiwa. Pia, iwasiliane na Hazina ili kupata maelekezo ya namna ya kutumia au kuwasilisha Fedha hizo katika mfuko Mkuu.**

### 4.7.4 Makusanyo Yaliyofanywa Nje ya Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki (GePG) Sh. 1,235,585,710.07

Serikali, kupitia mfumo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/20, ilianzisha Sera, mikakati, na hatua mbalimbali za kiutawala, ikiwa ni pamoja na Matumizi ya Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki (GePG). Aidha, Sehemu ya (6A) (1) - (2) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2017) inahitaji fedha za umma kukusanywa kupitia mfumo wa kielekroniki wa malipo ya Serikali (GePG).

Nilipitia ripoti za Makusanyo na taarifa ya Benki ya Wizara ya Uvuvi Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi (FRP) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020 na kubainisha makusanyo ya jumla ya Sh. 1,235,585,710.07 yalikusanywa nje ya Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki (GePG). Hii ni kinyume na Sheria ya Fedha za Umma, Sera za bajeti na hatua za kiutawala zimeanzisha ili kuzuia upotevu wa mapato.

Niliambiwa kuwa kutokufuatwa kwa Sheria hiyo kulitokana na kutokuwapo kwa mashine za mauzo (POS) na vifaa vya kuaminika vya mtandao vya uchapishaji wa ankara za madai kwa baadhi ya vituo vya makusanyo.

Pamoja na changamoto hizo, bado nasisitiza ukusanyaji wa mapato kwa mfumo wa fedha taslimu unaweza kupelekea uvujaji wa mapato na upotezaji wa makusanyo ya Serikali.

**Ninapendekeza Taasisi zote za Serikali zinazohusika na majukumu ya ukusanyaji kutafuta suluhisho juu ya changamoto za ukusanyaji wa mapato ikijumuisha changamoto za mashine za POS pamoja na mtandao ili kuendana na mikakati ya Serikali, Sera na hatua za kiutawala zilizoanzishwa.**

### 4.8 Athari ya Covid -19 katika Tathmini ya Makusanyo

Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali ilipanga kukusanya Makusanyo yasiyotokana na kodi Sh. bilioni 2.48 kutoka vyanzo mbalimbali vya ukusanyaji katika Balozi za Tanzania zilizofunguliwa nje ya nchi. Uhakiki wa Taarifa za Fedha ya Wizara ya Mambo ya Nje ulibainisha kuwa, jumla ya Sh. bilioni 8.87 zilikusanywa kupitia ofisi za Balozi. Hata hivyo, ukaguzi ulishidwa kuthibitisha kiasi cha fedha kilichokusanywa. Zaidi, utendaji wa makusanyo kwa kila Ubalozi, tathmini zaidi juu ya utii wa Sheria, pamoja na maagizo ya usimamizi wa Makusanyo havikuweza kuthibitishwa kutokana na athari ya Ugojwa wa Covid- 19. Hivyo, taarifa hii haitathibitisha kiwango cha uzingatifu wa sheria uliofanywa katika ofisi za Balozi mbalimbali na kutoa hakikisho juu ya Makusanyo halisi yaliyoripotiwa na Balozi husika.

# SURA YA TANO

# HESABU ZA TAIFA

## 5.1 Utangulizi
Sura hii inazungumzia masuala yanayohusiana na Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato, Deni la Taifa, Ukaguzi wa Awali wa Mafao ya Watumishi Waliomaliza Muda Kazini na Hesabu Jumuifu za Serikali.

## 5.2 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato
Sehemu hii inaangazia masuala yanayohusiana na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzishwa na Sheria ya Bunge Namba 11 ya 1995. Inawajibika kusimamia bila upendeleo makusanyo yote ya kodi za ndani,Ushuru wa Forodha na Tozo kwa niaba ya Serikali Kuu.

Mamlaka ya Mapato Tanzania huongozwa na Kamishna Jenerali. Inaundwa na idara nne za kiutendaji. Idara tatu zinahusika moja kwa moja na Ukusanyaji wa mapato. Nazo ni Idara ya Kodi za Ndani, Idara ya Walipa Kodi Wakubwa, na Idara ya Ushuru wa Forodha. Idara ya nne ya Upelelezi wa Kodi inayoshughulikia udanganyifu na ukwepaji wa kodi wa makusudi. Pia, Mamlaka ya Mapato Tanzania ina idara nyingine nane ndogondogo zinazosaidia utendaji wake.

### 5.2.1 Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Iliyopita
Nimepitia maendeleo ya utekelezaji wa mapendekezo 334 ya ukaguzi niliyoyatoa kwa miaka iliyopita kama linavyoonesha **Jedwali Na. 21.**

Kati ya mapendekezo yangu 334 ya ukaguzi, 64 (19%) yametekelezwa kikamilifu, 266 (80%) yanaendelea kutekelezwa, wakati manne (1%) yamepitwa na wakati kutokana na mabadiliko ya sheria.

**Jedwali Na. 21: Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Iliyopita kwenye Makusanyo ya Mapato**

| Mwaka wa fedha | Imetekelezwa | Inaendelea kutekelezwa | Haijatekelezwa | Haikutekelezwa kwa sababu ya mabadiliko ya sheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 2018/19 | 1 | 47 | - | 3 | 51 |
| 2017/18 | 36 | 67 | - | - | 103 |
| 2016/17 | 4 | 41 | - | - | 45 |
| 2015/16 | 7 | 34 | - | - | 41 |
| 2001/02 - 2014/15 | 16 | 77 | - | 1 | 94 |
| **Jumla** | **64** | **266** | **-** | **4** | **334** |
| **Asilimia** | **19%** | **80%** | **0** | **1%** | **100%** |

***Chanzo:*** *Barua ya ukaguzi wa Mapato ya mwaka wa fedha 2019/20*

Kati ya mapendekezo 266 yaliyopo katika utekelezaji, 38 (14%) yanahitaji uamuzi wa mamlaka zingine nje ya Mamlaka ya Mapato kama vile bodi za rufani za kodi, baraza la rufani za kodi, mahakama ya rufaa kwa kodi zilizo katika migogoro na Bunge kwa kesi ambazo idhini ya kufutwa imeombwa na Mamlaka ya Mapato kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Mapendekezo yaliyobaki 228 (86%) yapo chini ya usimamizi na utekelezaji wa Mamlaka ya Mapato.

Kwa ujumla, hali ya utekelezaji wa mapendekezo inaridhisha kiasi, hivyo Mamlaka inapaswa kuongeza ufuatiliaji, utekelezaji na kuimarisha usimamizi katika kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi ninayotoa.

### 5.2.2 Ukusanyaji wa Mapato Tanzania

Katika mwaka wa fedha 2019/20 Mamlaka ya Mapato ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 17,921.85 ukilinganisha na makisio yaliyowekwa ya shilingi bilioni 19,411.45. Makusanyo hayo ni upungufu wa kiasi cha shilingi bilioni 1,489.60 sawa na asilimia nane ya makisio ya Makusanyo. **Jedwali Na. 22** linaonesha mchanganuo wa makusanyo ya mapato kwa idara Tanzania Bara na Zanzibari.

**Jedwali Na. 22: Ukusanyaji wa Mapato kwa Idara (Tanzania Bara na Zanzibari)**

| Idara | Makisio (Shilingi Bilioni) | Makusanyo halisi (Shilingi Bilioni) | Makusanyo ziada (pungufu) | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Shilingi Bilioni | Asilimia (%) |
| Kodi za Ndani | 4,056.62 | 3,361.26 | (695.36) | 17 |
| Walipakodi Wakubwa | 7,965.44 | 7,904.05 | (61.39) | 1 |
| Ushuru wa forodha | 7,533.09 | 6,902.02 | (631,07) | 8 |
| Marejesho na uhamisho | (143.70) | (245,47) | 101,78 | 71 |
| Jumla ya Makusanyo | 19,411.45 | 17,921.85 | (1,489,60) | 8 |

***Chanzo:*** *Taarifa za Makusanyo za Mapato zilizokaguliwa 2019/20*

Utendaji wa idara zote tatu za ukusanyaji mapato uko chini ya makisio yaliyowekwa kwa mwaka 2019/20. Ijapokuwa mlipuko wa ugonjwa wa Covid 19 ilikuwa ni miongoni mwa sababu zilizopelekea kushuka kwa makusanyo.

Ulinganifu wa Idara unaonyesha kuwa Idara ya Walipa Kodi wakubwa ilichangia kwa asilimia 44 ya makusanyo halisi, ikifuatiwa na Idara ya Ushuru wa forodha asilimia 38 na Kodi za Ndani asilimia 18. Kiwango hiki hakihusishi Makusanyo ya Vocha za misamaha kutoka Serikalini. Ukusanyaji wa mapato halisi kwa mwaka wa fedha 2019/20 na 2018/19 kwa Idara unaonyeshwa na **Kielelezo Na. 10**

**Kielelezo Na. 10: Ulinganifu wa uchangiaji wa makusanyo halisi kwa Idara 2019/20 na 2018/19**




*Chanzo: Taarifa za Makusanyo za Mapato zilizokaguliwa 2019/20 na 2018/19*

Ulinganifu wa uchangiaji wa Makusanyo halisi ya mapato kwa Idara kwenye mwaka wa fedha 2018/19 na 2019/20 unaonyesha kuongezeka katika Idara zote. Jumla ya Makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2019/20 yameongezeka kwa asilimia 14 ukilinganisha na mwaka 2018/19. Ijapokuwa ukilinganisha na makisio ya Idara malengo hayakufikiwa kama inavyoonekana katika **Jedwali 23**.

### 5.2.3 Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato

Mwelekeo wa ukusanyaji wa Mapato wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka mitano iliyopita umeonyesha kuimarika kila mwaka kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali 23**.

**Jedwali Na. 23: Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka 2015/16 hadi 2019/20**

| Mwaka wa Fedha | Makisio (Shilingi Bilioni) | Makusanyo Halisi (Shilingi Bilioni) | Makusanyo ya Juu /(Chini) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 2019/20 | 19,451.12 | 17,930.88 | (1,520.25) | 8 |
| 2018/19 | 18,332.67 | 15,764.66 | (2,568.00) | 14 |
| 2017/18 | 17,365.05 | 15,405.40 | (1,959.65) | 11 |
| 2016/17 | 15,293.90 | 14,271.38 | (1,022.52) | 7 |
| 2015/16 | 12,541.52 | 12,679.81 | 138.29 | 1 |

***Chanzo:** Taarifa za Mahesabu ya Mapato za Mamlaka zilizokaguliwa 2015/16 hadi 2019/20*

Hata hivyo ufanisi katika ukusanyaji wa kodi kwa mwaka wa fedha 2019/20 umefikia asilimia 12.1 ukilinganisha na asilimia 11.6 mwaka 2018/19 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 23**. Ongezeko hili linatoa mwanya kwa serikali kuzidi kufanya juhudi katika kukusanya mapato.

Hata hivyo katika mwaka wa fedha 2019/20 ufanisi wa Mamlaka kwenye ukusanyaji wa Mapato kwa uwiano wa pato la ndani la Taifa umefikia asilimia 12.1 ukilinganisha na asilimia 11.6 mwaka 2018/19. Mchanganuo wa ulinganifu wa uwiano wa kodi na pato la ndani la Taifa kwa Nchi za Africa Mashariki unaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 24**

**Jedwali Na. 24: Ulinganifu wa Uwiano wa Kodi Dhidi ya Pato la Ndani kwa Nchi za Afrika Mashariki**

| Mwaka | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 | 2016/17 | 2015/16 |
|---|---|---|---|---|---|
| Tanzania | 12.10% | 11.60% | 12.30% | 12.40% | 12.20% |
| Rwanda | 15.90% | 16.00% | 15.40% | 15.00% | 15.10% |
| Uganda | 12.10% | 12.60% | 12.00% | 11.70% | 11.30% |
| Kenya | 15.80% | 16.90% | 16.90% | 17.80% | 18.00% |

***Chanzo**: Kitengo cha utafiti, Sera na mipango Cha Mamlaka ya Mapato*

**Naamini kuwa, ufanisi wa kodi Nchini unatoa nafasi ya kukuwa kwa ukusanyaji wa Mapato kwa kuongeza wigo wa kodi, kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi na kuhamasisha ulipaji wa kodi wa hiari ili kupunguza kiwango cha utegemezi wa bajeti kwa nchi.**

### 5.2.4 Masuala Yaliyojitokeza kwenye Ukusanyaji wa Mapato na Mapendekezo

#### 5.2.4.1 Kodi zilizoshikiliwa na Kesi Zilizopo katika Mamlaka za Rufaa za Kodi

Katika ukaguzi wangu wa mwaka huu nimebaini kuwa Mamlaka ya mapato imekuwa na kesi za muda mrefu katika Mamlaka za Rufaa za Kodi zenye thamani ya shilingi 360,081,657,690,115 na dola za Kimarekani 181,430,252 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 25.**

**Jedwali Na. 25: Kesi zilizokuwapo katika Mamlaka za Rufaa za Kodi hadi tarehe 30 Juni 2020**

| Mamlaka za Rufaa za Kodi | Idadi ya Kesi | Kodi zilizoshikiliwa kwenye Mapingamizi | |
|---|---|---|---|
| | | (Shilingi za Tanzania) | (Dola za Marekani) |
| Mahakama ya Rufaa | 20 | 176,832,218,835 | 150,137,310 |
| Baraza la Rufaa za Kodi | 94 | 2,681,308,049,509 | 23,451,738 |
| Bodi ya Rufaa za Kodi | 983 | 357,223,517,421,771 | 7,841,204 |
| **Jumla** | **1,097** | **360,081,657,690,115** | **181,430,252** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya mapato ya Mamlaka 2019/20 na bodi za rufaa 2019/20*

**Naishauri Serikali izidi kuboresha Mamlaka za rufaa za kodi kwa kuziongezea bajeti na rasilimali zingine ili kuziwezesha Taasisi hizi kusikiliza mapingamizi na kuyatolea maamuzi kwa wakati.**

#### 5.2.4.2 Usimamizi wa Malimbikizo ya Madeni ya Kodi.

Mapitio yangu ya malimbikizo ya madeni ya kodi kwenye rejista, Majalada ya walipa kodi, na mfumo wa ITAX yalibaini kutokuwapo kwa taarifa muhimu za kumbukumbu za tathmini ya kodi kwenye malipo na marekebisho ya makosa ya tathmini kwa kiasi cha shilingi 270,601,656,589. Hii imenipa ugumu kwangu wa kuhakiki usahihi wa taarifa hizi. Vivyo hivyo, malimbikizo ya madeni ya kodi ya jumla ya shilingi 13,244,425,721 yalibainishwa kuwa hayakusanyiki. Hata hivyo, baada ya uchunguzi zaidi nilibaini madeni ya kiasi cha shilingi 8,425,526,719 yapo kwenye mapingamizi ya kodi na kiasi cha shilingi 4,734,851,900 kinahusiana na walipa kodi ambao wanaendelea kulipa kodi. Pia, shilingi 84,047,102.02 Mamlaka haikuthibitisha sababu ya kuziainisha kama hazikusanyiki. Pia kiasi cha shillingi 1,304,887,952 kimepunguzwa

kwenye madeni ya kodi wakati hakuna udhibitisho wa malipo ya madeni hayo.

**Naishauri serikali kusahihisha taarifa za malimbikizo ya madeni ya kodi kwa kusuluhisha na kuhakiki taarifa hizo ili kusaidia kutambua madeni halisi na kuweka mikakati ya ukukusanyaji. Pia, kutumia mifumo zaidi katika upatikanaji na utunzaji wa taarifa za walipa kodi ili kuzuia uandaaji wa taarifa nje ya mifumo.**

#### 5.2.4.3 Ushughulikia na Utatuzi wa Mapingamizi ya Kodi

Katika ukaguzi wangu mwaka wa 2019/20 nilitathmini utendaji wa Mamlaka katika kutatua mapingamizi ya kodi na kubaini mapingamizi 44 yenye kodi ya thamani shilingi 38,780,078,621 yaliyopo katika Idara ya Walipakodi Wakubwa, Idara ya Upelelezi wa kodi na Idara ya kodi za Ndani ambayo hayajatatuliwa kwa muda unaotakiwa kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa huduma na mlipa kodi ya mwaka 2017. Kucheleweshwa kwa utatuzi wa mapingamizi ya kodi kunaathiri malengo ya ukusanyaji wa kodi kwani mapingamizi haya yanafunga kiasi kikubwa cha kodi.

**Naishauri Serikali ichukue hatua madhubuti ili kuhakikisha mapingamizi ya kodi yanatatuliwa kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuongeza maafisa wenye weledi na ujuzi wa kutosha kushughulikia mapingamizi ya kodi. Pia, kuwaongezea uwezo maafisa kwa kuwapatia mafunzo na kuimarisha mchakato wa ufanyaji tathmini za kodi.**

### 5.2.5 Kodi ambayo Haikutathiminiwa kwenye Makasha (Makontena) 281 Yaliyoondolewa Bandarini bila Kufuata Masharti ya Vibali vya Dharula.

Mapitio yangu niliyofanya mwaka huu kwenye bandari kavu binafsi (ICDs) nilibaini makontena 281 yalitolewa chini ya vibali vya dharula ambapo wamiliki wa bidhaa hizo walikiuka masharti ya vibali vya dharula kwa kutokufanya tathmini ya kodi na kulipa ndani ya masaa 48 baada ya kutoa mizigo bandarini kama inavyotakiwa na sheria.

**Naishauri Serikali kuhakikisha;**

**a) Waingizaji wa mizigo wanaotumia vibali vya dharura wanakamilisha taratibu za forodha kwa wakati baada ya kupokea bidhaa ili kuepuka upotevu wa mapato ya Serikali;**

**b) Tathmini ya ushuru wa forodha inafanyika na kodi inakusanywa**

**kwenye makontena 281 yalitolewa chini ya idhini ya vibali vya dharura; na,**

c) **Udhibiti unaimarishwa katika mfumo wa TANCIS kwenye usimamizi wa bidhaa zinazotolewa chini ya idhini ya vibali vya dharura.**

### 5.2.6 Magari na Bidhaa (Mitambo) Zilizoingizwa Nchini kwa Muda ambazo Hazijaondolewa Baada ya Muda Kuisha

Mapitio yangu ya taarifa za forodha kwenye magari 936 yaliyoingizwa nchini kwa muda kupitia mipaka ya forodha ya Namanga, Holili, Tarakea, Mtambaswala na Sirari yalibaini kuwa, Magari hayo yamekaa nchini zaidi ya muda ulioruhusiwa bila uthibitisho wa maombi ya waingizaji kuongezewa muda.

Pia, nilibaini bidhaa (mitambo) zenye thamani ya shilingi 20,250,246,269 na ushuru wa forodha shilingi 1,238,374,299 zilizoingizwa kwa muda nchini kupitia mipaka ya Namanga, KIA, Holili na Bandari kavu hazijaondolewa baada ya kumalizika kwa muda ulioruhusiwa kuwapo nchini, wala hazijarasimishwa kwa matumizi ya ndani kama sheria ya forodha inavyoelekeza.

Usimamizi usiojitosheleza kwenye magari na bidhaa (mitambo) zinazoingizwa nchini kwa muda unapelekea matumizi yasiyo halali ya bidhaa hizo nchini, hivyo kupoteza mapato ya Serikali.

**Naishauri Serikali:**

a) **Kufuatilia na kuhakikisha magari 936 yaliyoingizwa kwa muda bila kuondolewa yanakamatwa na kutozwa adhabu stahiki kwa kuchelewa kuondoshwa nchini. Pia kutoza ushuru wa forodha wa shilingi 1,238,374,299 kwa bidhaa (mitambo) ambazo hazijaondolewa nchini;**

b) **Kuhakikiksha ushuru wa forodha kwenye magari na bidhaa (mitambo) zinazorasimishwa kwa matumizi ya ndani unakusanywa kama sheria za forodha inavyoelekeza; na**

c) **Kushirikiana na idara ya Uhamiaji katika kubadilishana taarifa za waingizaji wa magari na bidhaa (mitambo) zinazoingizwa nchini kwa muda.**

### 5.2.7 Usimamizi wa Bidhaa Zilizopita Nchini kwenda Nchi Jirani

#### 5.2.7.1 Bidhaa Zinazopita kwenda Nchi Jirani ambazo Hazikuthibitishwa kutoka Nchini zenye Thamani ya Ushuru wa Forodha Shilingi 5,135,360,992

Katika ukaguzi wangu wa bidhaa zinazopita nchini kuelekea nchi jirani kupitia mipaka ya forodha ya Tunduma, Kasumulu, Rusumo, Kabanga, Mutukula, Namanga, Holili na Kigoma kwa kuangalia mfumo wa TANCIS na nyaraka za kusafirishia nilibaini kutothibitishwa kutoka nchini bidhaa zenye makadirio ya kodi ya forodha shilingi 5,135,360,992.

**Naishauri Serikali iimarishe udhibiti katika usimamizi wa bidhaa zinazopita nchini, ikiwa ni pamoja na kuthibitisha taarifa za utokaji katika mfumo wa TANCIS kwa bidhaa zinazopita ili kuhakikisha hazitumiki nchini kinyume na sheria kuepuka upotevu wa mapato ya Serikali.**

#### 5.2.7.2 Mafuta Yaliyopitiliza Muda wa Kukaa Nchini ambayo Yalipaswa kwenda Nchi Jirani yenye Ushuru wa Forodha Shilingi 12,136,729,035

Wakati wa Mapitio yangu kwenye ujazo wa mafuta yaliyopita kwenda nchi jirani nilibaini yafuatayo:

(a) Lita 2,471,629 za mafuta zenye makadirio ya ushuru wa forodha shilingi 1,970,211,327 yalibaki nchini bila kusafirishwa kwenda nchi zilizokusudiwa kwa muda uliopangwa wa siku 30. Zaidi, niligundua kati ya lita hizo kuna kiasi cha mafuta yaliyokaa kwa kipindi kirefu cha siku 365 bila kurasimishwa kwa matumizi ya ndani ili kutozwa ushuru unaotakiwa kama sheria ya forodha inavyoelekeza.

(b) Lita 14,078,214 za mafuta yenye ushuru wa forodha unaokadiriwa kufikia shilingi 10,432,300,878 zilizoshushwa nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda Zanzibar tangu Julai 2019 hazijaondoshwa wala kurasimishwa kwa matumizi ya ndani.

**Naishauri serikali kuimarisha mifumo ya udhibiti na usimamizi wa mafuta yanayopitia nchini ili kuepuka urasimishaji usio halali wa mafuta. Pia kukusanya ushuru wa forodha wa Sh.12,136,729,035 kwenye lita 16,549,843 za mafuta ambayo hayakuondoshwa nchini.**

### 5.2.8 Usimamizi wa Ukaguzi wa Walipakodi

Katika mapitio yangu ya mafaili ya ukaguzi wa walipa kodi kwa mwaka wa fedha 2019/20 nilibaini kuwapo kwa ukadiriaji wa chini wa kodi ya jumla ya shilingi 29,656,926,568 ikiwa kodi ya mapato shilingi 25,259,488,482, kodi ya uendelezaji ufundi stadi shilingi 915,303,425 na kodi ya zuio shilingi 3,482,134,661. Ukadiriaji huu wa chini wa kodi ya mapato umetokana na udanganyifu wa gharama za uzalishaji na uendeshaji wa biashara za walipa kodi kama riba za mikopo ya mabenki, ushuru wa huduma ya miji au majiji na manunuzi kwa ujumla.

Pia, umesababishwa na udanganyifu kwenye mauzo ya walipa kodi wakati wa uandaaji wa mahesabu ya mwaka na miamala ya kibiashara kati ya makampuni yenye umiliki mmoja. Vilevile ukadiriaji wa chini wa kodi ya uendelezaji ufundi stadi umetokana na udanganyifu wa walipa kodi kwenye gharama za mishahara ya wafanyakazi wakati kwenye kodi ya zuio umetokana na udanganyifu kwenye viwango vya gharama za huduma, gawio, riba, mrabaha na kodi za pango zinazolipwa ama kupokelewa na walipa kodi.

**Naishauri serikali kuhakikisha Mamlaka inapatiwa wakaguzi wa kodi wa kutosha na wenye ujuzi. Pia, iwajengee uwezo wakaguzi wakodi waliopo. Zaidi, iwasaidie kuuboresha mfumo wa kodi kuwezesha uchambuzi makini wa data.**

### 5.2.9 Usimamizi wa Adhabu, Ada, Faini na Riba

Ukaguzi wangu katika utendaji wa mamlaka ya mapato kwa mwaka wa fedha 2019/20 ulibaini baadhi ya sheria, kanuni na taratibu za kodi hazizingatiwi na walipa kodi kama inavyotakiwa. Hata hivyo, haikutolewa adhabu yoyote kwa walipa kodi kutotii sheria na taratibu. Yafuatayo ni makosa yaliyobainika:

(a) Adhabu ya shilingi 66,560,000 ambayo haikutozwa kwa mizigo 1,664 iliyochelewa kutoka katika sehemu za forodha bila kutolewa sababu katika mfumo wa TANCIS wala nyaraka za kusafirishia mizigo zilizowasilishwa wakati wa ukaguzi wangu.

(b) Hakuna adhabu ya asilimia mbili ya shilingi 2,254,607,733.86 iliyotozwa na kukusanywa kwa kucheleweshwa kwa malipo ya miamala 750 kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani na mafuta yaliyorasimishwa kwa matumizi ya ndani kwa

kutosafirishwa nje ya nchi yanayohusiana na makampuni 29 ya uuzaji wa mafuta.

(c) Adhabu ya shilingi 2,385,229,012.17 haikutozwa kwa bidhaa zinazosafirishwa kwenda nchi jirani zilizotolewa baada ya kumalizika kwa kipindi cha kisheria katika eneo la mpaka wa forodha wa Rusumo, Kabanga, Mutukula, Tunduma na Kasumulu.

Makosa yaliyoainishwa yamesababishwa na matumizi yasiyojitosheleza ya mfumo wa TANCIS kwa maafisa wa forodha wakati wa kukagua, kuchambua, na kuoanisha taarifa ziliyotolewa na walipa kodi.

**Naishauri Serikali kuhakikisha;**

**(a) Inasimamia sheria za kodi na kuweka mazingira rafiki ya ulipaji wa kodi kwa hiyali**

**(b) Adhabu zinatozwa na kukusanywa kutoka kwa walipa kodi wasiotii sheria za kodi; na**

**(c) Maafisa wa forodha wanapitia kwa ufasaha na kulinganisha taarifa zinazowasilishwa na walipa kodi ili kuepuka kutotoza adhabu stahiki kwa walipa kodi wasiotii sheria.**

### 5.2.10 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Kodi na Mapato Mengine ya Serikali

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini yafuatayo katika ukusanyaji wa mapato:

a) Kutokukusanywa kwa ushuru wa forodha na ada shilingi 408,723,375 kwenye lita 3,887,849 za shehena ya mafuta kutoka nje zilizokusudiwa kutumika katika shughuli za uchimbaji madini kutokana na kushindwa kwa udhibiti uliowekwa katika usimamizi wa tathmini ya kodi kwenye mfumo wa TANCIS.

b) Makadirio ya chini ya shilingi 8,895,045,787 ya kodi ya ongezeko la thamani yaliyofanywa na walipa kodi kutokana na tamko la chini la mauzo katika ritani za kila mwezi ikilinganishwa na mapato yaliyowasilishwa katika vitabu vya mahesabu ya mwaka vya walipakodi. Hii ilitokana na uhakiki usiojitosheleza wa taarifa zilizotolewa na walipa kodi kama vile ritani za malipo ya kodi ya ongezeko la thamani zilizowasilishwa kila mwezi, mauzo ya EFD, na taarifa za mahesabu ya mwaka

c) Udhaifu katika Mfumo wa usimamizi wa kodi ya majengo katika kutengeneza ankara za walipa kodi kwa wakati uliosababisha lengo la makusanyo kwa mwaka kutokufikiwa; na

d) Kutoshabihiana kwa taarifa za malimbikizo ya madeni ya kodi ya majengo kati ya rejista za madeni zilizoandaliwa ukilinganisha na taarifa zilizochukuliwa kwenye mfumo wa usimamizi wa kodi za majengo kwa mikoa mitano ya kikodi.

**Naishauri Serikali kuimarisha mifumo ya mapato ili kuwezesha ulinganifu na uthibitishaji wa taarifa za walipa kodi kuhakikisha ongezeko kwenye ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa ustawi wa taifa letu.**

## 5.3 Usimamizi wa Deni la Serikali na Huduma za Jumla

Deni la Serikali linajumuisha madeni yote inayodaiwa serikali ndani na nje ya nchi kupitia Serikali Kuu na wakala zake. Kwa madhumuni ya ufanisi katika usimamizi wa deni, Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango amepewa mamlaka ya kipekee ya kukopa kwa niaba ya serikali mikopo ya nje na ndani, na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali kama ilivyoainishwa chini ya vifungu 3,6, na 13 vya sheria ya mikopo, dhamana na ruzuku za serikali. Na. 30 ya 1974 kama iliyorejewa 2004 ikisomwa pamoja na marekebisho ya mwaka 2017.

### 5.3.1 Mchanganuo wa Deni la Serikali

Deni la Serikali kufikia tarehe 30 Juni 2020 lilikuwa Shilingi bilioni 56,757 ikilinganishwa na Silingi bilioni 53,105 lililoripotiwa mwaka wa fedha 2018/19. Kuna ongezeko la Shilingi bilioni 3,652, sawa na asilimia saba ikilinganishwana na shilingi bilioni 2,178 kwa mwaka uliopita.

Deni la Serikali linajumuisha deni la ndani na la nje Sh. bilioni 15,515 na bilioni Sh.41,242 kwa mwaka wa fedha 2019/20, mtawalia ikilinganishwa na Sh.bilioni 14,863 and Sh.bilioni 38,241 mwaka 2018/19. Kielelezo Na. 11 kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa deni kwa miaka mitatu iliyopita.

**Kielelezo Na. 11: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali kwa Miaka Mitatu**




*Chanzo: Hesabu za fedha fungu Na. 22-deni la serikali kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2018, 2019 na 2020.*

### 5.3.2 Mwenendo wa Deni la Ndani

Kwa mwaka 2019/20 deni la ndani limeongezeka kwa shilingi bilioni 652, sawa na 4% ya deni la ndani lililoripotiwa mwaka 2018/19. Mwenendo wa ukuaji wa deni la ndani kwa miaka mitatu umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 26**

**Jedwali Na. 26: Mwenendo wa Deni la Ndani kwa Miaka Mitatu (Deni Halisi)**

| Mwaka wa fedha | Thamani ya deni (Sh. bilioni) | Ongezeko | |
|---|---|---|---|
| | | (Sh. bilioni) | % |
| 2019/20 | 15,515 | 652 | 4 |
| 2018/19 | 14,863 | 131 | 1 |
| 2017/18 | 14,732 | 1,397 | 10 |

*Chanzo: Jedwali la mwenendo wa deni la serikali kwa miaka 2017/18 hadi 2019/20*

Vilevile, ukaguzi wangu ulibaini Serikali ilikopa jumla ya fedha zenye thamani ya Sh. bilioni 5,335. Kati ya hizo, Sh. bilioni 2,236 (sawa na 42%) zilikuwa mikopo ya muda mfupi na Shilingi bilioni 3,099 (sawa na 58%) zilikuwa mikopo ya muda mrefu kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 27**

**Jedwali Na. 27: Mwenendo wa Ukopaji wa Ndani kwa Miaka Mitatu (Thamani halisi)**

| | 2019/20 | | 2018/19 | | 2017/18 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukopaji wa | Sh. bilioni | % | Sh. bilioni | % | Sh. bilioni | % |
| Muda mrefu | 3,099 | 58 | 1,273 | 29 | 2,911 | 44 |
| Muda Mfupi | 2,236 | 42 | 3,075 | 71 | 3,753 | 56 |
| Jumla ya ukopaji | 5,335 | 100 | 4,348 | 100 | 6,664 | 100 |

*Chanzo: Jedwali la mwenendo wa deni la serikali kwa miaka 2017/18 hadi 2019/20*

### 5.3.3 Mwenendo wa Deni la Nje

Deni la nje kufikia tarehe 30 Juni 2020 lilikuwa Shilingi bilioni 41,242 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 3,001 (sawa na 8%) ikilinganishwa na deni la Shilingi bilioni 38,241 lililoripotiwa mwaka 2018/19 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 28**.

**Jedwali Na. 28: Mwenendo wa Deni la Nje kwa Miaka Mitatu**

| **Wakopeshaji** | **2019/20** | | **2018/19** | | **2017/18** | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Sh. Bilioni** | **%** | **Sh. bilioni** | **%** | **Sh. bilioni** | **%** |
| Taasisi za Kimataifa | 24,150 | 59 | 22,116 | 58 | 20,843 | 58 |
| Nchi Marafiki | 4,773 | 12 | 4,469 | 12 | 4,145 | 11 |
| Benki za kuwezesha biashara ya Forodha | 6,257 | 15 | 6,368 | 17 | 6,056 | 17 |
| wakopeshaji wa kibiashara | 6,062 | 15 | 5,288 | 14 | 5,151 | 14 |
| **Jumla ya deni** | **41,242** | **100** | **38,241** | **100** | **36,194** | **100** |
| **Ongezeko** | **3,001** | **8** | **2,047** | **6** | **3,448** | **11** |

*Chanzo: Jedwali la mwenendo wa deni la serikali kwa miaka 2017/18 hadi 2019/20*

Ukaguzi wangu umebaini ongezeko la deni la nje linasababishwa na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kutoka taasisi za kimataifa, nchi marafiki, benki za kuwezesha biashara ya forodha, na wakopeshaji wa kibiashara kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 29**

**Jedwali Na. 29: Mwenendo wa Ukopaji wa Nje kwa Miaka Mitatu**

| Wakopeshaji | 2019/20 | | 2018/19 | | 2017/18 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shilingi bilioni | % | Shilingi bilioni | % | Shilingi bilioni | % |
| Taasisi za Kimataifa | 2,393 | 49 | 1,557 | 45 | 1,986 | 50 |
| Nchi Marafiki | 143 | 3 | 165 | 5 | 125 | 3 |
| Benki za kuwezesha biashara ya Forodha | 170 | 3 | 496 | 14 | 493 | 13 |
| Wakopeshaji wa Kibiashara | 2,220 | 45 | 1,210 | 35 | 1,354 | 34 |
| **Jumla ya Fedha iliyokopwa** | **4,925** | **100** | **3,429** | **100** | **3,958** | **100** |

*Chanzo: Jedwali la mwenendo wa deni la serikali kwa miaka 2017/18 hadi 2019/20*

### 5.3.4 Matokeo ya Ukaguzi wa Usimamizi wa Deni la Serikali na Huduma za Jumla

#### 5.3.4.1 Uendeshaji wa Idara ya Usimamizi wa Madeni (DMD)

Katika ukaguzi wangu wa muundo wa Wizara ya Fedha na Mipango nilibaini kuanzishwa kwa idara ya usimamizi wa madeni (DMD) ili kusimamia shughuli zote zinazohusiana na madeni ya serikali. Idara ina vitengo vitatu ambavyo ni Uhamasishaji wa Rasilimali, Usimamizi wa Vihatarishi na Usimamizi wa kanzidata. Hatahivyo kuna muingiliano wa majukumu baina ya vitengo. Mathalani, kitengo cha Usimamizi wa kanzidata kina jukumu la utunzaji wa mikataba ya deni la nje jukumu ambalo pia ni la kitengo cha Uhamasishaji wa Rasilimali. Pia, nimebaini kutokuwapo kwa kitengo kinachohusika na uhasibu hivyo kupelekea kutofikia malengo ya idara.

**Ninaishauri serikali irekebishe muundo wa Wizara ya Fedha na Mipango ili kuwapo na kitengo kinachoshughulikia masuala ya uhasibu na kuzuia muingiliano wa majukumu ili kuimarisha uwajibikaji.**

#### 5.3.4.2 Usimamizi wa Mikataba ya Mikopo

Nilibaini uchelewaji kwenye kuanza na kuendelea kutumia fedha kutoka kwa wakopeshaji hali iliyosababishwa na mipango duni ya matumizi ya fedha za mikopo kabla ya kusaini mikataba ya ukopaji. Mpangilio dhaifu wa utekelezaji mikataba ya miradi umesababisha ongezeko la

gharama za ukopaji ikiwemo tozo ya kutengewa fedha (Commitment charge).

**Naishauri Serikali Kuweka mipango madhubuti ya matumizi ya fedha za mikopo kabla ya kusaini mikataba ya mikopo. Pia iimarishe usimamizi wakati wa utekelezaji ili kuepuka ucheleweshaji wa kuchukua fedha zilizokopwa ambazo zinasababisha ongezeko la gharama za mkopo, kama vile tozo ya kutengewa fedha (Commitment charge)**

#### 5.3.4.3 Ukosefu wa Kanzidata Moja ya Kitaifa kwa Miradi ya Maendeleo

Nilibaini kuwa, Wizara ya Fedha na Mipango ilipanga kuunda kanzidata moja ya taifa ya usimamizi wa taarifa za Miradi (NPMIS) tangu 2010. Hata hivyo, hadi Juni 2020 mfumo huo ulikuwa haujaanza kutumika kikamilfu. Zaidi ya hayo, nilibaini taarifa za miradi zimetawanyika katika Idara mbalimbali za wizara hiyo. Mathalani, kanzidata ya miradi inayofadhiliwa na misaada na fedha za wahisani inasimamiwa na Idara ya fedha za nje, wakati miradi inayofadhiliwa na mikopo inasimamiwa na idara ya mhasibu mkuu wa Serikali, kitengo cha deni la Serikali. Zaidi, kanzidata ya miradi inayotekelezwa kutumia mapato ya ndani inasimamiwa na divisheni ya bajeti. Hata hivyo, taarifa za utekelezaji wa miradi inasimamiwa na watekelezaji wa miradi husika, kinyume na matakwa ya kanuni 14(c) ya Kanuni za Mikopo, Ruzuku na Dhamana za Serikali ya mwaka 2003.

Kutokuwapo kwa kanzidata moja ya taifa ya usimamizi wa miradi inayotekelezwa na serikali kunaathiri ufuatiliaji, uratibu na uthaminishaji wa miradi katika ngazi ya taifa ambayo ingesaidia kurahisisha mchakato wa kufanya maamuzi.

**Naishauri Serikali iandae mpango kazi utakaowezesha kukamilisha utengenezaji na kutumika kikamilifu kwa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi kwa wadau wote ndani ya muda uliopagwa.**

#### 5.3.4.4 Majadiliano (Negotiations) Yanayohusu Kukopa kwa Serikali

Nilibaini kuwa majadiliano ya mikopo ya serikali hufanywa bila kuzingatia ubobezi wa watumishi wanaoshiriki katika majadiliano husika. Hii imetokana na kutokua na utaratibu rasmi wa kuteuwa kiongozi wa mazungumzo na timu mahsusi yenye ujuzi na weledi katika kufanya majadiliano ya mikopo yaletayo unafuu katika ukopaji wa serikali.

**Naishauri serikali iweke utaratibu rasmi wa kumteua kiongozi wa mazungumzo na timu mahsusi yenye ujuzi na weledi ili kufanya majadiliano ya mikopo yaletayo unafuu zaidi kwa Serikali.**

## 5.4 Usimamizi wa Huduma za Jumla

### 5.4.1 Kutohuishwa kwa Mwongozo wa Kitengo cha Pesheni kwa Zaidi ya Miaka 15

Nilibaini kuwa, kitengo cha pensheni kinatumia mwongozo wa mwaka 2005 ambao haujahuishwa kwa zaidi ya miaka 15, hivyo kutokuendana na mazingira ya sasa; hatimaye kukwamisha ufanisi katika kufanikisha wajibu wa Kitengo cha pensheni.

**Nashauri serikali kufanya maboresho kwenye mwongozo wa pensheni ili kuendana na mazingira ya sasa na kuongeza ufanisi katika kushughulikia pensheni za watumishi waliomaliza muda wao kazini**

### 5.4.2 Ukaguzi wa Awali wa Mafao ya Watumishi Waliomaliza Muda Kazini

Ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi waliomaliza muda kazini hufanyika kwa mujibu wa Ibara 143(2)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuidhinisha malipo kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kujiridhisha kuwa Ibara ya 136 ya Katiba imezingatiwa.

Ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi waliomaliza muda wao kazini hufanyika kwa kuzingatia Sheria za mafao ambazo ni pamoja na Sheria ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ya mwaka 2006, Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002, Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ya mwaka 1997, Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 2018, Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966 (Iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002), Sheria ya Utumishi wa Usalama wa Taifa ya mwaka 1996, Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2008, Sheria ya Mafao ya Kustaafu ya GEPF ya mwaka 2013, Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999, pamoja na Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 iliyo rekebishwa mwaka 2016.

Ukaguzi wa awali unafanyika kuhakiki usahihi wa mafao ya watumishi waliomaliza muda wao kazini yaliyoandaliwa na waajiri kuwalipa wanufaika ili kuwezesha kutambua makosa mapema kabla ya malipo kufanyika kwa lengo la kuhakikisha mafao hayazidishwi au kupunjwa. Makosa hayo ni; kipindi kisicho sahihi cha utumishi, mishahara isiyo sahihi iliyotumika kukokotoa mafao, michango ya watumishi isiyo sahihi na makosa ya majumuifu.

### 5.4.3 Mawanda ya Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wangu wa awali wa mafao ya watumishi waliomaliza muda wao kazini unahusisha watumishi wa umma ambao mafao yao hulipwa kutoka mfuko mkuu wa serikali. Mafao yanayolipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni: Pesheni kwa watumishi wa umma watoa huduma waliofanya kazi serikali za mtaa na serikali kuu (public servants with mixed service), askari na maafisa wa jeshi, walimu na maafisa usalama; mafao kwa watumishi waliomaliza mikataba ya uongozi wa kisiasa, wageni toka nje, wastaafu waliorejeshwa kwenye utumishi na raia walioajiriwa wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45; mafao kwa watumishi wasio kwenye masharti ya pensheni; pamoja na mafao kwa askari polisi.

### 5.4.4 Utekelezaji Ukaguzi wa Awali

Katika ukaguzi wangu wa mwaka huu nilikuwa na jumla ya majalada 2686 kwa ajili ya ukaguzi wa awali, ambapo 316 ni bakaa kutoka mwaka 2018/2019 na majalada 2370 yaliwasilishwa na maafisa masuuli katika mwaka wa ukaguzi 2019/20.

Kati ya majalada hayo, nilifanikiwa kukagua majadala 2502, ambapo majalada 2328 yenye thamani ya Sh. bilioni 154.27 niliyaidhinisha kwa malipo. Majalada 174 nilibaini yana mapungufu na kuyarejesha kwa ajili ya marekebisho kabla ya kuyaidhinisha. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 majalada 184 yalikuwa bado yanaendelea kukaguliwa katika ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

### 5.4.5 Matokeo ya Ukaguzi wa Awali wa Mafao

Wakati wa ukaguzi wangu wa awali wa mafao ya watumishi waliomaliza muda kazini kwa mwaka wa fedha 2019/20 nilibaini masuala yafuatayo:

#### 5.4.5.1 Kiasi cha Mafao Kilichokosewa na Maafisa Masuuli Wakati wa Ukokotoaji

Katika ukaguzi wangu wa majalada ya mafao 2328 niliyoyaidhinisha kwa malipo nilibaini majalada 372 (16%) yalikokotolewa kimakosa kama kipindi cha utumishi kisicho sahihi, mishahara iliyokosewa, makosa katika Michango ya hifadhi ya Jamii; pamoja na makosa mbalimbali katika ukokotoaji.

Kati ya 372, majalada 211 ya mafao yalikokotolewa zaidi ya kiwango stahiki kwa jumla ya shilingi milioni 652.59 na majalada 161 yalikokotolewa kwa kiwango pungufu kwa jumla ya shilingi milioni 430.04 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 30.**

**Jedwali Na. 30: Mafao Yaliyokokotolewa Kimakosa**

| Na | Maelezo | Mafao yaliyozidishwa | | Mafao yaliyopunjwa | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Majalada | Kiasi (Sh. Milioni) | Idadi ya Majalad a | Kiasi (Sh. Milioni) |
| 1 | Kipindi cha utumishi kisicho sahihi | 124 | 357.39 | 85 | 173.64 |
| 2 | Mishahara ya iliyokosewa | 30 | 163.41 | 45 | 115.71 |
| 3 | Makosa katika Michango ya hifadhi ya Jamii | 32 | 27.41 | 16 | 22.92 |
| 4 | Makosa mbalimbali katika ukokotoaji | 25 | 104.37 | 15 | 117.75 |
| | **Jumla** | **211** | **652.59** | **161** | **430.04** |

*Chanzo: Fomu za malipo ya mafao na uhakiki wa Mdhibiti Mkuu*

**Naishauri Serikali kuhakikisha inaimarisha mifumo ya udhibiti ya ndani ili kuepuka kufanya makosa kwenye ukokotoaji wa mafao ya watumishi waliomaliza muda wao kazini kabla ya kuwasilisha kwa ukaguzi wa awali ili kuwezesha ufanyaji wa malipo sahihi kwa wakati. Hii itaondoa hatari ya Serikali kupoteza fedha kutokana na kuzidisha malipo na kuepuka kuwapunja wastaafu malipo ya mafao.**

#### 5.4.5.2 Ucheleweshwaji wa Uandaaji wa Mafao

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2019/20 nilibaini ucheleweshaji uliofanywa na Maafisa Masuuli wa Serikali kwenye uandaaji na uwasilishwaji wa majalada 750 ya watumishi waliomaliza muda wao kazini kwenye ofisi yangu kwa ajili ya ukaguzi wa awali kwa kipindi cha miaka hadi 30 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 31**

**Jedwali Na. 31: Majalada Yaliyocheleweshwa Kuandaliwa na Kuwasilishwa kwa Ukaguzi wa Awali**

| Kipindi cha ucheleweshaji | *Idadi ya Majalada* |
|---|---|
| Hadi miaka 4 | 572 |
| Hadi miaka 9 | 91 |
| Hadi miaka 14 | 30 |
| Hadi miaka 20 | 26 |
| Hadi miaka 24 | 17 |
| Hadi miaka 30 | 14 |
| **Jumla** | **750** |

*Chanzo: Fomu za malipo ya mafao*

Ucheleweshwaji huu unaathili hali ya maisha ya wastaafu kwani wengi wao hutegemea mafao ya kustaafu kama pato la kuanzia maisha baada ya kumaliza utumishi wa umma.

**Naishauri serikali kuhakikisha inashughulikia kwa haraka na wakati majalada ya mafao ya watumishi ambayo nimebainisha makosa mbalimbali ili kuepuka ucheleweshaji wa malipo ya wastaafu.**

### 5.5 Ukaguzi wa Hesabu Jumuifu

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilirasimisha matumizi ya Kanuni za Uhasibu za Kimataifa katika Sekta ya Umma (IPSAS accrual basis of accounting) katika kuandaa hesabu kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Hivyo Serikali iliandaa hesabu jumuifu kwa mara ya kwanza kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2013 kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Uhasibu za Kimataifa katika Sekta ya Umma (IPSAS 35).

Hata hivyo serikali bado inakabiliwa na changamoto zinazoathiri kufanikisha kwa ukamilifu utekelezaji wa taratibu za hesabu jumuifu kama nilivyoona katika ukaguzi wangu wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2019/20. Changamoto hizo ni pamoja na:

### 5.5.1 Kukosekana kwa Mpango wa Uunganishaji wa Mfumo wa Uandaaji wa Hesabu Jumuifu (GACS) na Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) Pamoja na Mifumo Mingine ya Usimamizi wa Fedha Serikalini.

Nilipitia na kuainisha uunganishaji wa kimkakati wa Mfumo wa uandaaji wa Hesabu Jumuifu (GACS) na mifumo mingine mikubwa ya mahesabu serikalini. Nilibaini kuwa taarifa za fedha zilizokaguliwa za taasisi za Serikali haziingizwi kwenye mfumo wa GACS na mfumo wa taasisi husika ya utengenezaji taarifa hizo hivyo kuingizwa na wahasibu wa taasisi, kisha kuhahikiwa na kudhibitishwa na timu inayoandaa hesabu jumuifu kabla ya kujumuishwa kwenye hesabu jumuifu.

Ni maoni yangu kuwa, mchakato huu unakabiliwa na makosa ya kibinadamu na gharama za usimamizi ambapo unaweza kusababisha kutumia muda mwingi na mapungufu katika hesabu.

Nilijulishwa kuwa, mfumo wa Uandaaji wa Hesabu Jumuifu (GACS) utaunganishwa na Mfumo wa ulipaji Serikalini (MUSE) kuwezesha upatikanaji wa miamala kwa wakati mubashashara na Hesabu Jumuifu. Hata hivyo, nilibaini hakukuwa na mpango ulioanisha shughuli na muda wa namna ya kufanikisha uunganishaji wa mfumo wa GACS na MUSE pamoja na mifumo mingine ya hesabu serikalini.

Ni maoni yangu kuwa, kukosekana kwa mpango wa uunganishaji kunaweza kusababisha kukosekana hali ya uwajibikaji, umakini na kushindwa kutathmini mchakato wa uunganishaji utakaosabisha muendelezo wa mapungufu katika uandaaji wa hesabu jumuifu.

**Napendekeza serikali kuweka kipaumbele uunganishaji wa mfumo wa uuandaji wa hesabu jumuifu (GACS) na Mfumo wa Malipo Serikalini (MUSE) pamoja na mifumo mingine ya usimamizi wa fedha serikalini na kuunda timu ya pamoja ambayo itaandaa na kutekeleza mpango kwa ajili ya mchakato wa uunganishaji wa mifumo unaoleza hatua na matokeo.**

### 5.5.2 Kutofanyika kwa Tathmini ya Hali ya Kifedha kwenye Mfuko wa Hifadhi wa Watumishi wa Umma.

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu yalibaini Serikali ilitoa taarifa ya madeni ya Sh.19,095,594,000,000 ya mifuko ya pesheni ambayo hakijabadilika tangu mwaka wa fedha 2016/17 kinyume na Kifungu Na. 57(1) na (2) cha Sheria ya Mfuko wa hifadhi ya jamii ya utumishi wa umma 2018 (PSSSF) na Kifungu Na.57(a) cha Sheria ya Mifuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) 1997 ambazo zinaitaka bodi kufanya tathmini ya hali ya kifedha ya mifuko kila baada ya miaka mitatu, pia kuzingatia miongozo inayotolewa na bodi.

Ni maoni yangu kuwa, kukosekana kwa tathmini ya kitaalamu ya hali ya fedha ya mifuko ya pesheni kunaweza kusababisha kutoa taarifa za madeni katika hesabu jumuifu ambazo haziakisi ukweli na haki.

**Nashauri Serikali kufanya tathmini ya kitaalamu ya hali ya fedha ya mifuko ya pesheni na kutoa taarifa za madeni ya mifuko hiyo kwenye Hesabu Jumuifu kwa usahihi.**

### 5.5.3 Ujumuishaji wa Taarifa za Fedha za Taasisi za Serikali ambazo Zimekosa Umiliki wa Maafisa Masuuli au Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi

Kanuni ya 11(3)(a) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (iliyorekebishwa 2004) inaelekeza kwamba "Afisa Masuuli atahitajika kutia saini matumizi, taarifa za utendaji na taarifa za mahesabu zingine alizokasimiwa kusimamia chini ya masharti ya Sheria au Kanuni hizi, na kwa kufanya hivyo anakubali uwajibikaji wa kibinafsi kwa uwasilishaji taarifa sahihi kama ilivyoelekezwa katika kanuni hizi au na Mhasibu Mkuu wa Serikali".

Mapitio yangu ya sampuli 250 za taarifa za kifedha za taasisi za Serikali zilijumuishwa katika hesabu jumuifu zilizoandaliwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali nilibaini taarifa za kifedha za taasisi 111 sawa na 44.4% ya sampuli iliyochaguliwa havikuwa na saini za Maafisa Masuuli au Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi husika kuonesha umiliki na kukubali jukumu la usahihi, ukamilifu na uwasilishaji wake.

Niliangazia suala hili kupitia Aya Na 5.4.5 na 5.4.2.5 katika ripoti zangu za serikali kuu za mwaka 2017/18 na 2018/19 mtawalia. Bado taarifa

zilizojumuishwa kwenye hesabu jumuifu zina ukosefu wa umiliki wa Maafisa Masuuli husika.

**Ninasisitiza pendekezo langu la miaka iliyopita kuwa Serikali ijumuishe taarifa za kifedha za taasisi ambazo zimesainiwa na Maafisa Masuuli na Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi kwenye hesabu Jumuifu.**

### 5.5.4 Uondoshwaji wa Miamala katika Hesabu Jumuifu

Aya ya 40 (a) hadi (c) ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma (IPSAS 35) inaitaka taasisi inayoandaa taarifa Jumuifu kuunganisha mali, madeni, mapato na matumizi ya taasisi zinazodhibiti na zile taasisi zinazodhibitiwa. Pia, inataka kuondoa mali, madeni, mali halisi, mtaji, mapato, matumizi na mtiririko wa fedha kwa miamala baina ya taasisi zinazohusiana. Lengo la utaratibu huu ni kuondoa uwezekano wa kuripoti miamala mara mbili, na kuboresha uhalisia wa taarifa za hesabu jumuifu.

Mapitio yangu ya Taarifa za hesabu jumuifu na taarifa za kifedha za taasisi za kiserikali kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020 nilibaini mapungufu yafuatayo:

#### 5.5.4.1 Kutoondoshwa kwa Mikopo kwenye Deni la Serikali katika Hesabu Jumuifu Sh. Bilioni 2,464.5

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu ya mwaka ulioishia 30 Juni 2020 nilibaini kuwa jumla ya kiasi cha Sh 2,464,491,922,880 ikiwa ni nakisi ya serikali Sh. 780,154,646,991.25, hisa za serikali Sh 252,724,429,876.59, hati fungani maalum Sh 1,027,673,228,012.25, Dhamanaza serikali 403,939,617,999.91ambazo hazikuondolewa katika deni la serikali la Sh.51,327,383,136,000 lililoripiwa katika hesabu jumuifu.

#### 5.5.4.2 Kutoondoshwa kwa Dhamana za Serikali kwenye Hesabu Jumuifu Sh. Bilioni 1,192.9

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu yalibaini kuwa Kiasi cha Sh 1,230,069,507,000 ziliripotiwa kama dhamana za Serikali. Mapitio ya malelezo ya taarifa za fedha Na. 76 katika hesabu jumuifu na taarifa za fedha za Benki kuu ya Tanzania nilibaini kuwa, Sh1,192,981,801,000 zimejumuisha dhamana maalum za hazina Sh. 991,590,579,000 na ya Hisa za EPA Sh. 201,391,222,000 zinazomilikiwa na Benki ya Tanzania.Hata hivyo jumla ya salio la sh. 1,192,981,801,000 halikuondolewa kikamilifu

kwenye hesabu Jumuifu ya Sh. 1,230,069,507,000 kama inavyotakiwa na Aya 40 (c) ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma Na. 35.

### 5.5.4.3 Kutoondoshwa kwa Miamala ya Amana ya Kudumu Inayohusiana na Taasisi za Serikali Kuu Sh. bilioni 9.2.

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu yalibaini kuwa sh. 266,451,471,000 ziliripotiwa kama amana za kudumu. Mapitio ya kina ya taarifa ya maelezo Na. 71 (Note 71) yalibaini kuwa sh. 9,287,034,000 zilihusiana na amana za kudumu za Serikali kwenye benki za serikali/ taasisi za kifedha za serikali kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.32**, hatahivyo, kiasi hicho hakikuondolewa kwenye salio la hesabu jumuifu.

**Jedwali Na. 32: Kutoondolewa kwa Miamala ya Amana za Kudumu Inayohusiana na Taasisi za Serikali**

| Na. | **Taasisi zilizo na amana kutoka taasisi nyingine za serikali** | **Kiasi Sh. '000'** |
|---|---|---|
| 1 | Benki ya uwekezaji Tanzania | 7,611,802 |
| 2 | Mfuko wa uwekezaji (UTT) | 1,675,232 |
| | **Jumla** | **9,287,034** |

*Chanzo: Mfumo wa uandaaji hesabu jumuifu na Hesabu Jumuifu za mwaka wa fedha 2019/20*

### 5.5.4.4 Kutothibitishwa kwa Uondoshwaji wa Madai, Malipo ya Awali na Madai ya Mikopo Kiasi cha sh.687.8 Bilioni

Mapitio yangu ya taarifa za kifedha za taasisi za serikali (nakala ngumu) yalibaini kuwa, jumla ya Sh 687,874,113,000 ikiwa ni madai, malipo ya mapema na madai ya mikopo yanayohusu taasisi za serikali hayakuwa na ushahidi wa kuondoshwa katika hesabu jumuifu. Rejea **Kiambatisho Na. IX** kwa maelezo zaidi.

**Ninapendekeza Serikali ianzishe mfumo mahususi kwa ajili ya kuwezesha taasisi za serikali kuripoti taarifa zinazohusiana na kutekeleza mfumo wa uhakiki wa takwimu zilizoripotiwa kwaajili ya ufanisi katika uondoshwaji ili kuripoti takwimu sahihi**

### 5.5.5 Kutotambuliwa kwa Mashamba Makubwa ya Misitu katika Hesabu Jumuifu.

Aya ya 13 ya Viwango vya Kimataifa vya uandaaji Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSAS) Na. 27 inazitaka taasisi kutambua mali za kibaolojia au mazao ya kilimo iwapo taasisi ina Udhibiti wa mali uliotokana na matukio ya zamani, uwezekano wa mali hiyo kuleta faida za kiuchumi kwa taasisi hapo baadaye na kuwepo kwa uwezekano wa kupima thamani ya mali hiyo kwa uhakika.

Katika kupitia hesabu jumuifu nilibaini kuongezeka kwa thamani ya miti katika mashamba ya misitu kutoka Sh. 98,855,096,000 mwishoni mwa mwaka 2018/19 hadi Sh. 127,699,077,000 kufikia tarehe 30 Juni 2020 ikiwa ni hekta milioni 33.5 za misitu ya kupandwa na ya asili ikijumuisha hekta 308,442 za mashamba makubwa ya misitu ya kupandwa.

Mapitio yangu zaidi katika sampuli ya taarifa za kifedha za taasisi mojamoja yalibaini kuwa, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFSA) ina hekta 117,267 za mashamba makubwa ya misitu ya kupandwa yanayokidhi vigezo vya kutambuliwa; hata hivyo, hayakutambuliwa kwenye hesabu Jumuifu.

**Ninapendekeza Serikali ianzishe utaratibu wa kutambua misitu ya kupandwa na kuihasibu kwenye hesabu jumuifu kwa kufuata matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya uandaaji Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSAS) ili kuonesha thamani halisi ya mali zinazomilikiwa na serikali.**

### 5.5.6 Kutooneshwa kwa Taarifa ya Ufafanuzi wa Marekebisho au Usuluhishi wa Tarakimu Zilizoripotiwa katika Taarifa ya Mtiririko wa Fedha.

Aya Na. 28 & 29 ya viwango vya kimataifa vya uaandaji wa hesabu katika sekta ya umma (IPSAS 2) na Aya Na. 3.1.6 ya waraka Na.6 wa Mhasibu Mkuu wa hesabu za serikali wa maandalizi ya uandaaji na ufungaji waa taarifa za fedha za mwaka 2019/20 unazitaka taasisi za serikali zinazowasilisha mtiririko wa fedha unaotokana na shughuli za uendeshaji kwa kutumia njia ya moja kwa moja (direct method) kuonesha maelezo yanayoelezea marekebisho ya taarifa za kifedha na usuluhishi wa ziada / nakisi kutoka kwa shughuli za kawaida na mtiririko wa fedha kutoka kwa shughuli za uendeshaji. Usuluhishi huu unaweza kutolewa kama sehemu ya

taarifa ya mtiririko wa fedha au kwenye malelezo ya ziada ya taarifa za fedha.

Mapitio yangu ya taarifa za Mtiririko na za utendaji wa Fedha katika hesabu jumuifu nilibaini mapokeo ya Sh 8,452,485,087,000 na malipo ya Sh 9,445,308,089,000 katika shughuli za uendeshaji ambazo hayakusuluishwa za.(**Kiambatisho Na. X**). Nilibaini zaidi, mapokeo na malipo haya hayakutolewa taarifa ya ufafanuzi wa marekebisho au usuluhishi uliofanywa kufikia tarakimu zilizoripotiwa. Hivyo, sikuweza kubaini endapo mabadiliko ya mapato yaliyoripotiwa na malipo yaliyotolewa kutokana kutokuwepo kwa taarifa ya ufafanuzi ya marekebisho / usuluhishi kati ya mapokeo ya fedha na malipo yaliyoripotiwa katika taarifa ya mtiririko wa fedha na mabadiliko katika taarifa ya mizania ya fedha (statement of financial position) ( madai na madeni).

**Ninapendekeza Serikali kuimarisha ubora wa utaratibu wa mapitio ya hesabu jumuifu ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazojumuishwa zinaripotiwa kwa usahihi na kwa mujibu wa matakwa wa viwango vya kimataifa vya uaandaji wa hesabu katika sekta ya umma na Waraka Na. 6 wa Mhasibu wa serikalMkuu wa mwaka 2019/20.**

### 5.5.7 Kutokuwepo kwa Usuluhishi wa Mali za Kudumu Zilizonunuliwa na Kuripotiwa kwenye Mtiririko wa Fedha za Shughuli za Uwekezaji Dhidi ya Ongezeko la Kifedha Sh. Bilioni 635.9

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu yamebaini kutofautiana kwa Sh. 635,931,015,000 kati ya ununuzi wa mali za kudumu katika taarifa za Mtiririko wa Fedha za shughuli za uwekezaji ikilinganishwa na ongezeko la kifedha katika jedwali la mwenendo wa mali kama inavoonekana kwenye **Jedwali Na. 33**. Hatahivyo, hakukuwa na usuluhishi katika Hesabu Jumuifu kinyume na matakwa Aya 25 (a) ya Viwango vya Kimataifa vya uandaaji Hesabu katika Sekta ya Umma Na.2 (IPSAS 2).

**Jedwali Na. 33: Kutokuwepo kwa Usuluhishi wa Mali za Kudumu Zilizonunuliwa na Kuripotiwa kwenye Mtiririko wa Fedha Chini ya Shughuli za Uwekezaji Dhidi ya Ongezeko la Kifedha Sh.Bilioni 635.9**

| shughuli za uwekezaji | Inavyoonesha kwenye Mtiririko wa Fedha (Sh 000') | Ongezeko la Kifedha (Sh. 000') | Tofauti (SH.000') | Tofauti iliyoelezewa (Sh. 000') | Tofauti isiyoelezewa (Sh. 000') |
|---|---|---|---|---|---|
| Kumiliki hisa katika tanzu | 56,085,321 | 0 | 56,085,321 | 0 | 56,085,321 |
| kumiliki hisa katika Mashirika ya pamoja au ubia | 30,695,458 | 0 | 30,695,458 | 0 | 30,695,458 |
| Kumiliki mali za kudumu | 6,757,205,918 | 5,940,114,380 | 817,091,538 | 338,258,940 | 478,832,598 |
| kumiliki mali za uwekezaji | 74,056,143 | 50,543,270 | 23,512,873 | 0 | 23,512,873 |
| Kumiliki Mali za dhahania (Intangible Assets) | 78,861,153 | 78,861,153 | 0 | 0 | 0 |
| Kumiliki uwekezaji wa mtaji | 46,170,628 | 0 | 46,170,628 | 0 | 46,170,628 |
| Kumiliki mali za kibayolojia | 807,419 | 173,282 | 634,137 | 0 | 634,137 |
| **Jumla** | **7,043,882,040** | **6,069,692,085** | **974,189,955** | **338,258,940** | **635,931,015015** |

***Chanzo: Hesabu Jumuifu 2019/20***

**Ninapendekeza Serikali kuimarisha ubora wa utaratibu wa mapitio ya hesabu jumuifu ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazojumuishwa zinaripotiwa kwa usahihi na kwa mujibu wa matakwa wa viwango vya kimataifa vya uaandaji wa hesabu katika sekta ya umma na Waraka Na. 6 wa Mhasibu wa serikalMkuu wa mwaka 2019/20.**

## SURA YA SITA

## TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI NA UTAWALA BORA

### 6.1 Utangulizi

Udhibiti wa ndani ni mchakato muhimu uliowekwa na usimamizi wa taasisi kulinda mali, kukuza uwajibikaji, kuongeza ufanisi na kuzuia ubadhirifu.

Udhibiti wa mifumo ya ndani unajumuisha mambo matano yanayohusiana ili kuhakikisha mafanikio katika ufanisi wa shughuli za taasisi, taarifa za kuaminika za kifedha na uzingatiaji wa sheria na kanuni.

**Kudhibiti Mazingira**

Seti ya viwango, michakato na miundo hujenga msingi wa udhibiti wa ndani kwa taasisi yoyote. Menejimenti inapaswa kuhakikisha kuwa kuna viwango vya juu vya maadili. Pia, inapaswa kuandaa, kujumuisha na kusambaza kanuni za maadili.

**Tathmini ya Vihatarishi**

Kuwapo kwa mchakato endelevu wa kutambua vihatarishi vyote katika kufanikisha malengo ya taasisi hujenga msingi wa kudhibiti vihatarishi. Menejimenti inapaswa kufikiria uwezekano wa kutokea kwa ubadhirifu. Pia, inatakiwa kufanya tathmini kuhusu aina za ubadhilifu pamoja na mambo yanayoweza kusababisha ubadhirifu.

**Kudhibiti Shughuli**

Kuweka sera na taratibu za kuhakikisha kuwa maagizo ya menejimenti juu ya kudhibiti vihatarishi yanafuatwa ili kufikia malengo. Taratibu za mfumo wa udhibiti wa ndani zinaweza kuwa za udhibiti wa kuzuia na kutambua.

**Udhibiti wa Kuzuia**

Udhibiti wa kuzuia unalenga kuzuia makosa au udanganyifu kabla ya kutokea. Lengo ni kutambua makosa au ubadhirifu unaotokea kwa mara ya kwanza. Hii hujumuisha utunzaji madhubuti wa nyaraka,uidhinishaji wa ankara na uhakiki wa gharama , mgawanyo wa majukumu na kuhakikisha kuwa hakuna mtu mmoja ambaye yuko katika nafasi ya kuidhinisha, kurekodi, na kusimamia shughuli za kifedha na mali. Aidha, udhibiti wa kuzuia ni pamoja na kupunguza fursa ya upatikanaji wa mali na fedha za taasisi bila idhini.

**Udhibiti wa Kutambua**

Udhibiti wa kutambua hulenga kugundua tukio au hali isiyotarajiwa baada ya kutokea lakini kabla ya malengo ya mwisho kukamilika. Hii ni pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara wa usimamizi wa shughuli za uhasibu na ripoti pamoja na kupitia na kuangalia kazi, rekodi na usuluhisho. Pia, hufanyika kupitia uchambuzi wa tofauti kwa kulinganisha bajeti na uhalisia, kuhakiki orodha ya vifaa, ukaguzi wa ndani pamoja na kufanya marekebisho iwapo kuna tofauti zimejitokeza.

**Habari na Mawasiliano**

Hujumuisha kutambua, kupata na kutumia taarifa sahihi na zenye ubora kutoka katika vyanzo vyote vya ndani na nje.

**Shughuli za Ufuatiliaji**

Hujumuisha kutathmini ikiwa kila moja ya vifaa vitano vya udhibiti wa ndani vipo na vinafanya kazi.

Kulingana na Kanuni ya 11 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001, Maafisa Masuuli wa wizara na taasisi za serikali wanatakiwa kuanzisha na kudumisha mfumo madhubuti wa udhibiti wa ndani wa fedha na shughuli zote za taasisi.

Kwa hiyo, ukaguzi wa hesabu hupima ufanisi wa mfumo wa uthibiti wa ndani, kutoa taarifa ya mapungufu na kushauri taasisi kuboresha mfumo wa udhibiti wa ndani, kudhibiti utendaji kazi, na kuongeza mazoea ya kutoa taarifa za fedha. Ninatoa ripoti hii ili kuzijulisha wizara na taasisi za serikali kuhusu mapungufu yaliyobainika kwenye mfumo wa uthibiti wa ndani ambayo yanaweza kusababisha vihatarishi vya makosa katika taarifa za fedha.

Nilibaini baadhi ya taasisi ambazo zinahitaji uboreshaji katika maeneo ya mfumo wa udhibiti wa ndani. Maeneo hayo ni; mfumo wa Teknolojia ya habari (TEHAMA) kwenye maeneo yanayosaidia uandaaji wa taarifa za kifedha, udhibiti wa ndani unaohusiana na utoaji wa taarifa za kifedha, kufuata sera za serikali, sheria, na kanuni za uhasibu na kutoa ripoti za kifedha mara kwa mara, Ukaguzi wa Ndani, Kamati za Ukaguzi, michakato ya kudhibiti vihatarishi pamoja na tathmini ya ubadhirifu. Mapungufu haya yalitokea ndani ya Idara, Wakala na Wizara, Sekretarieti za Mkoa, Hospitali za Mkoa za Rufaa (RRH) na Taasisi Nyingine katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20.

## 6.2 Tathmini ya Ubadhirifu

Ubadhirifu ni kitendo chochote cha kukusudia au upungufu ulioundwa kudanganya wengine, na kusababisha mwathirika kupata hasara au mhalifu kupata faida. Kwa ujumla, udanganyifu huhusisha shughuli kama vile wizi, ufisadi, kula njama, utakatishaji fedha, rushwa na ulafi.

Kanuni ya 35 (2) ya Kanuni ya Fedha za Umma (PFR) ya mwaka 2001 inasema kwamba 'kuzuia, kugundua na kuchunguza ubadhirifu ni wajibu wa menejimenti. Hii ni pamoja na utengenezaji wa sera za vihatarishi vya ubadhirifu, mchakato wa usimamizi wa vihatarishi vya ubadhirifu, rejista ya vihatarishi vya ubadhirifu, kufanya ufuatiliaji, Pamoja na kupitia na kuongeza mfumo wa usimamizi wa vihatarishi. Hata hivyo, kufanya kazi za ukaguzi, ni jukumu la kitaalamu la mkaguzi wa ndani kuwa macho kuhusu vihatarishi vya ubadhirifu, na kuijulisha mamlaka inayohusika ndani ya wakati wowote kuhusu mashaka ya kuwapo kwa ubadhirifu.

Katika ukaguzi wangu nilifanya tathmini ya ubadhirifu katika Wizara na taasisi zake, Sekretarieti ya Mikoa, Wakala na Taasisi nyingine mbali mbali za serikali na kubaini mapungufu katika Taasisi 6 ikilinganishwa na Taasisi 4 zilizoripotiwa 2018/19. Hii inaonesha kuwa hakuna maboresho katika mwaka huu. Maelezo ya Taasisi pamoja na mapungufu yameelezwa katika **Jedwali Na. 34**

**Jedwali Na. 34: Tathmini ya Ubadhirifu**

| Na | Fungu | Taasisi | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| ***Wizara*** | | | |
| 1 | 53 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | • Hakuna mipango ya kubaini na kuzuia ubadhilifu iliyoidhinishwa<br>• Kutotekelezwa kwa majiribio ya udhibiti unaohusiana na ubadhilifu kwenye shughuli kuu za mapato, ununuzi, motisha na mamlaka ya usimamizi wa mali. |
| 2 | 62 | Wizara ya Ujenzi,Uchukuzi na Mawasiliano | Hakuna rejista ya ubadhilifu |
| ***Sekretarieti za Mikoa*** | | | |
| 1 | 79 | Morogoro | • Sekretarieti haina mpango wa kuzuia na kubaini ubadhilifu.<br>• Sekretarieti haijaanzisha tathmini ya |

| Na | Fungu | Taasisi | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| | | | vihatarishi juu ya vitendo vya ubadhilifu.<br>• Hakuna mchakato uliowekwa wa kutambua na kujibu vihatarishi na ubadhilifu. |
| 2 | 81 | Mwanza | • Sekretarieti haina mazoea ya kuwasiliana / kushirikisha vihatarishi katika kiwango cha Sekretarieti.<br>• Rejista ya vihashiria haikusahihishwa. |

*Chanzo: Barua ya Mapungufu kwa Menejimenti ya 2019/20*

**Ninapendekeza kwa Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa kuna sera, taratibu na muundo unaowezesha taasisi kutambua, rekodi na kufuatilia vihatarishi vya ubadhirifu. Hii ni pamoja na utaratibu wa kutoa taarifa za ubadhirifu kwa Bunge na mamlaka nyingine za juu.**

## 6.3 Tathmini ya Kuwapo kwa Ubadhirifu katika Taasisi za Serikali iligundua Maswala Yafuatayo;

### 6.3.1 Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) Kushindwa kupata Gari Lililoibiwa aina ya Toyota Land Cruiser Hard Top Lenye Namba ya Usajili STL 6516

Mapitio yalifanyika kwenye jalada la gari la TBA No.DB.302 / 494/15. Uhakiki wa mali ulifanyika tarehe 17 Agosti 2018. Mali hiyo ni gari aina ya Toyota Land cruiser Hard Top lenye Namba ya Usajili STL 6516, namba ya modeli H2J76R-RKMRS, namba ya injini IHZ-00899765, namba ya chasis JTEEB71J707042992, na lenye rangi nyeupe. Gari hilo lilinunuliwa mnamo Agosti 2018 alipewa Meneja wa Wakala wa Majengo Tanzania, Mkoa wa Lindi, kwa ajili ya matumizi ya ofisi. Liliibiwa tarehe 4 Desemba,2019 katika maegesho ya CCM-Mabibo Dar es Salaam. Hii ni kutokana na hati ya upotevu iliyowasilishwa tarehe 13 Desemba 2019 na dereva wa gari hilo.
Katika kipindi cha Ukaguzi, Novemba 2020, nilibaini kuwa hakukuwa na ripoti za maendeleo ya uchunguzi wala taarifa kutoka kwa polisi au menejimenti ya Wakala wa Majengo Tanzania kama kuna hali ya kupatikana tena kwa gari lililoibiwa.

**Ninapendekeza kwamba (a) Afisa Masuuli husika afuatilie udhibiti muhimu ambao unaokosekana ili uimarishwe, (b) Kuhakikisha**

usimamizi mzuri wa mali, pamoja na ufuatiliaji wa karibu kwa polisi na vyombo vingine vya uchunguzi ili kurejesha gari lililopotea na hatua za kisheria. zinachukuliwa kwa watumishi wanaohusika, na (c) Serikali ifanye udhibiti wa mali na usimamizi hasa katika uhakiki wa mali unatakiwa uongezeke na kufanyika mara kwa mara katika mwaka ambapo utafanyika ulinganisho kati ya mali halisi zilizopo dhidi ya zilizorekodiwa ili kupunguza idadi ya upotezaji wa mali.

### 6.3.2 Malipo yenye Shaka Yaliyofanyika kwenye Akaunti ya Masurufu Sh. 261,352,688.34

Nilikagua taarifa za fedha, Benki na nyaraka za uthibitisho wa malipo na kubaini Sh. 261,353,488.34 ziliwekwa kwenye akaunti ya masurufu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika mojawapo ya benki za biashara kwa vipindi tofauti. Hata hivyo, nilibaini kuwa menejimenti ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji haikutambua vyanzo vya fedha hizo na shughuli zilizopaswa kutekelezwa. Aidha, hakukuwa na mawasiliano yoyote yaliyofanywa na benki kuhusuiana na mapokezi ya fedha hizo.

Ukaguzi uliendelea kubaini kuwa, kiasi hicho cha fedha Sh.261,352,688.34 kilichukuliwa na mtunza fedha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutoka katika akaunti hiyo kwa kutumia nyaraka za fedha za kughushi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 35** hapa chini:

**Jedwali Na. 35: Rekodi za Kiasi kilichowekwa na kutolewa na Mtunza Fedha**

| Na. | Tarehe | Kiasi Kilichowekwa Sh. | Tarehe | Kiasi Kilichotolewa Sh. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 04 Septemba, 2019 | 78,885,720.00 | 04 Septemba, 2019 | 78,885,720.00 |
| 2. | 04 Septemba, 2019 | 44,261,516.34 | 04 Septemba, 2019 | 44,261,516.34 |
| 3. | 02 Oktoba, 2019 | 52,636,222.00 | 02 Oktoba, 2019 | 52,636,222.00 |
| 4. | 8 Novemba, 2019 | 25,143,400.00 | 4 Novemba, 2019 | 25,143,400.00 |
| 5. | 01 Novemba, 2019 | 30,000,000.00 | 6 Novemba, 2019 | 48,000,000.00 |
| | 04 Novemba, 2019 | 18,000,000.00 | | |
| 6. | 6 Novemba, | 2,754,830.00 | 7 Novemba, 2019 | |

| Na. | Tarehe | Kiasi Kilichowekwa Sh. | Tarehe | Kiasi Kilichotolewa Sh. |
|---|---|---|---|---|
| | 2019 | | | 12,425,830.00 |
| | 6 Novemba, 2019 | 200,000.00 | | |
| | 6 Novemba, 2019 | 8,500,000.00 | | |
| | 6 Novemba, 2019 | 1,000,000.00 | | |
| | **Jumla** | **261,381,688.34** | | **261,352,688.34** |

Katika kuangalia zaidi juu ya udhibiti wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nilibaini kuwa, usuluhisho wa benki wa taarifa za fedha kwenye akaunti ya masurufu haukufanywa kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai 2019 hadi sasa. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 162 (1) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 ambayo inahitaji taarifa za fedha za benki zifanyiwe usuluhisho angalau kila mwezi.

Hii inaashiria kuwapo kwa udhibiti dhaifu wa ndani kwenye usimamizi wa fedha katika akaunti za benki za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Ubadhirifu huo ulileta mianya kwa mtunza fedha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufanya ubadhirifu na kutoa fedha kwa kutumia nyaraka za kughushi. Kwa hivyo, Sh. 261,352,688.34 zimetumiwa vibaya bila ya benki ama Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutambua.

**Ninapendekeza kuwa;**

**(a) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liimarishe udhibiti wa ndani kwenye akaunti ya masurufu ili kuzuia kujirudia kwa matukio kama hayo; na**
**(b) Serikali kupitia vyombo vyake vya uchunguzi kuchunguza zaidi suala hilo na kuchukua hatua stahiki.**

### 6.4 Utawala Bora

Utawala bora ni Jumla ya seti ya mifumo, kanuni na miongozo inayoiongoza taasisi. Hutoa mwongozo wa jinsi taasisi inavyopaswa kuelekezwa au kudhibitiwa ili iweze kutimiza malengo yake kwa njia ambayo inaongeza thamani kwa taasisi na faida kwa wadau wote kwa muda mrefu.

Tafakari ya utawala bora na kanuni zake zimebuniwa ili kusaidia kuhakikisha kuwa, uhusiano kati ya viongozi na wanaoongozwa unakuwa vizuri na kupunguza vihatarishi vya matumizi mabaya ya nafasi au madaraka. Katika kutathmini kuwapo kwa mapungufu ya utawala bora katika taasisi za Serikali nilibaini makosa yafuatayo:

### 6.4.1 Mamlaka ya Mapato Tanzania Kutokufuata Utaratibu katika Kushikilia Fedha za Wakala wa Majengo Tanzania Sh. 3,888,982,830.50 kwa ajili ya Kulipa Deni la Kodi Sh. 6,986,794,187

Kanuni Na. 21 (1) ya Usimamizi wa Kodi (Kanuni za Jumla) ya mwaka 2016 inasema kwamba, mtu aliyekaguliwa kati ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya huduma anatakiwa kujibu kwa kina hoja zilizotolewa kuhusu matokeo ya ukaguzi. Kifungu kidogo cha kanuni ya 21(4) (a)-(b) kinasema kwamba, baada ya kupokea majibu chini ya kanuni hii, Kamishna Jenerali: (a) atajadili matokeo na majibu kwa mtu aliyekaguliwa na (b) baada ya kumaliza majadiliano, atoe " Ripoti ya mwisho ya Ukaguzi.

Uhakiki wa kina niliofanya kwenye nyaraka za madeni ya kodi ulibaini kuwa, tarehe 3 Aprili 2020, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilitoa hati ya madai yenye kumbukumbu Na: TRA / ILALA / ECM / 101-024-490 ya tarehe 03/4/2020 kwa Wakala wa Majengo Tanzania inayodai kodi jumla ya Sh. 6,986,794,187.00. Kodi hiyo iligawanyika kama ifuatavyo:- Kodi ya Maendeleo ya ufundi stadi (SDL), kodi ya mapato itokanayo na ajira (PAYE) na kodi ya zuio kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2014/15.

Mnamo tarehe 21 Mei 2020, jumla ya Sh. 3,888,982,830.50 zilichukuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoka katika akaunti za Benki ya TBA [CRDB na TIB] kama sehemu ya malipo ya deni lililobaki la ushuru la Sh. 6,986,794,187.00. Kutokutoa Ripoti ya mwisho ni kinyume na matakwa ya kanuni 21 b ya Usimamizi wa kodi (Kanuni za Jumla) ya mwaka 2016.
Kuchukuliwa kwa fedha za Wakala wa Majengo (TBA) (jumla ya Sh. 3,888,982,830.50) bila uhalali, usahihi, na ukamilifu wa tathmini ya deni la kodi kunaashiria kukwamisha mipango ya Serikali.

**Ninapendekeza kuwa Afisa Masuuli wa Wakala wa Majengo afanye ufuatiliaji na kuomba ripoti ya Mwisho ya Ukaguzi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania na kukubaliana juu ya uhalali, usahihi na ukamilifu wa deni la kodi iliyotathminiwa. Hata hivyo, Wakala wa Majengo Tanzania**

**alishaomba ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuingilia kati na kesi ilikuwa tayari imeshafunguliwa matokeo bado yanasubiriwa. Kwa hiyo, ufuatiliaji unahitajika ili kumaliza madeni ya kodi.**

### 6.4.2 Kutokuwapo kwa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Magonjwa ya Miti

Kifungu cha 3 (a) ya Sheria ya udhibiti wa mimea ya mwaka 1997 kinasema kwamba Waziri anaweza kutunga miongozo ya kuzuia na kudhibiti mashambulizi na kuenea kwa viumbe au magonjwa hatarishi nchini Tanzania iwapo kuna tukio la kutia shaka la viumbe vyovyote vyenye madhara, kilimo chochote au kuwapo kwa aina za mimea, au ukweli wowote unaofaa kuhusu tukio au udhibiti wa vijidudu hatari, au utumiaji wa vifaa maalum vya udhibiti wa mmea, au michakato ya udhibiti wa mimea.

Usimamizi wa magonjwa ya mimea unakusudia kupunguza uharibifu wa uchumi unaosababishwa na magonjwa ya mimea. Masuala ya kijamii na mazingira yanapaswa kudhibitiwa. Kinyume na malengo yaliyokusudiwa, nilibaini kuwa usimamizi na udhibiti wa magonjwa ya mimea haujaainishwa katika sera ya misitu, sheria ya misitu na kanuni za misitu.

Hii inaleta hatari kwamba hasara kubwa inaweza kutokea mara tu magonjwa yasiyotarajiwa yatakapoibuka; kwamba usimamizi na udhibiti wa magonjwa ya mimea lazima uelezwe katika sheria na udhibiti wa misitu, hususani kwa kila Mpango wa Usimamizi wa Misitu wa kila mwaka.Pia ukosefu wa sheria sahihi za misitu katika kudhibiti maswala ya aina hii inaweza kusababisha upotezaji mkubwa wa rasilimali za misitu na kusababisha upotevu wa rasilimali fedha na miti.

**Napendekeza Wakala anayehusika kurekebisha sheria na kanuni za misitu na kuingiza masuala ya kugundua, kudhibiti na kuzuia magonjwa ya misitu kwa kila mwaka katika Usimamizi wa Misitu. Pia, Wakala afanye kazi kwa karibu na kitengo cha afya chini ya Wizara ya Kilimo ili kuhakikisha kuwa kuna maendeleo endelevu ya mimea na utunzaji wa mazingira.**

### 6.4.3 Kushindwa Kuwatangaza Wataalamu kwenye Gazeti la Serikali

Gazeti linatoa taarifa ya kudumu, taarifa rasmi za umma na muhimu za kisheria na zisizo za kisheria ambazo zinaweza kutumiwa kusaidia michakato ya kisheria na mingineyo; na kuwa, hii ni njia ya kutangaza matangazo ya umma.

Taarifa rasmi kwa umma inaweza kuwekwa na watu au Taasisi zilizosajiliwa na kuthibitishwa kufanya kazi hizo rasmi, ambazo zina mamlaka ya kuandaa taarifa rasmi za ukweli.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, Baraza la Baraza la Wataalamu wa Mionzi (MRIPC) na Baraza la Wauguzi na Wakunga wa Tanzania wote hawakutangaza Wataalamu wao kwenye Gazeti la Serikali, kinyume na kanuni za ndani kama ilivyoonekana kwenye **Jedwali Na. 36** hapa chini

**Jedwali Na. 36: Kushindwa Kuwatangaza Wataalamu kwenye Gazeti la Serikali**

| Na. | Taasisi | Mapungufu |
|---|---|---|
| 1 | Baraza la Wataalamu wa Mionzi (MRIPC) | Katika mwaka 2018/19 na 2019/20, idadi ya wataalamu waliosajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Mionzi (MRIPC) ilikuwa 141 na 64 mtawalia lakini hakuna matangazo yaliyofanywa na Baraza la Wataalamu wa Mionzi (MRIPC) kulingana na mahitaji ya kifungu Na.38 (1) ya Sheria ya Baraza la Wataalamu wa Mionzi ya 2007. |
| 2 | Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania | Wauguzi na wakunga waliosajiliwa hawakutangazwa katika Gazeti la Serikali kama inavyotakiwa na kanuni Na. 11 ya Uuguzi na Ukunga (Usajili na Kanuni za leseni, ya mwaka 2010) |

*Chanzo: Barua ya Mapungufu kwa Menejimenti ya 2019/20*

Hali hii inamaanisha juhudi duni zinazofanywa na Baraza kutangaza taaluma zilizosajiliwa.

Kuna uwezekano wa kile kinachoitwa wataalamu bandia kuwapo bila kutambuliwa na menejimenti na Umma. Kutotangaza sifa za wataalam kunaweza kupunguza huduma zao, hivyo kupoteza mapato ya Serikali kutokana na ada kutoka kwa watoa huduma.

**Ninapendekeza Mabaraza kuhakikisha kuwa wanatangaza na kuchapisha majina ya Wataalamu katika Gazeti la Serikali kulingana na Sheria.**

### 6.4.4 Ukosefu wa Miongozo ya Uandaaji wa Taarifa za Kihasibu

Mwongozo wa uhasibu ni hati inayosimamia mifumo ya kihasibu, sera, taratibu, viwango na mwongozo inayofuatwa na kitengo cha uhasibu. Zaidi, muongozo unaweza kuwa katika mfumo wa fomu, chati ya akaunti na maelezo ya kazi. Mwongozo wa uhasibu ni zana muhimu ya kufanya kazi kwa Afisa Masuuli. Husaidia kusimamia kazi ya uhasibu, pamoja na kuwezesha kufuatilia utumiaji wa sera za uhasibu katika taasisi yote.

Katika kupitia nyaraka za taasisi, nilibaini kuwa taasisi tano (5), wizara mbili (2) na taasisi nyingine tatu (3) hazikuandaa miongozo ya kihasibu kwa ajili ya kazi zao ikilinganishwa na Taasisi saba (7) nilizoziripoti mwaka 2018/19, kuna punguzo la taasisi mbili (2), sawa na asilimia 28.57. Hii inaonesha kuwa kuna maboresho katika mwaka huu. Maelezo zaidi yanatolewa katika **Jedwali Na. 37**

**Jedwali Na. 37: Ukosefu wa Miongozo ya uandaaji wa Taarifa za Fedha**

| Na. | Fungu | Taasisi | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| ***Wizara*** | | | |
| 1 | 43 | Wizara ya Kilimo | Ukosefu wa kanuni za kifedha zinazohusiana na Akaunti ya Mfuko wa kusaidiana. |
| 2 | 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | Ukosefu wa Mwongozo wa Kusimamia Madai ya Fidia. |
| *Taasisi Nyingine* | | | |
| 1 | Taasisi ya Rasilimali za Madini (MRI) | | Kutokuwapo kwa Miongozo ya Fedha na Mwongozo ya Uhasibu |
| 2 | Kituo cha Gemolojia Tanzania (TGC) | | Hakuna sera/miongozo iliyoidhinishwa ya kuongoza michakato ya usimamizi |
| 3 | Taasisi ya Mafunzo ya Misitu (FITI) | | Kutokuwapo kwa mwongozo wa uzalishaji uliopitiwa na kuidhinishwa kama utaratibu wa udhibiti wa ndani wa shughuli za kila siku |

*Chanzo:Barua ya Mapungufu kwa Menejimenti 2019/20*

Ukosefu wa Mwongozo wa Uhasibu unaweza kusababisha mchakato wa kifedha kuidhinishwa na kupitishwa bila idhini ya menejimenti.

**Napendekeza Maafisa Masuuli kuharakisha mchakato wa kuendeleza Mwongozo wa kihasibu ili kuleta usimamizi madhubuti juu ya fedha za umma.**

### 6.4.5 Mapungufu katika Uendeshaji wa Akaunti ya Masurufu Sh.6,804,964,104.33

Nimekagua shughuli za akaunti ya masurufu kwa Taasisi tofauti na kubaini kuwa Sh. 6,804,964,104.33 zimelipwa kupitia akaunti ya benki ya masurufu kwa ajili ya kazi mbalimbali katika taasisi tano ndani ya mwaka. Katika kukagua nilibaini kuwa taasisi zilikuwa hazina daftari la fedha lililotunzwa wala taarifa za usuluhisho wa kibenki wa kila mwezi iliyoandaliwa. Hii ni kinyume na kanuni ya 162 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 ambayo inahitaji bakaa ya kila akaunti ya benki kama inavyooneshwa katika taarifa ya fedha za benki isuluhishwe na taarifa za usuluhisho za kibenki na bakaa za kitabu cha fedha angalau kila mwezi. Taarifa za usuluhisho za kibenki zitunzwe au kurekodiwa katika kitabu cha fedha.Orodha ya taasisi zenye mapungufu zimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 38** hapa chini.

Sababu za kutotunza daftari la fedha la akaunti ya masurufu na maandalizi ya taarifa ya usuluhisho wa kibenki wa kila mwezi hazikufahamika. Hali hii huleta ugumu katika kufahamu ukweli na usahihi wa miamala ya fedha iliyofanyika na bakaa zilizoripotiwa.

**Jedwali Na. 38: Mapungufu Yaliyojitokeza wakati wa Kuiendesha Akaunti ya Benki ya Masufuru**

| NA. | FUNGU | Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 29 | Wizara ya Mambo ya Ndani -Idara ya Magereza | Akaunti namba ya Masurufu 0150211137700 ambayo ipo benki ya CRDB. | 409,344,179.00 |
| 2 | 44 | Wizara ya Viwanda na Biashara | Benki akaunti namba. 50510032036 ya NMB na akaunti namba 0150211156000 ya CRDB Benki. | 232,590,000.00 |
| 3 | 46 | Wizara ya Elimu Sayansi na Tecknologia | Akaunti ya Masurufu namba 0150211138700 iliyopo CRDB Azikiwe Premier | 3,015,357,893 |
| 4 | 56 | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | Akaunti ya Masurufu ya NMB | 2,101,469,012.37 |
| 5 | 100 | Wizara ya Madini | Uchukuwaji wa fedha kutoka katika akaunti ya masurufu jumla ya Sh. 1,046,203,019.96 ilitumika kulipa moja kwa moja | 1,046,203,019.96 |

| NA. | FUNGU | Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| | | | wazabuni na makandarasi, kinyume na sheria na kanuni zinazohitajika | |
| **Jumla** | | | | **6,804,964,104.33** |

*Chanzo: Barua ya Mapungufu kwa Menejiment 2019/20*

Nina toa angalizo katika mapungufu yaliyojitokeza kwenye udhibiti wa ndani kwa taasisi, ambayo yanaweza kusababisha makosa, ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha zinazowekwa bila menejimenti kutambua.

**Ninapendekeza kwamba Maafisa Masuuli kuimarisha udhibiti wa ndani na kuandaa vitabu vya fedha na pia usuluhisho wa taarifa za fedha wa kila mwezi za benki ili kulinda masurufu ya fedha zinazohamishiwa kwenye Akaunti.**

### 6.4.6 Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani

Ukaguzi wa ndani ni kitengo kinachoanzishwa ndani ya taasisi ili kutathmini udhibiti wa ndani pamoja na utawala bora. Kitengo hiki hutoa tathmini ya uzingatiaji wa sheria na kanuni na kubaini mapungufu, kisha hutoa mapendekezo ya kuboresha mifumo ya udhibiti ili kufikia utoaji wa huduma wenye ufanisi.

Kanuni ya 28(1) ya kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inamtaka kila Afisa Masuuli kuanzisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kutoa uhakika wa ukamilifu na ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani ya taasisi kama inafanya kazi ipasavyo.

Tathmini yangu kuhusu ukaguzi wa ndani kwenye sampuli ya Wizara, Idara na Taasisi pamoja na Sekretarieti za Mikoa ilibaini kuwa, Taasisi ishirini na nane (28), zikiwamo Wizara na Idara tano (5), Sekretarieti za Mikoa nne (4), Taasisi nyingine kumi na tatu (13), na Hospital za Rufaa za Mikoa sita (6) zilionekana na mapungufu amabayo yalisababisha kutotimiza majukumu ya kitengo yafuatayo: kutokuanzishwa kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani, kutengewa bajeti ndogo, vitendea kazi hafifu na mipango ya ukaguzi wa ndani kutoidhinishwa na Kamati ya Ukaguzi, upungufu wa wafanyakazi pamoja na kutopata mafunzo kwa wafanyakazi. Orodha ya Taasisi zenye mapungufu kwenye kitengo cha Ukaguzi wa Ndani imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 39** na **Kiambatisho Na. XI.**

**Jedwali Na. 39: Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Wizara | Idadi ya Sekretarieti za Miko | Idadi ya Taasisi Nyingine | Idadi ya Wakala za serikali | Idadi ya Hospital za Rufaa | Jumla ya Taasisi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **2019/20** | 5 | 4 | 13 | 0 | 6 | 28 |
| **2018/19** | 5 | 11 | 6 | 2 | 0 | 24 |
| **2017/18** | 10 | 15 | 5 | 3 | 0 | 33 |

*Chanzo: Barua za mapungufu kwa menejiment 2019/20*

Jedwali Na. 37 hapo juu linaonesha ongezeko kwa idadi ya taasisi zenye mapungufu katika kutekeleza majukumu ya ukaguzi wa ndani; ambapo taasisi 24 ziliripotiwa mwaka 2018/19 na taasisi 28 ziliripotiwa mwaka 2019/20. Hivyo, kuna ongezeko la taasisi 4, sawa na 17%. Hii inaonesha kuwa hakuna maboresho katika eneo hili.

Kwa kukosekana ufanisi wa ukaguzi wa ndani, Taasisi hushindwa kubaini vihatarishi vya ubadhirifu na kutozingatiwa sheria na kanuni hakuwezi kugunduliwa na kurekebishwa kwa wakati unaofaa. Mbali na hayo, taasisi zinanyimwa fursa ya uhakikisho wa malengo na huduma ya ushauri ili kuongeza na kuboresha thamani.

**Ningependa kutoa ushauri kwa Maafisa Masuuli kuhakikisha Vitengo vya Ukaguzi wa ndani vimepatiwa rasilimali za kutosha na vinafanya kazi na kutekeleza majukumu yao, ikiwa ni pamoja na kutambua upungufu wa udhibiti wa ndani na kupendekeza hatua za kurekebisha kwa ufanisi.**

### 6.4.7 Tathmini kwenye Utendaji wa Kamati za Ukaguzi

Kamati za ukaguzi zinachukua jukumu muhimu katika kusaidia Taasisi kutekeleza majukumu yake ya usimamizi katika maeneo kama vile kupitia ripoti ya kifedha za Taasisi, mifumo ya udhibiti wa ndani, mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na kazi za ukaguzi wa ndani na nje.

Kanuni ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inahitaji kila Wizara au Mikoa kuwa na Kamati ya Ukaguzi.

Katika tathmini ya utendaji wa Kamati ya Ukaguzi, nilibaini kuwa Kamati ya Ukaguzi haikuandaa ripoti ya kila mwaka juu ya kazi zake. Kamati

haijawahi kukutana na wakaguzi wa nje angalau mara moja bila ya mtendaji na wajumbe kutoka katika taasisi iliyopo ili kuhakikisha kuwa hakuna suala ambalo halijatatuliwa. Pia, kulikuwa na ukosefu wa utaratibu wa kuziwajibisha Kamati ya Ukaguzi inayohusika inaposhindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Pamoja na kushindwa kufanya tathmini ya maendeleo ya Kamati ya Ukaguzi ambayo ni kinyume na sheria.

Tathmini hii ya utendaji wa Kamati za Ukaguzi ilifanyika katika sampuli za Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Wakala. Nilibaini kuwa, taasisi 24 ambazo ni pamoja na Wizara nne, Sekretarieti za Mikoa tisa, Wakala nne, Hospitali za Rufaa sita na Taasisi zingine tatu zilipatikana na maeneo kadhaa yenye mapungufu ambayo yanahitaji zaidi uimarishaji. Maeneo yenye mapungufu yameonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 40** na **Kiambatisho Na. XII**

**Jedwali Na. 40: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Wizara | Idadi ya Sekrestarieti | Idadi ya Wakala | Idadi ya Taasisi Nyingine | Idadi ya Hospitali za Rufaa | Jumla ya Taassisi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 4 | 7 | 4 | 3 | 6 | 24 |
| 2018/2019 | 11 | 9 | 3 | 8 | 0 | 31 |
| 2017/2018 | 12 | 11 | 3 | 4 | 0 | 30 |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti 2019/20*

Kwenye jedwali Na 38 hapo juu inaonesha kuwa, kuna kupungua kwa idadi ya Taasisi ambazo zina mapungufu makubwa katika Kamati ya ukaguzi. Nazo ni Wizara, Wakala na Taasisi nyingine 24 zilizoripotiwa mwaka huu, ikilinganishwa na Taasisi 31 nilizoziripoti mwaka jana. Hivyo, kuna upungufu wa taasisi 7, sawa na asilimia 29%. Hii inaonesha kuwa kuna maboresho katika mwaka huu. Maelezo ya kina ya hali ya utekelezaji ni kama inavyoonesha kwenye **Kiambatisho Na. XII**

**Kielelezo Na. 12** hapa chini kinaonesha mwenendo wa mapungufu katika utendaji wa Kamati za Ukaguzi kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2017/18, 2018/19 na 2019/20.

**Kielelezo Na. 12: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi**




Kutokuwapo kwa ufanisi wa Kamati ya Ukaguzi katika Taasisi kunaweza kupunguza ufanisi katika utendaji kwa jumla, na udhibiti wa utawala bora ndani ya Taasisi. Ni vigumu kuelewa kama Kamati za Ukaguzi na wanachama wake hufanya kazi zake kwa usahihi. Hii ni kutokana na kukosekana kwa njia ya kupima utendaji wao.

**Ninapendekeza Maafisa Masuuli waunde kamati madhubuti za Ukaguzi zinazoweza kutekeleza wajibu na madaraka kulingana na kanuni za fedha za umma 2001.**

### 6.4.8 Tathmini ya Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi

Usimamizi wa vihatarishi ni mchakato wa kutambua, kutathmini, kusimamia na kudhibiti matukio yanayowezekana ili kutoa hakikisho linalofaa kuhusu kufanikiwa kwa malengo ya taasisi.

Katika mwaka wa ukaguzi 2019/20, nilifanya tathmini ya michakato ya Usimamizi wa vihatarishi, muundo wake wote na jinsi unavyofanya kazi vizuri, usimamizi wa vihatarishi vikuu, pamoja na ufanisi wa udhibiti na majibu mengine ya vihatarishi. Tathmini ya Usimamizi wa vihatarishi kwenye sampuli za Wizara, Mikoa, Wakala na Taasisi nyingine nilibaini kuwa taasisi tisa (9) zilikuwa na mapungufu kwenye usimamizi wa vihatarishi. Nazo ni: Wizara moja (1), Taasisi Nyingine tatu (3), Wakala wa Serikali nne (4) na Hospital za Rufaa moja (1). Taasisi hizi zina mapungufu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na Rejista ya vihatarishi, kutokuwa na sera ya kudhibiti vihatarishi, Pamoja na kuwa na Rejista zisizoenda na wakati. Maelezo ya Taasisi pamoja na mapungufu ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 41** na **Kiambatisho Na. XIII.**

**Jedwali Na. 41: Tathmini katika Usimamizi wa Vihatarishi**

| Mwaka | Idadi ya Wizara | Idadi ya Sekretarieti za mikoa | Idadi ya Wakala wa Serikali | Idadi ya Taasisi nyingine | Idadi ya Hospitali za Rufaa | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019/20 | 1 | 0 | 4 | 3 | 1 | 9 |
| 2018/19 | 6 | 4 | 3 | 2 | 0 | 15 |
| 2017/18 | 2 | 3 | 2 | 1 | 0 | 8 |

*Chanzo: Barua za mapungufu wa menejimenti 2019/20*

Idadi ya Taasisi zenye mapungufu zimepungua; ambapo zimegundulika tisa (9) kwa mwaka huu ikilinganishwa na kumi na tano (15) za mwaka uliopita. Hivyo, zimepungua taasisi sita (6) ambazo ni sawa na asilimia 40. Hii inaonesha kuwa kuna maboresho katika mwaka huu.

**Kielelezo Na. 13** hapo chini pia kinaonesha tofauti ya miaka mitatu ya fedha kati ya 2017/18; 2018/19 na 2019/20 zenye mapungufu katika tathmini ya usimamizi wa vihatarishi:

**Kielelezo Na. 13: Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi**




*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti ya 2019/20*

Kutokuwapo kwa sera na utaratibu wa usimamizi wa vihatarishi na rejista hufanya malengo ya taasisi kuwa kwenye hatari kubwa, kwani si rahisi kuyashinda majanga yanapotokea ghafla. Vilevile, inakuwa ngumu kutoa

huduma bora kwa wadau na umma wote, punde majanga yanapotokea ghafla

**Ili kuhakikisha huduma bora kwa umma na utokeaji mdogo wa majanga yasiyotarajiwa Afisa Masuuli wanashauriwa kuimarisha michakato ya kudhibiti vihatarishi kwa kuhakikisha kuwa, vihatarishi vinatambuliwa, kutathminiwa, kusimamiwa na kudhibitiwa. Aidha usimamizi wa vihatarishi unapaswa kuwekwa katika shughuli za kila siku za taasisi na kufuatiliwa kwa kutoa ripoti za kawaida ambazo zitatumika kutengeneza upya rejista ya vihatarishi**

## 6.5 Kupitia Mifumo ya Mazingira ya TEHAMA

Udhibiti wa TEHAMA ni utaratibu au sera ambayo hutoa uhakikisho mzuri kwamba teknolojia ya habari (IT) inayotumiwa na Taasisi inafanya kazi kama ilivyokusudiwa, takwimu hizo ni za kuaminika; na kwamba, Taasisi inatii sheria na kanuni zinazotumika.Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA unalenga kufanya tathmini katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kuangalia udhibiti wa jumla ili kuona kama sera na taratibu zilizopo katika Serikali kutoa huduma za TEHAMA zinazosaidia Serikali.

Katika kutathmini mifumo ya TEHAMA na udhibiti wa mazingira katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Taasisi nyingine nilibaini kuwa taasisi zina mapungufu kama vile: hakuna sera ya TEHAMA, hakuna mpango mkakati, hakuna mwendelezo wa kibiashara, Kamati ya TEHAMA haijaundwa na kutokuwapo kwa mpango wa kuzuia majanga.

Matokeo ya ukaguzi yalionesha kwamba, katika sampuli ya taasisi 23 zilizopatikana na mapungufu ya TEHAMA, ni wizara tano, Sekretarieti ya Mikoa mbili, Wakala wa serikali tano, Taasisi Nyingine nane, Hospitali za Rufaa mbili, pamoja na Mfuko mmoja zilibainika kuwa na mapungufu katika TEHAMA. Baadhi ya mapungufu hayo ni kutokuandaa mpango na sera wa teknolojia ya habari na vifaa vya kuzuia majanga kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 42** hapo chini na **Kiambatisho Na. XIV**.

**Jedwali Na. 42: Kulinganisha Tathmini ya mazingira ya Habari na Teknolojia ya Mawasiliano (TEHAMA)**

| Mwaka wa Fedha | Idadi | Idadi | Idadi | Idadi | Idadi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wizara | Sekretarieti | Wakala | Taasisi Nyingine | Balozi | Taasisi |
| **2019/20** | 5 | 2 | 5 | 8 | 0 | 23 |
| **2018/19** | 4 | 8 | 3 | 2 | 1 | 18 |
| **2017/18** | 10 | 11 | 8 | 6 | 5 | 40 |

Jedwali hapo juu linaonesha kuwa kuna ongezeko la idadi ya Taasisi zenye mapungufu ya TEHAMA. Jumla ya taasisi zenye mapungufu katika mazingira ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika mwaka huu ni 23, ikilinganishwa na kumi na nane (18) za mwaka uliopita. Hii inaonesha ongezeko la Taasisi tano, (27.77%). Hii inaonesha kuwa hakuna maboresho katika mwaka huu.

Aidha, **Kielelezo Na. 14** hapo chini inaonesha ulinganisho wa tofauti ya miaka mitatu ya fedha kati ya 2017/18, 2018/19 na 2019/20 zenye mapungufu katika TEHAMA.

**Kielelezo Na. 14: Tathmini ya Mwenendo wa Mifumo ya TEHAMA**



Kielelezo hapo juu kinaonesha kuna ongezeko la taasisi zenye mapungufu ya TEHAMA kutoka taasisi 18 mwaka 2018/19 hadi 20 mwaka 2019/0.Hii inaonyesha hapakuwa na maboresho katika mazingira ya TEHAMA.

Kwa kukosekana sera ya TEHAMA, mpango mkakati wa TEHAMA,mpango wa kuzuia majanga, na mpango endelevu wa kibiashara, taarifa haziwezi kuoatikana kwa wakati panapotokea majanga. Hivyo, taarifa hupotea, jambo ambalo huzuia uendelevu wa shughuli za taasisi.

**Ninapendekeza Maafisa Masuuli kutoa kipaumbele katika uanzishaji na utumiaji wa Sera ya Teknolojia ya Habari, Mpango Mkakati wa TEHAMA, Mpango wa endelevu wa Biashara na mpango wa kuzuia majanga. Pia kuunda mpango mkakati wa TEHAMA.**

### 6.5.1 Ufanisi wa Mfumo wa Usimamizi wa Vifaa (CIMS) katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inamiliki mfumo unaoitwa Mfumo wa Usimamizi wa Vifaa(CIMS) ambao ulitengenezwa na Wakala wa Serikali Mitandao (eGA).

Katika kukagua Mfumo, niligundua changamoto za kiufundi zinazotokana na utengenezaji wa mfumo. Nazo ni hizi zifuatazo:

- Ukosefu wa dirisha la ripoti, ambalo linaweza kuchuja kesi mpya na kesi zilizofungwa kwa kipindi fulani. Mfumo huo hauwezi kuonesha kuhitimishwa kwa kesi na hukumu zilizotolewa.
- Kesi zilizofunguliwa baina ya serikali au taasisi za serikali zenyewe kwa zenyewe au dhidi ya watu wengine na hukumu iliyotolewa. Mfumo hauoneshi mtumiaji aliyesajili kesi hiyo.
- Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina sehemu ndogo kwenye seva ambayo inafanya kuwa ngumu kuhifadhi nyaraka kubwa na nyingi. Hali ya kesi nyingine huripotiwa kuwa hakuna maendeleo kwenye mfumo.

Ni mtazamo wangu kuwa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali bado haijapata tija iliyokusudiwa kutokana na kutumia mfumo huu.

**Ninapendekeza kwa Afisa Masuuli kuwasiliana na wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) ili boresha mfumo ili kukidhi mahitaji na kufikia lengo lililokusudiwa bila kucheleweshwa zaidi.**

### 6.5.2 Hakuna Usuluhisho wa Mapato Yanayokusanywa na Kuripotiwa kwenye Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT-HOMIS) na Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GEPG)

Kulingana na Utaratibu Na. 3.0 wa Kiwango cha Uendeshaji wa Malipo ya kielektroniki ya Serikali (GePG) wa Novemba, 2019, lazima kuwe na usuluhisho wa taarifa kila siku kati ya hati ya madai dhidi ya mfumo wa malipo ya serikali (GePG) na mfumo wa malipo ya serikali (GePG) dhidi ya taarifa za fedha za benki na kutoa ripoti inayoonesha dosari kwa mhusika.

Kinyume na kanuni hiyo hapo juu, Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRH) hazikufanya usuluhisho wa kila siku au kila mwezi kati ya Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT-HoMIS) na taarifa ya fedha za benki kupitia njia ya Serikali ya Malipo ya kielektroniki (GePG). Ufafanuzi zaidi umefafanuliwa katika **Jedwali Na. 43**

**Jedwali Na. 43: Hakuna Usuluhisho wa mapato yanayokusanywa na kuripotiwa kwenye Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT-HOMIS) na mfumo wa malipo ya serikali (GePG)**

| Na | Taasisi | Mapungufu |
|---|---|---|
| 1 | Singida RRH | Kulikuwa na tofauti kati ya makusanyo ambayo yaliripotiwa katika Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania GOTHOMIS Sh.1,075,534,700.00 na ukusanyaji ambao uliripotiwa katika taarifa ya benki kupitia mfumo wa malipo ya serikali GePG Sh. 2,025,455,394.62 kutoka Julai 2019 hadi Juni 2020 na kusababisha kiasi kisichosuluhishwa cha Sh .950,220,694.56 |
| 2 | Songwe RRH | Mfumo hauna uhusiano na mfumo wa benki. Hii inazuia usuluhisho wa madai wakati wa kuweka fedha benki, ikimaanisha kuwa hairuhusu kutoa ripoti za wabadilishaji; badala yake, usuluhishi hufanywa kwa njia za kienyeji, hivyo usababisha ucheleweshaji wa kuweka fedha benki.<br><br>Mapato yaliyokusanywa kutokana na kugawana gharama za pamoja kwa wakala aliye na mkataba (NHIF) hayakuunganishwa kwenye mfumo. |
| 3 | Ligula RRH | Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania GoT HoMIS hauna uhusiano na mifumo mingine ya hospitali kama vile maabara na mashine za mionzi. |

| Na | Taasisi | Mapungufu |
|---|---|---|
| 4 | Sekou Toure RRH | Makusanyo kupitia Mfumo wa malipo ya Serikali (GePG) yalikuwa kiasi cha Sh. 1,662,833,814 dhidi ya kiasi cha Sh.1,579,503,480 makusanyo kupitia Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania GoT-HoMIS na kusababisha kiasi ambacho hakina usuluhisho Sh. 83,330,334 |
| 5 | Mawenzi RRH | Kiasi cha Sh.572,631,465 kilikusanywa kupitia Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GOTHOMIS) na makusanyo kupitia taarifa ya benki kwenye mfumo wa malipo ya serikali (GePG) Sh.1,279,477,402 na kusababisha kiasi ambacho hakina usuluhisho Sh 706,845,937. |
| 6 | Iringa RRH | Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania GoT HoMIS hauna mahusiano na mifumo mingine ya hospitali kama maabara na machine za mionzi |

*Chanzo:Barua ya Mapungufu kwa Menejimenti 2019/20*

Kushindwa kufanya usuluhisho kati ya Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo Serikalini (GePG) na mifumo mingine ya ukusanyaji kunaweza kusababisha makosa ya muda mrefu ya wazi na yasiyo ya wazi yasigunduliwe na kurekebishwa ipasavyo. Thamani ya fedha iliyowekezwa kwenye mfumo haitaweza kupatikana kutoka katika Hospitali ya Rufaa za Mkoa; na inaweza kusababisha mwanya wa matumizi mabaya ya mapato badala ya kutatua shida.

**Ninapendekeza Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na mamlaka husika kuhakikisha kuwa mfumo unatumiwa vyema, na mapungufu ambayo nimeelekeza hapo juu yatafutiwe suluhisho.**

## SURA YA SABA

## UKAGUZI WA RASILIMALI WATU NA USIMAMIZI WA MISHAHARA

### 7.1 Utangulizi

Ili kuwa na Watumishi wa Umma wenye ubunifu,weledi, tija na wenye kukidhi vigezo vinavyoendana na malipo ya mishahara kwa kazi wanazofanya, Taasisi za Serikali zina jukumu na wajibu wa kuandaa mipango mizuri na inayojitosheleza,yenye uwiano mzuri ikiwa ni pamoja na kutenga rasilimali zenye kukidhi majukumu na mahitaji ya Watumishi.

Sura hii inaelezea masuala muhimu yaliyoibuliwa katika ukaguzi wa rasilimali watu na usimamizi wa mishahara katika Wizara, Idara na Wakala, Taasisi nyinginezo za Serikali na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Ukaguzi niliofanya katika eneo hili ulilenga kupitia na kujiridhisha kama kuna ufanisi wa mifumo ya Taasisi inayohusu usimamizi bora wa Sera, Kanuni, taratibu za utunzaji wa nyaraka, na taarifa za utendaji wa Watumishi wa Umma. Aidha, nilipitia mifumo ya usimamizi wa mishahara kwa kukagua nyaraka zote zinazohusu malipo ya mishahara na kuhakiki mapengo yaliyopo kati ya nyaraka za mishahara na taarifa za Watumishi kwenye mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu. Kwa ujumla, ukaguzi ulilenga katika kuangalia kama Taasisi za Umma zinafuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyowekwa ili kusimamia rasilimali watu na ulipaji wa mishahara.

Licha ya maboresho madogo yaliyoonekana kuhusu usimamizi wa rasilimali watu na mishahara kwa kulinganisha na miaka iliyopita,nimebaini mapungufu yanayohitaji maboresho na Serikali kutilia mkazo kama yanavyoelezwa hapa chini:

### 7.2 Upungufu wa Watumishi kwenye Taasisi za Umma

Aya Na. 83 (ii) ya Taarifa ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2019/20 iliweka mkazo katika kuongeza ubora wa nguvu kazi ili kukuza uchumi na maendeleo ya taifa.

Pia, Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, zinaelezea umuhimu wa kujaza nafasi za Watumishi wanaokoma Utumishi wa Umma kwa sababu mbalimbali. Aidha Ikama zilizoandaliwa na Taasisi za Umma

zinaonesha idadi ya Watumishi waliopo, wanaohitajika, na upungufu uliopo.

Katika kufanya ukaguzi wa kina, nilipitia taarifa mbalimbali zinazohusu Watumishi kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ikama za Taasisi za Serikali na kufanya tathmini ili kujiridhisha na utekelezaji wa mojawapo ya vipaumbele vya bajeti kinachosisitiza uboreshaji wa eneo la rasilimali watu katika Taasisi za Serikali na kubaini mapungufu yafuatayo:

### 7.2.1 Utoaji Usioridhisha wa Vibali vya Ajira Mpya Serikalini

Kanuni Na D.7 (1) na (4) za Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 zinaelezea jukumu la Sekretarieti ya Ajira katika kuhakikisha ujazaji wa nafasi za Utumishi wa Umma zilizoachwa wazi kwa kuajiri Watumishi wapya na kusimamia zoezi la ajira za Watumishi wa Umma.
Kwa mwaka huu wa ukaguzi, nimeona juhudi za Serikali katika kuboresha eneo la rasilimali watu kwa njia ya ajira impya. Aidha, nimebaini kuwa, Serikali ilipanga kuajiri Watumishi wapya 9,522 ,watumishi 8,927 kwa ajili ya Wizara, Idara na Wakala,na watumishi wengine 406 kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa na watumishi 185 kwa ajili ya Taasisi zingine.

Hata hivyo, tofauti na bajeti na mipango ya kuajiri iliyopo, nilibaini kuwa maombi ya kuajiri Watumishi wapya yaliyopokelewa kutoka Taasisi za Umma yalikua 29,805 ambayo ni sawa na 213% ya ajira zilizopangwa na Serikali kwa mwaka 2019/20,maombi hayo yalikuwa 28,057 kwa ajili ya Wizara,Idara na Wakala,1016 kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa na 732 kwa ajili ya Taasisi zingine za Serikali. Aidha ,katika maombi hayo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilikubali na kutoa vibali vya ajira za Watumishi wapya 9,225 kwa ajili ya Wizara,Idara na Wakala tu ambavyo havikutosheleza mahitaji ya ajira mpya za Watumishi zilizoombwa.

Kwa ujumla, Serikali haijaweza kujaza kikamilifu nafasi zilizo wazi katika Taasisi zake na hivyo kupelekea Taasisi nyingi kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa kutokana na idadi ndogo ya Watumishi. **Kielelezo Na. 15** kinaonesha uchambuzi kati ya ajira zilizopangwa, zilizoombwa na vibali vilivyotolewa.

**Kielelezo Na. 15: Uchambuzi wa ajira zilizopangwa, zilizoombwa na zilizotolewa na Serikali**




*Chanzo: Taarifa za Watumishi zilizotolewa na Ofisi ya Rais- UTUMISHI na UTAWALA BORA*

### 7.2.2 Upungufu wa Watumishi wa Umma katika Taasisi za Serikali

Nilipitia Ikama za Taasisi mbalimbali za Serikali ambazo zinaonesha idadi ya Watumishi waliopo, wanaohitajika na upungufu wa Watumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2019/20 na kubaini kuwapo kwa upungufu wa Watumishi 7,889 katika Taasisi 52 za Serikali. Upungufu huu ulisababishwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Taasisi husika kushindwa kufanya tathmini ya kutosha na kujaza nafasi zilizo wazi kwenye Taasisi za Serikali kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 44** na **Kiambatisho Na. XV**

**Jedwali Na. 44: Upungufu wa Watumishi katika Taasisi za Serikali.**

| Na | Jina la Taasisi | Idadi ya Taasisi | Watumishi wanaotakiwa | Watumishi waliopo | Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Wizara na Taasisi zake | 16 | 7932 | 5614 | 2318 |
| 2. | Wakala za Serikali | 8 | 3339 | 1,178 | 2,161 |
| 3. | Taasisi | 19 | 3860 | 2042 | 1818 |

| Na | Jina la Taasisi | Idadi ya Taasisi | Watumishi wanaotakiwa | Watumishi waliopo | Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| | nyingine | | | | |
| 4. | Sekretarieti za Mikoa | 9 | 3,147 | 1,555 | 1,592 |
| **Jumla** | | **52** | **18278** | **10389** | **7889** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ninaendelea kusisitiza kuwa, uhaba wa Watumishi wa Umma uliopo Serikalini unaathiri utendaji wa Taasisi za Serikali na kuzisababishia kutofikia malengo yaliyopangwa kwa ufanisi.

**Katika kuhakikisha tatizo la upungufu wa ajira linatatuliwa, ninapendekeza Serikali ifanye tathmini ya kutosha ya mahitaji ya Watumishi na kuongeza ajira za Watumishi wapya kwenye Taasisi zake, ili isaidie katika kutimiza malengo ambayo ni kutoa huduma zenye ubora na zinazokidhi mahitaji ya wananchi.**

## 7.3 Makato ya Mishahara Kutowasilishwa katika Taasisi Husika Sh.1, 557,988,754.82

Kifungu Na.18 na 19 vya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ya mwaka 2018 vinaelezea wajibu wa waajiri kukata na kulipa michango kwa niaba ya wafanyakazi wao kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa 20% ya mshahara wa mwezi wa kila mfanyakazi. Pia vinaeleza kuwa kutowasilisha makato hayo kwa wakati kutapelekea adhabu ya asilimia nusu ya kiasi ambacho Mwajiri ameshindwa kupeleka kama inavyotakiwa na Sheria.

Aidha, Kifungu Na.84 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, (Iliyorekebishwa 2012) kinataka kila kodi kadri ya kipato (PAYE) iwasilishwe kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ndani ya siku saba baada ya mwisho wa kila mwezi.

Hata hivyo, nilibaini Taasisi tisa zilichelewa kuwasilisha makato ya kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Bima ya Afya na Mamlaka ya Mapato ya kiasi cha Sh.1, 025,969,290.90 kwa kipindi cha kati ya miezi mitatu hadi 15 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 45**.

Pia, niligundua kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu Na. 44 na 60) ilichelewa kutuma fedha zinazohusiana na makato ya mishahara ya Watumishi wa Umma zenye thamani ya Sh.532,019,463.92 kwa Taasisi

saba zilizo chini ya wizara hiyo kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 46**

**Jedwali Na. 45: Makato yaliyocheleweshwa kuwasilishwa na Taasisi.**

| Na | Taasisi | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Bima ya Afya na Mamlaka ya Mapato | Kiasi (Sh.) | Muda (Miezi ) |
|---|---|---|---|---|
| **Wizara na Idara** | | | | |
| 1. | Wizara ya Viwanda na Biashara - Fungu Na. 44 na 60 | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) | 44,546,179 | 5 |
| 2. | Wizara ya Viwanda na Biashara - Fungu Na. 44 na 60 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma(PSSSF) | 74,886,779 | 15 |
| 3. | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya - Fungu Na. 91 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma(PSSSF) | 10,155,850 | 3 |
| | | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) | 8,760,210 | 3 |
| **Taasisi nyingine** | | | | |
| 4. | Shule ya Sekondari Kawawa JKT | Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 8,770,700 | 3 |
| | | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 2,214,305 | 3 |
| 5. | Shule ya Sekondari Jitegemee JKT | Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 200,049,200 | 11 |
| | | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 161,920,329 | 11 |
| 6. | Baraza la Madaktari Tanganyika | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma(PSSSF) | 1,567,500 | 7 |
| | | Mfuko wa Taifa wa | 627,000 | 7 |

| Na | Taasisi | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Bima ya Afya na Mamlaka ya Mapato | Kiasi (Sh.) | Muda (Miezi ) |
|---|---|---|---|---|
| | | Bima ya Afya (NHIF) | | |
| | | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 1,587,300 | 7 |
| 7. | Mamlaka ya Mapato Tanzania-Idara ya Matumizi (TRA) | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) | 419,027,376 | 1 |
| | | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma(PSSSF) | 5,784,345 | 1 |
| **Wakala** | | | | |
| 8. | Wakala wa vipimo Tanzania (WMA) | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 63,522,300 | 12 |
| 9. | Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) | 22,549,918 | 4 |
| **Jumla** | | | **1,025,969,291** | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

**Jedwali Na. 46: Fedha kwa Ajili ya Makato Zilizocheleweshwa Kutumwa**

| Na | Fungu | Taasisi | Kiasi (Sh.) | Muda (Miezi) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 44 | Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) | 17,643,809 | 2 |
| 2. | | Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) | 41,290,794 | 5 |
| 3. | | Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) | 308,623,571 | 4 |
| 4. | | Shirika la Utafiti wa Viwanda Tanzania (TIRDO) | 43,726,524 | 3 |

| Na | Fungu | Taasisi | Kiasi (Sh.) | Muda (Miezi) |
|---|---|---|---|---|
| 5. | | Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) | 86,887,893 | 3 |
| 7. | | Mamlaka ya Eneo Maalumu la Uwekezaji na Mauzo nje ya nchi na nchini Tanzania (EPZA) | 15,225,898 | 3 |
| 6. | 60 | Baraza la Ushindani Tanzania (FCT) | 12,316,425 | 11 |
| 7. | | Bodi ya leseni za Maghala Tanzania (TWLB) | 6,304,550 | 2 |
| **Jumla** | | | **532,019,464** | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejiment 2019/20*

Kwa maoni yangu, kuchelewa kuwasilisha makato yanayohusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Bima ya Afya na Mamlaka ya Mapato Tanzania, kunasababishwa na kutokuwa na utaratibu mzuri wa kufuatilia makato na uwasilishaji wa makato hayo kwa wakati. Aidha, ucheleweshaji huu unaweza kupelekea Taasisi husika kulipa malipo yasiyo na tija kutokana na adhabu zinazoweza kutolewa kwa kushindwa kuwasilisha makato kwa wakati ,pia inaweza kupelekea kuathiri mafao ya mwisho ya Watumishi pindi wanapokoma Utumishi wa Umma.

**Napendekeza kwa Maafisa Masuuli kuanzisha taratibu na mifumo wezeshi itakayohakikisha kuwa makato yatokanayo na mishahara yanawasilishwa kwenye Mifuko ya Bima ya Afya, Hifadhi ya Jamii pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa wakati ili kuepuka adhabu ambazo zimeainishwa kwenye sheria husika.**

### 7.4 Kutokulipa Madai ya Watumishi wa Umma Sh. 331,518,426,304.13

Kanuni Na. E.23 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009, inasisitiza kuwa madai ya Watumishi yalipwe mara tu yanapotokea.
Kupitia ukaguzi nilioufanya kwenye Taasisi 80 zenye madai ya Watumishi yanayozidi Sh.100,000,000 nimebaini kuwa, madai ya Watumishi yanayotokana na malimbikizo ya mishahara pamoja na posho mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2019/20 yalikuwa yamefikia Sh.331,518,426,304.13. Maelezo ya kina ya hali halisi ni kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. XVI.**

Aidha nimefanya ulinganisho ya madai ya Watumishi kati ya mwaka 2019/20 na kwaka 2018/19 na kubaini kuwapo kwa ongezeko la madai kutoka Sh. 307,612,008,474.46 hadi Sh. 331,518,426,304.14 sawa na asilimia 7.8 kama inavyoonekana kwenye kielelezo hapo chini.




*Chanzo: Taarifa za Fedha za Taasisi za Mwaka 2019/20*

Kwa maoni yangu, upungufu huu umesababishwa na serikali kutotenga fedha zinazotosha kwa ajili ya upandishaji wa vyeo tarajiwa, ajira za kwanza na stahiki za Watumishi kama posho za kukaimu, posho za safari na posho zingine zinazohusiana na ajira

Aidha, kutolipa madai ya Watumishi kwa wakati kunaweza kusababisha ongezeko la madeni kwenye Taasisi za Serikali pia kushusha utendaji wa Watumishi wa Umma katika kutoa huduma zilizo bora kwa wananchi.

**Ninashauri Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora pamoja na Maafisa Masuuli wote kuhakikisha kuwa madai ya Watumishi yanapewa uzito unaostahili na kulipwa bila kucheleweshwa.**

### 7.5 Kutorejesha Mishahara Isiyolipwa Sh.222, 683,585.95

Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa barua Na. EB.3/102/02/03 ya tarehe 28 Mei 2019 yenye kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wote kurejesha mishahara ambayo haikulipwa mwezi husika kwa sababu mbalimbali kwenda kwenye akaunti Na. 9921141201 iliyopo Benki Kuu ya Tanzania.

Katika ukaguzi niliofanya, nilibaini Taasisi mbili za Serikali ambazo zilikuwa na bakaa ya mishahara ambayo haikurejeshwa Wizara ya Fedha na Mipango inayofikia Sh.222,683,585.95 kwenye akaunti zao za amana. Upungufu huu umetokana na kutokuwapo kwa usimamizi wa kutosha wa kuhakikisha mishahara isiyolipwa inarudishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa wakati. **Jedwali Na. 47** linaonesha Taasisi na mishahara ambayo haikurejeshwa.

**Jedwali Na. 47: Mishahara ambayo Haijarejeshwa**

| Fungu Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 28 | Jeshi la Polisi Tanzania | 192,444,077.39 |
| 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. | 30,239,508.56 |
| **Jumla** | | **222,683,585.95** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ni maoni yangu kuwa, mapungufu yaliyoainishwa hapo juu yanaweza kupelekea kuwapo matumizi mabaya ya fedha za Umma na kusababisha Taasisi husika kutumia fedha hizo kwa matumizi mengine kinyume na malipo ya mishahara yaliyokusudiwa.

**Ninashauri kuwa Maafisa Masuuli wahakikishe mishahara hiyo iliyopo kwenye akaunti zao za amana inarudishwa kwenye akaunti iliyopo Benki Kuu kama ilivyolekezwa na barua kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.**

## 7.6 Malipo ya Mishahara kwa Watumishi Waliokoma Utumishi wa Umma Sh. 59,158,470

Kanuni Na 113(3) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inaelekeza Taasisi za Umma kuhakikisha malipo ya mishahara yanafanyika kwa Watumishi waliopo kwenye kumbukumbu za malipo baada ya kuwa wametambuliwa na kuingia kwenye mikataba ya makubaliano ya kazi.

Hata hivyo, kupitia ukaguzi nilioufanya wa Taarifa zinazohusu mishahara nimebaini kuwa, Taasisi tatu zilizo chini ya Wizara na Mamlaka ya Serikali zilifanya malipo yanayofikia Sh. 59,158,470 kwa Watumishi 22 waliokuwa wamekwisha koma Utumishi wa Umma. **Jedwali Na. 48** linaonesha mchanganuo wa malipo hayo.

**Jedwali Na. 48: Malipo ya Mishahara kwa Watumishi Waliokoma Utumishi wa Umma**

| Fungu Na. | Taasisi | Idadi ya Watumishi | Kiasi kilicholipwa |
|---|---|---|---|
| 40 | Mahakama ya Tanzania | 11 | 34,192,305.00 |
| 52 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | 7 | 21,646,000.00 |
| | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania | 4 | 3,320,165.00 |
| **Jumla** | | | **59,158,470.00** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Aidha, Kwa kulinganisha taarifa niliyoitoa mwaka 2018/19 na ukaguzi wa mwaka huu wa 2019/20 nimebaini kuwa kuna ongezeko la Taasisi kutoka moja hadi tatu ambazo zimefanya malipo ya aina hiyo. Pia, nimebaini kuwa tatizo hili linasababishwa na sababu zifuatazo; kuchelewa kuhuisha Taarifa za Watumishi kwenye Mfumo wa mishahara, kutokuwa na utaratibu wa kupitia taarifa za Watumishi mara kwa mara, kukosekana kwa mawasiliano mazuri kati ya Taasisi za Umma na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora na pia kuchelewa kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuwaondoa Watumishi waliokoma Utumishi wa Umma kwenye mifumo ya malipo ya mshahara.

Kwa maoni yangu , malipo kwa Watumishi waliokoma Utumishi wa Umma yanaweza kuisababishia Serikali hasara iwapo fedha zilizolipwa kwa Watumishi hao hazitarejeshwa Serikalini.

**Kwa kuwa mapungufu haya yameoneshwa kwenye taarifa zangu za nyuma, hivyo naendelea kuwashauri Maafisa Masuuli kuwa, wahakikishe wanaboresha mifumo ya mishahara na kufanya makubaliano na mifuko ya hifadhi ya jamii ili kurejesha fedha hizo kupitia mafao ya Watumishi hao.**

## 7.7 Watumishi wa Umma Wanaokaimu Nafasi za Juu kwa Zaidi ya Miezi Sita

Kanuni Na D.24 ya Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inaelekeza Watumishi wa Umma kukaimu nafasi za juu kwa muda usiozidi miezi sita, pia inaelekeza mamlaka za uteuzi kuhakikisha kuwa taratibu za kuthibitisha Watumishi wanaokaimu nafasi hizo zinakamilishwa katika muda unaotakiwa.

Hata hivyo ukaguzi wangu wa nyaraka za rasilimali watu ulibaini Watumishi 384 wa Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Taasisi nyingine za Serikali 43 wanakaimu nafasi za juu bila ya uteuzi kwa muda mrefu (kati ya miezi 8 hadi 106) kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 49** na **Kiambatisho Na. XVII**

**Jedwali Na. 49: Taasisi zenye Watumishi Wanaokaimu Zaidi ya Miezi Sita**

| Maelezo ya Taasisi | Idadi ya Tasisi | Idadi ya Watumishi wanaokaimu |
|---|---|---|
| Wizara na Idara | 13 | 172 |
| Wakala za Serikali | 10 | 121 |
| Taasisi nyingine | 11 | 67 |
| Sekretarieti za Mikoa | 9 | 24 |
| **Jumla** | **43** | **384** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ni maoni yangu kuwa kuendelea kuwapo kwa watumishi wanaokaimu kwa muda mrefu nafasi za juu bila kuthibitishwa kunapunguza motisha na uwajibikaji katika utendaji kazi.

**Pamoja na kugusia mapungufu haya kwenye taarifa za ukaguzi za miaka iliyopita, ninaendelea kushauri kuwa Maafisa Masuuli washirikiane na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Fedha na Mipango kutatua tatizo hili , Pia kuzingatia Sheria zilizowekwa ambazo zinatilia mkazo Watumishi kuthibitishwa katika vyeo vyao pale ambapo wanatimiza vigezo vilivyopo**

## 7.8 Taasisi za Umma Kutofanya Tathmini ya Ufanisi na Utendaji Kazi

Kanuni ya 22(1) ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2003 pamoja na Kanuni Na D.62 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 zinazitaka Taasisi za Umma kupitia na kufanya tathmini ya ufanisi kwa watendaji wake wote.

Katika Ukaguzi wangu wa mwaka 2019/20, nimebaini kuwa Taasisi 11 hazikufanya tathmini ya utendaji na ufanisi kwa Watumishi wake kinyume na matakwa ya Kanuni za Utumishi wa Umma.Nikilinganisha na taarifa yangu ya mwaka 2018/19, kuna ongezeko la Taasisi zisizofanya tathimini ya utendaji wa Watumishi kutoka Taasisi saba hadi 11. Hivyo, Serikali inatakiwa kuyafanyia kazi mapungufu yaliyoainishwa kwenye eneo hili na kuhakikisha kuwa Serikali inakuwa na Watumishi wenye tija katika kutimiza malengo yaliyowekwa. **Jedwali Na. 50** limeainisha Taasisi husika.

**Jedwali Na. 50: Taasisi ambazo Hazikupima Utendaji wa Watumishi**

| Na | Taasisi |
|---|---|
| **Wizara na Taasisi Zake** | |
| 1. | Wizara ya Viwanda na Biashara- Fungu Na. 44 |
| 2. | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka - Fungu Na. 35 |
| **Taasisi zingine** | |
| 3. | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa |
| 4. | SUMA JKT-Ulinzi |
| 5. | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa |
| 6. | Shule ya Sekondari ya Kawawa JKT |
| 7. | Ofisi ya Rais- Chuo Cha Utumishi wa Umma |
| 8. | Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania |
| **Wakala** | |
| 9. | Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo |
| 10. | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) |
| **Sekretarieti za Mikoa** | |
| 11. | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe – Fungu Na. 90 |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ni maoni yangu kuwa, kutofanya tathmini ya ufanisi na utendaji wa Watumishi, kunaweza kuathiri menejimenti za Taasisi husika kwa kushindwa kujua ufanisi wa Watumishi na hivyo kushindwa kuwapandisha vyeo Watumishi wanaostahili. Pia , kutasababisha menejimenti kutotambua mapungufu yaliyopo ili yaweze kurekebishwa kwa wakati.

**Ni ushauri wangu kuwa, Maafisa Masuuli wa kila Taasisi husika kufanya tathmini ya utendaji na ufanisi kwa Watumishi mara kwa mara ili kupima uwezo wao na kuwapa stahiki zenye kuendana na ufanisi wao wa kazi kutokana na matokeo ya tathmini walizofanya.**

## 7.9 Mishahara Iliyolipwa Chini ya Theluthi Moja ya Mishahara Ghafi

Kifungu Na. 3 cha Sheria ya Kurejesha Madeni ya mwaka 1970 na waraka uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wenye kumbukumbu Na. C/CE.45/271/01/l/87 wa tarehe 19/3/2009 vinataka mshahara wa mwezi anaolipwa mfanyakazi usiwe pungufu kwa kiasi cha moja ya tatu ya mshahara ghafi wake wa mwezi.

Hata hivyo, nilipitia na kukagua nyaraka mbalimbali za mishahara ya Watumishi kwa mwaka wa fedha 2019/20 na kubaini kuwapo kwa Taasisi 10 zenye Watumishi 112 waliopokea mshahara ulio chini ya moja ya tatu ya mshahara wa mwezi. Aidha, nilibaini kuwa upungufu huu unatokana na Sheria mpya ya Bodi ya mikopo ya elimu ya juu ambayo imeongeza makato ya wanufaika wa mikopo kutoka asilimia 8% hadi 15% ya mshahara.

Pia, ulinganisho kati ya ripoti ya mwaka 2018/19 na mwaka 2019/20 unaonesha Watumishi wenye makato makubwa wamepungua kwa 16% kutoka Watumishi 134 hadi 112. Hivyo, naendelea kuzishauri Taasisi husika kuzingatia kikamilifu Sheria zinazohusu makato na ulipaji wa Mishahara. Taarifa zaidi kuhusu upungufu huu inaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 51.**

**Jedwali Na. 51: Orodha ya Taasisi zenye Watumishi wenye Makato Makubwa**

| Na | Taasisi | Idadi ya Watumishi |
|---|---|---|
| 1. | Wizara ya Viwanda na Biashara-Fungu Na. 44 | 4 |
| 2. | Wizara ya Viwanda na Biashara-Fungu Na. 60 | 2 |
| 3. | Wizara ya Afya,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto- Fungu Na. 52 | 13 |
| 4. | Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. | 24 |
| 5. | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro – Fungu Na. 70 | 10 |
| 6. | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga -Fungu Na. 86 | 6 |
| 7. | Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 13 |
| 8. | Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi | 6 |
| 9. | Hospitali ya Rufaa ya Wagonjwa wa Akili ya Mirembe na Chuo cha Isanga | 22 |
| 10. | Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania | 12 |
| **Jumla** | | **112** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ni maoni yangu kuwa, kutodhibiti kiwango cha makato ya mishahara kwa Watumishi, kunaweza kuathiri utendaji na ufanisi wao na kuathiri utendaji wa Taasisi za Serikali kiujumla.

**Kwa kuwa, Ripoti zangu za miaka ya nyuma zilionesha mapungufu kama yaliyoonekana kwenye ukaguzi wa mwaka huu wa fedha, hivyo ninaendelea kushauri Maafisa Masuuli wa Taasisi husika kuhakikisha kuna udhibiti wa uidhinishaji mikopo. Pia, kufanya mawasiliano ya karibu na Taaasisi za kifedha ili kutotoa mikopo kwa wafanyakazi kinyume na kiwango kinachotakiwa.**

### 7.10 Malipo ya Posho za Kukaimu Bila Idhini ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora Sh. 73,688,534

Kanuni Na. D. 19(1)-(3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 inaelezea namna ya kulipa Watumishi wanaokaimu nafasi mbalimbali za uongozi kwa kipindi kinachozidi siku 14.

Ukaguzi nilioufanya wa nyaraka na mifumo ya rasilimali watu na mishahara umebaini kuwa wakala za Serikali mbili zililipa kiasi cha Sh. 73,688,534 kwa Watumishi 13 waliokuwa wanakaimu nafasi mbalimbali bila ya kuwa na idhini kutoka kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Idadi ya Watumishi hao imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 52** hapa chini.

**Jedwali Na. 52: Malipo ya Kukaimu bila Idhini**

| Na | Jina la Wakala | Idadi ya Watumishi | Kiasi kilicholipwa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Wakala wa Huduma za Ufundi na Umeme Serikalini | 10 | 67,518,734.00 |
| 2. | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania | 3 | 6,169,800.00 |
| **Jumla** | | | **73,688,534.00** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ni maoni yangu kuwa, posho za kukaimu zilizolipwa hazikuwa na uhalali na hivyo, kiasi cha fedha kilicholipwa kingeweza kutumika kulipia matumizi mengine yenye tija zaidi.

**Ninashauri Maafisa Masuuli husika wahakikishe wanapata idhini kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kabla ya kuteua na kulipa Watumishi wanaokaimu nyadhifa mbalimbali na kuhakikisha fedha zilizolipwa kwa malipo yasiyo na uhalali zinarudishwa Serikalini.**

### 7.11 Malipo yaliyofanyika kwa Watumishi Wasiokuwa na Mikataba Halali Sh.105, 609,740

Kanuni Na. D.33 (1) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 inaelezea waajiri kuingia mkataba unaoonesha masharti ya kazi husika kwa Watumishi wanaoajiriwa kwa ajira ya pensheni au isiyo ya pensheni.

Ukaguzi niliofanya katika eneo hili, umebaini Taasisi nne za Umma zilizofanya malipo yanayofikia Sh.105,609,740 kwa ajili ya Watumishi 15 waliaojiriwa kwa muda mfupi kwa masharti yasiyo ya pensheni bila ya kuwa na mikataba. Malipo hayo yamefanyika kinyume na Kanuni ya Kudumu ya Utumishi wa Umma kama yanavyooneshwa kwenye **Jedwali** Na. **53**

**Jedwali Na. 53: Malipo kwa Watumishi wasiokuwa na Mikataba**

| Na | Taasisi ya Serikali | Idadi ya Watumishi | Kiasi kilicholipwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa | 3 | 4,845,240.00 |
| 2. | Hospitali ya Rufaa ya Wagonjwa wa Akili ya Mirembe na Chuo cha Isanga | 2 | 10,544,000.00 |
| 3. | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tumbi | 7 | 64,540,500.00 |
| 4. | Idara ya Zana za Kilimo SUMA JKT | 3 | 25,680,000.00 |
| **Jumla** | | | **105,609,740.00** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kwa kutokuwa na mikataba, Taasisi hizo zinaweza kushindwa kudhibiti utendaji wa Watumishi hao. Pia, kunaongeza hatari ya kulipa adhabu zisizostahili endapo kutatokea migogoro kwani Taasisi hazitakuwa na uthibitisho wa masharti yaliyopo kwenye mikataba baina ya Taasisi na Watumishi.

**Ninashauri menejimenti za Taasisi za Umma nilizoziorodhesha hapo juu kuhakikisha zinafuata matakwa ya Sheria, Kanuni na Taratibu katika kuandaa na kuhuisha mikataba pale inapokuwa imeisha muda wake. Pia, kuhakikisha zinafanya tathmini za mara kwa mara ili kubaini utendaji wa watumishi hao.**

### 7.12 Kutoandaa Mipango ya Mafunzo

Mpango wa mafunzo ni muhimu sana katika kupanga taratibu nzuri wa kutoa mafunzo kwa Watumishi na kuwaongezea ujuzi ambao utawasaidia kukuza utendaji wao wa kazi. Kanuni Na. G.1 (7) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009, inataka Taasisi zote za Umma kuandaa mipango ya mafunzo kwa kuangalia mahitaji ya Watumishi na malengo ya Taasisi husika.

Hata hivyo, ukaguzi nilioufanya umebaini Taasisi saba ambazo hazikuandaa mpango wa mafunzo kinyume na Kanuni za Utumishi wa Umma zinavyoelekeza. **Jedwali Na. 54** linaonesha Taasisi husika.

**Jedwali Na. 54: Taasisi ambazo Hazikuandaa Mpango wa Mafunzo**

| Na | Taasisi za Umma |
|---|---|
| 1. | Idara ya Uhamiaji - Fungu Na. 93 |
| 2. | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa – Fungu Na. 57 |
| 3. | Tume ya Utumishi wa Walimu - Fungu Na. 2 |
| 4. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania |
| 5. | Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori Tanzania |
| 6. | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania |
| 7. | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini |

***Chanzo**: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Aidha, nilibaini kuwa sababu ya kutoandaa mipango ya mafunzo ni kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha zilizotengwa kwa zoezi hilo. Pia, ni maoni yangu kuwa, kutoandaa mipango ya mafunzo kunaweza sababisha Taasisi husika kutofikia malengo yaliyopangwa ya mafunzo kwa watumishi na kuathiri utendaji na ufanisi wa Watumishi.

**Ninashauri menejimenti za Taasisi za Serikali husika kuhakikisha kuwa mipango ya mafunzo inaandaliwa ili kuongeza ujuzi wa Watumishi kwenye nyanja za utendaji, uzalishaji na motisha ya kufanya kazi kutokana na mafunzo watakayoyapata,kutenga fedha kwa ajili ya zoezi hilo na Wizara ya Fedha na Mipango kulipa Fedha zilizotengwa na Taasisi husika.**

## SURA YA NANE

## UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI, MIFUKO MAALUMU YA FEDHA, BODI ZA MABONDE YA MAJI, HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA NA TAASISI NYINGINE

### 8.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Wakala wa Serikali 34, Mifuko Maalumu ya Fedha 14, Taasisi Nyingine za Serikali 53, Bodi 15 za Mabonde ya maji na Hospitali 32 za Rufaa za Mkoa na Hospitali Maalumu.

Katika Sura hii nimeonesha masuala mahususi na mtambuka yanayohitaji kushughulikiwa na Serikali, Bunge, Bodi ya Ushauri ya Wizara na Menejimenti za Taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za Taasisi hizo.

### 8.2 Masuala Yaliyobainika katika Ukaguzi wa Wakala za Serikali

Katika ukaguzi wa Wakala za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambazo zimeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala ya mwaka 1997, nimebaini mapungufu kadhaa kuhusu uendeshaji na usimamizi wa kifedha wa Wakala hizo. Aidha, nimeangalia ni jinsi gani Wakala zinasimamia mipango iliyowekwa ya ufuatiliaji wa maendeleo ya miradi yao. Kwa ajili hiyo, yafuatayo ni masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa Wakala wa Serikali.

#### 8.2.1 Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Lengo kuu la TBA ni kutoa makazi bora kwa Serikali na Watumishi pamoja na kutoa ushauri katika masuala ya Ujenzi kwa Serikali. Ukaguzi wa uendeshaji wa TBA ulibaini mapungufu yafuatayo:

##### 8.2.1.1 Maendeleo Yasiyoridhisha katika Ujenzi wa Majengo ya Serikali Mkoani Dodoma – Sh. 46,628,482,327.13

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini kuwa Wakala wa Majengo Tanzania ilikuwa imechelewesha ujenzi wa majengo mbalimbali ya serikali katika mkoa wa Dodoma yenye thamani ya Sh. 46,628,482,327.13, kama ilivyowasilishwa hapa chini:

**(a) Ujenzi wa Jengo la Kanda la Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – Kanda ya kati**

Nilibaini kuwa Wakala wa Huduma za Misitu ya Tanzania ililipa malipo ya awali ya Sh. 2,000,000,000 kwa Wakala wa Majengo Tanzania mnamo tarehe 2 Agosti 2017, ili kugharamia ujenzi wa ofisi ya Kanda ya kati. Hata hivyo, nilibaini ujenzi huu ulikuwa bado haujaanza kwa miaka mitatu mpaka kipindi cha ukaguzi, Septemba 2020. Aidha, nilibaini kuwa TBA ilikuwa ikifanya kazi ya usanifu wa jengo hilo kwa miaka mitatu; na kazi hiyo ya usanifu imekamilika, lakini bado kazi za ujenzi hazikuwa zimeanza.

**(b) Ujenzi wa Jengo la Ofisi za TANESCO katika Mkoa wa Dodoma**

Mnamo tarehe 13 Julai 2020, Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) ilisaini mkataba wenye nambari: PA/001/2019-20/HQ/W/038 na Wakala wa Majengo Tanzania kwa ajili ya kujenga jengo la ofisi mkoani Dodoma kwa bei ya kandarasi ya Sh. 5,433,474,335.06, huku muda wa ujenzi ulipangwa kuisha mnamo tarehe 13 Desemba 2020. Hata hivyo, mpaka kipindi cha ukaguzi, mnamo tarehe 22 Septemba 2020, TBA ilikuwa bado haijawasilisha vifaa vya ujenzi na wataalamu muhimu wanaohitajika katika eneo la ujenzi kwa muda wa miezi miwili mpaka wakati wa Ukaguzi, tarehe 22 Septemba 2020.

**(c) Ujenzi wa Jengo la Ofisi za TANROADS Njendengwa katika Mkoa wa Dodoma**

Mnamo tarehe 19 Septemba 2017, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilisaini hati ya makubaliano (MOU) yenye nambari: MOU/2017/2018/HQ/W na Wakala wa Majengo Tanzania, kwa ajili ya kujenga jengo la ofisi mkoani Dodoma kwa bei ya kandarasi ya Sh. 30,130,732,932.07. Ujenzi ulipangwa kuisha mnamo tarehe 30 Novemba 2019. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi Septemba 2020, nilibaini maendeleo ya kazi za ujenzi yalikua asilimia 33, huku TANROADS ikiwa imelipa jumla ya Sh. 9,919,057,921,56 kwa TBA. Aidha, niligundua kuwa TANROADS haikua imetoa nyongeza ya muda wa mkataba kwa TBA, tokea kuisha kwa muda wa mkataba wa tarehe 30 Novemba 2019.

**(d) Ujenzi wa Makao makuu na Ofisi ya Kanda ya Tume ya Maadili katika Mkoa wa Dodoma**

Tume ya Maadili ilisaini mkataba wenye nambari: IE/022/2015-2016/W/02 na Wakala wa Majengo Tanzania, kwa ajili ya kujenga

jengo la ofisi mkoani Dodoma kwa bei ya kandarasi ya Sh. 9,064,275,060 huku muda wa kuanza kwa mradi ukiwa ni tarehe 15 Juni 2019 na ujenzi ulipangwa kukamilika mnamo tarehe 15 Desemba 2022. Katika ukaguzi wa mkataba huu nilibaini kuwa TBA ilitumia asilimia 50% ya muda wa mradi huku maendeleo ya mradi yalikuwa ni 20% tu kama ilivyoonekana muda wa ukaguzi Septemba 2020. Hali hii imeuweka mradi huu katika hatari ya kuchelewa kukamilika na kuongezeka maradufu kwa gharama ya mradi. Aidha, Tume ya Maadili ililipa TBA malipo ya awali ya Sh. 1,317,911,515.12, ambayo ni 15% ya gharama ya mkataba, lakini bado, mradi unatekelezwa kwa kasi ndogo.

Kwa maoni yangu, udhaifu uliotajwa hapo juu unachangiwa na usimamizi usioridhisha wa fedha za miradi, vifaa vya ujenzi, upungufu wa wataalamu pamoja na upungufu wa mitambo ya ujenzi. Kwa maoni yangu, maendeleo yasiyoridhisha ya ujenzi wa majengo ya serikali mkoani Dodoma, yameathiri malengo ya serikali ya kuhakikisha kuwa serikali nzima inahamia Dodoma kwenye makao makuu mapya ya nchi.

**Kwa hivyo, ninapendekeza serikali itathmini uwezo wa TBA kusimamia na kukamilisha ujenzi wa miradi tajwa, pamoja na kuangalia njia za kutafuta ufumbuzi wa changamoto za TBA kama uhaba wa fedha, uhaba wa vifaa vya ujenzi na mitambo pamoja na ukosefu wa wataalamu wa kutosha.**

#### 8.2.1.2 Kutokukamilika kwa Uhamisho wa Umiliki wa Nyumba za CDA kwenda TBA – Sh. 54,697,668,000

Nilibaini kuwa TBA ilipokea nyumba 431 zenye thamani ya Sh. 54,697,668,000 kutoka CDA kufuatia amri ya Rais ya kuivunja CDA mnamo tarehe 15 Mei 2017. Hata hivyo, ukaguzi wangu wa hati za viwanja ulibaini nyumba hizi bado zina nyaraka zinazosoma jina la CDA.

Ni maoni yangu kwamba ucheleweshaji wa kuhamisha umiliki wa nyumba hizi kwenda kwa CDA unaweza kuingiza TBA kwenye uwezekano wa kupoteza umiliki wa nyumba 431 endapo itatokea migogoro ya umiliki.

**Ninapendekeza TBA na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuhakikisha upatikanaji wa hati hizi za umiliki ili kuepusha uwezekano wa kuwapo kwa migogoro ya umiliki.**

### 8.2.2 Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA)

Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) ni wakala ambao hutoa huduma za ndege za VIP kwa maafisa wa serikali; pia TGFA inasaidia na kusimamia ndege zote za serikali ya Tanzania. Ukaguzi wa shughuli za TGFA ulibaini mapungufu yafuatayo:

#### 8.2.2.1 Kutokulipwa kwa Tozo za Kukodisha Ndege za Serikali na ATCL - Sh. 71,482,878,617

TGFA iliingia mikataba mitatu na ATCL mnamo tarehe 3 Oktoba 2016, 10 Desemba 2018 na 24 Julai 2018. Mikataba hiyo ya kukodi ndege za serikali: Bombardier Dash 8 – Q400 (ndege nne), Airbus A220-300 (ndege mbili) na Boeing B787-8 (ndege mbili). Kifungu cha 4 na 11.10 cha Makubaliano kilimtaka mkodishaji kulipa kila mwezi tozo ya kodi na fedha ya akiba ya matengenezo katika kiwango maalumu kilichoainishwa. Katika ukaguzi wa makubaliano haya nilibaini kuwa, TGFA ilimtoza ATCL kiasi cha Sh. 79,626,383,417, ikiwa gharama ya kukodi ndege na fedha ya akiba ya matengenezo. Hata hivyo, TGFA ilipokea jumla ya Sh. 8,143,504,800 kutoka ATCL, huku jumla ya Sh. 71,482,878,617 ikiwa haijalipwa mpaka tarehe 30 Juni 2020. Kiasi hicho ambacho hakijalipwa kinajumisha Sh. 28,396,194,200 ya tozo ya kodi na Sh. 43,086,684,417 ya fedha za akiba za matengenezo.

Aidha, licha ya juhudi za TGFA kufuatilia tozo ambazo hazijalipwa, nimebaini kuwa ATCL ilieleza kuwa mazingira ya biashara ya sasa hivi yamesababisha kampuni kupata changamoto ya kulipa viwango vilivyowekwa na mkataba. Kutokana na hilo, nimebaini kuwa TGFA iliwasilisha suala hilo kwa Bodi ya Kumshauri Waziri (MAB). Bodi husika ilielekeza kuwa TGFA, ATCL na wawakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Uchukuzi) wakae pamoja na kupitia tozo hizi.

Ni maoni yangu kuwa, kutokulipwa kwa gharama hizo yenye thamani ya Sh. 71,482,878,617 kunaiweka TGFA katika hatari ya kushindwa kutekeleza matengenezo ya ndege husika kama miongozo ya ndege inavyotaka; hivyo, kupunguza muda wa maisha ya ndege husika na utendaji kazi wake.

**Ninashauri Serikali ihakikishe kwamba ATCL inakuwa na mkakati ambao utasaidia kampuni kulipa gharama iliyobakia ya Sh. 71,482,878,617 na kufanya tathmini ya viwango vya tozo kutoka kwenye mkataba ili kupata viwango sahihi.**

#### 8.2.2.2 Gharama Kubwa ya Matengenezo ya Ndege Isiyofanya Kazi – Sh. 3,916,377,800

Sura ya 14 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma ya 2019 inaainisha kwamba "Kila Afisa Masuuli atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa, mpango wa matengenezo ya mali umeandaliwa na kuzingatiwa. Lengo la mpango wa matengenezo ni kuhakikisha kuwa mali inaendelea kutumika kwa kusudio lililopangwa, utoaji wa huduma, na matumizi mazuri ili kuongeza faida kwa taasisi.

Nilibaini kuwa, TGFA ilitumia jumla ya Sh. 3,916,377,800 kwa hati ya malipo namba 180000234/316, iliyolipwa kwa TIB Corporate Bank mnamo 14 Februari na 26 Aprili 2018 ikiwa gharama za huduma ya matengenezo makubwa ya ndege aina ya Fokker 28-5H-CCM ya mwaka 1978. Hata hivyo, wakati wa ziara yangu kwenye hifadhi ya ndege za Serikali Dar es Salaam mnamo 19 Agosti 2020, nilibaini kuwa ndege hiyo ilikuwa haifanyi kazi na ilikuwa imetelekezwa tangu mwaka 2015. Aidha, niligundua kuwa, TGFA iliwasilisha suala hili kwa Wizara ya Fedha na Mipango ikiomba ifanyike tathmini ya kina juu ya ndege hiyo ili kuweza kuishauri Serikali juu ya uamuzi sahihi wa hatua za kuchukua.

Hata hivyo, ninaona uamuzi wa kuwekeza fedha za walipa kodi zenye thamani ya Sh. 3,916,377,800 kufanya ukarabati mkubwa wa ndege bila ya kufanyika tathmini ya kina ya gharama na faida haukuwa sahihi, na hivyo, kusababisha hasara kwa taifa.

**Ninapendekeza vyombo vya serikali vya kiuchunguzi kupitia mchakato mzima wa matengenezo yanayohusiana na ndege hii na kuchukua hatua kwa wote waliohusika kama ukiukwaji utabainika.**

### 8.2.3 Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)

Wakala ilianzishwa chini ya mamlaka ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 kwa ajili ya kutoa huduma za Umeme, Mitambo na Elektroniki, Huduma za vivuko pamoja na Ukodishaji Mitambo kwa taasisi za serikali na Umma kwa ujumla. Ukaguzi nilioufanya juu ya shughuli za TEMESA niligundua mapungufu yafuatayo:

#### 8.2.3.1 Makusanyo ya Kivuko ambayo Hayajapelekwa Benki na Hayapo Kituoni – Sh. 81,194,650

Katika ukaguzi wa uendeshaji wa TEMESA nilibaini kuwa Kituo cha Kivuko cha Magogoni kilikusanya jumla ya Sh. 5,757,041,950 ikiwa ni tozo za kivuko kwa kipindi kilichoanzia tarehe 1 Julai 2019 hadi 30 Juni 2020. Hata hivyo, kati ya pesa zilizokusanywa, ni Sh. 5,675,847,300 tu ndizo zilizowekwa kwenye akaunti ya Benki inayosimamiwa na Makao Makuu ya TEMESA, ikiacha jumla ya kiasi cha Sh. 81,194,650 kikiwa bado hakijawekwa benki hadi muda wa ukaguzi, tarehe 31 Julai 2020. Aidha, nilibaini kuwa kiasi hicho cha fedha ambacho hakikuwekwa benki pia hakikuwa kwenye himaya ya kituo. Kwa maoni yangu, fedha hizi ambazo hazijawekwa benki kuna uwezekano kwamba zimetumiwa vibaya au kutumiwa katika shughuli zingine. Hii ni kinyume na kanuni ya 60 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka, 2001.

#### 8.2.3.2 Ubadhirifu uliofanywa wa Kufungua Hundi Zilizofungwa na Kuchukua Fedha Taslimu – Sh. 201,008,694.79

Nimebaini tukio linalohusiana na ubadhirifu wa kutoa fedha taslimu kiasi cha Sh. 201,008,694.79 benki kwa kutumia hundi 28 zilizolipwa kuanzia tarehe 1 Julai 2019 mpaka 30 Juni 2020. Ubadhirifu huu ulifanywa na mtumishi asiye muaminifu wa TEMESA akishirikiana na watumishi wa benki mojawapo ya biashara, wakitumia akaunti ya benki ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo zilizopo kwenye benki hiyo. Malipo haya yalihusisha hundi za benki zilizokua zimefungwa na kutolewa kwa ajili ya kulipa kodi ya zuio na kodi nyinginezo kwa Kamishna wa Mapato ya Ndani ambapo zilifunguliwa na kutolewa fedha taslimu, ikiwa ni kinyume na Kanuni ya 159 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inayotaka kila afisa anayesaini hundi ajiridhishe kuwa hundi imeandikwa vizuri na pia, maelezo ya “counterfoil” yanalingana na kwenye hundi husika.

Aidha, nilibaini kuwa TEMESA iliwasilisha suala hilo polisi kwa sababu ubadhirifu huu ulifanyika zaidi ya miaka mitano nyuma. Benki husika imerejesha TEMESA jumla ya Sh. milioni 723 kufidia hasara. Hata hivyo, ni maoni yangu kuwa, ubadhirifu uliobainika unaashiria kuwa udhibiti wa ndani wa TEMESA unaohusiana na usimamizi wa fedha sio mzuri na unaweza kuendelea kuruhusu vitendo vya udanganyifu na kusababisha serikali kupata hasara kubwa ya fedha.

**Ninapendekeza Taasisi za Serikali za Kiuchunguzi kufanya uchunguzi juu ya ukusanyaji wa mapato katika Kituo cha Kivuko cha Magogoni, na kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika ikiwa ukiukwaji wowote utabainika. Aidha, ninapendekeza TEMESA iboreshe mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha mfumo unafanya kazi vizuri katika kuzuia ubadhirifu.**

#### 8.2.3.3 Mfumo Usio Madhubuti wa Tiketi za Kielektroniki Katika Kituo cha Feri cha Magogoni - Sh. 2,594,116,600

TEMESA ilianzisha mfumo wa tiketi za kielektroniki katika Kituo cha Kivuko cha Magogoni mnamo tarehe 22 Juni 2018, ikiwa na lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaohusika na makusanyo ya mapato. Hivyo basi, nilipitia ripoti ya mauzo kwa mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na ripoti ya uhakiki wa tiketi iliyotokana na mfumo na kubaini kuwa TEMESA iliuza jumla ya tiketi 21,447,004 zenye thamani ya Sh. 5,757,048,150. Hata hivyo, ni tiketi 9,122,690 tu zenye thamani ya Sh. 3,162,931,550 ndizo zilizothibitishwa na mashine (scanned) na kuacha jumla ya tiketi 12,324,314 zenye thamani ya Sh. 2,594,116,600 ambazo zilitumika bila ya kuthibitishwa na mashine (not scanned) kama ilivyoelezwa kwenye **Jedwali Na. 55** hapa chini.

**Jedwali Na. 55: Uthibitishaji wa Tiketi za Abiria Nje ya Mfumo**

| Aina | Tiketi zilizotoloewa bila ya kuthibitishwa (a) | Bei ya tiketi (b) | Gharama ya tiketi zilizotoloewa bila ya kuthibitishwa (Sh.) (c) = (a x b) |
|---|---|---|---|
| Watu wazima | 11,802,473 | 200 | 2,360,494,600 |
| Baiskeli | 85,262 | 300 | 25,578,600 |
| Mikokoteni | 22,911 | 1500 | 34,366,500 |
| Watoto chini ya miaka 14 | 254,162 | 50 | 12,708,100 |
| Serikali | 261 | 2000 | 522,000 |
| Mabasi madogo ya watu chini ya 15 | 715 | 3500 | 2,502,500 |
| Pikipiki | 89,146 | 500 | 44,573,000 |
| Wanyama wa kufugwa | 211 | 1000 | 211,000 |
| Mizigo iliyozidi kilo 50 | 1,414 | 500 | 707,000 |
| Mizigo isiyozidi kilo 50 | 2,473 | 200 | 494,600 |
| Pikipiki ya magurudumu matatu ya abiria | 9,038 | 1300 | 11,749,400 |
| Pick-ups iziyozidi tani 1.5 | 261 | 2000 | 522,000 |
| Magari madogo | 30,458 | 1500 | 45,687,000 |

| Aina | Tiketi zilizotoloewa bila ya kuthibitishwa (a) | Bei ya tiketi (b) | Gharama ya tiketi zilizotoloewa bila ya kuthibitishwa (Sh.) (c) = (a x b) |
|---|---|---|---|
| Magari ya wastani | 23,853 | 2000 | 47,706,000 |
| Trekta yenye behewa | 6 | 7500 | 45,000 |
| Trekta bila behewa | 482 | 7500 | 3,615,000 |
| Pikipiki ya matairi matatu | 1,101 | 1800 | 1,981,800 |
| Magari yaliyobeba abiria zaidi ya 15 mpaka 29 | 87 | 7500 | 652,500 |
| **Jumla** | **12,324,314** | | **2,594,116,600** |

*Chanzo: Taarifa ya mauzo na taarifa ya ukaguzi wa tiketi*

Ni maoni yangu kuwa, TEMESA itashindwa kukusanya na kuharibu tiketi zilizotolewa kwa wasafiri ambazo hazijadhibitishwa kutokana na foleni na hivyo, kutoa nafasi kwa tiketi hizo kutumika tena na kusababisha serikali kupoteza mapato. Pia, kuna hatarishi ya tiketi ambazo hazijadhibitishwa zilizokusanywa kutoka kwa wateja kuuzwa tena na wafanyakazi wasio waaminifu kwa ajili ya manufaa binafsi.

**Kwa hiyo, ninapendekeza TEMESA itathmini mfumo wa ukaguzi wa tiketi (scanning machines) na kuhakikisha kuwa mashine hizo zinafanya kazi kwa kiwango cha juu katika kukagua tiketi zilizotolewa ili kuondoa hatari ya kupoteza mapato.**

### 8.2.4 Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)

Wakala ulianzishwa ili kutengeneza, kudumisha na kusimamia mtandao wa barabara kuu na za mikoa kwa gharama nafuu, salama na mazingira endelevu sambamba na mkakati wa kupunguza umaskini na sera nyingine za Serikali kupitia nguvu kazi yenye uwezo na motisha. Katika ukaguzi wa TANROADS nilibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi wa miradi ya ujenzi wa barabara kama ilivyoainishwa hapa chini:

**(a) Kutokukatwa kwa Tozo ya Ucheleweshaji Kazi Katika Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Makutano - Natta (Sanzate) (50 km): Kipande cha 1 – Sh. 5,459,428,648.81**

TANROADS iliingia kwenye mkataba namba: TRD/HQ/1032/2012/13 mnamo tarehe 5 Aprili 2013 na M/s Mbutu Bridge JV Contractors, kwa ajili

ya ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta (Sanzate) (km 50 km) kwa bei ya kandarasi ya Sh. 54,594,286,488.06 (Bila kodi ya ongezeko la thamani). Muda wa mkataba ulipangwa kumalizika tarehe 16 Mei 2015 lakini uliongezwa mpaka tarehe 28 Februari 2019. Hata hivyo, nilibaini kuwa kazi za ujenzi hazikuwa zimekamilika wakati wa ukaguzi mnamo tarehe 18 Novemba 2020, huku muda wa mkataba ukiwa umemalizika tangu tarehe 28 Februari 2019 bila ya kuongezwa.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kazi za ujenzi hazikuwa zimekamilika wakati wa ukaguzi mnamo tarehe 18 Novemba 2020, huku muda wa mkataba ukiwa umemalizika tangu tarehe 28 Februari 2019 bila ya kuongezwa. Aidha, nilibaini TANROADS haijamkata mkandarasi tozo ya kuchelewesha mradi kinyume na Kifungu cha 22 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC) kinachotaka mkandarasi akatwe asilimia 0.1 ya gharama ya mkataba kwa siku kama tozo ya ucheleweshaji wa kazi, ambapo mradi huu ulichelewa kukamilika kwa siku 629 mpaka wakati wa ukaguzi. Aidha, Kifungu cha 23 cha SCC kimeweka kiwango cha juu cha tozo ya ucheleweshaji wa kazi kuwa ni asilimia 10 tu ya gharama ya mkataba, sawa na Sh. 5,459,428,648.81 (10% x Sh. 54,594,286,488.06). Ni maoni yangu kuwa, kutokana na mradi huu kuchukua zaidi ya miaka minane bila ya kukamilika umeongeza mzigo mkubwa kwa walipa kodi kutokana na kuongezeka kwa gharama maradufu.

**Kutokana na hayo hapo juu, ninapendekeza TANROADS kukomboa tozo ya ucheleweshaji wa kazi yenye thamani ya Sh. 5,459,428,648.81 kutoka kwa mkandarasi ili kufidia gharama za ziada ambazo Serikali imeingia kutokana na mradi huu kuchelewa kukamilika. Pia, napendekeza TANROADS imsimamie mkandarasi vizuri ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.**

### (b) Kuanza kwa Ujenzi wa Daraja la Kigogo – Busisi Bila ya Kuwapo kwa Cheti cha Tathmini ya Athari ya Mazingira

Kifungu cha 81 (3) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ya mwaka 2004, kinataja kuwa kibali au leseni ya utekelezaji wa mradi wowote au utekelezaji unaotokana na matakwa ya sheria yoyote haitamwezesha mtekelezaji au muanzilishi kutekeleza au kusababisha utekelezaji mradi au shughuli bila ya kuwa na Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira kinachotolewa na Sheria hii. Aidha, Kifungu cha 81 (4) kinataja kwamba, mtu yeyote atakayekiuka kifungu kidogo cha 3 atakuwa ametenda kosa.

TANROADS iliingia kwenye mkataba namba: TRD/HQ/1006/2019/20 mnamo tarehe 29 Julai 2019 na M/s China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) akiungana na M/s China Railway 15 Bureau Group Corporation (CR15G), kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Kigogo – Busisi (mita 3200) na barabara mbadala (km 1.66) kwa bei ya kandarasi ya Sh. 592,608,692,836 (Bila kodi ya ongezeko la thamani). Muda wa mkataba ulipangwa kumalizika tarehe 24 Februari 2024.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kazi za ujenzi zilianza mnamo tarehe 25 Februari 2020 bila ya kuwapo kwa Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira kinachotolewa na NEMC ambapo ni kinyume na sheria tajwa hapo juu. Aidha, TANROADS ilikuwa bado hajapokea cheti hicho kutoka NEMC mpaka muda wa ukaguzi Desemba 2020. Ni maoni yangu kuwa TANROADS kutopata cheti cha athari ya mazingira kinaongeza hatarishi ya mradi kuathiri vibaya mazingira, na Wakala inaweza kuingia kwenye gharama za ziada ikiwa itatozwa faini na NEMC kwa kosa lililofanyika kinyume na Kifungu 81 (4) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka, 2004.

**Ninapendekeza TANROADS kufuata Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kwa kuhakikisha miradi ya ujenzi wa barabara utekelezaji wake unaanza pale tu baada ya kupata Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira kutoka NEMC. Pia, ninapendekeza NEMC ifanye tathmini ya athari ya mazingira kwenye mradi huu iliyosababishwa na utekelezaji wa mradi bila Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira.**

**(c) Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Mkataba wa Huduma ya Ushauri ya Upembuzi wa Udongo na Miamba, Usanifu wa Kina wa Kihandisi na Matayarisho ya Makabrasha ya Zabuni ya Hatua za Kuzuia Mafuriko katika Bonde la Jangwani – Dola za Marekani 905,123.95**

TANROADS iliingia kwenye mkataba mnamo tarehe 22 Januari 2019 na M/s Delters na M/s Wema Consultants, kwa ajili ya huduma ya ushauri ya Upembuzi wa Udongo na Miamba, Usanifu wa Kina wa Kihandisi na Matayarisho ya Makabrasha ya Zabuni juu ya hatua za kuzuia mafuriko katika bonde la Jangwani kwa bei ya ushauri ya Dola za Marekani 478,339.50, iliyoongezwa mpaka Dola za Marekani 905,123.95. Muda wa

mkataba ulipangwa kumalizika tarehe 22 Juni 2019 lakini uliongezwa mpaka tarehe 9 Desemba 2020.

Ukaguzi niliofanya kwenye mkataba huu umebaini kuwa huduma ya ushauri kwa hatua ya kwanza ambayo ni upembuzi yakinifu ulikamilika mnamo tarehe 20 Novemba 2019. Taarifa hii ya upembuzi yakinifu ilipendekeza hatua kadhaa kuchukuliwa kwenye eneo husika kama kuchimba mkondo mpana na kuongeza kina cha mto, kufanya kazi za muda za kulinda kituo cha mabasi, kujenga daraja jipya la nguzo na kuhamisha kituo cha mabasi ya mwendokasi ndani ya kipindi cha miaka mitatu, kitendo ambacho kiliifanya TANROADS kumwagiza mshauri kuanza hatua ya pili ya usanifu wa hatua zilizopendekezwa na mshauri kwa makubaliano ya nyongeza ya kazi (addendum) ya tarehe 9 Juni 2020.

Hata hivyo, nilibaini kasi ndogo ya utekelezaji wa mkataba huu wa huduma ya ushauri ambapo ripoti ya mwisho ya usanifu, tathmini ya mazingira na makabrasha ya zabuni ambazo zilikuwa na muda wa kuwasilishwa wa tarehe 9 Desemba 2020 hazikuwa zimewasilishwa mpaka muda wa ukaguzi tarehe 16 Desemba 2020.

Kwa maoni yangu, kuchelewa kukamilika kwa mkataba wa huduma ya ushauri kunaathiri kufanyika kwa manunuzi ya mkataba wa ujenzi wa hatua za kudumu zilizopendekezwa, huku eneo husika lina tabia ya kukumbwa na mafuriko ya mara kwa mara. Aidha, ucheleweshaji unaongeza hatari ya TANROADS kuingia kwenye gharama za kusafisha eneo ili kupunguza maji yaliyofurika. Huko nyuma, TANROADS iliingia gharama ya Sh. 2,4,56,276,080 kwa ajili ya kufanya kazi za haraka za kusafisha na kuondoa uchafu kwenye bonde la mto msimbazi.

**Ninapendekeza TANROADS imsimamie vizuri mshauri ili kuhakikisha huduma ya usanifu inakamilika kwa wakati na hivyobasi, kuwezesha serikali katika kubajeti na kutoa fedha za utekelezaji wa hatua za kudumu katika eneo husika.**

**(d) Uchepushaji Usioridhisha wa Fedha za Miradi - Sh. 3,619,633,562**

Sura ya 7.1 ya Kanuni za Wakala Tendaji (Wakala wa Barabara Tanzania) (Uanzishwaji) (iliyorekebishwa mwaka 2020) inataja kwamba, Matumizi ya TANROADS yanatakiwa yaendane na mpango wa biashara ulioidhinishwa na

Katibu Mkuu na kwa namna ambayo itawezekana kuhusisha matumizi yote na vyanzo vya fedha na sababu ya matumizi ya pesa.

Nimebaini kuwa fedha za miradi zenye thamani ya Sh. 3,619,633,562 zilichepushwa kutoka kwenye kusudi la miradi husika kwenda miradi mingine kwa matumaini kwamba, fedha hizo zingerudishwa pale tu TANROADS angepokea fedha za miradi hiyo kutoka Hazina. Hata hivyo, nilibaini fedha hizo zilizochepushwa hazikuwa zimerudishwa mpaka muda wa ukaguzi, Novemba 2020. Kwa maoni yangu, uchepushaji huu wa fedha unaongeza uwezekano wa utekelezaji usioridhisha wa miradi iliyopangwa kwa sababu fedha za kutekeleza miradi husika zitakosekana pale zinapohitajika.

**Ninapendekeza TANROADS ielekeze fedha zilizoidhinishwa kwenye miradi husika na kufuata utaratibu sahihi wa kupata idhini ikiwa kuna hitaji la kuhamisha fedha za mradi.**

### 8.2.5 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

Lengo la TARURA ni kufanya matengenezo endelevu na gharama nafuu na maendeleo ya Mtandao wa Barabara Vijijini na Mijini ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi ya kijamii nchini Tanzania. Katika ukaguzi wa TARURA nimebaini mapungufu yafuatayo:

#### 8.2.5.1 Kumpatia Mkataba Mzabuni Asiyekidhi Vigezo - Sh. 1,179,910,730

Kanuni Na 204 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inataja kwamba: ukiukwaji wa masharti ya kibiashara unaohalalisha zabuni kukataliwa ni pamoja na yafuatayo: (b) kushindwa kukidhi matakwa ya uhalali wa zabuni na; (k) kushindwa kuwasilisha nyaraka muhimu zinazohitajika kwenye kabrasha la zabuni ili kuweza kutathmini zabuni iliyokidhi vigezo kwa kiwango kikubwa kama ilivyoelezewa kwenye masharti ya zabuni.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa TARURA ilimpatia mikataba mitatu yenye thamani ya Sh. 1,179,910,730 mzabuni aliyeshindwa kukidhi vigezo vya uhalali wa zabuni na hakuwasilisha nyaraka muhimu za kuwezesha kufanyika kwa tathmini ya zabuni. Maelezo ya mapungufu yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 56:**

**Jedwali Na. 56: Mikataba Aliyopatiwa Mzabuni Ambaye Hajakidhi Vigezo**

| Maelezo ya Zabuni | Bei ya zabuni (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|
| Mkataba wa kuboresha barabara ya mji wa Nzega kwa kiwango cha Lami (AE/092/2019/2020/TBR/W/48) mkataba alipewa M/s Baclema Company Ltd | 492,411,810 | TDS Sharti Na. 19 linataka mzabuni awe na vigezo vifuatavyo:<br>• Awe na fedha za kutosha zisizopungua Sh. 200 milioni; na,<br>• Awe na taarifa ya benki kutoka taasisi ya fedha inayotambulika<br>Hata hivyo, mzabuni aliwasilisha taarifa ya benki iliyo na kiasi hasi cha Sh. 99 milioni kinyume na sharti lililotajwa hapo juu. |
| Ujenzi wa daraja na barabara mbadala za Nhobola iliyopo barabara ya Kitangiri - Mbogwe - Nhele (AE/092/2019/2020/TBR/W/81) mkataba alipewa M/s Baclema Company Ltd | 487,499,000 | TDS Sharti Na. 3.1 linataka mzabuni awe amesajiliwa kama kampuni ya kihandisi daraja V na Zaidi. Hata hivyo, TARURA ilmpatia kazi mzabuni aliyesajiliwa kama mhandisi daraja la VI, chini ya masharti ya TDS. |
| Ujenzi wa makalvati ya mduara kwenye barabara ya Isanga-Lusu - Choma cha Nkola (AE/092/2019/2020/TBR/Q/W/05) mkataba alipewa M/s Baclema Company Ltd | 199,999,920 | TDS Sharti Na. 19 linataka mzabuni awasilishe uthibitisho wa kuwa na fedha zizisopungua Sh. 88 milioni kwa njia ya taarifa za benki au makubaliano ya mkopo kutoka taasisi ya fedha inayotambulika.<br>Mbali na hivyo, TARURA ilimpatia mkataba kwa mzabuni aliyeonesha mkopo wa benki wa Sh. 88 milioni bila ya uthibitisho wa makubaliano na benki kinyume na TDS hapo juu. |
| **Jumla** | **1,179,910,730** | |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa maejimenti ya TARURA*

Ni maoni yangu kwamba, kumpatia mkataba mzabuni ambaye hajakidhi vigezo, kunaongeza hatarishi la kufanya ununuzi wa Wakandarasi wasio na uwezo hivyo, kusababisha kazi kukosa ubora na kupata hasara ya thamani halisi ya fedha kwenye miradi husika.

**Kutokana na mapungufu yaliyotajwa hapo juu, Napendekeza TARURA kuhakikisha Sheria za Ununuzi na Kanuni zake zinafuatwa.**

### 8.2.5.2 Miradi ya Barabara Iliyotelekezwa - Sh. 1,959,810,460

Kanuni ya 243 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inataka kwamba: kwa mikataba ya ujenzi na huduma, taasisi za manunuzi zinatakiwa kufuatilia utendaji kazi wa mkandarasi ili uendane na mpango wa kazi uliotajwa kwenye mkataba kwa kufuatilia taarifa za siku, wiki, au mwezi kutoka kwa msimamizi wa mradi kutoka katika taasisi ya manunuzi.

Kwenye ukaguzi wangu wa usimamizi wa miradi, nimebaini kuwa miradi ya ujenzi wa barabara yenye thamani ya Sh. 1,959,810,460 imetelekezwa na wakandarasi mbalimbali kabla ya kukamilika. Pia, nimebaini kuwa sababu kuu ya tatizo hili ni kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi pamoja na usimamzi usioridhisha wa miradi kama ilivyoelezwa kwenye **Jedwali Na. 57**:

**Jedwali Na. 57: Miradi Iliyotelekezwa**

| Maelezo ya mkataba | Gharama ya mkataba (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|
| Mkataba wa kuboresha barabara ya mji wa Nzega kwa kiwango cha Lami (AE/092/2019/2020/TBR/W/48)) | 492,411,810.00 | Mkandarasi alitelekeza mradi mnamo Septemba 2020 kutokana na kutolipwa kiasi cha Sh. 344,388,000 |
| Ujenzi wa daraja na barabara mbadala za Nhobola iliyopo barabara ya Kitangiri - Mbogwe - Nhele (AE/092/2019/2020/TBR/W/81) | 487,499,000.00 | Mkandarasi ametelekeza mradi huku kazi zenye thamani ya Sh. 35,660,000 zikiwa hazijafanyika. |
| Uboreshaji wa barabara ya mji wa Mugumu (1.0KM) kwa matabaka mawili ya lami (DBSD) AE/092/2019-2020/MAR/W/45 | 496,856,650.00 | Wakandarasi wametelekeza hii miradi kwa kutokulipwa |

| | | |
|---|---|---|
| **Uboreshaji wa barabara ya Nyankanga-Nyakatende kwa kiwango cha lami (1.0KM) (AE/092/2019-2020/MAR/W/43)** | 483,043,000.00 | |
| **Jumla** | **1,959,810,460.00** | |

**Chanzo:** Barua ya mapungufu kwa TARURA

Kutokana na hayo yaliyotajwa hapo juu, kuna uwezekano wa kuongeza mzigo kwa walipa kodi kutokana na ongezeko la gharama ya miradi husika, pamoja na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara.

**Kwa hivyo, ninapendekeza TARURA kuhakikisha utekelezaji wa miradi hii unaanza na kukamilika kwa wakati kwa kuhakikisha wakandarasi wanalipwa katika muda muafaka. Pia, kuwaongezea wafanyakazi ujuzi wa usimamizi wa miradi.**

### 8.2.6 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFSA)

Wakala imeundwa kwa madhumuni ya kuhakikisha: Kuwapo kwa usimamizi madhubuti na wenye ufanisi na tija wa rasilimali za misitu na nyuki; kuongeza ubora na thamani ya kifedha katika kutoa huduma kwa umma; na kuendelea kukuza na kuboresha uwezo wa kutoa huduma kwa umma. Katika ukaguzi wa shughuli za TFSA nilibaini mapungufu yafuatayo:

#### 8.2.6.1 Uchimbaji wa Madini katika Hifadhi ya Misitu Bila Kibali - Sh. 614,153,600

Kanuni Na 33 (1) ya Kanuni za Udhibiti wa Misitu ya mwaka 2004 inataja kwamba hakuna mmiliki wa leseni ya madini au leseni ya kutafuta madini atastahili kuingia sehemu yoyote ya hifadhi ya msitu katika eneo lolote la nchi, au la mitaa kwa shughuli za uchimbaji madini au utafutaji wa madini isipokuwa awe amepewa kibali na Mkurugenzi au Afisa Mkuu Mtendaji kwa sababu hiyo. Aidha, kanuni ya 33 (2) imetaja kwamba hakuna mtu atakayechukua au kuondoa miamba, mawe, na mchanga isipokuwa ana kibali kilichotolewa na Mkurugenzi kwa sababu hiyo.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa kampuni inayoitwa M/s Ward Investment Company Ltd inaendesha mashine ya kuchimba na kusaga miamba kwa ajili ya kufanya biashara katika Hifadhi ya Msitu ya Chigongwe tangu mwaka 2002, bila kuwa na kibali kutoka kwa TFSA, kinyume na kanuni iliyoelezwa hapo juu. Aidha, niligundua pia kuwa kampuni hiyo ina leseni ya madini kutoka Wizara ya Madini, ambapo leseni

hiyo ni moja ya sharti la kuomba kibali kutoka TFSA. Hata hivyo, Kampuni ya M/s Ward Investment Company Ltd ilishindwa kuomba kibali kutoka TFSA; hivyo, kukosa kigezo cha kuendesha shughuli za uchimbaji katika Hifadhi ya Misitu ya Chigongwe kwa miaka 18. Tatizo hili linaleta wasiwasi kuhusu ni jinsi gani limeachwa kuendelea bila kuthibitiwa kwa miaka 18.

Maoni yangu ni kuwa uchimbaji katika hifadhi ya msitu bila kibali umeinyima TFSA mapato ya miaka 18 yenye thamani ya Sh. 614,153,600 kwa sababu ya kutokukusanywa kwa ushuru uliotajwa chini ya Kanuni ya 29 (1) ya Udhibiti wa Misitu, 2004 (marekebisho ya mwaka 2017). Pia, nina wasiwasi juu ya hali ya mazingira katika eneo hilo. Hii ni kwa sababu ya ukosefu wa mpango wa usimamizi wa mazingira, ambao ni muhimu katika kuhakikisha utunzaji wa mazingira.

**Ninapendekeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara ya Madini na Mamlaka ya Mapato Tanzania na NEMC kutathmini tozo zote zinazohitajika kukusanywa kutoka kwa mwekezaji huyu, pia, kuhakikisha tathmini inafanyika juu ya athari ya mazingira ya eneo husika.**

### 8.2.7 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)

Malengo ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ni kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kugawa kiba ya chakula kwa ufanisi na tija. Nimepitia shughuli za NFRA na kubaini mapungufu yafuatayo:

#### 8.2.7.1 Kutolipiwa kwa Gharama ya Chakula Kilichotolewa kwa Ajili ya Kukabiliana na Janga la Njaa na Maafa - Sh. 167,376,994,882.48

Wakati wa ukaguzi wa Wakala, niligundua kuwa kutoka mwaka 2007/08 hadi mwaka 2018/19, NFRA ilitoa tani 365,779.549 za mahindi zenye thamani ya Sh. 167,376,994,882.48 kwa Ofisi ya Waziri Mkuu ili kukabiliana na baa la njaa na majanga yaliyotokea katika maeneo tofauti ya nchi. Hata hivyo, nilibaini kuwa hadi wakati wa ukaguzi wangu mnamo mwezi Novemba 2020, Ofisi ya Waziri Mkuu (Idara ya Usimamizi wa Maafa) ilikuwa haijalipia gharama ya chakula kilichotolewa na NFRA kwa kipindi kinachokaribia mwaka mmoja hadi miaka 12 . Uchambuzi wa gharama ya mahindi yaliyotolewa na NFRA inaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 58:**

**Jedwali Na. 58: Gharama za Usambazaji wa Mahindi Ambazo Hazijalipwa na Waziri Mkuu**

| Kipindi | Tani | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2007/08 to 2014/15 | 364,304.549 | 166,447,544,945.82 |
| 2016/17 | 1,275.000 | 828,750,000 |
| 2018/19 | 200.000 | 100,699,936.66 |
| **Jumla** | **365,779.549** | **167,376,994,882.48** |

**Chanzo:** Barua ya mapungufu kwa menejimenti ya NFRA

Ni maoni yangu kwamba, kutokufidiwa kwa gharama ya chakula kilichotolewa kunaweza kuathiri uwezo wa NFRA wa kununua na kuhifadhi chakula cha kutosha kwa akiba ya taifa. Pia, kupelekea serikali kushindwa kukabiliana na majanga ikiwa janga la njaa litatokea.

**Ninashauri Wizara ya Fedha na Mipango iandae mpango wa uhakiki wa deni hili ili kubaini uhalali wake na kuishauri Serikali juu ya njia bora itakayohakikisha huduma iliyotolewa inafidiwa kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya madeni.**

### 8.2.8 Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)

Malengo ya GCLA ni Kutoa huduma bora za kimaabara na zenye gharama nafuu na udhibiti kwa serikali,taasisi,asasi na umma kwa ujumla kwa madhumuni ya kulinda afya ya binadamu na mazingira. Katika ukaguzi wa shughuli za GCLA nilibaini mapungufu yafuatayo:

#### 8.2.8.1 Malimbikizo Yasiyolipwa ya Ada za Uchunguzi wa Kimaabara - Sh. 10,052,727,912.94

Kifungu cha 36 (3) cha Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Kemia ya Serikali ya mwaka 2016 inasema, ada na tozo za huduma zinazotolewa kwa sampuli au vielelezo vinavyohusiana na maswala ya jinai, majanga, ulinzi na usalama au sampuli nyingine yoyote yenye maslahi ya umma yanatakiwa kugharimiwa na serikali.

Nilibaini kuwa GCLA ilifanya vipimo kadhaa vya kiuchunguzi kuhusu sampuli zinazohusiana na maswala ya uhalifu, majanga, ulinzi na usalama kwa niaba ya Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai pamoja na Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevya. Kutokana na

kazi hiyo, GCLA iliwasilisha madai ya Sh. 10,052,727,917.94 kwa taasisi hizo za kiuchunguzi ambapo hadi muda wa ukaguzi wangu hapo Desemba 2020, madai hayo ya GCLA yalikuwa bado kulipwa. Maelezo ya taasisi zenye madeni yameoneshwa **Jedwali Na. 59:**

**Jedwali Na. 59: Malimbikizo Yasiyolipwa ya Ada za Uchunguzi wa Kimaabara**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai | 10,038,424,928.94 |
| 2 | Mamlaka kuzuia na kupambana na dawa ya kulevya | 14,302,984.00 |
| **Jumla** | | **10,052,727,912.94** |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejiment*

Ni maoni yangu kwamba, kukosekana kwa mpango mkakati wa kukusanya madai haya, kunaweza kusababisha hatari ya kuathiri utoaji wa huduma wa Wakala; hivyo, kupelekea kuathiri taasisi za serikali na wananchi wanaotegemea huduma za GCLA.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha madeni haya ya taasisi za kiuchunguzi yanalipwa ili kusaidia GCLA katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, pamoja na kuandaa mkakati utakaohakikisha huduma iliyotolewa inalipwa kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya madeni.**

## 8.3 Masuala Mtambuka Yanayohusu Wakala za Serikali

Wakati wa ukaguzi wa Wakala Tendaji, niliona masuala mtambuka kadhaa ambayo yalibainika katika Wakala mbali mbali na kwa sababu ya umuhimu wake yanahitaji kuripotiwa kwa umma kama ninavyoeleza hapa chini:

### 8.3.1 Kutokulipwa kwa Madeni ya Wakandarasi, Wahandisi Washauri, na Wasambazaji - Sh. 783,392,176,735.35

Kifungu cha 54 cha GCC kinasema kuwa: Mwajiri atamlipa Mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na Meneja wa Mradi ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kila hati ya muda ya malipo. Mwajiri akichelewesha malipo, Mkandarasi atalipwa riba ya kuchelewesha malipo katika hati ya malipo inayofuata. Aidha, Kifungu cha 19.3 cha GCC kinataja kwamba Malipo yatafanywa na taasisi ya manunuzi, ndani ya siku sitini (60) baada ya msambazaji

kuwasilisha madai. Ikiwa taasisi ya manunuzi itachelewesha malipo, Msambazaji atalipwa riba ya kuchelewesha malipo.

Nilibaini kuwa Wakala nne za Serikali zilikuwa na madai ya malipo ya Sh. 783,392,176,735.35 kutoka kwa wakandarasi, washauri na watoa huduma kinyume na vifungu vilivyotajwa hapo juu. Kwa umuhimu wake, TANROADS ilikuwa na deni[7] kubwa lenye thamani ya Sh. 770,119,541,338.75 kutoka kwa wakandarasi na washauri kutokana na kuchelewa kupata fedha za kutekeleza miradi kutoka Hazina. Maelezo yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 60** hapa chini.

**Jedwali Na. 60: Malipo Yaliyochelewa Kulipwa ya Wakandarasi, Washauri na Wasambazaji**

| Wakala | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | Madai ambayo hayajalipwa ya wakandarasi na washauri | 770,119,541,338.75 |
| Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | Madai ambayo hayajalipwa ya wasambazaji wa vifaa vya ujenzi | 1,144,426,032.65 |
| Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) | Madai ambayo hayajalipwa ya wakandarasi na washauri | 12,002,403,927.95 |
| Wakala Wa Barabara Za Vijijini Na Mijini (TARURA) | Madai ambayo hayajalipwa ya wakandarasi na washauri | 125,805,436.00 |
| **Jumla** | | **783,392,176,735.35** |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Ni maoni yangu kwamba, ucheleweshaji wa kulipa madai haya kunaongeza hatari ya kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na riba inayotozwa kwenye malipo yaliyochelewa na kwa hivyo kuongeza mzigo wa gharama kwa walipa kodi.

**Ninarudia mapendekezo yangu ya mwaka uliopita kwamba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuja na mikakati ambayo itahakikisha madeni yanalipwa pale tu muda ulioruhusiwa kimkataba unapofika. Pia, Serikali inapaswa kuzingatia ulipwaji wa madeni yaliyopo kabla ya kuamua kuingia kwenye mikataba mipya. Aidha,**

[7] TANROADS ilikua na deni la Sh. 624,677,604,000 lililoripitiwa katika taarifa za fedha zinazoishia tarehe 30 Juni 2020, kati ya deni hilo, Sh. 593,785,965,000 ni deni linalotokana na madai ya wakandarasi na washauri. Hatahivyo, mpaka wakati wa ukaguzi tarehe 16 Novemba 2020, madeni ya wakandarasi na washauri yaliongezeka mpaka Sh. 770,119,541,338.75, ikiwa ni ongezeko la Sh. 176,333,576,338.75 (30%) kwa muda wa miezi minne.

**ninapendekeza TBA ilipe watoa huduma kwa wakati ili kuepusha changamoto ya ukosefu wa vifaa vya ujenzi kwenye maeneo ya ujenzi ambayo yanakwamisha shughuli za ujenzi.**

### 8.3.2 Fedha za Wakala Tendaji Zilizotaifishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania – Sh. 66,834,646,659.16

Kifungu cha 59 cha Sheria ya usimamizi wa kodi (Toleo 439 iliyorekebishwa mwaka 2019) inataja kwamba: ikiwa (a) malipo ya kodi hayajafanyika kwenye siku au baada ya siku ya mwisho ya kuwasilisha malipo; au (b) notisi iliyotolewa kwa mtu aliyetajwa kwenye kifungu cha 81 haijatekelezwa, kiasi cha kodi ambayo hakijalipwa kitakombolewa kwa njia ya mahakama ya ndani ya nchi. Aidha, Kifungu cha 67 (1) kinataja kuwa ikiwa mlipa kodi kashindwa kulipa kwa muda, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato atakomboa kiasi husika kwa kumwandikia mdai ambaye anadaiwa na mlipa kodi kwa notisi ya maandishi akimtaka mtu huyo alipe fedha hizo kwa Kamishna Mkuu.

Kwa kuzingatia hilo, nilibaini kuwa TRA ilifanya tathmini ya kodi kwa Wakala tatu za Serikali kwa muda maalumu na kugundua kuwapo kwa malimbikizo kadhaa ya kodi ambayo yalisababisha TRA kutaifisha Sh. 66,834,646,659.16 kutoka kwenye akaunti za benki za Wakala husika. Kwa maelezo angalia **Jedwali Na. 61** hapa chini.

**Jedwali Na. 61: Wakala ambao Fedha Zao Zimetaifishwa na TRA**

| Na | Wakala | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Vipimo (WMA) | 831,075,974.00 | TRA ilitaifisha kiasi tajwa kutokana na kutokulipwa kwa kodi ya malipo kadiri ya kipato (PAYE) yenye thamani ya Sh. 4,323,778,677 (pamoja na riba za kuchelewesha malipo) |
| 2 | Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | 62,114,587,854.66 | TRA ilitaifisha kiasi tajwa kutokana na kutolipwa kwa kodi ya ongezeko la thamani yaliyotokana na malipo ya mkandarasi wa ujenzi wa jengo la abiria III katika Kiwanja cha kimataifa cha Mwalimu Nyerere. |
| 3 | Wakala wa Majengo Tanzania | 3,888,982,830.50 | TRA ilitaifisha kiasi tajwa kwa sababu ya kutokulipwa kwa kodi ya ujuzi (SDL), kodi ya malipo kadiri ya |

| Na | Wakala | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | (TBA) | | kipato (PAYE), na kodi ya zuio zenye thamani ya Sh. 6,986,794,187. |
| | **Jumla** | **66,834,646,659.16** | |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Ni maoni yangu kuwa kasoro zilizojitokeza zinahusiana na uelewa mdogo wa sheria za kodi, pamoja na kutotolewa kwa fedha za kutekeleza miradi na Hazina.

**Ninapendekeza Wakala kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanaohusika na masuala ya kodi wanapewa ujuzi wa kutosha juu ya sheria za usimamizi wa kodi. Pia, napendekeza serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kutafuta njia ambazo miradi mikubwa ya ujenzi itapewa msamaha wa kodi ili kulinda maslahi ya kitaifa.**

### 8.3.3 Usimamizi Usioridhisha wa Dhamana za Mikataba - Sh. 35,145,710,896.75

Kifungu kidogo cha 60.1 cha GCC kinataka mkandarasi awasilishe dhamana ya utendaji kazi kabla ya tarehe iliyoelezwa kwenye barua ya kukubali kazi na dhamana hiyo ikiwa ni ya benki, inatakiwa iwe halali mpaka siku 28 kutoka siku ya kutolewa kwa cheti cha kumaliza kazi; na kwa dhamana ya bima inatakiwa iwe mwaka mmoja baada ya kutolewa kwa cheti cha kumaliza kazi.

Aidha, Kifungu Kidogo cha 59.1 cha GCC kinataka mwajiri afanye malipo ya awali kwa mkandarasi kwa kiasi kilichotajwa kwenye Masharti Maalum ya Kimkataba pale tu mkandarasi atakapo wasilisha dhamana ya benki isiyokuwa na masharti, na dhamana hiyo inatakiwa iwe halali mpaka muda ambapo malipo hayo ya awali yatakombolewa, lakini gharama za dhamana zitaendeleaa kupungua kwa kiasi kitakacholipwa na mkandarasi.

Hata hivyo, ukaguzi wangu wa shughuli za Wakala Tendaji umebaini kuna usimamizi usioridhisha wa dhamana zenye thamani ya Sh. 35,145,710,896.75 kama inavyoelezewa hapo chini:

- Nimebaini Wakala tatu zilitekeleza miradi ya ujenzi bila ya kuwapo kwa dhamana ya utendaji yenye thamani ya Sh. 25,701,247,154.35, kinyume na Kifungu 60.1 cha GCC.
- Niligundua kwamba, wakala nne zilifanya malipo ya awali yenye thamani ya Sh. 9,444,036,368.80 kwa wakandarasi na washauri ili

kusaidia katika ujenzi. Hata hivyo, malipo hayo ya awali hayakuwa na dhamana ya kibenki kinyume na Kifungu 59.1 cha GCC. Jedwali hapo chini linaonesha Wakala ambazo zinatekeleza miradi bila ya dhamana.

**Jedwali Na. 62: Wakala Ambao Zinatekeleza Miradi Bila ya Dhamana**

| Na | Wakala | Dhamana za utendaji (Sh) (a) | Dhamana za malipo ya awali (Sh.) (b) | Jumla (c) = a + b |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | 12,584,887,052.00 | 9,192,035,264.00 | 21,776,922,316.00 |
| 2 | Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | | 153,000,000.00 | 153,000,000.00 |
| 3 | Wakala wa Huduma za Misitu (TFSA) | | 49,001,104.80 | 49,001,104.80 |
| 4 | Wakala Wa Barabara Za Vijijini Na Mijini (TARURA) | 781,075,885.55 | 50,000,000.00 | 831,075,885.55 |
| 5 | Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) | 12,335,711,590.40 | | 12,335,711,590.40 |
| | **Jumla** | **25,701,674,527.95** | **9,444,036,368.80** | **35,145,710,896.75** |

**Chanzo:** Barua ya mapungufu kwa menejimenti

Kwa kuzingatia yaliyotajwa hapo juu, nina maoni kwamba usimamizi duni wa dhamana za mikataba unaweza kuzihatarisha Wakala kupata hasara iwapo wakandarasi watashindwa kutekeleza makubaliano ya kimkataba au kutekeleza kazi.

**Kwa hivyo, ninapendekeza Wakala zianzishe udhibiti wa ndani ambao utahakikisha usimamizi wa kutosha wa dhamana za mkataba, vile vile kuhakikisha masharti ya mkataba yanazingatiwa kabla ya kufanya malipo ya awali kwa wakandarasi/washauri.**

### 8.3.4 Wakala wenye Makusanyo ya Mapato ya Ndani Yasiyoridhisha

Kifungu cha 12 (2) (a) cha Sheria za Wakala cha mwaka, 1997 kinazitaka Wakala kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia njia za kisasa za kibiashara, na kuhakikisha kwamba, kwa njia yoyote, mapato yake yanatosha kugharamia matumizi ya Wakala hizo.

Hata hivyo, nilibaini Wakala 12 ambazo zinaendeshwa kibiashara lakini makusanyo ya mapato ya ndani yalikuwa chini sana kwa kiwango cha kuanzia 21% mpaka 83% ikilinganishwa na kiwango cha bajeti. Taasisi zenye makusanyo madogo zimeoneshwa kwenye
**Jedwali** Na. **63** hapa chini.

**Jedwali Na. 63: Wakala wenye Makusanyo ya Mapato ya Nndani Yasiyoridhisha**

| Na. | Wakala | Bajeti (Sh.) (a) | Makusanyo (Sh.) (b) | Makusanyo Pungufu (Sh.) (c)=a-b | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) | 30,127,280,000.00 | 5,032,200,404.00 | 25,095,079,596.00 | 83 |
| 2 | Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) | 2,027,416,251.00 | 522,519,834.00 | 1,504,896,417.00 | 74 |
| 3 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | 48,177,407,717.00 | 18,052,775,556.00 | 30,124,632,161.00 | 63 |
| 4 | Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) | 75,300,000,000.00 | 32,384,065,050.29 | 42,915,934,949.71 | 57 |
| 5 | Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na | 5,956,342,095.00 | 2,592,650,736.00 | 3,363,691,359.00 | 56 |

| Na. | Wakala | Bajeti (Sh.) (a) | Makusanyo (Sh.) (b) | Makusanyo Pungufu (Sh.) (c)=a-b | % |
|---|---|---|---|---|---|
| | Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo (ASA) | | | | |
| 6 | Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini kitengo cha uchimbaji visima, zamani ikijulikana DDCA | 9,487,870,955.00 | 5,194,721,983.00 | 4,293,148,972.00 | 45 |
| 7 | Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TGLA) | 1,330,310,000.00 | 788,937,644.00 | 541,372,356.00 | 41 |
| 8 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | 23,362,507,000.00 | 15,089,241,049.00 | 8,273,265,951.00 | 35 |
| 9 | Chuo cha Maji | 3,231,559,750.00 | 2,188,930,811.00 | 1,042,628,939.00 | 32 |
| 10 | Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 66,459,054,320.00 | 49,399,042,664.00 | 17,060,011,656.00 | 26 |
| 11 | Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi ( (FETA) | 1,500,000,000.00 | 1,128,451,514.00 | 371,548,486.00 | 25 |
| 12 | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) | 62,382,507,082.00 | 49,126,353,737.00 | 13,256,153,345.00 | 21 |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Aidha, ukaguzi wangu umebaini kuwa mapungufu haya yanatokana na mifumo isiyo madhubuti ya makusanyo ya mapato, ukosefu wa kitengo kinachoshughulika makusanyo ya mapato, pamoja na mapungufu kwenye matayarisho ya mchakato wa bajeti. Kwa maoni yangu, ukusanyaji usioridhisha wa mapato unaweza kuathiri shughuli za Wakala na

kusababisha utegemezi usioisha wa ruzuku ya serikali kugharamia shughuli za Wakala hivyo, kuongeza mzigo kwa walipa kodi.

**Ninapendekeza kwa Wizara husika zinasosimamia Wakala hizi kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Bodi za Ushauri (MAB) ili kujiridhisha kama zinafanya wajibu wao wa kutathmini utendaji kazi wa Wakala. Pia, kubuni na kuanzisha njia madhubuti zitakazohakikisha utendaji kazi madhubuti wa Bodi za Ushauri (MAB). Pia, napendekeza kwa Wakala husika kuhakikisha kunakuwa na mfumo madhubuti wa makusanyo, idara maalum inayoshughulikia makusanyo na kuhakikisha ubora kwenye matayarisho ya bajeti.**

## 8.4 Masuala Yaliyobainika Katika Kaguzi za Taasisi Mbalimbali za Serikali

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini masuala muhimu yanayohusiana na taasisi mbalimbali za serikali ambazo yanahitaji kusuluhishwa na serikali pamoja na kujulikana kwa walipa kodi kama inavyoelezewa hapa chini:

### 8.4.1 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ina jukumu la uandikishaji na utoaji wa vitambulisho vya taifa kwa wananchi na wakazi wanaotambulika kisheria. Wakati wa Ukaguzi wa shughuli za NIDA nilibaini mapungufu yafuatayo:

#### 8.4.1.1 Usimamizi Usioridhisha wa Kadi za Kutengenezea Vitambulisho vya Taifa – Sh. 3,399,973,019

Mnamo tarehe 21 Aprili 2011, NIDA iliingia kwenye Mkataba na M/s IRIS Corporation Berhad of Malaysia (Supplier) kwa ununuzi wa bidhaa na vifaa vya utekelezaji wa mfumo wa Kadi za Taifa kwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa gharama ya Dola 149,956,303. Muda wa mkataba uliisha tokea tarehe 14 Machi 2018 (miaka mitatu nyuma) bila ya kuongezwa kwa muda.

Ukaguzi wangu wa mkataba huu umebaini kuwa kulikuwa na makubaliano ya kusambaza kadi 25,000,000 mpaka kipindi cha Ukaguzi, Novemba 2020, nilibaini kwamba msambazaji aliwasilisha kadi 13,735,728 tu. Aidha, uchambuzi wangu ulibaini kwamba, kati ya kadi zilizowasilishwa, NIDA imetumia kadi 6,180,015 kutengeneza vitambulisho vya taifa na kubakiza kadi 5,084,257 zikiwa hazijatumika.

Hata hivyo, nimebaini kuwa kati ya kadi 5,084,257 zilizobakia, ni kadi 4,657,500 tu ndizo zilikuwa zimehifadhiwa kwenye bohari, huku kadi 426,757 zenye thamani ya Sh. 3,399,973,019[8] zikiwa zimeharibika na hazifai kwenye matumizi ya kutengeneza vitambulisho vya taifa. Licha ya menejimenti ya NIDA kueleza kuwa imetuma barua kwenda kwa mkandarasi (IRIS) ili afanye usuluhisho wa kadi zilizoonekana na matatizo na kubadilisha na kadi mpya, ni maoni yangu kuwa, kuna hatari ya NIDA kupata hasara ikiwa IRIS atashindwa kubadilisha kadi hizo ambazo hazifai kutokana na kukosekana kwa mkataba halali kati ya NIDA na M/s IRIS Corporation Berhad.

**Ninapendekeza kwa NIDA kuboresha udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa kadi za kutengenezea vitambulisho vya taifa. Pia kuhakikisha kuwa M/s IRIS Corporation Berhad inatimiza ahadi ya kufanya usuluhishi wa kadi ambazo hazifai na kubadilisha na kadi mpya.**

#### 8.4.1.2 Kutokukusanywa kwa Mapato ya Kutoa Taarifa - Sh. 44,609,955,500

Kifungu cha 16 (c) cha Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, ya mwaka 2014 kinataka malipo ya Sh. 500 kama ada kwa mtu mwenye nia ya kutumia taarifa zilizo chini ya himaya ya NIDA au kila mara akibonyeza kitufe kupata taarifa.

Hata hivyo, nimebaini kuwa NIDA iliruhusu taasisi 40 kupata taarifa za watu waliosajiliwa kwenye kanzidata ya NIDA bila kufanya malipo kwa NIDA kama sheria inavyotaka. Ukaguzi wangu wa ziada wa mfumo, ulibaini taasisi hizo zilibonyeza kitufe kupata taarifa mara milioni 89.2 ambapo NIDA angeweza kukusanya mapato ya Sh. 44,609,955,500. Aidha, nilibaini kukosekana kwa makubaliano ya kisheria kati ya NIDA na taasisi husika ndio sababu ya mapato hayo kutokukusanywa. Hivyo, ni maoni yangu kuwa, serikali inakosa fedha ambazo zingesaidia NIDA kugharamia shughuli zake na kupunguza utegemezi kwa serikali.

---

[8] Gharama ya kila kadi ni Dola za Marekani 3.452 sawa na Sh. 7,967 kwa kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni cha BOT mnamo tarehe 30 June 2020; hivyobasi, kadi 426,757 mara Sh. 7,967 ni sawasawa na Sh. 3,399,973,019

**Ninashauri NIDA ishirikiane na taasisi za serikali zinazonufaika na taarifa za watu waliosajiliwa kutoka kanzidata ya NIDA ili kuhakikisha kuwa makubaliano ya kisheria yanafikiwa.**

### 8.4.2 Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

Jukumu kuu la Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ni kukuza na kuwezesha upatikanaji bora wa huduma za kisasa za nishati katika maeneo ya vijijini kwa upande wa Tanzania Bara. REA ilianza kufanya kazi mnamo Oktoba 2007. Katika ukaguzi wa shughuli za REA na usimamizi wa mikataba nilibaini mapungufu yafuatayo kama yalivyochambuliwa hapa chini:

#### 8.4.2.1 Nguzo za Umeme Zenye Kasoro Zilizowekwa Mkoani Lindi - Sh. 1,065,696,000

Mnamo tarehe 17 Julai 2017, REA iliingia mkataba wenye namba: AE/008/2016-17/HQ/G/09-Lot 4 na M/s State Grid Electrical & Technical Work Ltd kwa ajili ya kuweka umeme vijijini katika mkoa wa Lindi (awamu ya III) kwa bei ya kandarasi ya Sh. 20,878,061,665.12 na Dola za marekani 4,794,467.15 (ikijumuisha kodi ya ongezeko). Muda wa kuisha kwa mkataba ulikuwa tarehe 25 Juni 2020 lakini uliongezwa mpaka tarehe 31 Desemba 2020.

Kwenye ukaguzi wa mkataba huu, nilibaini kuwa mkandarasi aliweka nguzo za umeme 6,541 zenye thamani ya Sh. 2,965,562,433.33 katika mkoa wa Lindi. Hata hivyo, wakati wa kutembelea mradi mnamo Oktoba 2020 niliona kwamba kati ya nguzo zilizowekwa, nguzo za umeme 2,612 (40%) zenye thamani ya Sh. 1,065,696,000 zilikuwa na nyufa. Mbali na hivyo, mkandarasi hakuwa amebadilisha nguzo hizo zenye kasoro. Hii ni kinyume na Kifungu 23.6 cha GCC kinachomtaka mkandarasi kusahisha au kubadilisha bidhaa au sehemu ya vifaa ikiwa bidhaa hizo au vifaa vimeshindwa kufaulu jaribio au ukaguzi.

Ukaguzi wangu wa ziada ulionesha kwamba, nyufa kwenye nguzo zilitokana na kuwekwa kwa nguzo za mbao ambazo hazikuwa zimekomaa (bado changa), hata hivyo, tatizo hilo halikuweza kugundulika katika jaribio la kiwandani (factory acceptance test). Ni maoni yangu kwamba, nguzo hizo zenye kasoro zinaweza kusababishia serikali kuingia kwenye gharama ya ziada ya kubadilisha nguzo hizo baada ya miaka michache ijayo ikiwa mkandarasi atashindwa kurekebisha tatizo lililobainika.

**Ninashauri REA kuchunguza nguzo zote za umeme zilizowekwa na mkandarasi na kumuagiza abadilishe nguzo zote zenye kasoro zitakazobainika. Pia, ninapendekeza REA ichunguze mchakato mzima wa jaribio la kiwandani (factory acceptance test) lililofanyika ili kubaini sababu ya jaribio hilo kushindwa kutambua nguzo hizo zenye kasoro na kama ikibainika kuna hujuma, REA inatakiwa ichukue hatua kwa waliohusika.**

### 8.4.3 Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) ilianzishwa kwa Sheria Namba 4 ya 2012 na ilipewa jukumu ya kuratibu na kufanya utafiti wa mifugo ambao utatoa teknolojia ya kuboresha na kudumisha maendeleo ya sekta ya mifugo nchini. Kwenye ukaguzi wa TALIRI nilibaini mapungufu yafuatayo:

#### 8.4.3.1 Matrekta Mabovu Yaliyoonunuliwa kutoka NDC - Sh. 251,800,000

Mnamo tarehe 21 Mei 2019, TALIRI iliingia kwenye mkataba na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kwa ajili ya kusambaza matrekta manne (aina ya URSUS 6012 85HP 2WD) kwa gharama ya Sh. 251,800,000. Kifungu cha 6 cha Mkataba huu kilitaja kuwa gharama ya mkataba iwe ni ya mkopo na marejesho yake yatafanyika kwa kiasi cha Sh. 10,057,000 kwa mwezi.

Katika ukaguzi wa mkataba huu, nilibaini kuwa NDC iliwasilisha matrekta manne na TALIRI yalizigawa katika vituo mbalimbali. Hata hivyo, niligundua kuwa matrekta mawili yaliyopelekwa Tanga na Mpwapwa yalikuwa na shida za kiufundi kama vile ufanyaji kazi wenye shida kwenye maeneo yafuatayo: mfumo wa mafuta, mfumo wa majimaji (hydrolic), mabomba, mfumo wa breki, pamoja na mfumo wa umeme. Ukaguzi wangu wa ziada ulibaini kuwa TALIRI iliingia gharama za ziada za matengenezo ya muda mfupi kwa matrekta haya kwa kiasi cha Sh. 14,034,000.

**Ni maoni yangu kuwa matrekta haya yanye kasoro yaliyoosambazwa na NDC hayaakisi thamani ya fedha kwa upande wa TALIRI. Pia, taasisi inakuwa kwenye hatari kubwa ya kuingia gharama za juu katika kufanya matengenezo ya matrekta. Hivyo basi, ninashauri matrekta haya yarudishwe NDC na kubadilishwa na kupata matrekta ambayo hayana kasoro.**

### 8.4.4 Kampuni Tanzu Ya Mzinga (Mzinga Holding Company Limited)

#### 8.4.4.1 Kutokulipwa kwa Kodi ya Faida ya Kampuni kwa Miaka Mitatu Mfululizo – Sh. 207,416,646

Kifungu cha 91 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, ya mwaka 2004 kinasema kuwa, kila mtu atajaza na kuwasilisha marejesho ya kodi kwa Kamishna wa Kodi za Mapato sio chini ya miezi mitatu baada ya kuisha kwa mwaka wa mapato. Aidha, imeelezwa pia kwenye Kifungu 98 (1)(c) kuwa ikiwa mtu ameshindwa kuwasilisha marejesho ya kodi kwa mwaka wa mapato kama inavyotakiwa na kifungu 91 (1), atawajibika na adhabu ya kila mwezi au sehemu ya mwezi ambapo mawasilisho hayakufanyika.

Kwenye ukaguzi wangu wa Kampuni Tanzu ya Mzinga nilibaini kuwa, Kampuni ilishindwa kulipa kodi ya faida ya kampuni yenye thamani ya Sh. 207,416,646 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa muda mfululizo wa miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 mpaka 2019/20, kutokana na kushindwa kuandaa na kuwasilisha marejesho ya kodi kwa Kamishna wa TRA kinyume na sheria hapo juu. Ni maoni yangu kwamba tatizo hilo limeinyima serikali mapato ambayo yangeweza kugharamia miradi ya kimkakati na pia, inaingiza kampuni kwenye matatizo ya kikodi ambayo yataathiri kampuni kifedha.

Aidha, ninaona kiasi hiki cha kodi ambayo haijawasilishwa cha Sh. 207,416,646 kilichooneshwa kwenye kitabu cha mahesabu kinaweza kuwa kidogo ikilinganishwa na shughuli za kampuni kwa miaka mitatu.

**Ninashauri TRA kufanya tathmini ya kodi kwa Kampuni husika ili kubaini kiasi halisi ambacho hakijalipwa na kuhakikisha malipo yanafanyika.**

### 8.4.5 Shirika la Nyumbu (TATC)

TATC ilianzishwa kwa kusudi la kuwa na Kituo bora cha kuendeleza ubunifu wa teknolojia ya Magari nchini Tanzania. Ukaguzi nilioufanya kwenye shughuli za TATC niligundua mapungufu kama yalivyoelezwa hapa chini:

#### 8.4.5.1 Mapungufu kwenye Malipo ya Vibarua – Sh. 139,293,000

Katika mwaka huu wa ukaguzi, niligundua kuwa TATC ililipa jumla ya Sh. 139,293,000 kama gharama za vibarua. Hata hivyo, ukaguzi wangu wa vocha za malipo ulibaini yafuatayo:

- Malipo yalifanywa kwa watu ambao hawakutajwa kwenye vocha za malipo bila ya kuwa na nguvu ya wakili au barua ya utawala kinyume na matakwa ya Kanuni 94 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 ambayo inataka ikiwa malipo yamefanyika kwa mtu mwingine badala ya aliyetajwa kwenye vocha, mamlaka inayohusiana na malipo hayo inatakiwa iambatanishe vocha ya malipo pamoja na nakala ya wakili au barua ya utawala au kusajili malipo hayo Hazina.
- Vocha za Malipo hazikuwa zimeambatishwa na maelezo ya kutosheleza ya huduma iliyotolewa na kwa ujumla, vocha ziliandika gharama za vibarua bila ya kuonesha ni shughuli gani wamefanya na muda waliotumia. Hii ni kinyume na Kanuni 86 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma, ya mwaka 2001 inayotaka vocha ya malipo kuwa na maelezo ya kutosheleza kuhusiana na huduma iliyotolewa kama tarehe, idadi, umbali, gharama ili kusaidia uhakiki bila kuangalia taarifa nyingine.

**Ni maoni yangu kuwa, tatizo lililooneshwa hapo juu limetokana na udhibiti usiroridhisha wa ndani wa usimamizi wa matumizi na kama hatua stahiki hazitachukuliwa itaweza kusababisha fedha za serikali kutumika vibaya. Hivyo basi, nashauri TACT kusahisha mapungufu yalioonekana kwenye malipo ya vibarua na kufuatilia ili kudhibitisha uhalali wa malipo hayo.**

## 8.5 Masuala Yaliyobainika Katika Ukaguzi wa Mifuko Maalumu

Mifuko maalum ilianzishwa na serikali kwa ajili ya kukusanya fedha ambazo zitatumika kwa shughuli maalumu. Pia, Mifuko maalumu inahakikisha uwajibikaji na kutoa ukweli kwa walipa kodi kwamba fedha zao zinatumika katika shughuli zilizokusudiwa. Nilipitia shughuli za Mifuko na kubaini masuala muhimu ambayo yanahitaji uboreshaji kama ilivyoelezwa hapo chini:

### 8.5.1 Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa

Mfuko ulianzishwa kwa malengo ya kufanya maombi maalumu au ya jumla kwa taifa kwa ajili ya kuchangia kwa njia ya fedha au mali kwa ajili ya kuokoa maisha, mali, na kupunguza athari au kurudisha hali ya kawaida

kwa jamii iliyoathirika na majanga. Kwenye ukaguzi wa opersheni za Mifuko Maalumu nilibaini yafuatayo:

#### 8.5.1.1 Kutotumika kwa Fedha za Kupambana na Janga la COVID 19 – Sh. 4,314,702,035

Katika mwaka wa ukaguzi 2019/20, nilibaini kuwa Mfuko wa Usimamizi wa Maafa ulipokea Sh. 4,314,702,035 kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kupambana na janga la COVID 19. Hata hivyo, nilibaini kuwa Mfuko haukuwa umetumia fedha hizi ukisubiria maelekezo kutoka vyombo husika.

**Ninashauri serikali kuanzisha mpango kazi wa matumizi ya fedha hizo ili kuepuka vihatarishi vinavyohusiana na kutotumika kwa fedha hizo kama ubadhirifu au kuchepushwa.**

### 8.5.2 Mfuko wa Taifa wa Mambo Kale (NFA)

NFA ina jukumu la kuhifadhi, kulinda na kusimamia rasilimali za urithi wa kitamaduni. Ukaguzi wangu wa shughuli za NFA umebaini mapungufu yanayohusiana na usimamizi wa matumizi kama ilivyoelezwa hapo chini:

#### 8.5.2.1 Malipo Yenye Shaka ya Tamasha la Urithi – Sh. 153,000,000

Nilibaini kuwa NFA ililipa gharama ya Sh. 153,000,000 kwa taasisi mbalimbali za seikali na ambazo si za serikali kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa tamasha la urithi ambalo lilifanyika tarehe 21 Septemba mpaka tarehe 27 Oktoba 2019. Hata hivyo, nilishindwa kujiridhisha na malipo yaliyofanywa kutokana na kukosekana kwa nyaraka muhimu kama risiti za mapokezi ya fedha kutoka kwa wanufaika pamoja na ripoti za utekelezaji wa shughuli husika ili kujiridhisha kwamba fedha zilizotolewa zimefikia walengwa na zimetumika kwa lengo lililokusudiwa ambapo ni kinyume na Kanuni 86 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001. Mchanganuo wa fedha zilizolipwa umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 64** hapo chini.

**Jedwali Na. 64: Malipo yaliyofanywa kwa walengwa ambayo hayajathibitishwa**

| Tarehe | Hundi Na. | Aliyelipwa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 23/09/2019 | 398546 | Trust Foundation | 10,000,000 |
| 11/10/2019 | 398580 | Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara | 10,000,000 |
| 15/10/2019 | 398591 | TANAPA Gombe | 29,000,000 |
| 12/10/2019 | 398596 | TASUBA | 8,000,000 |
| 17/10/2019 | 308617 | Dodoma Maendeleo | 10,000,000 |
| 17/10/2019 | 308619 | RAS Mwanza | 65,000,000 |

| Tarehe | Hundi Na. | Aliyelipwa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 17/10/2019 | 398623 | Halmashauri ya Wilaya ya Karatu | 11,000,000 |
| 24/10/2019 | 398629 | RAS Geita | 10,000,000 |
| **Jumla** | | | 153,000,000 |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti ya NFA*

Kukosekana kwa nyaraka zinazohitajika, kunanipa mashaka ya kuwa fedha hizi zinaweza kuwa zimetumiwa vibaya kwa matumizi binafsi au kutumika kwa shughuli ambazo hazijaidhinishwa.

**Ninashauri vyombo vya uchunguzi kufanya uchunguzi juu ya fedha zilizotolewa ili kubaini kama kweli walengwa walipokea fedha hizo na kuzitumia katika shughuli zilizo stahili.**

### 8.5.3 Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori (TWPF)

Lengo kuu la TWPF ni uhamasishaji wa rasilimali fedha ambazo zinahitajika kusaidia na kudumisha ulinzi wa wanyamapori pamoja na juhudi za uhifadhi nchini Tanzania. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa shughuli za TWPF, nilibaini mapungufu kama inavyooneshwa hapa chini:

#### 8.5.3.1 Kutokuendelezwa kwa Ardhi Iliyonunuliwa Tangu Mwaka 2003 - Sh. 1,210,000,000

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini kuwa tarehe 19 Septemba 2003, TWPF ilinunua ardhi yenye nambari ya kiwanja 2467/27, Jengo la III, mtaa wa Bibi Titi Mohammed, Dar es Salaam kwa gharama ya Sh. 1,210,000,000.

Aidha, ukaguzi wangu ulibaini kuwa TWPF ilipanga kujenga jengo katika kiwanja ambapo tarehe 04 Februari 2011 (miaka minane baada ya kununua kiwanja), TWPF iliingia mkataba namba IE-028/2009-10/C/01 na M/s QD Consult (T) Ltd kwa ajili ya kupata huduma za ushauri za usanifu wa jengo, matayarisho ya kabrasha la zabuni na usimamizi wa ujenzi wa jengo la Kakakuona kwa gharama ya mkataba ya Dola za Marekani 3,863,513.65 sawa sawa na Sh. 6,421,159,688 (Kiwango cha Sh. 1,662/Dola kwa wakati huo).

Kutokana na hayo, nilibaini kuwa mshauri alifanikiwa kukamilisha awamu ya usanifu na kuwasilisha kwa mwajiri ripoti ya kina ya usanifu, michoro na kabrasha la zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mnamo tarehe 15 Mei 2012 (mwaka mmoja baadaye), na mshauri alilipwa kiasi cha Sh. 4,511,552,869 kwa kazi hiyo.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kazi za ujenzi wa jengo zilikuwa hazijaanza tokea ripoti ya usanifu ilivyowasilishwa Mei 2012. Hii inamaanisha kuwa TWPF hajaendeleza ardhi hii kwa kipindi cha miaka 17 kufikia muda wa ukaguzi wangu mnamo Septemba 2020, licha ya Taasisi kuingia jumla ya gharama ya Sh. 5,721,552,869 kwenye uwekezaji huu kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 65**

**Jedwali Na. 65: Gharama Iliyoingiwa na TWPF kwa Uwekezaji Ambao Haujaendelezwa**

| Tarehe | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 19/09/2003 | Malipo yaliyofanywa ya ardhi | 1,210,000,000 |
| 15/05/2012 | Malipo yaliyofanywa kwa kazi ya usanifu wa Jengo | 4,511,552,869 |
| **Jumla** | | **5,721,552,869** |

*Chanzo: barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Ni maoni yangu kuwa, kutoendelezwa kwa ardhi iliyonunuliwa tangu mwaka 2003 (miaka 17 nyuma mpaka muda wa ukaguzi Septemba 2020) kumesababishwa na udhaifu wa menejimenti wa kufanya maamuzi ya uwekezaji, na hii imepelekea kuwapo kwa hatarishi la kupoteza thamani halisi ya fedha kwenye uwekezaji uliofanywa kwenye ardhi pamoja na gharama zilizoingiwa za usanifu wa jengo.

**Kutokana na hayo hapo juu, ninapendekeza TWPF kuendeleza mradi wa ujenzi wa jengo la Kakakuona ili kupata thamani halisi ya fedha juu ya uwekezaji uliofanyika. Pia, ninapendekeza kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuchunguza kama kuna uzembe uliosababisha uwekezaji kutoendelezwa, na kuchukua hatua kwa wahusika ikiwa uzembe utabainika.**

## 8.6 Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)

CDCF ni Mfuko ulianzishwa kwa lengo la kuchochea maendeleo ya majimbo ya uchaguzi ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Sheria Na. 16 ya Mwaka 2009 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

### 8.6.1 Majimbo Yenye Kiasi Kikubwa cha Fedha ambazo Hazijatumika - Sh. 245,994,088.96

Kifungo cha 6 (2) cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009 kinataka fedha zilizowekwa kwenye akaunti ya majimbo ziwe za

mwendelezo, na zinatakiwa ziendelee kutoka mwaka mmoja kwenda mwingine, pamoja na fedha zilizorudishwa kwenye akaunti au ambazo hazijatumika kwa sababu yeyote.

Hatahivyo, nilibaini kuwa kuna kiasi kikubwa ambacho hakijatumika kwenye fedha zilizopelekwa kwenye akaunti za benki za majimbo na halmashauri ili kugharamia miradi iliyoidhinishwa ya CDCF. Mpaka kipindi cha ukaguzi, kiasi cha Sh. 245,994,088.96 hakikuwa kimetumika kwenye majimbo 12, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 66** hapo chini:

**Jedwali Na. 66: Majimbo yenye Kiasi Kikubwa ambacho Hakijatumika**

| Na. | Jimbo | Kiasi (Sh.) | Halmashauri |
|---|---|---|---|
| 1 | Mpendae | 23,110,964.00 | Halmsahauri ya manispaa ya mji |
| 2 | Kikwajuni | 5,343,036.00 | |
| 3 | Mwera | 12,085,274.68 | Halmashauri ya manispaa ya Magharibi A |
| 4 | Fuoni | 40,232,925.00 | |
| 5 | Dimani | 5,093,856.00 | |
| 6 | Kiembesamaki | 43,131,652.00 | Halmashauri ya manispaa ya Magharibi B |
| 7 | Muyuni | 31,760,579.00 | Halmashauri ya wilaya ya kusini B |
| 8 | Makuduchi | 14,223,751.00 | |
| 9 | Chambani | 27,511,966.00 | Halmashauri ya Mji Mkoani |
| 10 | Bumbwini | 5,033,576.18 | Halmashauri ya wilaya ya Kaskazini B |
| 11 | Tumbatu | 13,608,741.78 | Halmashauri ya wilaya ya Kaskazini A |
| 12 | Kijini | 5,149,504.32 | |
| 13 | Gando | 5,397,849.00 | Halmashauri ya Mji Wete |
| 14 | Mtambwe | 5,484,420.00 | Halmashauri ya Mji Wete |
| 15 | Konde | 8,825,994.00 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| **Jumla** | | **245,994,088.96** | |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Ukaguzi unaonesha kuwa, kuwapo kwa kiasi kikubwa cha fedha ambazo hazijatumika kumetokana na kushindwa kwa menejimenti kutoa maamuzi kwa wakati juu ya miradi ya kutekelezwa, kukosekana kwa uratibu na jamii ya chini, na kuwapo kwa vipaumbele ambavyo havijaidhinishwa na wanachama wa majimbo. Ni maoni yangu kuwa, kuwapo kwa kiasi kikubwa ambacho hakijatumika kunamaanisha shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa kwa mwaka ulioisha 30 Juni 2020; na hivyo basi, malengo ya miradi hayakufikiwa.

**Ninashauri kwa menejimenti: (a) katika ngazi ya halmashauri, kusambaza uelewa kwenye jamii ya jinsi gani maombi ya fedha za CDCF yanafanyika, na kuboresha ushirikiano na usimamizi wa shughuli za jamii ya chini katika ngazi ya halmashauri (b) kuhakikisha kuna kuwa na usimamizi wa mara kwa mara wa shughuli za kila siku.**

### 8.6.2 Fedha za CDCF Zilizotumika Nje ya Malengo Kusudiwa – Sh. 19,342,385

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kiasi cha fedha cha Sh. 19,342,385 za CDCF zilitumika na halmshauri mbalimbali kwa kazi ambazo ni nje ya malengo ya fedha husika. Hii ni kinyume na Kifungu 19 (3) cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009 ambacho kinataja kwamba, fedha zilizotajwa kwenye sheria hii hazitakiwi kutumika kwa malengo ya kusaidia chama cha siasa au shughuli za kisiasa au kusaidia taasisi za kidini au shughuli za kidini. Maelezo ya matumizi yaliyo nje ya malengo kusudiwa yanaonekana kwenye **Jedwali Na. 67**:

**Jedwali Na. 67: Fedha za CDCF Zilizotumika kwa Nje ya Kusudio**

| Na. | Halmashauri | Jimbo | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya wilaya ya Kaskazini A | Chaani | Malipo ya saruji kwaajili ya kusaidia watu walioathirika na janga la mvua (Sh. 2,981,860) na malipo ya huduma ya matengenezo ya gari (Sh. 2,191,555) | 5,173,415 |
| 2 | Halmashauri ya wilaya ya kati | Uzini | Ununuzi wa jenerata katika msikiti wa Ghana | 480,000 |
| | | | Malipo ya umeme ya msikiti wa Ghana | 1,500,000 |
| 3 | Halmashauri ya wilaya ya kusini | Makunduchi | Ukarabati wa uwanja kwaajili ya matayarisho ya mwenge wa uhuru | 12,188,970 |
| **Jumla** | | | | **19,342,385** |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Ni maoni yangu kwamba, mapungufu haya yanatokana na udhibiti usioridhisha wa matumizi ya fedha za CDCF. Hivyo basi, kuna hatari ya malengo ya fedha za mradi za CDCF hayatafikiwa kama ilivyokusudiwa.

**Ninashauri halmashauri kuhakikisha kwamba fedha za mradi zinatumika kama zilivyoidhinishwa. Pia, kiasi kilichohojiwa kikombolewe kutoka kwa wahusika.**

### 8.6.3 Kutorejeshwa kwa Fedha Zilizokopwa na Wizara - Sh. 4,083,913,175.08

Kanuni 62 (4) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inatamka kuwa hakuna mtu ataruhusiwa kukopa au kuazima au kusababisha ukopaji wa fedha zilizokusanywa chini ya kanuni hii kwa namna au malengo yoyote.

Hata hivyo, katika kipindi cha ukaguzi wa shughuli za Mifuko maalumu, nilibaini kuwa wizara mbali mbali zilikopa jumla ya Sh. 4,083,913,175.08 kutoka mifuko maalumu mitatu bila ya kurudisha kiasi hicho kama ilivyoelezewa kwenye **Jedwali Na. 68** hapo chini:

**Jedwali Na. 68: Fedha zilizokopwa na Wizara**

| Na. | Jina la Mfuko | Kiasi kilichokopwa (Sh.) | Taasisi iliyokopeshwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Uwezeshaji wa Maendeleo ya Madini (EMDF) | 521,831,816.56 | Wizara ya Madini |
| 2 | Akaunti ya Mfuko wa Barabara-TAMISEMI | 3,442,788,003.52 | OR - TAMISEMI |
| 3 | Mfuko wa Maji Taifa Wizara ya Maji | 119,293,355.00 | Wizara ya Maji |
| | **Jumla** | **4,083,913,175.08** | |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Ni maoni yangu kwamba, kutokurudishwa kwa fedha zilizokopwa na Wizara kunaweza kuhatarisha shughuli za Mifuko Maalumu na kusababisha malengo ya bajeti kutofikiwa.

**Kutokana na hapo juu, ninashauri Wizara kuhakikisha kwamba kiasi kilichokopwa kinarudishwa kwenye Mifuko husika. Pia Seikali iandae mwongozo utakaosaidia menejimenti ya mifuko hii kukabiliana na ukopaji wa Wizara.**

## 8.7 Masuala Yaliyobainika Katika Ukaguzi Wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali Maalumu

Kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ndani ya nchi, mnamo tarehe 01 Julai 2020, Serikali ilihamisha hospitali zote za rufaa kwenda Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, ukaguzi wangu wa hospitali hizi za rufaa za mikoa pamoja na hospitali maalumu ulibaini mapungufu yanayohitaji maboresho kama ilivyoelezewa hapo chini:

### 8.7.1 Mashine ya Kusukuma Dawa Iliyotelekezwa kwa Miaka Minane katika Hospitali ya Mkoa ya Rufaa Songea

Katika ukaguzi wangu wa Hospitali ya Mkoa ya Rufaa Songea, nilibaini kuwa Mashine ya kusukuma dawa (infusion pump) ambayo ni maalum kwa kusukuma majimaji kwenye mwili wa mgonjwa katika kiasi kinachodhibitiwa ilitelekezwa bila kutumika kwa muda wa miaka minane. Aidha, nilibaini kuwa, hospitali haina mkakati wa kutumia mashine ambayo ilichangiwa na taasisi ya Water Reed Tanzania Program mnamo mwaka 2012; na hivyo basi, kuna hatari kuwa mashine hii itaharibika.

**Ninashauri hospitali husika kuhakikisha mashine hii inafanya kazi ili kuboresha huduma za afya zinayotolewa kwa wananchi pamoja na hospitali husika kupata thamani ya fedha ya mashine hii.**

### 8.7.2 Mkataba Wenye Shaka wa Kukodisha na Kuazima Kifaa cha Utabibu Kati ya Hospitali ya Mkoa ya Rufaa Musoma na SMAI Medical Company Ltd

Nilibaini kuwa mnamo tarehe 1 Juni 2019, Hospitali ya Mkoa ya Rufaa Musoma iliingia mkataba na SMAI Medical Company Ltd kwa ajili ya kukodisha na kuazima kifaa cha utabibu (hormone analyzer machine and ECHO machine). Muda wa mkataba ulikuwa miezi sita tokea siku ya kusaini makubaliano ambao ulipangwa kuisha tarehe 1 Desemba 2019.

Aidha, nilibaini kuwa mkataba ulitaka mgawanyo wa 50% ya faida inayopatikana kwenye huduma inayotolewa kwa kutumia mashine hiyo ambapo hospitali ililipa Sh. 52,344,000 kwa SMAI Medical Company Ltd. Hata hivyo, ukaguzi wangu wa makubaliano ulibaini mapungufu yafuatayo:

**(a) Mkataba kutekelezwa Bila ya kupata Idhini kutoka Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto**

Nilibaini kuwa utekelezaji wa mkataba ulianza tarehe 1 Juni 2019 baada ya kusainiwa na afisa wa afya, mwanasheria na mtoa huduma, kinyume na matakwa ya mkataba yanayotaka mkataba usainiwe na Katibu Mkuu. Aidha, nilibaini kuwa mkataba haukuwa na nguvu ya uwakili ya mkodishaji pamoja na mwanasheria aliyeshuhudia makubaliano; hivyo, nikashindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa mkataba husika.

**(b) Kushindwa Kuthibitisha Mchakato wa Manunuzi**

Kifungu 61 (1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinataka taasisi ya manunuzi kuhifadhi mchakato mzima wa manunuzi ambao umefanyika pamoja na maamuzi yaliyofikiwa na sababu yake na taarifa hizo zinatakiwa zihifadhiwe kwa kipindi kisichopungua miaka mitano kutoka siku ya kukamilika kwa mkataba. Nilibaini kwamba Hopsitali ya Mkoa ya Rufaa Musoma haikuhifadhi taarifa za mkataba huu kinyume na sheria tajwa.

Pamoja na kwamba mashine haikuwapo katika himaya ya hospitali wakati wa ukaguzi mnamo mwezi Oktoba 2020, ni maoni yangu kwamba, makubaliano haya yana chembechembe za rushwa na inawezekana yameisababishia serikali hasara.

**Hivyo basi, ninashauri Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuchunguza mkataba huu na kuchuka hatua za kisheria kama ikibainika kuna ubadhirifu.**

### 8.7.3 Kasi Ndogo ya Ujenzi wa Majengo ya Hospital za Rufaa za Mkoa

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilikagua hospitali za rufaa na kubaini kuwa kuna ucheleweshaji wa ujenzi wa majengo ya hopitali kama ilivyoelezwa kwenye **Jedwali Na. 69** hapo chini:

**Jedwali Na. 69: Ucheleweshaji wa Ujenzi wa Majengo ya Hospitali**

| Hospitali | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|
| **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Sokoine** | • Mnamo Aprili 2018, Hospitali ya Sokoine ilianza ujenzi wa wodi ya watoto kwa kutumia utaratibu wa ujenzi bila kutumia mzabuni (force account) kwa muda wa miezi mitatu mpaka Julai 2018 na kwa gharama ya Sh. 93,478,882.50. |

| Hospitali | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|
| | • Hata hivyo wakati natembelea eneo la ujenzi mnamo tarehe 3 Oktoba 2020, nilibaini kwamba hospitali haikuwa imekamilisha ujenzi ambapo maendeleo ya ujenzi yalikuwa asilimia 70.<br>• Aidha, nilibaini hospitali ilihifadhi vifaa vya ujenzi kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja bila kuvitumia. |
| **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa** | • Mnamo tarehe 5 Juni 2020, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa iliingia kwenye mkataba wa utaratibu wa ujenzi bila kutumia mzabuni (force account) na Magereza ya Iringa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura awamu ya kwanza kwa makadirio ya gharama ya Sh. 19,024,119. Muda wa ujenzi ulikadiriwa kuisha tarehe 05 Oktoba 2020 (miezi mnne mbele).<br>• Wakati natembelea eneo la ujenzi mnamo tarehe 08 Oktoba 2020, nilibaini kwamba hospitali ilitumia jumla ya Sh. 10,758,630 kwa ajili ya kazi za ujenzi. Hata hivyo, maendeleo ya kazi yalikuwa asilimia 53 huku muda wa mradi ukiwa umeisha kwa asilimia 100. |
| **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Ligula** | • Katika ziara yangu kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Ligula, nimebaini kuwa ujenzi wa jengo la upasuaji umetelekezwa katika hatua ya msingi. Pia, nilibaini kuwa mradi ulikuwa unatekelezwa na Ofisi ya Katibu tawala Mtwara kabla ya kuhamishiwa hospitali na ulisimama tangu mwaka 2019.<br>• Aidha, nilibaini kuwa Ofisi ya Tatibu Tawala Mtwara ulikabidhi mradi bila ya kuwapo kwa taarifa au mkataba wa ujenzi husika.<br>• Pia, niliona kuwapo kwa nyufa kubwa kwenye msingi, ukuta na paa la jengo la idara ya wagonjwa.<br>• Hivyobasi, ni maoni yangu kuwa kwa hali ya sasa ya jengo hilo la idara ya wagonjwa, kuna uwezekano mkubwa wa jengo kuanguka kama hatua za haraka hazitachukuliwa. |
| **Hospitali ya Rufaa ya Maweni** | • Mnamo tarehe 13 Juni 2019, hospitali ilipokea Sh. 532,967,370 kutoka Wizara ya Afya kwaajili ya kujenga jengo la upasuaji kwa kutumia utaratibu wa ujenzi bila kumtumia mzabuni (force account). Mradi ulipangwa kuanza tarehe 1 Agosti 2019, na |

| Hospitali | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|
| | kukamilika tarehe 28 Februari 2020.<br>• Hata hivyo, nilipotembelea mradi Oktoba 2020, nilibaini ujenzi ulikuwa bado kwenye hatua za msingi na hii inaonesha kwamba mradi ulichelewa zaidi ya miezi nane tokea muda wa kukamilika kwa mradi wa tarehe 28 Februari 2020. |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Ni maoni yangu kuwa, miradi hii ilichelewa kutokana na sababu mbalimbali kama kuchelewa kwa fedha za kutekeleza miradi pamoja na usimamizi usioridhisha wa miradi ya ujenzi inayotelekezwa bila ya kumtumia mzabuni (force account).

**Ninashauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuhakikisha fedha za miradi ya ujenzi zinatolewa kwa wakati pamoja na kuboresha udhibiti wa ndani kwenye miradi inayotekelezwa kwa utaratibu usio na mzabuni (force account).**

### 8.7.4 Hasara Iliyotokana na Madai Kukataliwa na Mfuko wa Bima ya Afya – Sh. 2,179,268,577.86

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini katika Hospitali za Rufaa 26 kuwapo kwa madai ya matibabu yaliyokataliwa na NHIF yenye thamani ya Sh. 2,179,268,577.86 kutokana na makosa katika ujazaji wa taarifa za wagonjwa pamoja na mfumo duni wa kuhifadhi taarifa za wagonjwa. Aidha, nimebaini kuwa madai haya yaliyokataliwa yameongezeka kwa Sh. 695,876,632.67 (47%) ukilinganisha na madai yenye thamani ya Sh. 1,483,391,945.19 ambayo yalikataliwa kwenye ripoti yangu ya mwaka uliopita, 2018/19. Rejea **Kiambatisho Na. XVIII** kwa maelezo zaidi

**Ingawa naelewa ukataaji wa madai ya Hospitali za Rufaa unaathiri mapato ya hospitali hizi, ninashauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kupitia mfumo mzima wa malipo kwa bima ya afya ili kubaini mapungufu katika uthibiti wa ndani unaosababisha madai ya hopsitali kukataliwa na NHIF. Pia, kuangalia njia bora ya kuanzisha mfumo utakaowezesha matumizi mazuri ya bima ya afya nchini.**

### 8.7.5 Kutokuharibiwa kwa Dawa Zilizokwisha Muda Wake wa Kutumika – Sh. 238,708,163

Kanuni Na. 10 ya Kanuni za Chakula, Madawa na Vipodozi ya mwaka 2015, inataka maamuzi ya kuanzisha mchakato wa uharibifu wa bidhaa ambazo hazifai kuwa unafanywa na Mamlaka, Mkoa, Wilaya au Hospitali, Mmiliki wa sehemu husika, msimamizi au mkaguzi.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kuna dawa zilizoisha muda wake zenye thamani ya Sh. 238,708,163 ambazo hospitali hazijaziteketeza. Ni maoni yangu kuwa tatizo hili linatokana na udhibiti usioridhisha wa usimamizi wa madawa na kuendelea kuhifadhi dawa zilizoisha muda wake bila kuziharibu kunaleta uwezekano mkubwa wa madhara kwa wananchi kama zitatumiwa kwa bahati mbaya au kutua katika mikono ya watumishi wasio waaminifu. Kwa maelezo ya taasisi zenye madawa yaliyoisha muda wake angalia **Kiambatisho Na. XVIII**.

Ninashauri serikali kuhakikisha kwamba dawa zilizoisha muda wake zinateketezwa ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kwa wananchi ikiwa dawa hizi zitatumika kwa bahati mbaya. Pia, nashauri kuboresha usimamizi wa dawa kwenye hospitali.

### 8.7.6 Ununuzi wa Dawa Bila Idhini ya Bohari Kuu ya Madawa (MSD)

Kanuni ya 140 (5) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inataka kuwa, ikiwa bidhaa za dawa zinazotaka kununuliwa na taasisi ya manunuzi haipo MSD, basi Bohari inatakiwa ndani ya siku moja ya kazi tokea kupokea ombi kutoa notisi ya kutopatikana kwa dawa kwenda taasisi ya manunuzi.

Hata hivyo, nilibaini hospitali mbili za rufaa zilinunua dawa na vifaa vya utabibu vyenye thamani ya Sh. 480,023,534.26 kutoka kwa watoa huduma binafsi bila ya kupata idhini kutoka MSD ili kuthibitisha kutokuwapo kwa dawa hizo kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. XVIII.**

Ni maoni yangu kuwa udhaifu huu unaongeza hatari ya ununuzi wa dawa na vifaa vya utabibu kutoka kwa watoa huduma binafsi ambavyo havina ubora au kwa gharama kubwa ikilinganishwa na gharama ya MSD, na hivyo kusababisha hasara kwa taifa.

**Ninashauri hospitali kupata idhini ya MSD kabla ya kufanya manunuzi ya madawa kutoka kampuni binafsi kama matakwa ya Kanuni 140 (5) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma, 2013.**

## 8.8 Masuala Mtambuka Yanayohusiana na Ukaguzi wa Wakala, Taasisi, Mifuko, Mabonde Ya Maji Na Hopsitali Za Rufaa

Katika ukaguzi wangu wa Wakala, Mabonde ya Maji na Mifuko Maalumu ya Serikali, nilibaini masuala ambayo yalibainika maeneo mbalimbali yanaohusiana na usimamizi wa matumizi yanayohitaji maboresho kama ifuatavyo:

### 8.8.1 Malipo Yenye Mashaka – Sh. 145,115,666

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini malipo yenye mashaka ya Sh. 145,115,666 yaliyofanywa na taasisi mbalimbali. Kwa maelezo zaidi angalia **Jedwali Na. 70**.

**Jedwali Na. 70: Malipo Yenye Shaka**

| Taasisi | Kiasi (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|
| Wakala wa Maabara za Mifugo Tanzania (TVLA) | 9,984,800.00 | Malipo haya yalifanywa kwa Bodi ya Kumshauri Waziri mnamo tarehe 18 na 27 Februari 2020 huku muda wa bodi hiyo ukiwa umekwisha muda wake tangu tarehe 31 Agosti 2018 (miaka miwili nyuma) |
| Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 67,518,734.00 | Malipo ya fedha za kukaimu kwa wafanyakazi waliokaimu kwenye nafasi mbalimbali bila ya kupata idhini ya OR-UTUMISHI kinyume na D.19 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009 na Muongozo Namba 1 wa utumishi wa umma wa mwaka 2015. |
| Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa (TMA) | 5,040,000.00 | Malipo ya mshahara wa mfanyakazi aliyefariki kwa miezi minne kuanzia Oktoba 2019 mpaka Januari 2020 kinyume na Kanuni 113 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 |
| Mfuko Wa Taifa Wa Mambokale (NFA) | 19,488,000.00 | NFA ilifanya malipo ya usambazaji wa bango kwa ajili ya sherehe za maadhimisho ya Urithi; hata hivyo, bango hilo lilipokelewa mnamo tarehe 1 Novemba 2019 ikiwa ni siku tano baada |

| Taasisi | Kiasi (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|
| | | ya kukamilika kwa sherehe hiyo iliyofanyika tarehe 27 Oktoba 2019. |
| Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu (ADEM) | 21,340,000.00 | Kuendana na Mpango wa utumishi wa ADEM, Sura ya 2.1 inataka mkufunzi wa daraja PTSS 10-11 alipwe mshahara wa Sh. 1,210,000 kwa mwezi, huku mkufunzi mwenye daraja PTSS 12 alipwe mshahara wa Sh. 1,598,000 kwa mwezi. Hatahivyo, nimebaini mkufunzi mmoja aliyeajiriwa mnamo tarehe 1 Desemba 2015 kwa daraja PTSS 10-11 alilipwa Sh. 1,598,000 kwa mwezi badala ya Sh. 1,210,000, na kusababisha malipo ya ziada ya Sh. 21,340,000 kwa miezi 55 mpaka tarehe 30 Juni 2020. |
| Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) | 3,744,132.00 | Kwenye ukaguzi wa wanafunzi wanaonufaika na ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi kwa programu ya uendeshaji wa hoteli, nilibaini NCT ililipa kiasi cha Sh. 3,744,132 kwa wanafunzi watatu ambao hawakuwapo chuoni kwenye mwaka wa masomo 2019/20. |
| Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) | 18,000,000.00 | Nilibaini kuwa RITA ililipa Sh. 18,000,000 kwa wafanyakazi 10 kama fedha za nyumba bila ya kuwa na kibali kunachotajwa kwenye L.34 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009. |
| **Jumla** | **145,115,666.00** | |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti.*

Ijapokuwa malipo hayo yanakiuka sheria, kanuni na miongozo mbalimbali, ni maoni yangu kuwa kuna hatarishi serikali inaweza kupata hasara kutokana na malipo yasiyo halali, hivyo, kutopata thamani halisi ya fedha iliyotumika.

**Hivyo, nashauri taasisi husika zihakikishe malipo haya yasiyo halali yanakombolewa kutoka kwa wahusika. Pia, nashauri taasisi kuboresha uthibiti wa ndani juu ya usimamizi wa matumizi.**

### 8.8.2 Malipo Yenye Nyaraka Pungufu - Sh. 5,740,994,515.65

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini malipo yenye thamani ya Sh. 5,740,994,515.65 ambayo hayakuwa na nyaraka za kujitosheleza kinyume na Kanuni 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001. Kwa maelezo zaidi angalia **Jedwali Na. 71**

**Jedwali Na. 71: Taasisi zenye Malipo yenye Nyaraka Pungufu**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wakala Wa Huduma Za Misitu Tanzania (TFS) | 200,061,021.00 |
| 2 | Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) | 451,457,684.00 |
| 3 | Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza | 530,446,323.79 |
| 4 | Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) | 87,738,385.00 |
| 5 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | 46,083,900.00 |
| 6 | Shirika la Mzinga | 3,584,216,021.15 |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya MkoaTemeke | 172,156,483.32 |
| 8 | Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) | 101,242,748.39 |
| 9 | Wakala Wa Barabara Za Vijijini Na Mijini (TARURA) | 72,860,000.00 |
| 10 | Kituo cha Mafunzo ya Takwimu cha Afrika Mashariki (EASTC) | 98,097,349.00 |
| 11 | Hospitali ya rufaa ya mkoa wa Dodoma | 257,424,600.00 |
| 12 | Hospitali ya rufaa ya mkoa wa Tabora | 139,210,000.00 |
| | **Jumla** | **5,740,994,515.65** |

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa menejimenti*

Ukaguzi wangu wa ziada ulionesha kwamba malipo yasiyokuwa na nyaraka za kujitosheleza yameongezeka kwa Sh. 3,533,070,609.75 (160%) ikilinganishwa na Sh. 2,207,923,905.90 zilizobainika kwenye ripoti ya mwaka uliopita (ya mwaka 2018/19). Hii inaashiria utekelezeji usioridhisha wa mapendekezo niliyoyatoa kwa mwaka uliopita. Ni maoni yangu kwamba, upungufu huu unaweza kuwa umesababishwa na ubadhirifu wa fedha za umma. Kama ubadhirifu huu hautadhibitiwa, serikali itapoteza fedha zake kwenye malipo yasiyo halali, hivyo, thamani halisi ya fedha kutopatikana kwenye matumizi hayo.

**Ninashauri taasisi husika kuhakikisha nyaraka pungufu hizo zinapatikana na kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki wa kikaguzi. Pia, kuhakikisha wanaboresha udhibiti wa ndani.**

### 8.8.3 Malipo Yaliyofanywa Nje ya Bajeti - Sh. 5,251,454,739.70

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilifanya ukaguzi wa usimamizi wa bajeti kwa taasisi mbalimbali na kubaini kuna malipo yenye thamani ya Sh. 5,251,454,739.70 yaliyofanywa nje ya bajeti kinyume na Kanuni 46 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 iliyorekebishwa 2004 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 72** hapo chini.

**Jedwali Na. 72: Taasisi Zilizofanya Malipo Nje ya Bajeti**

| Na | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA) | 153,603,589.00 |
| 2 | Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | 2,054,266,378.01 |
| 3 | Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza | 2,234,644,183.20 |
| 4 | Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TWMA) | 204,473,000.00 |
| 5 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania(TIA) | 165,850,921.86 |
| 6 | Mfuko wa Taifa wa Maji - Wizara ya Maji | 110,838,982.63 |
| 7 | Wakala Wa Barabara Za Vijijini Na Mijini (TARURA) | 327,777,685.00 |
| | **Jumla** | **5,251,454,739.70** |

**Chanzo:** Barua ya mapungufu kwa menejimenti

Aidha, uchambuzi wangu wa ziada ulionesha kwamba, ikilinganishwa na mwaka uliopita, malipo yaliyofanywa nje ya bajeti yameongezeka kwa Sh. 2,813,087,232.72 (115%) kutoka Sh. 2,438,367,506.98 kwenye mwaka wa fedha 2018/19 na ni maoni yangu kwamba, udhaifu huu unaathiri utekelezaji wa shughuli ziilizoidhinishwa na kusababisha kutokufikiwa kwa malengo ya bajeti.

**Ninashauri taasisi husika kuhakikisha kwamba malipo yanafanywa kuendana na bajeti, na kama kuna hitaji lakufanya malipo nje ya bajeti, taasisi zinatakiwa kuhakikisha mchakato wa kuomba na kupata idhini kutoka kwa mamlaka husika unafuatwa. Pia, nashauri taasisi kuboresha udhibiti wa ndani kwenye usimamizi wa bajeti.**

# SURA YA TISA

# UNUNUZI NA USIMAMIZI WA MIKATABA

## 9.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania inatambua umuhimu wa usimamizi bora wa ununuzi wa Umma na Mikataba kama suala la msingi la kuhakikisha rasilimali za Umma zinatumika kwa ufanisi na uwajibikaji. Kutokana na umuhimu huo Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 (Na marekebisho yake ya mwaka 2016) pamoja na Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, (na marekebisho yake ya mwaka 2016) zilitungwa. Sheria hizi zinaweka utaratibu wa kisheria, usimamizi wa Taasisi za ununuzi pamoja na michakato ya ununuzi katika sekta ya umma.

Katika kutimiza majukumu yangu ya kisheria kama yalivyoainishwa katika kifungu Na. 48 (3) cha Sheria iliyotajwa hapo juu, nimejumuisha katika Sura hii mapitio na ukaguzi wa taratibu na michakato ya ununuzi wa umma na pia kiwango cha uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma. Matokeo ya Ukaguzi wa kina wa Ununuzi na Mikataba yanapatikana katika ripoti zilizotolewa kwa Menejimenti ya Taasisi husika. Yafuatayo ni baadhi ya Mapungufu makubwa yaliyobainika katika ukaguzi wa usimamizi wa Ununuzi na Mikataba katika Taasisi za Serikali Kuu na Sekretarieti za Mikoa.

## 9.2 Mapungufu Yaliyobainika katika Ununuzi wa Huduma za Kisheria Zenye Thamani ya Sh. 2,757,322,034 kwa Dharura

Katika kipindi cha ukaguzi huu nilibaini kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (**Fungu Na. 19**) ilifanya ununuzi wa huduma za kisheria kwa njia ya dharura kutoka kampuni ya Uwakili ya M/S Shakespeare Martineau Kuiwakilisha Serikali katika kesi mbili (Konoike Construction dhidi ya Serikali ya Tanzania na Wallis dhidi ya Serikali ya Tanzania) katika Jiji la London. Aidha, nilibaini kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikiuka Kanuni ya 63 (3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka, 2013 (kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 22 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2016) ambayo inamtaka Afisa Masuuli kuwasilisha ombi la idhini (retrospective approval) kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ununuzi wa dharura; kinyume chake hakukuwa na ushahidi wowote unaonesha kuwa ombi hilo liwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Halikadhalika, nilibaini kutokuwapo kwa Mkataba ulioingiwa kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kampuni tajwa hapo juu licha ya kwamba kiasi cha Sh 2,757,322,034 kililipwa kama ada ya uwakili kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kinyume na kanuni ya 233(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma(kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 73 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka, 2016). Ni maoni yangu kwamba malipo yanayofanyika bila kuwa na Mkataba yanaweza kutengeneza mianya ya malipo yasiyo halali. Pia yanaweza kupelekea kutoendana na utaratibu mzima wa kutekeleza huduma za Kisheria.

**Naishauri Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuomba idhini ya kuhalalisha toka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa manunuzi ya dharura kama ilivyoelekezwa katika Sheria tajwa hapo juu. Vilevile, katika manunuzi mengine ya baadaye napendekeza kuzingatia kuwapo kwa mkataba kati ya pande husika.**

### 9.3 Mapungufu Yaliyobainika katika Mkataba wa Uwekezaji kwenye Mradi wa Mfumo Salama wa Mawasiliano wenye Thamani ya Sh 129,555,020,000

Mnamo tarehe 7 Novemba, 2009, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (**Fungu Na. 57**) iliingia Mkataba na Kampuni ya ZTE Corporation ya Nchini China kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Mfumo Salama wa Mawasiliano (Independent Mobile Secured Networks-IMSN) kwa gharama ya Dola za Marekani 98,000,000 sawa na Sh. 129,555,020,000 za Tanzania.

Utekelezaji wa Mkataba ulianza tarehe 12 Novemba 2012, ambapo Mkandarasi alipaswa kutekeleza yafuatayo: Ujenzi wa Minara 151 ya Mawasiliano, ununuzi na usafirishaji wa vifaa toka Nchini China hadi Dar es Salaam, kufunga majenereta 88, ununuzi wa magari matatu, kutoa mafunzo kwa watumishi, kutoa huduma ya matengenezo, pamoja na msaada wa kiufundi kwa kipindi cha miaka mitano baada ya kukamilika kwa mradi. Kwenye Mkataba huo, Wizara ilipaswa kutekeleza yafuatayo: upatikanaji wa umeme kwenye minara yote, kununua/kukodisha maeneo ya kujengwa minara, kupata mawasiliano kwenye minara, kulipa ada, kodi na tozo zote katika bandari ya Dar es Salaam, kutoa usalama katika minara ya mawasiliano na kujenga nyumba mbili za kusimamia mawasiliano (Control houses). Hata hivyo, katika kupitia Makubaliano hayo ya kimkataba nilibaini mapungufu yafuatayo:

Wizara ilishindwa kutekeleza majukumu yake ya mkataba kama yalivyotajwa hapo juu. Hatua hii ilipelekea Mkandarasi kujenga minara 132 kati ya 151 kama fidia ya gharama za ziada zilizofanywa na Mkandarasi kwa niaba ya Wizara bila ya kuwa na Makubaliano.

Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi ilipaswa kukamilika mwaka 2015. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi huu Agosti 2020, awamu ya kwanza haikuwa imekamilika. Hali hii ilipelekea awamu ya pili ya mradi kutokuanza.

Aidha, nilibaini kati ya Watumishi 52 waliopata mafunzo ni wanne tu waliosalia katika Mradi. Wengine wamepangiwa majukumu mengine na wengine wakiwa wamestaafu kazi, hivyo kupelekea uhai wa miradi huu kutiliwa shaka.

**Naishauri Wizara kusimamia kwa karibu mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa mradi tajwa hapo juu ili kuweza kupata thamani halisi ya fedha na kufikia malengo yaliyokusudiwa.**

### 9.4 Kukosekana kwa Makubaliano (Concession Agreement) baina ya Wizara ya Ujenzi na Mfuko wa Pensheni wa NSSF katika ukusanyaji wa mapato katika Daraja la Nyerere (Kigamboni)

Kifungu Na. tatu cha Mkataba (Finance Agreement) wa Ujenzi wa Daraja la Nyerere (Kigamboni) wa tarehe 20 Novemba, 2014 baina ya Wizara ya Ujenzi **(Fungu Na. 98)** na Mfuko wa Pensheni wa NSSF kinaagiza kuwapo kwa Makubaliano (Concession Agreement) katika kubuni, kujenga, kufadhili, kuendesha daraja Nyerere kati ya Mmiliki (Wizara ya Ujenzi) na Mwekezaji (NSSF). Gharama za ujenzi wa Daraja la Nyerere (Kigamboni) ilikuwa katika uwiano wa asilimia 60 za mwekezaji (NSSF) na asilimia 40 za Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi. Vile vile kifungu Na. 12 cha Mkataba wa ufadhili (Finance Agreement) kinabainisha uendeshaji na ukarabati wa daraja hilo kuwa jukumu la NSSF kama itakavyokuwa imeainishwa kwenye Makubaliano (Concession Agreement).

Katika ukaguzi wangu, nilibaini ujenzi wa Daraja na njia zake ulikamilika tangu tarehe 30 Juni 2016. Hata hivyo, uendeshaji wa Daraja umekuwa ukifanyika bila ya kuwapo kwa Makubaliano (Concession Agreement) baina

ya Wizara na NSSF kinyume na kifungu tajwa hapo juu. Ni maoni yangu kuwa kukosekana kwa Makubaliano hayo kunaiondolea NSSF uhalali wa kisheria wa kukusanya na kutambua mapato katika taarifa za fedha kutoka kwa watumiaji wa daraja hilo.

**Naaendelea kusisitiza Wizara kuwasiliana na Mamlaka husikia pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha kuwa jambo hilo linafanyiwa kazi kwa wakati.**

### 9.5 Ununuzi Uliofanyika Nje ya Mpango wa Mwaka wa Ununuzi Sh. 15,129,146,553

Kifungu Na. 49(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka, 2011 kinaagiza Taasisi za ununuzi kuzingatia Mpango wa ununuzi wa Mwaka. Hata hivyo, katika ukaguzi wa Wizara, Idara, na Sekretarieti za Mikoa, Taasisi saba zilibainika kufanya ununuzi wa vifaa na huduma wenye thamani ya Sh. 15,129,146,553 nje ya mpango wa mwaka wa ununuzi. Kwa kuwa ununuzi huu ulifanyika nje ya mpango wa mwaka wa ununuzi, hali hiyo ilipelekea matumizi nje ya bajeti ya Taasisi husika. Upungufu huu ulitokana na udhaifu kwenye maandalizi ya mpango wa ununuzi na bajeti katika Taasisi husika. **Jedwali Na. 73** linaonesha Taasisi zilizofanya ununuzi nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka.

**Jedwali Na. 73: Taasisi Zilizofanya Ununuzi Nje ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka**

| Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---:|
| 53 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | Ununuzi wa Huduma za Ushauri na Ulinzi | 131,192,986 |
| 14 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi | 2,709,297,900 |
| 99 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | Uchimbaji wa Visima, Mabwawa na Ujenzi wa Uzio | 2,428,349,273 |
| 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. | Ununuzi wa huduma za Ulinzi | 177,798,040 |
| 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Ununuzi wa Magari Ishirini (20) | 1,373,706,909 |
| 79 | Sekretarieti ya Mkoa | Ununuzi wa mbegu za | 93,453,152 |

| Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|
| | wa Morogoro | mahindi na vifaa vya Ujenzi | |
| N/A | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | Ununuzi wa vifaa vya Ofisini, vilainishi na mafuta ya magari, ukarabati wa magari pamoja na huduma za bima na usafi | 8,215,348,293 |
| **Jumla** | | | **15,129,146,553** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ikilinganishwa na mwaka 2018/2019, kuna ongezeko la Sh 11,523,371,141 kwa ununuzi uliofanyika bila ya kufuata Mpango wa Ununuzi wa Mwaka. Katika mwaka wa 2018/19 jumla ya taasisi saba zilifanya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh 3,605,775,412 nje ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka.

**Nazishauri Taasisi za Serikali Kuu kuzingatia Mpango wa Ununuzi wa mwaka na pia nahimiza Taasisi kufanya tathmini halisi ya mahitaji na tafiti za bei za soko ili kupata taarifa za kutosha za kuwezesha upangaji na utekelezaji mzuri wa shughuli za ununuzi.**

### 9.6 Ununuzi wa Bidhaa na Huduma Bila ya Ushindanishi Sh. 1,099,982,377

Katika Ukaguzi wa ununuzi nilibaini jumla ya taasisi saba za Serikali Kuu zilikiuka kanuni ya 163 & 164 ya kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 63 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma mwaka, 2016). Kanuni hizi zinataka Taasisi za Ununuzi kuzingatia upatikanaji wa nukuu za bei zisizopungua tatu kutoka kwa Wazabuni tofauti ili kuweza kupata bei ya ushindani. Hata hivyo, nilibaini kufanyika kwa ununuzi wa bidhaa na huduma wenye thamani ya Sh 1,099,982,377 kutoka kwa Wazabuni mbalimbali bila ya ushindanishi wa bei kinyume na Sheria tajwa hapo juu. Taasisi ambazo hazikuzingatia kanuni tajwa hapo juu zimeorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 74**

**Jedwali Na. 74: Ununuzi Uliofanyika Bila Ushindanishi**

| Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|
| 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Ununuzi wa sare za jeshi, samani na vifaa mbalimbali vya Ofisini | 288,127,480 |
| 39 | Jeshi la Kujenga Taifa | Ununuzi wa vifaa vya shamba, dawa za kuua wadudu, kukodisha matrekta, na upimaji wa sampuli ya udongo | 536,362,986 |
| 52 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto | Ununuzi wa vifaa vya Ofisini | 51,000,000 |
| 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | Ununuzi wa vifaa vya umeme | 16,307,280 |
| 90 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi | 106,210,983 |
| 92 | Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) | Ununuzi wa huduma mbalimbali siku ya Ukimwi Duniani | 84,265,048 |
| 74 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma | Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Buhigwe | 17,708,600 |
| **Jumla** | | | **1,099,982,377** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Nimebaini kuwa, ununuzi uliofanyika bila ya ushindanishi umepungua katika Taasisi za Serikali toka Sh 4,643,629,092 hadi Sh 1,099,982,377 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita. Katika mwaka wa fedha 2018/19 jumla ya taasisi nane zilifanya ununuzi bila ya ushindani.

**Nashauri Menejimenti za Wizara, Idara na Sekretarieti ya Mikoa husika kuzingatia ushindanishi katika ununuzi ili kuweza kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi.**

## 9.7 Ongezeko la Gharama kwenye Huduma ya Mkandarasi Mshauri Sh. 13,262,485,816

Mnamo tarehe 11 Machi 2013, Wizara ya Maji (**Fungu Na. 49)** iliingia mkataba na Kampuni ya LAHMEYER GKW Consult GmbH ya Ujerumani kwa ajili ya huduma ya usimamizi wa uandaaji wa mikataba, usimamizi wa Miradi ya maji katika Miji ya Kigoma, Lindi na Sumbawanga kwa mkataba wenye thamani ya Pauni 2,885,375 sawa na Sh. 4,595,334,786 kwa tarehe 11 Aprili 2013). Muda wa mkataba ulikuwa miezi 46 kuanzia tarehe 11 Aprili 2013 hadi tarehe 10 Februari 2017.

Kanuni ya 319 ya Kanuni za Ununuzi ya mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016) inaitaka kila Taasisi inayofanya Ununuzi kuhakikisha kuwa utendaji wa mkandarasi unasimamiwa kulingana na mkataba.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mshauri alipewa nyongeza (addenda) 10 za mkataba. Nyongeza ya mwisho ikiwa ni ya tarehe 30 Agosti hadi 30 Oktoba 2020, kutokana na kuchelewa kwa kazi za msingi za Mkandarasi katika Miji ya Lindi, Kigoma na Sumbawanga. Kwenye nyongeza za mikataba, Mkandarasi Mshauri alilipwa Pauni 5,097,090 (sawa na Sh. 13,262,485,816 za Kitanzania kwa tarehe 30 Juni 2020) ikiwa ni sawa na 176.7% ya mkataba wa Mkandarasi Mshauri wa Pauni 2,885,375.

Nilijulishwa kuwa, kazi za Mkandarasi kwenye Miji ya Sumbawanga na Lindi zimekamilika isipokuwa Mji wa Kigoma ambapo kazi za ujenzi wa chanzo cha maji zinategemewa kuanza mwezi Juni, 2021.

Nilibaini kuwa, katika nyongeza ya mkataba ya Pauni 4,339,059 (85%) hakukuwa na kibali cha Mamlaka husika ya kuidhinisha Bajeti. Hii ni kinyume na kanuni ya 110(4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 (kama zilivyorekebishwa 2016) zinazoelekeza kuwa, mabadiliko ya mkataba yasiongeze thamani ya mkataba kwa zaidi ya asilimia kumi na tano ya mkataba wa awali bila kibali cha mamlaka inayoidhinisha bajeti.

Ongezeko la mkataba kiasi cha Pauni 5,097,090 ni hasara kwa Serikali maana fedha hizi zingeweza kutumika kwa ajili ya Miradi mingine ya maji kwa ajili ya manufaa ya Watanzania.

**Ninashauri kuwa Afisa Masuuli wa Wizara ya Maji aimarishe usimamizi wa miradi kwa Wakandarasi na Washauri ili kuhakikisha kuwa Miradi inakamilika bila kuchelewa ili kupata thamani ya fedha kwenye Miradi ya Maji**

### 9.8 Ununuzi wa Vifaa ambavyo Havikukaguliwa Sh 1,485,976,283

Kwa mujibu wa Kanuni ya 244(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) vifaa vilivyonunuliwa na Taasisi za ununuzi vinapaswa kukaguliwa ili kuthibitisha kama vinakidhi matakwa na viwango vilivyoainishwa katika mkataba. Aidha, Kanuni ya 245 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inamtaka Afisa Masuuli kuteua kamati ya ukaguzi na mapokezi ya vifaa ambayo itawajibika kukagua, kuthibitisha ubora wa vifaa au huduma na kupokea pindi zinaponunuliwa kutoka kwa Wazabuni

Katika Ukaguzi wangu nilibaini kuwa jumla ya taasisi nane za Serikali Kuu zilifanya ununuzi wa vifaa venye thamani ya Sh. 1,485,976,283 bila ya kukaguliwa ili kuhakiki ubora wake kuendana mkataba. Vilevile, Maafisa Masuuli hawakufanya uteuzi wa kamati za ukaguzi na mapokezi ya vifaa na huduma kama ilivyoelekezwa kwenye kanuni tajwa hapo juu kwa ajili ya kukagua vifaa pindi vinapopokelewa **Jedwali Na. 75** linaonesha orodha ya taasisi zilizohusika.

**Jedwali Na. 75: Vifaa Vilivyonunuliwa bila Kufanyiwa Ukaguzi**

| Fungu Na. | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | Ununuzi wa vifaa vya Tehama, Vifaa vya Ofisini, bendera na mahema | 967,729,908 |
| 78 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya | Ununuzi wa Vifaa vya Ofisini | 40,556,630 |
| 73 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | Ununuzi wa Vifaa vya ujenzi | 16,070,967 |
| 74 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma | Ununuzi wa Vifaa vya ujenzi | 24,640,813 |
| 88 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar Es Salaam | Ununuzi wa Kompyuta, Kompyuta mpakato na Mashine ya kurudufu | 18,192,017 |
| 86 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | Ununuzi wa Vifaa vya ujenzi na Ofisini. | 120,733,846 |

| Fungu Na. | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 25 | Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | Ununuzi wa vifaa vya Tehama ,samani za Ofisini na Kompyuta Mpakato | 77,224,390 |
| 13 | Kitengo cha Uchunguzi wa Fedha | Ununuzi wa Kanzi data, Samani na Mashine ya Kurudufu | 220,827,712 |
| **Jumla** | | | **1,485,976,283** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Aidha, tatizo la Kufanya Ununuzi wa Vifaa bila kukaguliwa limeongezeka kwa idadi ya taasisi. Hata hivyo, limepungua kwa kiasi ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/2019, ambapo taasisi saba za Serikali Kuu zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. 1,620,940,789 bila ya kukaguliwa.

Kupokea vifaa bila kukaguliwa na kukubaliwa na kamati ya ukaguzi na mapokezi ya vifaa na huduma kunaweza kukatoa fursa kwa Taasisi za umma kununua vifaa na huduma zisizokuwa na viwango au zisizofuata mahitaji ya ununuzi.

**Nawashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi za Serikali Kuu kuteua kamati ya mapokezi na ukaguzi wa vifaa na huduma pale inapotokea Taasisi husika imefanya ununuzi wa vifaa na huduma.**

## 9.9 Mafuta ya Magari na Vifaa Vilivyonunuliwa bila Kuingizwa kwenye Vitabu vya Stoo Sh. 1,034,263,676

Kanuni ya 198 na 203 ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2001 (kama zilivyorejewa mwaka 2004) zinaagiza kuwa vifaa vilivyonunuliwa, vilivyotolewa na bakaa vinapaswa kuingizwa kwenye kurasa tofauti katika vitabu vya stoo vikionyesha taarifa za ununuzi na matumizi.

Hata hivyo, wakati wa Ukaguzi wangu nilishindwa kujiridhisha na matumizi ya vifaa vya stoo na mafuta ya magari yenye thamani ya Sh. 1,034,263,676 katika taasisi 11 za Serikali Kuu. Hii ni kwa kuwa taasisi hizo hazikuingiza taarifa za vifaa vilivyonunuliwa katika rejista za stoo baada yakuvipokea. **Jedwali Na. 76** linaonyesha orodha ya taasisi husika.

**Jedwali Na. 76: Orodha ya Taasisi Zilizonunua Vifaa na Mafuta Bila Kuingizia kwenye Rejista za Stoo**

| Fungu Na. | Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| 53 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto | Ununuzi wa vipuri vya magari | 21,243,874 |
| 14 | Idara ya Uokoaji na Zimamoto | Ununuzi wa Vifaa vya Zima Moto na vifaa vya Ofisini | 575,221,094 |
| 62 | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano | Ununuzi wa Vifaa vya Ofisini | 15,242,966 |
| 49 | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Ununuzi wa vifaa vya Tehama na Mawasiliano | 21,207,000 |
| 63 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | Ununuzi wa kadi za CHF | 33,900,000 |
| 87 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi | 102,551,541 |
| 90 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi na Ofisini | 113,270,979 |
| 4 | Ofisi ya Rais-Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | Ununuzi wa Vifaa vya Ofisini | 36,071,991 |
| 74 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi | 90,674,610 |
| 88 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam | Ununuzi wa Mafuta ya Magari | 3,536,001 |
| 80 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | Ununuzi wa Mafuta ya Magari | 21,343,620 |
| **Jumla** | | | **1,034,263,676** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Aidha, ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/2019 nilibaini kupungua kwa kiasi kikubwa kwa taasisi kutokuingiza vifaa kwenye vitabu vya stoo ambapo mafuta na vifaa vyenye thamani ya Sh. 5,493,672,834 havikuingizwa katika vitabu vya stoo kwa mwaka wa fedha 2018/2019

Mafuta na Vifaa kutoingizwa kwenye vatabu vya stoo kunaweza kupelekea upotevu wa Mali za Serikali.

**Napendekeza Taasisi zote za Serikali Kuu zihakikishe zinaingiza vifaa na mafuta kwa wakati katika vitabu ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali katika kutoa huduma kwa wakati.**

### 9.10 Ununuzi Uliofanyika bila ya Kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni Sh. 1,560,986,067

Kwa mujibu wa kifungu Na. 35(2) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011(kama kilivyorekebishwa na Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka, 2016) pamoja na Kanuni ya 55 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa na Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka, 2016) vinaagiza ununuzi wa bidhaa na huduma kuidhinishwa na bodi ya Zabuni. Katika kukagua uzingatiaji wa vifungu hivi, nilibaini kuwa Taasisi 11 za Serikali Kuu zilifananya ununuzi wa bidhaa na huduma vyenye thamani ya Sh 1,560,986,067 bila ya kuidhinishwa na Bodi za Zabuni kinyume na vifungu tajwa hapo juu. **Jedwali Na. 77** linaorodhesha Taasisi zilizofanya ununuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni

**Jedwali Na. 77: Ununuzi Uliofanyika Bila ya Kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni**

| Fungu Na. | Taasisi | Malelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Ununuzi wa vifaa vya Ujenzi, vipuri vya Magari na vifaa vya pampu | 266,814,903 |
| 57 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Jeshi la kujenga Taifa | Ununuzi wa Vifaa vya Mawasiliano, Diski ya Kompyuta na kifaa cha kuhifadhia data | 51,145,200 |
| 62 | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano | Ununuzi wa vipuri vya Magari | 28,837,785 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | Ununuzi wa vifaa vya Ofisini pamoja na chakula na Viburudisho | 68,628,923 |
| 77 | Sekretarieti ya Mkoa wa | Ununuzi wa huduma za kurudufu mtihani wa Darasa | 121,120,052 |

| Fungu Na. | Taasisi | Malelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| | Mara | la saba pamoja na matengenezo ya Magari | |
| 78 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya | Ununuzi wa Chakula na Viburudisho | 11,501,280 |
| 90 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi ,vifaa vya Ofisini, dawa na mafuta ya gari | 661,785,903 |
| 46 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | Malipo ya kodi ya pango | 185,374,800 |
| 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | Ujenzi wa uzio - Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Ngorongoro | 12,895,000 |
| 72 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | Ununuzi wa vifaa mbalimbali vya Ofisini | 104,432,221 |
| 56 | Ofisi ya Rais-Usimamizi wa Nyaraka na Utunzaji wa Kumbukumbu | Ununuzi wa vifaa mbalimbali vya Ofisini | 48,450,000 |
| **Jumla** | | | **1,560,986,067** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Nilibaini kuendelea kuongezeka kwa kutozingatiwa kwa kifungu hiki cha Sheria katika taasisi za Serikali Kuu. Ununuzi uliofanyika bila ya idhini ya Bodi ya zabuni umeongezeka kwa Sh 1,101,304,571 toka Sh 459,681,496 mwaka 2018/19 hadi Sh 1,560,986,067 katika mwaka huu wa fedha.

**Nashauri Menejimenti za Taasisi husika kuzingatia kikamilifu Sheria ya Ununuzi wa Umma ili Bodi za Zabuni ziweze kufanya kazi zake za kuidhinisha ununuzi kama sheria inavyoagiza.**

## 9.11 Vifaa na Mali Zilizolipiwa lakini Hazikupokelewa Sh. 6,826,831,027

Katika Taasisi za Serikali Kuu nilizokagua, nilibaini ununuzi wa Vifaa na Mali zenye thamani ya Sh 6,826,831,027 zilizoagizwa na kulipiwa lakini hazikupokelewa. Makubaliano yalibainisha kuwa ununuzi ulipaswa kukamilika kati ya wiki mbili hadi miezi mitatu lakini Wazabuni walishindwa kutekeleza matakwa ya mikataba. Taasisi zilizohusika na ununuzi usiopokelewa zimeorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 76.**

**Jedwali Na. 78: Vifaa na Mali Zilizolipiwa Lakini Hazikupokelewa**

| Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---:|
| 52 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto | Ununuzi wa Magari Tisa(9) kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) | 1,090,654,835 |
| 99 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | Ununuzi wa Magari mawili Tisa na Pikipiki tatu kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) | 380,000,000 |
| 65 | Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu | Ununuzi wa Magari matano kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini-GPSA | 1,022,290,162 |
| 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | Ununuzi wa vifaa vya umeme | 41,134,760 |
| 3 | Tume ya Taifa ya mipango na matumizi ya Ardhi | Utengenezaji wa Kanzi data | 41,000,000 |
| 52 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto | Ununuzi wa vifaa vya Hospitalini | 4,251,751,270 |
| **Jumla** | | | **6,826,831,027** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/2019 Taasisi zilizolipia vifaa na Mali bila kupokelewa zimebaki saba. Hata hivyo kiasi cha fedha kilichohusika kimeongezeka toka Sh 587,652,750 kwa mwaka uliopita hadi kufikia Sh. 6,826,831,027. Hali hii inaashiria bado kuna upungufu katika kuzingatia makubaliano ya Mkataba katika ununuzi.

**Nashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa wazabuni wanazingatia vipengele vya mikataba walivyokubaliana pamoja na kukamilisha mikataba yao bila kuchelewa zaidi**

### 9.12 Ununuzi Bidhaa na Huduma Nje ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma(TANePS) Sh. 227,490,940

Kanuni ya 342(1&2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) inaziagiza Taasisi za ununuzi kuzingatia matumizi ya mfumo wa kielekitroniki katika ununuzi wa Umma. Pia kupitia Waraka Na 4 wa mwaka 2019, Wizara ya fedha inazitaka Taasisi zote za Umma kutumia mfumo wa kielekitroniki wa ununuzi kuanzia tarehe 1 Januari mwaka 2020.

Katika ukaguzi nilibaini kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki **(Fungu Na. 34**) ilianza kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Kielekitroniki kama ilivyoagizwa na Waraka tajwa hapo juu. Hata hivyo, Wizara ilifanya ununuzi wa bidhaa na huduma wa kiasi cha Sh. 227,490,940 nje ya Mfumo wa Ununuzi wa Kielekitroniki (TANePS).

**Kwa kuwa mfumo huu unaongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa Umma, naishauri Menejimenti ya Wizara kuhakikisha mchakato wa ununuzi unatumia mfumo wa kielekitroniki wa TANePS kama inavyoelekezwa na Waraka tajwa hapo juu.**

### 9.13 Kuchelewa Kukamilika kwa Kazi za Ujenzi, Ununuzi wa Bidhaa na Utoaji wa Huduma zenye Thamani ya Sh. 69,823,269,658

Ukaguzi wa utekelezaji wa miradi, ununuzi wa bidhaa na utoaji wa huduma ulibaini kuwa jumla ya Taasisi 15 za Serikali Kuu zilishindwa kukamilisha utekelezaji wa Mikataba baina yao na Wakandarasi/Wazabuni mbalimbali katika vipindi vilivyoainishwa katika Mikataba. Upungufu huu ulipelekea kutokamilika kwa wakati kwa baadhi ya miradi na kuchelewa kuletwa kwa bidhaa na utoaji wa huduma. Vilevile, ulisababisha kazi kufanyika chini ya kiwango.

Katika ukaguzi wangu nilibaini pia kuwa jumla ya miradi 21 yenye thamani ya Sh. 69,823,269,658 ilitekelezwa nje ya kipindi cha Makubaliano ya Mikataba. Nilibaini kuwa miradi hii kuchelewa kukamilika kwa kipindi kati ya mwezi mmoja na miaka 12 kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. XIX**

Maoni yangu ni kuwa kuchelewa kukamilika kwa Miradi kunaweza kupelekea ongezeko la gharama, kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, pamoja na kukosa thamani halisi ya fedha.

**Menejimenti za Taasisi husika zinashauriwa kuzingatia kanuni ya 114 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) katika usimamizi bora wa Mikataba. Pia, nazishauri Taasisi husika kufuatilia fedha Hazina ili kuweza kutekeleza miradi hiyo kwa wakati. Vilevile, napendekeza mikataba ifanyike kwa awamu ili kuweza kuiepusha Serikali na riba itokanayo na kuchelewa kulipa madai ya Wakandarasi.**

## 9.14 Mapungufu Yaliyobainika katika Utekelezaji wa Miradi Mbalimbali.

### 9.14.1 Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi Kikombo-Dodoma Sh. 30,246,348,255

Ukaguzi ulibaini kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (**Fungu Na. 38**) linafanya ujenzi wa Makao Makuu Kikombo-Dodoma kwa mfumo wa nguvu kazi (Force Acount) kwa makadirio ya gharama ya Sh 30,246,348,255 kwa muda wa miezi 24 toka mwezi Machi, 2020. Katika ukaguzi uliofanyika eneo la mradi tarehe 19 Oktoba 2020, nilibaini kasi ndogo katika utekelezaji wa mradi ambapo kazi nne zilizopaswa kukamilika kabla ya tarehe 8 Oktoba, 2020 hazikuwa zimekamilika. Kazi hizo wakati wa ukaguzi zilikuwa katika hatua zifuatazo, zege la msingi (82%), kufunga mbao kwenye mkanda wa msingi (42%), ujenzi wa ukuta wa msingi (42%), kurudishia kifusi na kushindilia (20%).

Vilevile, nilibaini mshauri wa mradi aliyeteuliwa (Idara ya Ushauri ya Wizara ya Ulinzi) kusimamia mradi hakuwahi kufika eneo la mradi wala kutoa taarifa ya maendeleo ya mradi. Ni maoni yangu kuwa kukosekana kwa ripoti ya mshauri juu ya maendeleo ya mradi kunamaanisha kuwa Idara ya Ushauri ya Wizara ya Ulinzi haikutoa huduma za ushauri ipasavyo.

**Nashauri ujenzi wa Mradi huu kutekelezwa kama ilivyopangwa kwenye mpango kazi. Vilevile, nashauri kuwe na Makubaliano ya kimkataba kati ya Jeshi na Idara ya Ushauri ya Wizara ya Ulinzi.**

### 9.14.2 Mapungufu Yaliyobainika katika Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo Mbalimbali ya Mahakama yenye Thamani ya Sh. 40,950,961,181

Mahakama ya Tanzania (**Fungu Na. 40**) ilianzisha Miradi ya ujenzi wa Mahakama 42 kati ya mwaka 2017 na 2020 kwa gharama ya Sh 40,950,961,181. Wakati wa Ukaguzi nilibaini kuwa jumla ya Mahakama 21 zimekamilika na zinatumika, Mahakama 11 zimekamilika na Mahakama kumi zipo katika hatua za mwisho za kukamilika. Pia, nilibaini kuwa Mahakama iliingia Mikataba na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Chuo cha Ardhi, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) pamoja na Kampuni ya HAB kwa ajili ya usimamizi wa Miradi tajwa hapo juu kwa mujibu wa kanuni ya 252 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka, 2013 (na marekebisho yake ya mwaka, 2016)

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini mapungufu mbalimbali katika Miradi yote 42. Mapungufu hayo yamebainika kwenye mfumo wa maji taka, ukamilishaji wa paa, mfumo wa umeme, umaliziaji wa kuta na mfumo wa ukusanyaji maji. Mapungufu haya yalitokana na usimamizi usioridhisha wa Wakandarasi Washauri.

Pia, nilibaini kuwa usanifu wa Miradi hii ulikuwa na mapungufu ambapo majengo hayakuwa na mfumo wa utambuzi wa majanga ya moto, mfumo wa umeme wa dharura pamoja na mfumo wa TEHAMA. Kwa maoni yangu, Mahakama haikupata thamani halisi ya fedha katika utekelezwaji wa miradi hii kutokana na mapungufu yaliyobainika hapo juu.

**Naishauri Menejimenti ya Mahakama kuhakikisha mapungufu yote yaliyobainika katika ukaguzi yanafanyiwa kazi ili kuhakikisha majengo yanadumu kwa muda mrefu. Pia, iongeze umakini katika usimamizi wa Miradi inayoendelea ili mapungufu yaliyobainika yasijirudie**

## 9.15 Ukaguzi wa Kina wa Ununuzi na Usimamizi wa Mikataba

Ukaguzi wa kina wa usimamizi wa Mikataba ulifanyika katika Ofisi 36 za Wilaya za RUWASA katika mikoa 19. Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kupima kama kulikuwa na mifumo madhubuti katika kusimamia Miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ili kupata matumizi bora ya rasilimali zilizotengwa na kufikia malengo yaliyo kusudiwa. **Jedwali Na. 79** lina taarifa ya Wilaya zilizohusika na ukaguzi huu.

**Jedwali Na. 79: Wilaya zilizofanyiwa Ukaguzi wa Kina wa Usimamizi wa Mikataba**

| Na. | Mkoa | Ofisi Za Ruwasa Wilaya Zilizokaguliwa | Mikataba/Miradi Iliyokaguliwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | Arumeru & Karatu | 2 |
| 2. | Dodoma | Bahi & Mpwapwa | 2 |
| 3. | Geita | Bukombe & Geita | 2 |
| 4. | Kagera | Missenyi & Biharamulo | 2 |
| 5. | Katavi | Tanganyika & Mpanda | 2 |
| 6. | Kigoma | Kigoma & Ujiji | 2 |
| 7. | Kilimanjaro | Moshi & Rombo | 4 |
| 8. | Lindi | Lindi & Ruangwa | 2 |
| 9. | Mbeya | Chunya & Mbarali | 3 |
| 10. | Morogoro | Mvomero | 1 |
| 11. | Mtwara | Masasi & Tandahimba | 3 |
| 12. | Mwanza | Magu & Sengerema | 2 |
| 13. | Njombe | Njombe & Wanging'ombe | 2 |
| 14. | Pwani | Mkuranga | 2 |
| 15. | Rukwa | Kalambo & Sumbawanga | 2 |
| 16. | Ruvuma | Namtumbo & Songea | 2 |
| 17. | Singida | Ikungi & Singida | 2 |
| 18. | Tabora | Kaliua & Nzega | 2 |
| 19. | Tanga | Lushoto & Mkinga | 2 |
| **JUMLA** | | | **41** |

*Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Mapungufu yaliyoibuliwa wakati wa ukaguzi ni kama inavyoelezwa hapa chini.

### 9.15.1 Kutokuwapo kwa Nyaraka za Ununuzi kwa Miradi yenye Thamani ya Sh. 429,435,913

Kanuni ya 15 (1) (b-d) na (6) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 (kama zilivyorekebishwa za mwaka 2016) inahitaji taasisi zinazofanya ununuzi kutunza taarifa za michakato ya ununuzi ikiwa ni pamoja na nyaraka za mialiko ya zabuni, tathmini ya zabuni na taratibu za utoaji tuzo kwa muda usiopungua miaka mitano tangu tarehe ya kukamilika kwa mkataba.

Nimekagua majalada ya zabuni ya Mradi wa kusambaza maji katika kijiji cha Lakuyi kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora yenye thamani ya Sh. 429,435,913 na kubaini kutokuwapo kwa matangazo ya zabuni, rejista za kupokelea zabuni, risiti za kukiri mapokezi, nyaraka za ufunguzi wa zabuni, nyaraka zilizowasilishwa na Wazabuni, mihutasari ya Bodi ya Zabuni iliyoidhinisha tuzo ya mkataba na nyaraka za upekuzi wa

mkataba. Nyaraka zilizokosekana zimepelekea ukaguzi wa Miradi hiyo kutofanyika kwa ufanisi.

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa nyaraka za michakato ya zabuni kumepunguza mawanda ya ukaguzi. Aidha, hali hii imepelekea ukiukaji wa Kanuni za Ununuzi wa Umma ambazo ni uaminifu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji.

**Napendekeza kuwa uongozi wa RUWASA uwasilishe nyaraka zilizokosekana Ofisini kwangu kwa ajili ya ukaguzi na kwa siku zijazo kuhakikisha nyaraka zote za ununuzi zinahifadhiwa vyema kwa ajili ya mapition na ukaguzi pindi zitakapohitajika.**

### 9.15.2 Mapungufu katika Dhamana za Malipo ya Awali yenye Thamani ya Sh. 609,487,673

Kifungu Na. 53.2 cha masharti ya jumla ya Mkataba (General Conditions of Contract (GCC) kinawataka Wakandarasi kutumia malipo ya awali kulipia vifaa, mitambo, bidhaa na gharama za kuleta vifaa vinavyohitajika katika utekelezaji wa Mikataba na kuonesha matumizi ya malipo hayo kwa kuwasilisha nakala za ankara au nyaraka kwa Meneja wa Mradi. Kwa upande mwingine kifungu Na. 25 cha masharti mahsusi ya mkataba (Specific Conditions of Contract (SCC) kinahitaji malipo ya awali kuwa 20% ya mkataba na yalipwe ndani ya siku 28 baada ya kuwasilishwa kwa dhamana inayokubalika, wakati kifungu Na. 24 kinatoa kiwango kilichokubaliwa kukatwa kwenye malipo kuwa 20% katika hati za malipo kwa mkandarasi. Aidha, kifungu Na. 59.1 cha masharti ya jumla ya mkataba na 24 cha masharti mahsusi ya mkataba vinamtaka Mkandarasi kuwasilisha dhamana ya Benki isiyo na masharti yenye kiasi sawa na malipo ya awali ambayo itabaki kuwa hai hadi malipo yote yatakaporejeshwa.

Katika ukaguzi huu nimebaini mikataba mitatu yenye thamani ya Sh. 2,431,663,902 ikiwa na mapungufu katika dhamana za malipo ya awali ziliyowasilishwa, malipo na urudishwaji wake. Maelezo zaidi yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 80**

**Jedwali Na. 80: Mikataba yenye Hati za Dhamana na Malipo ya Awali yenye Mapungufu**

| Mkoa | Ofisi ya Wilaya | Jina la Mradi | Namba ya Mkataba | Kiasi Cha Mkataba (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| Mtwara | Masasi | Ukarabati wa Mradi wa kusamba za maji kwa kijiji cha mwena hadi Liloya | LGA/083/ 2016 LOT 01 | 857,962,800 | Malipo ya awali Sh. 111,885,700 hayakukatwa kwenye malipo ya mkandarasi. |
| Lindi | Ruangwa | Ujenzi wa Mradi wa kusamba za maji kijiji cha Chienjele | LGA /RDC/056 /WSDP/W /2017-2018/44 | 565,868,727 | Dhamana ya malipo ya awali iliisha muda wake kabla Sh. 29,868,960 haijakatwa kutoka kwa Mkandarasi. |
| Mbeya | Mbarali | Ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji kijiji cha Luduga-Mawindi-Awamu ya I | DM/RUWASA/RWS/ 1/LM.Lot 1/vol. Mimi | 1,007,832,375 | Nyaraka za matumizi ya malipo ya awali Sh. 467,732,977.4 hazikuwasilishwa kwa msimamizi wa Mradi. |
| **Jumla** | | | | **2,431,663,902** | **609,487,637** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kwa maoni yangu, kuisha kwa muda wa dhamana za malipo ya awali kabla ya kurudisha fedha iliyolipwa na kutokukata malipo ya awali kwa wakandarasi wakati wa malipo yao kunaiweka RUWASA katika hatari ya kupoteza fedha za Umma pale wakandarasi wanaposhindwa kuendelea na mkataba. Aidha, wasimamizi wa miradi kushindwa kufuatilia kwa makini mkataba kunaweza kusababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa Mradi.

**Napendekeza RUWASA ikate fedha ya malipo ya awali kikamilifu kutoka kwa Wakandarasi katika malipo yao yanayofuata. Aidha, kwa siku zijazo, RUWASA ihakikishe dhamana zinatolewa kwa kipindi chote cha kurudisha fedha za malipo ya awali ili kuepuka upotevu wa fedha za**

Umma; na Wakandarasi husika wawasilishe kwa wasimamizi wa miradi ankara zote zitokanazo na matumizi ya malipo ya awali kwa ajili ya tathmini.

### 9.15.3 Mikataba Iliyotekelezwa Bila ya Kuwapo kwa Dhamana za Utendaji Sh. 14,578,220,387

Kanuni ya 29 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inahitaji Taasisi zinazofanya ununuzi kuwataka Wazabuni walioshinda zabuni kuwasilisha dhamana za utendaji ili kuhakikisha mikataba inatekelezwa kwa uaminifu, na malipo ya wafanyakazi wote, wasambazaji, mafundi na wakandarasi wasaidizi wa Mradi (kama wapo) yanafanyika kwa uaminifu.

Nimekagua Majalada ya Mikataba katika Ofisi tano za Wilaya za RUWASA na kubaini kuwa mikataba yenye thamani ya Sh. 14,578,220,387 ilitekelezwa bila dhamana za utendaji kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 81**

**Jedwali Na. 81: Mikataba Iliyotekelezwa Bila Dhamana za Utendaji**

| MKOA | OFISI YA WILAYA | NAMBA YA MKATABA | MAELEZO YA MKATABA | GHARAMA YA MKATABA (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| Njombe | Njombe | Ujenzi wa mfumo wa kusambaza maji katika vijiji vya Usetule-Mahongole | LGA/166/2018/ 2019/W/01 | 7,996,231,305 |
| Mtwara | Masasi | Ukarabati wa Mradi wa maji vijiji vya Mwena hadi Liloya | LGA/083/2016/ 2017/W/21 LOT 01 | 4,471,710,595 |
| Singida | Ikungi | Ujenzi wa mfumo wa kusambaza maji katika Kijiji cha Mtunduru | LGA/146/2018/ 2019/W/02 | 405,007,269 |
| Dodoma | Mpwapwa | Ujenzi wa Mradi wa kusambaza maji katika kijiji cha Kidenge | LGA/023/2016/ 2017/W/21 | 1,070,460,729 |
| Katavi | Tanganyika | Ujenzi wa Mradi wa kusambaza maji katika kijiji cha Kabungu | LGA.099/2017/ 2018/W/WATER /02/Lot 1 | 634,810,489 |
| **Jumla** | | | | **14,578,220,387** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa hati za dhamana za utendaji kunaiweka RUWASA katika hatari ya kupoteza rasilimali zake kwa miradi inayoendelea

endapo wakandarasi watashindwa kutekeleza kikamilifu mikataba au wakisitisha utekelezaji wa miradi husika.

**Napendekeza katika siku zijazo, RUWASA ihakikishe mikataba yote inakuwa na hati za dhamana za utendaji ili kulinda maslahi yaliyopo katika utekelezaji wa miradi hiyo kwa ufanisi.**

### 9.15.4 Mapungufu katika Dhamana za Utendaji kwa Mikataba yenye Thamani ya Sh. 14,246,041,291

Kifungu Na. 54 cha masharti ya jumla ya Mkataba, kinahitaji hati za dhamana ya utendaji kufidia kipindi chote cha Mkataba na kuwa hati hizo ziwe hai hadi mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kutolewa cheti cha kukamilika Mradi. Aidha, kifungu hiki kimeongeza kuwa, dhamana ya utendaji inapaswa kutolewa kwa kiasi na aina, na kwa benki au dhamana inayokubalika na mwajiri.

Nimebaini utekelezaji wa Mikataba nane yenye thamani ya Sh. 14,246,041,291ambayo dhamana zake za utendaji zilikwisha muda wake, hazikuwa na muda wa kudhamini utekelezaji wa Mkataba, na kutolipwa kiasi cha dhamana baada ya kusitisha mkataba. Aidha, nimebaini mkataba mmoja wenye thamani ya Sh. 1,041,021,700 ambao thamani iliyopo katika hati ya dhamana ya utendaji ilikuwa ndogo kuliko kiasi kilichoainishwa kwenye mkataba kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 82**

**Jedwali Na. 82: Mikataba ambayo Dhamana Zake za Utendaji zina Mapungufu**

| Mkoa | Ofisi ya Wilaya | Namba ya Mkataba | Maelezo ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| Rukwa | Sumbawanga | LGA/097/2017/2018/WS/W/05 | Ujenzi wa bwawa la maji Kijiji cha Ikozi awamu ya II | 2,943,086,780 | Dhamana ya utendaji iliisha muda wake wakati ujenzi wa Mradi unaendelea. |
| Kigoma | Kigoma | LGA/043/2016/2017/W/15 | Ujenzi wa Mradi wa kusambaza maji Vijiji vya Kaseke, Kimbwela na | 1,163,496,000 | Dhamana ya utendaji haikuwa na muda wa kudhamini utekelezaji wa Mkataba. |

| Mkoa | Ofisi ya Wilaya | Namba ya Mkataba | Maelezo ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Nyamoli | | |
| Katavi | Mpanda | LGA/161/2017-2018/BHL/W/05/LOT 2 | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa Vijiji vya Mtakuja na Songambele | 600,702,298 | Dhamana ya utendaji iliisha muda wake wakati ujenzi wa Mradi unaendelea. |
| Ruvuma | Songea | LGA/182/HQ/W/2016/2017/06 | Uboreshaji wa Mradi wa maji vijiji vya Madaba, Mtepa, Lituta na Kipingo Wilayani Madaba | 1,041,021,700 | Sh. 74,815,420 kiasi cha dhamana hakikulipwa baada ya kusitisha Mkataba. |
| | | | | | Dhamana ya utendaji ya Sh. 74,815,420 badala ya Sh. 312,306,510 iliwasilishwa na kusababisha upungufu wa Sh. 237,491,090. |
| Lindi | Lindi | LGA/053/2017/2018/HQ/W/35/LOT 2 | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa ajili ya vijiji vya Cheleweni, Narunyu, tandangongoro, na Muungano | 2,726,843,629 | Dhamana ya utendaji iliisha muda wake wakati ujenzi wa Mradi unaendelea. |
| Mbeya | Chunya | LGA /075/W/2017/2018/29 | Ujenzi wa Mfumo wa Maji kwa Mji Mdogo wa Makongolosi | 2,809,674,259.52 | Dhamana ya utendaji iliisha kabla ya kumalizika kwa kipindi cha matazamio (yaani kutoa cheti cha ukamilishaji). |

| Mkoa | Ofisi ya Wilaya | Namba ya Mkataba | Maelezo ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| Tanga | Wilaya ya Lushoto | LDC /LGA/004/RWSSP/AWAMU ya I&II/2013-2014/W/11 | Ujenzi wa Mradi wa maji katika vijiji vya Shume, Manolo na Madala | 2,961,216,624.30 | Dhamana ya utendaji iliisha muda wake wakati ujenzi wa Mradi unaendelea. |
| **Jumla** | | | | **14,246,041,291** | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kwa maoni yangu, kumalizika muda wa dhamana za utendaji, dhamana za utendaji kuwa na thamani ndogo kuliko inayotakiwa au kutoainisha kipindi cha udhamini na kushindwa kurejesha kiasi kilicho dhaminiwa baada ya kusitishwa kwa mkataba, kumeiweka RUWASA katika hatari ya kupoteza fedha endapo Wakandarasi watashindwa kutekeleza miradi hiyo.

**Napendekeza RUWASA ihakikishe, Wakandarasi wanahuisha dhamana za utendaji. Mbali na hilo, katika siku zijazo, Mikataba yote iwe na dhamana za utendaji kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba ili kuepuka upotevu wa rasilimali za Umma na pia kuweza kupata thamani ya fedha katika miradi hiyo.**

### 9.15.5 Miradi Iliyotekelezwa bila ya Kuwekewa Bima Sh. 34,615,031,380

Kifungu Na. 7 cha masharti mahsusi ya mkataba na Kifungu Na. 14.1 cha masharti ya jumla ya mkataba vinahitaji wakandarasi kuweka bima kwa ajili ya vihatarishi mbalimbali kutoka tarehe ya kuanza kazi hadi mwisho wa kipindi cha matazamio ya mkataba.

Nimebaini Wakandarasi 10 kuwa walitekeleza Mikataba katika Ofisi nane za Wilaya za RUWASA bila kuweka bima ya mitambo, vifaa na wafanyakazi katika Miradi hiyo kama ilivyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 83**

## Jedwali Na. 83: Mikataba Iliyotekelezwa Bila Kuwekewa Bima

| MKOA | OFISI YA WILAYA | JINA LA MRADI | NAMBA YA MKATABA | GHARAMA YA MKATABA (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| Katavi | Tanganyika | Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza Maji Katika Kijiji cha Kabungu | LGA.099/2017/2018/W/WATER/02/Lot 1 | 634,810,489 |
| Rukwa | Sumbawanga | Ujenzi wa bwawa kwa ajili ya Kijiji cha Ikozi awamu ya II | LGA/097/2017/2018/WS/w/05 | 2,943,086,780 |
| Kigoma | Kigoma | Ujenzi wa Kusambaza miundombinu ya maji katika Vijiji vya Kaseke, Kimbwela na Nyamoli | LGA/043/2016/2017/W/15 | 1,163,496,000 |
| Singida | Singida | Ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha Mungumaji | LGA/115/SMC/2018/2019/W/NO.1 | 339,375,031 |
| Njombe | Wanging'ombe | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa Vijiji viwili Igando- Kijombe | LGA/153/2017/2018/W/01 | 12,437,407,360 |
| | Njombe | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa ajili ya Usatule-Mahongole | LGA/166/2018/2019/W/01 | 7,996,231,305 |
| Mbeya | Chunya | Ujenzi wa Mradi wa Maji kwa Mji Mdogo wa Makongolosi | LGA /075/W/2017/2018/29 | 2,809,674,260 |
| Tanga | Lushoto | Ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha Shume/Manolo/Madala | LDC /LGA/004/RWSSP/AWAMU ya I&II/2013-2014/W/11 | 2,961,216,624 |
| Pwani | Mkuranga | Ujenzi wa Mradi wa maji katika Kijiji cha Mwanambaya | LGA/012/WS/2017/2018/w/01-02 | 2,347,737,221 |
| | | Ujenzi wa Mradi wa maji katika Kijiji cha Mkerezange | LGA/012/WS/2017/2018/w/01-03 | 981,996,310 |
| **Jumla** | | | | **34,615,031,380** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa bima kumeiweka RUWASA katika hatari ya ucheleweshwaji wa miradi endapo matukio hatarishi yatatokea.

**Napendekeza RUWASA ihakikishe kuwa katika siku zijazo, Miradi inakatiwa Bima ili kuepuka madhara kama vile kuchelewa katika utekelezaji pamoja na upotevu wa rasilimali za Umma.**

### 9.15.6 Miradi Iliyotekelezwa Bila Vifaa vya Sh. 1,070,460,729 Kufanyiwa Majaribio ya kKuthibitisha Ubora

Kanuni ya 246 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inahitaji kwa suala la kiufundi au kisayansi bidhaa au vifaa vitumwe kwa mtaalamu au mtu anayestahili kwa ajili ya vipimo na majaribio ya ubora. Vilevile, matakwa ya kuthibitisha ubora wa vifaa kwa mkataba Na. LGA/023/2016/2017/W/21 wenye thamani ya Sh. 1,070,460,729 kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha Kidenge, Wilayani Mpwapwa yamefafanuliwa katika ‘’British Standard (BS 6920) (Suitainability of non-metallic material).

Mapitio ya majalada ya mkataba yalibaini kutokuwapo kwa taarifa za majaribio ya kuthibitisha ubora wa vipimo vya mabomba ya maji huku Mkandarasi akiwa tayari ameshalipwa kiasi cha Sh. 648,235,950 kwa kazi zilizotekelezwa.

Kwa maoni yangu, kutokuwapo kwa taarifa za majaribio na vipimo vya mabomba ya maji kuthibitisha ubora kunaashiria kutofanyika kwa majaribio ya vifaa vya ujenzi. Hivyo, kuiweka RUWASA katika hatari ya kutumia vifaa duni ambavyo vinaweza kuathiri utekelezaji wa Mradi na kusababisha upotevu wa fedha za Serikali.

**Napendekeza kwa siku zijazo RUWASA ihakikishe upimaji wa vifaa vinavyotumika katika kutekeleza miradi ya maji unafanyika kama inavyotakiwa ili kuongeza ubora wa kazi za ujenzi zinazofanyika na hivyo kukidhi mahitaji ya miradi husika**

### 9.15.7 Kazi Zilizotekelezwa na Kulipwa bila Kuthibitishwa Sh. 716,936,724

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016) inahitaji Taasisi zinazofanya ununuzi kuidhinisha malipo kulingana na vipimo na uthibitisho, katika vipindi au hatua zilizooneshwa katika Mikataba.

Mapitio ya hati za malipo na majalada ya Mikataba yalibaini kuwa Ofisi mbili za Wilaya za RUWASA zililipa Sh. 716,936,724 kwa Wakandarasi kwa kazi zilizofanyika. Hata hivyo, hakukuwa na vipimo (measurement sheets) ambavyo vinathibitisha kiasi cha kazi ambazo zimetekelezwa na kulipwa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 84**

**Jedwali Na. 84: Kazi Zilizotekelezwa na Kulipwa Bila Kuthibitishwa**

| MKOA | OFISI YA WILAYA | JINA LA MRADI | NAMBA YA MKATABA | GHARAMA YA MKATABA (Sh.) | KIASI KILICHOULIZWA |
|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | Mpwapwa | Ujenzi wa Mradi wa kusambaza maji katika kijiji cha Kidenge | LGA/023/2016/2017/W/21 | 1,070,460,730 | 648,235,950 |
| Singida | Ikungi | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa ajili ya Kijiji cha Mtunduru | LGA/146/2018/2019/W/02 | 405,007,269 | 68,700,774 |
| **Jumla** | | | | **1,475,467,999** | **716,936,724** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Kwa maoni yangu, kulipa kazi zilizotekelezwa bila kuzithibitisha kunaweza kusababisha malipo zaidi au malipo kwa kazi ambazo hazikufanyika na hivyo kupoteza fedha za umma.

**Napendekeza RUWASA itoe ushahidi unaoonyesha kuwa Wakandarasi walistahili malipo kwa kazi hizo ambazo hazikupimwa. Aidha, katika siku zijazo RUWASA ikague na kupima kiasi cha kazi zilizotekelezwa kabla ya kuthibitisha na kufanya malipo ili kuepuka malipo kwa kazi ambazo hazikufanyika.**

### 9.15.8 Kutoidhinishwa kwa Ununuzi na Mabadiliko ya Mikataba yenye Thamani ya Sh. 747,496,754

Kanuni ya 110(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) inasema "mapendekezo ya mabadiliko kama kuongeza au kupunguza kazi ambayo si ya lazima au yanayotoka nje ya mkataba, na ambayo hubadilisha mawanda, kiwango au lengo la mkataba husika, yanatakiwa yapelekwe kwa Bodi ya Zabuni kabla maelekezo hayajatolewa kwa Mkandarasi". Aidha Kanuni ya 55(2) inahitaji Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kupeleka ununuzi na maelezo yake kwa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kuidhinishwa.

Nilikagua Majalada ya Mikataba na kubaini mabadiliko ya mkataba ya Sh. 615,725,019 ambayo yalifanyika bila idhini ya Bodi za Zabuni. Aidha, nimebaini Ofisi tatu za Wilaya ya Arumeru, Karatu na Sengerema ambapo Bodi za Zabuni hazikuidhinisha ununuzi wa Sh. 131,771,735. Maelezo zaidi yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 85**

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

## Jedwali Na. 85: Mikataba yenye Ununuzi na Tofauti Zisizoidhinishwa na Bodi ya Zabuni

| Mkoa | Ofisi ya Wilaya | Jina la Mradi | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Tofauti (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | Karatu | Ukarabati wa Mradi wa kusambaza maji Getamock | 2019/20 'FORCE ACCOUNT' | 82,782,671 | 62,093,895 | RUWASA Ililipa Sh. 62,093,895 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni. |
| | Arumeru | Ukarabati wa Mradi wa Maji wa PBR katika Kijiji cha Tarakwa | 2019/20 'FORCE ACCOUNT' | 42,000,000 | | |
| Katavi | Mpanda | Ujenzi wa Mradi wa Kusambaza Maji Katika Kijiji cha Kabungu. | LGA.099/2017 /2018/W/WA TER/02/Lot 1 | 634,810,489 | 105,955,829 | Kazi za ziada za Sh. 105,955,829 zilizofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni. |
| Kagera | Biharamulo | Utafiti wa maji na Uchimbaji wa Visima 12 vya maji katika Kijiji cha Kagoma | LGA/032/2018 /2019/HQ/WS DP/W/01-LOT 3 | 328,440,000 | 301,070,000 | Mkataba uliainisha uchimbaji wa visima 12 kijiji cha Kagoma. Kisima kimoja tu kilichimbwa kagoma wakati visima 11 vilichimbwa lusahunga, Nyakanazi, Nyambele na Ntumagu bila idhini ya Bodi ya Zabuni. |
| Dodoma | Bahi | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa Kijiji cha Kimara Wilayani Bahi | LGA/024/2017 /2018/W/02-LOT II | 637,897,271 | 50,420,000 | Meneja wa Wilaya aliidhinisha mabadiliko ya mkataba ya Sh. 50,420,000 kwa mkandarasi bila idhini ya bodi ya Zabuni. |
| Mwanza | Sengerema | Ujenzi wa kisima cha Kasisa | FORCE ACCOUNT | 321,536,644 | 69,677,840 | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi vya Sh. 69,677,840.2 haukuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. |
| Mbeya | Mbarali | Ujenzi wa Mradi wa Maji Luduga Mawindi-Lot 2 | DM/RUWASA/ RWS/1/LM.Lot 2/vol. Mimi | 3,683,571,612 | 151,079,190 | Mabadiliko ya Sh. 151,079,190 hayakuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. |
| Tanga | Mkinga | Ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha Mwakijembe | LGA/133/2015 - 2016/HQ/W/2 0 | 1,742,436,894 | 7,200,000 | Mkandarasi alitumia bomba la 'Unplasticized Polyvinyl Chloride (UPVC)' badala ya bomba la DI lililoainishwa katika mkataba bila idhini ya meneja wa Mradi wala Bodi ya Zabuni. |
| **Jumla** | | | | **7,473,475,581** | **747,496,754** | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kwa maoni yangu, ununuzi na mabadiliko yaliyofanywa baada ya kusaini mikataba bila idhini ya Bodi za Zabuni yamefanyika kinyume na taratibu na yanaweza kusababisha ununuzi wa vifaa duni na kazi isiyo na ubora na kusababisha upotevu wa fedha za Umma.

**Napendekeza kwamba katika siku zijazo, RUWASA ihakikishe mabadiliko ya Mkataba na ununuzi ya vifaa yanaidhinishwa na Bodi za Zabuni, vinginevyo kuwe na idhini baada ya ununuzi huo(retrospective approval).**

### 9.15.9 Ucheleweshwaji wa Malipo ya Sh. 7,677,733,256 na Kutolipwa kwa Sh. 3,948,025,764 kwa Kazi Zilizotekelezwa na Wakandarasi

Kanuni ya 44(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inasema, "kwa madhumuni ya kusaidia na kukuza makampuni ya ndani na kuyawezesha Makampuni hayo kutimiza majukumu yao ya kandarasi, Taasisi zinazofanya ununuzi zihakikishe malipo kwa wazabuni yanafanyika kwa wakati". Aidha, Kifungu Na. 51.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba yaliyopo katika Mwongozo wa Nyaraka za Zabuni za mwaka 2018 kinataka waajiri walipe Wakandarasi kiasi kilichothibitishwa na wasimamizi wa miradi hiyo ndani ya siku 28 tokea tarehe ya kila hati. Malipo yatakayochelewa yatatozwa riba katika malipo yanayofuata kwa kiwango cha riba cha mikopo ya kibiashara kilichopo kwa wakati huo.

Mapitio ya Mikataba 41 yalibaini kuwa katika Mikataba 19 (45% ya Mikataba iliyokaguliwa) wakandarasi waliomba madai ya kazi zilizokamilika zenye thamani ya Sh. 11,625,759,020. Hata hivyo, malipo ya Sh. 7,677,733,256 yalichelewa kulipwa kwa siku 17 hadi siku 720 na Sh. 3,948,025,764 hazikulipwa hadi wakati wa ukaguzi huu (Disemba 2020). Hali ya ucheleweshwaji wa malipo imeongezeka kwa asilimia 268 kutoka Sh. 3,160,163,746 mwaka jana hadi Sh. 11,625,759,020 mwaka huu. Angalia maelezo katika **Jedwali Na. 86**

## Jedwali Na. 86: Mikataba ambayo Malipo Yalichelewa Kufanyika au Kutolipwa Kabisa

| Mkoa | Ofisi ya Wilaya | Jina la Mradi | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Kiasi Kinachodaiwa (Sh.) | Kiasi Kilicholipwa (Sh.) | Kiasi Ambacho Hakijalipwa (Sh.) | Ucheleweshaji (Siku) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimanjaro | Moshi | Ujenzi wa Mradi wa Maji Wa Tella Mande | 905,475,000 | 352,237,000 | 352,237,000 | - | > 62 |
| Katavi | Tanganyika | Ujenzi wa Mradi wa Maji Katika Kijiji cha Kabungu | 634,810,489 | 128,021,829 | 128,021,829 | - | 360 |
| Rukwa | Sumbawanga | Ujenzi wa bwawa la maji kwa ajili ya Kijiji cha Ikozi awamu ya II | 2,943,086,780 | 1,178,845,709 | 1,178,845,709 | - | 104-188 |
| | Kalambo | Ujenzi wa Mradi wa Maji Mambwekenya | 651,008,400 | 141,838,456 | 141,838,456 | - | 73 |
| Kigoma | Ujiji | Ujenzi wa Mradi wa Maji kwa Kijiji cha Mgumile | 721,438,645 | 59,415,800 | 59,415,800 | - | 720 |
| Dodoma | Bahi | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa Kijiji cha Kimara Wilayani Bahi | 637,897,271 | 346,340,718 | 280,765,758 | 65,574,960 | 60-162 |
| Mwanza | Magu | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa vijiji vya Nsola-Bubinza | 1,001,742,500 | 392,942,295 | 206,609,400 | 186,332,895 | 180-330 |
| Morogoro | Mvomero | Ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha Lubungo | 430,104,045 | 377,438,519 | 261,200,470 | 116,238,049 | 65-143 |
| Tabora | Kaliua | Mradi wa Maji katika kijiji cha Wachawaseme-Kaliua | 535,729,732 | 286,412,381 | 223,568,205 | 62,844,176 | 17-234 |
| Singida | Singida | Ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha Mungumaji | 339,375,031 | 280,454,624 | - | 280,454,624 | >150 |
| Ruvuma | Namtumbo | Mradi wa maji Kijiji cha Likuyusekamaganga | 4,915,864,910 | 1,243,855,345 | 1,063,39,2291.50 | 180,463,053 | 80-273 |
| Lindi | Lindi | Ujenzi wa Mradi wa maji vijiji vya Cheleweni, Narunyu, tandangongoro na Muungano | 2,726,843,629 | 694,922,395 | 694,922,395 | - | 120-210 |
| | Ruangwa | Ujenzi wa Mradi wa maji Chienjele. | 565,868,727 | 277,878,687 | 277,878,687 | - | 92-152 |
| Njombe | Wanging'o | Ujenzi wa Mradi wa maji Vijiji | 12,437,407,360 | 1,821,437,422 | 1,821,437,422 | | 108 |

| Mkoa | Ofisi ya Wilaya | Jina la Mradi | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Kiasi Kinachodaiwa (Sh.) | Kiasi Kilicholipwa (Sh.) | Kiasi Ambacho Hakijalipwa (Sh.) | Uchelewes haji (Siku) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | mbe | viwili Igando- Kijombe | | | | - | |
| | Njombe | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa ajili ya Usatule-Mahongole | 7,996,231,305 | 1,899,492,435 | - | 1,899,492,435 | >150 |
| Mbeya | Chunya | Ujenzi wa Mradi wa Maji kwa Mji Mdogo wa Makongolosi kutekelezwa | 2,809,674,260 | 948,594,625 | 406,179,843 | 542,414,782 | 120-240 |
| Tanga | Lushoto | Ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha Shume, Manolo, Madala | 2,961,216,624 | 495,534,440 | - | 495,534,440 | >192 |
| Pwani | Mkuranga | Ujenzi wa Mradi wa maji kijiji cha Mwanambaya | 2,347,737,221 | 179,966,520 | 173,943,911 | 6,022,609 | 150 |
| | | Ujenzi wa Mradi wa maji kijiji cha Mkerezange | 981,996,310 | 520,129,820 | 407,476,079 | 112,653,741 | 210 |
| Jumla | | | 46,543,508,239 | 11,625,759,020 | 7,677,733,256 | 3,948,025,764 | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kwa maoni yangu, kuchelewa kwa malipo kumesababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa miaka hadi miwili na hivyo kuwanyima wanufaika huduma za maji. Hii pia inaweza kusababisha ongezeko la gharama za miradi kutokana na adhabu ya riba.

**Napendekeza kuwa RUWASA ihakikishe kwamba katika siku zijazo, kazi zote zilizokamilika zinathibitishwa na kulipwa kwa wakati ili kukamilisha Miradi kwa haraka, utoaji wa huduma ya maji kwa jamii na kulinda maslahi ya pande zote za kimkataba.**

### 9.15.10 Ucheleweshaji wa Utekelezaji na Ukamilishaji wa Miradi yenye thamani ya Sh. 47,254,841,965

Kifungu Na. 20.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba yaliyopo katika Mwongozo wa Nyaraka za Zabuni za mwaka 2018 kinataka Wakandarasi kuanza utekelezaji wa kazi kwa wakati na kufanya majukumu yao kulingana na mipango ya kazi iliyowasilishwa na kuhuishwa na kupitishwa na msimamizi wa Mradi na kukamilisha kazi hizo kwa tarehe zilizokusudiwa.

Nimebaini kuwa miradi 20 (48% ya miradi 42 iliyojumuishwa kwenye sampuli) yenye thamani ya Sh. 47,254,841,965 ilichelewa kukamilika kwa kipindi cha kuanzia miezi 2 hadi miaka 5 kinyume na vifungu vya Mikataba ambavyo vinahitaji Miradi hiyo kuanza na kukamilika ndani ya muda uliopangwa. Hii ina maanisha ongezeko la 44% kutoka mwaka 2018/19 ambapo Miradi ya Sh. 32,706,164,240 ilichelewa kukamilika. Maelezo zaidi yameoneshwa katika **Jedwali Na. 87**

**Jedwali Na. 87: Miradi Iliyochelewa Kutekelezwa na Kukamilika**

| Mkoa | Ofisi Ya Wilaya | Jina La Mradi | Gharama Ya Mkataba (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Arusha | Karatu | Ukarabati wa Mradi wa maji Getamock | 82,782,671 | Mradi ulikadiriwa kuwa wa miezi mitatu kutoka tarehe 30.03.2020 hadi 30.06.2020 lakini hadi kufikia 22.10.2020, Mradi huo ulikuwa haujakamilika (miezi minne). |
| Kilima njaro | Moshi | Ujenzi wa Mradi wa Maji Wa Tella Mande | 905,475,000 | Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kuanzia tarehe 19.01.2019 hadi 31.03.2020. Hata hivyo, |

| Mkoa | Ofisi Ya Wilaya | Jina La Mradi | Gharama Ya Mkataba (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | | | | hadi 30.12.2020 Mradi haukukamilika (miezi tisa). |
| | Rombo | Ujenzi wa Mradi wa maji Leto | 605,500,538 | Miradi ilitakiwa kukamilika tarehe 30.01.2020. Hadi kufikia Desemba 2020 (miezi 11) Mradi haujakamilika. |
| | | Ujenzi wa Mradi wa maji Shimbi | 724,239,438 | |
| Katavi | Mpanda | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa Vijiji vya Mtakuja na Songambele | 600,702,298 | Tarehe ya kuanza kwa Mradi ilikuwa 29.04.2019 na ilitarajiwa kumalizika tarehe 29.10.2019 lakini hadi kufikia 30.12.2020 (miezi 14) Mradi huo haukukamilika. |
| Rukwa | Sumba wanga | Ujenzi wa bwawa kwa ajili ya Kijiji cha Ikozi awamu ya II | 2,943,086,780 | Mkataba ulitakiwa kuanza tarehe 02.10.2018 na kukamilika tarehe 01.04.2019. Hata hivyo, hadi 21.11.2020 (miezi 19), Mradi huo bado haujakamilika. |
| Kigoma | Kigoma | Ujenzi wa Mradi wa maji katika Vijiji vya Kaseke, Kimbwela na Nyamoli | 1,163,496,000 | Kuchelewa kwa miezi 18 kuanzia tarehe ya mwisho ya kukamilika kwa marekebisho ambayo ilikuwa 26.07. 2019 hadi tarehe ya ukaguzi huu tarehe 15.01.2021. |
| Dodom a | Mpwap wa | Ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha Kidenge | 1,070,460,730 | Hadi kufikia tarehe 28.11.2020 (miezi 10 baada ya tarehe iliyopaswa kukamilisha mkataba, yaani tarehe 13.01.2020), Mradi haukuwa umekamilika. |
| Mwanz a | Magu | Ujenzi wa Mradi wa maji Nsola-Bubinza | 1,001,742,500 | Mkataba ulipangwa kuanza tarehe 12.12.2017 lakini ulianza tarehe 06.02.2018 na ulipaswa kukamilika |

| Mkoa | Ofisi Ya Wilaya | Jina La Mradi | Gharama Ya Mkataba (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | | | | tarehe 12.06.2018 na kufanyiwa marekebisho hadi tarehe 05.08.2018. Hata hivyo, hadi tarehe 31.10.2020 (miezi 26), Mradi huo haukuwa umekamilika. |
| Mtwara | Tandahimba | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa Kijiji cha Mkwiti | 3,271,950,518 | Mradi huu ulipaswa kuanza tarehe 01.01.2018 na kukamilika tarehe 31.12.2018 na kisha kuongezewa muda mpaka tarehe 30.01.2020. Hata hivyo, hadi mwezi Disemba 2021 (miezi 23) Mradi huo haukuwa umekamilika. |
| Morogoro | Mvomero | Ujenzi wa Mradi maji katika kijiji cha Lubungo | 430,104,045 | Kazi ilitarajiwa kutekelezwa kuanzia tarehe 04.10.2018 hadi tarehe 06.03.2019 na kutoa nyongeza ya muda hadi tarehe 30.11.2020. Hata hivyo, hadi tarehe 25.01.2021 (miezi 2), Mradi huo haukuwa umekamilika. |
| Tabora | Kaliua | Ujenzi wa Mradi wa Maji katika kijiji cha Wachawaseme-Kaliua | 535,729,732 | Kipindi cha utekelezaji kilikuwa miezi minne kuanzia tarehe 01.06.2020 hadi tarehe 28.09.2020 lakini hadi mwezi Novemba, 2020 (miezi miwili) Mradi haukuwa umekamilika. |
| Geita | Bukombe | Ujenzi wa Mradi wa Maji wa Nampalahala (Awamu ya II) | 514,915,618 | Miradi hii ilitakiwa kuanza mwezi Juni, 2020 na kukamilika mwezi Agosti, 2020 lakini hadi tarehe 20 Novemba 2020 (miezi mitatu) miradi |
| | Geita | Ujenzi wa kituo cha kuchotea | 428,367,976 | |

| Mkoa | Ofisi Ya Wilaya | Jina La Mradi | Gharama Ya Mkataba (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | | maji Nyakagwe | | hiyo haikuwa imekamilika. |
| Ruvuma | Namtumbo | Mradi wa maji kwa Kijiji cha Likuyusekamaganga | 4,915,864,910 | Mradi huo ulitakiwa kuanza tarehe 16.11.2017 na kukamilika tarehe 15.11.2018 lakini hadi kufikia tarehe 07.01.2021 (miezi 26) Mradi huo haukuwa umekamilika. |
| Njombe | Wangin g'ombe | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa Vijiji viwili Igando- Kijombe | 12,437,407,360 | Tarehe ya kuanza utekelezaji wa Mradi huo ilikuwa 09.07.2018 na ulipaswa kukamilika tarehe 08.07.2019. Aidha, ilitolewa nyongeza ya muda hadi tarehe 31.12.2020. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Novemba, 2021 (miezi 11), Mradi huo ulikuwa haujakamilika. |
| | Njombe | Ujenzi wa Mradi wa maji Usetule-Mahongole | 7,996,231,305 | Tarehe ya kuanza utekelezaji wa Mradi ilikuwa 23.05.2019 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 22.11.2019. Hata hivyo, hadi mwezi Novemba 2021 (miezi 24) Mradi ulikuwa haujakamilika. |
| Mbeya | Mbarali | Ujenzi wa Mradi wa Maji kutoka Luduga Mawindi-Awamu II | 3,683,571,612 | Mkataba ulianza tarehe 11.06.2015 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 10.12.2015. Hata hivyo, hadi tarehe 30.11.2020 (miezi 60) Mradi huo haukuwa umekamilika. |
| Tanga | Lushoto | Ujenzi wa Mradi wa maji katika kijiji cha | 2,961,216,624 | Mradi ulitakiwa kukamilika tarehe 30.06.2020 lakini hadi |

| Mkoa | Ofisi Ya Wilaya | Jina La Mradi | Gharama Ya Mkataba (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | | Shume, Manolo na Madala | | kufikia tarehe 16.12.2020 (miezi sita) Mradi haukuwa umekamilika. |
| Pwani | Mkuranga | Ujenzi wa kisima cha maji katika Kijiji cha Mkerezange | 981,996,310 | Mradi ulitakiwa kuanza tarehe 28.07.2018 na kukamilika tarehe 27.04.2019. Hata hivyo, hadi Kufikia mwezi Desemba 2020 (miezi 20), Mradi huo haukuwa umekamilika. |
| **Jumla** | | | **47,254,841,965** | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Kwa maoni yangu, kutekeleza miradi kwa kusuasua na kuchelewa kukamilika, kumezinyima jamii husika kupata huduma ya maji kwa muda uliopangwa. Hii pia imeiweka RUWASA katika hatari ya kulipa gharama kubwa ambazo zinaweza kusababishwa na kupanda kwa bei.

**Napendekeza kwamba kwa siku zijazo, RUWASA isimamie Miradi kwa ufanisi ili kuepuka ucheleweshwaji wa Miradi na gharama kubwa. Aidha, Uongozi wa RUWASA unapaswa utoze fidia ya ucheleweshaji wa miradi (liquidated damages) kutoka kwa Wakandarasi kwa mujibu wa Mikataba.**

### 9.15.11 Kutelekezwa kwa Miradi yenye Thamani ya Sh. 1,126,445,914

Kifungu Na. 19.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba yaliyopo katika Mwongozo wa Nyaraka za Zabuni za mwaka 2018 kinamtaka mkandarasi kutekeleza na kufanya kazi kwa mujibu wa vigezo na masharti ya mkataba.

Nimebaini katika Ofisi ya RUWASA Wilaya ya Ikungi Mkandarasi alitelekeza eneo la kazi kwa miezi 6 kuanzia tarehe 10 Machi, 2020 hadi 25 Septemba, 2020 ambapo Mradi ulisitishwa ukiwa umetekelezwa kwa 17%. Vilevile, nilitembelea Mradi wa Mgumile-Ujiji tarehe 04 Januari 2021 na kubaini kuwa Mkandarasi hakuwa kwenye eneo la Mradi tangu 13 Machi, 2018 (miezi 34) bila idhini ya Meneja wa Mradi. Vilevile, nimebaini miundombinu ya Mradi ilikuwa imeathiriwa na maji yaliyofurika. **Jedwali Na. 88** linatoa maelezo zaidi ya mikataba.

**Jedwali Na. 88: Miradi Iliyotelekezwa na Wakandarasi kwa Zaidi ya Miezi Sita**

| MKOA | OFISI YA WILAYA | JINA LA MRADI | NAMBA YA MKATABA | GHARAMA YA MKATABA (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| Kigoma | Kigoma-ujiji | Ujenzi wa Mradi wa maji Mgumile | LGA/042/2013-2014/12 | 721,438,645 |
| Singida | Ikungi | Ujenzi wa Mradi wa maji Kijiji cha Mtunduru | LGA/146/2018/2019/W/02 | 405,007,269 |
| **JUMLA** | | | | **1,126,445,914** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Kwa maoni yangu, kutelekeza miradi kumesababisha kutokamilika kwake na hivyo kutopatikana kwa huduma ya maji kwa jamii iliyolengwa. Mbali na hilo, kusimama kwa kazi kumesababisha uharibifu wa kazi iliyokwishafanyika awali na kunaweza kusababisha upotevu zaidi wa rasilimali za Umma endapo hali hiyo itaendelea.

**Napendekeza kuwa uongozi wa RUWASA uhakikishe Miradi inakamilika bila kucheleweshwa zaidi na Wasimamizi wa Miradi husika wafanye ufuatiliaji na usimamizi wa kutosha wa Miradi hiyo.**

### 9.15.12 Kushindwa kutoza Fidia ya Kuchelewesha Kazi Sh. 1,227,502,011

Kanuni ya 112(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 na kifungu Na. 57.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba yaliyopo katika Mwongozo wa Nyaraka za Zabuni za mwaka 2018 vinataka taasisi zinazofanya ununuzi kuwatoza fidia wazabuni kwa kiwango cha asilimia 0.1 hadi asilimia 0.15 ya jumla ya mkataba hadi jumla ya kiasi cha dhamana ya utendaji kwa kuchelewa kutoa huduma au kufanya kazi.

Nimebaini RUWASA imeshindwa kutoza fidia (liquidated damages) ya Sh. 1,227,502,011 kwa mikataba minne ikiwa ni ukomo wa dhamana ya utendaji iliyowasilishwa na asilimia 0.10 ya thamani ya mikataba kwa siku itokanayo na kuchelewa kwa Miradi. Maelezo zaidi yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 89** hapa chini

**Jedwali Na. 89: Mikataba ambayo Haikutozwa Fidia ya Ucheleweshaji Miradi**

| Mkoa | Ofisi Ya Wilaya | Jina La Mradi | Na. Ya Mkataba | Gharama Ya Mkataba (Sh.) | Ucheleweshaji (Siku) | Tozo Ya Fidia (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kagera | Missenyi | Ujenzi wa Mradi wa maji kijiji cha Kakunyu | LGA/038/RWSSP/18/2013/2014 | 875,845,000 | 312 | 116,349,600 |
| Kigoma | Kigoma | Ujenzi wa Mradi wa Maji Vijiji vya Kaseke, Kimbwela na Nyamoli | LGA/043/2016/2017/W/15 | 1,163,496,000 | 539 | 174,524,400 |
| Mtwara | Tandahimba | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa Kijiji cha Mkwiti | LGA/087/WS/2017/2018/w/16 | 3,271,950,518 | 100 | 327,195,051 |
| Njombe | Wanging'ombe | Ujenzi wa Mradi wa maji Igando-Kijombe | LGA/153/2017/2018/W/01 | 12,437,407,360 | 49 | 609,432,960 |
| **Jumla** | | | | **14,476,748,360** | | **1,227,502,011** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Kwa kutokutoza fidia ya ucheleweshaji miradi, RUWASA haikuhakikisha kuwa wakandarasi wanakamilisha miradi hiyo kwa wakati. Hali hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za miradi.

**Napendekeza Uongozi wa RUWASA utoze fidia ya Sh. 290,874,000 kwa Miradi iliyocheleweshwa na kuendelea kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji unaozingatia masharti ya mikataba ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kuepuka gharama za ziada.**

### 9.15.13 Kusitishwa kwa Mikataba Yenye Thamani ya Sh. 7,400,458,243 na Marekebisho ya Sh. 888,273,369 Bila Kutoa Taarifa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kanuni ya 113(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, inawataka Maafisa Masuuli kupeleka kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali orodha ya Wakandarasi walioshindwa kutekeleza Mikataba ndani ya muda uliowekwa au walioshindwa kufuata matakwa ya mikataba bila sababu zinazokubalika na kusababisha kuvunjika kwa Mikataba kwa ajili ya taarifa na hatua stahiki. Aidha, sehemu ya 3(d) ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 inamtaka Afisa masuuli kuwasilisha ripoti kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kwa marekebisho yoyote, mabadiliko au tofauti katika Mikataba akitoa maelezo juu ya sababu na athari kwa gharama za Mkataba.

Katika ukaguzi nimebaini Mikataba mitatu katika mikoa ya Singida na Ruvuma ambapo RUWASA ilisitisha mikataba yenye thamani ya Sh. 7,400,458,243 kutokana na Wakandarasi kushindwa kutekeleza miradi hiyo. Hata hivyo, taarifa za kusitishwa kwa mikataba hazikuwasilishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama sharia inavyoelekeza. Aidha, nimebaini kuwa Ofisi ya RUWASA Wilaya ya Mkuranga ilirekebisha bei ya Mkataba kwa kupunguza kiwango cha awali kwa asilimia 20 bila kuwasilisha suala hilo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma. Maelezo zaidi yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 90**

**Jedwali Na. 90: Mikataba iliyositishwa na kurekebishwa bila kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| MIKATABA ILIYOSITISHWA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MKOA** | **OFISI YA WILAYA** | **JINA LA MRADI** | **NAMBA YA MKATABA** | **GHARAMA YA MKATABA (Sh.)** |
| Singida | Ikungi | Ujenzi wa Mradi wa maji Kijiji cha Mtunduru. | LGA/146/2018/2019/W/02 | 405,007,269 |
| Ruvuma | Songea | Uboreshaji wa Mradi wa maji vijiji vinne katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kwa awamu ya I. | LGA/182/HQ/W/2016/2017/06 | 2,079,586,064 |
| | Namtumbo | Ujenzi wa Mradi wa maji kwa kijiji cha Likuyuseka maganga. | LGA/105/CTR/2016/2017/W/RWSSP/01 | 4,915,864,910 |
| JUMLA | | | | 7,400,458,243 |
| MIKATABA ILIYOREKEBISHWA | | | | |
| Pwani | Mkuranga | Ujenzi wa kisima cha maji Kijiji cha Mwanambaya. | LGA/012/WS/2017/2018W/01-02 | Kutoka Sh. 1,243,033,303 hadi Sh. 977,760,819 (punguzo la Sh. 265,272,484) |
| | | Ujenzi wa kisima cha maji Kijiji cha Mkerezange. | LGA/012/WS/2017/2018W/01-03 | Kutoka Sh. 2,971,819,267 hadi Sh. 2,348,818,382 (punguzo la Sh. 623,000,885) |
| JUMLA YA MAREKEBISHO (Sh.) | | | | 888,273,369 |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/2020*

Kwa maoni yangu, kushindwa kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kunapunguza uadilifu, uwazi na uwajibikaji katika manunuzi ya umma. Hali hii inaweza pia kusababisha Wakandarasi kuendelea na tabia ya kutelekeza miradi.

**Napendekeza kwa Uongozi wa RUWASA kuhakikisha kuwa katika siku zijazo taarifa za Mikataba iliyositishwa na kurekebishwa inawasilishwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya taarifa na kuchukua hatua stahiki.**

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

## SURA YA KUMI

## USIMAMIZI WA MATUMIZI

### 10.1 Utangulizi

Taasisi za Serikali hutumia fedha kwa ajili ya ununuzi wa huduma na bidhaa kwa mujibu wa idhini kama inavyotolewa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uidhinishaji wa matumizi huongozwa na sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali kama inavyotolewa na mamlaka husika kila wakati. Taasisi zinapaswa kuwa na mfumo bora na madhubuti wa udhibiti ili kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha yanafanywa kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi wangu umeendelea kufanya tathmini ya mifumo ya udhibiti wa matumizi na kutoa mapendekezo ili kuboresha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Sura hii inatoa mapungufu yaliyobainika kwenye matumizi yaliyofanywa na Wizara, Sekretarieti za Mikoa kwa mujibu wa sheria na kanuni. Ingawa kuna maboresho yamefanyika katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kutokana na mapendekezo yangu, hata hivyo, maboresho zaidi yanahitajika. Nimeendelea kubaini dosari kadhaa kwenye usimamizi wa matumizi ikiwa ni pamoja na matumizi yasiyo na nyaraka toshelezi, matumizi kupitia vifungu vya matumizi visivyo sahihi, matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhishwa, matumizi yasiyo na tija, kuchelewa kurejesha masurufu, kutokukata kodi ya zuio (withholding tax) na kupeleka Mamlaka ya Mapato na kushindwa kudai risiti za kielekitroniki kutoka kwa wazabuni baada ya kufanya malipo. Katika aya zifuatazo nimeeleza kwa kina dosari nilizozibaini pamoja na mapendekezo yangu ili kuboresha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

### 10.2 Fedha ambazo Hazikutumika za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Hazikurejeshwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutoka Halmashauri Sh. 716,706,995

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri (ambao ni wasimamizi wa Uchaguzi) kuwa fedha zote zitakazobaki baada ya zoezi la kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura kukamilika zirejeshwe kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kupitia akaunti maalumu iliyopo Benki Kuu ya Tanzania.

Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipeleka jumla ya Sh.43,263,677,359 mikoa yote 26 ya Tanzania Bara pamoja na

Zanzibar kwa ajili ya kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kati ya fedha hizo, zilizokuwa zimetumika ni Sh. 42,546,970,364. Hivyo, kulikuwa na bakaa kiasi cha Sh. 716,706,995 katika Halmashauri 70 kwenye mikoa 19 ambazo hazijarejeshwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya matumizi husika kukamilika kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na.XX**

Nilishindwa kubaini kiasi cha fedha ambacho kilitumika pamoja na bakaa katika Halmashauri za Wilaya ya Kasulu na Uvinza ambazo zilipelekewa Sh. 262,059,500 na Sh. 219,632,000 mtawalia. Hii ni kwa sababu Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya walishindwa kunipa nyaraka husika. Muhtasari wa fedha ambazo hazijarejeshwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.Uchambuzi wa fedha ambazo hazikurejeshwa kwa mikoa ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 91** hapa chini

**Jedwali Na. 91: Mikoa ambayo Halmashauri Hazijarejesha Fedha Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

| Na. | Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na. | Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dodoma | 30,980,894 | 11 | Mwanza | 5,568,395 |
| 2 | Singida | 2,036,540 | 12 | Kagera | 4,490,089 |
| 3 | Ruvuma | 243,710 | 13 | Tabora | 27,816,991 |
| 4 | Kilimanjaro | 7,226,800 | 14 | Pwani | 679,547 |
| 5 | Tanga | 20,614,486 | 15 | Rukwa | 1,060,000 |
| 6 | Geita | 1,259,427 | 16 | Mbeya | 4,144,080 |
| 7 | Kigoma | 383,750,051 | 17 | Songwe | 310,390 |
| 8 | Arusha | 90,096,797 | 18 | Dar es Salaam | 16,603,114 |
| 9 | Manyara | 72,712,445 | 19 | Shinyanga | 20,708,660 |
| 10 | Mara | 26,404,579 | **Jumla** | | **716,706,995** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ni maoni yangu kuwa, dosari hii imetokana na ufuatiliaji usioridhisha wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuhakikisha kuwa fedha zote ambazo hazijatumika zinarejeshwa. Vilevile, imetokana na Halmashauri husika kukiuka maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kushindwa au kuchelewa kurejesha fedha ambazo hazijatumika Tume ya Taifa ya

Uchaguzi kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha hizo. Kitendo cha Halmashauri za Wilaya ya Kasulu na Uvinza kushindwa kutoa nyaraka kuhusiana na matumizi ya fedha kinazuia mawanda ya ukaguzi, hivyo kunisababisha kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.

**Ninashauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa na mfumo madhubuti utakaowezesha usimamizi wa matumizi ya fedha zinazotumwa Halmashauri na kuhakikisha kuwa fedha ambazo hazijatumika zinarejeshwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Vilevile, Wakurugenzi wa Wilaya za Kasulu na Uvinza kuhakikisha kuwa nyaraka zinawasilishwa kwenye ofisi yangu kwa ajili ya ukaguzi.**

### 10.3 Matumizi Yasiyo na Tija Sh. 453,782,820

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2001, matumizi yasiyo na tija ni matumizi ambayo hayana manufaa na yangeweza kuepukwa. Hivyo, malipo haya ni hasara na yanapaswa kuwa sehemu ya hasara kwenye taarifa ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ili yaweze kuchunguzwa na Kamati za Fedha za Bunge.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Wizara mbili zilifanya matumizi kiasi cha Sh. 453,782,820.35 ambayo hayana tija kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 92** hapo chini.

**Jedwali Na. 92: Malipo Yasiyo na Tija**

| Na. | Taasisi | Kiasi(Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Fungu Na. 52 | 451,155,502 | Gharama ya kuchelewa kuondosha mizigo bandarini ambayo ni magari 50 ya wagonjwa na pikipiki 50. |
| 2 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi ( Uvuvi - Fungu Na. 64) | 2,627,318.35 | Malipo ya adhabu kwa kuchelewa kupeleka makato ya watumishi Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. |
| **Jumla** | | **453,782,820.35** | |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ninaamini kuwa, matumizi yasiyo na tija hutokana na mfumo wa udhibiti wa matumizi usioridhisha. Bila ya kuwa na mfumo madhubuti wa udhibiti wa matumizi ya fedha, Serikali itaendelea kupata hasara kutokana na matumizi ambayo yangeweza kuepukika.

**Ninashauri kuwa Maafisa Masuuli pamoja na wote wanaohusika kufanya maamuzi kuhakikisha mifumo ya usimamizi wa fedha inaimarishwa ili kuepuka matumizi yasiyo na tija.**

### 10.4 Matumizi Yenye Nyaraka Pungufu Sh. 7,320,136,708 na Hati za Malipo Ambazo Hazikuwasilishwa Wakati wa Ukaguzi Sh. 2,638,372,956.12

Nilibaini kuwa, taasisi 36 zilifanya malipo yenye jumla ya Sh. 7,320,136,708 bila kuwa na nyaraka stahiki na toshelezi katika mwaka huu wa ukaguzi. Kitendo hiki ni kinyume na kanuni ya 86 ya Kanuni za Fedha za za mwaka 2001 zinazoelekeza kuwa malipo yote ya fedha za umma yawe na nyaraka toshelezi na stahiki.

Aidha, hati za malipo zenye jumla ya Sh. 2,638,372,956.12 katika taasisi nne hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi hivyo sikuweza kujiridhisha uhalali wa malipo hayo. Kwa mujibu wa kanuni ya 18 (1)(f) na (2) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001, malipo ambayo nyaraka zake hazijawasilishwa ni hasara ya fedha na yanapaswa kujumuishwa kwenye taarifa ya Hasara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Rejea **Jedwali Na. 93** hapa chini na **Kiambatisho Na. XXI** kwa Maelezo Zaidi.

**Jedwali Na. 93: Hati za Malipo Ambazo Hazikuwasilishwa Wakati wa Ukaguzi**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania - Fungu Na. 38 | 2,293,308,795 |
| 2 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Fungu Na. 52 | 95,691,921.20 |
| 3 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Fungu Na. 34 | 72,853,524.42 |
| 4 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi - Fungu Na. 61 | 176,518,715.50 |
| **Jumla** | | **2,638,372,956.12** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Mtiririko wa malipo yenye nyaraka pungufu kwa miaka mitano ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 94** hapo chini.

**Jedwali Na. 94: Malipo yenye Nyaraka Pungufu kwa Miaka Mitano**

| Na. | Mwaka wa Fedha | Idadi ya Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 2019/20 | 36 | 7,320,136,708 |
| 2 | 2018/19 | 39 | 5,060,449,260 |
| 3 | 2017/18 | 40 | 4,369,240,033 |
| 4 | 2016/17 | 27 | 4,508,127,243 |
| 5 | 2015/16 | 29 | 12,504,745,476 |

***Chanzo: Ripoti za Serikali kuu kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19 na Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20.***

Kutokana na jedwali hapo juu, mtiririko wa matumizi yenye nyaraka pungufu yamepungua kwa idadi ya taasisi. Hata hivyo, yameongezeka kwa kiasi cha malipo ikiashiria kuwa maboresho zaidi kwenye usimamizi wa fedha yanahitajika.

Ni maoni yangu kuwa chanzo cha kuwa na matumizi yenye nyaraka pungufu na kutokuwasilisha hati za malipo ni kuwa na mfumo dhaifu wa udhibiti na Maafisa Masuuli kushindwa kuchukua hatua stahiki kwa maafisa wanaosababisha udhaifu huu. Ninaamini kuwa hii inaweza kuwa ishara ya kufanyika kwa matumizi ya udanganyifu na mabaya. Mawanda yangu ya Ukaguzi yalizuiwa hivyo sikuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.

**Ninashauri Maafisa Masuuli husika kuendelea kuhakikisha mifumo ya udhibiti wa fedha inaimarishwa ili kuhakikisha kuwa matumizi yanayofanyika yanakuwa na nyaraka stahiki na toshelezi. Vilevile, hatua stahiki zichukuliwe kwa maofisa wanaosababisha dosari hizi.**

### 10.5 Madai ya Matibabu Yaliyokataliwa na Mfuko wa Bima ya Afya Sh. 24,160,690

Jeshi la Polisi lina makubaliano na Mfuko wa Bima ya Afya ya kuwatibu wagonjwa kupitia bima ya afya na kupeleka madai ili kurejeshewa fedha za matibabu kutoka Mfuko wa Bima ya Afya. Mfuko wa Bima ya Afya umetoa miongozo na maelekezo mbalimbali ya kuzingatia wakati wa kutoa huduma za afya kwa wanachama wake.

Katika mwaka wa fedha 2019/20 Jeshi la Polisi halikurejeshewa fedha kutoka Mfuko wa Bima ya Afya kiasi cha Sh. 24,160,690 kwa kushindwa kuzingatia maelekezo ya ujazaji wa fomu za Bima wakati wa matibabu. Vituo vya Afya vya Polisi vilitumia jumla ya Sh. 109,614,050 kuwahudumia wanachama wa Bima ya afya lakini kati ya kiasi hicho fedha iliyorejeshwa ni Sh. 85,453,360 tu na fedha jumla ya Sh.24,160,690 haikurejeshwa kutonana na dosari mbalimbali.

Dosari mbalimbali katika ujazaji wa fomu za Bima ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa taarifa muhimu kama vile; majina ya wagonjwa na sahihi za madaktari, ripoti za majibu ya vipimo vya wagonjwa, kutoa huduma nje ya mawanda ya Mfuko wa Bima ya Afya, Pamoja na matumizi ya kadi za Bima ya Afya zilizokwisha muda wake. Sababu nyingine ni kuwapo kwa maombi yaliyotumwa mara mbili, kutokuzingatia bei za Mfuko wa Bima ya

Afya, kulaza wagonjwa na kujaza siku zisizo sahihi, kukosekana kwa maelezo ya huduma zilizotolewa, n.k

Kutokurejeshwa kwa fedha kutoka Mfuko wa Bima ya Afya husababisha kupungua kwa mapato ya vituo vya afya, ambayo inaweza kusababisha kupungua kwa ubora wa huduma zinazotolewa. Fedha hizi ambazo hazijarejeshwa ni hasara kwa Jeshi la Polisi na kusababisha upungufu wa uwezo wa kuhudumia wagonjwa.

**Ninashauri uongozi wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa fomu za Bima ya Afya zinajazwa kikamilifu, zinahakikiwa na kuidhinishwa kabla ya kupelekwa Mfuko wa Bima ya Afya. Pia, ni vyema kushirikiana na Mfuko wa Bima ya Afya kuhakikisha mafunzo zaidi yanatolewa jinsi ya kuzingatia miongozo na maelekezo ya namna ya ujazaji wa fomu ili kupunguza dosari.**

### 10.6 Matumizi Yaliyofanyika Nje ya Bajeti Sh. 24,408,396,381

Kifungu Na. 27(4) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaelekeza kuwa, matumizi ya fedha za Serikali yanatakiwa yaendane na bajeti iliyoidhinishwa.

Nilibaini kuwa, taasisi sita zilifanya matumizi yenye jumla ya Sh. 24,408,396,381 ambayo hayakuwa kwenye bajeti kinyume na sheria ya bajeti ya mwaka 2015. Matumizi kinyume na bajeti huathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali hivyo taasisi kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mchanganuo wa taasisi zilizofanya matumizi nje ya bajeti ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 95** hapo chini.

**Jedwali Na. 95: Matumizi Nje ya Bajeti**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Tume ya Taifa katika Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) – Fungu Na. 18 | 4,760,000.00 |
| 2 | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano - Fungu Na. 62 | 38,150,000.00 |
| 3 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Fungu Na. 53 | 257,906,556.28 |
| 4 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Fungu Na. 52 | 24,024,009,125 |
| 5 | Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu - Fungu Na. 65 | 50,477,500.00 |
| 6 | Sekretarieti ya Mkoa Songwe | 33,093,200.00 |
| **Jumla** | | **24,408,396,381** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kwa miaka mitano iliyopita, mtiririko wa kuongezeka au kupungua kwa tatizo hili ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 96** hapo chini.

**Jedwali Na. 96: Matumizi Yaliyofanywa Nje ya Bajeti kwa Miaka Mitano**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Taasisi | Kiasi (Sh.) | Mabadiliko ya Kiasi ukilinganisha na mwaka uliopita |
|---|---|---|---|
| 2019/20 | 6 | 24,408,396,381 | 24,408,396,381 |
| 2018/19 | 0 | 0 | 0 |
| 2017/18 | 0 | 0 | (3,044,072,276) |
| 2016/17 | 8 | 3,044,072,276 | (1,953,889,688) |
| 2015/16 | 15 | 4,997,961,964 | 3,699,588,043 |
| 2014/15 | 13 | 1,298,373,921 | |

**Chanzo**: *Ripoti za Serikali kuu kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19 na Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

**Ninashauri menejimenti husika kuhakikisha kuwa matumizi yote yanazingatia bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoelekezwa kwenye Sheria ya Bajeti.**

### 10.7 Malipo yenye Mapungufu Sh. 53,345,000

Kanuni ya 11 ya Kanuni za Fedha ya mwaka 2001 inaelekeza Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa fedha na rasilimali walizopewa kusimamia wanazisimamia vizuri na kuzitunza. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi mbili zilifanya malipo yenye jumla ya Sh. 53,345,000 yenye mapungufu kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 97** hapo chini.

**Jedwali Na. 97: Malipo yenye Mapungufu**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali – Fungu Na. 16 | 50,400,000 | Malipo kwa ajili ya posho ya nyumba kwa kila mwezi kwa watumishi wasiostahili. |
| 2 | Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu Na. 69 | 2,945,000 | Malipo kwa ajili ya matibabu ambayo ni sehemu ya huduma za Mfuko wa Bima ya Afya. |
| **Jumla** | | **53,345,000** | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ni maoni yangu kuwa, malipo yaliyofanyika hayakuweza kuwa na uhalali kwa sababu hayana idhini stahiki. Kufanya malipo kinyume na sheria, kanuni na taratibu ni ukiukwaji wa sheria ambao unasababisha upotevu wa fedha za serikali.Fedha hizi zingetumika kwenye shughuli zenye tija zaidi kwa taasisi.

**Ninaendelea kushauri kuwa Maafisa Masuuli katika taasisi zao kuhakikisha kuwa sheria na taratibu za fedha zinazingatiwa, endapo kuna upungufu wa kisheria, kibali maalumu kipatikane kwa maandishi.**

### 10.8 Malipo Yaliyofanywa kwenye Vifungu Visivyohusika Sh. 657,493,929

Kanuni Na. 46(2) ya Kanuni za Fedha ya mwaka 2001 inaelekeza kila kifungu cha mapato na matumizi kifanyike kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, taasisi 16 zilifanya malipo yenye jumla ya Sh. 657,493,929 kupitia vifungu visivyohusika kinyume na Kanuni 46(2) ya Kanuni za Fedha. Malipo yanayofanywa kwenye vifungu visivyo sahihi sio tu kwamba huipotosha taarifa za fedha, lakini pia huharibu taswira ya bajeti na husababisha baadhi ya vifungu kutumika zaidi na vingine kutumika chini

ya bajeti iliyoidhinishwa; hivyo, kuathiri mali na gharama kwenye taarifa za fedha. Mchanganuo wa taasisi hizo ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 98** hapo chini.

**Jedwali Na. 98: Malipo Yaliyofanywa kwenye Vifungu Visivyohusika**

| Na. | Taasisi | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Rais - Bodi ya Mishahara katika Utumishi wa Umma - Fungu Na. 09 | 86,081,603.00 |
| 2 | Tume ya Taifa katika Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) - Fungu Na. 18 | 5,770,000.00 |
| 3 | Wizara ya Mambo ya Ndani - Fungu Na. 51 | 38,400,580.00 |
| 4 | Wizara ya Viwanda na Biashara - Fungu Na. 44 | 54,626,938.00 |
| 5 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Fungu Na. 34 | 64,180,930.47 |
| 6 | Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu Na. 37 | 47,587,904.18 |
| 7 | Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu - Fungu Na. 65 | 143,714,226.00 |
| 8 | Mamlaka ya Kupambana na Kuzuia Dawa za Kulevya-Fungu Na. 91 | 10,600,000.00 |
| 9 | Sekretarieti ya Mkoa Kagera | 41,517,609 |
| 10 | Sekretarieti ya Mkoa Mbeya | 36,348,565 |
| 11 | Sekretarieti ya Mkoa Arusha | 42,274,337 |
| 12 | Sekretarieti ya Mkoa Dar es Salaam | 16,266,500 |
| 13 | Sekretarieti ya Mkoa Lindi | 6,432,000 |
| 14 | Sekretarieti ya Mkoa Manyara | 1,580,000 |
| 15 | Sekretarieti ya Mkoa Shinyanga | 11,926,500 |
| 16 | Tume ya Taifa ya mipango na matumizi ya Ardhi - Fungu Na. 03 | 50,186,236 |
| **Jumla** | | **657,493,929** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kwa kulinganisha na miaka iliyopita, isipokuwa mwaka 2017/18, mtiririko unaonesha kuwa dosari hii imeendelea kuwapo bila kuwa na mabadiliko makubwa, hii inaashiria kuwa Maafisa Masuuli wanapaswa kuongeza juhudi ili kuhakikisha bajeti inazingatiwa. Rejea **Kielelezo Na. 16** hapo chini

**Kielelezo Na. 16: Mtiririko wa Malipo Yaliyofanywa kwenye Vifungu Visivyohusika**




**Ninashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa malipo yote yanafanyika kulingana na vifungu sahihi vilivyoidhinishwa kwenye bajeti, ikibidi idhini ya kuhamisha fedha kwenye vifungu itolewe kwa mujibu wa Kanuni za Fedha.**

### 10.9 Malipo Yaliyofanyika bila Kudai Risiti za Kielekitroniki Sh. 1,560,639,544.29

Ukaguzi ulibaini kuwa taasisi 21 zililipa jumla ya Sh. 1,560,639,544.29 kwa wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za kielekitroniki kinyume na matakwa ya kifungu Na. 36(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya 2015 na Kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Kodi ya Mapato (Vifaa vya Kielekitroniki) za mwaka 2012. Rejea **Jedwali Na. 99** hapo chini kwa maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 99: Taasisi Zilizofanya Malipo bila kudai Risiti za Kielekitroniki**

| Na. | Taasisi | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto – Fungu Na. 52 | 438,860,329.46 |
| 2 | Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo - Fungu Na. 96 | 22,729,932 |
| 3 | Wizara ya Katiba na Sheria – Fungu Na. 41 | 23,093,438 |
| 4 | Wizara ya Maji – Fungu Na. 46 | 48,859,623.19 |
| 5 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi – Fungu Na. 61 | 629,470,323 |
| 6 | Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu Na. 37 | 19,991,309.60 |
| 7 | Mamlaka ya Kupambana na Kuzuia Dawa za Kulevya- Fungu Na. 91 | 22,781,763.20 |
| 8 | Sekretarieti ya Mkoa Kagera | 18,289,598.44 |
| 9 | Sekretarieti ya Mkoa Njombe | 66,452,733 |
| 10 | Sekretarieti ya Mkoa Ruvuma | 21,775,137.60 |
| 11 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia – Fungu Na. 46 | 17,275,740 |
| 12 | Tume ya Kudhibiti UKIMWI | 24,458,038 |
| 13 | Sekretarieti ya Mkoa Arusha | 17,825,880 |
| 14 | Sekretarieti ya Mkoa Kigoma | 30,582,066 |
| 15 | Sekretarieti ya Mkoa Mtwara | 45,568,807.00 |
| 16 | Sekretarieti ya Mkoa Lindi | 65,576,725.00 |
| 17 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Fungu Na. 48 | 12,603,858.80 |
| 18 | Ofisi ya Makamu wa Rais - Fungu Na. 31 | 7,094,000.00 |
| 19 | Sekretarieti ya Mkoa Manyara | 13,180,965 |
| 20 | Sekretarieti ya Mkoa Tanga | 9,330,376.00 |
| 21 | Sekretarieti ya Mkoa Shinyanga | 4,838,901.00 |
| | **Jumla** | **1,560,639,544.29** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita, kuna ongezeko la Sh. 606,542,367.03 wakati Idadi ya Taasisi imeongezeka kutoka 18 hadi 21.

Hii inaonesha kuwa dosari hii bado ipo. **Kielelezo Na. 17** hapa chini inaonesha mwenendo wa dosari hii kwa miaka mitano mfululizo .

**Kielelezo Na. 17: Mtiririko wa Malipo Yasiyokuwa na Risiti za Kielekitroniki**




| | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 | 2016/17 | 2015/16 | 2014/15 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Taasisi | 21 | 18 | 20 | 29 | 39 | 26 |
| Kiasi (Sh.) | 1,547,458,579 | 940,916,212.2 | 1,432,407,818 | 1,551,184,131 | 7,790,299,407 | 6,185,012,346 |

Kutokudai risiti za kielekitroniki kunasababisha mianya ya ukwepaji wa kodi hivyo kudhoofisha juhudi za Serikali kukusanya mapato.

**Ninashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha wanazingatia Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 kwa kudai risiti za kielekitroniki kwa wazabuni. Ninatoa wito kwa Maafisa Masuuli kuacha kufanya manunuzi kwa wazabuni ambao hawatumii vifaa vinavyotoa risiti za Kielekitroniki.**

## 10.10 Kutokukata Kodi ya Zuio na Kutowasilishwa Kodi Hiyo Mamlaka ya Mapato Tanzania Sh. 60,035,534

Kwa mujibu wa kifungu Na. 83(1)(c)(ii) na 84 (1) vya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa mwaka 2019), kodi ya zuio inapaswa kukatwa kwenye ada za huduma, malipo ya manunuzi ya bidhaa na malipo ya mikataba na kuwasilishwa Mamalaka ya Mapato Tanzania ndani ya siku saba baada ya mwisho wa mwezi.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, taasisi tano zilishindwa kukata kodi ya zuio au kuwasilisha kodi ya zuio jumla ya Sh. 60,035,534 Mamlaka ya Mapato Tanzania kinyume na Sheria ya Kodi ya Mapato. Rejea **Jedwali Na. 100** hapo chini kwa maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 100: Orodha ya Taasisi ambazo Hazikukata Kodi ya Zuio**

| Na. | Taasisi | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali – Fungu Na. 16 | 10,214,628 |
| 2 | Tume ya Taifa katika Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) – Fungu Na. 18 | 14,564,899 |
| 3 | Wizara ya Maliasili na Utalii – Fungu Na. 69 | 675,000 |
| 4 | Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri-Fungu Na. 30 | 2,649,387 |
| 5 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi – Fungu Na. 64) | 31,931,620.08 |
| **Jumla** | | **60,035,534.08** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ikilinganishwa na ripoti za miaka iliyopita, kuna ongezeko la kiasi cha Sh. 36,534,316 kuhusiana na dosari hii, Ongezeko hili linaonesha kuwa juhudi zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli kushughulikia tatizo hili hazikuzaa matunda. Mtiririko kwa miaka mitano ni kama inavyoonekana hapo chini.

**Jedwali Na. 101: Mtiririko wa Mabadiliko Kiasilimia kwa miaka mitano**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Taasisi | Kodi Zuio ambayo Haikukatwa (Sh.) | Mabadiliko kiasilimia |
|---|---|---|---|
| 2019/20 | 4 | 60,035,534 | 155 |
| 2018/19 | 5 | 23,501,217 | -97 |
| 2017/18 | 7 | 722,173,494 | 562 |
| 2016/17 | 10 | 109,163,824 | -89 |
| 2015/16 | 9 | 990,181,705 | 43 |
| 2014/15 | 6 | 692,539,424 | |

**Chanzo**: *Ripoti za Serikali kuu kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19 na Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20.*

Ni Maoni yangu kuwa, kushindwa kukata kodi kunasababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

**Ninashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa kodi ya zuio inakatwa na kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kama inavyoelekezwa na Sheria ya Kodi ya Mapato.**

### 10.11 Usimamizi wa Masurufu Usioridhisha

Kanuni ya 103 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001 inaelekeza kuwa masurufu yarejeshwe mara baada ya dhumuni la masurufu hayo kuisha na kwa vyovyote vile, mwisho wa mwaka wa fedha husika, vinginevyo iwe imeruhusiwa na kanuni nyingineyo ya Kanuni za Fedha.

Kila mwaka, nimetoa rai kuhusu usimamizi wa masurufu usioridhisha, kama vile masurufu kutokutumiwa ipasavyo, ucheleweshaji wa kurejesha masurufu baada ya muda kuisha, kutokuwa na daftari la masurufu na watumishi kupewa masurufu mengine kabla ya kurejesha waliyopewa mwanzo.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini kuwa taasisi 15 zilikuwa na masurufu jumla ya Sh. 2,115,877,781 ambayo hayajarejeshwa. Vilevile, kumekuwa na ucheleweshaji wa kurejesha masurufu ya kiasi cha Sh. 196,090,597 baada ya muda wake kuisha, hadi siku 364 kwa taasisi tatu. **Jedwali Na. 102** hapa chini linaonesha mchanganuo wa masurufu ambayo hayajarejeshwa.

**Jedwali Na. 102: Masurufu ambayo Hayajarejeshwa**

| Na. | Taasisi | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali - Fungu 19 | 57,499,980 |
| 2 | Jeshi la Magereza - Fungu Na. 29 | 82,313,640 |
| 3 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Fungu Na. 52 | 47,065,000 |
| 4 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Fungu Na. 57 | 273,127,390 |
| 5 | Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Umma - Fungu Na. 94 | 14,694,000 |
| 6 | Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri - Fungu Na. 30 | 30,000,000 |
| 7 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Fungu Na. 34 | 457,264,729 |
| 8 | Wizara ya Katiba na Sheria - Fungu Na. 41 | 8,066,343 |
| 9 | Wizara ya Viwanda na Biashara - Fungu Na. 44 | 29,765,000 |
| 10 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi - Fungu Na. 61 | 278,492,668 |
| 11 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia - Fungu Na. 46 | 365,556,034 |
| 12 | Sekretarieti ya Mkoa Lindi | 21,929,600 |
| 13 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Fungu Na. 48 | 433,493,690 |
| 14 | Tume ya Huduma ya Walimu - Fungu Na. 2 | 4,476,000 |
| 15 | Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi | 12,133,707 |
| | **Jumla** | **2,115,877,781** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Taarifa zaidi za ucheleweshwaji wa kurejesha masurufu ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 103 na 104** hapo chini.

**Jedwali Na. 103: Taasisi ambazo Masurufu Yalichelewa Kurejeshwa**

| Na | Taasisi | Kiasi(Sh.) | Kuchelewa |
|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Fungu 16 | 44,540,176 | Hadi siku 270 |
| 2 | Tume ya Taifa katika Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) - Fungu 18 | 95,305,070 | Hadi siku 180 |
| 3 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali - Fungu 19 | 56,245,351 | Siku tatu hadi 364 |
| **Jumla** | | **196,090,597** | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

**Jedwali Na. 104: Mtiririko wa Masurufu Yasiyorejeshwa kwa miaka mitano**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2019/20 | 15 | 2,115,877,781 |
| 2018/19 | 25 | 5,430,595,090 |
| 2017/18 | 28 | 6,356,450,927 |
| 2016/17 | 7 | 135,767,151 |
| 2015/16 | 9 | 397,575,730 |
| 2014/15 | 3 | 232,695,369 |

*Chanzo: Ripoti za Serikali kuu kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19 na Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20.*

Mtiririko wa kutokurejesha masurufu kwa wakati kwa kipindi cha miaka sita unaonesha kuwa bado kuna udhaifu kwenye usimamizi wa fedha kwenye sekta ya Umma ikiwa ni pamoja na usimamizi wa masurufu kwa kuzingatia Kanuni za Fedha. Iwapo hali hii itaendelea inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Umma.

**Ninaendelea kushauri Maafisa Masuuli kuboresha mifumo ya udhibiti kwenye usimamizi wa masurufu ili kuhakikisha masurufu yanarejeshwa kwa wakati kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha.**

### 10.12 Mapungufu Kwenye Uidhinishaji wa Malipo Sh. 3,233,703,014.33

Kanuni ya 88(1) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001 inaelekeza kuwa Afisa Masuuli au afisa yeyote aliyekasimiwa na Afisa Masuuli anaweza kuidhinisha hati ya malipo kabla ya kufanya malipo.

Ukaguzi huu pia umebaini kuwa taasisi saba zilifanya malipo yenye jumla ya Sh. 3,233,703,014 bila ya hati za malipo husika kuidhinishwa.

Kukosekana kwa saini za waidhinishaji wa malipo kwenye hati za malipo umesababishwa na udhaifu kwenye mifumo ya udhibiti katika uandaaji na uidhinishaji wa hati za malipo. Kuna hatari kuwa watumishi wasio waaminifu wanaweza kutumia fursa hii kutumia vibaya fedha za Umma.

Ikilinganishwa na mwaka uliopita, idadi ya taasisi zenye dosari hii imepungua kutoka taasisi nane hadi saba wakati kiwango kimeongezeka kutoka Sh. 719,479,937.89 hadi Sh. 3,233,703,014.33. Hii inaonesha kuwa menejimenti husika zinatakiwa kuboresha mifumo ya udhibiti ili kuhakikisha kuwa malipo yanaidhinishwa ipasavyo. Rejea **Jedwali Na. 105** hapo chini kuona orodha kamili.

**Jedwali Na. 105: Taasisi zenye Dosari kwenye Kuidhinisha Malipo**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto – Fungu Na. 52 | 42,362,000.00 |
| 2 | Tume ya Taifa katika Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) -Fungu Na.18 | 1,989,440.00 |
| 3 | Msajili wa Vyama vya Siasa -Fungu Na. 27 | 10,489,624.00 |
| 4 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi -Fungu Na. 61 | 119,207,203.00 |
| 5 | Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu -Fungu Na. 65 | 20,155,000.00 |
| 6 | Sekretarieti ya Mkoa Simiyu | 2,270,000.00 |
| 7 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania -Fungu Na. 38 | 3,037,229,747.33 |
| **Jumla** | | **3,233,703,014.33** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

**Ninashauri menejimenti za taasisi husika kuhakikisha kuwa hati zote za malipo zinaidhinishwa na maafisa husika kwa mujibu wa kanuni za fedha.**

### 10.13 Ukaguzi wa Fedha za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Ukaguzi wa fedha za uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika tarehe 24 Novemba, 2019 na kusimamiwa na Halmashauri, Sekretarieti za Mikoa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI).

Ili kufanikisha zoezi la uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipokea fedha kiasi cha Sh. 14,361,005,109 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya Sh. 11,216,727,241.86 zilikuwa zimetumika, Kati ya fedha zilizobaki Sh. 2,506,507,196 zilirudishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, Sh. 596,393,671.24 hazikutumika; na Sh. 41,377,000 zilitolewa benki kwa ajili ya malipo mbalimbali, ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 zilikuwa hazijalipwa kwa wahusika.

Muhtasari wa dosari zilizobainika wakati wa ukaguzi ni kama ifuatavyo.

#### 10.13.1 Kubadili Matumizi ya Fedha za Uchaguzi bila Kibali Sh. 1,628,589,361

Nilibaini kuwa OR-TAMISEMI na Halmashauri 29 zililipa jumla ya Sh. 1,628,589,361 kwa ajili ya matumizi ambayo hayakuwa kwenye bajeti ya shughuli za Uchaguzi. Pia, hakukuwa na ushahidi wa kibali cha matumizi hayo. Matumizi hayo ni kama vile, ununuzi wa mafuta ambayo hayakutumika kwenye shughuli za uchaguzi, uandaaji wa maelekezo ya uanzishwaji wa maeneo ya kiutawala ya Serikali za Mitaa, malipo ya hati za ardhi za Halmashauri, ukarabati wa magari na kompyuta ambazo hazikuwa zinatumika kwenye uchaguzi na kufuatilia utatuzi wa migogoro sehemu za kambi za wakimbizi. Rejea **Jedwali Na. 106** kwa maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 106: Halmashauri Zilizobadili Matumizi ya Fedha za Uchaguzi**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Karatu | 6,264,980.53 | 16 | Wilaya ya Nyasa | 33,920,000 |
| 2 | Wilaya ya Longido | 7,210,000.00 | 17 | Wilaya ya Songea | 7,287,000 |
| 3 | Wilaya ya Monduli | 4,600,000 | 18 | Manispaa ya Songea | 1,800,000 |
| 4 | Wilaya ya Ngorongoro | 1,100,000 | 19 | Manispaa ya Tabora | 2,565,000 |
| 5 | Wilaya ya Kibondo | 3,623,750 | 20 | Wilaya ya Nzega | 14,500,000 |
| 6 | Wilaya ya Uvinza | 5,200,000 | 21 | Wilaya ya Hai | 13,312,726 |

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Wilaya ya Njombe | 56,462,939 | 22 | Wilaya ya Moshi | 2,620,000 |
| 8 | Wilaya ya Kongwa | 3,136,000 | 23 | Wilaya ya Simanjiro | 23,484,000 |
| 9 | Wilaya ya Kilosa | 24,293,777 | 24 | Wilaya ya Magu | 15,465,254 |
| 10 | Wilaya ya Mkinga | 2,612,500 | 25 | Wilaya ya Kwimba | 23,251,100 |
| 11 | Wilaya ya Muheza | 20,983,000 | 26 | Wilaya ya Ukerewe | 6,436,640 |
| 12 | Wilaya ya Lindi | 14,576,620 | 27 | Wilaya ya Buchosa | 118,638,575 |
| 13 | Wilaya ya Madaba | 3,311,000 | 28 | Manispaa ya Ilemela | 30,703,000 |
| 14 | Mji wa Mbinga | 25,182,000 | 29 | Wilaya ya Sengerema | 3,464,062 |
| 15 | Wilaya ya Namtumbo | 17,623,000 | 30 | OR-TAMISEMI | 1,134,962,435 |
| **Jumla** | | | | | **1,628,589,361** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kufanya matumizi nje ya lengo lililokusudiwa iliathiri utekelezaji shughuli nyingine za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**Ninashauri Afisa Masuuli OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa fedha za uchaguzi zinatumika kama ilivyokusudiwa, au kuomba kibali kutoka Mlipaji Mkuu wa Serikali kabla ya matumizi. Vilevile, hatua stahiki zichukuliwe kwa maafisa waliohusika kutumia fedha kinyume na malengo ya uchaguzi.**

### 10.13.2 Matumizi yenye Nyaraka Pungufu

OR-TAMISEMI, na ofisi 46 za Serikali za Mitaa (Halmashauri 41 na Sekretarieti za mikoa mitano) zilifanya malipo yenye jumla ya Sh. 2,141,019,933 yenye nyaraka pungufu kama vile risiti za kukiri mapokezi,malipo kutokuwa na sahihi za walipwaji, ukosefu wa taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizofanyika,na kutokuingiza mali kwenye vitabu.

Kwa upande mwingine, hati za malipo jumla ya Sh. 389,160,384.31 hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi na OR-TAMISEMI na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Sekretarieti za Mikoa miwili na Halmashauri nne). Hivyo, nilishindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo. Vilevile, nilibaini kuwa, fedha kiasi cha Sh. 76,374,000 zilichukuliwa benki lakini menejimenti ya OR-TAMISEMI ilishindwa kuwasilisha uthibitisho wa shughuli zilizofanyika. Kwa taarifa zaidi, tazama **Jedwali Na. 107 na 108** hapo chini.

**Jedwali Na. 107: Taasisi Zilizofanya Malipo yenye Nyaraka Pungufu**

| Na. | Halmashauri/ Taasisi | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri/Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Longido | 2,438,840 | 25 | Mji wa Tunduma | 7,359,000 |
| 2 | Wilaya ya Meru | 2,000,000 | 26 | Wilaya ya Ileje | 8,790,000 |
| 3 | Wilaya ya Kalambo | 27,513,592 | 27 | Mji wa Mbinga | 20,070,000 |
| 4 | Wilaya ya Sumbawanga | 59,400,000 | 28 | Wilaya ya Kilolo | 10,860,000 |
| 5 | Manispaa ya Sumbawanga | 36,850,000 | 29 | Sekretarieti ya Mkoa Iringa | 16,681,826 |
| 6 | Wilaya ya Nkasi | 6,246,000 | 30 | Sekretarieti ya Mkoa Tabora | 12,367,470 |
| 7 | Wilaya ya Maswa | 54,565,008 | 31 | Wilaya ya Sikonge | 2,148,000 |
| 8 | Sekretarieti ya Mkoa Simiyu | 25,320,070 | 32 | Wilaya ya Tabora | 55,495,961 |
| 9 | Wilaya ya Bariadi | 17,998,416 | 33 | Wilaya ya Nzega | 72,443,000 |
| 10 | Wilaya ya Busega | 8,400,000 | 34 | Wilaya ya Kishapu | 10,867,300 |
| 11 | Wilaya ya Itilima | 95,928,040 | 35 | Manispaa ya Shinyanga | 32,550,000 |
| 12 | Wilaya ya Meatu | 54,910,400 | 36 | Wilaya ya Babati | 170,595,579 |
| 13 | Wilaya ya Bariadi | 39,288,000 | 37 | Wilaya ya Simanjiro | 138,425,000 |
| 14 | Wilaya ya Mpimbwe | 4,427,320 | 38 | Sekretarieti ya Mkoa Kilimanjaro | 963,795 |
| 15 | Sekretarieti ya Mkoa Katavi | 96,159,000 | 39 | Wilaya ya Hai | 145,435,400 |
| 16 | Wilaya ya Kibiti | 67,300,756 | 40 | Wilaya ya Moshi | 317,433,102 |
| 17 | Wilaya ya Rufiji | 11,495,000 | 41 | Wilaya ya Bunda | 9,210,000 |
| 18 | Wilaya ya Chalinze | 10,987,000 | 42 | Mji wa Bunda | 4,831,200 |
| 19 | Manispaa ya Kigoma Ujiji | 10,722,000 | 43 | Sekretarieti ya Mkoa Mara | 7,550,000 |
| 20 | Wilaya ya Buhigwe | 46,216,348 | 44 | Wilaya ya Butiama | 10,405,000 |
| 21 | Wilaya ya Uvinza | 22,434,000 | 45 | Wilaya ya Serengeti | 59,780,000 |
| 22 | Wilaya ya Liwale | 11,380,000 | 46 | Sekretarieti ya Mkoa Mwanza | 32,015,142 |

| Na. | Halmashauri/ Taasisi | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri/Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 23 | Wilaya ya Lindi | 6,550,000 | 47 | OR-TAMISEMI | 267,397,368 |
| 24 | Wilaya ya Songwe | 8,816,000 | | **Jumla** | **2,141,019,933** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

**Jedwali Na. 108: Hati za Malipo ambazo Hazikuwasilishwa**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Sekretarieti ya Mkoa Simiyu | 16,071,404.76 |
| 2 | Sekretarieti ya Mkoa Pwani | 6,038,100.00 |
| 3 | Wilaya ya Gairo | 15,880,700.00 |
| 4 | Wilaya ya Nachingwea | 147,659,591.57 |
| 5 | Wilaya ya Kilwa | 48,790,000 |
| 6 | Manispaa ya Lindi | 62,700,818 |
| 7 | Wilaya ya Kishapu | 65,747,583.53 |
| 8 | OR-TAMISEMI | 26,272,186.45 |
| **Jumla** | | **389,160,384.31** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

### 10.13.3 Ununuzi Maradufu wa Vidau vya Wino na Wino wa Mihuri Sh. 199,991,209

OR-TAMISEMI ilielekeza mamlaka zote za Serikali za Mitaa kwenye bajeti zao kununua vitu vyote kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na vidau vya wino na wino wa mihuri. Nilibaini kuwa, OR-TAMISEMI ilinunua vifaa hivyo kwa gharama ya Sh. 199,991,209 ambavyo havikutumika wakati wa uchaguzi hivyo kutopatikana kwa thamani ya fedha.

**Nashauri OR-TAMISEMI kuboresha udhibiti wa mfumo wa bajeti za Halmashauri na kuwa na mpango madhubuti ili kuepuka bajeti zenye vifungu maradufu na ununuzi wa vifaa hivyohivyo. Pia, kuwa na mpango wa matumizi ili kuhakikisha vifaa vilivyonunuliwa vinatumika.**

### 10.13.4 Malipo Nje ya Bajeti Sh. 244,778,685.68

Afisa Masuuli OR - TAMISEMI alitoa maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri akisisitiza kuzingatia bajeti kama ilivyoidhinishwa kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka 2019.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Halmashauri 14 hazikuzingatia maelekezo hayo kwa kufanya matumizi kiasi cha Sh. 244,778,685.68 nje ya bajeti iliyoidhinishwa kama ilivyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 109** lifuatalo.

**Jedwali Na. 109: Taasisi zilizofanya Malipo Nje ya Bajeti**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Jiji la Arusha | 11,304,237 |
| 2 | Wilaya ya Meatu | 29,603,234.68 |
| 3 | Manispaa ya Tabora | 33,750,000.00 |
| 4 | Wilaya ya Tabora | 3,610,000 |
| 5 | Manispaa ya Temeke | 34,500,000 |
| 6 | Wilaya ya Bunda | 12,568,672 |
| 7 | Mji wa Bunda | 9,987,200 |
| 8 | Mji wa Tarime | 5,258,997 |
| 9 | Wilaya ya Nkasi | 26,840,885 |
| 10 | Wilaya ya Kisarawe | 18,940,860 |
| 11 | Wilaya ya Mafia | 16,596,000 |
| 12 | Wilaya ya Rufiji | 15,665,600 |
| 13 | Wilaya ya Kibiti | 9,653,000 |
| 14 | Wilaya ya Chalinze | 16,500,000 |
| | Jumla | **244,778,685.68** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kwavile shughuli zote zilipangwa na Halmashauri kabla ya kuidhinishwa bajeti, kufanya matumizi nje ya bajeti huenda ikahusisha matumizi yasiyofaa ya fedha za uchaguzi.

**Ninashauri Wakurugenzi Watendaji husika kuhakikisha wanazingatia maelekezo kama yanavyotolewa na mamlaka husika. Pia hatua stahiki zichukuliwe kwa maafisa waliohusika kufanya malipo nje ya bajeti.**

### 10.13.5 Malipo Yaliyofanyika bila Kudai Risiti za Kielekitroniki Sh. 388,837,928

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Halmashauri 24 na Sekretarieti ya Mkoa mmoja zililipa jumla ya Sh. 388,837,928 kwa wazabuni mbalimbali wa huduma na vifaa bila kudai risiti za kielekitroniki kinyume na Kanuni 28(1) ya Kodi ya Mapato, 2012. Rejea **Jedwali Na. 110** hapo chini kwa orodha kamili.

**Jedwali Na. 110: Taasisi zilizofanya Malipo bila Kudai Risiti za Kielekitroniki**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) | Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Ngorongoro | 17,949,424 | 14 | Wilaya ya Uvinza | 5,143,476 |
| 2 | Wilaya ya Chato | 31,184,400 | 15 | Wilaya ya Karagwe | 6,457,000 |
| 3 | Wilaya ya Kalambo | 6,670,000 | 16 | Wilaya ya Kyerwa | 22,657,650 |
| 4 | Wilaya ya Nsimbo | 8,254,000 | 17 | Wilaya ya Missenyi | 4,800,500 |
| 5 | Wilaya ya Mlele | 38,769,257 | 18 | Wilaya ya Kilolo | 12,585,000 |
| 6 | Sekretarieti ya Mkoa Katavi | 8,168,967 | 19 | Manispaa ya Iringa | 4,550,000 |
| 7 | Wilaya ya Mafia | 6,664,000 | 20 | Wilaya ya Mufindi | 1,239,000 |
| 8 | Wilaya ya Rufiji | 12,247,412 | 21 | Wilaya ya Musoma | 4,349,500 |
| 9 | Wilaya ya Mkuranga | 11,674,700 | 22 | Wilaya ya Rorya | 26,343,004 |
| 10 | Wilaya ya Kibiti | 45,468,414 | 23 | Wilaya ya Tarime | 33,400,766 |
| 11 | Manispaa ya Kigoma Ujiji | 11,975,260 | 24 | Mji wa Tarime | 21,773,200 |
| 12 | Wilaya ya Kibondo | 4,407,000 | 25 | Wilaya ya Serengeti | 40,527,998 |
| 13 | Wilaya ya Buhigwe | 1,578,000 | | **Jumla** | **388,837,928** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kutokudai risiti za kielekitroniki kunadhoofisha juhudi za Serikali kukusanya mapato.

**Ninashauri menejimenti za taasisi husika kudai risiti za kielekitroniki malipo yanapofanyika kwa wazabuni wa mali na huduma. Vilevile, kuacha ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni wasiotoa risiti za kielekitroniki.**

### 10.13.6 Masurufu Yasiyorejeshwa Sh. 111,799,630

Agizo Na. 40(3) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inaelekeza kuwa, masurufu yarejeshwe ndani ya siku 14 baada ya kukamilika kwa kazi husika. Kushindwa kufanya hivyo sio tu kwamba masurufu yasiyorejeshwa yatakatwa kwenye mshahara kwa mtumishi

husika kwa kiwango maalumu, bali kutoza adhabu ya tozo kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa.

Ukaguzi ulibaini kuwa masurufu yenye jumla ya Sh. 111,799,630 yaliyotolewa kwa maafisa mbalimbali kwenye taasisi 11 yalikuwa hayajarejeshwa hadi kufikia tarehe 30 June 2020. Orodha ya taasisi zenye masurufu inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 111**

**Jedwali Na. 111: Halmashauri Ambazo zina Masurufu Yasiyorejeshwa**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Bukoba | 10,904,430 |
| 2 | Wilaya ya Chato | 2,435,000 |
| 3 | Wilaya ya Hai | 10,440,000 |
| 4 | Manispaa ya Iringa | 4,550,000 |
| 5 | Wilaya ya Kilwa | 1,200,000 |
| 6 | Wilaya ya Kishapu | 4,752,500 |
| 7 | Wilaya ya Liwale | 5,320,000 |
| 8 | Wilaya ya Nachingwea | 7,030,000 |
| 9 | Sekretarieti ya Mkoa Lindi | 58,705,200 |
| 10 | Wilaya ya Tabora | 4,624,500 |
| 11 | Wilaya ya Urambo | 1,838,000 |
| **Jumla** | | **111,799,630** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Kutokurejesha masurufu kwa wakati inaweza kusababisha fedha kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa au kutumika vibaya.

**Ninashauri kuwa Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa masurufu yote yanarejeshwa kwa wakati. Pia, hatua stahiki zichukuliwe kwa maafisa wasiorejesha masurufu kama ilivyoelekezwa na Agizo namba 40(3) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.**

### 10.13.7 Viashiria vya Ubadhirifu katika Fedha za Uchaguzi kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Sh 46,000,000

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilipokea kiasi cha Sh. 402,475,268 kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (**OR-TAMISEMI**) kugharamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika tarehe 24 Novemba, 2019 katika Mitaa 142 na Kata 23. Fedha hizo zilipaswa kutumika kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa tu na si kwa matumizi mengine. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo;

Kiasi cha Sh. 46,000,000 kililipwa kama Masurufu kwa maafisa wa Halmashauri kwa ajili ya kukodi magari ya matangazo ili kuhamasisha

wananchi kushiriki uchaguzi huo. Fedha hiyo ililipwa tarehe 16 Desemba, 2019 licha ya kwamba uchaguzi ulifanyika tarehe 24 Novemba, 2019. Baada ya kupitia nyaraka za marejesho ya masurufu (*retirement particulars*) nilibaini kuwa baadhi ya hati za madai (*invoices*) zilikuwa za tarehe za mwezi Machi, 2020 licha ya kuwa uchaguzi ulikwisha fanyika. Vilevile, hati za madai hazikuonesha idadi ya magari, muda wa kutoa matangazo wala gharama kwa kila gari.

**Kutokana na mapungufu yaliyotajwa hapo juu, kuna uwezekano kuwa fedha jumla ya Sh. 46,000,000 zilitumika kwa malengo yasiyokusudiwa. Ninamshauri Afisa Masuuli kufanya uchunguzi wa masurufu hayo na kuchukua hatua stahiki.**

### 10.13.8 Ununuzi kwa kutumia Masurufu zaidi ya Kiwango Sh. 149,944,500

Kanuni ya 166(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma yam waka 2013 (na marekebisho ya mwaka, 2016) inaeleza bayana ununuzi mdogo wa bidhaa na huduma unaweza kufanyika moja kwa moja kutoka maduka makubwa au maduka ya dawa, kama thamani ya ununuzi haizidi kikomo kilichowekwa katika jedwali la saba la Kanuni za Ununuzi.

Katika ukaguzi wa fedha za uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri mbalimbali nilibaini ununuzi wa bidhaa na huduma jumla ya Sh. 149,944,500 ulifanyika kwa fedha taslimu/masurufu bila ya kuzingatia kikomo cha Sh. 5,000,000 cha ununuzi mdogo kama ilivyoelekeza na kanuni tajwa hapo juu. **Jedwali Na. 112** hapo chini linaonesha Taasisi zilizofanya ununuzi kwa kutumia masurufu.

**Jedwali Na. 112: Halmashauri Zilizofanya Ununuzi kwa Kutumia Masurufu Sh 149,944,500**

| Na | Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Maswa | 20,643,500 |
| 2 | Wilaya ya Itilima | 13,597,500 |
| 3 | Wilaya ya Meatu | 33,356,000 |
| 4 | Manispaa ya Lindi | 11,250,000 |
| 5 | Manispaa ya Musoma | 71,097,500 |
| **Jumla** | | **149,944,500** |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2019/20*

Ununuzi kwa kutumia masurufu/fedha taslimu zaidi ya kiwango cha Sh. 5,000,000 ni ukiukwaji wa Kanuni ya 166(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 (na marekebisho ya mwaka, 2016).

**Natoa ushauri kwa menejimenti ya Halmashauri husika kuhakikisha zinazingatia kikamilifu Sheria ya Ununuzi wa Umma Na 7 ya mwaka 2011 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) pamoja na Kanuni zake.**

## SURA YA KUMI NA MOJA

## USIMAMIZI WA MALI NA MADENI

### 11.1 Utangulizi

Katika kusimamia mali na madeni, Serikali imeandaa Sheria, Kanuni, miongozo na taratibu kwa ajili ya udhibiti na usimamizi wa mali na madeni ya Serikali kuanzia utunzaji wa kumbukumbu, matumizi, utathmini wa mali na utoaji wa taarifa. Katika ukaguzi wa mwaka 2019/20 nilijikita katika kuhakikisha uwepo wa tija na uwajibikaji katika matumizi ya mali za umma pamoja na madeni. Aidha, nililenga kujiridhisha kama Serikali inasimamia ipasanyo matumizi ya mali na mtiririko wa fedha ili kupunguza hatari na hasara zitokanazo na kuchelewa kulipa madeni kwa wakati.

### 11.2 Ukaguzi wa Usimamizi wa Mali

Katika ukaguzi niliofanya mwaka huu wa fedha, 2019/20 nimebaini mapungufu kadhaa ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha udhibiti wa mali za serikali. Mapungufu hayo ni kama yafuatayo;

#### 11.2.1 Udhibiti Usioridhisha wa Usajili wa Magari ya Serikali katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Secta ya Ujenzi)

Kifungu Na. 62 cha Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara) kinaeleza kuwa Mhandisi Mkuu wa Umeme na Mitambo wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano atahifadhi na kutunza Rejista ya Magari yote ya Serikali pamoja na Trela zinazomilikiwa na Serikali. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa taratibu za usajili wa magari ya serikali nilibaini mapungufu mbalimbali kama yanavyoonekana hapa chini:

a) Nilibaini kuwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano haishiriki katika zoezi la kukagua magari baada ya kuwasili ili kuthibitisha kuwa yanakidhi vigezo“specifications” vilivyotolewa na Taasisi/Wizara wakati wa kuagiza gari; hivyo, kuwapo na uwezekano wa muuzaji husika kukiuka vigezo “specifications” vilivyotolewa wakati wa kuanza mchakato wa ununuzi wa magari.

b) Vilevile, nilibaini kutokuwapo kwa mfumo wa Kielektroniki wa kunakili na kutunza taarifa za usajili wa magari. Wakati wa ukaguzi magari yalikuwa yanasajiliwa kwenye nyaraka na taarifa kuandikwa katika Rejista maalumu. Hivyo, kuna uwezekano kuwa taarifa za

usajili kupotea kutokana na utunzaji wa taarifa na kumbukumbu usioridhisha.

c) Aidha, nilibaini kuwa baada ya usajili kufanyika, Wizara inatoa vyeti vya usajili wa magari. Hata hivyo, kwa kutumia utaratibu huu ni vigumu kuweka maelezo ya ziada ya mali kwa mfano gari inapohamishwa kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine, gari inapouzwa n.k. Hivyo Wizara inaweza kupata shida kusahihisha taarifa za gari ikiwa kuna uhitaji. Wakati wa ukaguzi wa sampuli ya magari yaliyosajiliwa kutoka mwaka wa fedha 2007/08 hadi 2019/20 nilibaini kuwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilikuwa imesajili jumla ya magari 27,595 ya Serikali Kuu na kuyapatia majina ya usajili: ST, na DF, yakifuatiwa na nambari maalumu. Pia, nilibaini kuwa regista ya usajili wa magari haikuwa na taarifa ya magari yaliyouzwa, kufutiwa usajili, au umiliki wake uliohamishiwa kwenda Taasisi zingine.

d) Niligundua kuwa vyeti vya usajili wa magari vinavyotolewa na Wizara havionyeshi namba ya kadi ya gari. Hivyo, ni vigumu kulinganisha idadi ya magari yaliyosajiliwa pamoja na vyeti vya usajili vilivyotolewa.

e) Pia, kuna kanzidata ya taarifa za magari ya Serikali zinazotunzwa katika taasisi mbalimbali, hivyo kuwa vigumu kutambua idadi kamili ya magari ya serikali. Katika Ukaguzi nilioufanya, nilibaini kuwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inasajili magari ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali pamoja na magari ya Polisi, Jeshi la zima moto, na Idara ya uhamiaji tofauti na hapo taasisi zingine kama Mamlaka ya Mapato Tanzania inasajili magari ya Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika ya Umma. Pia, magari ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania wanasajili magari yao wenyewe

Mapungufu yaliyobainika hapo juu yanatokana na kukosekana kwa miongozo na taratibu zilizo ainishwa vizuri kuhusu usajili wa magari ya serikali. Hivyo, kupelekea magari ya serikali kuwa katika hatari ya kutumika vibaya na pengine kusababisha hasara kwa serikali.

**Hivyo, ninaishauri Serikali kuandaa Miongozo itakayosimamia mchakato wa usajili wa Magari ya Serikali. Aidha, ninapendekeza Serikali ianzishe mfumo wa Kielektroniki utakotumika katika usajili na uhifadhi wa taarifa za magari, pikipiki na mitambo yote inayomilikiwa na Serikali**

pamoja na yale ya Jeshi la wananchi, jeshi la Polisi, jeshi la zima moto na idara ya Uhamiaji utakao simamiwa na wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (sekta ya ujenzi) ili Serikali iweze kudhibiti magari yake.

### 11.2.2 Utunzaji Hafifu wa Daftari la Mali za Serikali Zisizo Hamishika

Aya ya 12 ya Muongozo wa Kusimamia Mali za Kudumu za Serikali wa 2019, inataka rejista ya mali kuhifadhiwa na Mlipaji Mkuu wa serikali kwenye mfumo wa pamoja na kufuata Viwango vya kimataifa vya uhasibu. Muongozo unataka rejista ya mali iwe na taarifa muhimu za mali kama nambari ya usajili wa gari, nambari ya orodheshwaji wa mali, nambari ya utambuzi wa mali, nambari ya kiwanja, tarehe ya ununuzi wa mali, gharama n.k.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Wizara na Idara tisa, Sekretarieti nne za Mkoa, Wakala tano wa Serikali na Taasisi zingine 11, zilikuwa na regista za mali zenye taarifa pungufu huku taasisi nyingine hazikuwa na regista ya mali. Pia, nilibaini rejista ya mali kwenye taasisi hizo hazikua zimehuishwa ili kwenda na wakati au zilikosa taarifa muhimu za mali ikijumuisha tarehe ya ununuzi wa mali, maelezo ya mali, gharama ya mali kwa muda uliobakia baada yakutoa gharama ya uchakavu, uhamishaji na uuzaji wa mali. Orodha kamili ya taasisi hizo inaonyeshwa katika **Jedwali Na. 113**

**Jedwali Na. 113: Orodha ya Taasisi zenye Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika**

| Na. | Jina la Taasisi | Maelezo |
|---|---|---|
| **Fungu** | **Wizara/Idara** | |
| **18** | Tume ya Kitaifa ya UNESCO | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| **37** | Ofisi ya Waziri Mkuu | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 40 | Mahakama ya Tanzania | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 44 | Wizara ya Viwanda Na biashara | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 46 | Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 52 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 60 | Wizara ya Viwanda na Biashara | kutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |

| Na. | Jina la Taasisi | Maelezo |
|---|---|---|
| 68 | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano | utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| Na | **Taasisi nyingine za Serikali** | |
| 1 | Kampuni ya Mzinga | kutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |
| 2 | Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Jamii (CBCTC) | kutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |
| 3 | Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 4 | Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela Afrika | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 5 | Kituo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 6 | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania | kutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |
| 7 | Mfuko wa Maendeleo | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 8 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Morogoro | Kutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Njombe | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 10 | Hospitali ya Rufaa ya Sokoine | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 11 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| Na | **Wakala** | |
| 1 | Wakala wa huduma za manunuzi wa Serikali | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 2 | Wakala wa Mbegu za Kilimo | Kutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |
| 3 | Wakala wa Kitaifa wa Utafiti wa Nyumba na Ujenzi | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 4 | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini Tanzania (TARURA) | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 5 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| Na. | **Sekretarieti za Mkoa** | |
| 1 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | Kutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |
| 2 | Sekretarieti ya mkoa wa Kigoma | Utunzaji hafifu wa daftari la mali zisizo hamishika |
| 3 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | Kkutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |
| 4 | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | Kutokuwapo kwa rejista ya mali isiyohamishika |

*Chanzo: Taarifa za fedha zilizo kaguliwa kwa mwaka 2019/20*

Kukosekana kwa daftari la mali za kudumu pamoja na kukosekana kwa taarifa muhimu za mali katika daftari ya mali ni udhaifu mkubwa katika kulinda mali za serikali dhidi ya upotevu, matumizi mabaya, uharibifu, wizi, na matumizi yasiyoruhusiwa.

**Ninashauri kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, ambaye ni msimamizi mkuu wa mali zote za Umma kuhakikisha kuwa Maafisa Masuuli wa Taasisi zote za Umma (a) Wanatunza daftari la mali za kudumu lenye taarifa zote muhimu kulingana na muongozo wa Mali za Serikali wa mwaka 2019 katika Taasisi zao, (b) Kuhakikisha kuwa Taasisi zinakuwa na nakala ngumu na laini za daftari la mali za kudumu ili kuwezesha uhakiki wa mali na taarifa zinazohusiana na mali kufanyika kwa urahisi.**

### 11.2.3 Mali za Serikali Zilizotelekezwa au Kutotumika kwa Muda Mrefu bila ya Kufanyiwa Matengenezo au Kuuzwa.

Aya 22 ya Mwongozo wa kusimamia Mali za umma wa 2019 unahitaji kupima uchakavu wa mali, haswa wakati mali husika haitumiki, haifanyi kazi au imeharibika. kwa maneno mengine mali hiyo haiwezi kuendelea kutoa huduma inayotakiwa na taasisi. kila mwaka Afisa masuuli anatakiwa kupima uchakavu wa mali ili kuona kama thamani halisi ya mali imepungua.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Taasisi 40 za serikali zilikuwa na magari 293, pikipiki 82, na mali nyingine 2437 ambazo zimetelekezwa kwa muda mrefu bila kutumika. Pia hapakuwa na uthibitisho unaoonyesha kuwa Afisa Masuuli alifanya tathmini ya thamani ya mali za kudumu ili kufanya maamuzi ya aidha kuendelea kufanyia matengenezo mali hizo au kuziuza kama inavyoelekezwa kwenye muongozo wa Serikali na kanuni ya 254 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001.

Aidha, nilifanya ulinganisho wa mali zilizotelekezwa bila ya kuuzwa zilizo ripotiwa katika Taarifa yangu ya mwaka wa fedha 2018/19 na kubaini ongezeko kutoka mali 379 kwa mwaka 2018/19 hadi 2812 kwa mwaka 2019/20. Tazama **Kielelezo Na. 18** hapo chini na **Kiambatisho Na. XXIII** hukusu orodha ya taasisi zilizo na mali zilizotelekezwa.

**Kielelezo Na. 18: Mwenendo wa Mali zisizotumika kwa Muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa.**




Kushindwa kufanya tathimini ya thamani ya mali zisizo tumika kwa muda mrefu hasa magari ina athari hasi katika kuongeza gharama za ukarabati na mapato yanayotokana na uuzaji wa mali hizo.

**Ninapendekeza Mlipaji Mkuu wa Serikali, kwa kushirikiana na Maafisa Masuuli wa taasisi husika, kufanya tathmini ya thamani ya mali ili kuweza kufanya uamuzi stahiki na kwa wakati kuhusiana na matengenezo au uuzaji wa mali.**

### 11.2.4 Ukosefu wa nyaraka za umiliki wa Ardhi na Majengo

Barua yenye kumbukumbu namaba CAB142/626/01/A/42 ya tarehe 26/09/2014 kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi, na barua yenye kumbukumbu namba CNA.32/572/01/96 kutoka kwa Msajili wa Hazina ilielekeza taasisi zote za serikali kuwa na hati miliki ya viwanja vinavyomilikiwa na Serikali.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Taasisi 22 zikiwemo Wizara na Sekretarieti za Mikoa hazikuwa na hati miliki za ardhi wanayomiliki. Aidha, ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19, Taasisi 10 hazikuwa na nyaraka za umiliki wa Ardhi, hivyo kuwa na ongezeko la Taasisi 12 sawa na asilimia 120%. Ongezeko hili limesababishwa na uongozi wa taasisi husika kutoweka mkazo na juhudi katika upatikanaji wa hati miliki za Ardhi wanayomiliki.

**Jedwali Na. 114**: Orodha ya Taasisi Zisizo na nNyaraka za Umiliki wa Ardhi linaonesha orodha ya taasisi za Serikali ambazo hazikuwa na hati miliki ya ardhi.

**Jedwali Na. 114: Orodha ya Taasisi Zisizo na nNyaraka za Umiliki wa Ardhi**

| Na. | Jina la Taasisi | Thamani haikuwapo | Thamani ya mali Sh. |
|---|---|---|---|
| Fungu Na. | Wizara/Idara | | |
| 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika masharaiki | thamani haikuwapo | - |
| 37 | Ofisi ya Waziri mkuu | thamani haikuwapo | - |
| 46 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Technolojia | - | 6,767,259,639 |
| 56 | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | - | 1,000,000,000 |
| 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | thamani haikuwapo | - |
| 64 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | | 466,975,200 |
| 68 | Wizara ya Ujenzi , Uchukuzi na Mawasiliano (fungu Na. 68) | thamani haikuwapo | - |
| Na. | Taasisi zingine za Serikali | | |
| 1 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songwe | - | 322,719,800 |
| 2 | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa | thamani haikuwapo | - |
| 3 | Bodi ya Maabara ya Afya Binafsi | - | 11,298,700 |
| Na. | Wakala | - | - |
| 1 | Kituo cha jemolojia Tanzania | thamani haikuwapo | - |
| 2 | Wakala wa Majengo Tanzania | thamani haikuwapo | |
| 3 | Mamlaka ya viwanja vya ndege | - | 323,154,618,850 |
| 4 | Wakala wa huduma za ununuzi wa Serikali | - | 8,715,000,000 |
| 5 | Wakala wa Elimu na Mafunzo | - | |

| Na. | Jina la Taasisi | Thamani haikuwapo | Thamani ya mali Sh. |
|---|---|---|---|
| | ya uvuvi | | 9,621,750,000 |
| 6 | Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Makazi | thamani haikuwapo | - |
| Na. | sekretarieti ya Mkoa | | |
| 1 | Sekretarieti ya Mkoa Simiyu | - | 3,032,164,000 |
| 2 | Sekretarieti ya Mkoa Iringa | thamani haikuwapo | - |
| 3 | Sekretarieti ya Mkoa Ruvuma | - | 1,652,667,220 |
| 4 | Sekretarieti ya Mkoa Arusha | thamani haikuwapo | - |
| 5 | Sekretarieti ya Mkoa Mwanza | - | 316,974,000 |
| 6 | Sekretarieti ya Mkoa Manyara | thamani haikuwapo | - |
| | Jumla | - | 355,061,427,409 |

*Chanzo: Taarifa za fedha zilizo kaguliwa kwa mwaka 2019/20*

Kutokuwapo kwa hati miliki ya ardhi inaweza kusababisha Serikali kuingia katika migogoro ya ardhi na wananchi.

**Ninapendekeza kuwa, kutokana na umuhimu wa nyaraka hizi kisheria na umuhimu wa kuwa na ushahidi wa umiliki wa mali za umma, Maafisa Masuuli wote watiilie mkazo upatikanaji wa Hati miliki kwa Kamishna wa Ardhi ili kupata Hati hizo.**

### 11.2.5 Majengo ya Serikali Yaliyotelekezwa, Ukarabati Usiokamilika, Majengo Yasiyomaliziwa Kujengwa na Viwanja Visivyoendelezwa.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Serikali ilikuwa na Majengo yaliyotelekezwa,majengo ambayo ukarabati wake haujakamilika, Majengo yasiyomaliziwa kujengwa na viwanja visivyoendelezwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Kati ya taasisi 121 zilizokaguliwa mwaka huu wa fedha, nilibaini kuwa taasisi sita zilikuwa na majengo yaliyotelekezwa, majengo chakavu na majengo yasiyokamilika kwa muda mrefu, taasisi saba zilikuwa na ujenzi wa majengo ambao kasi ya ujenzi ilikuwa ndogo. Aidha, Taasisi tatu

zilikuwa na viwanja ambavyo havijaendelezwa kwa muda mrefu kama ilivyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na. XX**

Kuwapo kwa majengo yaliyotelekezwa, yasiyofanyiwa ukarabati au majengo yasiyokamilika kwa muda mrefu, kuchelewa kuendeleza viwanja vya serikali na ujenzi wa taratibu kusababisha kuongezeka kwa gharama za ujenzi, mazingira yasiyo rafiki katika kazi, na kupotea kwa muda, fedha na mali hizo.

**Ninapendekeza Serikali itenge fedha za kutosha ili kuwezesha ukarabati wa majengo yaliyotelekezwa, yalichochakaa na kumalizia ujenzi wa majengo yasiyokamilika kwa muda uliopangwa**

**Ninapendekeza kuwa, Serikali itafute vyanzo mbadala vya fedha ili kukamilisha ujenzi wa majengo haya, kufanya ukarabati na kuendeleza viwanja vinavyomilikiwa na Serikali.**

### 11.2.6 Ukosefu wa Mpango wa Ukarabati wa Mali na Utunzaji wa Kumbukumbu

Aya ya 14 ya Muongozo wa Usimamizi wa Mali wa Mwaka 2019 inaelekeza kuwa kila Afisa Masuuli anatakiwa kuwa na mpango wa matengezo ya mali wanazozimiliki ili kuhakikisha kuwa mali za Serikali zinatunzwa vizuri na kutumika kama zilivyokusudiwa na si vinginevyo. Hii ni pamoja na utoaji wa huduma na matumizi ya kiuchumi ili kuongeza tija kwa Taasisi husika.

Pia Kanuni ya 137 (4) (a) ya kanuni za Ununuzi ya Umma ya mwaka 2013 (zilizorekebishwa,2016) inataka kila taasisi inayofanya ununuzi kutunza taarifa za matengenezo, ukarabati na ubadilishwaji wa kila gari, Mitambo na vifaa, uwekaji wa umeme, kiyoyozi na jokofu kwa ajili ya kukaguliwa na Wizara inayohusika na uhandisi umeme na mitambo, Mdhibiti na mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Mamlaka na Wakala.

Nilibaini kuwa, Taasisi 16 hazina mpango wa matengenezo ya mali wala hazitunzi kumbukumbu kuhusiana na matengenezo au ukarabati wa magari, mitambo, na mali zingine, kinyume na matakwa ya aya ya 14 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Serikalli wa mwaka 2019, pamoja na Kanuni ya 137(4) (a) ya Kanuni za ununuzi ya Umma za mwaka 2013 (zilizorekebishwa mwaka 2016). Ikilinganishwa na mwaka 2018/19, Taasisi zenye mapungufu haya zimepungua kutoka taasisi 17 (2018/19) hadi 16 (2019/20). Mapungufu yaliyobainika yanatokana na Taasisi husika kushindwa kuwa na mikakati madhubuti ya matengenezo ya magari na mali

zingine kama miongozo inavyoelekeza. Orodha ya Taasisi zenye mapungufu yaliyoelezwa hapo juu zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 115** hapa chini.

**Jedwali Na. 115: Orodha ya Taasisi zisizo na Mpango wa ukarabati na utunzaji wa kumbukumbu.**

| Na. | Jina la Taasisi |
|---|---|
| **Wizara/Idara** | |
| 1 | Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (fungu Na. 24) |
| 2 | Ofisi ya Makamu wa Rais (fungu Na. 31) |
| 3 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (fungu Na. 46) |
| 4 | Wizara ya maliasili na utalii (fungu Na. 69) |
| 5 | Ofisi ya Rais - Tume ya utumishi wa uma (fungu Na. 94) |
| **Sekretarieti za Mkoa** | |
| 1 | Sekretarieti ya Mkoa Iringa |
| 2 | Sekretarieti ya Mkoa Kilimanjaro |
| 3 | Sekretarieti ya Mkoa Njombe |
| **Taasisi nyingine** | |
| 1 | Kampuni ya Ulinzi SUMSJKT |
| 2 | Shilika la huduma za kitaifa (SUMA HQ) |
| 3 | Hopitali ya Rufaa ya Mkoa Amana |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tumbi |
| 5 | Hospitali ya Rufaa Ya Mkoa Morogoro |
| 6 | Tume ya Pamoja ya Fedha |
| **Wakala** | |
| 1 | Wakala wa usajili wa ufilisi na udhamini (RITA) |
| 2 | Wakala wa huduma za ununuzi wa Serikali |

*Taarifa za fedha zilizo kaguliwa kwa mwaka 2019/20*

Kukosekana kwa mpango wa matengenezo ya mali za Serikali pamoja na kushindwa kutunza kumbukumbu kuhusiana na historia ya mali, utendaji wake, ukarabati na matengenezo ni ukiukwaji wa sheria zilizotajwa hapo juu ambazo zinapelekea manejimenti kushindwa kufanya maamuzi sahihi kuhusiana na usimamizi wa mali.

**Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Taasisi Nyingine zinashauriwa kuandaa mpango wa matengenezo ya mali na kuhakikisha kuwa taarifa kuhusiana na matengenezo ya mali za Serikali zinahifadhiwa vizuri.**

### 11.2.7 Mali za Serikali Kutoandikwa Namba za Utambulisho au Kutokusajiliwa Sh. 49,028,233,598

Aya ya 9 ya Muongozo wa Usimamizi wa Mali za Kudumu za Serikali wa mwaka 2019 inataka kila mali ya kudumu iliyonunuliwa au kupokelewa na taasisi ya umma kuandikwa namba ya utambilisho kutegemea na aina ya mali husika. Kwa mfano, magari yatambuliwe kwa namba ya usajili, ardhi itambuliwe kwa namba ya kiwanja, wakati samani na vifaa vingine vitambulike kwa namba ya utambuzi wa mali husika.

Wakati wa ukaguzi, Taasisi 16 zilizokuwa na mali za kudumu ambazo hazijaandikwa namba ya utambulisho kama inavyoelekezwa na Aya ya 9 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Kudumu za Serikali ya mwaka 2019. Pia, nilibaini kuwa pikipiki nne zenye thamani ya Sh 10,819,200 zilizo nunuliwa na Sekretariati ya Mkoa wa Kagera na kuhifadhiwa bila kusajiliwa katika mfumo wa usajili wa magari ya serikali.

Aidha, nilibaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango, Hospitali ya Rufaa ya Iringa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Ligula ambazo zimeweka rekodi ya juu ya thamani ya mali zisizo na nambari za utambulisho zenye thamani ya Sh. 46,751,382,233, Sh. 491,747,100 na Sh. 481,171,725 mtawalia. Orodha kamili ya taasisi zenye mali za kudumu zisizo na namba za utambulisho zimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 116** hapa chini.

**Jedwali Na. 116: Orodha ya taasisi zenye mali zisizo na namba ya utambulisho**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi Sh |
|---|---|---|
| **Fungu** | **Wizara/Idara** | |
| **50** | Wizara ya Fedha na Mipango | 46,751,382,233 |
| **Na.** | **Taasisi Nyingine** | |
| **1** | Chuo cha Uhasibu Tanzania | 480,331,213 |
| **2** | Hospitali ya Rufaa Mkoa Amana | 69,367,554 |
| **3** | Hospitali ya Rufaa Mkoa Iringa | 491,747,100 |
| **4** | Hospitali ya Rufaa Mkoa Tumbi | 261,649,720 |
| **5** | Hospitali ya Rufaa Mkoa Morogoro | - |
| **6** | Hospitali ya Rufaa Mkoa Mbeya | 335,632,300 |
| **7** | Balaza la Madawa Tanganyika | 22,463,703 |
| **8** | Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) | - |
| **9** | Hospitali ya Rufaa Bukoba | - |
| **10** | Hospitali ya Rufaa Ligula | 481,171,725 |
| **11** | Hospitali ya Rufaa Maweni | 88,670,210 |
| **Na.** | **Sekretarieti za mkoa** | |

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi Sh |
|---|---|---|
| 1 | Sekretarieti ya Mkoa Kagera | 10,819,200 |
| 2 | Sekretarieti ya Mkoa Kigoma | 17,746,000 |
| 3 | Sekretarieti ya Mkoa Dar es Salaam | 17,252,640 |
| 4 | Sekretarieti ya Mkoa Morogoro | - |
| | **Jumla** | **49,028,233,598** |

*Chanzo: Taarifa za fedha zilizo kaguliwa mwaka wa fedha 2019/20*

Kitendo cha Taasisi husika za Serikali kushindwa kusajili au kuweka namba za utambulisho katika mali inazozimiliki kinaweza kusababisha upotevu au ubadhilifu wa mali husika.

**Ninapendekeza kuwa Taasisi husika; (a) kuchukuwa hatua na kuhakikisha kuwa mali zote zilizopo na zilizonunuliwa zinaandikwa namba ya utambulisho ili kuzuia wizi au matumizi yasiyokusudiwa ya mali husika, (b) Kukagua na kuandaa taarifa ya mara kwa mara juu ya mifumo iliyopo ya kulinda mali, usajili na uorodheshaji wa mali zinazomilikiwa na serikali kama ilivyoelekezwa kwanye Muongozo wa Mali za kudumu za Serikali.**

### 11.2.8 Kushindwa Kufanya Tathmini ya Thamani (Impairement Tests) na Muda Uliobaki wa Matumizi ya Mali za Kudumu

Kwa mujibu wa Aya ya 12.1 (ii) na (iii) ya Muongozo wa usimamizi wa Mali za umma wa mwaka 2019, unaelekeza kwamba mali inatakiwa kukaguliwa kila mwaka ili kuweza kubaini kipindi kilicho baki cha utumikaji. Kwa mali ambazo thamani yake imekwisha kabisa na bado inatumiwa na taasisi ya umma, Afisa Masuuli atamshauri Milipaji Mkuu wa serikali juu ya muda uliorekebishwa wa matumizi kwa mali husika.

Aidha, Aya ya 67 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS 17) inataka Taasisi kupitia angalau mara moja kila mwisho wa mwaka wa fedha makadirio ya muda wa matumizi ya mali za kudumu ili kuona kama makadirio yaliyofanywa awali yanatofautiana kwa kiasi kikubwa na hali halisi ya mali, na iwapo kuna tofauti kubwa ni vyema kufanya mabadiliko ya makadirio kulingana na matakwa ya IPSAS 3.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa taasisi saba hazikupitia makadirio ya muda wa matumizi wa mali za kudumu na thamani, kama inavoelekezwa na Aya ya 12.1(II) na (III) ya Muongozo wa usimamizi wa mali za Umma 2019 na para 67 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSA 17).Kushindwa kufanya hivyo kumesababisha idadi kubwa ya mali za kudumu kuoneshwa kwenye vitabu kuwa hazina thamani, ilhali

mali hizo zinaendelea kutumika. Idadi ya Taasisi zenye dosari hii zimepungua kutoka Taasisi 10 (2018/19) hadi Taasisi saba (2019/20).

Orodha ya Taasisi ambazo zimepatikana na mapungufu niliyoyaeleza hapo juu zimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 117** hapa chini:

**Jedwali Na. 117: Orodha ya Taasisi Zisizofanya Tathimi ya Mali na Muda wa Matumizi**

| Na. | Jina la Taasisi | Gharama Sh |
|---|---|---|
| **Fungu** | **Wizara/Idara** | |
| **28** | Jeshi la Polisi Tanzania | Hakuna thamani |
| **52** | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | 647,656,926 |
| **27** | Msajili wa Vyama vya Siasa | 61,775,800 |
| **34** | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | 8,655,674,601 |
| **61** | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 9,847,894,800 |
| **Na.** | **Taasisi Nyingine** | |
| **1** | Mamlaka wa Maabara za Serikali | 703,871,686 |
| **2** | Mfuko wa pembejeo za kilimo (AGITF) | Hakuna thamani |
| | **Jumla** | **19,916,873,813** |

*Chanzo: Taarifa za fedha zilizo kaguliwa mwaka wa fedha 2019/20*

Kushindwa kupitia makadirio ya muda wa matumizi ya Mali za Kudumu angalau mara moja kila mwisho wa mwaka ni ukiukwaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma.

**Kulingana na Mapungufu hayo hapo juu, ninapendekeza, Wizara / Idara, Sekretarieti za Mkoa na Wakala za Serikali, kuzingatia mahitaji ya aya ya 67 "IPSAS" 17 na aya ya 12.1 ya Muongozo wa Mali za Kudumu za Serikali wa Mwaka,2019**

### 11.2.9 Mali Zilizonunuliwa na Nyumba Zilizojengwa Lakini Zilikuwa Hazitumiki Sh. 1,080,654,947

Nilibaini kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songea zilifanya manunuzi ya mali za kudumu zenye thamani ya Sh. 31,676,700, lakini hadi wakati wa ukaguzi unakamilika zilikuwa bado hazijaanza kutumika. Pia nilibaini kuwa Sekretarieti za Mikoa ya Iringa, Singida na Mwanza zimekamilisha ujenzi wa majengo ya wakuu wa Wilaya kwa jumla ya Sh. 1,048,978,247 lakini nyumba hizo zilikuwa hazijaanza kutumika kutokana na sababu tofauti, ikiwamo kusubiri mchakato wa makabidhiano.

Ni maoni yangu kuwa ucheleweshaji wa kutumia mali hizo unazuia jamii kunufaika na huduma hiyo. Angalia **Jedwali Na. 118** hapa chini kwa maelezo ya mali zilizonunuliwa lakini hazitumiki.

**Jedwali Na. 118: Orodha ya Taasisi Zilizonunua Mali na Kujenga Majengo Bila Kutumika.**

| Na. | Jina la Taasisi | Gharama Sh. | Maelezo |
|---|---|---|---|
| **Na.** | Sekretarieti za Mkoa /Hospitali za Rufaa | | |
| **1** | Sekretarieti ya Mkoa Kagera | 10,819,200 | Manunuzi ya pikipiki nne |
| **2** | Sekretarieti ya Mkoa Iringa | 384,994,900 | Jengo la Makazi ya Mkuu wa Wilaya Kilolo likusubiri makabidhiano |
| **3** | Sekretarieti ya Mkoa Singida | 533,983,347 | Jengo la makazi ya Mkuu wa Wilaya |
| **4** | Sekretarieti ya Mkoa Mwanza | 130,000,000 | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na jengo la Makazi |
| **5** | Hospitali ya Rufaa Songea | - | Mashine ya kitengo cha Infusion kutoka kwa wafadhili ikingojea kujengwa chumba maalumu |
| **6** | Hospitali ya Rufaa Iringa | 20,857,500 | Kununuliwa kwa mashine ya kusafishia damu (Dialysis Machine) inayosubiri wataalam |
| | **Jumla** | **1,080,654,947** | |

*Chanzo: Taarifa za fedha za mwaka 2019/20*

**Ninapendekeza kwa Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa mali zilizonunuliwa au nyumba zilizojengwa ambazo hazitumiki zinatumika mapema iwezekanavyo.**

### 11.2.10 Mapato Ambayo Yayajapokelewa Sh. 1,032,851,584,396

Hadi tarehe 30 Juni 2020, Taasisi 78 ikiwa ni pamoja na Wizara, Wakala, Idara, Sekretarieti za Mikoa, Bodi za mabonde ya maji na taasisi zingine ziliripoti mapato yasiyopokelewa ya jumla ya Sh. 1,032,851,584,396 ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 41,497,847,243 kilichoripotiwa mwaka wa fedha 2018/19 kwa taasisi 24 zilizokuwa zimekaguliwa, ikiwa ni ongezeko

la Sh. 991,353,737153 . Hii inatokana na baadhi ya taasisi kutokuwa na mpango mkakati wa ukusanyaji wa madeni na ukosefu wa sera ya mkopo madhubuti katika usimamizi wa mapato. Taasisi ambazo zilibainika kuwa na mapato ambayo hayajapokelewa zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. XXIV**

Pia, nilibaini kuwa asilimia 32% ya mapato yasiyokusanywa ni kutoka kwa Wakala wa barabara Tanzania yenye jumla ya Sh. 326,494,427,000, ikifuatiwa na Wakala wa hifadhi ya chakula ya Taifa (NFRA) Sh. 168,735,362,231 sawa na 16%, Wakala wa ndege za Serikali (TGFA) Sh. 96,254,812,943 sawa na asilimia 9, Wizara ya Ardhi, Nyumba na makazi Sh. 62,694,370,208 sawa na asilimia 6, wakati Taasisi nyingine zina jumla ya Sh 378,672,612,014 sawa na 37% ya mapato yote yasiyokusanywa. Taarifa hizi zinaonekana katika **Kielelezo Na. 19** hapa chini.

**Kielelezo Na. 19: Uwiano wa Mapato Yasiyolipwa**




*Chanzo: Taarifa za fedha za mwaka 2019/20*

Kushindwa au kuchelewa kukusanya madeni huathiri uendeshaji na ukuaji wa Taasisi za Serikali kwa sababu ya kukosa mtaji wa kutosha.

**Katika suala hili, napendekeza Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti ya Mkoa na taasisi nyingine za kiserikali kuandaa mikakati ya kuhakikisha kuwa mapato yasiyopokelewa yanakusanywa kwa wakati.**

**Pia, ninaendelea kusisitiza kuwa, Maafisa Masuuli wenye mapato ambayo hayajakusanywa kwa muda mrefu kuweka bidii zaidi katika kukusanya Mapato yasiyopokelewa kabla hayajafika hatua ya kutokusanyika na kusababisha hasara ya mapato ya Serikali.**

### 11.3 Usimamizi wa Madeni

Katika ukaguzi huu nilibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi wa madeni ya taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

#### 11.3.1 Madeni Tarajiwa (Kesi ambazo Hazijafanyiwa Maamuzi) Sh. 314,321,747,130

Madeni tarajiwa ni madeni ya msingi yanayoweza kutokea katika siku zijazo, baada ya maamuzi ya Mahakama kutokana na madai yaliyowasilishwa mahakamani, kama vile kesi ya mashtaka na ya kisheria.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwapo kwa taasisi 23 za Serikali zilikuwa na kesi katika mahakama mbalimbali dhidi ya Makampuni na watu binafsi ambazo zinasubiri maamuzi ya mahakama zenye madai ya jumla ya Sh 314,321,747,130. katika mwaka wa fedha 2018/19 madeni tarajiwa yalikuwa Sh 639,940,032,405 hivyo kuna punguzo la Sh. 321,983,095,275 (sawa na asilimia 50). Mwenendo unaonyesha kuwa kuna maboresho katika usimamizi wa madeni tarajiwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 20** na **Jedwali Na. 119.**

**Kielelezo Na. 20: Mwenendo wa Madeni Tarajiwa**




*Chanzo: Taarifa za fedha zilizo kaguliwa za mwaka 2019/20*

**Jedwali Na. 119: Orodha ya Taasisi zenye Kesi Mahakamani**

| | Jina la Taasisi | Kiasi Sh |
|---|---|---|
| **Fungu** | **Wizara/Idara** | |
| **28** | Jeshi la Polisi Tanzania | 20,107,961,728 |
| **37** | Ofisi ya Waziri Mkuu | 6,546,922,629 |
| **48** | Wazira ya Ardhi, Nyumba na Makazi | 17,464,810,000 |
| **49** | Wizara ya Maji | 8,796,619,937 |

| | Jina la Taasisi | Kiasi Sh |
|---|---|---|
| **52** | Wizara Ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | 226,066,533,554 |
| **57** | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa | 6,161,842,578 |
| **68** | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 68) | 1,388,553,088 |
| **69** | Wizara ya Maliasili na Utalii | 15,858,176,993 |
| **96** | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo | 525,351,200 |
| **99** | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 1,781,272,732 |
| **98** | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 98) | 5,026,857,181 |
| **Na.** | **Sekretarieti ya Mkoa** | |
| **1** | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | 385,770,495 |
| **2** | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | **366,710,083** |
| **3** | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | **255,093,735** |
| **4** | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | 186,738,360 |
| **Na** | **Taasisi nyingine za Serikali** | - |
| **1** | Shirika la Mzinga | 1,949,533,504 |
| **2** | Kampuni Hodhi ya Mzinga | - |
| **Na.** | **Wakala** | |
| **1** | Wakala wa Majengo Tanzania | 79,293,760 |
| **2** | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania | 1,334,705,573 |
| **3** | Kituo Cha Mafunzo ya Utafiti Afrika Mashariki | - |
| **4** | Baraza la Famasia | - |
| **5** | Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es salaam | 39,000,000 |
| **6** | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini Tanzania | - |
| | **Jumla** | **314,321,747,130** |

*Chanzo: Taarifa za fedha za mwaka 2019/20*

Kuna hatari ya kuingia katika matumizi yasiyo na faida kwa Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na taasisis zingine za Serikali yatokanayo na faini

ambayo itatakiwa kulipwa mahakamani iwapo Wizara, wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa zitashindwa kesi, pia kuna gharama kubwa ambazo zinaingiwa katika kufuatilia hizi kesi.

**Ninapendekeza Serikali isisitize kila Taasisi kuwa na mikakati inayofaa juu ya kudhibiti madeni tarajiwa kwa kuzingatia mazingira yao ili kuhakikisha kuwa hatari zinaweza kudhibitiwa na kupunguzwa kwa kadri inavyowezekana.**

### 11.3.2 Matumizi Ambayo Hayajalipwa Sh. 3,126,442,872,063

Katika mapitio ya taarifa za fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020, nilibaini kuwa taasisi 122 zikiwemo Wizara, Idara, Wakala, Sekretariet za mikoa, Bodi za mabonde ya maji, na taasisi zingine za Serikali ziliripoti matumizi yasiyolipwa jumla ya Sh 3,126,442,872,063. Katika mwaka uliopita matumizi yasiyolipwa yalikuwa Sh. 2,687,140,232,434 kwa taasisi 82 zilizokuwa zimekaguliwa, ikiwa ni ongezeko la Sh. 439,302,639,629. Orodha ya Taasisi zenye matumizi yasiyolipwa zinapatikana katika **Kiambatisho Na. XXV.**

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa ilikuwa na matumizi yasiyolipwa ya jumla ya Sh. 1,048,126,088,747 sawa na asilimia 34 ya madeni yote, ikifuatiwa na Jeshi la Polisi Sh. 631,402,753,421 sawa na asilimia 20, Wakala wa barabara Tanzania Sh 624,677,604,000 (20%), Wizara ya Afya (fungu 52) Sh. 261,935,267,270 (8%) na Taasisi nyingine zilikuwa na Sh 564,959,247,041 sawa na asilimia 18 ya jumla ya matumizi yasiyolipwa kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 21** hapa chini.

**Kielelezo Na. 21: Uwiano wa Matumizi Yasiyolipwa**




*Chanzo: Taarifa za fedha za mwaka 2019/2020*

Kuwapo kwa matumizi mengi yasiyolipwa kunatokana na bajeti iliyotengwa kwa taasisi kuwa ndogo kulingana na matumizi halisi pamoja na ucheleweshwaji wa kutoa fedha kutoka Hazina. Kushindwa kulipa madeni kwa wakati kuna athari kwa taasisi za Serikali, ikiwa ni pamoja na Serikali kupata sifa mbaya kwa wazabuni, wakandarasi na watoa huduma zingine.

**Ninapendekeza kuwa Serikali itoe fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa ili kupunguza mkusanyiko wa matumizi yasiyolipwa ambayo yanaweza kuchafua taaswira ya taasisi na kupunguza uaminifu wake kwa watoa huduma.**
**Pia, Afisa Masuuli wanashauriwa kuweka msisitizo katika kupunguza/kulipa madeni yaliyopo kabla ya kuingia katika madeni mapya.**

### 11.3.3 Madai ya Matibabu ya Hospitali za India

Katika ukaguzi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (fungu Na. 52) nilibaini kuwapo kwa madai ya jumla ya Sh. 16,863,835,368 yaliyotokana na matibabu katika hospitali za rufaa nchini India kwa mwaka wa fedha 2019/20. Deni hilo limepungua kwa Sh. 2,310,982,225 ikilinganishwa na mwaka 2018/19, ambapo deni lilikuwa Sh. 19,174,817,593 kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 120** hapa chini:

**Jedwali Na. 120: Muelekeo wa madeni ya Hospitali za India**

| Maelezo | Kiasi cha fedha Sh |
|---|---|
| Bakaa 01/07/2019 | 19,174,817,593 |
| Madai yaliyo pokelewa kwa mwaka 2019/20 | 0 |
| **Juma ya Madai** | **19,174,817,593** |
| Toa madai yaliyo lipwa 2019/20 | 2,310,982,225 |
| Bakaa 30/06/2020 | **16,863,835,368** |

*Chanzo: uthibitisho wa barua toka Wizara ya Afya yenye kumbukumbu Na. CHA.226/44604/11 ya tarehe 1/12/ 2020*

Katika mwaka wa fedha 2019/20 hapakuwa na madai mapya ya matibabu katika hospitali za rufaa za India kwa sababu Serikali imesitisha utaratibu wa kupeleka wagonjwa nchini India kupata matibabu kwa mkopo. Pia niligundua kuwa idadi ya wagonjwa wanaokwenda nchini India kwa matibabu imepungua kutoka wagonjwa 82 mwaka 2018/19 hadi wagonjwa 45 mwaka 2019/20 kwa gharama ya Sh. 2,942,164,702, Upungufu huu

umetoka na matokeo chanya ya maboresho huduma za matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Benjamini Mkapa, na Hospitali zingine za Kanda.

**Napendekeza kuwa, Wizara ya Fedha na Mipango itoe fedha za kutosha ili kulipa deni lililobaki la matibabu katika hospitali za rufaa za India ili kuepuka hatari ya kuongezeka kwa deni kwa sababu ya kubadilika kwa viwango vya ubadilishaji wa fedha.**

## SURA YA KUMI NA MBILI

## UKAGUZI WA VYAMA VYA SIASA

### 12.1 Utangulizi

Sehemu hii ya ripoti inaeleza mambo ya msingi yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa vyama vya siasa kwa mwaka wa fedha 2019/20. Nimetoa mapendekezo kwenye kila hoja ya ukaguzi iliyotolewa. Ni imani yangu kuwa Makatibu Wakuu wa vyama vya siasa watatekeleza mapendekezo yangu kwa namna ambayo itaboresha usimamizi wa rasilimali za chama kwa masilahi ya umma.

### 12.2 Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (a) (2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorejewa mwaka 2019), kila chama cha siasa kinatakiwa kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa za fedha kila mwaka kabla au tarehe 30 Septemba kwa ajili ya ukaguzi. Ukaguzi wa vyama vya Siasa ulilenga kupitia mifumo ya fedha na mifumo ya udhibiti wa ndani mahususi kwenye usimamizi na uhifadhi wa rasimali za chama.

Ofisi yangu ilipokea na kukagua Taarifa za fedha za mwaka 2019/20 za vyama 17 kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu, vyama viwili[9] havikuwasilisha taarifa zao za fedha. Hata hivyo, nilitathmini mifumo yao ya udhibiti wa ndani ili kuthibitisha iwapo inajitosheleza katika kulinda rasilimali za chama. Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi yanayohitaji menejiment za vyama vya siasa kuyafanyia kazi:

#### 12.2.1 Mapungufu Yanayohusu Usimamizi wa Fedha Sh. 593,180,714

Katika mapitio ya Kanuni za Fedha za Chama cha Mapinduzi pamoja na Taarifa za fedha nilibaini kuwa, wafanyakazi saba wa Ofisi ya CCM Lumumba, Dar es Salaam walipewa masurufu ya jumla ya Sh.30,364,440 kabla hawajarejesha masufuru waliopewa awali, kinyume na matakwa ya Kanuni za Fedha za CCM za mwaka 2018. Pia, nilibaini kuwa wafanyakazi sita wa ofisi hiyo walichelewa kurejesha masufuru waliyochukuwa ya jumla ya Sh. 41,101,150 kwa kipindi cha kuanzia siku 80 hadi 475. Kadhalika, nilibaini masufuru ya jumla ya Sh. 173,249,334 yalitolewa kwa

[9] Democratic Party na Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)

wafanyakazi 55 ambayo yalikuwa hayajarejeshwa hadi Februari 2021 wakati wa kipindi cha ukaguzi. Pia, nilibaini kuwa Ofisi ya CCM ya Mkoa wa Mwanza haikukusanya kodi za pango za jumla ya Sh. 348,465,790 kutoka kwa wapangaji 149 wa uwanja wa mpira wa CCM Kirumba na Ofisi ya CCM ya Mkoa wa Mwanza. Mapungufu haya yamesababishwa na udhaifu wa mifumo ya fedha ya ndani ya Chama cha Mapinduzi.

**Ninapendekeza uongozi wa CCM kuongeza udhibiti ambao utahakikisha kuwa rasilimali za chama zinatunzwa na kulindwa ipasavyo.**

### 12.2.2 Mapungufu Yanayohusu Usimamizi wa Ununuzi Sh. 349,869,400

Ofisi ya CCM Lumumba, Dar es Salaam, ilitumia jumla ya Sh. 27,095,000 kwa ajili ya kununua bidhaa na huduma. Hata hivyo, CCM haikuomba nukuu za bei kutoka wa wazabuni watatu. Pia, hakukuwa na ushahidi unaoonesha kuwa Chama cha Mapinduzi kilitumia taratibu za ununuzi zenye uwazi na ushindani kama ilivyoelekezwa na kanuni za Fedha za CCM, matokeo yake bidhaa na huduma zilizonunuliwa zinaweza kuwa za bei za juu.

Kanuni Na. 6.1 (m) ya Kanuni za Fedha za CCM za mwaka 2018 imeelekeza kuwa manunuzi yote ya bidhaa na huduma yalipwe kwa kutumia hundi au kulipa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki ya mhusika. Hata hivyo, nilibaini kuwa Afisi Kuu ya CCM Zanzibar ilinunua na kulipa fedha taslimu Sh. 75,056,000 kwa wazabuni, kinyume na matakwa ya Kanuni za Fedha za CCM za mwaka 2018. Pia, nilibaini kuwa CCM ilinunua bidhaa za jumla ya Sh. 247,718,400 bila ya kuziandikisha kwenye Daftari la mali za kuhifadhia mali. Kutokuandikwa kwa bidhaa hizo ndani ya rejista kulisababisha nishindwe kuthibitisha iwapo bidhaa zilizonunuliwa, zilipokelewa na kutumiwa na chama.

Maelezo yaliyotolewa hapo juu ni ushahidi kuwa kuna udhaifu ndani ya Chama cha Mapinduzi katika kusimamia rasilimali za chama; na mapungufu hayo yana hasara kwa Chama cha Mapinduzi.

**Ninapendekeza uongozi wa CCM kuhakikisha kuwa manunuzi yote yanafanyika kwa usawa na ushindani ili kupata thamani halisi ya fedha na kulinda rasilimali za chama.**

### 12.2.3 Magari Mawili Yaliyonunuliwa na Chama cha Wananchi (CUF) Yalisajiliwa kwa Majina Binafsi

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa Chama Cha wananchi (CUF) kilihamisha jumla ya Sh. 72,981,268 kwenda kwenye akaunti ya mmojawapo wa wanachama ili kununua magari mawili kutoka Japan. Nilibaini kuwa manunuzi hayo yalifanywa na mwanachama huyo, ambapo fedha zilihamishwa kutoka akaunti ya mwanachama huyo kwenda akaunti ya muuzaji wa magari iliyopo Japan. Pia, nilibaini kuwa menejimenti ya chama ilifanya manunuzi ya gari bila ya kupata idhini ya Kamati Kuu ya chama, kinyume na matakwa ya Kanuni za Fedha za CUF.

Pia, nilibaini kuwa magari yaliyonunuliwa yalisajiliwa kwa kutumia majina ya mwanachama huyo badala ya jina la Baraza la Wadhamini la CUF. Uandikishwaji wa mali za chama kwa kutumia jina la mwanachama badala ya jina la Baraza la Wadhamini unatia shaka kuhusu umiliki wa mali hizo. Maelezo yaliyotolewa na menejimenti ya chama ni kuwa, usajili wa magari ya chama kwa kutumia majina binafsi badala ya jina la Baraza la Wadhamini la CUF ulifanywa ili kuepuka urasimu wa taratibu za forodha ambazo zingechelewesha ulipaji na utoaji wa magari tajwa.

**Katika suala hili, ninapendekeza uongozi wa CUF kuhakikisha kuwa magari tajwa yanasajiliwa kwa kutumia jina la Baraza la Wadhamini la CUF.**

### 12.2.4 Mapungufu katika Usimamizi wa Bajeti ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Sh. 377,430,000

Kanuni Na. 2.9.4 ya Kanuni za Fedha za CHADEMA za mwaka 2019, inaeleza kuwa baada ya Kamati kuu ya chama kupokea makadirio ya bajeti yaliyoandaliwa na Katibu Mkuu wa chama na wajumbe wa Sekretarieti kwa mapitio, itaiwasilisha Baraza Kuu kwa ajili ya kuidhinishwa. Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini kuwa CHADEMA ilitumia jumla ya Sh. 100,000,000 kwa shughuli mbalimbali za chama ambazo hazikuwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa na Baraza Kuu la Chama. Pia, chama kilinunua magari matano yenye jumla ya thamani ya Sh. 227,430,000 na kutumia Sh. 50,000,000 kununua nyumba kwa ajili ya Ofisi ya Kanda ya Serengeti. Hata hivyo, matumizi hayo hayakuwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa na Baraza Kuu la Chama. Maelezo yaliyotolewa na menejimenti ya CHADEMA ni kuwa, matumizi yasiyokuwa kwenye bajeti hutokea kulingana na mazingira

ya kisiasa yaliyopo, ambapo sio rahisi kutenga bajeti kwa kuzingatia uhalisi. Kutumia fedha jumla ya Sh. 377,430,000 kwa ajili ya shughuli zilizo nje ya bajeti kulikwamisha utekelezaji wa shughuli za chama zilizoidhinishwa. Hivyo, kusababisha CHADEMA kutofikia malengo yake ya kisiasa katika mwaka huu wa fedha.

**Kuhusiana na hili, ninapendekeza kwa uongozi wa CHADEMA kuhakikisha kuwa matumizi yote yanayofanyika kuendana na bajeti ili kutoa uwajibikaji wa rasilimali za chama kwa uwazi.**

### 12.2.5 Matumizi Yasiyokuwa na Tija Yaliyofanywa na CHADEMA kwenye Urejeshaji wa Mkopo Sh. 19,800,000

Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa mkataba wa mkopo kati ya mmojawapo wa viongozi wa chama na Taasisi moja ya mikopo nchini. CHADEMA ilimdhamini kiongozi huyo mkopo wa jumla wa Sh.33,000,000. Kiongozi huyo alitakiwa kufanya marejesho ya Sh. 3,300,000 kila mwezi kwa kipindi cha miezi 10 kuanzia mwezi Septemba 2019 hadi Juni 2020. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2019, kiongozi huyo alikuwa amerejesha jumla ya Sh. 13,200,000 tu kati ya Sh. 33,000,000 anazodaiwa kabla ya kukihama chama hicho. Kutokana na kutolipwa kwa deni hilo, CHADEMA ililipa deni lililobaki hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 la jumla ya Sh. 19,800,000. Ni maoni yangu kuwa, malipo ya Sh. 19,800,000 yaliyofanywa na CHADEMA ni matumizi mabaya ya rasilimali za chama. Hii ni kwa sababu hakukuwa na ushahidi kutoka taasisi hiyo ya fedha unaoonesha ugumu wa kumpata mkopaji huyu; ambapo CHADEMA ingechukuwa hatua ya kurejesha mkopo kulingana na makubaliano ya mkataba wa mkopo.

**Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza kuwa CHADEMA kumfuatilia kiongozi huyo ili arejeshe kiasi hicho cha fedha ili kujenga imani kwa wanachama juu ya usimamizi wa rasilimali za chama.**

### 12.2.6 Matumizi Yaliyofanyika Bila ya Kuwapo kwa Yyaraka Toshelezi Sh. 347,521,794

Nilipitia taarifa za matumizi na nyaraka za malipo za vyama vya siasa na kubaini kuwa vyama vya siasa 11 vilifanya malipo yenye jumla ya Sh. 347,521,794 bila ya kuambatisha nyaraka toshelezi. Katika mahojiano yangu na uongozi wa vyama husika, nilielezwa kuwa baadhi ya nyaraka hazijulikani zilipo. Hata hivyo, hadi muda wa taarifa hii, vyama hivyo vya

siasa vilivyotajwa havikuwasilisha nyaraka zilizokosekana; hivyo, sikuweza, kuhakiki uhalali na uhalisia wa malipo yaliyofanyika.

**Jedwali Na. 121: Matumizi ya Vyama vya Siasa**

| Na. | Jina la Chama | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Alliance for Democratic Change (ADC) | 6,340,000 |
| 2 | Democratic Party ( DP) | 17,163,000 |
| 3 | Union for Multi-Party Democracy (UMD) | 4,086,000 |
| 4 | African Democratic Alliance (ADA-TADEA) | 3,114,800 |
| 5 | Alliance for African Farmer's Party (AAFP) | 929,200 |
| 6 | Sauti ya Umma (SAU) | 3,035,000 |
| 7 | Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) | 14,785,000 |
| 8 | Civic United Font (CUF) | 287,193,000 |
| 9 | National Reconstruction Alliance (NRA) | 7,950,000 |
| 10 | National League for Democracy | 750,794 |
| 11 | Alliance for Change and Transparency (ACT -WAZALENDO) | 2,175,000 |
| | **Jumla** | **347,521,794** |

*Chanzo: Ripoti za vyama*

Hata hivyo, kuna upungufu wa malipo yasiyoambatishwa na nyaraka toshelezi ikilinganishwa na mwaka jana (2018/19), kutoka Sh. 2,132,906,798 hadi Sh. 347,521,794 kwa idadi ile ile ya vyama vya siasa. Huu ni ushahidi tosha kuwa uongozi wa vyama vya siasa umetekeleza mapendekezo yangu.

**Ninapendekeza kuwa mifumo ya udhibiti wa ndani wa vyama vya siasa iboreshwe ili malipo yote yanayofanyika yawe na nyaraka toshelezi kabla ya idhini ya malipo kutolewa.**

### 12.2.7 Mapungufu Yanayohusiana na Kutokuzingatiwa kwa Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (kama ilivyorejewa mwaka 2019) na Sheria ya Usajili wa Bodi za Udhamini Sura ya 318

Nilipitia Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019 na Sheria ya Usajili wa Bodi za Udhamini Sura ya 318 ili kubaini yafuatayo: iwapo vyama vya siasa vinafuata Sheria zilizotajwa hapo juu, kuthibitisha iwapo rasilimali fedha zinazopokelewa na vyama vya siasa zinatumika kama ilivyotarajiwa, taarifa za mali zinazomilikiwa na vyama vya siasa zinawasilishwa kwa Msajili wa vyama, rejista za uanachama zimehuishwa na kuwasilishwa kwa Msajili wa vyama vya Siasa, kuthibitisha iwapo vyama vya siasa vinaandaa taarifa zake za fedha kwa kuzingatia mwongozo wa uandaaji wa taarifa za fedha na kwa kutumia mfumo wa kimataifa wa

uaandaji hesabu za Umma (IPSAS) na kuwasilishwa ofisini kwangu kabla au mnamo tarehe 30 Septemba 2020 kwa ajili ya ukaguzi, pamoja na kuthibitisha iwapo vyama vya siasa vinawasilisha ritani ya kila mwaka ya wajumbe wote wa Baraza la Wadhamini kwa Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali (RITA) ndani ya kipindi cha mwezi mmoja kutoka tarehe ya kutolewa kwa cheti cha usajili. Katika ukaguzi wangu nilibaini mambo yafuatayo:

**a) Kuchelewa kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya Ukaguzi**

Kifungu Na. 18A (2) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 kinaelekeza vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu kuandaa taarifa zao za fedha za mwaka na kuwasilisha Ofisini kwangu si zaidi ya tarehe 30 Septemba ya kila mwaka kwa ajili ya ukaguzi. Chama cha DP na Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) havikuwasilisha Ofisini kwangu taarifa za fedha za mwaka 2019/20 kama inavyoelekezwa na Kifungu Na. 18A (2) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258. Zaidi, nilibaini kuwa vyama vitano vilichelewa kuwasilisha taarifa zao za fedha kwa kipindi kati ya siku 42 hadi 126 baada ya tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa taarifa za fedha za mwaka 2019/20. Hii ni kinyume na matakwa ya kifungu Na. 18A (2)(a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 kama ilivyooneshwa hapo chini.

**Jedwali Na. 122: Orodha ya Vyama vya Siasa Vilivyochelewa Kuwasilisha Taarifa za Fedha**

| Na. | Jina la Chama | Tarehe ya uwasilishaji | Ucheleweshaji (Siku) |
|---|---|---|---|
| 1 | Chama cha Kijamii (CCK) | 11-Jan-21 | 103 |
| 2 | Sauti ya Umma (SAU) | 18-Jan-21 | 110 |
| 3 | National Reconstruction Alliance (NRA) | 3-Feb-21 | 126 |
| 4 | National League for Democracy | 27-Jan-21 | 119 |
| 5 | Union for Multi-Party Democracy (UMD) | 11-Nov-20 | 42 |

*Chanzo: Ripoti za vyama*

**Ili kufanikisha zoezi la ukaguzi wa vyama vya siasa kwa wakati, ninapendekeza viongozi wa vyama vya siasa kuajiri wahasibu wenye sifa ili kuandaa taarifa za fedha kitaalamu na kuwasilishwa Ofisini kwangu kwa wakati. Pia, namshauri Msajili wa Vyama vya Siasa kusimamia na kuhakikisha taarifa za fedha za vyama vya siasa zinawasilishwa kwa wakati.**

### b) Ukiukwaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Taasisi za Umma Katika Uandaaji wa Taarifa za Fedha

Kulingana na kanuni za vyama vya siasa (Uhasibu wa fedha) za mwaka 2019, vyama vyote vilivyosajiliwa vimeelekezwa kuandaa taarifa zao za fedha za mwaka kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma (IPSAS). Viwango hivyo vinataka taasisi zinazoandaa taarifa za fedha kuandaa Taarifa ya Mizania, Taarifa ya Utendaji ya Fedha, Taarifa ya Mtiririko wa Fedha, Taarifa ya Mabadiliko ya mtaji na maelezo ya ziada yanayojumuishwa kwenye Taarifa za fedha.

Hata hivyo, nilibaini kuwa vyama 10 vya siasa havikuandaa taarifa zao za fedha kama inavyoelekezwa na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma (IPSAS); badala yake, viliandaa taarifa za mapato na matumizi tu bila ya kuandaa taarifa zingine. Hii ni kinyume na matakwa ya Kifungu Na. 3(1) cha kanuni za vyama vya siasa (uhasibu wa fedha) za mwaka 2019. Hivyo, nilishindwa kuthibitisha mali, madeni na mitaji iliyotolewa na vyama vya siasa ambavyo havikuandaa taarifa za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma (IPSAS).

Pia, nilibaini kuwa taarifa za fedha zilizoandaliwa hazikuwa na saini ya Mkuu wa Idara ya Fedha au Mhasibu Mkuu, kinyume na Sheria ya Wakaguzi na Wahasibu (usajili) Na.2 ya mwaka 1995. **Jedwali Na.123** hapo chini linaonesha orodha ya vyama vyama vya siasa vilivyoandaa taarifa za fedha bila ya kufuata mfumo wa IPSAS.

**Jedwali Na. 123: Orodha ya vyama vya siasa vilivyoandaa taarifa za fedha bila ya kufuata mfumo wa IPSAS**

| Na. | Jina la Chama |
|---|---|
| 1 | Alliance for Democratic Change (ADC) |
| 2 | Union for Multi-Party Democracy (UMD) |
| 3 | United People's Democratic Party (UPDP) |
| 4 | Alliance for African Farmer's Party (AAFP) |
| 5 | Demokrasia Makini |
| 6 | Tanzania Labour Party (TLP) |
| 7 | Chama cha Kijamii (CCK) |
| 8 | Sauti ya Umma (SAU) |
| 9 | National Reconstruction Alliance (NRA) |
| 10 | National League for Democracy (NLD) |

*Chanzo: Ripoti za vyama*

Orodha ya vyama vya siasa vilivyoandaa taarifa za fedha bila ya kufuata mfumo wa IPSAS imeongezeka kutoka vyama tisa kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2018/19 hadi vyama 10. Hali hii inaonesha kuwa menejimenti za vyama vya siasa havikufanyia kazi mapendekezo yangu.

**Ninapendekeza kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhakikiksha kuwa vyama vya siasa vinafuata Kanuni za Vyama vya Siasa (fedha) za mwaka 2019 pamoja na kuandaa taarifa za fedha kwa kufuata Viwango vya Kimataifa wa Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Taasisi za umma (IPSAS).**

#### 12.2.8 Mapungufu Kuhusiana na Usimamizi wa Mapato ya Vyama yaliyokusanywa na Vyama vya Siasa Vinane Sh.244,583,800

Baada ya kupitia utaratibu wa kukusanya mapato ndani ya vyama vya siasa nilibaini kuwa, vyama vya siasa vinane vilikusanya jumla ya Sh. 244,583,800 kutoka vyanzo mbalimbali kama vile mikopo, misaada, michango kutoka kwa wanachama na kuzitumia fedha hizo kabla ya kuzipeleka benki. Hii ni kinyume na matakwa ya Kifungu Na. 15(1) cha Sheria ya vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019. Kwa mujibu wa kifungu hicho, vyama vyote vya siasa vyenye usajili vinatakiwa kuwa na akaunti za benki za chama ambazo zitapokea mapato yote kabla ya kuyatumia.

Pia, wakati wa ukaguzi nilishindwa kuthibitisha iwapo fedha zilizokusanywa ziliripotiwa kwa usahihi na zimetumika kama ilivyoripotiwa kwenye taarifa za matumizi. Orodha ya vyama vya siasa vilivyohusika na hoja hii imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 124** hapa chini.

**Jedwali Na. 124: Kiasi cha fedha ambacho hakijawekwa benki na vyama vinane vya Siasa**

| Na. | Jina la Chama | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Democratic Party (DP) | 27,400,000 |
| 2 | African Democratic Alliance (ADA-TADEA) | 4,894,800 |
| 3 | Chama cha Ukombozi wa Umma ( CHAUMMA) | 10,500,000 |
| 4 | Alliance for African Farmer's Party (AAFP) | 1,209,000 |
| 5 | United Democratic Party (UDP) | 15,580,000 |
| 6 | Tanzania Labour Party (TLP) | 10,000,000 |
| 7 | Alliance for Change and Transparency (ACT - WAZALENDO) | 120,000,000 |
| 8 | NCCR-Mageuzi | 55,000,000 |
| | **Jumla** | **244,583,800** |

*Chanzo: Ripoti ya vyama*

Idadi ya vyama vya siasa vilivyotumia fedha za mapato kabla ya kupelekwa benki imepungua kutoka vyama tisa kwa mwaka wa fedha 2018/19 hadi vyama vinane; ambapo kiasi kilichoripotiwa kimepungua kutoka Sh. 543,844,248 hadi Sh. 244,583,800. Hii inaonesha maboresho yaliyofanywa na menejimenti za vyama vya siasa katika eneo hili.

**Ninapendekeza kuendelea kufanyia kazi mapendekezo yangu ili kuongeza udhibiti wa fedha za Vyama kama inavyoelekezwa na Sheria ya vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa 2019.**

### 12.2.9 Matamko ya Mali za Vyama vya Siasa Kutopelekwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa

Kifungu Na. 14(1) (ii) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019, kimeelekeza kuwa kila chama cha siasa chenye usajili wa kudumu kuandaa tamko la mali na kuliwasilisha kwa Msajili wa vyama vya Siasa. Hata hivyo, nilibaini kuwa Chama cha ADC, Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) na TLP havikuandaa na kuwasilisha matamko ya mali za chama kwa Msajili wa vyama vya Siasa. Hii ni kinyume na matakwa ya Kifungu Na. 14 (1)(ii) cha Sheria ya vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019.

Kwa uongozi wa vyama vya Siasa kushindwa kuwasilisha matamko yao ya mali kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, Msajili wa Vyama vya Siasa hatakuwa na uhalisi wa taarifa za mali za vyama; na endapo vitaingia kwenye migogoro ya mali, Msajili wa Vyama vya Siasa atashindwa kufanya usuluhishi.

Idadi ya Vyama vya Siasa ambavyo havikupeleka matamko ya mali za vyama kwa Msajili wa Vyama vya Siasa haijabadilika ukilinganisha na ripoti yangu ya mwaka jana na hivyo kuonesha kuwa ushauri wangu haukufanyiwa kazi.

**Ninashauri kuwa viongozi wa Vyama vya Siasa waandae tamko la mali na kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kwa wakati. Pia, ninasisitza kuwa, Msajili wa Vyama vya Siasa aendelee kuvifuatilia Vyama vya Siasa vilivyotajwa ili matamko ya mali zao yawasilishwe.**

#### 12.2.10 Rejista za Wanachama Hazikuhuishwa

Kulingana na Kifungu Na. 8C cha Sheria ya vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019, kila chama cha siasa kinatakiwa kuhuisha rejista za wanachama na viongozi katika kila ngazi ya Utawala.

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kuwa chama cha UMD, UDP, NCCR-Mageuzi, na Demokrasia Makini havikuhuisha rejista za wanachama na viongozi wake, kinyume na matakwa ya kifungu Na. 8C cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorekebishwa mwaka 2019. Hivyo, ukaguzi wangu ulishindwa kuthibitisha idadi halisi ya wanachama ili kukadiria kwa usahihi kiwango cha michango ambacho hakikupokelewa katika kipindi hicho.

Ikilinganishwa na ripoti yangu ya mwaka jana (2018/19), kumekuwa na maboresho madogo yaliyofanywa na viongozi wa vyama vya Siasa katika kutekeleza mapendekezo yangu, kwani idadi ya vyama vya siasa ambavyo havikuhuisha rejista zao za wanachama na viongozi imebaki sawa na mwaka jana.

**Kuhusiana na suala hili, bado ninasisitiza uongozi wa vyama vya siasa vilivyotajwa kuhuisha rejista zao za wanachama na viongozi na kuzipeleka rejista hizo kwa Msajili wa Vyama vya Siasa.**

#### 12.2.11 Ritani ya Mwaka ya Wajumbe wa Baraza la Wadhamini Haikuwasilishwa kwa Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali

Kifungu Na. 16 (3) cha Sheria ya Usajili Wadhamini Sura ya 318 kinaagiza kuwa, kila Bodi ya Wadhamini iliyosajiliwa inatakiwa kupeleka ritani ya wajumbe wa Baraza la Wadhamini kwa Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali (RITA) kila mwaka ndani ya kipindi cha mwezi mmoja baada ya tarehe ilipoundwa.Ritani hiyo inapaswa kuonesha majina ya wajumbe wa Baraza la Wadhamini pamoja na anwani zao.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) hakikuwasilisha ritani ya wajumbe wa Baraza la Wadhamini tangu mwaka 2006, na hakukuwa na maelezo kutoka kwa viongozi wa CHAUMMA kuhusiana suala hili. Utaratibu huu ni kinyume na Kifungu Na. 16 (3) cha Sheria ya Usajili wa Wadhaminii Sura ya 318.

**Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza uongozi wa CHAUMMA kuwasilisha ritani ya wajumbe wa Baraza la Wadhamini kwa Kabidhii Wasii Mkuu wa Serikali (RITA) kila mwaka bila ya kuchelewesha. Pia, ninamshauri Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali kusimamia uwasilishaji wa ritani za wajumbe wa Baraza la Wadhamini kwa wakati.**

# SURA YA KUMI NA TATU

# KAGUZI MAALUMU

## 13.1 Utangulizi

Mbali na kufanya ukaguzi wa kifedha kila mwaka, Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalumu pale itakapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo au kuna hatari zilizotathminiwa wakati wa ukaguzi wa kisheria au zilizopo katika mpango wangu wa ukaguzi wa kila mwaka. Kwa kawaida, ukaguzi maalumu hufanyika pale panapokuwa na sababu ya msingi, ikiwa ni pamoja na kuongeza thamani kwa umma, na ikiwa kuna rasilimali za kutosha kufanya hivyo. Pia, Sheria hii inaruhusu mtu yeyote au taasisi, mamlaka za umma, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka za serikali za mitaa na vyombo vingine kumuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalumu.

## 13.2 Matokeo ya Kaguzi Maalumu Zilizofanyika kwenye Wizara, Idara, Wakala na Mifuko Maalumu

Katika mwaka huu wa fedha 2019/20, nimekamilisha kaguzi maalumu 15. Kati ya hizo, kaguzi maalumu saba ziliombwa na TAKUKURU, kaguzi nyingine tano ziliombwa na vyombo vingine, na kaguzi tatu zilianzishwa na ofisi yangu kulingana na tathmini ya hatari za udanganyifu na mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi wangu wa taarifa za fedha za mwaka 2018/19. Orodha ya kaguzi maalumu zilizoombwa na TAKUKURU zimebainishwa hapo chini.

**Jedwali Na. 125: Orodha ya Kaguzi Maalumu**

| Na. | Jina la Ukaguzi Maalumu | Taasisi iliyoomba |
|---|---|---|
| 1. | Ukaguzi Maalumu wa ujenzi wa uzio wa usalama kwenye uwanja wa ndege wa Bukoba | TAKUKURU |
| 2. | Ukaguzi Maalumu wa ujenzi wa shule ya msingi Tumaini | TAKUKURU |
| 3. | Ukaguzi Maalumu wa ujenzi wa shule ya sekondari ya mahitaji maalumu ya Patandi uliofanyika Chuo cha Ualimu Patandi - Mkoa wa Arusha | TAKUKURU |
| 4. | Ukaguzi Maalumu wa Ununuzi wa Vifaa Tiba uliofanyika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya | TAKUKURU |
| 5. | Ukaguzi Maalumu wa Mikabata ya Ushauri Elekezi wa | TAKUKURU |

| Na. | Jina la Ukaguzi Maalumu | Taasisi iliyoomba |
|---|---|---|
| | Huduma za Usanifu na Usimamizi wa Utanuzi wa Bomba la Maji Kutoka Ziwa Viktoria kwenda Miji ya Tabora, Igunga na Nzega uliotekelezwa na Wizara ya Maji ( Awamu ya I na II) | |
| **6.** | Ukaguzi Maalumu wa Malipo ya Fidia ya Ardhi yaliyofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | TAKUKURU |
| **7.** | Ukaguzi Maalumu wa Mradi wa Ukarabati wa Majengo, Mifumo ya maji na majitaka, Miundombinu Ya Tehama Na Mifumo Ya Umeme Chuo Cha Ualimu Ilonga, Kilosa Mkoani Morogoro | TAKUKURU |

Ripoti hii haijaonesha masuala yaliyobainishwa kwenye taarifa za kaguzi maalumu zilizoombwa na TAKUKURU. Hata hivyo, matokeo na mapendekezo ya kaguzi hizo yamewasilishwa TAKUKURU kuendelea na taratibu zingine za kisheria.

Mbali na ripoti za TAKUKURU, nimewasilisha pia ripoti za Kaguzi Maalumu kwa Taasisi na Mamlaka zilizoomba kaguzi hizi na zile ambazo Ofisi yangu imezianzisha. Ni mategemeo yangu kuwa, mapendekezo yote yaliyotolewa wakati wa ukaguzi yatafanyiwa kazi na mamlaka zilizoomba Ofisi yangu kufanya Kaguzi hizi Maalumu. Orodha ya kaguzi maalumu zilizofanyika zimebainishwa katika jedwali la hapa chini.

**Jedwali Na. 126: Orodha ya Kaguzi Maalumu Zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/20**

| Na. | Jina la Ukaguzi Maalumu | Taasisi iliyoomba |
|---|---|---|
| **1.** | Ukaguzi Maalumu wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii, Tamasha la Urithi na uanzishwaji chaneli ya Tanzania Safari na Studio ya Kutangaza Utalii | CAG |
| **2.** | Ukaguzi Maalumu wa matumizi ya fedha za utekelezaji miradi ya upangaji wa matumizi ya ardhi yaliyofanywa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi | CAG |
| **3.** | Ukaguzi Maalumu wa Mali za CUF na ACT-Wazalendo | Msajili wa vyama vya Siasa |
| **4.** | Ukaguzi Maalumu wa Matumizi ya Fedha za Ruzuku zilizotolewa na Mfuko wa uwezeshaji Sekta ya Fedha (FSDT) kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) | NIDA |
| **5.** | Ukaguzi Maalumu wa Fedha za Shirika la Kuhudumia | UNICEF |

| Na. | Jina la Ukaguzi Maalumu | Taasisi iliyoomba |
|---|---|---|
| | Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) zilizotumiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | |
| 6. | Ukaguzi Maalumu wa Mfumo wa Usajili uliofanyika Ofisi ya RITA DODOMA | CAG |
| 7. | Ukaguzi Maalumu juu ya tuhuma za ubadhirifu wa Kodi ya Zuio iliyokusanywa na Wakala wa Fundi na Umeme Serikalini (TEMESA) | Waziri Mkuu |
| 8. | Ukaguzi Maalumu wa Fedha za Ruzuku na Mali za Chama cha NCCR-Mageuzi | Msajili wa vyama vya Siasa |

*Chanzo: Ripoti za kaguzi Maalumu*

Kwa kuzingatia mbinu zangu za ukaguzi na Hadidu za Rejea zilizotolewa, ninabainisha masuala ya msingi niliyoyagundua. Nayo ni haya yafuatayo:

### 13.2.1 Ukaguzi Maalumu wa Mfuko wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii, Tamasha la Urithi na uanzishwaji chaneli ya Tanzania Safari na Studio ya Kutangaza Utalii

Ukaguzi ulilenga kuthibitisha iwapo makusanyo ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2019/20 yalitumika kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa. Pia, kuthibitisha iwapo uanzishwaji wa Chaneli ya Safari Tanzania, Tamasha la Urithi na Studio ya Utangazaji wa Utalii ulifuata taratibu zilizoainishwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Ukaguzi huu ulibaini masuala yafuatayo:

#### 13.2.1.1 Usimamizi usioridhisha wa Mfuko wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii Sh. 34,985,150,310.80

Katika kupitia uendeshaji wa akaunti za benki za makusanyo ya tozo za mfuko wa maendeleo ya utalii inayosimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, nilibaini kuwa Wizara hiyo ilikusanya tozo ya jumla ya Sh. 37,237,508,966.72 kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20. Wizara ya Maliasili na Utalii ilitumia jumla ya kiasi Sh. 28,823,036,258.72 kati ya kiasi chote kilichokusanywa, sawa na asilimia 77 ya makusanyo yote, Sh. 5,427,177,528, Sh. 2,808,369,533 na Sh. 100,000,000 zilihamishwa na Mkurugenzi wa Utalii kwenda Bodi ya Utalii, Chuo cha Taifa cha Utalii na Makumbusho ya Taifa, mtawalia, bila kuwa na idhini ya Afisa Masuuli wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Kamati ya Ushauri ya mfuko.

Pia, nilibaini kuwa jumla ya matumizi ya Sh. 6,875,458,200.34 yalilipwa kutoka kwenye Mfuko wa Tozo wa Maendeleo ya Utalii bila ya idhini ya Afisa Masuuli. Hii ni kinyume na Kanuni Na.88 (1) ya Kanuni za Fedha Za mwaka 2001 na Kanuni Na. 9(2) na 11 ya Kanuni za Tozo za Maendeleo ya Utalii za mwaka 2013. Pamoja na haya, nilibaini matumizi ya jumla ya Sh.16,363,437,737.11 bila ya kuwa na Hati za Malipo. Pia, yalibainika matumizi mengine ya jumla ya Sh. 11,156,910,952.25 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi.

Pia, nilibaini kuwa hadi kipindi cha ukaguzi, Kamati ya Ushauri ya Mfuko haikuundwa, kinyume na Kanuni Na. 9 (3) na 9 (4) (a-g) ya Kanuni za Tozo za Maendeleo ya Utalii za mwaka 2013. Mapungufu hayo yanaonesha kuwa, akaunti ya Tozo hizo haikusimamiwa ipasavyo na Mkurugenzi wa Utalii na Mhasibu ambapo walitoa fedha bila ya idhini ya Kamati ya Ushauri na Afisa Masuuli wa Wizara kufahamishwa.

Pia, ukaguzi wangu ulibaini kuwa kiasi cha Sh.500,000,000 kililipwa na Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) moja kwa moja kwa Bodi ya Utalii ya Taifa bila kupitia kwenye akaunti ya Tozo za Maendeleo ya Utalii. Hii ni kinyume na Kanuni ya 9 (1) na (2) ya Kanuni za Tozo za Maendeleo ya Utalii za mwaka 2013. Pia, nilibaini kiasi cha Sh. 89,343,421.10 kilitumiwa na Makumbusho ya Taifa kwenye matumizi yasiyoendana na shughuli za kiutalii.

Kwa maoni yangu, Mkurugenzi wa Utalii na Mhasibu waliokuwa wanahusika na usimamizi wa Mfuko wa Makusanyo ya tozo za maendeleo ya utalii walitumia vibaya fedha za tozo za utalii jumla ya Sh. 34,984,150,310.80 kinyume na Kanuni ya Tozo za Maendeleo ya Utalii za mwaka 2013.

**Napendekeza serikali ichukue hatua dhidi ya wahusika wote waliobainika kwa matumizi mabaya ya fedha za tozo za Maendeleo ya utalii.**

### 13.2.1.2 Mapungufu katika Uanzishwaji na Uendeshaji wa Tamasha la Urithi Sh. 2,085,494,988

Mnamo tarehe 15 Septemba 2018, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania alizindua Tamasha la Urithi ili kukuza utalii na urithi wa kitaifa. Kamati iliyoundwa iliidhinisha bajeti ya Sh.1,603,703,404 kwa ajili ya utekelezaji wa hafla hiyo. Hata hivyo, bajeti hiyo haikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kupitia ukaguzi wangu, nilibaini kuwa hakukuwa na mpango wa utekelezaji wa Tamasha la Urithi. Kutokana na kukosekana kwa mpango wa utekelezaji ulioidhinishwa, nilibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii iliomba wakala zake nne[10] kuchangia jumla ya Sh.1,000,000,000 ambazo hazikuwa kwenye bajeti zao ili kuwezesha kufanyika kwa Tamasha hilo. Ili kuongezea bajeti hiyo, Wizara ya Maliasili na Utalii ilichangia Sh. 299,085,677, na Mfuko wa Tozo wa Maendeleo ya Utalii ulichangia Sh. 270,838,527; ambapo hizi zote hazikuwa kwenye bajeti. Jumla ya Sh. 1,569,924,204 ilipatikana ili kufanikisha utekelezaji wa tamasha hilo.

Wakati wa Utekelezaji, nilibaini kuwa Kituo cha televisheni cha Clouds na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) walilipwa jumla ya Sh. 629,700,014 na Sh. 201,463,784, mtawalia, kwa ajili ya kuonesha matangazo ya Tamasha la Urithi. Hata hivyo, hakukuwa na risiti za kielektroniki zilizotolewa. Aidha, Serikali haikukusanya kodi ya zuio ya Sh. 31,485,000.70 na Sh.10,073,189.20 kutoka Kituo cha Televisheni cha Clouds na Shirika la Utangazaji wa Taifa (TBC). Timu ya ukaguzi haikupewa ushahidi unaoonesha kuwa manunuzi ya huduma za matangazo kutoka Shirika la Utangazaji wa Taifa (TBC) na Kituo cha televisheni cha Clouds zilipatikana kwa njia ya ushindani na usawa.

Pia, ukaguzi wangu ulibaini kuwa jumla ya Sh.487,258,000 zilipelekwa kwenye Taasisi saba[11] kwa ajili ya utekelezaji wa Tamasha la Urithi. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ili kuthibitisha matumizi hayo. Kadhalika, nilibaini matumizi ya Sh. 585,515,000 yaliyolipwa na Mhasibu wa Mfuko wa Tozo ya Maendeleo ya

[10] TANAPA ( Sh. 250,000,000), TFS (Sh. 250,000,000), NCAA ( Sh. 250,000,000) and TAWA (Sh. 250,000,000)

[11] NMT ( Sh. 115,020,000), Arusha (Sh. 130,000,000), Dodoma ( Sh. 24,338,000), Dar es Salaam (Sh.77,900,000), Mwanza (Sh. 60,000,000), Arusha ( Sh. 30,000,000) na BASAZA ( Sh. 50,000,000)

Utalii bila ya kuwa na nyaraka toshelezi; hivyo, nilishindwa kuthibitisha uhalali na usahihi wa malipo hayo.

Vilevile, nilibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ililipa Sh. 140,000,000 kwa Kampuni ya Wasafi kwa ajili ya wasanii ambao wangetangaza Utalii wa ndani katika mikoa sita ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Moshi, Iringa, na Dodoma. Hata hivyo, hakukuwa na mkataba wowote uliosainiwa kati ya Kampuni ya Wasafi na Wizara ya Maliasili na Utalii. Hivyo, sikuweza kuhakiki wigo wa kazi pamoja na huduma zilizotolewa na kampuni ya Wasafi.

Pia, nilibaini kuwa Hati ya malipo kwa Kampuni ya Wasafi iliambatanishwa na wasifu wa kampuni hiyo. Pia, kulikuwa na maagizo ya Waziri wa Maliasili na Utalii yakielekeza malipo kwa Kampuni ya Wasafi. Katika mahojiano na Waziri huyo, alikiri kuwa Kampuni ya Wasafi iliomba zabuni ya kutangaza tamasha hilo kwenye mikoa iliyotajwa na kutoa maagizo ya kufanya malipo hayo.

Ni maoni yangu kuwa, kiasi cha Sh.140,000,000 kilicholipwa kwa kampuni ya Wasafi kufuatia maelekezo ya Waziri wa Maliasili na Utalii haiendani na Kanuni za Maadili za Utumishi wa Umma.

**Ninapendekeza hatua stahili zichukuliwe na Serikali dhidi ya wote waliohusika na usimamizi usioridhisha wa fedha za mfuko wa Tozo wa Tozo za Maendeleo ya Utalii.**

### 13.2.2 Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (NCAA) Zilifadhili Tamasha la Upandaji wa Mlima Kilimanjaro Bila ya Kuwapo Kwenye Bajeti Sh. 171,998,045

Mnamo tarehe 28 Septemba 2019, Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii alizindua shindano lililoitwa Kigwangalla Kili Challenge la mwaka 2019 lililolenga kuhamasisha watu kupanda Mlima Kilimanjaro. Shindano hilo lilitumia jumla ya Sh. 171,998,045 ambayo zilitolewa na NCAA (Sh.114,500,000) na TANAPA (Sh. 57,498,045) bila kuwamo katika bajeti zao za mwaka wa fedha 2019/20. Pia, nilibaini kuwa Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia kaimu Katibu wake, alizielekeza NCAA na TANAPA kufadhili shindano hilo. Maelekezo haya yalikiuka Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, kinachowapa mamlaka

Maafisa Masuuli kuidhinisha malipo na sio Mawaziri wala Makatibu wa Mawaziri.

Fedha iliyotolewa na TANAPA ililipa Kampuni ya Utalii ya Ahsante Tours and Safaris Sh. 57,498,045 kwa ajili ya gharama za malazi za wapandaji mlima. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi ulioonesha kuwa Kampuni ya Ahsante Tours and Safaris ilipewa kazi hiyo kwa njia ya ushindani. Pia, hakukuwa na mkataba wa kazi hiyo uliowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Ni maoni yangu kuwa, maagizo yaliyotolewa na Waziri kupitia Katibu wake yalikiuka Sheria ya fedha za Umma na Kanuni za Maadili za Utumishi wa Umma. Maagizo haya yalisababisha TANAPA na NCAA kutumia Sh.171,998,045 nje ya bajeti iliyoidhinishwa. Ufadhili wa shindano hili umepunguza utekelezaji wa shughuli za TANAPA na NCAA ambazo zilikuwa zimetengwa kwenye bajeti kwa maslahi ya umma.

**Ninapenekeza hatua stahili zichukuliwe dhidi ya Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Katibu wake kwa ukiukaji wa Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma.**

### 13.2.3 Matumizi ya Ofisi ya Waziri Kugharamiwa na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (NCAA) na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kupitia maagizo Sh. 148,229,045

Nilibaini kuwa, Kaimu Katibu wa Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii alitoa maagizo kwa Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (NCAA) na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kulipia matumizi ya Ofisi ya Waziri Sh.92,296,045 na Sh. 55,933,000 kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii, mtawalia. Taasisi hizo hazikuwa na bajeti ya malipo hayo; na ukaguzi wangu ulibaini baadhi ya shughuli za taasisi zilizowekwa katika mipango yao hazikutekelezwa. Maombi ya fedha na idhini ya malipo kutolewa na Waziri ni ukiukaji wa masharti ya Kifungu Na. 8(1) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001. Pia, ni kinyume na Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma.

**Ninapendekeza hatua stahili zichukuliwe dhidi ya Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Katibu wake kwa kutumia fedha za NCAA na TFS kwa maslahi yao binafsi.**

### 13.2.4 Ukaguzi Maalumu wa Matumizi ya Fedha za Utekelezaji Miradi ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi Yaliyofanywa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Nilianzisha ukaguzi huu kufuatia madai kuhusu matumizi mabaya ya fedha zilizotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) na zile zilizopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ukaguzi wangu ulijikita katika kubaini ukweli wa madai yaliyotolewa. Katika ukaguzi wangu, nilibaini masuala yafuatayo:

#### 13.2.4.1 Mapungufu Yaliyobainika kwenye Malipo ya Shughuli za Upangaji wa Matumizi ya Ardhi

**a) Mapungufu Yaliyoibuliwa Kwenye Usimamizi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Sh.93,291,415.46**

Wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), nilibaini kuwa mmoja wa maafisa wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi alitumia jumla ya Sh. 5,630,000 ambazo hazikuwa kwenye bajeti. Pia, Sh. 5,580,000 zilitumika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa na mmoja wa maafisa bila idhini ya Mkurugenzi Mkuu. Pia, nilibaini kuwa kiasi cha Sh. 8,560,000 kilichukuliwa na mmoja wa wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa kutekeleza shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi katika vijiji kumi[12] vya Wilaya ya Chato kwa kudanganya idadi ya siku zinazostahili kulipwa kwa walengwa waliohudhuria mafunzo hayo.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilifadhili matumizi ya mkutano wa Bodi ya Mkurugenzi kwa gharama ya Sh. 69,041,415.46 kutoka kwenye fedha zilizotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais ili kutekeleza shughuli za upangaji matumizi ya ardhi katika wilaya za Nyasa, Mbinga, Ludewa, Makete na Kyela. Shughuli za upangaji na matumizi ya ardhi katika wilaya zilizotajwa hazikufanyika hadi wakati wa ukaguzi wangu mnamo mwezi Mei 2020; na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi haijarejesha fedha hizo. Kadhalika, nilibaini kuwa mmoja wa maafisa alilipwa posho ya jumla ya Sh. 4,480,000 zaidi ya siku zilizoidhinishwa.

---

[12] Nyambogo, Nyambiti, Makurugusi, Mkungo, Busalala, Ilemela, Musasa, Kasala, Mikonto na Kamanga

**b) Mapungufu Yanayohusiana na Kughushi Nyaraka za Malipo Sh. 160,780,000**

Wakati wa ukaguzi maalumu nilibaini yafuatayo kuhusiana na kughushi nyaraka za malipo: mmojawapo wa maafisa alighushi mihuri ya wenyeviti watano[13] wa vijiji na maafisa kata wa mkoa wa Singida na kujipatia kiasi cha Sh.12,810,000. Afisa mwingine alijipatia kiasi cha Sh. 16,840,000 kwa kudanganya tarakimu za malipo kwenye hati za malipo za vijiji vitatu[14] vya Wilaya ya Magu. Afisa mmoja alibadilisha kiasi na siku za malipo na kudanganya idadi ya walengwa wanaostahili kulipwa na kujipatia kiasi cha 16,270,000 katika vijiji vitano[15] vya Wilaya ya Mkalama na kijiji cha Sigili wilayani Nzega. Afisa mmoja katika Wilaya ya Igunga alighushi siku za malipo na kujipatia Sh. 7,120,000; na afisa mwingine huko Uvinza alighushi majina ya walengwa, saini, pamoja na siku zao za malipo na kujipatia Sh. 7,930,000 kinyume cha sheria.

Pia, nilibaini kuwa maafisa sita katika wilaya saba[16] walighushi saini za walengwa na kujipatia jumla ya Sh. 38,160,000. Pia, nilibaini ushirikano kati ya wafanyakazi wanne kutoka Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, mmoja kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) na wawili kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi ambao walidanganya siku za malipo na kujipatia kiasi cha Sh. 61,650,000 huko wilaya Kondoa, Kiteto, Muheza, Handeni, Makete, Nyasa, Mbinga na Wilaya za Uvinza.

**c) Mapungufu yanayohusu uwasilishaji wa risiti za udanganyifu Sh. 88,280,060**

Wakati wa kukagua uhalali wa Hati za masurufu, nilibaini kuwa stakabadhi kutoka kwa wauzaji wa mbao za matangazo zilighushiwa na maafisa sita na kujipatia jumla ya Sh. 44,122,000 katika wilaya saba[17]. Zaidi ya hayo, afisa mmoja katika Wilaya za Uvinza aliwasilisha risiti za nyumba za kulala wageni zilizokuwa za udanganyifu na kujipatia kiasi cha Sh.1,230,000, kinyume cha sheria.

Pia, nilibaini kuwa stakabadhi za huduma ya kunakili nyaraka za Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi zilighushiwa na maafisa wawili katika Wilaya za Muleba na Misenyi na kujipatia Sh.3,853,500. Kadhalika,

---

[13] Nkwae, Ntondo, Mrama, Madamigha, na Ifombou,
[14] Iseni, Nyang'hanga, na Lumeji
[15] Nyahaa, Mpambala, Lugongo, Mkiko na Munguli
[16] Makete, Chemba, Mbinga, Handeni, Nyasa, Kiteto na Muheza
[17] Mbogwe, Chato, Singida, Mkalama, Nzega, Muleba na Igunga

nilibaini kuwa, afisa mmoja aliwasilisha risiti za kughushi za gari lililokodiwa katika Wilaya ya Mbinga na kujipatia kiasi cha Sh.3,200,000. Vilevile, nilibaini maafisa tisa wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi walighushi risiti za kielektroniki na walijipatia sh. 35,874,560.

**Katika suala hili, ninapendekeza hatua stahili za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya Mkurugenzi Mkuu na Mhasibu Mkuu. Vilevile, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya maafisa wote waliohusika kwenye ubadhirifu wa fedha za umma katika Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.**

### 13.2.5 Ukaguzi Maalumu wa Mali za CUF na ACT-Wazalendo

Ukaguzi huu ulifanyika kufuatia madai kwamba mali zilizokuwa zinamilikiwa na Chama cha Wananchi (CUF) zilichukuliwa na chama cha ACT-Wazalendo, kubainisha ukweli iwapo majengo ya Chama cha Wananchi (CUF) yaliporwa au kukaliwa na Chama cha ACT-Wazalendo kinyume cha sheria, pamoja na kuhakiki iwapo chama cha ACT-Wazalendo kinamiliki mali zake kihalali. Yafuatayo ni matokeo ya uchunguzi wangu:

#### 13.2.5.1 Chama cha Wananchi (CUF) kinamiliki magari tisa na Pikipiki 27 yenye Majina ya Watu Binafsi

Nilipitia rejista ya mali za CUF na matamko ya mali za chama kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuanzia mwaka 2015 hadi 2019 na kubaini kuwa, CUF inamiliki magari 17, pikipiki nne, majenereta makubwa manne, samani na vifaa vingine vya ofisi. Hata hivyo, nilibaini kuwa mnamo mwaka 2017/18, CUF iliwasilisha tamko la mali kwa Msajili wa Vyama vya Siasa lilioonesha kuwa inamiliki magari 16 kati ya 17 yaliyoorodheshwa kwenye Daftari lake la Mali. Pia, nilibaini kuwa gari moja ambalo halikuorodheshwa kwenye tamko hilo lilikuwa linamilikiwa kihalali na mmoja wa wanachama.

Pia, niliomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ithibitishe uhalali wa magari yaliyotajwa kwenye tamko la mali. TRA walieleza kuwa CUF inamiliki kihalali magari manane. Magari mengine matatu yalisajiliwa kwa majina ya wanachama watatu, na magari sita yamesajiliwa kwa majina ya Mkurugenzi wa zamani wa fedha na uchumi. Wanachama watatu waliotajwa na TRA kuwa walithibitisha kutomiliki magari husika, licha ya magari husika kusajiliwa kwa majina yao. Hata hivyo, sikuweza kubaini sababu za CUF kusajili magari haya kwa kutumia majina ya watu binafsi.

Aidha, CUF haikuorodhesha pikipiki 23 inazodai kuzimiliki katika mikoa mbalimbali kwenye daftari lake la mali. Kwenye tamko la mali la mwaka 2015/16 liliowasilishwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa CUF iliripoti kumiliki pikipiki 35 Tanzania Bara na 4 huko Zanzibar. Hata hivyo, CUF haikuweza kuthibitisha maelezo ya pikipiki zingine 12 zilizopo kwenye tamko la mali kwa Msajili wa vyama vya Siasa la mwaka 2015/16. TRA ilithibitisha kuwa pikipiki zote 27 zilisajiliwa kwa kutumia majina ya watu na kampuni binafsi. Kati ya pikipiki hizo 27, pikipiki 22 zilimilikiwa na mtu mmoja, pikipiki 2 zilimilikiwa na watu wawili tofauti, pikipiki 2 zingine zilikuwa zinamilikiwa na kampuni moja na pikipiki 1 ilikuwa inamilikiwa na kampuni nyingine tofauti.

Pia, nilibaini kuwa pikipiki 3 kati ya pikipiki 27 zilikuwa kwenye Ofisi za CUF licha ya kuwa zilikuwa mbovu; na pikipiki 24 zilizobaki hazikuonekana. Sikuweza kupata mahojiano na watu waliokabidhiwa ili kujua ukweli kuhusiana na umiliki wao. Hata hivyo, Katibu Mkuu CUF alieleza kuwa pikipiki zilizoorodheshwa kwenye tamko la mali ni mali za CUF. Hata hivyo, hakuweza kuwasilisha nyaraka za ununuzi pamoja na kushindwa kutoa maelezo kuhusiana na sababu za chama cha Wananchi (CUF) kuandikisha pikipiki hizo kwa kutumia majina ya watu binafsi.

**Kwa Kuzingatia yaliyotajwa hapo juu, ninapendekeza kwa uongozi wa Chama cha Wananchi (CUF) kuhakikisha kuwa mali zote za chama zinasajiliwa kwa jina la Baraza la Wadhamini la CUF. Mali ambazo zina majina ya watu zibadilishwe na kusajiliwa kwa jina la Baraza la Wadhamini la CUF.**

### 13.2.5.2 Chama cha Wanachi (CUF) Kilikosa Nyaraka za Kuthibitisha Umiliki wa Pikipiki 24 na Magari 24

Naibu Katibu Mkuu aliwasilisha orodha ya magari 24 na pikipiki 50 zinazodaiwa kutumiwa na CUF huko Zanzibar. Hata hivyo, Naibu Katibu Mkuu hakuwasilisha nyaraka za ununuzi/umiliki wa magari na pikipiki hizo. Naibu Katibu Mkuu Zanzibar alieleza kuwa CUF inamiliki magari na pikipiki zilizoorodheshwa licha ya nyaraka hizo kuchukuliwa na viongozi wa chama waliohamia chama cha ACT Wazalendo. Aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wote walieleza kuwa magari na pikipiki zilizoorodheshwa zilinunuliwa na mwanachama mmoja katika vipindi tofauti bila ya kutaja chanzo cha fedha kilichotumika kununua mali hizo.

Hata hivyo, katika kuthibitisha ukweli huo, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar alionesha mkanda mfupi wa video uliorekodiwa wakati wa ugawaji wa magari na pikipiki hizo kwa viongozi wa chama hicho mnamo mwezi Oktoba 2015. Kupitia video hiyo, nilibaini kuwa magari 13 yalitolewa kwa viongozi hao, ingawa sikuweza kuona idadi ya pikipiki zilizogawiwa. Kati ya magari 13 yaliyoonekana, niligundua magari 4 tu ndio yaliyo kwenye orodha ya magari 24 yaliyowasilishwa. Magari 11 hayakuwamo kwenye orodha ya magari iliyowasilishwa. Niliiomba Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) kuthibitisha taarifa za umiliki za magari na pikipiki zilizowasilishwa. Bodi ya Mapato Zanzibar ilieleza kuwa, pikipiki 26 zilisajiliwa kwa jina la Baraza la Wadhamini la Chama cha Wananchi (CUF) na pikipiki 24 zilizobaki zilisajiliwa kwa majina ya watu binafsi.

Mbali na hayo, Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) ilithibitisha kuwa magari yote 24 hayakusajiliwa kwa jina la CUF; badala yake, yalisajiliwa kwa majina ya watu binafsi. Mwanachama mmoja wa chama hicho alidai kumiliki magari yote 24; na alieleza kuwa alinunua kwa gharama ya Sh.140,000,000, ikiwa ni pamoja na Sh.70,000,000 zilizotolewa na mwanachama mwingine. Hata hivyo, mwanachama huyo hakuweza kuthibitisha madai yake. Licha ya ukweli kuwa CUF iliwasilisha majina ya viongozi waliopokea pikipiki 50, sikuweza kuthibitisha kuwapo kwa pikipiki hizo kwenye ofisi za CUF. Katika mahojiano, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar alithibitisha kuwa wanachama hao ni miongoni mwa viongozi waliojiunga na chama cha ACT Wazalendo; na waliondoka na pikipiki walizokabidhiwa.

Katika kupitia nyaraka, nilibaini kuwa tamko la mali kwa Msajili wa Vyama vya Siasa la mwaka 2015/16 na 2017/18 na rejista za mali za chama kuanzia mwaka 2015 hadi 2019 zilizokuwa zikitunzwa makao makuu ya chama cha CUF Buguruni, Dar es Salaam, hazikuorodhesha magari 24 na pikipiki 50. Pia Bodi ya Mapato ya Zanzibar haikuthibitisha kuwa chama cha CUF kinamiliki magari na pikipiki tajwa. Kwa kuzingatia ukweli kuwa tamko la mali za CUF kwa Msajili wa Vyama vya Siasa halikuonesha magari na pikipiki zilizotajwa, na kwa kuwa baadhi ya wanachama walithibitisha kuwa magari na pikipiki zilizotajwa sio mali ya chama cha Wananchi (CUF), ukaguzi wangu haukuweza kuthibitisha iwapo Chama cha Wananchi (CUF) kinamiliki magari 24 na pikipiki 50 zilizotajwa.

**Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza Msajili wa Vyama vya Siasa kuwezesha upatanisho kati ya Chama cha Wananchi (CUF) na wanachama wa zamani wa CUF waliohamia chama cha ACT Wazalendo ili kufanikisha makabidhiano ya mali.**

### 13.2.5.3 Utata wa Umiliki Magari Sita Yaliyosajiliwa kwa Majina ya Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi

Kumekuwa na mashaka kuhusiana magari sita ambayo chama cha Wananchi (CUF) kilidai kumiliki wakati yalisajiliwa kwa majina ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi. Kupitia nyaraka na mahojiano yaliyofanyika niliweza kubaini ukweli ufuatao:

#### a) Ukweli unaohusiana na Chanzo cha fedha Dola za Marekani 85,637 zilizotumika kununua magari sita

Kama ilivyoelezwa hapo juu, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilithibitisha kuwa magari sita kati ya 17 yalisajiliwa kwa majina ya Mkurugenzi wa Zamani wa Fedha na Uchumi. Kupitia ukaguzi wangu, nilibaini dokezo sabili lilioonyesha kuwa CUF kutumia Dola za Marekani 85,637 (sawa na Sh. 169,989,445) kununua magari sita kutoka Dubai. Dokezo hilo linaonesha kuwa, Chama cha Wananchi (CUF) kilipokea Dola za Marekani 100,000 ambazo sikuweza kuthibitisha chanzo chake kwa kuwa wahusika waliotajwa kwenye dokezo walikataa kuelezea chanzo cha fedha. Mwenyekiti wa Chama alieleza kuwa alimkabidhi Dola za Marekani 100,000 Mkurugenzi wa zamani wa Fedha na Uchumi kununua magari hayo sita, ambayo yalitumika kwenye uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Hata hivyo, hakuweza kutoa ushahidi wowote. Pia, alieleza kuwa alipata fedha hizo kutoka vyanzo mbalimbali lakini hakuwasilisha ushahidi wowote.

Mkurugenzi wa zamani wa Fedha na Uchumi alieleza kuwa anamiliki magari hayo sita yaliyosajiliwa kwa majina yake, na aliyatoa kukisaidia chama wakati wa kipindi cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi uliowasilishwa. Pia, alikana kupokea kiasi cha Dola za Marekani 100,000 kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama.

#### b) Ukweli kuhusu aliyekuwa Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi kununua magari kwa niaba ya Chama cha Wananchi (CUF)

Maelezo ya Mkurugenzi wa zamani wa Fedha na Uchumi kwamba anamiliki magari yaliyotajwa yanapingana na tamko la mali za chama  kwa Msajili wa Vyama vya Siasa la tarehe 19 Septemba 2016 linaloonesha kuwa magari sita yaliyotajwa ni miongoni mwa magari 19 yaliyojumuisha kwenye tamko

la mali licha ya nambari za usajili kutoandikwa. Pia, madai yake yanapingana na barua ya ndani aliyoiandika na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu akiomba fedha kwa ajili ya kulipia ushuru wa forodha na ada ya bandari jumla ya Sh. 139,959,603 kwa ajili ya kugomboa magari sita yaliyoingizwa kutoka nje ya nchi. CUF ililipa jumla ya Sh.136,000,707, na magari hayo aliyakabidhi kwa Chama cha Wananchi (CUF) kupitia barua ya tarehe 1 Juni 2015, pamoja na nyaraka za manunuzi. Mkurugenzi wa zamani wa Fedha na Uchumi alieleza kuwa suala hili liko Mahakamani; hivyo hakueleza sababu za nyaraka za gari yake binafsi kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu CUF. Pamoja na hayo yaliyosemwa, alikataa kutambua saini iliyopo kwenye fomu za Tamko la Mali na hakueleza chanzo cha Sh. 136,000,707 zilizotumika kugombolea gari bandari huku akisisitiza kuwa suala hilo liko mahakamani.

**c) Ukweli kuhusu mantiki ya Chama cha Wananchi (CUF) kutumia majina ya watu binafsi wakati wa mchakato wa usajili wa magari**

Aliyekuwa katibu Mkuu wa CUF alieleza kuwa CUF iliazima magari hayo kutoka kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa fedha na Uchumi. Hata hivyo, hakutoa ushahidi wa kuonesha chanzo cha fedha na nyaraka za kukabidhi magari hayo. Madai yake yanapingana na maelekezo aliyotoa kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi ya kubadilisha majina ya usajili wa magari kuwa jina la Baraza la Wadhamini la CUF. Katika nyakati tofauti, Mwenyekiti wa Chama alifafanua kuwa magari yaliyotajwa yalisajiliwa kwa majina ya watu binafsi ili kuzuia uwezekano wa urasimu ambao ungechelewesha chama cha wananchi (CUF) kushiriki katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Katibu Mkuu (Tanzania Bara) alifafanua kuwa mchakato wa usajili usingeweza kukamilika katika kipindi kifupi kabla ya uchaguzi mkuu wa 2015. Baada ya uchaguzi, Chama cha Wananchi (CUF) kiliingia katika mgogoro na wanachama wake waliohamia chama cha ACT-Wazalendo na nyaraka zote. Pia, alikiri kuwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi hakuwahi kukisaidia chama mali yoyote. Pia, alieleza kuwa Chama cha Wananchi (CUF) hakiwezi kuwasilisha taarifa za mali binafsi kwa Msajili wa vyama. Hivyo, mali zote zilizoorodheshwa kwenye tamko la mali la chama ni mali halali za chama ijapokuwa Chama cha CUF kilishindwa kuthibitisha chanzo za fedha jumla ya Dola za Marekani 100,000 iliyotumika kununulia magari husika kipindi cha uchunguzi wangu.

Kwa kuzingatia mahojiano na matamko ya mali za chama kwa Msajili wa vyama vya Siasa yaliyowasilishwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi na nyaraka za ndani zilizopitiwa, nakubaliana na ukweli uliotolewa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi, aliyekuwa Katibu Mkuu, Mwenyekiti wa Chama, Naibu Katibu Mkuu (Tanzania Bara), Naibu Katibu Mkuu walipokuwa pamoja kabla ya mgogoro ikilinganishwa na ushahidi uliotolewa wakati chama kikiwa kwenye mgogoro. Kwa kuwa ukaguzi wangu unategemea nyaraka na maelezo wakati Chama hakikuwa kwenye mgogoro, hivyo katika hili, ni wazi kuwa Chama cha Wananchi (CUF) kinamiliki magari tajwa licha ya kusajiliwa kwa majina ya Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi.

**Kuhusiana na hili, ninapendekeza kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuwezesha upatanisho baina ya chama cha wananchi (CUF) na waliokuwa wanachama wa Chama cha Wananchi (CUF) waliohamia Chama cha ACT Wazalendo, na kufanikisha makabidhiano ya mali zinazomilikiwa na chama na kuhakikisha kuwa zinasajiliwa kwa jina la Baraza la Wadhamini.**

### 13.2.6 Ukaguzi Maalumu kuhusu Matumizi Yaliyofanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Kwenye Fedha za Ruzuku Zilizotolewa na Mfuko wa uwezeshaji sekta ya Fedha (FSDT)

Ofisi yangu ilianzisha ukaguzi huu ili kubaini ukweli iwapo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ilitumia fedha za mradi kutoka Mfuko wa uwezeshaji sekta ya Fedha (FSDT) kama ilivyotakiwa, kuthibitisha iwapo nyaraka zilizotumka zilikuwa halali, matumizi yaliyofanyika yalipata kibali kama ilivyoainishwa kwenye mkataba wa mradi, kuthibitisha iwapo matumizi yaliyoidhinishwa yalikuwa halali, stahili na sahihi, kuthibitisha iwapo Mamlaka ya Vitambulisho vya Umma (NIDA) ilifuata taratibu za manunuzi ya umma wakati wa ununuzi wa vifaa vya mradi, pamoja na kubaini ukweli juu ya tuhuma kuwa mfumo wa matangazo kwa umma ulionunuliwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) haukuwahi kuwapo. Yatokanayo na ukaguzi wangu ni kama ifuatavyo:

#### 13.2.6.1 Lengo la Mradi la Kuzalisha Namba za Utambuzi wa Taifa (NIN) Halikufikiwa Licha ya Dola za Marekani 1,153,588 Sawa na Sh.2,595,573,000 Kutumika na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

Mfuko wa uwezeshaji sekta ya Fedha (FSDT) na NIDA walisaini makubaliano ya ruzuku Na. FSDT/NIDA/09/16 mnamo tarehe 23 Machi 2017 kwa madhumuni ya kuiwezesha NIDA kuzalisha Namba za Utambuzi wa Taifa (NIN) takribani 20,000,000 kwa kutumia taarifa za wapiga kura za mwaka 2015. Zoezi hilo lilipangwa kukamilika tarehe 21 Februari 2018. Uchunguzi wangu ulibaini kuwa mfuko wa uwezeshaji sekta ya fedha (FSDT) ilitoa Dola za Marekani 1,153,588 kati ya Dola za Marekani 3,000,000 walizokubaliana ili kukamilisha lengo hili. Hata hivyo, sikuweza kupata ushahidi wa Namba za Utambuzi (NIN) zilizozalishwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) licha ya Dola za Marekani 1,153,588 kutumiwa na NIDA ili kukamilisha lengo hili. Pia, niligundua kuwa FSDT na NIDA walitarajia kusaini mkataba mpya wa nyongeza ili kukamilisha shughuli za mradi. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi wangu, mwezi Agosti 2019, makubaliano hayo yalikuwa hayajafikiwa.

Ni maoni yangu kuwa, fedha za mradi jumla ya Dola za Marekani 1,153,588 (sawa na Sh.2,595,573,000) zilizotumiwa na NIDA hazikuleta tija kutokana na lengo la Mradi kutofikiwa. Hasara waliopata wafadhili wa mfuko wa uwezeshaji sekta ya fedha (FSDT) imesababisha na menejimenti ya NIDA kushindwa kusimamia ipasavyo shughuli za mradi.

**Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza kwamba kabla ya marejeo ya Mkataba mpya wa ruzuku Mfuko wa uwezeshaji sekta ya Fedha, NIDA inapaswa kukagua mahitaji yake halisi na kujiridhisha kama yanaendana na madhumuni ya mradi yanayokusudiwa.**

#### 13.2.6.2 Matumizi ya Mradi ya Jumla ya Dola za Marekani 292,763.18 (sawa na Sh. 658,717,155) yalidanganywa kwenye Ripoti Jumuifu ya Matumizi ya Mradi iliyowasilishwa FSDT na NIDA

Nilipitia ripoti Jumuifu ya Matumizi ya Mradi iliyowasilishwa na Mfuko wa uwezeshaji sekta ya Fedha FSDT na kugundua kuwa kati ya Dola za Marekani 480,934 sawa na Sh. 1,082,101,500 zilizotumwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Benki ya NIDA mnamo tarehe 12 Aprili 2017, NIDA ilitumia Dola za Marekani 357,170.82 sawa na Sh 803,634,345 na ilikuwa na bakaa ya Dola za Marekani USD 123,763.18 hadi kufikia Machi 2018. Hata

hivyo, katika ripoti hiyo, ilioneshwa kuwa NIDA ilitumia kiasi chote cha Dola za Marekani 480,934 zilizopokelewa licha ya Dola za Marekani 123,763.18 kutokutumiwa na NIDA. Pia, iliripotiwa kuwa mzabuni mmoja alilipwa Dola za Marekani 275,000 licha ya kuwa amelipwa Dola za Marekani 135,000 tu. Kwa hivyo, NIDA ilizidisha matumizi ya Dola za Marekani 140,000, ambazo hazikulipwa kwa Mzabuni aliyetajwa. Pia, NIDA ilionesha kutumia Dola za Marekani 391,594 kwa ajili ya kununua leseni za windows, darmalog, na leseni za algorithms. Baada ya ukaguzi wa taarifa za msingi zilizowasilishwa na FSDT nilibaini kuwa NIDA ilitumia Dola za Marekani 362,594 tu kwa bidhaa zilizotajwa, na Dola za Marekani 29,000 zilizoripotiwa kutumika zilikuwa hazijatumika.

Ni maoni yangu kuwa, kuonesha matumizi zaidi ya matumizi halisi kwenye Ripoti Jumuifu ya Matumizi ya Mradi kunaashiria kuwapo kwa usimamizi usiofaa wa fedha za mradi, pia kunatia mashaka ya kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha husika.

**Hivyo, ninapendekeza kufanyika kwa uhakiki wa pamoja wa matumizi ya mradi kati ya NIDA na FSDT ili kuthibitisha uhalali wa matumizi ya mradi yaliyoripotiwa kabla ya kusainiwa kwa makubaliano mapya ya ruzuku.**

### 13.2.6.3 Ununuzi Bila ya Kushirikisha Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi (PMU) - Dola za Marekani 220,200

Tarehe 21 Aprili 2011 NIDA ilisaini Mkataba Na. AE/06/2009/2010/G.08 na mkandarasi (shirika la IRIS Berhad). Mkataba ulihusu kusambaza bidhaa na kutekeleza mfumo wa utambulisho unaotumia teknolojia ya "Smart" kwa kupitia utaratibu wa ushirikiano wa umma na taasisi binafsi (PPP). Mkataba huo ulikamilika mnamo tarehe 23 Juni 2013 kwa mkandarasi (Shirika la IRIS Berhad) kukamilisha vitu vilivyobaki kwenye mkataba wa awali. Kuanzia tarehe 23 Juni 2013 hapakuwa na makubaliano mengine kwa ajili ya utekelezaji.

NIDA ilimpa zabuni Shirika la IRIS Berhad ya kununua leseni za darmalog, Biometric Algorithms na usafishaji kanzidata, uhamishaji, na utunzaji wa mfumo kwa jumla ya Dola za Marekani 220,200 (sawa na Sh. 495,450,000). Mchakato wa ununuzi ulikamilishwa bila ushiriki wa Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi (PMU), kinyume na kifungu Na. 33 (1) (d) na 38 (a) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011

(iliyorekebishwa mwaka 2016). Pia, nilibaini kuwa maafisa wawili walipitisha manunuzi hayo na kumuidhinisha mkandarasi kufanya mabadiliko kwenye kanzidata ya NIDA kwa kutumia Fomu za kufanya mabadiliko kwenye mfumo (CRF) zilizoidhinishwa na wao bila idhini ya Mkurugenzi Mkuu.

Ni maoni yangu kwamba, manunuzi yaliyotajwa hapo juu hayakufuata matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 (iliyorekebishwa mwaka 2016). Nina uhakika kwamba, hakuna thamani halisi ya fedha iliyopatikana kwenye manunuzi yaliyofanyika.

**Kwa maelezo hapo juu, ninapendekeza hatua za kinidhamu zilichukuliwe kwa maafisa waliohusika, ambao walizuia taratibu za ununuzi kufuatwa.**

### 13.2.6.4 NIDA Ilitumia Jumla ya Sh. 151,051,838 ambayo Haikuendana na Masharti ya Mkataba wa Ruzuku

Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa awamu sita kwa ajili ya kuandaa miundombinu, kuzalisha na kusambaza Namba za Utambuzi wa Taifa (NIN) kwa umma kupitia mfumo wa taarifa fupi (SMS) hadi kufikia tarehe 21 Februari 2018. Nilibaini kuwa, NIDA ilipokea Dola za Marekani 480,934 (sawa na Sh. 1,082,101,500) mnamo 12 Aprili 2017 kutoka Mfuko wa uwezeshaji Sekta ya Fedha (FSDT) kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi kwa awamu ya kwanza.

Baada ya kupitia taarifa za mradi, nilibaini NIDA ilitumia jumla ya Sh. 151,051,838 kwa ajili ya matumizi ambayo hayahusiani na mradi. Kati ya kiasi kilichotumika, jumla ya Sh. 149,551,838 zilitumika kufadhili mazoezi ya usajili na utambulisho, na Sh. 1,500,000 zilitumika kufadhili mikutano ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Sh. 28,123,979 zilitumiwa kama posho ya kujikimu na dizeli kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya BVR, na Sh. 22,197,900 zilitumika kufadhili maonesho ya sabasaba na nane nane, kinyume na makubaliano ya ruzuku.

Malipo ya Sh. 151,051,838 yaliyoidhinishwa na maafisa wa NIDA yalikuwa hayaendani na malengo ya mradi; hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za mradi.

**Katika suala hili, ninapendekeza kuchukuliwa kwa hatua za kinidhamu kwa maafisa wa NIDA waliochepusha fedha za mradi kwenye matumizi mengine.**

### 13.2.7 Ukaguzi Maalumu wa Fedha za Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) Zilizotumiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa kuthibitisha iwapo matumizi ya Fedha za Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) yaliyofanywa na Idara ya Ustawi wa Jamii (DSW) iliyopo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto yalifuata makubaliano ya mradi. Pia, kubaini iwapo kulikuwa na mapungufu kwenye usimamizi wa fedha za UNICEF, kuthibitisha iwapo ununuzi wa bidhaa na huduma ulifuata Taratibu za manunuzi, na kubainisha kama kulikuwa na upungufu wowote. Ukaguzi ulibaini yafuatayo:

#### 13.2.7.1 Mapungufu Yaliyoibuliwa kwenye Usimamizi wa Fedha za UNICEF

**a) Mapungufu Yanayohusiana na Kughushi Yyaraka za Malipo**

Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) lilitoa Sh. 1,052,939,000 kwa ajili ya Idara ya Ustawi wa Jamii (DSW) ili kufadhili matumizi ya kawaida kuanzia 1 Januari 2018 hadi 31 Agosti 2020. Pia, nilibaini kuwa Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) hapo awali lilifadhili Idara ya Ustawi wa Jamii na kulikuwa na bakaa ya Sh. 6,877,500 hadi kufikia tarehe 1 Januari 2018. Jumla ya kiasi cha Sh.1,059,816,500 kilikuwapo kwenye Idara ya Ustawi ya Jamii (DSW) ili kutekeleza shughuli mbalimbali za UNICEF katika kipindi hicho. UNICEF iliidhinisha posho ya kila siku ya kujikimu (DSA) ilipwe kwa maafisa wote na washiriki kwa kiwango kilichoidhinishwa na Serikali.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii (DSW) ililipa posho ya jumla ya Sh.15,020,000 kwa washiriki 78, zaidi ya kiwango cha posho ya kujikimu kila siku kilichoidhinishwa na Serikali; hivyo kusababisha matumizi mabaya ya fedha za UNICEF. Pia, nilibaini kuwa wafanyakazi tisa wa Idara ya Ustawi wa Jamii (DSW) walidanganya siku walizotumia kutekeleza majukumu tisa ya mradi, hivyo kupelekea kulipwa Sh. 20,480,000 ambayo hawakustahili. Pia, Idara ya Ustawi wa Jamii ililipa

kiasi cha Sh. 12,375,000 kwa wawezeshaji watano wa nje bila ya kuwapo kwa mikataba.

Watumishi wanane wa Idara ya Ustawi wa Jamii (DSW) walidanganya majina ya washiriki na kujipatia kiudanganyifu Sh. 4,311,000. Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) lilifanya ukaguzi wa matumizi ya fedha ilizozitoa kwa Idara ya Ustawi wa Jamii mwezi Julai 2020 na kukamilisha ukaguzi huo mwezi Agosti 2020. Lilibaini kuwa, hati za malipo saba zilizowasilishwa wakati wa ukaguzi huo zilibadilishwa tarakimu,majina ya walipwaji na siku za malipo.

Mapungufu hayo yanaonesha kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii (DSW) haikuwa na mifumo imara ya udhibiti wa ndani yenye uwezo wa kugundua, kupunguza na kutaarifu matukio yote yanayohusiana na matumizi mabaya ya fedha, kughushi nyaraka za malipo.

**b) Mapungufu Yanayohusu Uzingatiaji wa Taratibu na Miongozo ya Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF)**

Kulingana na taratibu na Miongozo ya UNICEF, Idara ya Ustawi wa jamii ilitakiwa kukata asilimia 10 na 15 kwenye posho za kila siku za kujikimu zinazolipwa kwa washiriki na wawezeshaji iwapo watahudumia chai na chakula cha mchana. Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii haikukata kiasi cha Sh 41,963,500 kutoka kwenye malipo ya huduma ya chai na chakula cha mchana kwenye malipo ya shughuli 20 za Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) licha ya kuwahudumia chai na chakula cha mchana washiriki na wawezeshaji.

Pia, nilibaini kuwa watumishi wawili wa Idara ya Ustawi wa Jamii waliwasilisha nyaraka za masurufu zisizokuwa timilifu, hivyo sikuweza kuhakiki uhalali wa malipo ya Sh. 6,679,000 yaliyofanyika. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa watumishi 10 wa Idara ya Ustawi wa Jamii (DSW) walitumia Sh.105,310,060 zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa katika kutekeleza shughuli za UNICEF ambazo ni zaidi ya asilimia 20 bila kuomba idhini kutoka UNICEF.

Pia, nilibaini kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii (DSW) ilifungiwa kupokea fedha za UNICEF kwa miezi 10 kwa sababu ya kuchelewa kutoa mrejesho wa matumizi wa shughuli 23 za jumla ya Sh. 562,427,000. Pia, Idara ya Ustawi wa Jamii ilitumia Sh. 200,851,061 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa

mbalimbali bila kufuata taratibu za manunuzi ya umma kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2011 (kama iliyorekebishwa mwaka 2016).

**Ninapendekeza Idara ya Ustawi wa Jamii kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kulinda matumizi ya fedha za miradi ya wafadhili. Pia, ninapendekeza hatua stahili za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya Watumishi wote waliohusika na ubadhirifu wa fedha za UNICEF.**

### 13.2.8 Ukaguzi Maalumu wa Mfumo wa Usajili Katika Ofisi ya RITA DODOMA

Ofisi yangu ilipokea tuhuma kwamba Mfumo wa Kiraia wa Usajili uliopo katika Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kuwa haukuundwa vizuri; ambapo risiti moja ya Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG) inaweza kuruhusu uchapishaji wa vyeti na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali. Vilevile, kulikuwa na tuhuma za utumiaji wa vitabu visivyotambulika katika utoaji wa vyeti vya kuzaliwa na ndoa; hivyo kusababisha Serikali kupoteza mapato.

Pia, kulikuwa na tuhuma kwamba vyeti vya kuzaliwa na ndoa havikuwa kwenye kanzidata ya Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) na kuthibitisha ukweli wa tuhuma zilizotolewa. Kufuatia ukaguzi wangu kuhusiana na jambo hili, yalibainika yafuatayo:

#### 13.2.8.1 Hasara Iliyotokana na Usimamizi Usioridhisha wa Mfumo wa Kiraia wa Usajili na Mfumo wa Mozilla Uliofanywa na RITA Sh. 116,460,500

Katika kupitia mifumo ya makusanyo ya mapato iliyopo RITA kuanzia mwezi Januari 2018 hadi Aprili 2020, nilibaini kuwa RITA inatumia mfumo wa Kiraia wa Usajili (civil registration system) kwa ajili ya utoaji wa vyeti vya kuzaliwa na vifo pale malipo ya ada husika yatakapofanyika kupitia Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG). RITA imekuwa ikitoa vyeti ya ndoa bila ya kutumia mfumo. Kabla ya kununua mfumo huo wa Usajili wa Kiraia, RITA ilikuwa na mfumo mwingine wa Usajili (mozilla registration system) ambao ulikuwa unatoa vyeti vya kuzaliwa na vifo.

Mwaka 2015, RITA ilihama kutoka kwenye mfumo wa usajili wa Mozilla na kutumia mfumo mpya wa Usajili (civil registration system). Kupitia ukaguzi wangu, niligundua kuwa mfumo wa usajili wa Kiraia (CRS) hauruhusu

unakilishaji wa namba za risiti. Zaidi, ilibainika kuwa mfumo huo unaruhusu namba yoyote inayoingizwa kwenye hatua ya uhakiki wa malipo ambayo sio batili au ya kujirudia.

Kuanzia mwezi Juni 2018, RITA ilianza kutumia Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG), ambapo ilianza kukusanya mapato yake kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato (POS) zilizounganishwa kwenye Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG) . Hata hivyo, Mfumo wa Usajili wa Kiraia (CRS) haujaunganishwa na Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG).

Wakati wa ukaguzi wangu, sikuweza kuthibitisha vyeti ya kuzaliwa 6,180 vyenye jumla ya thamani ya Sh. 84,586,000 vilivyochapishwa na Mfumo Usajili wa Kiraia (CRS) kwa kutumia Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG) kuanzia mwezi Juni 2018 hadi Juni 2020. Pia, sikuweza kuthibitisha iwapo vyeti ya kuzaliwa 3,861 vyenye thamani ya Sh. 14,694,600 vilivyochapishwa na Mfumo wa Usajili wa Mozilla kwa kutumia taarifa za mapato yaliyokusanywa kutokana na Stakabadhi kutoka Serikalini.

Pia, nilibaini kuwa jumla ya Sh.99,280,550 zilichukuliwa kutokana na miamala ya hapo juu. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh. 40,063,500 kilichukuliwa na maofisa saba. Pia, sikuweza kutambua majina ya wafanyakazi waliochukua jumla ya Sh. 59,217,000. Wafanyakazi hao walikuwa wakiingiza namba za stakabadhi au za risiti za Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini GePG na kuchapisha vyeti kutoka kwenye mfumo wa Kiraia au Mozilla.

Kutokuunganishwa kwa Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini GePG na CRS umewezesha ubadhirifu wa kiasi kilichoripotiwa kwa kuwa kulikuwa na mapungufu katika mfumo wa kukubali risiti yoyote ya malipo inayoingizwa bila kuthibitisha kiasi halisi kilicholipwa. Upungufu huu umepunguza uhalisia wa taarifa za mapato zinazoripotiwa kutoka kwenye mfumo wa CRS.

Pia, ukaguzi wangu ulibaini vyeti vya vifo 289 vyenye thamani ya Sh. 2,222,500 vilivyochapishwa kutoka kwenye mfumo wa CRS bila ya kuonekana kwenye Mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG) kuanzia mwezi Juni 2018 hadi Juni 2020. Wafanyakazi watatu wa RITA ofisi

ya Wilaya ya Dodoma walidanganya na kuchapisha vyeti 20 vyenye thamani ya Sh. 77,500 kutoka kwenye Mfumo wa Usajili wa Mozilla bila ya kuzionesha kwenye ripoti ya makusanyo ya mapato kwa kutumia stakabadhi za Serikali.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa karatasi za vyeti 15,125 zenye thamani ya Sh. 6,050,000 zilizonunuliwa kutoka kwa mzabuni zimeachwa bila ya kutumika kwa kukosa namba ya utambuzi. Vyeti vya kuzaliwa vya watoto 368 vilitolewa na kuandikishwa kwenye rejista ya maombi ya utoaji wa vyeti, lakini havikuonekana kuchapishwa kwenye mfumo wa Usajili wa Kiraia uliopo ofisi za RITA Dodoma.

Sikuweza kuthibitisha nakala 50 za vyeti vya ndoa zenye thamani ya Sh. 2,500,000 na vitabu vya ndoa 16 vyenye thamani ya Sh 12,380,000 vilivyotolewa kwa Msajili wa wilaya ya Dodoma kuanzia mwezi Januari 2018 hadi Aprili 2020. Ni maoni yangu kuwa, RITA haikupitia kwa umakini mfumo wa usajili wa Mozilla ili kubaini udhaifu wake ambao mfumo mpya haukutatua. Hii imesababisha Serikali kukosa mapato ya jumla ya Sh. 116,460,550.

**Ninapendekeza hatua stahili za kinadhamu dhidi ya wahusika wote waliofanya ubadhirifu wa mapato ya Serikali. Pia, ninapendekeza adhabu kali zitolewe kwa wale waliohusika na ununuzi wa mfumo wa usajili (CRS) usiojitosheleza.**

### 13.2.9 Ukaguzi Maalumu Kuhusiana na Tuhuma za Ubadhirifu wa Kodi ya Zuio Iliyokusanywa na Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA)

Ukaguzi wangu ulilenga kuthibitisha iwapo tuhuma kuhusiana na Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA) kushindwa kuwasilisha makusanyo ya Kodi ya Zuio ya jumla ya Sh. 780,000,000 zilizokusanywa kutoka kwenye malipo ya wazabuni na makandarasi kwenda kwa Kamishna wa Kodi za Ndani, pamoja na kubainisha hasara iliyopatikana na wahusika wa ubadhirifu huo.  Masuala yafuatayo yalibainika wakati wa ukaguzi wangu

#### 13.2.9.1 Kodi za Zuio Zilizokokotolewa Kimakosa - Sh. 11,217,209.93

Kuanzia mwezi Julai 2015 hadi Juni 2020, nilibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) iliingia mikataba 193 na makandarasi, Wahandisi Washauri na watoa huduma mbalimbali kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa bidhaa na huduma zenye jumla ya Sh. 557,497,940,683.73 na Dola za Marekani 11,603,900.75. Ukaguzi wa mfumo wa Kihasibu wa Epicor ulibaini kuwa kodi ya zuio ya jumla ya Sh. 1,069,249,601.13 ilikusanywa kutoka kwenye malipo ya jumla ya Sh.39, 153,601,041.62 yaliyolipwa na Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA) kupitia hati za malipo 380 kuanzia mwezi Julai 2015 hadi Juni 2020 kwa ununuzi wa bidhaa, huduma na ujenzi kwa kiwango cha asilimia 2, 5 na 10.

Pia, nilibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA) ilikokotoa kiusahihi kodi ya zuio kwenye hati 356 zenye thamani ya Sh. 35,525,406.97 kati hati za malipo 380 zilizolipwa. Kadhalika, TEMESA ilikokotoa kimakosa kodi ya zuio katika hati za malipo 24 zenye thamani ya Sh.3,916,075,634.64 kama ifutavyo: Hati za malipo 14 zenye thamani ya Sh.1,259,868,733.11 ambazo kodi ya zuio iliyokokotolewa ni Sh. 44,539,299.87 badala ya Sh. 41,820,009.74. Hivyo, kusababisha malipo ya ziada ya Sh. 2,719,290.13 yaliyofanywa na TEMESA. Pia, hati za malipo 10 zenye thamani ya Sh. 2,656,206,901.54 ambazo Kodi ya zuio iliyokokotolewa kimakosa ilikuwa Sh. 56,119,909.59 badala ya Sh. 64,617,829.39. Hivyo, kusababisha kodi ya zuio kulipwa pungufu kwa Sh. 8,497,919.80.

#### 13.2.9.2 Hasara Iliyopatikana kwa Kodi za Zuio Kughushiwa na Wafanyakazi wa TEMESA na wa benki ya Kibiashara Sh. 709,152,607.07

Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA) ilipeleka hundi 429 zilizofungwa zenye thamani ya Sh. 1,894,988,144.28 kwa ajili ya malipo mbalimbali kwenye mojawapo ya benki ya kibiashara. Kati ya hundi zilizowasilishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA), hundi za jumla ya Sh. 1,069,249,601.13 zilikuwa ni kwa ajili ya malipo ya kodi ya zuio kwenda kwa Kamishna wa Kodi za Ndani. Wakati wa ukaguzi, Benki hiyo iliwasilisha hundi 368 za TEMESA zenye jumla ya Sh. 1,746,186,740.42 kati ya Hundi 429 zilizoombwa wakati wa ukaguzi. Benki hiyo haikuwasilisha Hundi 61 zenye thamani ya Sh.148,801,403.86 kwa kuwa ilishindwa kuzipata.

Baada ya kuzipitia Hundi zilizowasilishwa, nilibaini kuwa hundi 142 zilizofungwa zenye thamani ya Sh. 709,152,607.07 kati ya 368 zilizowasilishwa kwa ajili ya Kumlipa Kamishna wa kodi za Ndani zilibadilishwa na kuwa Hundi za wazi na kulipwa kama fedha taslimu Sh. 585,531,414.53 kwa Mtunza fedha wa TEMESA, na Sh. 61,898,037.46 zililipwa kwa Kampuni mbili na Sh. 61,632,155.08 zililipwa kwa watu wengine watatu.

TEMESA ilithibitisha kuwa haikuwa na mahusiano yoyote ya kibiashara na kampuni tajwa pamoja na watu waliolipwa. Katika uchunguzi wangu, nilibaini kuwa ubadhirifu huu ulifanywa kwa ushirikiano mkubwa baina ya wafanyakazi wa benki hiyo na baadhi ya maafisa wa Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA). Mtunza fedha wa TEMESA hakuandaa namba za utambuzi wa malipo ya kodi ili kutambua malipo ya kodi za zuio. Mtunza fedha wa TEMESA alikuwa akighushi saini za watoa fedha, na benki hiyo ilikuwa haifanyi uhakiki wa saini ili kuthibitisha uhalisi wa saini za waidhinishaji wa TEMESA waliopo kwenye taarifa za benki. Katika mahojiano, maafisa wa benki hiyo walieleza kuwa walikuwa wakiwasiliana na mojawapo wa watia saini aliyethibitisha kuwa Mtunza fedha huyo aliruhusiwa kuchukua fedha taslimu kwa kutumia Hundi zilizofungwa.

Ukweli huu unapingana na taratibu za kibenki kwa kuwa sio rahisi kwa hundi zilizofungwa kulipwa fedha taslimu bila ya ufuatiliaji wa kina au uwasilishaji wa hundi mpya zilizokuwa wazi zinazoweza kuchukua fedha taslimu. Kwa kuwa maafisa wa Benki hiyo walifahamu kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikuwa ikipokea malipo ya kodi ya zuio kwa kutumia namba za utambuzi za malipo ya kodi, ni dhahiri kuwa kitendo cha mtunza fedha kuweza kulipa kodi ya zuio kwa fedha taslimu kiliiashiria benki hiyo kuwa kulikuwa na ishara za wizi, na wangeweza kuwasiliana na mteja wao, TEMESA.  Kwa ukweli huo, ni dhahiri kuwa mifumo ya udhibiti ya ndani ya benki hiyo ilikuwa dhaifu, hivyo, kusababisha ubadhirifu wa kodi za zuio, jumla ya Sh. 709,152,607.07, uliofanywa na Mtunza fedha wa TEMESA.

### 13.2.9.3 Kodi za Zuio Zilizokusanywa na TEMESA na Kutowasilishwa TRA - Sh. 866,160,442.04

Nilibaini kuwa zaidi ya Sh. 709,152,607.07 zilizokusanywa TEMESA kama kodi ya zuio na kuchukuliwa, kinyume na utaratibu na Mtunza fedha TEMESA. Pia, wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa hundi 57 kwa ajili ya malipo ya kodi ya zuio kwa Kamishna wa Kodi za Ndani zenye thamani ya Sh.164,107,502.97 kutoka kwa Wakala wa Ufundi na Umeme Serikalini (TEMESA) hazikuwasilishwa kwa Benki hiyo kwa ajili ya malipo. Kati ya Hundi hizo, TEMESA iliwasilisha hundi nne tu kwa ajili ya ukaguzi na hundi 53 zilizobaki zenye thamani ya Sh. 155,182,550.45 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Kati ya hundi nne zilizowasilishwa, TEMESA ililipa hundi moja ya Sh. 7,099,668 mwezi Julai 2020.

Hivyo, ninathibitisha kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) haikupokea malipo ya kodi ya zuio ya jumla ya Sh. 866,160,442.04 kati ya kiasi cha Sh. 709,512,607.07 kilichochukuliwa na Mtunza fedha wa TEMESA, na Hundi 53 zenye thamani ya Sh. 157,007,834.97 zilizoandaliwa na TEMESA na hazikuwasilishwa kwenye benki hiyo.

Ni maoni yangu kuwa, mifumo ya udhibiti ya ndani ya benki hiyo ilishindwa kubaini saini zilizoghushiwa na kuruhusu hundi zilizofungwa kufunguliwa na kulipwa fedha taslimu. Pia, mifumo ya udhibiti wa ndani ndani ya TEMESA, ikijumuisha ukosefu wa ueledi kwenye kuandaa taarifa za usuluhishi wa kibenki na kutokuwapo kwa mgawanyo wa majukumu, ndiyo chanzo kikubwa cha ubadhirifu huu.

**Ninapendekeza kiasi cha Sh. 709,512,607.07 kirejeshwe kutoka kwa wahusika waliotajwa, na hatua stahili za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao. Pia, ninashauri mifumo ya udhibiti wa ndani iliyopo TEMESA iboreshwe, ikiwamo mgawanyo wa majukumu na mzunguko wa majukumu ya kazi.**

### 13.2.10 Ukaguzi Maalumu wa Fedha za Ruzuku na Mali za Chama cha NCCR-Mageuzi

Ofisi yangu ilifanya ukaguzi maalumu katika chama cha NCCR-Mageuzi ili kuthibitisha tuhuma kwamba, mali za Chama cha NCCR-mageuzi zilizonunuliwa kwa fedha za ruzuku ziliuzwa bila ya kufuata taratibu za Chama na kuthibitisha iwapo mojawapo wa viongozi wa Chama alijipatia mali za Chama bila kufuata sheria. Katika ukaguzi wangu, nilibaini masuala yafuatayo:

#### 13.2.10.1 Mapungufu yanayohusu usimamizi wa mapato Sh. 567,630,501.31

Kati ya mwezi Julai 2012 na Juni 2019, Chama cha NCCR-Mageuzi kilikusanya mapato ya jumla ya Sh. 1,147,320,438.97, kati ya kiasi hicho Sh. 635,718,509.27 zilipokelewa kutoka Serikalini kutokana na uwakilishi wa madiwani na wabunge. Msajili wa Vyama vya Siasa alithibitisha kukipelekea chama cha NCCR-Mageuzi ruzuku ya Sh. 405,199,515.96 katika kipindi tajwa. Hata hivyo, Msajili wa Vyama vya Siasa hakuweza kuthibitisha kupeleka ruzuku ya Sh. 230,518,993.31 kwa Chama cha NCCR-Mageuzi.

Taarifa zilizowasilishwa na Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusiana na fedha ilizozituma kwenda chama cha NCCR-Mageuzi zilikuwa na makosa, ikiwemo marudio na kusahulika kwa tarakimu. Pia, nilibaini kuwapo kwa mapato yenye jumla ya Sh. 326,411,508 yaliyokusanywa na Chama cha NCCR-Mageuzi kutoka vyanzo mbalimbali lakini hayakupelekwa benki, kinyume na Kifungu Na. 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019; na mapato ya jumla ya Sh.10,700,000 ambayo hayakuwa na stakabadhi.

**Ninapendekeza chama cha NCCR-Mageuzi kutoa stakabadhi na kuweka benki makusanyo yake yote. Pia, ninashauri Msajili wa Vyama vya Siasa kutunza taarifa za ruzuku zinazotolewa kwenye vyama vya Siasa na kufanya uhakiki mara kwa mara.**

#### 13.2.10.2 Mapungufu kwenye Usimamizi wa Mali za Chama

Nilipitia rejista za mali pamoja na tamko la mali lilowasilishwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa tarehe 02 Machi 2018 na kubaini kuwa, viwanja vitatu vinavyomilikiwa na Chama cha NCCR-Mageuzi ambavyo taarifa zake kwenye Ofisi za Ardhi zinaonesha majina ya watu binafsi na havina Hatimiliki. Pia, nilibaini viwanja saba ambavyo Baraza la Wadhamini la Chama cha NCCR-Mageuzi halikuwa na taarifa zake, na kwa sasa Chama cha NCCR-Mageuzi kimepoteza haki ya umiliki. Nilibaini samani za Ofisini zilizotolewa na Mwenyekiti wa Chama ambazo taarifa zake hazipo kwenye rejista ya mali za Chama.

Kadhalika, nilibaini nyumba mbili zilizopo Bunju B - Kinondoni, viwanja vilivyopo Zanzibar na Kigoma vilivyonunuliwa na Chama cha NCCR-Mageuzi kati ya mwaka 2002 hadi 2015 ambavyo taarifa zake hazikuwahi kuingizwa kwenye rejista ya mali za Chama. Pia, nilibaini kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi hakikuwahi kuwasilisha matamko ya mali za Chama kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuanzia mwaka 1992/93 hadi 2015/16, kinyume na Kifungu Na. 14(1)(a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019.

**Kutokana na mapungufu yaliyoelezwa hapo juu, ninapendekeza Chama cha NCCR-Mageuzi kutambua mali zote inazomiliki na kutunza taarifa zilizohuishwa na kuwasilisha matamko ya mali kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kulingana na Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 iliyorejewa mwaka 2019.**

#### 13.2.10.3 Bakaa na Marejesho ya Mkopo Bila ya Ushahidi wa Utoaji Sh. 190,925,500

Nilipitia vitabu vya mapokezi ya mapato na kubaini kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi kilipokea mikopo yenye jumla ya Sh. 255,925,500 kutoka kwa wanachama wanne na taasisi moja. Kwenye mikopo hiyo, nilibaini kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi kilipokea mikopo ya jumla ya Sh. 65,000,000 kutoka kwa mwanachama mmoja kupitia akaunti za benki za chama, ambapo mikopo ya jumla ya Sh. 190,925,500 ilipokelewa kwa fedha taslimu. Pia, Chama cha NCCR-Mageuzi hakikuwasilisha rejista ya mikopo, mikataba, na mihtasari ya vikao vya Kamati Kuu iliyopitisha kupokelewa kwa mikopo hiyo.

Kwa kuwa hakuna rejista wala mikataba, ukaguzi wangu ulishindwa kuthibitisha iwapo Chama cha NCCR-Mageuzi kilitumia jumla ya mikopo ya Sh.190,925,500 iliyopokelewa kama fedha taslimu kwa shughuli za chama. Pia, nilibaini kuwa mojawapo wa wakopeshaji mwenye mkataba alidai kukikopesha chama Sh.170,000,000, ingawa taarifa zilizopo kwenye Chama zinaonesha kuwa fedha iliyopokelewa ni Sh. 153,940,000 tu. Hakukuwa na ushahidi unaoonesha bakaa ya Sh.16,060,000 kupokelewa na Chama.

Pia, nilibaini kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi kilipokea Sh. 65,000,000 kupitia akaunti za benki na Sh. 88,940,000 ilipokelewa fedha taslimu. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi ulioonesha kuwa mikopo iliyotolewa fedha taslimu ilipokelewa na kutumiwa na Chama licha ya kuelezwa na mkopeshaji. Pia, nilibaini kuwa chama cha NCCR-Mageuzi kilirejesha Sh. 86,000,000 kwa mkopeshaji licha ya kupokea Sh.65,000,000. Hivyo, mkopeshaji alipokea kwa udanganyifu malipo ya Sh. 21,000,000 na mkopo ambao hakuutoa kwenye Chama.

Kadhalika, nilibaini marejesho ya jumla ya Sh. 45,637,500 kwa wanachama watatu na Sh. 4,500,000 kwenda kwenye Taasisi moja ambayo Chama cha NCCR-Mageuzi hakikuwasilisha mikataba wala mihtasari ya vikao vya Kamati Kuu iliyoidhinisha mikopo tajwa kurejeshwa.

**Hivyo, ninapendekeza Chama cha NCCR-Mageuzi kuchukua hatua stahili kuhakikisha Sh. 21,000,000 na Sh. 45,637,500 zinarejeshwa kwa mkopeshaji na wanachama waliotajwa.**

#### 13.2.10.4 Mapungufu Yaliyoibuliwa kwenye Uuzaji wa Nyumba ya Tarime

Chama cha NCCR-Mageuzi kilinunua nyumba iliyopo Wilaya ya Tarime katika Kiwanja Na. 196 Kitalu M mtaa wa Sabasaba tarehe 26 Juni 2000 kutoka kwa mfanyabiashara maarufu kwa Sh. 5,000,000. Mwezi Julai 2016, aliyekuwa Katibu Mkuu alianzisha mchakato wa mauzo ya nyumba hiyo, ambayo iliuzwa tarehe 29 Desemba 2016 kwa Sh. 55,000,000. Nilibaini kuwa aliyekuwa Katibu Mkuu alifuata taratibu ambazo hazikubainishwa kwenye Kanuni na Sera za fedha za Chama cha NCCR-Mageuzi za mwaka 2015 lakini mauzo hayo yalifanyika kwa utaratibu ulio na udhibiti bora.

Pia, nilibaini kuwa aliyekuwa Katibu Mkuu aliuza nyumba hiyo bila kupata idhini ya Baraza la Wadhamini la Chama. Pia, Chama cha NCCR-Mageuzi

hakikuomba kibali kutoka kwa Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali cha uuzaji wa nyumba hiyo, kinyume na Kifungu Na. 9 cha Sheria ya Usajili wa Udhamini Sura ya 318.

Kupitia mahojiano, nilibaini kuwa mnunuzi alilipa fedha taslimu Sh. 65,000,000 kwa aliyekuwa katibu Mkuu kama bei ya ununuzi wa nyumba. Kati ya fedha hizo, Katibu Mkuu aliweka Sh. 50,000,000 kwenye akaunti za benki za Chama na kutumia Sh. 5,000,000 kwa ajili ya kurejesha kodi za pango na gharama zingine za uwakala, ambazo zilijumuishwa kwenye bei ya kuuzia iliyopo kwenye mkataba. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka za matumizi ya Sh. 10,000,000 zilizodaiwa kutumiwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wakati wa uuzaji wa nyumba hiyo; hivyo, nilishindwa kuthibitisha matumizi ya fedha hizo. Pia, Chama cha NCCR –Mageuzi hakikulipa Kodi ya ongezeko la mtaji ya Sh. 5,000,000 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenye mauzo yaliyopatikana kutokana na uuzaji wa nyumba hiyo, kinyume na Kifungu Na. 39 cha Sheria ya Mapato ya Kodi ya mwaka 2004 (iliyorejewa mwaka 2008).

**Kuhusiana na hili, ninapendekeza kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi kichukuwe hatua stahili za Kisheria dhidi ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama ili arejesha kiasi cha Sh. 10,000,000 alichokichukua kinyume na utaratibu. Mamlaka ya Mapato Tanzania ihakikishe inadai Chama cha NCCR-Mageuzi kodi ya ongezeko la thamani.**

### 13.2.10.5 Nyumba Inayodaiwa Kuwa ni ya Chama Inamilikiwa na Kiongozi wa Chama Kinyume na Utaratibu

Tarehe 19 Mei 2002, Baraza la Wadhamini la Chama cha NCCR-Mageuzi lilinunua nyumba mbili zilizopo Bunju, Dar es Salaam kwa Sh. 2,900,000 na kulipa kodi ya jengo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni tarehe 06 Agosti 2007. Katika mahojiano, kiongozi mmoja wa Chama alidai kununua nyumba hizo kwa kutumia fedha zake binafsi na kukipa Chama cha NCCR-Mageuzi kama msaada. Pia, alieleza kuwa Baraza la Wadhamini la Chama cha NCCR-Mageuzi lilishindwa kusimamia nyumba hizo, hivyo vikao vya Kamati Kuu vilipitisha maazimio kuwa nyumba hizo kurejeshwa kwake. Hata hivyo, Kiongozi huyo hakuwasilisha ushahidi kuthibitisha ukweli huo. Pia, Chama cha NCCR-Mageuzi hakikuwasilisha mihtasari ya vikao vya Kamati Kuu wala Baraza la Wadhamini vilivyopitisha kuwa nyumba hizo kurejeshwa kwa Kiongozo huyo.

Pia, nilibaini kuwa Kiongozi huyo aligawa nyumba hizo kwa rafiki yake ambaye ukaguzi ulishindwa kutambua anuani yake. Kwa kuwa nyumba husika zilikuwa kwenye eneo lisilopimwa, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni haikuweza kumtambua mmiliki wa sasa wa nyumba hizo kwa kuwa taarifa za umiliki wake hazikuwamo kwenye Kanzidata yao. Maelezo yaliyotolewa hapo juu, ni dhahiri kuwa Kiongozi huyo alijimilikisha nyumba za Chama kwa manufaa binafsi.

**Katika muktadha huu, ninapendekeza Chama cha NCCR-Mageuzi kuchukua hatua stahili dhidi ya Kiongozi huyo na nyumba tajwa zirejeshwe kwenye Chama cha NCCR-Mageuzi.**

### 13.2.10.6 Mgogoro wa Umiliki wa Shamba la hekari 56 lililopo Kijiji cha Kiromo, Bagamoyo

Nilipitia rejista za mali za Chama na kuwaomba Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali na Msajili wa Vyama vya Siasa kuthibitisha umiliki wa Shamba la hekari 56 lililopo Kijiji cha Kiromo, Bagamoyo linalodaiwa kumilikiwa na Chama cha NCCR-Mageuzi. Msajili wa Vyama vya Siasa na Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali walikiri kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi hakikuwahi kutoa taarifa zozote za umiliki wa shamba hilo. Pia, Chama cha NCCR-Mageuzi hakina taarifa zozote zinazohusiana na Shamba hilo.

Hata hivyo, tarehe 27 Desemba 2011, Mwenyekiti wa kijiji cha Kiromo aliandika barua isiyokuwa na anuani na kuthibitisha umiliki wa Shamba hilo kwa mojawapo wa viongozi wa Chama. Pia, nilibaini kuwa kiongozi huyo aliuza heka 47 za Shamba hilo kwa mojawapo ya Kampuni kwa Sh. 164,500,000. Hata hivyo, Kiongozi huyo hakuwasilisha taarifa yoyote yenye ushahidi wa umiliki wa Shamba hilo. Katika muktadha huo, ni dhahiri kuwa kiongozi huyo hamiliki Shamba hilo. Ukweli uliolezwa hapo juu ni ushahidi tosha kuwa Chama cha NCCR-Mageuzi wala Kiongozi huyo hawamiliki shamba tajwa.

**Ninapendekeza Vyombo vya Uchunguzi kuanzisha uchunguzi ili kuthibitisha kuwapo kwa jinai kwenye uuzaji wa Shamba hilo. Kisha, hatua stahili za kisheria zichukuliwe kwa Kiongozi huyo.**

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho Na. I: Orodha ya Hati za Ukaguzi Zilizotolewa

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tume ya Huduma za Walimu | 2 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka |
| 2 | Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi | 3 | Hati Inayoridhisha | Hati Mbaya | Hati Yenye Shaka |
| 3 | Ofisi ya Rais – Idara ya Usimamizi wa Nyaraka na Kumbukumbu | 4 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 4 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 5 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 5 | Msajili wa Hazina | 7 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha |
| 6 | Ofisi ya Rais – Bodi ya Mishahara ya Watumishi wa Umma | 9 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 7 | Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC) | 10 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 8 | Tume ya Huduma za Mahakama | 12 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 9 | Kitengo cha Uchunguzi wa Fedha | 13 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 10 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | 14 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Msisitizo | | |
| 11 | Tume ya Usuluhishi na Maridhiano | 15 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 12 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 16 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 13 | Tume ya UNESCO | 18 | Hati Mbaya | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa |
| 14 | Wakili Mkuu wa Serikali | 19 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Haikuwapo |
| 15 | Ofisi ya Rais – Ikulu | 20 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 16 | Idara ya Hazina | 21 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 17 | Idara ya Deni la Taifa na Huduma za Jumla | 22 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka |
| 18 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 23 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 19 | Tume ya Maendeleo na Ushirika | 24 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 20 | Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 25 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 21 | Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais | 26 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 22 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 27 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 23 | Idara ya Jeshi la Polisi | 28 | Hati Inayoridhisha | Hati | Hati |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 24 | Idara ya Huduma za Magereza | 29 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 25 | Ofisi ya Rais – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 30 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 26 | Ofisi ya Makamu wa Rais | 31 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 27 | Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 32 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 28 | Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Umma | 33 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 29 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | 34 | - | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha |
| 30 | Huduma ya Taifa ya Mashtaka (NPS) | 35 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha |
| 31 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 37 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 32 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania (TPDF) | 38 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 33 | Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) | 39 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 34 | Mahakama ya Tanzania | 40 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 35 | Wizara ya Katiba na Sheria | 41 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 36 | Bunge la Tanzania | 42 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 37 | Wizara ya Kilimo | 43 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 38 | Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (Fungu Na. 44) | 44 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 39 | Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi | 46 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 40 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 48 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 41 | Wizara ya Maji | 49 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 42 | Wizara ya Fedha na Mipango | 50 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 43 | Wizara ya mambo ya Ndani | 51 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 44 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) | 52 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 45 | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 53) | 53 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 46 | Tume ya Haki za Binadam na Utawala Bora | 55 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 47 | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 56 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 48 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 57 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Msisitizo | Yenye Masuala ya Msisitizo | Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 49 | Wizara ya Nishati | 58 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 50 | Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 59 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 51 | Wizara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji (Fungu Na. 60) | 60 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 52 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) | 61 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 53 | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 62) | 62 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 54 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) | 64 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 55 | Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu | 65 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 56 | Ofisi ya Rais – Sekretarieti ya Ajira | 67 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 57 | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 68) | 68 | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha |
| 58 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 69 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 59 | Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya | 91 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 60 | Tume ya Kuzuia Ukimwi (TACAIDS) | 92 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 61 | Idara ya Huduma za uhamiaji | 93 | Hati Inayoridhisha | Hati | Hati Yenye |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Inayoridhisha | Shaka |
| 62 | Ofisi ya Rais- Tume ya Utumishi wa Umma | 94 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 63 | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | 96 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha |
| 64 | Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 98) | 98 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 65 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) | 99 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 66 | Wizara ya Madini | 100 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Haikuwapo |
| 67 | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | 36 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha |
| 68 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu | 47 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 69 | Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe | 54 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | 63 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 71 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 70 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala | Hati Inayoridhisha |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ya Msisitizo | |
| 72 | Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani | 71 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 73 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | 72 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 74 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | 73 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma | 74 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 76 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 75 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 77 | Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi | 76 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha |
| 78 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mara | 77 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 79 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya | 78 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 80 | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | 79 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | 80 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 82 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | 81 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 83 | Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma | 82 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 84 | Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga | 83 | Hati Inayoridhisha | Hati | Hati |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 85 | Sekretarieti ya Mkoa wa Singida | 84 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 86 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora | 85 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 87 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | 86 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 88 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | 87 | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 89 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam | 88 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 90 | Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa | 89 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha |
| 91 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | 90 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 92 | Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara | 95 | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha |
| 93 | Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu (ADEM) | Wakala | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa |
| 94 | Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 95 | Wakala wa Usajili na Utoaji wa Leseni za Biashara | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye | Hati |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | (BRELA) | | | Shaka | Inayoridhisha |
| 96 | Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) | Wakala | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 97 | Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa (DDCA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 98 | Mamlaka wa Mtandao wa Serikali (e-GA) | Mamlaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 99 | Kituo cha Mafunzo ya Takwimu Mashariki mwa Afrika | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 100 | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo (FETA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 101 | Wakala wa Utafiti wa Miamba Tanzania (GST) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 102 | Wakala wa Maabara za Serikali | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 103 | Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini (GPSA) | Wakala | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 104 | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo (LITA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 105 | Chuo cha Taifa cha Utalii | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 106 | Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa |
| 107 | Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) | Wakala | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 108 | Wakala wa Afya na Usalama Sehemu za Kazi (OSHA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 109 | Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 110 | Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 111 | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Haikuwapo | Haikuwapo |
| 112 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSuBa) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka |
| 113 | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 114 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 115 | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi Tanzania (TEMESA) | Wakala | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 116 | Wakala wa Huduma za Misutu Tanzania (TFSA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 117 | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa (TaGLA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 118 | Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 119 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | Wakala | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 120 | Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa (TMA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 121 | Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati | Hati |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 122 | Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 123 | Wakala wa Maabara za Mifugo Tanzania (TVLA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 124 | Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 125 | Chuo cha maji | Wakala | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 126 | Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) | Wakala | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 127 | Mfuko wa Mikopo ya Wafanyakazi Hazina | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 128 | Mfuko wa Udhamini wa pembejeo za kilimo (AGITF) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 129 | Mfuko wa Uwezeshaji Maendeleo ya Madini (EMDF) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 130 | Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Ushirika (ISCF) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 131 | Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo(LDF) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 132 | Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (NFA) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 133 | Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Majanga | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 134 | Mfuko wa Taifa katika Sekta ya Maji (NWF) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati | Hati |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 135 | Mfuko wa Maendeleo ya Hatimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 136 | Mfuko wa Barabara (TAMISEMI) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 137 | Bodi ya Mfuko wa Barabara (Fungu Na. 98) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 138 | Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 139 | Mfuko wa Kulinda Wanyamapori Tanzania (TWPF) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 140 | Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) | Mfuko | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 141 | Bodi ya Bonde la Maji la Ndani | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 142 | Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Nyasa | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 143 | Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Rukwa | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 144 | Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Tanganyika | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 145 | Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Viktoria | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 146 | Bodi ya Bonde la Maji, Pangani | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 147 | Bodi ya Bonde la Maji, Rufiji | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 148 | Bodi ya Bonde la Maji, Ruvuma na Pwani ya Kusini | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 149 | Bodi ya Bonde la Maji, Wami/Ruvu | Bodi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 150 | Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Taka Handeni | Mamlaka ya Maji | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 151 | Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Taka Mafinga | Mamlaka ya Maji | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa | Haikukaguliwa |
| 152 | Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Taka Makonde | Mamlaka ya Maji | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 153 | Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Taka Maswa | Mamlaka ya Maji | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 154 | Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Taka Mugango/Kiabakari/Butiama | Mamlaka ya Maji | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 155 | Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Taka Wanging'ombe | Mamlaka ya Maji | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 156 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 157 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bombo-Tanga | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 158 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye | Ilikaguliwa Chini |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Shaka | ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 159 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Dodoma | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 160 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Geita | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 161 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Iringa | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 162 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Katavi | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 163 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Kitete Tabora | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 164 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Ligula-Mtwara | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 165 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Manyara | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 166 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Maweni-Kigoma | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 167 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mawenzi-Kilimanjaro | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 168 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mbeya | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 169 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Morogoro | RRH | Hati Mbaya | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 170 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mount Meru | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 171 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Musoma | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 172 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mwananyamala | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 173 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Njombe | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 174 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sekou-Toure Mwanza | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 175 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Shinyanga | RRH | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 176 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Simiyu | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 177 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Singida | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ya Mkoa |
| 178 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sokoine-Lindi | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 179 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songea Ruvuma | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 180 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songwe | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 181 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sumbawanga Rukwa | RRH | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 182 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Temeke | RRH | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 183 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tumbi- Kibaha | RRH | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya Sekretarieti ya Mkoa |
| 184 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Mbeya | ZRH | Hati Inayoridhisha | Ilikaguliwa Chini ya MOHCDGEC (Vote 52) | Ilikaguliwa Chini ya MOHCDGEC (Vote 52) |
| 185 | Hospitali Maalumu ya Benjamin Mkapa | SH | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa | Haikukaguliwa |
| 186 | Hospitali Maalumu ya Magonjwa ya Kuambukiza Kibong'oto | SH | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa | Haikukaguliwa |
| 187 | Hospitali maalumu ya Mirembe Hospital & Isanga Institution | SH | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa | Haikukaguliwa |
| 188 | ACT WAZALENDO | PP | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 189 | African Democratic Alliance (ADA-TADEA) | PP | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni |
| 190 | Alliance For African Farmers Party (AAFP) | PP | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni |
| 191 | Alliance for Democratic Change (ADC) | PP | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni | Hati Inayoridhisha |
| 192 | Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) | PP | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka |
| 193 | Chama Cha Kijamii (CCK) | PP | Hati Yenye Shaka | Hati Yenye Shaka | Hati Yenye Shaka |
| 194 | Chama Cha Mapinduzi(CCM) | PP | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha |
| 195 | Chama cha Sauti ya Umma (SAU) | PP | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni |
| 196 | Chama Cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) | PP | - | Kushindwa kutoa Maoni | Hati Mbaya |
| 197 | Civic United Front (CUF) | PP | Hati Yenye Shaka | Hati Mbaya | Hakikukaguliwa |
| 198 | Demokrasia Makini | PP | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni |
| 199 | Democratic Party (DP) | PP | - | Kushindwa kutoa Maoni | Hati Inayoridhisha |
| 200 | National League for Democracy (NLD) | PP | Hati Yenye Shaka | Hati Mbaya | Hati Mbaya |
| 201 | National Reconstruction Alliance (NRA) | PP | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni |
| 202 | NCCR- MAGEUZI | PP | Hati Inayoridhisha | Hati Mbaya | Hati Yenye Shaka |
| 203 | Tanzania Labour Party (TLP) | PP | Kushindwa kutoa | Kushindwa | Kushindwa |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Maoni | kutoa Maoni | kutoa Maoni |
| 204 | Union for Multi-Party Democracy (UMD) | PP | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni |
| 205 | United Democratic Party (UDP) | PP | Hati Yenye Shaka | Kushindwa kutoa Maoni | Hati Inayoridhisha |
| 206 | United Peoples' Democratic Party (UPDP) | PP | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni | Kushindwa kutoa Maoni |
| 207 | Mpango wa Kujitathimini Kwa Nchi za Afrika (APRM) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 208 | Chuo cha Ardhi Morogoro | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Haikuwapo |
| 209 | Chuo cha Ardhi Tabora | TN | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa | Haikukaguliwa |
| 210 | Chuo cha Utunzaji Nyuki (BTI) | TN | Hati Inayoridhisha | Haikuwapo | Haikuwapo |
| 211 | Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) | TN | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa | Haikukaguliwa |
| 212 | Mamlaka ya Uvuvi Kina Kirefu | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 213 | Baraza la Afya ya Mazingira (EHPC) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha |
| 214 | Chuo cha Mafunzo ya viwanda vya misitu(FITI) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa |
| 215 | Chuo cha Mafunzo ya Misitu (FTI) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 216 | Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 217 | Chuo cha Usimamizi wa Mahakama (IJA) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 218 | Shule ya Sekondari Jitegemee | TN | Hati Inayoridhisha | Hati | Haikukaguliwa |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Inayoridhisha | |
| 219 | Shule ya Sekondari Kawawa JKT | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa |
| 220 | Chuo cha Sheria Tanzania | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 221 | Bodi ya mikopo serikali za mitaa (LGLB) | TN | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 222 | Chuo cha Mafunzo cha Serikali za Mitaa (HOMBOLO) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 223 | Baraza la Madawa Tanganyika (MCT) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 224 | Baraza la Wataalamu wa Mionzi na Picha (MRIPC) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 225 | Chuo cha Rasilimali Madini (MRI) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 226 | Tume ya Madini | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Haikukaguliwa |
| 227 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki-Idara ya Zanzibar (SV 1003) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 228 | Shirika la Mzinga | TN | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha |
| 229 | Kampuni Hodhi ya Mzinga | TN | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizos |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 230 | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 231 | Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela Afrika (NM-AIST) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 232 | Baraza la Wataalamu wa Macho | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 233 | Chuo cha Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi (PWTI) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 234 | Baraza la Famasia | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 235 | Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 236 | Bodi ya Maabara Binafsi ya Afya | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 237 | Bodi ya Ushauri Hospitali Binafsi | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 238 | Mkakati wa Kukuza na Kuratibu Biashara Tanzania (MKURABITA) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 239 | Mfuko na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 240 | SUMA JKT - Idara ya Zana za Kilimo | TN | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 241 | SUMA JKT – Idara ya Ulinzi | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 242 | SUMA JKT HQ - Shirika la Uzalishaji mali | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 243 | SUMA JKT - Hesabu Jumuifu | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 244 | SUMA JKT- Idara ya Kilimo na Viwanda | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 245 | SUMA JKT -Idara ya Ujenzi | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 246 | Taasisi ya utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) | TN | Hati Inayoridhisha | Haikuwapo | Haikuwapo |
| 247 | Shirika la Nyumbu (TATC) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 248 | Bpdi ya Filamu Tanzania (TFB) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 249 | Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Haikuwapo |
| 250 | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 251 | Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 252 | Taasisi ya Uthibitisho wa Mbegu- Tanzania (TOSCI) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 253 | Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi (TPFCS) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Haikukaguliwa |
| 254 | Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo |
| 255 | Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha |
| 256 | Bodi ya Usajili wa Mpango Mji | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

| Na | Taasisi | Fungu/ Aina | 2019/20 | 2018/19 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 257 | Baraza la Wataalamu wa Tiba Asilia na Tiba mbadala za Afya (TAHPC) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 258 | Chuo cha Uongozi | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 259 | Baraza la Wataalamu wa Mifugo Tanzania (VCT) | TN | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 260 | Hesabu Jumuifu za Taifa | MM | Hati Inayoridhisha | Hati Yenye Shaka | Hati Inayoridhisha |
| 261 | Mfuko Mkuu wa Hazina | MM | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 262 | TRA - Matumizi | TRA | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 263 | TRA - Mapato | TRA | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

## Kiambatisho Na. II: Taasisi Zilizopata Hati Zenye Shaka

### 1. Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu (ADEM)

- **Kutokukokotolewa kwa uchakavu kwa Vitabu vyenye Thamani ya Sh. 5,384,360**

Kinyume na aya ya 59 ya IPSAS 17, Vitabu vyenye thamani ya Sh. 5,384,360 vimewekwa kwa thamani yake halisi ya awali chini ya kifungu cha Mali, Mitambo na Vifaa bila kushuka kwa thamani. Hivyo, imepelekea gharama za uchakavu kuwa pungufu na kuongezeka kwa thamani ya mali hizo kama ilivyooneshwa katika Taarifa ya Mizania. Wakati huohuo, sikuweza kukokotoa kiasi cha uchakavu kwa sababu hakukuwa na kiwango cha kutumika kukokotoa uchakavu.

- **Dosari zilizojitokeza katika Taarifa ya Usuluhishi wa Mtiririko wa Fedha kutoka kwenye Shughuli za Uendeshaji hadi kwenye Nakisi,**
  Nilifanya usuluhishi na kubaini Dosari katika taarifa ya matumizi,mali na madeni kinyume na Waraka wa Mhasibu Mkuu wa Serikali wenye kumbukumbu Na. EG.3 / 102/05/03/009 wa tarehe 8 Mei 2020 juu ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa mwaka ulioisha tarehe 30 Juni 2020. Dosari hizo ni kama zifuatazo:

  a) Sikuweza kuhakiki Marekebisho ya mwaka uliopita yenye kiasi cha Sh. 55,067,742.98 yaliyojumlishwa katika nakisi. Hii ni kwa sababu hakukuwa na nukuu ya ufafanuzi ambayo ingetoa maelezo yake.
  b) Ongezeko la Madai na Malipo ya Kabla lenye jumla ya Sh. 17,099,640 liliripotiwa kwa ziada kimakosa kwa sababu lilijumlishwa badala ya kutolewa. Hali hiyo imepelekea kuongeza kimakosa mtiririko wa fedha taslimu unaotokana na shughuli za uendeshaji kwa Sh. 34,199,280 kwa sababu iliripotiwa Sh. 526,838,895.15 badala ya Sh. 492,639,615.15
  c) Gharama za Uchakavu zilizojumlishwa katika nakisi zilipunguzwa kimakosa kwa Sh. 4,744,489.35; gharama hizo zilijumlishwa Sh. 540,631,364.37 badala ya Sh. 545,375,853.72.

- Kinyume na IPSAS 19, taasisi imeonesha deni la kodi ya ardhi la Sh. 169,347,600 kama deni tarajiwa badala ya kuripoti kama deni halisi kwenye Taarifa ya Mizania.

### 2. United Democratic Party (UDP)

- Chama cha UDP kimeripoti madeni katika Taarifa ya Mizania ya Sh. 1,268,000 kufikia tarehe 30 Juni 2020 wakati kwa mwaka uliopita wa 2018/2019, madeni yalikuwa jumla Sh. 2,155,994. Hata hivyo, ukaguzi haukuweza kupata nyaraka kama ankara, vocha za malipo wala orodha ya wazabuni waliolipwa kiasi cha Sh. 887,994.

- Bakaa ya fedha taslimu na fedha linganishi iliyoripotiwa ni Sh. 203,932. Hata

hivyo, taarifa ya usuluhishi ya kibenki haikuwasilishwa wakati wa ukaguzi kwa ajili ya kupata uhakika wa bakaa iliyoripotiwa, wakati taarifa ya benki inaonyesha bakaa ya Sh. 100 tu hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020. Pia, Uongozi wa Chama ulieleza kuwa haukuwa na fedha taslimu kwa ajili ya matumizi madogo madogo kufikia tarehe 30 Juni 2020.

- Pia nilibaini kuwa, Chama hakina vitabu muhimu vya Uhasibu kama kitabu cha fedha, leja, kitabu cha safari, bajeti iliyoidhinishwa na rejesta ya vifaa.

- Nukuu za ufafanuzi zinazojumuisha muhtasari wa sera muhimu za uhasibu na maelezo mengine ya taarifa za fedha hazijawasilishwa kulingana na mahitaji ya aya 1.129 ya IPSAS

- Hakukuwa na usawa wa bakaa ya fedha katika Taarifa ya Mtiririko wa Fedha ikilinganishwa na bakaa iliyoonyeshwa katika Taarifa ya Mizania kufikia 30 Juni 2020, kinyume na IPSAS 2.56

**3. Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini (GPSA)**

- **Ziada iliyotokana na Mauzo ya vifaa Sh. 8,782,661,000 haikuripotiwa kwa usahihi katika Taarifa za Fedha**

Taarifa za Mauzo na manunuzi ya mafuta iliyotumika katika kuandaa hesabu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 hazikuwa sahihi. Hatimaye, ziada ya Sh. 8,782,661,000 iliyoripotiwa katika Taarifa ya utendaji (performance) haiwezi kuwa sahihi pia.

Ukaguzi haukuweza kubaini kiasi kilichokosewa kwa kuwa taarifa za mauzo na manunuzi hazikuwa zenye kuaminika.

- **Kutokuwa sahihi kwa Bakaa ya Wadaiwa katika Taarifa ya Mizania**

GPSA ilikuwa inadai jumla ya madai Sh. 3,661,256,000 kama ilivyoonekana katika taarifa za fedha. Tuliandika barua kwa wadaiwa 19 ili kuthibitisha madeni yao. Hata hivyo, kati ya hao ni wadaiwa wanne tu (yaani RAS Morogoro, NEC, OR-TAMISEMI na TANROADS) walijibu na wote hawakukubaliana na jumla ya deni la Sh. 2,114,131,893.09 lililoripotiwa na GPSA. Waliobaki 15 hawakujibu barua zetu.

**4. Chama Cha Kijamii (CCK)**

**Kutofanana kwa Kiasi kati ya hesabu na Nukuu zake za Ufafanuzi (notes) kwa Sh. 56,867,166**

Ukaguzi wangu wa hesabu ulibaini kwamba, kwa mujibu wa Taarifa ya utendaji (Perfomance) kiasi kilichoripotiwa cha Mapato na Matumizi ya kiutawala kilikuwa Sh. 44,081,166 na Sh. 51,434,000, mtawalia. Vivyo hivyo, kwa mujibu wa Taarifa ya Mizania jumla ya Sh. 38,934,000 iliripotiwa kama kiasi cha wanachama na mali

nyingine.

Kinyume chake, mapitio yangu ya Nukuu za Ufafanuzi kwa hesabu yalibaini kwamba mapato na Matumizi ya kiutawala yaliripotiwa kwa kiasi cha Sh. 15,437,166 na Sh. 5,018,834, mtawalia; wakati Sh. 57,126,000 iliripotiwa katika nukuu ya Ufafanuzi kama kiasi cha wanachama na mali nyingine. Matokeo yake, nimebaini dosari kubwa ya kiasi kilichoripotiwa kati ya hesabu na Nukuu za Ufafanuzi kwa Sh. 56,867,166

**5. Civic United Front (CUF)**

- **Kutothibitishwa kwa bakaa ya fedha taslimu na fedha linganishi kiasi cha Sh. 32,429,793**

Taarifa ya Mizania ya Chama ilionyesha bakaa ya fedha taslimu na fedha linganishi kiasi cha Sh. 690,991,274, Hata hivyo, kiasi hicho kimejumuisha bakaa ya benki Sh. 28,746,721 na bakaa taslimu Sh. 3,683,072 ambazo hazikuweza kuthibitishwa kutokana na kutokuwapo kwa nyaraka muhimu kama kitabu cha fedha, taarifa za miamala ya benki pamoja na usuluhishi wake na ripoti ya fedha taslimu kufikia tarehe 30 Juni 2020.

- **Kutokuwapo kwa Nukuu ya Ufafanuzi ya Usuluhishi wa Ziada**

Chama hakikuweza kuripoti usuluhishi wa ziada au nakisi kutoka katika shughuli za kawaida dhidi ya Mtiririko wa Fedha taslimu unaotokana na shughuli za Uendeshaji, kinyume na aya ya 2 ya IPSAS 2.

- **Kutoripotiwa kwa Deni la Sh. 2,500,000**

Chama kiliingia mkataba wa kununua magari yenye thamani ya jumla ya Sh. 18,000,000. Kiasi chote kilijumuishwa katika Jedwali la Mali, Mitambo na Vifaa. Hata hivyo, Chama kiliweza kulipia Sh. 15,500,000 na kubaki kinadaiwa Sh. 2,500,000. Kiasi hicho cha deni Sh. 2,500,000 hakikutambuliwa kama deni kwa Chama, hivyo madeni ya Chama kupungua kimakosa kwa kiasi hicho.

- **Mkopo wa Sh. 68,598,000 Uliopokelewa Haukuingizwa katika Akaunti ya Benki**

Kifungu Na. 15 (1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 iliyorekebishwa mwaka 2019 kinataka kila Chama cha Siasa kilichosajiliwa rasmi kupitia kwa wadhamini wake kumiliki akaunti ya benki ya chama; ambapo fedha zote zitakazopokelewa na chama zinapaswa kuhifadhiwa katika akaunti hiyo. Kinyume na sheria hiyo, mapitio yangu ya taarifa za miamala ya benki yalibaini mkopo wa Sh. 68,598,000 ulipokelewa kwa fedha taslimu kutoka kwa wanachamana na kutumika bila ya kuhifadhiwa katika akaunti ya benki ya chama. Pia, matumizi

hayo hayakutambulika katika hesabu. Hivyo, Taarifa ya utendaji ilikuwa na dosari kwa kiasi tajwa hapo juu.

**6. Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA)**

Madeni ya Wakala yamejumuisha Sh. 107,854,335.90 ambayo uongozi umeshindwa kuyathibitisha. Hii inamaanisha Uongozi umeripoti kimakosa madeni kwa ziada kwa kuyajumlisha madeni ambayo hayawezi kuthibitika. Hivyo, matumizi yalipaswa yapungue kwa Kiasi cha Sh. 107,854,335.90 na nakisi nayo ipungue kwa kiasi hicho.

Nyaraka (Vocha) za Malipo zenye jumla ya Sh. 99,273,908.39 hazikuwa na nyaraka toshelezi. Pia vocha ya malipo yenye kiasi cha Sh. 1,968,840 hazikuonekana. Hii inafanya jumla ya malipo ya Sh. 24,600,530,414.09 kutothibitika.

**7. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga**

- **Kiasi cha Mali, Mitambo na Vifaa kimeripotiwa kwa Zaidi ya Sh. 1,007,068,510.57**

Niliipitia Taarifa ya Mizania tarehe 30 Juni 2020 pamoja na nukuu za ufafanuzi na kubaini kiasi kilichoripotiwa cha Mali, Mitambo na Vifaa (PPE) katika Taarifa ya Mizania ni Sh. 9,251,700,328, wakati jedwali la Mali, Mitambo na Vifaa (katika ukurasa wa 36 wa hesabu) limeonyesha Mali hizo kwa thamani ya Sh. 8,244,631,817.43. Hivyo, kiasi kilichoripotiwa kimeongezeka kimakosa kwa Sh. 1,007,068,510.57.

- **Kushindwa Kutoa Maelezo kwenye Tofauti Kubwa Zilizojitokeza Kati ya Kiasi cha Bajeti na Kiasi Halisi.**

Uongozi ulishauriwa utoe maelezo hayo lakini hesabu iliyowasilishwa upya haikutoa maelezo kwenye tofauti kubwa zilizojitokeza kati ya kiasi cha bajeti na kiasi halisi, kinyume na aya ya 14 na 29 ya IPSAS 24.

- **Kushindwa kuelezea Uhalisia wa kosa la kipindi kilichopita**

Ilibainika kwamb,a katika Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji, uongozi ulifanya marekebisho kwenye Limbikizo la Ziada kwa kiasi cha Sh. 349,281,474. Hata hivyo, hakukuwa na nukuu ya ufafanuzi kwenye taarifa ya fedha inayoelezea uhalisia wa kosa hilo la kipindi kilichopit. Hii ni kinyume na aya ya 54 ya IPSAS 3, hivyo nimeshindwa kuthibitisha usahihi wa kiasi kilichoripotiwa.

- **Limbikizo la Ziada limeripotiwa kwa Upungufu**

Katika Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji kwa mwaka wa fedha 2018/19 na 2019/20

uongozi uliripoti bakaa ya mwisho ya limbikizo la ziada kwa Sh. 297,691,341 na Sh. 194,449,403; wakati katika Taarifa ya Mizania kwa mwaka fedha 2018/19 na 2019/20 uongozi uliripoti limbikizo la ziada kwa Sh. 194,449,403.46 na Sh. 297,691,341, mtawalia. Pia Bakaa ya mwisho ya Limbikizo la Ziada Sh. 297,691,341 katika Taarifa Mabadiliko ya Mtaji kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2019 haikuletwa kama bakaa ya kufungu Na.lia katika Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020. Hivyo, kiasi cha Limbikizo la Ziada katika Taarifa Mabadiliko ya Mtaji kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020 kilichoripotiwa kina upungufu kwa Sh. 297,691,341. Pia, Limbikizo la Ziada lililoripotiwa katika Taarifa ya Mizania lina upungufu kwa kiasi cha Sh. 194,449,403

- **Kiasi kilichoripotiwa cha Mishahara na Mafao ya watumishi kimeripotiwa kimakosa kwa Zaidi ya Sh. 27,000,000**

Kutokana na ukokotoaji wangu, kiasi kilichoripotiwa cha Mishahara na Mafao ya watumishi katika Taarifa ya Ufanisi wa Fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020 haikuwa sahihi ambapo kuna matumizi hayo yameripotiwa kimakosa kwa Zaidi ya Sh. 27,000,000.

- Kushindwa kufafanua taarifa ya usuluhishi ya faida/nakisi kutoka kwenye shughuli za kawaida dhidi ya Taarifa ya Mtiririko wa Fedha unaotokana na shughuli za Uendeshaji kinyume na aya Na. 29 ya IPSAS 2.
- **Kutobainishwa kwa miamala baina ya Taasisi na Wenye uhusiano na Taasisi (Related party transactions).**

Ijapokuwa niliushauri uongozi wa Hospitali kuboresha maelezo ya miamala ya wenye wenye mahusiano na Hospitali kama inavyotakiwa na aya ya 34 ya IPSAS 20 kwa kujumuisha mishahara ya viongozi muhimu, lakini hakuna maboresho yaliyofanywa katika hesabu mpya iliyowasilishwa.

## 8. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa- Sumbawanga

- **Kuripotiwa kimakosa kwa gharama za uchakavu kwa Upungufu wa Sh. 20,898,383.33**

Kiasi cha Sh. 395,929,634.15 kimeripotiwa kama gharama za uchakavu katika nukuu ya Ufafanuzi na. 43. Kati ya kiasi hicho kilichoripotiwa katika mwaka wa fedha, kiasi cha Sh. 2,334,950 kinahusiana na gharama za uchakavu wa Mitambo na mashine badala ya Sh. 23,233,333.33 iliyopaswa kuripotiwa, hivyo kupelekea kuripotiwa kwa upungufu wa gharama za uchakavu kwa kiasi cha Sh. 20,898,383.33.

- **Kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka uliopita cha mapato yasiyotokana na kodi cha Sh. 1,053,177,993 hakikuweza kuonekana katika nukuu yake ya Ufafanuzi**

Taarifa ya Mtiririko wa Fedha imejumuisha Sh. 1,053,177,993 iliyoripotiwa kama mapato yasiyotokana na kodi ya mwaka uliopita chini ya nukuu yake ya ufafanuzi Na. 31. Hata hivyo, kiasi hicho hakionekani katika nukuu yake ya ufafanuzi.

- **Kutofautiana kwa kuripoti Matumizi yaliyopita ya Vifaa na bidhaa kumepelekea Tofauti ya Sh. 100,418,700**

Taarifa ya Mtiririko wa Fedha imejumuisha Sh. 1,027,862,166.58 iliyoripotiwa kama matumizi ya vifaa na bidhaa ya mwaka uliopita. Hata hivyo, kiasi hicho kilichoripotiwa kimetofautiana na kiasi cha Sh. 927,443,466.58 kilichoripotiwa katika Nukuu yake ya ufafanuzi na. 20; hivyo kupelekea tofauti ya Sh. 100,418,700

**9. National League for Democracy (NLD)**

- Mapato yaliyoripotiwa kimakosa ambapo, Mapato na Ruzuku yaliripotiwa Sh 760,263 lakini jumla ya mapato yaliyopashwa kuripotiwa ni Sh 960,263.
- Taarifa isiyo sahihi kwa takwimu za mwaka uliopita ambapo, makusanyo ya Michango na Matumizi yaliripotiwa kimakosa kwa Sh 13,860,000 na Sh 22,222,834 badala ya Sh 1,386,000 na Sh 2,222,834 mtawaliwa.

**10. Hoapitali ya Rufaa ya Mkoa-Temeke**

**a) Masurufu yasiyotambuliwa katika taarifa za Fedha Sh 60,812,720**

Nilibaini, Masurufu ya jumla ya Sh 60,812,720 yasiyotambuliwa katika Taarifa za Fedha kwa hivyo, Noti 51 ya madai ilipunguzwa kwa Sh 60,812,720 wakati Nukuu ya Ufafanuzi 20 ya Ugavi na Matumizi na Nukuu ya Ufafanuzi Na. 20 ya gharama za Matengenezo ziliongezwa kwa Sh 57,272,720. Bakaa iliyobaki ya Sh 3,540,000 ilitumika kununua Mfumo wa X-Ray Soft hivyo kupelekea kupunguzwa kwa Nukuu ya Ufafanuzi Na. 51 ya madai na kuongezwa kwa Nukuu ya Ufafanuzi Na. 61 ya Mali zisizoshikika (interngible Asset) kwa kiasi hicho hicho.

**b) Madeni yasiyoweza kuthibitishwa Sh 253,315,280**

Noti 64 ya madeni imeripoti jumla ya Sh 1,378,112,178. Kati ya jumla ya kiasi kilichoripotiwa, sikuweza kuthibitisha uwepo na usahihi wa madeni ya Sh 248,743,780 kwa sababu ya kukosakana kwa nyaraka zinazojumuisha ankara, noti ya Uwasilishaji na Orodha za malipo. Walakini ulinganifu wa rejista ya madeni na kiwango katika ankara ulibaini, rejista ya mmadeni iliripoti Sh 4,571,500 juu kuliko kiwango cha Ankara Halisi.

## Kiambatisho Na. III: Taasisi Zilizopata Hati Mbaya

**1. Tume ya Taifa katika Shirika la UNESCO (Fungu Na. 18)**

- **Kutoonyeshwa kwa Bakaa Zilizorekebishwa za Miaka ya Nyuma**

Nimebaini utofauti wakati nikilinganisha bakaa ya mwaka uliopita na bakaa iliyoanza mwaka huu unaoishia tarehe 30 Juni 2020 katika Taarifa ya Mizania, Taarifa ya utendaji, Taarifa ya Mtiririko wa Fedha Taslimu na Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji. Marekebisho yaliyofanyika pamoja na nyaraka zilizotumika kupitisha marekebisho hayo (journal voucher) hazikuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki. Hivyo, sikuweza kuthibitisha ukweli na uhalisia wa bakaa zilizorekebishwa za Miaka ya Nyuma ambapo ni kinyume na IPSAS 3.

- **Kutofanana kwa Bakaa ya Ziada/Nakisi na Mtaji**

Nimebaini kutofanana kwa bakaa ya Ziada, Limbikizo la Nakisi na Jumla ya Mtaji katika Taarifa ya Mizania, Taarifa ya utendaji na Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji. Limbikizo la Nakisi limeripotiwa kwa Sh. 96,826,173.38 katika Taarifa ya Mizania, wakati limeripotiwa kwa Sh. 165,556,243.38 katika Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji.

- **Marekebisho ya mwaka uliopita ya Sh. 51,904,570.10 katika Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji hayakuhakikiwa**

Sikuweza kuhakiki marekebisho ya mwaka uliopita ya Limbikizo la Nakisi kiasi cha Sh. 51,904,570 kilichobainishwa katika Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji kufikia tarehe 30 Juni 2019. Maboresho hayo si kwamba yapo kinyume na IPSAS 3 lakini hayakuwa na nyaraka zilizopitisha maboresho hayo kwa ajili ya uhakiki, hivyo sikuweza kuyathibitisha.

- **Kuongezeka kwa matumizi kwa Sh. 68,730,070 kutokana na kujumuisha Matumizi ya masurufu ambayo hayajakamilika.**

Upitiaji wangu wa Taarifa ya utendaji ulibaini kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa na vifaa kimakosa kwa kiasi cha Sh. 68,730,070. Kiasi hicho kimetokana na masurufu ambayo hayajerejeshwa ambayo yalifanywa kuwa matumizi badala ya kurekodiwa kama masurufu yanayosubiri marejesho.

- **Kutofanana kwa Usuluhishi wa Malipo kwa Mtiririko wa Fedha Unaotokana na Shughuli za Uendeshaji kwa Sh. 53,690,353**

Nilibaini kutofanana kwa Sh. 53,690,353 katika kulinganisha Mtiririko wa fedha niliokokotoa unaotokana na shughuli za uendeshaji kiasi cha Sh. 1,388,066,700 wakati kiasi kilichoripotiwa katika Taarifa ya Mtiririko wa Fedha ni Sh. 1,458,311,709. Nina wasiwasi kuwa, kutofautiana kwa kiasi hicho kunaweza

kupelekea dosari ya matumizi hayo katika Taarifa ya utendaji au Taarifa ya Mtiririko wa Fedha.

- **Kuripotiwa Kimakosa Madeni ya Muda Mfupi kwa Zaidi ya Sh. 2,643,200**

Nilikokotoa jumla ya madeni ya muda mfupi na kubaini kuwa yaliripotiwa kimakosa kwa zaidi ya Sh. 2,643,200 kwa sababu yaliripotiwa kwa Sh. 222,064,477.71 badala ya Sh. 219,421,277.71 niliyokokotoa; hivyo kusababisha Taarifa za Mizania kufikia tarehe 30 Juni, 2020 kuwa na dosari.

- **Kuripotiwa Kimakosa Nakisi kwa Zaidi ya Sh. 4,000,000**

Nilikokotoa kiasi cha Nakisi kilichoripotiwa kwa kulinganisha mapato ya Sh. 1,415,268,394.22 na matumizi yaliyofanyika ya Sh. 1,508,094,567.60 kama ilivyoripotiwa katika Taarifa ya utendaji. Matokeo yake, Nakisi ni Sh. 92,826,173 na sio Sh. 96,826,173.38 iliyoripotiwa, hivyo kuwa na ongezeko la nakisi kwa kiasi cha Sh. 4,000,000

- **Kutoandaliwa kwa Taarifa ya Usuluhishi ya Mtiririko wa Fedha Unaotokana na shughuli za uendeshaji**

Kinyume na mwongozo wenye kumbukumbu na. EG.3/102/05/03/009 wa tarehe 8 Mei 2020, nilibaini kuwa Tume haikuandaa Taarifa ya Usuluhishi ya mtiririko wa fedha unaotokana na shughuli za uendeshaji katika Taarifa za Fedha za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020.

**2. Hospitali ya Rufaa - Morogoro**

**a) Makosa ya Kujumlisha katika kukokotoa Malipo ya Fedha Taslimu Sh. 606,297,324.23**

Upitiaji wa Taarifa ya Mtiririko wa Fedha ulibaini jumla ya malipo yaliyokokotolewa ili kupata Mtiririko wa Fedha unaotokana na shughuli za uendeshaji yalikuwa na makosa ya ujumlishaji kwa Sh. 606,297,324.23.

**b) Makosa katika Kukokotoa Ziada ya Sh. 1,186,209,971.25**

Ukokotozi wangu katika kuifikia Ziada katika Taarifa ya utendaji ulibaini makosa ya kihesabu kwa Sh. 1,186,209,971.25

- Kushindwa kutoa maelezo katika tofauti kubwa iliyoripotiwa kati ya bajeti dhidi ya taarifa ya kiasi halisi, kinyume na aya ya 14 &29 ya IPSAS 24.

- Kushindwa kuwianisha taarifa ya usuluhishi ya ziada/nakisi kutoka kwenye shughuli za kawaida dhidi ya taarifa ya Mtiririko wa Fedha unaotokana na shughuli za uendeshaji kinyume na aya ya 29 ya IPSAS 2.
- Kushindwa kuelezea uhalisia wa kosa la kipindi kilichopita la Sh. 10,066,671,390, kinyume na aya ya 54 ya IPSAS 3
- Katika Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji, Uongozi ulifanya maboresho

| | |
|---|---|
| | kwenye Fedha za Walipa Kodi kwa Sh. 10,066,671,390 lakini hakukuwa na nukuu ya ufafanuzi kwenye hesabu kuelezea uhalisia wa kosa hilo la kipindi kilichopita, hivyo nimeshindwa kuthibitisha kiasi hicho. |

**Kiambatisho Na. IV: Taasisi ambazo Hazikupata Maoni**

| **1. Alliance for Democratic Change (ADC)** |
|---|
| Uongozi wa Chama hauna utaratibu wa kutumia vitabu rasmi vya uhasibu, hivyo uwezo wangu wa kupata taarifa muhimu ulidhibitiwa. Kwa hivyo, sikuweza kujiridhisha kwa njia nyingine yoyote uhalali na usahihi wa hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. |
| **2. Tanzania Labour Party (TLP)** |
| Sikuweza kuthibitisha bakaa zote zilizoonyeshwa katika Taarifa ya Mizania na Taarifa ya utendaji kwa sababu uongozi wa Chama haukuweza kunipa nyaraka za kuthibitisha uhalali wa kiasi kilichoripotiwa katika taarifa hizo za fedha. |
| **3. Union for Multiparty Democracy (UMD)** |
| Taarifa za Fedha za Chama zilizowasilishwa hazikuandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma, ambapo vingetumika kama msingi wa kufanya tathmini |
| **4. United Peoples' Democratic Party (UPDP)** |
| Hesabu za Chama zilizowasilishwa hazikuandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma, ambapo vingetumika kama msingi wa kufanya tathmini |
| **5. African Democratic Alliance (ADA-TADEA)** |
| • Uongozi wa Chama haukuandaa leja kuu na urari wa fedha kwa kiasi kilichoripotiwa katika hesabu hivyo mawanda ya ukaguzi yalikwazwa kwani sikuweza kupata taarifa kamili. Kwa hiyo, sikuweza kwa namna yoyote kuhakiki usahihi na ukweli wa taarifa za fedha za Chama.<br><br>• Mapitio yangu ya taarifa za fedha za chama kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 yalibaini kuwa Chama kilifanya matumizi ya jumla ya Sh. 4,894,800. Kati ya matumizi hayo, niliweza kukagua vocha za malipo zenye jumla ya Sh. 1,780,000 lakini nyaraka za matumizi yaliyobakia ya kiasi cha Sh. 3,114,800 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.<br><br>• Taarifa ya Mizania imejumuisha Sh. 200,610 zilizoripotiwa kama Fedha Taslimu na Fedha Linganishi katika nukuu ya Ufafanuzi na. 26 (a&b). Kati ya hizo, Sh. 186,110 ni bakaa ya fedha zilizopo benki ya NMB na Sh. 14,500 ni bakaa ya fedha taslimu kwa ajili ya matumizi madogo madogo. Hata hivyo, sikuweza kuthibitisha kuwapo kwa bakaa hizo; kwani Akaunti ya Benki ya NMB haijatumika kwa Zaidi ya mwaka mmoja, pia ripoti ya kuhesabu bakaa ya fedha taslimu mwisho wa mwaka haikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. |

| |
|---|
| |
| **6. Sauti ya Umma** |

- **Kutokuwapo kwa Taarifa ya Mtiririko wa Fedha**

Taarifa za Fedha za Chama cha SAU zilizowasilishwa kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020 hazikujumuisha Taarifa ya Mtiririko wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2019/20.

- **Kutokuwapo kwa Taarifa ya kuonyesha taarifa za fedha zimeandaliwa kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika.**

Nukuu za Ufafanuzi kwa taarifa za fedha hazikuwa na taarifa inayoeleza kama hesabu za Chama zimeandaliwa kwa mujibu wa viwango vya kiuhasibu vinavyokubalika, na kama kuna sababu za kwenda tofauti na viwango hivyo. Pia, kuonesha kama taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kufuata Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992, iliyorekebishwa mwaka 2019.

- **Kutokuwapo kwa Nukuu za ufafanuzi, muhtasari wa sera muhimu za kiuhasibu na nukuu nyingine za ziada**

Hesabu iliyoandaliwa na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi haikuwa na Nukuu za ufafanuzi, sera muhimu za kiuhasibu zinazoelezea miongozo, wala sheria na viwango vilivyotumika na Chama katika kuandaa taarifa za fedha.

- **Uwasilishwaji Usio Sahihi wa Ripoti ya Mwenyekiti**

Ripoti ya Mwenyekiti imekosa taarifa muhimu zitakazoweza kumsaidia mtumiaji wa hesabu kufanya maamuzi juu ya Chama. Mfano wa taarifa zilizokosekana ni Rasilimali na Uwezo wa Chama, Mapitio ya utendaji wa Chama, Utekelezaji wa mipango na bajeti kwa mwaka 2019/20, Mipango ya baadae ya chama na makisio ya mtiririko wa fedha.

- **Utumiaji Usio Sahihi wa Muda wa Kutumia Mali za kudumu.**

Jedwali la kwanza la Kanuni Na. 28(3) la Kanuni (Masuala ya Uhasibu) za Vyama vya Siasa za mwaka 2019 linatoa mwongozo wa Muda wa Utumiaji Mali za kudumu za vyama vya siasa katika kukokotoa uchakavu wa Mali hizo. Kinyume chake, Chama kilitumia muda usio sahihi wa matumizi ya Mali kwa samani za Ofisi na kompyuta.

- **Kutokuwapo kwa Tamko la Uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha**

Sheria Na. 33 ya mwaka 1972 ya Bodi Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi, iliyorekebishwa kwa Sheria Na. 2 ya mwaka 1995 inataka kuwe na tamko la uthibitisho katika Taarifa za Fedha kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha.

Taarifa ya Fedha iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi haikujumuisha tamko la uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha katika kutambua majukumu yake ya kuhakikisha taarifa za fedha zimendaliwa kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika.

- **Madeni ya Sh. 8,745,103 Hayana Nyaraka Toshelezi**

Katika Taarifa ya Mizania, Chama kimeripoti madeni ya Sh. 8,745,103. Hata hivyo, madeni hayo hayakua na nyaraka toshelezi ili kuniwezesha kuthibitisha uwepo wa

madeni hayo.

- **Kutokuwapo kwa Vocha za Malipo kwa Matumizi ya Sh. 3,035,000**

Matumizi ya Sh. 3,035,000 ambayo ni gharama za pango Sh. 3,000,000 na Matumizi ya Ofisi Sh. 35,000 kama yalivyooneshwa katika Nukuu ya Ufafanuzi Na. 6 ya hesabu hayakuwa na vocha za malipo.

- **Msingi wa Uandaaji wa Taarifa za Fedha na Kipimo cha Kutambua Mapato na Matumizi Inatofautiana na Miongozo ya Kiuhasibu Inayokubalika**

Katika Nukuu ya Ufafanuzi Na. 1 kuhusu misingi ya uandaaji wa hesabu, ilielezwa kwamba hesabu zimeandaliwa kwa misingi ya kiuhasibu ya fedha isiyo taslimu (Accrual Basis Accounting), lakini nukuu ya Ufafanuzi Na. 2 na 3 zimeeleza kwamba mapato yatatambulika pale yatakapopokelewa na matumizi yatatambulika pale tu yatakapotumika, ambapo hiyo ni misingi ya kiuhasibu ya fedha taslimu (Cash basis Accounting).

## 7. National Reconstruction Alliance (NRA)

- **Kushindwa Kuthibitisha Matumizi Yaliyoripotiwa ya Sh. 7,950,000.**

Chama cha NRA hakikuweza kutoa nyaraka za malipo ya Sh. 7,950,000 zilizotumika katika mwaka wa fedha. Hivyo, sikuweza kujiridhisha na uhalali wa malipo hayo.

- **Kutofuatwa kwa Viwango Kubalifu vya Kimataifa wakati wa Uandaji wa Taarifa za Fedha**

Kanuni Na. 3 (1) ya Kanuni za Vyama vya Siasa (Masuala ya Uhasibu) za mwaka 2019 inataka kila Chama cha Siasa kuandaa na kuwasilisha hesabu kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma (IPSAS). Chama cha NRA hakikuandaa hesabu kwa mujibu wa viwango hivyo. Hivyo, nimeshindwa kutoa maoni yangu kwa hesabu hizo kutokana na kutofuatwa kwa matakwa ya IPSAS.

## 8. Alliance for Africa Farmers Party (AAFP)

Hesabu za Chama zilizowasilishwa hazikuandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma ambapo vingetumika kama msingi wa kufanya tathmini. Badala yake, Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020 ndio iliyowasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 3 (1&2) ya Kanuni za Vyama vya Siasa (Masuala ya Uhasibu) za mwaka 2019 inayotaka kila Chama cha Siasa kuandaa na kuwasilisha hesabu kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma(IPSAS).

## 9. Demokrasia Makini

Hesabu za Chama zilizowasilishwa hazikuandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma, ambapo vingetumika kama msingi wa kufanya tathmini. Badala yake, Taarifa ya Mapato na Matumizi Taslimu, Nukuu za Ufafanuzi na Rejesta ya Mali za Kudumu kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020 ndivyo vilivyowasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 3 (1&2) ya Kanuni za Vyama vya Siasa (Masuala ya Uhasibu) za mwaka 2019 inayotaka inayoelekeza uandaaji na uwasilishaji wa hesabu kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma (IPSAS).

## Kiambatisho Na. V: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mwaka Uliopita

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2018/19 | **Majibu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali**<br>Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) Kwa kushirikiana na Maafisa Masuuli wanapaswa kuweka juhudi zaidi katika utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kulingana na mpango wa utekelezaji | Serikali kupitia Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani katika Wizara ya Fedha na Mipango inaimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Serikali (GARI-ITS) ili kuhakikisha kuwa mpango kazi na uchambuzi wa umri wa ripoti umejumuishwa katika mfumo. | Majibu ya Serikali yamezingatiwa, nitathibitisha juu ya utekelezaji wa mapendekezo yangu ya ukaguzi yaliyosalia katika kipindi kijacho cha ukaguzi | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 2 | 2018/19 | **Makusanyo ya Halmashauri yasiyoripotiwa Mfuko Mkuu Sh. bilioni 553.378**<br>Nashauri Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Halmashauri zikishirikiana na Sekretarieti za Mikoa kuboresha mifumo na kuongeza ufahamu juu ya jukumu la kuwasilisha Taarifa za makusanyo Mfuko Mkuu. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 3 | 2018/19 | **Mikopo ya Nje isiyoripotiwa Mfuko Mkuu Sh. bilioni 1,171.91**<br>Naendelea kutoa msisitizo wa | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekazo limerudiwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ushauri nilioutoa kipindi cha nyuma, juu ya kufanya usuluhisho katika taarifa za fedha na kuboresha mifumo ya fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi. | | | |
| 4 | 2018/19 | **Uwiano wa Makisio na Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Kawaida**<br>Ni maoni yangu kwamba kutokutolewa kwa fedha za matumizi ya kawaida na kulipa madeni kunaweza kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 5 | 2018/19 | **Uwiano wa Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Kawaida na Matumizi halisi yaliyofanyika**<br>Maoni yangu kwamba, kuwapo wa bakaa ya fedha zisizotumika kunamaanisha kutotekelezwa au utekelezaji hafifu wa shughuli zilizokusudiwa au uwezo hafifu wa Taasisi katika kutumia fedha zilizotolewa kwa wakati. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 6 | 2018/1 | **Uwiano wa Makisio na Fedha** | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji | Pendekezo |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | 9 | **zilizotolewa kwa shughuli za Maendeleo**<br>Ni maoni yangu kuwa, utolewaji hafifu wa fedha za maendeleo kunaathiri utekelezaji wa vipaumbele vya bajeti ya mwaka na miradi ya maendeleo. | | wa mapendekezo ya ukaguzi | halijatekelezwa |
| 7 | 2018/19 | **Uwiano wa Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Maendeleo na Matumizi halisi yaliyofanyika**<br>Napendekeza fedha za maendeleo zitolewe kwa wakati. Pia Maafisa Masuuli wa Mafungu husika waongeze juhudi katika kuhakikisha kwamba miradi ya Maendeleo iliyopangwa inatekelezwa ndani ya kipindi kilichopangwa. | Serikali inazingatia kutolewa kwa fedha kulingana na upatikanaji. | Jibu la Serikali limezingatiwa, bado nasisitiza kutolewa kwa fedha kwa wakati ili kuharakisha shughuli zilizopangwa | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 8 | 2018/19 | **Kutokuwasilishwa kwa Maduhuli Mfuko Mkuu Sh. 4,128,070,205**<br>Ni ushauri wangu, kuhakikisha Sheria ya Fedha na miongozo inayotolewa inafuatwa ili kuwezesha maduhuli yanayokusanywa kuwasilishwa Mfuko Mkuu. | Wizara ya Fedha ilitoa Waraka wa uhasibu no 6 wa 2019/2020 ambao unawaongoza maafisa masuuli kukusanya makusanyo kwa kufuata sheria ya fedha za umma na maagizo mengine. | Jibu la Serikali limezingatiwa, bado nasisitiza kufuata Sheria ya Fedha juu ya ukusanyaji wa mapato | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | 2018/19 | **Makusanyo ya Viza yaliyofanyika dirishani Kiasi cha Sh. 646,083,432.07**<br>Nashauri Balozi zote kuhakikisha makusanyo yote yanafanyika Benki na kuwasilishwa Mfuko Mkuu ili kuchangia Bajeti ya mwaka husika. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo Halijatekelezwa |
| 10 | 2018/19 | **Kutokurudishwa Mfuko Mkuu Fedha zilizokaa muda mrefu katika Akaunti za Amana Sh. 3,389,301,017.92**<br>Ninazishauri menejimenti za Wizara na balozi husika kutii sheria tajwa hapo juu, pia kuwasiliana na Hazina ili kupata maelekezo na namna ya kutumia ama kuwasilisha fedha hizo katika mfuko Mkuu. | Wizara ya Fedha ilitoa waraka wa uhasibu no 6 wa 2019/2020 ambao unawaongoza maafisa masuuli kusanya makusanyo kwa kufuata sheria ya fedha za Umma na maagizo mengine. | Jibu la Serikali limezingatiwa,hata hivyo bado ninasisitiza juu ya ufafanuzi kutoka hazina kuhusu fedha ambazo hazijatumiwa zilizowekwa katika akaunti za amana na akaunti zingine zilizolala. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 11 | 2018/19 | **Kutokusanywa kwa maduhuli yanayotokana na Makosa ya Barabarani Sh. 4,570,783,000**<br>Maoni yangu kwamba, kutokukusanya mapato kunainyima Serikali kutumia fedha hizo katika shunguli nyingine. Nazishauri Taasisi zinazihusika kuhakikisha | Serikali imeboresha mfumo kwa kuunganisha mfumo wa barabarani na wavuti ya mamlaka ya mapato Tanzania ili wavunjaji wa sheria za barabarani wasiruhusiwe kufanya upya leseni zao za kuendesha gari isipokuwa wamelipa bili zao za awali. Kwa kuongezea, Serikali | Jibu la Serikali limezingatiwa, nitathibitisha majibu wakati wa ukaguzi ujao ikiwa ni pamoja na uhakiki wa mfumo. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kwamba mpango mkakati unawekwa ili kuhakikisha makusanyo yote yanayotokana na tozo za uvunjaji wa Sheria barabarani yanakusanywa. | bado inafanya juhudi zaidi kuhakikisha kuwa magari hayo yenye madeni yaliyobaki yanapatikana na bili zao na adhabu zinalipwa. | | |
| 12 | 2018/19 | **Shughuli zilizotekelezwa nje ya Bajeti Sh. 2,583,161,865**<br>Ni mapendekezo yangu kwa Wizara kuhakikisha kwamba matumizi yote yanabajetiwa na kupitishwa na Bunge ili kuzuia utekelezaji wa shughuli za dharura zinazoweza kusababisha marejeo ya Bajeti kwa kiasi kikubwa, pia kuhakikisha marejeo yote ya Bajeti yanapitishwa na Waziri wa Fedha na Mipango kabla ya utekelezaji. | Serikali itahakikisha kuwa shughuli zinatekelezwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na kwa sababu hiyo Serikali imeidhinisha sh. 107,000,000 / = kwa shughuli za Tamasha la Urithi katika Wizara ya Maliasili na bajeti ya Utalii katika mwaka wa fedha 2020/21 | Jibu la Serikali limezingatiwa, bado nasisitiza kuhakikisha shughuli zinapangiwa bajeti na kuidhinishwa kabla ya utekelezaji | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 13 | 2018/19 | **Changamoto katika ukusanyaji wa mapato na mapendekezo**<br>a)Kuwapo kwa kesi za kodi za muda mrefu katika Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB), Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT) na Mahakama ya Rufaa (CAT)<br>Bodi na Rufaa ya kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya | i) Baadhi ya mapendekezo inahitaji mabadiliko ya mfumo, haya yatasuluhishwa pole pole.Mamlaka ya mapato Tanzania itakapoboresha / kukuza mifumo<br>ii) Mamlaka ya mapato Tanzania imeingia makubaliano ya malipo kwa awamu na baadhi ya walipa kodi ili kuepukana na malimbikizo | Jibu la Serikali limezingatiwa, bado nasisitiza kusuluhisha kwa wakati migogoro ya ushuru inayosubiri usuluhishi na kuweka mkakati wa kutatua changamoto katika ukusanyaji wa | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Rufaa, kuziongezea bajeti na kutoa fedha za kutosha ili kuziwezesha Taasisi hizi kusikiliza na kuhitimisha kesi za kodi kwa wakati.<br>b) Madeni ya kodi<br>Naishauri Serikali iongeze jitihada katika ukusanyaji wa kodi kutoka kwa walipakodi wanaodaiwa. Jambo hili linaweza kufanikiwa kwa kuboresha na kukiongezea uwezo kitengo cha ukusanyaji wa madeni na kuwa na mikakati ya kuhakikisha kuwa kodi zote zinakusanywa kwa Wakati, hivyo kuzuia malimbikizo ya madeni ya kodi<br>c) Kuchelewa Kutatua Mapingamizi ya Kodi<br>Naishauri Serikali kuhakikisha mapingamizi ya kodi yanashughulikiwa na kutatuliwa kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuongeza maafisa wenye weledi na ujuzi wa kutosha wa kushughulikia mapingamizi hayo ya kodi; pia, | ya kodi ya muda mrefu.<br>iii) Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania umechukua hatua kadhaa katika kutekeleza mapendekezo ambayo bado hayajatekelezwa<br>iv) Mahakama ya kodi na mahakama ya Rufaa ya kodi, Mahakama zote mbili zinafanya vikao viwili vya mahakama. | mapato. | |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuwaongezea uwezo maafisa hao.<br>d) Upungufu wa Rasilimali na wakaguzi wa kodi wenye weledi<br>Naishauri serikali kuboresha utendaji kazi wa Mamlaka kwa kuhakikisha kuwa kitengo cha wakaguzi wa kodi kinakuwa na wafanyakazi wa kutosha, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wakaguzi na wakadiriaji wa kodi.<br>e) Udhibiti usioridhisha katika kushughulikia mizigo iliyoingia nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi na kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine<br>Naishauri Serikali kuhakikisha taratibu za forodha zinafuatwa; mizigo inayoingia nchini au kuzalishwa nchini kwa ajili yakusafarishwa kwenda nchi nyingine inasimamiwa vizuri; na kodi na tozo za adhabu kwa mizigo iliyouzwa au kutumika nchini kinyume cha taratibu zinakusanywa.<br>f)Kutofanyika kwa minada katika | | | |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | bidhaa zilizokaa kwa muda mrefu katika maghala ya forodha<br>Naishauri serikali kufanya minada mara kwa mara ili kukomboa kodi kwenye bidhaa zilizotelekezwa na kukaa muda mrefu kwenye maghala yao ya forodha. Njia hii itazuia upotevu wa mapato na kusaidia bidhaa zisiharibike. | | | |
| 14 | 2018/19 | **Usimamizi wa Pingamizi za Ushuru**<br>**Kodi zilizopo kwenye kesi za muda mrefu katika Mamlaka za Rufaa za Kodi**<br>Naishauri Serikali iboreshe utendaji wa mamlaka za rufani za kodi kwa kuhakikisha zinakuwa na bajeti ya kutosha, kutoa fedha na rasilimali nyingine za kutosha ili mamlaka hizi ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; Hivyo, kusikiliza na kuhitimisha kesi za kodi kwa wakati. | a) Serikali imeboresha utendaji wa ofisi za rufaa ya Kodi kwa kutenga fedha za kutosha na rasilimali zingine kwa shughuli za ofisi za rufaa ili kuwezesha usikilizaji na kumaliza kesi za ushuru kwa wakati. | Jibu la Serikali limezingatiwa, uhakiki juu ya utekelezaji utathibitishwa ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 15 | 2018/19 | **Mapungufu katika kushughulikia mapingamizi ya kodi**<br>Naishauri Serikali: | Serikali kupitia mamlaka ya mapato Tanzania imeongeza idadi ya wafanyikazi wenye uwezo na | Jibu la Serikali limezingatiwa, utekelezaji | Pendekezo lipo katika hatua ya |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | (a) Kuongeza ufanisi katika kushughulikia mapingamizi ya kodi yanayoletwa na walipakodi ili kuyamaliza mapingamizi yaliyokaa muda mrefu. Hili linawezekana kwa kuongeza idadi ya watumishi wenye uzoefu na ujuzi pamoja na kuwaongezea mafunzo watumishi wa kitengo cha huduma za Kiufundi na Kitengo cha Ukaguzi wa Kodi na kuboresha utoaji wa makadirio ya kodi.<br>(b) Kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Mapato inafanya uhakiki wa kutosha wa mapingamizi ya kodi yanayowasilishwa na walipa kodi ili kujiridhisha iwapo yanakidhi vigezo vya sheria ya usimamizi wa kodi kabla ya kuyashughulikia. Sheria hii inataka, pamoja na mambo mengine, mapingamizi yote ya kodi yawasilishwe kwa Kamishna wa Mamlaka ndani ya siku thelathini tangu tarehe ambayo maamuzi ya kodi yalifanyika, yakiambatana na malipo ya amana (ambayo ni kiasi | uzoefu katika kitengo cha ukaguzi wa Ushuru na kitengo cha huduma za kiufundi<br>b) Imepanga kuhakikisha kuwa pingamizi za ushuru zinawasilishwa ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya huduma ya makisio ya ushuru na malipo ya amana za kisheria zinazodaiwa | utathibitishwa ukaguzi ujao ikiwa ni pamoja na uhakiki wa idadi ya wafanyakazi walioongezwa. | utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ambacho ni kikubwa kati ya kiasi cha kodi isiyopingwa au moja ya tatu ya kodi inayopingwa). | | | |
| 16 | 2018/19 | **Usimamizi wa malimbikizo ya kodi**<br>i) Madeni ya Kodi yaliokaa muda mrefu - Shilingi 276,197,724,204.<br>Kushindwa kukusanya madeni ya muda mrefu kunapunguza uhakika wa kuyakusanya na kunaweza kuikosesha Serikali mapato.<br>ii) Kuchelewa kukusanya na ufuatiliaji usioridhisha wa madeni ya kodi Shilingi 42,859,547,757.15<br>Naishauri Serikali iongeze jitihada na kuboresha mikakati katika usimamizi, ufuatiliaji na ukusanyaji wa madeni ya kodi; na kuhakikisha kuwa, kodi zote na tozo zinakusanywa kwa wakati. Pamoja na mambo mengine, Serikali inaweza kufanya makubaliano na walipakodi ili malipo ya kodi yafanyike kwa awamu. Mikakati hii itapunguza malimbikizo ya madeni ya kodi | Serikali imekuwa ikitekeleza mipango anuwai kuhakikisha kuwa mapato ya ushuru yanakusanywa kwa wakati unaofaa | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo ninasisitiza kuweka juhudi zaidi katika kukusanya ushuru, utekelezaji utathibitishwa ukaguzi ujao | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | yaliyokaa muda mrefu bila kukusanywa.<br>Naishauri Serikali iongeze jitihada na kuboresha mikakati katika usimamizi, ufuatiliaji na ukusanyaji wa madeni ya kodi; na kuhakikisha kuwa, kodi zote na tozo zinakusanywa kwa wakati. | | | |
| 17 | 2018/19 | **Utekelezaji wa Msamaha wa Riba na Adhabu kwenye Madeni ya Kodi**<br>Naishauri Serikali kuwaongezea walipakodi uelewa na umuhimu wa kutumia kwa wakati fursa ya msamaha wa riba na adhabu za kodi ili kuwasaidia walipa kodi kupunguza madeni yao ya kodi na kuongeza mapato kwa Serikali. | Uhamasishaji wa msamaha wa kodi umeendelezwa na kusababisha jumla ya maombi 9,406 kati ya hayo maombi 8,687 yalipitishwa na jumla ya kodi kuu iliyolipwa ni Sh. 322,321,367,828 | Majibu ya Serikali yamezingatiwa mwenendo wa ukusanyaji mapato na matokeo yake vitathibitishwa ukaguzi ujao | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 18 | 2018/19 | **Usimamizi wa Makusanyo ya Kodi**<br>Udhibiti usioridhisha katika ukusanyaji wa kodi kwenye mafuta yaliyoingizwa kutoka nchini nyingine kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi<br>a)Kodi za forodha Shilingi | Mamlaka ya mapato Tanzania inaendelea kuimarisha upatanisho wa kila mwezi wa bili za shehena na tathmini ili kupunguza hatari ya kuwa na ushuru wa malipo ya nyongeza isiyolipwa ya Sh. 124,696,085 mamlaka ya mapato | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo bado ninasisitiza kuhakikisha<br>a)Kodi ya forodha kwenye mafuta iliyohojiwa ya | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 124,696,085 zilizokadiriwa kwenye mafuta lakini hazikulipwa<br>b) Kodi na ada za bandari ambazo hazikukadiriwa na kulipwa Shilingi 3,577,249,115<br>c) Kutokusanya riba ya Shilingi 1,360,550,338.62 baada ya malipo ya kodi kucheleshwa<br>**Naishauri Serikali**:<br>a). Kufuatilia kwa karibu ukadiriaji na ukusanyaji wa kodi za forodha, zikiwamo Shilingi 124,696,085 kutoka kwenye makampuni ya mafuta.<br>b). Ichukue hatua za kukadiria na kukusanya kodi na ada za bandari shilingi 3,577,249,115. C). Kuhakikisha kuwa riba na adhabu zinazotokana na ucheleweshwaji wa malipo ya kodi zinakusanywa; pia Serikali ikusanye riba ya shilingi 1,360,550,338.62 ambayo haikukusanywa hapo awali. | Tanzania imepata ushuru wa jumla ya Sh. 19,262,547 na ilani kwa wakala ya tarehe 15/04/2020 imetumwa kwa Benki ya Equity kupata kiasi kilichobaki cha Sh. 105,433,538 zinazohusiana na UKOD Tanzania mdogo. Uongozi wa mamlaka ya mapato Tanzania umekukusanya jumla ya Sh. 1,216,419,971 na kuwasilisha ushahidi kwa mkaguzi kukaguliwa, juhudi za kupata kiasi kilichobaki cha Sh. 144,130,367.62 zinaendelea.<br>Serikali itaendelea kujitahidi zaidi kupitia mamlaka ya mapato Tanzania kuhakikisha riba na adhabu na malipo ya ushuru yaliyocheleweshwa vinakusanywa. Ushahidi wa ukusanyaji utawasilishwa kwa wakaguzi kwa ukaguzi | Sh.124,696.085 inalipwa kwa ukamilifu.<br>b)Kodi na ada za bandari Sh.3,577,249,115 zilizokadiriwa kulipwa zinalipwa na<br>c) Riba na adhabu zinatozwa kwa kucheleweshwa kwa ushuru Sh. 1,360,550,338.62 zilizohojiwa. | |
| 19 | 2018/19 | **Udhibiti usioridhisha wa bidhaa na mafuta yanayosafirishwa kwenda nchi nyingine** | Serikali kupitia mamlaka ya mapato Tanzania imeboresha mfumo wa ufuatiliaji wa shehena | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo uthibitisho wa | Pendekezo lipo katika hatua ya |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | a)Kodi za forodha kwenye bidhaa zinazosafirishwa kwenda nchi nyingine ambazo hazikuthibitishwa kutoka nje ya nchi Shilingi 127,583,275,392.74<br>b) Bidhaa kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine ambazo ilithibitishwa kwenye mfumo lakini ushahidi wa nyaraka ulikosekana Shilingi 299,804,063.32<br>(c) Kutokusanywa kwa tozo za adhabu ya Shilingi 167,307,834.91 zilizotokana na bidhaa kuchelewa kutoka nchini kwenda nchi husika<br>**Naishauri Serikali:**<br>(a).iimarishe udhibiti katika usafirishaji na utokaji wa bidhaa, ikiwa ni pamoja na kuthibitisha katika mfumo wa TANCIS kwa bidhaa zinazokwenda nchi nyingine, na kukusanya ushuru wa forodha, riba na tozo stahiki kwa bidhaa zilizouzwa nchini kinyume na taratibu.<br>(b) Kukusanya tozo za adhabu zinazotokana na bidhaa kuchelewa | za elektroniki (ECTS) na udhibiti umeimarishwa. Ushuhuda wa kukosekana kwa jumla ya Sh. 299,804,063.32 uliwasilishwa kwa mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi<br>b) Mamlaka ya mapato Tanzania, pia imetoa notisi za mahitaji kwa wakala wote wa kusafisha (CFAs) ili kupata adhabu ya dhamana ya kuchelewesha kuondoka kwa bidhaa za usafirishaji ambazo ni Sh. 167,307,834.91 ifikapo mwisho wa Juni 2020.<br>Serikali kupitia mamlaka ya mapato Tanzania inahakikisha kwamba adhabu ya dhamana kwa kuchelewa kutoka kwa bidhaa za usafirishaji hukusanywa kwenye shughuli zote. Hii inatarajiwa kuzuia uingizwaji haramu wa bidhaa bila malipo ya ushuru. | uboreshwaji wa mfumo utaangaliwa ukaguzi ujao ikiwa ni pamoja na uhakiki wa nyaraka zilizowasilishwa kwangu. | utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kutoka nchini kwenda nchi nyingine ili kuzuia uwezekano wa bidhaa hizo kuuzwa nchini bila kulipiwa kodi stahiki. | | | |
| 20 | 2018/19 | **Bidhaa zilizokaa kwa muda mrefu kwenye maghala ya forodha na bidhaa zinazoingia nchini kwa muda maalumu**<br>**Naishauri Serikali**;<br>(a) Kufanya maamuzi kwa wakati ya kuuza katika minada bidhaa zilizokaa kwenye maghala ya forodha kwa zaidi ya siku 60 ili kukomboa kodi ya bidhaa hizo.<br>(b) Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye bidhaa na magari yanayoingizwa nchini kwa muda maalumu, na kukusanya kodi kwenye bidhaa na magari ambayo hayakurudi nchi yalikotoka na kukusanya tozo za adhabu na riba kwa kuuza nchini bidhaa na magari hayo kinyume na sheria za forodha. (c) Kuimarisha udhibiti na ufuatiliaji katika bidhaa na magari yanayoingizwa nchini kwa muda | Serikali kupitia mamlaka ya mapato Tanzania imeanzisha hatua kadhaa;<br>a)Kutambua bidhaa zilizodumu katika ofisi tofauti za forodha<br>b) Ukaguzi kwa mamlaka ya mapato Tanzania kuhusiana na nyaraka unaonyesha yafuatayo;<br>i) miamala miwili yenye thamani ya Sh. 15,372,399.88 na ushuru uliopachikwa Sh. 12,822,231<br>ii) Vibali vya kuongezewa muda vilipewa kwa shehena zinazohusiana na miamala tisa yenye thamani ya ushuru dola za kimarekani (USD) 1,949,266.42 na ushuru uliopachikwa jumla ya Sh. 1,677,942,396 | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo uthibitisho wa hatua zilizoanzishwa, zitathibitishwa ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | maalum ili kuzuia kuuzwa nchini bila kulipiwa kodi stahiki. | | | |
| 21 | 2018/19 | **Udhibiti usioridhisha kwenye bidhaa zinazoingizwa nchini kinyume na sheria za forodha.**<br>**Nashauri Serikali**;<br>Kuboresha udhibiti katika kushughulikia kesi za makosa ya kikodi ili kuzihitimisha kwa wakati na kukusanya kodi zinazotokana na makosa hayo ili kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali. | Menejimenti ya Mamlaka ya mapato Tanzania inakubaliana na mapendekezo ya mkaguzi na itahakikisha kwamba adhabu zote zinazobaki zinakusanywa au bidhaa zilizokamatwa zinakabiliwa na taratibu za utupaji. Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) iliwasilisha ushahidi wa kibali juu ya ushuru wa nyongeza, adhabu na riba ya jumla ya Sh. 106,094,872.18 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ili ikaguliwe | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo bado nasisitiza juu ya kuimarisha udhibiti ili kuepuka upotezaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kuhakiki nyaraka zilizowasilishwa kwangu. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 22 | 2018/19 | **Usimamizi wa Deni la Serikali(Udhibiti wa deni la Serikali)**<br>Kutopokea fedha za mikopo muda mrefu baada ya kusaini Mikataba ya mikopo<br>Napendekeza Serikali iwe na utaratibu wa kusimamia, kutathimini na kufuatilia mapokezi na matumizi ya fedha za mikopo. | Pendekezo halijajibiwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Utaratibu huo utapelekea watekelezaji wa miradi kuhasibu ipasavyo mapokezi na matumizi ya fedha za mikopo.Pia kuwapo utaratibu wa kuwianisha mikataba ya mikopo iliyosainiwa na fedha zilizopokelewa kutokana na mikataba hiyo. | | | |
| 23 | 2018/19 | **Huduma za jumla**<br>Napendekeza Serikali iwe na kanzidata ya wanaostahili malipo ili kuwezesha usuluhishi wa pamoja wenye tija na kulinda fedha za umma kuliko kutegemea ankara zitolewazo na wakala (LAPF) pekee | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 24 | 2018/19 | **Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu**<br>Mafao ya Hitimisho la Kazi yaliyokokotolewa chini ya kiwango stahiki – Sh. 117,449,527.42<br>**Ucheleweshwaji wa Uaandaji wa Mafao**<br>Mapendekezo Serikali ihakikishe kuwa Waajiri wanazingatia Sheria za mafao kwa kuandaa mapema na kuwasilisha majalada ya wastaafu | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kwa ajili ya ukaguzi na malipo. | | | |
| 25 | 2018/19 | **Kuchelewa kwa utayarishaji na uwasilishaji wa maelezo ya mafao ya wastaafu**<br>Serikali kuhakikisha waajiri wanazingatia sheria za mafao ya mwisho kuhusu utayarishaji wa mapema na uwasilishaji wa maelezo ya wastaafu kwa ukaguzi wa mapema na malipo | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 26 | 2018/19 | **Majalada yenye Hoja ambayo hayakurudishwa kwa Ukaguzi wa awali**<br>Mapendekezo<br>¤ Waajiri wanapaswa kufanyia kazi hoja za ukaguzi na kurudisha majalada kwa wakati au kuomba ufafanuzi kutoka Ofisi yangu pale inapobidi.<br>¤ Serikali ihakikishe waandaaji wanazingatia, Sheria, Kanuni, Waraka na miongozo ya mafao wakati wa uandaaji. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijajibiwa |
| 27 | 2018/19 | **Majalada yaliyoidhinishwa kwa malipo kurudishwa kwa ukaguzi kwa mara nyingine** | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijajibiwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mapendekezo Serikali inashauriwa kuweka adhabu kali kwa wale wote watakaorudisha majalada yaliyokwisha lipwa kwa ajili ya ukaguzi. Kadhalika, Serikali inatakiwa kuboresha mifumo ya malipo kwa ajili ya kugundua na kuzuia malipo ya mara ya pili. | | | |
| 28 | 2018/19 | **Mikopo iliyoingiwa mikataba lakini haikutolewa kwa muda mrefu**<br>Serikali inapaswa kuweka utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ambao utafuatilia utoaji na matumizi ya fedha zinazotokana na deni la umma. | Serikali kupitia wizara ya Fedha imeweka utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ili kufuatilia malipo na matumizi ya fedha zinazotokana na deni la Umma | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo utaratibu utathibitishwa ukaguzi ujao | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 29 | 2018/19 | **Mapitio ya Mfumo wa Utengenezaji wa Hesabu Jumuifu (GACS)**<br>Napendekeza Serikali iweke mkakati mahususi kuwezesha Taasisi kuripoti viwango sahihi vya miamala kati ya Taasisi za kiserikali na kutekeleza mfumo wa uhakiki wa viwango vinavyoripotiwa kwa ajili ya | Serikali kupitia usimamizi wa mhasibu mkuu wa Serikali inaboresha Mfumo wa Utengenezaji wa Hesabu Jumuifu (GACs) ambazo zitaweza kutahadharisha popote ambapo takwimu zinatofautiana kabla ya mfumo kuruhusu uondoaji utekelezwe | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo Mfumo wa Utengenezaji wa Hesabu Jumuifu (GACs )utathibitishwa ukaguzi ujao | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | uondoshwaji ili kuboresha utoaji taarifa sahihi. | | | |
| 30 | 2018/19 | **Udhibiti Usiojitosheleza kwenye Matumizi ya Jumla ya Mfumo wa GACS**<br>Napendekeza serikali kutekeleza utambuzi wa shughuli za watumiaji kwenye mfumo, kuhakikisha mfumo unafanya kazi kwenye https na kuandaa mazingira ya majaribio ya mfumo | Serikali kupitia kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali tayari imeujaribu mfumo na mazingira yake. Mfumo utahamishiwa eGA kwa ajili ya usalama | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo mfumo wa (GACs) utathibitishwa ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 31 | 2018/19 | **Uondoshwaji wa Miamala katika Hesabu Jumuifu**<br>Napendekeza serikali iweke mkakati mahususi kwa ajili ya kuwezesha taasisi kuripoti viwango sahihi vya miamala kati ya taasisi za kiserikali na kutekeleza mfumo wa uhakiki wa viwango vinavyoripotiwa kwa ajili ya uondoshwaji ili kuboresha utoaji taarifa sahihi. | Serikali ilitoa waraka wa uhasibu no 6 wa 2019/2020 ambao unasisitiza kufichuliwa kwa shughuli za ndani ambazo zitaruhusu utekelezaji ili kuhalalisha mfumo wa takwimu zilizoripotiwa kuondoa takwimu kati ya vyombo vya Serikali vya ndani. | Majibu ya Serikali yamezingatiwa,hata hivyo nimelirudia pendekezo langu kutokana na umuhimu wake. | Pendekezo limerudiwa |
| 32 | 2018/19 | **Hesabu zilizojumuishwa zikiwa na tarehe tofauti na hesabu Jumuifu Bila Kufanyiwa Marekebisho** | Serikali kupitia menejimenti kuu ya mhasibu imetoa waraka nambari 6 wa 2019/20 kuongoza maafisa masuuli kutia saini taarifa za | Majibu ya Serikali yamezingatiwa,hata hivyo nimelirudia pendekezo langu | Pendekezo limerudiwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Narejea tena mapendekezo yangu ya miaka iliyopita kwa Serikali kuwa, tarehe za Taasisi zinazodhibitiwa ziweze kuoanishwa na tarehe ya taasisi inayodhibiti au kuandaliwa taarifa za hesabu za nyongeza na marekebisho stahiki kama matakwa ya Aya 46 ya IPSAS 35 na Waraka wa Hazina Na.12 wa tarehe 9 Januari 2015. | kifedha kwa lengo la ujumuishaji. | kutokana na umuhimu wake | |
| 33 | 2018/19 | **Taarifa kwenye hesabu jumuifu bila kusainiwa/kuidhinishwa na Afisa Masuuli au Bodi za Wakurugenzi**<br>Narejea tena mapendekezo yangu ya mwaka uliopita kuwa, Serikali ifanye majumuisho ya hesabu za Taasisi ambazo zimesainiwa na Maafisa Masuuli husika na wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 34 | 2018/19 | **Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani**<br>Kulingana na suala hili, ninapendekeza kuwa, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinapaswa kuwa huru na kupewa zana za kutosha za ukaguzi na Wafanyakazi | Serikali kupitia Idara Kuu ya mkaguzi mkuu wa ndani inaimarisha kazi ya ukaguzi wa ndani katika Sekta za Umma kupitia mafunzo juu ya ustadi wa ukaguzi wa hatari na viwango | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo ushahidi wa mafunzo utathibitishwa ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji. |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wanapaswa kupatiwa mafunzo ya ujuzi wa ukaguzi unaotokana na vihatarishi na taaluma za kihasibu. Menejimenti inapaswa kutoa msaada na kutoa rasilimali za kutosha kwa ukaguzi wa ndani, na kukubali wakaguzi walete maboresho katika Taasisi. | vingine kama ilivyoainishwa katika mfumo wa mazoezi ya kitaalam ya kimataifa (IPPF) | | |
| 35 | 2018/19 | **Mapungufu Kwenye Utendaji wa Kamati za Ukaguzi** Napendekeza Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba kamati za Ukaguzi zinachukua jukumu muhimu katika kusaidia Taasisi kutekeleza majukumu yake ya usimamizi katika maeneo kama vile kupitia ripoti ya kifedha za Taasisi, mifumo ya udhibiti wa ndani, mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na kazi za ukaguzi wa ndani na nje. Pia, kuweka sheria kwenye Kamati husika ili kuhamasisha uwajibikaji pale inaposhindwa kutekeleza majukumu yake. | Serikali kupitia wizara ya Fedha imeweka utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ili kufuatilia malipo na matumizi ya fedha. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini utathibitishwa ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji. |
| 36 | 2018/1 | **Tathmini ya Kutambua na Kuzuia** | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji | Pendekezo |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | 9 | **Ubadhirifu**<br>Napendekeza kuwa, tathmini ya ubadhilifu ifanywe na Taasisi kwa kuanzisha utaratibu wa kugundua viashiria na kuzuia ubadhilifu ili kusaidia Taasisi kupunguza matukio ya udanganyifu na ubadhilifu. | | wa mapendekezo ya ukaguzi. | halijatekelezwa. |
| 37 | 2018/19 | **Utawala Bora**<br>**Kutofanya kazi kitengo cha tathmini cha madini na vibali nje ya nchi katika Wakala wa Utafiti wa Miamba Tanzania(GST)**<br>Ninapendekeza kuwe na mawasiliano kati ya Wizara mama, Tume ya Madini na mamlaka husika juu ya utofautiano katika Sheria ya Madini ya mwaka 2017 na kanuni zake ili kufanya mapitio ya suala hilo na kuoanisha hali hiyo. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 38 | 2018/19 | **Ukosefu wa Sheria na kanuni zitakazosaidia Kituo cha uzalishaji mifugo kwa njia ya chupa (NAIC)**<br>Kwa hivyo, napendekeza Menejimenti ya Wizara na NAIC kutazama tena Sheria ambazo | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | zilianzisha Taasisi za NAIC mnamo mwaka 1972 na kuhakikisha kuwa Sheria na Kanuni husika zimetayarishwa sambamba na majukumu na malengo ya Taasisi. | | | |
| 39 | 2018/19 | **Kutokutekelezwa kwa shughuli za kupunguza VVU na UKIMWI** Hivyo, ninapendekeza Taasisi zote zihakikishe kuwa na programu za kupunguza VVU na UKIMWI kulingana na maagizo ya Serikali. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 40 | 2018/19 | **Ukosefu wa Miongozo ya Uandaaji wa Taarifa za Kihasibu** Napendekeza Maafisa Masuuli kuharakisha mchakato wa kuendeleza Mwongozo wa kihasibu ili kuleta usimamizi madhubuti juu ya fedha za umma | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 41 | 2018/19 | **Ukosefu wa Namna ya Kushughulikia Malalamiko** Kwa hivyo, napendekeza Menejimenti ziunde utaratibu mpya wa kimfumo na kumbukumbu wa utunzaji sahihi wa malalamiko yaliyopatikana kutoka kwa wadau wa TOSCI pamoja na wakulima. | Uongozi utaweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko pia rejista itaanzishwa kwa ajili malalamiko ya ndani na nje. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo nasisitiza kuwa na utaratibu wa kushughulikia malalamiko. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji. |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 42 | 2018/19 | **Kasi ndogo ya kutatua malalamiko yanayopokelewa**<br>Hivyo, ninapendekeza menejimenti ya Tume kwa kushirikiana na mamlaka husika za uteuzi wa Kamishna na Wizara ya Fedha na Mipango kutenga bajeti ya kuwezesha Tume kutekeleza majukumu yake ipasavyo. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 43 | 2018/19 | **Bodi za menejimenti za Idara ya Kumbukumbu na uhifadhi wa nyaraka kuisha muda wake**<br>Ninapendekeza Menejimenti ya Idara za Usimamizi wa Nyaraka na Kumbukumbu kuwasiliana na mamlaka zenye jukumu la uteuzi ili kufanya uteuzi wa Bodi za Ushauri na Bodi ya Waasisi wa Taifa; hatimaye kuhakikisha kwamba wajibu uliotajwa kwenye Sheria unatekelezwa | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 44 | 2018/19 | **Tathmini ya Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi**<br>Ninashauri Maafisa Masuuli kuimarisha michakato ya usimamizi wa vihatarishi kwa kuhakikisha | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuwa kuna tathmini ya vihatarishi, usimamizi wa vihatarishi, upatikanaji na utekelezaji wa mpango mkakati ulioidhinishwa ili kuwezesha Taasisi katika kufafanua dira nzima ya kufikia malengo. | | | |
| 45 | 2018/19 | **Kupitia Mifumo ya Mazingira ya TEHAMA** Ninapendekeza kwa Maafisa Masuuli wa Taasisi husika kuhakikisha usimamizi endelevu wenye ubora na viwango cha Kimataifa, Taasisi zote zilizobainika kuwa na mapungufu ya TEHAMA wapitie mifumo ya mtandao na kuhakikisha kuwa watumiaji wenye sifa na wasimamizi wa mifumo wanaangaliwa | Serikali kupitia PO-PSMGG imechukua hatua zifuatazo. i) Miongozo iliyoandaliwa ya Serikali mtandao, na viwango na miongozo ya kiufundi kuongoza Taasisi za Umma juu ya utekelezaji mzuri wa matumizi ya mipango ya Serikali mtandao. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo miongozo itathibitiwa na kukaguliwa katika ukaguzi ujao | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 46 | 2018/19 | **Kutofanya tathmini ya utoleshevu wa watumishi** Katika kuondoa changamoto ya upungufu wa watumishi, napenda kuishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kwa kuanza kutatua | Serikali kupitia POPSM imeunda mfumo mpya wa kukuza na kusimamia rasilimali watu (HCMIS), ambao pamoja na mambo mengine umekusudiwa kuwezesha urekebishaji na uwekaji upya wa | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo narudia maoni yangu ya ukaguzi | Pendekezo limerudiwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | upungufu katika Ofisi za Balozi zilizopo nchi mbalimbali kwani ndio zinatoa taswira halisi ya nchi katika utoaji wa huduma kama ilivyoonekana katika Ubalozi wa Tanazania, Geneva Uswisi ambapo watumishi waliopo wanahitajika kuwakilisha Tanzania katika shughuli za kimataifa zinazofanyika Vienna-Austria. Pia, Ubalozi wa Tanzania New York Marekani unahitajika kuwakilisha nchi katika vikao ambavyo idadi yake ni kubwa na haiendeni na watumishi waliopo; hivyo kupelekea nchi kukosa uwakilishi katika shughuli za kimataifa. | wafanyikazi ndani ya Taasisi za umma na utumishi wa umma kwa jumla. | | |
| 47 | 2018/19 | **Malipo ya matumizi ya mtandao na runinga yaliyolipwa nyumbani kwa watumishi wa Ubalozini Sh. 30,936,027.39**<br>Hivyo, ninashauri Afisa Masuuli anayehusika na Balozi kuzingatia Kanuni na Taratibu zilizoainishwa katika Kanuni za Huduma za Nje ya Nchi (Tanzania Foreign Service | Serikali kupitia wizara ya Mambo ya nje itahakikisha kwamba balozi zitazingatia sana kanuni za utumishi wa umma za huduma za kigeni. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo ninasisitiza juu ya kufuata Kanuni za Huduma za Kigeni za Tanzania katika balozi. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Regulations | | | |
| 48 | 2018/19 | **Watumishi Wanaokaimu kwa Muda Mrefu**<br>Bado naendelea kusisitiza kuwa Maafisa Masuuli wakishirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kukidhi matakwa ya kanuni za kudumu kwa kufanya uteuzi wa vyeo husika kwa wakati; halikadhalika, kuandaa mpango wa kujaza nafasi zinazotarajiwa kuwa wazi. | Utaratibu wa kuteua watumishi waandamizi wa Umma wanaohudumu katika nafasi za kukaimu unasimamiwa na Miongozo anuwai ya Utumishi wa Umma pamoja na Maagizo ya kudumu ya 2009 na kuanzishwa kwa waraka no.3 wa 2018. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo narudia maoni yangu ya ukaguzi. | Pendekezo limerudiwa |
| 49 | 2018/19 | **Makato makubwa katika mishahara ya watumishi**<br>Hivyo, naendelea kuwasisitizia Maafisa Masuuli kutoruhusu watumishi kukopa zaidi ya kipato chao; na kwa mikopo iliyochukuliwa pasipo taasisi kujua basi makato yasifanyike katika mshahara wa mtumishi husika. | Maafisa wa masuuli wa MDA wote wanapaswa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa utendaji wazi. | Majibu ya Serikali yamezingatiwa, hata hivyo nitathibitisha makato ya wafanyikazi ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 50 | 2018/19 | **Kutofanya tathmini za ufanisi wa utendaji kazi**<br>Ninaendelea kuwashauri Maafisa Masuuli katika Taasisi zote kufanya tathmini ya ufanisi kwa watendaji | Ni jukumu la maafisa masuuli kusimamia utekelezaji wa mapitio ya utendaji na mfumo wa tathmini (OPRAS) ikiwa ni pamoja na kusaini mikataba ya utendaji wa | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo bado ninasisitiza kukaguliwa mara kwa mara kwa utendaji | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wao ili tathmini hiyo itumike katika kupandisha vyeo na kuwanyima mafunzo watumishi. | wafanyikazi na tathmini ya utendaji ya wafanyakazi katika Taasisi ya Umma. | wazi na pia mafunzo na ukuzaji kufanywa kwa wafanyakazi kwa utendaji mzuri wa kazi. | |
| 51 | 2018/19 | **Malipo kwa watendaji wasiokuwapo katika utumishi wa Umma Sh. 196,131,000**<br>Bado ninaendelea kuwashauri Maafisa Masuuli kuwaondoa kwa wakati watumishi wote wasiostahili kulipwa mshahara. Pia wafanye uwianishaji baina ya taarifa zilizopo katika orodha ya malipo na uwepo wa watumishi waliohudhuria kazini. | Mfumo wa malipo ya mishahara ya Serikali (GSPP) ndio mfumo uliopo kusaidia waajiri kuidhinisha kila mfanyakazi anayepaswa kulipwa kwa mwezi husika kabla ya pesa kutolewa kwenye akaunti zao za benki | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo bado ninasisitiza juu ya uhakiki wa wafanyakazi waliopo ili kuepuka upotezaji zaidi wa mfuko wa Umma. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 52 | 2018/19 | **Uhamisho wa watumishi usiofungamana na orodha ya malipo ya mshahara**<br>Hivyo, ninawashauri Maafisa Masuuli kuwa na utaratibu wa kuhuhisha taarifa za mishahara katika mfumo wa LAWSON kwa wakati. Pia, washirikiane kwa karibu na hazina na ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma | Waajiri watasisitizwa kufanya sahihisho la kawaida kwa wafanyikazi waliohamishwa katika Mfumo (HCMIS), mfumo huu mpya umeshughulikia suala hili kwa kuboresha usimamizi wa uhamishaji wa mfanyakazi ndani ya utumishi wa umma ikiambatana mshahara. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo bado ninasisitiza kuhakikisha sitisho la kawaida la data za wafanyikazi Lawson | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | na Utawala Bora kuhakikisha kila mtumishi analipiwa mshahara katika kituo chake cha kazi | | | |
| 53 | 2018/19 | **Kutofuata sheria za wafanya kazi katika ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini**<br>Hivyo, ninawashauri Maafisa Masuuli wa Balozi husika kudumisha na kufuata sheria za ajira katika nchi husika ili kuepuka kuzorotesha uhusiano baina ya nchi na pengine kushitakiwa | Ubalozi utazingatia sheria zote za nchi hifadhi kudumisha uhusiano wa kimataifa. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo bado ninasisitiza juu ya pendekezo langu la ukaguzi kwa balozi kufuata sheria. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 54 | 2018/19 | **Uwezo wa kujiendesha kwa Wakala kwa kutumia vyanzo vya mapato ya makusanyo ya ndani katika kugharamia Bajeti za Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo**<br>Hivyo, napendekeza kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuziagiza Wakala hizi (Kutokana na aina ya shughuli zao) kuwa na uhuru wa kifedha kwa kutumia makusanyo yao ya mapato ya ndani kugharamia bajeti zao. Uamuzi huu utapunguza utegemezi wa ruzuku | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kutoka serikalini na hivyo kupelekea kiasi kitakachookolewa kupelekwa kwenye sehemu nyingine zenye uhitaji. | | | |
| 55 | 2018/19 | a)**Utoaji pungufu wa fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida Sh. 287,733,119,762**<br>Ni maoni yangu, kwamba upungufu huu unaweza kudhibitiwa pale ambapo Wakala wataelekeza rasilimali kwenye kuboresha utoaji wa huduma bora ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani itakayosaidia kuondoa tofauti endelevu ya makisio na uhalisia wa upatikanaji wa fedha.<br>b) Utoaji pungufu wa fedha za bajeti ya maendeleo - Sh. 113,584,781,943<br>Ninapendekeza kwa Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) kubuni vyanzo vipya vya mapato ya serikali ili kuhakikisha kuwa fedha inayotengwa kwenye bajeti ya Serikali inakusanywa. Pia, Wakala zinashauriwa kuboresha mapato | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | yao ya ndani ili kupunguza utegemezi wa ruzuku ya moja kwa moja kutoka Hazina<br>c) Kutofikiwa kwa makisio ya ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vya ndani kwa Sh. 142,893,900,979 | | | |
| 56 | 2018/19 | **Ukaguzi wa uhamishaji wa Mapato kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina**<br>Pia, nashauri Wakala wote kubuni njia za kuongeza mapato, na mapato hayo ya ziada yawasilishwe Hazina kuendana na Kifungu 12 (2) na (3) cha Sheria za Wakala wa Serikali ya mwaka 1997 iliyorekebishwa 2009. Vilevile, Serikali inashauriwa kupitia Sheria inayotoa muongozo wa uwasilishaji wa Makusanyo Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kuongeza Wakala wanaotakiwa kupeleka gawio ili kusaidia kuongeza wigo wa mapato ya Serikali | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 57 | 2018/19 | **Madeni ya Taasisi za Serikali Sh.1,034,281,306,562**<br>Ninapendekeza kuwa Serikali | Serikali kutekeleza mfumo wa msingi wa bajeti ya fedha. Chini ya mpangilio huu mgao wa fedha ni | Majibu ya Serikali yamezingatiwa, hata hivyo bado nasisitiza | Pendekezo lipo katika hatua ya |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kupeleka kiasi cha fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa ili kusaidia malipo ya madeni yaliyoiva. Pia, Serikali inashauriwa kufanya uhakiki kamili juu ya madeni ili kuhakikisha kuwa ni halali, hayajaongezwa na bado malipo hayajafanyika. Pia, Maafisa Masuuli wanashauriwa kuhakikisha ulipwaji wa madeni ya zamani kwanza kabla ya kuingia kwenye mikataba mipya | kulingana na kiwango cha mapato kilichokusanywa wakati kwa mwezi. | kufanya uhakiki kamili juu ya malipo yanayoripotiwa | utekelezaji |
| 58 | 2018/19 | **Madai ya Taasisi za Serikali Sh. 1,320,290,717,755**<br>Ninapendekeza kwamba Taasisi za Serikali zitafute njia fasaha za ukusanyaji wa madai kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mawakala binafsi wa ukusanyaji madeni, kutumia mpango maalumu wa Hazina wa kukusanya madeni ya taasisi za Serikali (Treasury offset programme) na njia ya mahakama. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijajibiwa |
| 59 | 2018/19 | **Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)** | Adhabu iliyotolewa kwa kucheleweshwa malipo ya IPC | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata | Pendekezo lipo katika |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | a) Riba iliyotozwa kutokana na ucheleweshaji wa malipo Sh. 224,025,668,187<br>Ninapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuja na mikakati / sera ambayo itahakikisha madeni yanalipwa pale tu muda ulioruhusiwa kimkataba unapofika. Pia, Serikali inapaswa kuzingatia ulipwaji wa madeni yaliyopo kabla ya kuamua kuingia kwenye mikataba mipya.<br>b Malipo ya awali kwa Wakandarasi yasiyo na Dhamana – Sh. 14,842,607,293<br>Ni maoni yangu kwamba, kuna hatari ya kupoteza fedha za walipakodi pale ambapo mkandarasi atatelekeza mradi kabla ya kurudisha malipo ya awali. Kwa hivyo, napendekeza menejimenti ya TANROADS kuongeza usimamizi wa kutosha na kuhakikisha kuwa malipo haya ya awali yanalindwa na dhamana au fedha yote imerejeshwa na | ilitokana na kucheleweshwa kwa fedha kutoka kwa Serikali.TANROADS imelipa Sh. 151,801,905,931.18 kati ya Sh. 224,025,668,187 zilizowekwa kama riba kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Januari 2020.<br>Uongozi wa TANROADS umekuwa ukishughulikia suala hili kuhakikisha kuwa mikataba yote imetekelezwa kikamilifu | hivyo bado ninasisitiza kupata kiasi kilichobaki. | hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mkandarasi husika. | | | |
| 60 | 2018/19 | **Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA**<br>a)Ukarabati wa kivuko cha MV. Misungwi katika Kituo cha Kigongo – Busisi mkoani Mwanza<br>b) Ununuzi wa kivuko kipya kitakachofanya safari kati ya Chato - Mharamba na Nkome wilayani Chato<br>c) Ununuzi wa kivuko kipya kitakachofanya safari kati ya Mafia na Nyamisati, wilaya ya Mafia mkoani Pwani<br>d) Ukarabati mkubwa wa kivuko cha MV – Kigamboni mkoa wa Dar es Salaam<br>e) Ununuzi wa Kivuko Kipya kitakachofanya safari Kati ya Kayenze na Bezi, Wilaya ya Ilemela Mkoani Mwanza<br>Ni maoni yangu kwamba udhaifu ulioainishwa hapo juu umechangiwa na uwezo mdogo wa Wakala katika kusimamia miradi. Hii inaweza sababisha kukosekana | Jitihada zinaendelea kuhakikisha kuwa usimamizi wa kutosha katika miradi yote inayotekelezwa, inaboreshwa pia udhibiti wa ndani umekuwa ukiimarishwa | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo ukaguzi wa miradi hii utafanywa ukaguzi ujao kuhusu utendaji wao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kwa thamani halisi ya Fedha Kwa hivyo, napendekeza menejimenti ya TEMESA ihakikishe miradi yote inasimamiwa vizuri na inakamilishwa ndani ya wakati. Pia, kubuni njia madhubuti ya usimamizi wa ndani juu ya usimamizi wa miradi na kuwawezesha watumishi wa wakala kwa mafunzo ya ugavi na usimamizi wa mikataba. | | | |
| 61 | 2018/19 | **Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA**<br>a)Hasara iliyopatikana kutokana na usimamizi usioridhisha wa Manunuzi na Mikataba - Sh. 280,351,400<br>b) Kukosekana kwa usawa uliopelekea Mzabuni mwenye bei ya chini kuondolewa kwenye mchakato wa Zabuni na kusababisha hasara ya Sh. 44,956,000<br>c) Hasara iliyotokana na mpango duni wa manunuzi Sh. 150,377,400 | Mameneja wa Mikoa waliamriwa kupitia barua iliyo na Kumb. Na. EB.29 / 345.01 / 23 ya tarehe 23/4/2020 kuteua washiriki waliohitimu katika timu zao za tathmini ili kuepusha kurudia makosa kama hayo wakati wa tathmini ya zabuni. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo ukaguzi wa muundo wa timu zilizoteuliwa utafanywa ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | d) Hasara iliyotokana na kushindwa kudai fedha ya Dhamana ya utendeji kazi wa Mkandarasi kwa mkataba uliovunjwa – Sh. 54,074,000<br>e) Hasara iliyotokana na malipo ya kazi za ujenzi wa barabara ambazo hazikufanyika – Sh. 30,944,000<br>f) Ongezeko la Mkataba Zaidi ya Asilimia 15 bila idhini ya Mamlaka inayopitisha bajeti na Bodi ya Wazabuni Sh. 188,251,059<br>Kwa hivyo napendekeza menejimenti ya TARURA kufuata maelekezo ya Kanuni ndogo. 110 (4) na (5) ya PPR, 2013 (iliyorekebishwa mwaka 2016) na pia, upungufu wa kutofuata kanuni za manunuzi uchunguzwe na hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika | | | |
| 62 | 2018/ 19 | **Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**<br>a)Hasara iliyopatikana kwa kuhamisha eneo la ujenzi baada ya kazi za ujenzi kuanza Sh. 691,451,121 | Serikali itahakikisha kuwa katika mwaka ujao wa fedha itatenga bajeti ili kurudisha fedha zilizokopwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo uhakiki utafanywa katika ukaguzi ujao juu ya marejesho ya kiasi | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ni maoni yangu kwamba, hasara iliyopatikana imetokana na uzembe wa Halmashauri ya Babati; kwa hiyo, napendekeza Wakala kutafuta gharama halisi ya hasara na kiasi hicho kifidiwe na Halamashauri husika. Pia, napendekeza OR-TAMISEMI wachunguze uzembe wa ugawaji hati mbili kwa kiwanja kimoja na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wahusika.<br>b) Kutorudishwa kwa kiasi kilichokopwa na Wizara ya Kilimo Sh. 301,191,597.55<br>Ni maoni yangu kuwa, ukopaji huu wa mara kwa mara wa Wizara kwa Wakala unatakiwa kuzuiliwa kwa sababu unaathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa kwenye bajeti ya mwaka ya Wakala kutokana na kutokuwapo kwa uhakika katika urudishwaji wa mikopo husika. Kwa hivyo napendekeza Serikali kupitia kwa Katibu Mkuu | | kilichokopwa na pia halmashauri husika kufidia hasara iliyopatikana ya Sh.691,451,121 | |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiongozi kutoa maagizo madhubuti yatakayodhibiti ukopeshaji kati ya taasisi za Serikali. Pia, napendekeza kwa Wizara ya Kilimo kurudisha kiasi baki cha mkopo kwa NFRA. | | | |
| 63 | 2018/19 | **Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)**<br>a)Udhaifu uliobainika katika Ujenzi wa Majengo ya Serikali<br>b) Usanifu na Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).<br>c) Mapitio ya Usanifu, Uboreshaji na Ujenzi wa Jengo la Makao makuu ya TANROADS kwenye Kiwanja Na.8, Kitalu 'F' katika eneo la Uwekezaji la Njedengwa Manispaa ya Dodoma<br>d) Usanifu na Ujenzi wa Makao makuu na Ofisi ya Kanda ya Tume ya Maadili katika Mkoa wa Dodoma<br>Hivyo basi, napendekeza menejimenti ya TBA kuelekeza rasilimali zake katika kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa | Uongozi wa wakala wa majengo Tanzania (TBA) kutumia rasilimali zake kufanikisha lengo lake la kimsingi la kutoa huduma za ushauri kwa Serikali na kutengeneza mikakati inayofaa katika tasnia ya ujenzi. | Jibu la Serikali limezingatiwa hata hivyo, bado nasisitiza juu ya mikakati inayoendelea ya TBA kuweza kumudu changamoto katika tasnia ya ujenzi. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | huduma ya ushauri huku wakitengeneza mbinu sahihi zitakazowawezesha kufanya kazi za ujenzi kwa ufasihi. | | | |
| 64 | 2018/19 | **Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA)**<br>a) Utelekezaji wa Mashine za Majaribio ya Kusukuma Maji kwa Kipindi cha Miaka 6 - Sh. 840,000,000<br>Ninapendekeza kwa menejimenti ya DDCA kutafuta suluhisho mbadala la kuhakikisha kuwa vifaa hivi vinatumika kufikia lengo lililokusudiwa. Pia, napendekeza udhaifu ulioainishwa kuchunguzwa na taasisi za uchunguzi ili kubaini kama kuna uzembe wowote katika hatua ya ununuzi | Ili kutumia jenereta, injini na vifaa vingine vya vitengo vya majaribio ya kusukuma vilivyowekwa kwenye trela, sasa tunazuia vitengo hivyo na kuzipachika kwenye magari yetu na kuzitumia kufanya shughuli za majaribio ya kusukuma maji. | Jibu la Serikali limezingatiwa,hata hivyo bado nasisitiza kwa pendekezo langu juu ya DDCA kuhakikisha kuwa mashine zinatumika kufikia lengo lililokusudiwa | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 65 | 2018/19 | **Masuala yaliobainika katika Kaguzi za Taasisi za Serikali Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)**<br>a) Mwenendo mdogo wa utoaji wa Nambari na Kadi za Vitambulisho vya Taifa | Pendekezo halijajibiwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hivyo, napendekeza menejimenti ya NIDA kuharakisha mchakato mzima wa utoaji wa nambari za vitambulisho vya utaifa ili kuwezesha watumiaji wa simu za mkononi kufuata maagizo ya TCRA ya kuhakikisha laini zote za simu zinasajiliwa<br>b) Uwezekano wa Hasara kutokana na kutokukusanywa kwa Malipo ya awali yaliyofanywa kwenye Mkataba ulioisha muda wake – Sh. 28,215,446,470<br>Napendekeza kwa Menejimenti ya NIDA kufidia deni la malipo ya awali la Sh. 28,215,446,470 na madai ya mkandarasi yenye thamani ya Sh. 13,651,584,240.42 na kuhakikisha kiasi kilichobakia cha Sh. 14,563,862,229.58 kinakusanywa kutoka kwa Mkandarasi. Pia, wizara mama (Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi) ifuatilie kuhakikisha Mamlaka inakusanya deni hilo<br>c) Upotevu wa Vifaa vinavyosaidia | | | |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mashine za Biometrika za Uandikishaji wa Wapiga kura (BVR) Kwa hivyo, napendekeza NIDA ichukue hatua za haraka kuhakikisha upatikanaji mbadala wa vifaa vyote vilivyopotea ili kurejesha kasi ya uandikishaji. Pia, NIDA inashauriwa kuhakikisha usalama wa vifaa vya usajili na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa ili kurejesha vifaa vilivyopotea pamoja na hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wahusika wa wizi | | | |
| 66 | 2018/ 19 | **Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Kwa hivyo, napendekeza REA:**<br>a) Kasi ndogo ya kuunganisha umeme kwa wateja wa maeneo ya Vijijini<br>kuwa na mpango wa uhamasishaji ili kuelimisha jamii ya vijijini umuhimu wa umeme katika kuinua uchumi wao;<br>(b) kuwataka wakandarasi wote kuwasilisha ratiba za upokeaji wa vifaa na kuhakikisha kufuatwa kwa | Wakala unafanya kampeni uhamasishaji kwa maeneo yote ya mradi kupitia redio za mitaa / jamii na vipindi vya Runinga kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa umeme na matumizi yake kwao kuweza kuchukua hatua haraka juu ya fursa zilizopo za kuungiwa umeme kwa Sh. 27,000 / =<br>Serikali kupitia POSM imechunguza suala hilo na kuthibitisha kuwa ilikuwa na idhini sahihi kupitia | Jibu la Serikali limezingatiwa,hata hivyo<br>Uhakiki wa vielelezo vilivyoainishwa utafanyika ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | masharti ya mkataba yanayohusu uwasilishaji wa vifaa kwa wakati<br>c) Ulipaji wa Mishahara kwa Wafanyakazi wasio hudumu kwenye Wakala wa Nishati Vijijini - Sh. 146,021,086.40<br>Hivyo, napendekeza menejimenti ya REA kuhakikisha kunakuwa na udhibiti madhubuti juu ya usimamizi wa mishahara. Pia mapungufu haya yachunguzwe na OR-UTUMISHI ili kuhakikisha kwamba watumishi hao hawanufaiki na mshahara miwili. | barua Kumb. Na. MNRT / PF / 3633/19 ya tarehe 12/06/20 19 na CCD.92 / 273/01 / D / 45 ya tarehe 18/12 / 2019. Zaidi ya hayo, iligundulika kuwa mshahara wa wafanyikazi uliohamishwa ulipangwa na wakala kabla ya kuhamishiwa kwa Taasisi zingine na viwango vyao vya mishahara vilikuwa juu ikilinganishwa na mishahara ya Taasisi zilizowapokea. | | |
| 67 | 2018/19 | **Kampuni ya Mzinga Holding Limited**<br>a) Hasara iliyotokana na Miradi ya Ujenzi, Sh. 318,150,958.15<br>Kwa hivyo, napendekeza menejimenti ya Kampuni ya Mzinga Holding kujumuisha gharama zote za mradi kutokana na uhalisia wa soko katika kipindi cha kuomba Zabuni. Pia, nashauri upitiaji wa kina wa michoro na bili ya vipimo na kuonesha mapungufu yoyote | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kabla ya kuingia mkataba.<br>b) Masurufu yaliyotolewa kwa watumishi wasiohudumu kwenye kampuni – Sh. 626,881,740<br>Hivyo, napendekeza Kampuni ya Mzinga Holding kuwasilisha ushahidi wa watumishi waliohamishiwa kwenye kampuni; na kama itashindikana kiasi hicho kilichotolewa kwa watumishi hao kirudishwe..<br>c) Malipo pungufu ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) Sh. 306,848,832.34<br>Hivyo napendekeza kwa Menejimenti ya Kampuni ya Mzinga kuwasilisha Kiasi hicho cha Sh. 306,848,832.34 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Pia, Mamlaka ya Mapato inashauriwa kufanya ukaguzi wa kodi kwenye nyaraka za Kampuni ili kubaini kama kuna uvunjaji wowote wa Sheria ya Kodi | | | |
| 68 | 2018/ 19 | **shirika la Mzinga**<br>a) Kutofanyiwa kazi kwa Mpango Mkakati wa Shirika | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hivyo, napendekeza menejimenti ya Shirika la Mzinga kuunda mpango mkakati mpya utakaojumuisha shughuli zote ambazo zinafanyika lakini hazikuelezwa kabla na kuondoa malengo yasiyotekelezeka ili kutoa mwelekeo madhubuti kwa ukuaji wa Shirika. | | | |
| 69 | 2018/19 | **Kikosi Kazi cha Jeshi la Polisi Tanzania (TPFCS)**<br>a) Ukosefu wa Mapato kwa muda wa miaka mitatu mfululizo<br>Hivyo basi, napendekeza kwa Waziri wa Mambo ya Ndani kuangalia vizuri uhitaji wa TPFCS; kama itaonekana haina umuhimu tena nashauri ivunjwe ili kupunguza taasisi za serikali ambazo hazina faida | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 70 | 2018/19 | **Masuala yaliyobainika kwenye Kaguzi za Bodi za Mabonde ya Maji**<br>Utoaji pungufu wa fedha za Mpango wa maendeleo wa Maji (WSDP) Kwa Sh. 31,299,787,199.39 | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Maswa<br>Kutowasilishwa kwa Pampu zilizonunuliwa tokea Machi 2017 – Sh. 76,670,000<br>Ninapendekeza kwa Bohari Kuu ya Maji kurudisha malipo yaliyofanywa ya manunuzi hayo pamoja na riba ya mkopo kutoka Benki Kuu ya Tanzania kuanzia tarehe ya malipo ya awali mpaka tarehe ya kufanyika marejesho hayo. Pia, Wizara ya Maji inashauriwa kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo hayo. | | | |
| 71 | 2018/19 | **Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Maswa**<br>**Bomba la Kuelea ambalo halijawasilishwa Tangu Machi 2017; Shilingi 76,670,000**<br>Ninapendekeza DDCA kurudisha kiasi hicho kilichokopwa kutokana na riba inayoendana na Benki kuu ya Tanzania kutoka tarehe ambayo kilipochukuliwa hadi tarehe ambayo kiasi kitarudishwa. | Serikali ilivunja DDCA na mali zote na mambo mengine yote yanayoihusu yalihamishiwa DAWASA. DAWASA imeagizwa kukagua na kufanya ufuatiliaji wa ununuzi wa pampu ya kuelea | Majibu ya Serikali yamezingatiwa, hata hivyo nasisitiza utekelezaji wa pendekezo langu la ukaguzi. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ninashauri Wizara ya Maji ifuate utekelezaji wa mapendekezo haya | | | |
| 72 | 2018/19 | **Masuala yaliyobainika katika Kaguzi za Mifuko maalumu**<br>a) Kutohamishwa kwa ushuru wa Mafuta na Usafirishaji kwenda Bodi ya Mfuko wa Barabara - Sh. 7,063,022,941<br>Hivyo basi, napendekeza kwa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhamisha kiasi kilichobaki cha Sh. 7,063,022,941 kwenda Mfuko wa Barabara. | Serikali kupitia Wizara ya fedha na mipango imepanga kuhamisha kiwango kilichobaki kwa mafungu ya takriban bilioni mbili kwa mwezi. Kufikia 31 Mei, 2020 kiasi cha Sh. 4,720,869,494.63 tayari kimehamishiwa kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara ikiacha kiasi cha Sh. 2,342,153,463.37 | Majibu ya Serikali yamezingatiwa ,hata hivyo nasisitiza utekelezaji wa pendekezo langu la ukaguzi kwa kurejeshwa kiasi kilichobaki cha Sh. 2,342,153,463.37 | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 73 | 2018/19 | **Masuala yaliobainika wakati wa Kaguzi wa Hospitali za Rufaa za Mkoa**<br>Ninapendekeza kwa Serikali kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa rasilimali watu na vifaa ili kuwezesha utoaji wa huduma bora; Pia, Wizara ya Afya inashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kuhusu utoaji wa taratibu | Serikali kupitia MoHCDGEC imechukua hatua kadhaa kushughulikia changamoto ya uhaba wa wafanyikazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa. | Jibu la Serikali limezingatiwa, nitathibitisha mipango ya ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ya uanzishwaji wa Bodi ya Zabuni kwa Hosptali hizi; na mwisho napendekeza kwa Hospitali ziboreshe udhibiti wa ndani ili kupunguza hasara ya madai kukataliwa na Mfuko wa Bima ya Afya. | | | |
| 74 | 2018/19 | **Mambo Mtambuka Yaliyobainika Katika Ukaguzi wa Wakala, Mifuko Maalumu ya Fedha, Bodi za Mabonde ya Maji, Taasisi Nyingine za Serikali na Hospitali za Rufaa za Mikoa**<br>a)Matumizi yenye nyaraka pungufu ya Sh. 2,207,923,905.90<br>Ninapendekeza uboreshaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani kwa kuimarisha uangalizi, ufuatiliaji na uboreshaji wa mifumo kielotroniki ili kupunguza matumizi mabaya yanayotokana na matumizi haya yenye nyaraka pungufu. Kwa kufanya hivyo, thamani ya fedha ya matumizi ya fedha za umma itapatikana; pia kupunguza upotoshaji katika taarifa ya | Serikali kupitia mhasibu mkuu imetoa Waraka Na. 6 wa 2019/2020 ambao unatoa mwongozo kwa maafisa masuuli kuzingatia na kufuata Sheria na Kanuni zinazosimamia uwajibikaji wa Fedha za Umma. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo ufuatiliaji zaidi utafanywa ili kuhakikisha kufuata kamili kwa sheria iliyotolewa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kifedha<br>b) Malipo yaliyofanyika bila kudai Risiti za Kielekitroniki (EFD) – Sh. 1,388,736,882.86<br>Bado ninasisitiza katika pendekezo langu la mwaka uliopita kwa taasisi za Serikali kudai risiti za EFD wakati wa kufanya malipo kama inavyotakiwa na Kifungu 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru, ya mwaka 2015; Pia, taasisi hizi zinahimizwa kuacha kufanya biashara na Wauzaji ambao hawatumii mashine za EFD.<br>c) Masurufu yasiyorejeshwa ya Sh. 3,278,769,064.56<br>Kutokana na Kanuni 103 (2) ya PFR, 2001, masurufu yanatakiwa kufanyiwa marejesho ndani ya siku 30 kabla ya mwaka wa fedha kuisha, tokea masurufu yalipotolewa. Hivyo, napendekeza masurufu ambayo hayajarudishwa kwenye kipindi tajwa kukombolewa kutoka kwa wahusika. | | | |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | d) Kutowasilishwa kwa Kodi ya Zuio kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania – Sh. 521,458,769.60<br>e) Matumizi yaliyofanyika nje ya Bajeti | | | |
| 75 | 2018/19 | **Mapungufu kwenye usimamizi wa Ununuzi**<br>a) Ununuzi uliofanyika bila kuwapo mkataba/ makubaliano Sh. 280,998,828<br>Nashauri menejimenti ya Taasisi za Serikali: (a) kuhakikisha shughuli yoyote ya manunuzi inakuwa na mikataba ya makubaliano;<br>(b) Kuhakikisha ushindani katika mchakato wa utoaji wa zabuni kama Kifungu. 163 & 164 cha Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013. Aidha, nashauri wanasheria katika taasisi za serikali husika kushauri vizuri jinsi ya kuboresha udhibiti juu ya usimamizi wa mkataba. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 76 | 2018/19 | **Mapungufu ya Ujumla ya kutozingatiwa kwa Sheria**<br>**Mapungufu yaliyobainika katika** | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Mkataba wa ununuzi wa Mahema ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi yenye thamani ya Sh 6,306,146,740**<br>a)Tathmini ya kina (Due diligence/post qualification) ya kumpata Mzabuni haikufanyika<br>b) Vipimo, maelezo na ubora (Specifications and quality) wa Mahema kutojumuishwa kwenye mchakato wa Zabuni<br>C)Maoni ya Mwanasheri Mkuu wa Serikali kutojumuishwa katika Mkataba<br>d) Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuchelewesha Malipo ya awali kwa Mzabuni<br>e) Nyongeza ya muda wa Mkataba<br>Kutokana na mapungufu yaliyobainika hapo juu, nilibaini kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilishindwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mkataba wa ununuzi wa Mahema. Hivyo, napendekeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhakikisha inasimamia | | | |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kikamilifu Mkataba huo ili Serikali iweze kupata thamani halisi ya fedha | | | |
| 77 | 2018/19 | **Ununuzi wa vifaa na huduma nje ya Mpango wa ununuzi wa Mwaka Sh 3,605,775,412**<br>Nashauri Taasisi za Serikali Kuu kuzingatia mpango wa ununuzi wa mwaka. Vilevile natoa wito kwa menejimenti ya taasisi husika kufanya utafiti ili kupata taarifa za kutosha katika kuandaa mpango wa ununuzi wa mwaka unaoendana na bajeti ya Taasisi husika. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 78 | 2018/19 | **Mapungufu yaliyobainika katika Mkataba wa ununuzi wa betri, viunganishio na vifaa vingine vya kubadilishwa katika Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Sh 1,647,512,344**<br>Naishauri Wizara katika ununuzi wa aina hii kushirikiana na TTCL katika mchakato mzima wa ununuzi, ikiwa ni pamoja na kuteua kamati ya ukaguzi na mapokezi ya vifaa, ili kuweza kujihakikishia thamani | Mkongo wa kitaifa wa ICT Broadband (NICTBB) ni wa Serikali ni huduma ya mtandao ambayo inasimamiwa na wizara ya Ujenzi, uchukuzi na mawasiliano | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo, nasisitiza juu ya thamani ya pesa kupatikana kutoka kwa manunuzi ya Serikali | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | halisi ya fedha inapatikana | | | |
| 79 | 2018/19 | **Ununuzi wa Vifaa na huduma bila mikataba Sh 5,460,101,227**<br>Ni muhimu Ununuzi wa Umma ukaambatishwa na nyaraka za kutosha za mikataba; ili, kama kutatokea mmoja kushindwa kutimiza makubaliano, ziweze kukubalika mbele ya sheria. Ili kushughulikia mapungufu katika kuvunja Sheria za ununuzi katika Taasisi za umma, nashauri Taasisi zizingatie sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake kwa kuingia makubiliano ya Mikataba inayokubalika mbele ya Sheria. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 80 | 2018/19 | **Ununuzi wa viatilifu ambavyo havikusambazwa kwa walengwa vyenye thamani ya Sh 3,341,158,850**<br>Ni maoni yangu kuwa kushindwa kusambaza madawa hayo kwa Wakulima kwa wakati kunaweza kupelekea Serikali kupoteza fedha kutokana muda wa matumizi madawa hayo kuisha. Ninashauri | Serikali kupitia wizara ya kilimo itaendelea kuzingatia kutoa kiwango cha chini kinachohitajika cha kemikali ya kilimo zenye muda mrefu wa matumizi kama bafa ya dharura. Kati ya lita 113,178 za kemikali zilizozingatiwa wakati wa ukaguzi wa lita 89,409 zimesambazwa kubaki na lita 23,769 katika hisa. Usambazaji wa | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo orodha ya usambazaji itathibitishwa ukaguzi ujao | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | menejimenti ya Wizara ya Kilimo (Fungu Na 43) kuchukua hatua za haraka kusambaza madawa hayo kwa wakulima. | hisa zilizobaki utaendelea kadri mahitaji yanavyotokea | | |
| 81 | **2018/19** | Ripoti ya Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) ikizingatia jinsi Taasisi za Serikali Kuu zilivyozingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016 na Kanuni zake za Mwaka 2013 (zilizorekebishwa mwaka 2016) | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 82 | 2018/19 | Taratibu za Manunuunuzi ya muda mrefu ambayo hayaendani na Mazingira ya Ubelgiji ya Ukarabati wa Nyumba ya Makazi na Ofisi ya Chancery.<br>Ninapendekeza uongozi kuwasiliana na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa mwongozo wa utekelezaji wa ununuzi katika nchi za kigeni. Ninapendekeza pia kupatikana kwa pauni 9,279.66 sawa na Sh. 24,470,463.42 kutoka kwa | Serikali kupitia wizara ya mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imechukua hatua za kuendelea na mchakato wa ununuzi wa ukarabati wa majengo ya ofisi. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo nasisitiza kuwasiliana na PPRA kufuata mwongozo wa utekelezaji wa ununuzi katika nchi za kigeni. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | walengwa waliotumiwa kwa shughuli zisizotarajiwa. | | | |
| 83 | 2018/19 | **Mapokezi ya Vifaa visivyokaguliwa Sh 1,620,940,789** Kupokea vifaa bila kukaguliwa na kukubaliwa na kamati ya ukaguzi na mapokezi ya vifaa na huduma kunaweza kukatoa fursa kwa taasisi za umma kununua vifaa na huduma zisizokuwa na viwango au zisizofuata mahitaji ya ununuzi. Nawashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi za Serikali Kuu kuteua kamati ya mapokezi na ukaguzi wa vifaa na huduma pale inapotokea Taasisi husika imefanya ununuzi wa vifaa na huduma. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 84 | 2018/19 | **Mapungufu yaliyobainika katika Ujenzi wa Mahakama kumi na Sita (16) zenye thamani ya Sh 10,351,638,077** Ni maoni yangu kwamba, kuendelea kuchelewa kwa Mradi huu kunaweza kupoteza rasilimali za umma; hivyo naishauri Mahakama kuongeza umakini | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | katika ufuatiliaji wa mradi huu ili ukamilike kwa wakati | | | |
| 85 | 2018/19 | **Vifaa vilivyonunuliwa bila kuingizwa kwenye Vitabu vya Stoo Sh 5,493,672,843**<br>Napendekeza Taasisi zote za Serikali Kuu zihakikishe zinaingiza vifaa/mafuta kwa wakati katika vitabu ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali katika kutoa huduma kwa wa. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 86 | 2018/19 | **Wakala wa Ugavi na Huduma za ununuzi (GPSA) ulifanya ununuzi wa basi lisilokidhi viwango Sh 508,288,800**<br>Naishauri Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na GPSA kufanya ufuatiliaji wa karibu wa basi jipya ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa. | Wizara ilipokea barua yenye Rejea Na. AE/005/HQ/2017-18/TPP/G/14/01 ya tarehe 24/12/2019 kutoka GPSA ikifahamisha kuwa m / s Scania akubali kupeleka basi mpya kuchukua nafasi ya lile la kwanza.Walakini, menejimenti itaendelea kufuata wakala wa huduma za ununuzi wa Serikali kuchukua nafasi ya basi mpya kwa barua yetu ikiwa na rejea Na .CEA.165 / 228 / 01A / 136 ya tarehe 06/05/2020 | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo nasisitiza juu ya kubadilisha mabasi ya zamani na kupata mapya, pia taratibu za kinidhamu dhidi ya maafisa waliohusika katika ununuzi huu na na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya muuzaji | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 87 | **2018/** | Ununuzi usioidhinishwa na Bodi ya | Pendekezo halijajibiwa | Nasisitiza utekelezaji | Pendekezo |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | **19** | Zabuni Sh. 459,681,496 | | wa mapendekezo ya ukaguzi | limerudiwa |
| 88 | **2018/ 19** | **Mapungufu yaliyobainika katika Mkataba wa ukusanyaji mapato kwenye Viwanja vya Taifa na Uhuru**<br>Hivyo, naishauri Wizara kuboresha ufuatiliaji wa mkataba wa makusanyo katika viwanja vya Taifa na Uhuru ili Serikali isipate hasara. Pia nashauri Afisa Masuuli azingatie miongozo ya Serikali katika Ununuzi | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 89 | **2018/ 19** | **Vifaa na huduma zilizolipiwa lakini hazikupokelewa Sh 587,652,750**<br>Nashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa wazabuni wanazingatia vipengele vya mikataba walivyokubaliana pamoja na kukamilisha mikataba yao bila kuchelewa zaidi. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 90 | **2018/ 19** | **Kuchelewa kukamilika kwa kazi za ujenzi zenye thamani ya Sh 22,312,690,753**<br>Pia, nazishauri taasisi husika | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kufuatilia wa fedha Hazina ili kuweza kutekeleza miradi hiyo kwa wakati. Vilevile, napendekeza mikataba ifanyike kwa awamu ili kuweza kuiepusha Serikali na riba itokanayo na kuchelewa kulipa madai ya Wakandarasi. | | | |
| 91 | **2018/19** | **Gharama zenye shaka za kukodi ndege binafsi Sh.20,976,000** Wizara inapaswa kutoa hoja za msingi zilizosababisha kutumia ndege binafsi, badala ya kutumia ndege za Serikali | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 92 | **2018/19** | Ripoti ya PPRA kwa Ufuataji wa MDAs na Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 (iliyorekebishwa 2016) na Kanuni zake za 2013 (kama ilivyorekebishwa mnamo 2016)<br>Ukaguzi ulitafuta kubaini ikiwa mikataba imekuwa ikitekelezwa au ilikuwa ikitekelezwa kwa mujibu wa masharti ya mikataba na ikiwa malengo na thamani ya pesa ilifanikiwa katika matumizi ya fedha za umma. Kulingana na | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | rasilimali zilizopo na vigezo vya uteuzi wa PEs kukaguliwa, PPRA iliweza kufanya ukaguzi kwa PE 104 zilizo na MDA 43 | | | |
| 93 | **2018/19** | **Dosari katika kuhaulisha fedha za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu Dodoma Sh. 1,746,146,300**<br>ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu na zaidi kufanya ufuatiliaji kwa kushirikisha vyombo vya kiuchunguzi ili kuthibitisha uwajibikaji wa Sh. 1,746,146,300. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 94 | **2018/19** | Dosari kwenye malipo yaliyofanywa na Jeshi la Polisi katika ujenzi wa majengo Sh. 806,685,000<br>a)Gharama za vibarua zililipwa miezi saba kabla ya kununua vifaa vya ujenzi Sh. 355,200,000<br>b) Gharama za vibarua zililipwa kwa mtu binafsi badala ya fundi mchundo Sh. 145,200,000<br>c) Gharama za vibarua zililipwa zaidi katika ujenzi wa nyumba 30 zilizoko Medeli Mashariki Dodoma | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Sh. 92,640,000<br>d) Gharama za vibarua kwenye ujenzi wa nyumba 30 zilizoko Medeli ya Mashariki Dodoma ambazo hazikuwa kwenye bajeti Sh. 105,000,000<br>e) Malipo yaliyozidishwa katika ujenzi wa nyumba za wafanyakazi Sh. 54,000,000<br>f) Bidhaa hewa zilizolipiwa kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Polisi Dodoma Sh. 54,645,000<br>g) Kutelekezwa kwa shughuli za ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Polisi<br>Ni maoni yangu kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kutumia vibaya fedha za Serikali, hivyo kuzuia kufikia malengo yaliyokusudiwa na kuchelewa kutekeleza kazi ambazo zimekwishalipiwa kunaweza kupelekea kuomba hela zaidi na kusababisha uwezekano wa kufanya malipo mara mbili kwa | | | |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | sababu ya ufuatiliaji hafifu. Menejimenti ya Jeshi la Polisi inashauriwa:<br>(a) kuimarisha udhibiti na kufanya ufuatiliaji wa karibu katika kusimamia kazi ambazo hazijakamilika<br>(b) kuchukua haraka hatua stahiki kwa wahusika wote waliolipwa na hakuna kazi iliyofanyika na<br>(c) Kuhakikisha Kamati zinafanya kazi hizi muhimu ambazo zinapaswa kuelezwa vizuri kwenye uteuzi wao. Aidha, napendekeza kuwa menejimenti ya Jeshi la Polisi kuwa makini sana katika kutumia utaratibu wa kujenga bila kutumia wakandarasi (Force Account) kwa kufanya usimamizi wa karibu sana na kuwa na uwajibikaji wenye ufasaha, vinginevyo utaratibu huu unaweza kupelekea kuwapo kwa utovu wa nidhamu ya fedha. | | | |
| 95 | **2018/ 19** | Gharama kubwa za kukodi viti, mahema na Magari binafsi katika | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya | Pendekezo halijatekelez |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Jeshi la Wananchi wa Tanzania Sh. 489,801,253.13<br>Kwa siku za usoni, inapendekezwa kununua viti, mahema na magari ili kupunguza gharama za kukodi na kuepuka kuingia gharama kubwa kila mwaka wa fedha | | ukaguzi | wa |
| 96 | **2018/19** | Risiti ya kielektroniki yenye udanganyifu iliyopokelewa na Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga Sh. 70,000,000<br>Napendekeza kuwa menejimenti ya Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga kuzifahamisha Mamlaka ya Uchunguzi ili kubaini chanzo cha tatizo. Licha ya hiyo, Serikali kwa ujumla ihakikishe Wazabuni wanakiri mapokezi kwa kutumia risiti za Kielektroniki za ukweli katika malipo ya vitu na huduma. | Suala hilo liliripotiwa kwa Mamlaka ya mapato Tanzania kwa hatua stahiki kuchukuliwa kwa muuzaji anayehusika kwa maandishi kwa kumbukumbu Na.EA.230 / 258/03/17 ya tarehe 17/1/2020 na TRA ilijibu ipasavyo na barua zao zenye kumbukumbu Na.TRA. 30RM / 19 / CPO / 39 / VOL.1 / 195 ya tarehe 21/04 / 2010. Kwa kuongezea, usimamizi wa RAS uliandika barua ya kufuata kwa TRA yenye nambari ya kumbukumbu EA.23 / 258/03/46 ya tarehe 04/04/2020. | Majibu ya Serikali yamezingatiwa, hata hivyo menejimenti ya Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga inapaswa kufahamisha mamlaka ya uchunguzi ili kubaini chanzo cha tatizo hili. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 97 | **2018/19** | **Kutotumika ipasavyo kwa akaunti ya masurufu katika Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga Sh. 615,737,000** | Maagizo kutoka hazina ya kutohamisha fedha za maendeleo ambao hazijatumika kwenda Akaunti ya Amana kama ilivyokuwa | Majibu ya Serikali yamezingatiwa, hata hivyo nitathibitisha utaratibu wa ununuzi | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ni mapendekezo yangu kuwa malipo yote yafanyike kwa kutumia hundi zilizofungwa au kulipa Wazabuni moja kwa moja kwa kutumia mfumo wa kufanya malipo kwa njia za kibenki (TISS) baada ya kukamilisha taratibu za manunuzi na kuepuka kutumia akaunti ya masurufu. | katika mwaka wa fedha uliopita 2017/2018, hivyo kuwa na pesa nyingi zilizopokelewa kwa ajili ya kazi ya ujenzi iliyokubaliwa na mabadiliko ya sera ya kutumia "Force akaunti" kwa madhumuni yaliyokubaliwa, hapo hakukuwa na njia mbadala bora zaidi ya kulipa kupitia akaunti ya "RAS imprest". | uliotumiwa katika ukaguzi ujao | |
| 98 | **2018/ 19** | **Miamala yenye udanyanyifu katika Ofisi ya Hazina ndogo Morogoro Sh. 71,958,000**<br>Napendekeza kuwa, Menejimenti ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ifanye ufuatiliaji wa karibu kwa ajili ya uwajibikaji. Pia, Ofisi ndogo zinapaswa kuimarisha udhibiti wa ndani ulio bora ikiwemo mgawanyo wa majukumu, kufanya kwa wakati usuluhisho wa kibenki, kufanya mahesabu ya fedha taslimu kwa kushutukiza na kufanya tathmini za mara kwa mara juu ya viashiria vya udanyanyifu | Uongozi umeweka hatua za kudhibiti, kama mgawanyo wa majukumu ambayo hupunguza nafasi za kufanya makosa na ulaghai .Pia upatanisho katika mfumo umeboreshwa ambao unaweza kufanywa kila siku. Hizi zitawezesha kutambua makosa mara moja. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo ufuatiliaji wa karibu unapaswa kufanywa kupata maafisa wanaohusika pia udhibiti ufanywe ili kuepuka kitendo hicho kutokea siku zijazo. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 99 | **2018/** | **Matumizi yasiyo na nyaraka** | Serikali kupitia mhasibu Mkuu | Jibu la Serikali | Pendekezo |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | **19** | **toshelezi Sh. 5,060,449,260.43** **Maafisa** Masuuli wanashauriwa pia kuimarisha udhibiti wa ndani kwenye utunzaji wa nyaraka za fedha kutoka hatua za mwanzo nyaraka zinapotengenezwa, kuhifadhiwa, kutafutwa na kuharibiwa kwa nyaraka hizo. Hivyo, hatua za kusahihisha hilo tatizo zizingatiwe kulingana na kanuni ya 24 ya Kanuni za Fedha za Umma | imetoa waraka wa uhasibu namba 6 wa 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia sheria na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma | limezingatiwa, hata hivyo maafisa wa uhasibu wanapaswa kuzingatia sheria na kanuni za serikali zaidi ya hayo uhakiki wa nyaraka zilizohojiwa mkono utafanywa ukaguzi ujao. | lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 100 | **2018/19** | Malipo yaliyofanyika bila kuidhinishwa Sh. 719,479,937.89 Ninapendekeza kwa Maafisa Masuuli husika kuhakikisha kuwa malipo yote yanaidhinishwa ipasavyo katika hatua zote na mifumo ya udhibiti wa ndani inayohusiana na uidhinishwaji wa malipo inaimarishwa ili kuiepushia Serikali hasara. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 101 | **2018/19** | **Matumizi yaliyolipwa zaidi Sh. 459,198,571.87** Kwa hiyo, Napendekeza kuwa: (a) Maafisa Masuuli waimarishe | Serikali kupitia mhasibu mkuu wa Serikali imetoa waraka wa uhasibu namba 6 wa 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli | Jibu la Serikali limezingatiwaa, hata hivyo ninasisitiza Afisa uhasibu anayehusika | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mifumo ya udhibiti wa ndani katika kuchakata malipo, (b) Kuokoa kiasi kilicholipwa Zaidi na fedha hizo kutumika kwenye matumizi kama yalivyoidhinishwa kwenye bajeti. | kuzingatia sheria na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma | kuimarisha udhibiti wa ndani juu ya mfumo wa usindikaji wa malipo na Kufanya malipo ya kiwango kilicholipwa zaidi. | |
| 102 | 2018/19 | **Udhaifu katika Usimamizi wa Masurufu Sh. 5,430,595,090.29** Ninazishauri Menejimenti za Taasisi husika kuhakikisha kuwa masurufu yanarejeshwa mara tu lengo la kutolewa fedha hizo linapokamilika na muda huo haupaswi kuzidi siku 14 za kazi. Vinginevyo, kiasi kilichosalia kikatwe kwenye mshahara au mafao mengine au kutoka kiasi kingine kutoka kwa mshika masurufu kama inavyotakiwa na Kanuni ya 103(2) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 | Serikali kupitia mhasibu mkuu wa Serikali umetoa waraka wa uhasibu namba 6 wa 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia sheria na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma | Jibu la Serikali limezingatiwa, nasisitiza maafisa wa uhasibu kuzingatia sheria ya Umma na Kanuni juu ya usimamizi wa fedha | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 103 | 2018/19 | **Kodi ya zuio ambayo haikukatwa kwenye malipo Sh. 23,501,217.63** Napendekeza kuwa menejimenti ya taasisi husika zihakikishe kodi za | Serikali kupitia mhasibu mkuu wa Serikali umetoa waraka wa uhasibu namba 6 wa 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia sheria na kanuni juu ya | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo bado ninasisitiza juu ya ulipaji wa kodi iliyosalia. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | zuio ambazo hazikukatwa zinalipwa bila kuchelewa; na kwa siku zijazo, kodi ya zuio inapaswa kukatwa ipasavyo na kuwasilishwa kwa Kamishna kama inavyotakiwa katika vifungu vya sheria iliyotajwa | uwajibikaji kwa fedha za Umma | | |
| 104 | **2018/19** | **Malipo yaliyofanyika bila kudai risiti za kielektroniki Sh. 895,372,760**<br>Kwa hiyo, napendekeza kuwa Maafisa Masuuli waache kufanya biashara na Wazabuni wasiotumia vifaa vya kielektroniki au hati za madai zilizounganishwa na Mamlaka ya Mapato na kuhakikisha kuwa kwa siku za usoni uzingatiaji wa sheria za kodi unatiliwa maanani muda wote. | Serikali kupitia mhasibu mkuu wa serikali umetoa waraka wa uhasibu namba 6 wa 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia sheria na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma | Jibu la Serikali limezingatiwa,hata hivyo bado ninasisitiza maafisa wa uhasibu kuacha kushirikiana na wasambazaji ambao wanashindwa kutoa risiti za EFD au ankara zinazohusiana na TRA na kuhakikisha kuwa katika siku zijazo sheria za kodi zinafuatwa | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 105 | **2018/19** | **Matumizi yasiyo na tija Sh. 948,931,276.65**<br>**Ninapendekeza** kwa Maafisa Masuuli husika kuweka jitihada kubwa katika kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ambayo itahakikisha kuwa Kanuni ya 21(2) | Serikali kupitia mhasibu mkuu wa Serikali umetoa waraka wa uhasibu namba 6 wa 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia sheria na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo nasisitiza maafisa wanaohusika wa uhasibu kuimarisha udhibiti wa ndani ambao utahakikisha | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inazingatiwa ipasavyo | | kufuata Sheria 21 (2) ya kanuni za fedha za Umma za 2001 | |
| 106 | **2018/19** | **Matumizi`yaliyofanyika kimakosa kwenye vifungu visivyohusika Sh. 1,807,238,083.84** **Napendekeza** kuwa Maafisa Masuuli wasiidhinishe matumizi ambayo hayaendani na bajeti iliyoidhinishwa kulingana na vifungu husika na itakapoonekana kuna ulazima, kibali kiombwe kulingana na kifungu cha 41 cha Sheria Na.11 ya Bajeti ya mwaka 2015. | Serikali kupitia mhasibu mkuu wa Serikali umetoa waraka wa uhasibu namba 6 wa 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia sheria na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo nasisitiza Maafisa Masuuli kutoidhinisha matumizi ambayo hayaingii katika bajeti iliyoidhinishwa | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 107 | **2018/19** | **Mikopo ya fedha ambayo haijarejeshwa Sh. 167,753,068** Napendekeza kuwa menejimenti husika zihakikishe fedha zilizokopwa zinarejeshwa na kutumika kwenye malengo/shughuli zilizokusudiwa | Serikali kupitia mhasibu mkuu wa Serikali umetoa waraka wa uhasibu namba 6 wa 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia sheria na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo bado ninapendekeza kuhakikisha fedha zilizokopwa zinarudishwa na zitumike kwa malengo / shughuli zilizokusudiwa | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 108 | **2018/19** | **Tozo kubwa za pango kwa ajili ya nyumba za makazi ya Balozi Sh. 1,016,202,708**<br>Napendekeza Balozi husika kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Jumuiya ya Afrika Mashariki kukarabati nyumba za makazi ili kupunguza gharama kubwa za pango na kuepuka kulipa gharama hizohizo kila mwaka wa fedha | Mikakati ya Wizara ni kupunguza gharama za uendeshaji wa balozi, wizara imetenga Sh. bilioni 20 katika bajeti ya 2020/21 kwa ujenzi, ukarabati wa uzio na nyumba za balozi. Hii itawezesha balozi kutumia nyumba za Serikali badala ya kukodisha ambayo ni ghali sana. | Jibu la Serikali limezingatiwa, nitathibitisha ukarabati katika ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 109 | **2018/19** | **Malipo yasiyo na nyaraka toshelezi katika Balozi mbalimbali Sh. 645,066,378.66**<br>Napendekeza kwa Menejimenti za Balozi husika kuimarisha udhibiti wa ndani wa utunzaji wa nyaraka za fedha kuanzia hatua za mwanzo nyaraka zinapotengenezwa, kuhifadhiwa, kutafutwa na kuharibu hizo nyaraka. Kwa hiyo, hatua za kurekebisha tatizo hili zinapaswa kufanyiwa kazi kulingana na Kanuni ya 24 ya Kanuni za Fedha za Umma. | Balozi zimeimarisha udhibiti wa ndani kulingana na kanuni za huduma za kifedha, Kwa kuhakikisha nyaraka zote zilizoombwa zinapatikana kwa ukaguzi. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo nyaraka zitathibitishwa katika ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 11 | **2018/** | **Malipo yaliyofanywa na Ubalozi** | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji | Pendekezo |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 0 | **19** | **wa Tanzania Kampala bila kibali cha muidhinishaji Sh. 70,758,790**<br>Kwa hiyo, napendekeza kwa siku zijazo malipo yote yawe na kibali kutoka kwenye mamlaka ya uidhinishaji. | | wa mapendekezo ya ukaguzi | halijatekelezwa |
| 111 | **2018/19** | Majengo yaliyotelekezwa, ukarabati usiokamilika na Viwanja visivyoendelezwa katika Sekretarieti za Mikoa na Balozi | Kwa mwaka wa fedha 2020/21,wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa imetenga Sh. 20,000,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa ofisi za balozi na nyumba za mabalozi,fensi za moroni-comoro,muscat-oman,kigali,bujumbura riyand,lilongwe,nairobi,kinshasa,washington DC | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo ukarabati utathibitishwa ukaguzi ujao | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 112 | **2018/19** | **Ubalozi wa Tanzania London Viwanja vya Balozi visivyoendelezwa**<br>Kuhusiana na changamoto iliyotajwa hapo juu, napendekeza: -<br>▫ Kuzingatia vigezo na masharti ya mkataba mara baaada ya mkataba kusainiwa ili kuzuia riba inayoweza | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuepukwa, kuchelewa kwa kazi kukamilika, kuongezeka kwa gharama za ujenzi na mazingira yasiyo salama ya kufanya kazi. Pia, nilitoa taarifa hiyo katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18 ambapo majengo saba (7) ya Ubalozi yalitelekezwa na yanahitaji ukarabati mkubwa.<br>▫ Kukarabati majengo ya Balozi za Tanzania kwa wakati kutasaidia Serikali kuepuka kodi kubwa inayolipa kwa ajili ya Ofisi pamoja na nyumba za watumishi na kupata thamani ya fedha.<br>▫ Serikali kuanzisha mipango madhubuti na endelevu ya ukarabati na ujenzi wa majengo ya Balozi zetu ambao unaweza kutekelezwa kwa awamu. Kufanya hivyo kutaisaidia Serikali kutatua changamoto za majengo zinazokabili Balozi za Tanzania. Hii ni kwa kuwa ukarabati na ujenzi unahitaji fedha nyingi ambazo haziwezi kupatikana mara moja. | | | |

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 113 | **2018/19** | **Ukosefu wa Nyaraka za Umiliki wa Ardhi na Majengo ya Umma**<br>Katika suala hili, ninaishauri Kurugenzi ya Usimamizi wa Mali za Umma iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ikishirikiana na Wiraza ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kuharakisha zoezi la taasisi za Serikali kupata Hati Miliki ya maeneo yao kutokana na umuhimu wa nyaraka zo kisheria | a) Wizara ya Fedha na Mipango imetoa Waraka wa Uhasibu namba 3 wa mwaka 2016/17 kuwaagiza maafisa masuuli wote kujumuisha ardhi na ujenzi katika Daftari la mali zao.<br>b) Wizara ya Ardhi na Makazi imetoa maagizo kwa mawaziri wote kuyapima, kuyathamini na kupata hati miliki ardhi zote zilizo chini ya wizara yao kupitia barua kumbukumbu Na. AB 225/305/01 ya Septemba, 2016<br>c) Wizara ya Fedha na Mipango inafanya uhakiki maalum wa mali zote za kudumu zinazomilikiwa na wizara, idara, Wakala, mamlaka za Serikali za mitaa na Taasisi za Serikali. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hati za umiliki ardhi na majengo ya Serikali zitathibitishwa ukaguzi ujao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 114 | **2018/19** | **Ukosefu wa Mpango wa Ukarabati wa Mali na Utunzaji wa Kumbukumbu**<br>Ninapendekeza kuwa, Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi zizingatie matakwa ya Kanuni ya 276 ya Kanuni za Fedha za Umma | Wizara ya Fedha na mipango imetoa Toleo la 2 la Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019. Sehemu ya 14 ya Mwongozo huu inaamuru Maafisa masuuli wote kuwa na mpango wa matengenezo na kuhakikisha kuwa | Jibu la Serikali limezingatiwa,hata hivyo mpango wa ukarabati wa mali na utunzaji wa kumbukumbu utahakikiwa ukaguzi | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | na Kifungu cha 11 cha Miongozo ya Mali ya mwaka 2012 kwa kuweka katika Mpangilio wa Matengenezo wa Mwaka (Annual Maintenance Plan) mali zote zinazomilikiwa/zinazotumika na taasisi. Pia, kuhakikisha kwamba matengenezo yote yanarekodiwa katika vitabu vya kumbukumbu na rejista zingine. Aidha, nasisitiza kwamba, mpango uwe unahuishwa mara matengenezo yanapokamilika. | matengenezo yanafanywa kwa mali zote zilizo chini ya ulinzi wao. | ujao. | |
| 115 | **2018/19** | **Kushindwa kufanya tathmini ya thamani (impairement tests) na muda uliobaki wa matumizi ya Mali za Kudumu**<br>Wizara na Balozi zinatakiwa kufuata matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma visivyo vya msingi wa Taslimu (IPSAS 17) na Mwongozo wa Mali za Kudumu Na.6 (3) katika kuandaa Hesabu. | Wizara ya Fedha na mipango imetoa Toleo la 2 la Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019. Sehemu ya 21 katika Mwongozo huu unaelekeza maafisa masuuli wote kukagua muda wa matumizi wa mali angalau kila mwaka wa Fedha. Idhini ya kufanya hivyo hutolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) baada ya kuombwa na maafisa masuuli. | Jibu la Serikali limezingatiwa, bado ninasisitiza kwa maafisa masuuli na Serikali kwa ujumla kuzingatia mahitaji ya IPSAS 17 inayotoa na Mwongozo wa Mali ya Serikali Namba 6 (3) katika kuandaa taarifa za kifedha. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 116 | **2018/19** | **Mali zilizonunuliwa na Nyumba zilizokamilika hazitumiki Sh.** | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya | Pendekezo halijatekelez |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **1,659,696,336**<br>Hivyo, ninapendekeza kwa menejimenti za Taasisi husika kuhakikisha kuwa kunakuwa na matumizi bora ya rasilimali fedha kwa kujenga nyumba au kununua mali zinazoendana na wakati uliopo. Aidha, Taasisi zihakikishe kuwa nyumba zilizokamilika zinatumiwa ili thamani ya fedha zilizowekezwa kwenye ujenzi iweze kupatikana | | ukaguzi | wa |
| 117 | **2018/19** | **Mapato ambayo hayajapokelewa Sh. 41,497,847,243**<br>Pia, ninapendekeza kuwa Maafisa Masuuli wenye mapato ambayo hayajakusanywa kwa zaidi ya miaka miwili kuweka bidii zaidi katika kukusanya madeni hayo kabla hayajafika hatua ya kutokusanyika na kusababisha hasara ya mapato ya Serikali | Serikali kupitia Mhasibu mkuu imetoa Waraka wa Uhasibu namba 6 wa mwaka 2019/20 ambao unawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia sheria, na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma. | Jibu la Serikali limezingatiwa, hata hivyo nasisitiza kuweka mikakati zaidi juu ya ukusanyaji wa mapato | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 118 | **2018/19** | **Usimamizi wa Madeni)**<br>**Madeni tarajiwa (Kesi ambazo hazijafanyiwa maamuzi**<br>Kuhusiana na suala hili, | Serikali kupitia Mhasibu mkuu imetoa Waraka wa Uhasibu namba 6 wa mwaka 2019/2020 ambao unawakumbusha maafisa masuuli | Jibu la Serikali limezingatiwa, nasisitiza juu ya kudhibiti hatari | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ninapendekeza kwamba athari zitokanazo na madeni tarajiwa zinapaswa kusimamiwa katika mfumo ambao uchambuzi na kipimo cha athari huunda msingi wa kuweka mkakati wa usimamizi wa athari na kubuni zana bora za kukabiliana na athari. | kuzingatia sheria na kanuni juu ya uwajibikaji kwa fedha za Umma. | zinazohusika na kesi za kisheria | |
| 119 | 2018/19 | Matumizi ambayo hayajalipwa Sh. 2,687,140,232,434<br>Kuchelewa kulipa Fidia ya Ardhi ya Mradi wa Mchuchuma na Liganga kiasi cha Sh. 11,037,183,021<br>Kwa hali hiyo, ninapendekeza malipo kwa walengwa wa fidia ya ardhi kufanywa kulingana na Sheria na Kanuni zilizotajwa hapo juu ili kuepusha gharama kuongezeka kutokana riba. Kukosa kulipa fidia sio tu kuongeza kiasi cha fidia lakini pia kunawanyima haki wanufaika kwani hawawezi kuendeleza ardhi yao. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 120 | 2018/19 | **Ukaguzi wa Vyama vya Siasa**<br>**Chanzo cha Fedha Kilichopokelewa Benki** | Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa (RPP) imeandika barua kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa | Majibu ya Serikali yamezingatiwa, hata hivyo nasisitiza | Pendekezo lipo katika hatua ya |

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **hakikubainishwa na Chama cha Wananchi (CUF)- Sh. 422,990,000** Kwa muktadha huu, ninapendekeza uongozi wa Chama cha Wananchi (CUF) kutoa stakabadhi kwenye mapato yote yanayokusanywa kutoka kwa wanachama na ruzuku inayopokelewa kutoka Serikalini au kwa wafadhili. Pia, kiasi hicho kiripotiwe kwenye taarifa za fedha za Chama. | Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum juu ya mwenendo wa jumla wa maswala ya kifedha ya Chama cha Wananchi (Civic United Front). Kwa sasa (11-06-2020) CAG anaendelea na ukaguzi. Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa (RPP) inasubiri matokeo ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hatua inayofaa itachukuliwa mara tu ukaguzi maalum utakapomalizika. | kutangaza vyanzo vya mapato katika taarifa za fedha.Hali halisi itajulikana baada ya kukamilisha ukaguzi wangu. | utekelezaji |
| 121 | 2018/19 | **Mali zinazomilikiwa na Chama cha Wananchi (CUF) hazina Usimamizi wa Kutosha** Kwa yaliyotajwa hapo juu, ninapendekeza Chama cha Wananchi (CUF) kifatilie upatikanaji wa Hatimiliki za nyumba zilizopo Zanzibar na kufanya mabadiliko kwenye taarifa za magari ili kuonesha majina ya Chama cha Wananchi (CUF). | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 122 | 2018/19 | **Mali zinazomilikiwa na Chama cha Wananchi (CUF) hazina Usimamizi wa Kutosha** | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza ufuatiliaji wa kina ufanywe na uongozi wa Chama cha Wananchi (CUF) ili mkopo tajwa urejeshwe. | | | |
| 123 | 2018/19 | **Utoaji wa Fedha wenye mashaka kwenye Akaunti ya Benki ya Chama cha Wananchi (CUF)- Sh. 416,000,000**<br>Katika suala hili, ninapendekeza mifumo ya udhibiti ya ndani ya Chama cha Wananchi (CUF) iboreshwe na uchunguzi uanzishwe ili kupata uwajibikaji wa matumizi ya Sh. 416,000,000 ambayo nyaraka zake hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 124 | 2018/19 | **Hakuna Makubaliano Kwenye Marejesho ya Mikopo iliyofanywa na Chama cha Wananchi (CUF)- Sh. 222,850,000**<br>Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza mapitio ya ujumla ya malipo yote yaliyofanyika na kama itabainika kulikuwa na malipo yasiyostahili basi kiasi | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | husika kirejeshwe | | | |
| 125 | 2018/19 | **Viwanja 5,261 vinavyomilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) Havina Hati ya Umiliki**<br>Ninapendekeza kwa uongozi wa CCM kuharakisha mchakato ili Hati hizo zipatikane kwa wakati. | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 126 | 2018/19 | **Matumizi yasiyokuwa na Tija ya Kumfidia Mpangaji aliyeondolewa na Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi kwenye Jengo alilopangishwa Pasipo kufuata Taratibu - Sh. 60,000,000**<br>Ni maoni yangu kuwa kiasi cha Sh. 60,000,000 kilicholipwa kama fidia ya hasara hakina umuhimu wowote kwa kuwa hakuna faida yoyote iliyopokelewa na Jumuiya ya Wazazi kwenye malipo yaliyofanyika. Kuhusiana na hili, ninapendekeza Jumuiya ya Wazazi (CCM) kufuata vigezo na masharti yaliyoainishwa kwenye mikataba iliyoingiwa ili kupunguza hasara ya fedha itakayosababishwa na fidia | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 12 | 2018/1 | **Ushiriki hafifu wa Chama cha CCM** | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji | Pendekezo |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | 9 | **kwenye Kampuni ya Madawa inayomilikiwa kwa ubia**<br>Kuhusu suala hili, ninapendekeza ushiriki wa karibu kwenye miradi yote inayotekelezwa na CCM. Pia, kuna haja ya mikataba yote kurejewa ili kuendana na mazingira ya kibiashara ya sasa.. | | wa mapendekezo ya ukaguzi | halijatekelezwa |
| 128 | 2018/19 | **Mradi wa Ubia ulioanzishwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) haujatekelezwa**<br>Katika hili, ninapendekeza uongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kurejea upya mkataba wa ubia uliosainiwa ili kuendana na mahitaji mapya ya uwekezaji ambao unafanywa na CCM kwa sasa | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 129 | 2018/19 | **Matumizi ambayo Hayakuidhinishwa na Halmashauri Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) - Sh.205,419,100**<br>Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza uongozi wa CHADEMA kufanya malipo kwa kufuata bajeti iliyoidhinishwa na | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Halmashauri Kuu wakati wa utekelezaji wa shughuli za Chama | | | |
| 130 | 2018/19 | **Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka Toshelezi – Sh. 2,132,906,798**<br>Kwenye suala hili, ninapendekeza mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye vyama tajwa iimarishwe ili kulinda rasilimali za chama na wanachama | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 131 | 2018/19 | **Mapato yaliyokusanywa na vyama vya siasa 10 hayajapelekwa benki- Sh. 534,844,248**<br>Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza kwa uongozi wa vyama vya siasa vilivyotajwa vitoe risiti kwenye mapato yote yatakayopokelewa na kiasi husika kiwasilishwe benki kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorekebishwa mwaka 2019). | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 132 | 2018/19 | **Taarifa za kifedha za vyama vya siasa 9 ziliandaliwa bila kufuata Mfumo wa Taarifa za Fedha unaotumika**<br>Kuhusiana na suala hili, | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ninapendekeza Vyama vya Siasa vilivyooneshwa kuandaa taarifa za kifedha kwa kutumia mfumo wa IPSAS ili kuoanisha usawa na ulinganisho wa taarifa za kifedha zinazoandaliwa na Vyama vya Siasa | | | |
| 133 | 2018/19 | **Vyama vya Siasa Vinne (4) havikuandaa Rejista ya Wanachama iliyoboreshwa**<br>**Kwa kuzingatia** hapo juu, ninapendekeza uongozi wa vyama vya siasa kuboresha rejista ya wanachama na hivyo kuendana na matakwa ya Kifungu Na.8(C) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorekebishwa mwaka 2019). | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |
| 134 | 2018/19 | **Taarifa za usuluhishi wa kibenki hazikuandaliwa na vyama vya siasa vinane (8)**<br>Kuhusu suala hili, napendekeza uongozi wa Vyama vya Siasa vilivyotajwa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kuandaa taarifa za usulushi wa benki kila mwezi ili kupunguza fursa za ubadhirifu au matumizi mabaya ya | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Pendekezo la kikaguzi | Majibu ya Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | fedha za mwanachama zilizopo benki. | | | |
| 135 | 2018/19 | **Mali zinazomilikiwa na vyama vya siasa hazikuingizwa kwenye rejista ya mali wala kuwasilishwa kwa Msajili wa vyama vya siasa** Kwa kuzingatia hili, napendekeza kwamba uongozi wa vyama vya siasa vilivyotajwa kuandaa rejista za mali; na rejista hizo zipelekwe kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, kama ilivyoelekezwa na kifungu Na.14 (1) (b) (ii) cha Sheria ya vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorekebishwa mwaka 2019). | Pendekezo halijatekelezwa | Nasisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi | Pendekezo halijatekelezwa |

## Kiambatisho Na. VI: Hali ya Utekelezwaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Maalum ya kwa Miaka Mitatu

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka 2018/19** | | | | |
| | 12.3.1 | **Ukaguzi Maalumu kuhusu mkataba Na. AE/008/2015-2016/HQ/C/3 kati ya REA na SMEC International Pty Ltd na mkataba Na. AE./008/2016-2017/HQ/G/9,10, na 11 kati ya REA na wakandarasi 29 kwenye vipengele vya utafiti na usanifu wa kina** | **Kutokana na matokeo ya ukaguzi huo maalum, nashauri kwamba:**<br>Menejimenti ya ALAT iimarishe mifumo ya Udhibiti wa Ndani. Hii ni kwa kuwa udhaifu mkubwa uliotambuliwa umetokana na kushindwa kwa mfumo wa udhibiti.<br>Uchunguzi wa kina, hatua za kisheria na za kinidhamu zinapaswa kuchukuliwa kwa maafisa hao kwa kutotimiza majukumu yao kwa ufanisi, hivyo kusababisha hasara kwa fedha za ALAT.<br>Udhibiti wa ndani kuhusiana na makusanyo ya mapato uimarishwe, na makusanyo yasiyopelekwa benki yenye thamani ya Sh. 14,330,000 yanapatikana na kuwekwa kwenye akaunti husika.<br>Mkataba ulioingiwa kati ya Menejimenti ya ALAT na M/S Vision Investment hauhuishwi upya baada ya kukamilika. Hii ni kwa kuwa, asili yake ya kuwapo si wazi. Zaidi, Menejimenti lazima ihakikishe kuwa makusanyo yasiyowasilishwa kiasi cha Sh | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | 90,000,000 na M/S Vision Investment yanarejeshwa. | |
| 1 | 12.3.1.1 | REA ilibatilisha Ripoti ya Ushauri ya SMEC katika Mchakato wa Zabuni ya Wakandarasi ishirini na tisa (29) kwa ajili ya Usambazaji wa Umeme kwenye Awamu ya Tatu ya REA (Mzunguko wa Kwanza) na kusababisha hasara ya Sh. 1,083,301,547.62 | Kwa hivyo, ninapendekeza hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya wale waliohusika kuisababishia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) hasara ya Sh. 1,083,301,547.63. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 2 | 12.3.1.2 | Wakandarasi wanne (4) wa Usambazaji wa Umeme Vijijini walilipwa Sh. 335,707,277 nje ya wigo wa kazi iliyothibitishwa kwenye mkataba wa awali na kabla ya nyongeza ya marekebisho kusainiwa | Kwa hali hii, napendekeza uongozi wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) wakati wote kutekeleza malipo kulingana na vigezo na masharti, kama ilivyoainishwa kwenye mikataba. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.3.2 | **Ukaguzi Maalumu kuhusu Mradi wa Ujenzi (jengo la ushirka) unaomilikiwa na Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) Tanzania** | | |
| 3 | 12.3.2.1 | Mapungufu kwenye usanifu wa Mradi yamesababisha gharama za nyongeza za vinyunyizi moto Sh. 999,517,100 | Kwa kuzingatia ukweli uliotajwa hapo juu, ninapendekeza uongozi wa TFC kupeleka mbele suala la uzembe wa kitaalamu uliosababishwa na ConsAfrica Limited kwa Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Ujenzi Architects (AQRB) kwa hatua stahiki za kinidhamu. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 4 | 12.3.2.2 | Uthibitisho wa kazi kwa ajili ya malipo na Mhandisi Mshauri (Consafrica Limited) ulitokana na Makisio ya Mahitaji (BOQ) bila ya Kupima Kazi halisi zilizofanyika- Sh.4,001,851,250 | Kwa kuzingatia hayo yaliyotajwa, napendekeza hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya Consafrica Limited kwa uzembe uliosababishwa wakati wa kupitisha malipo yasiyofaa kwa Kampuni ya Uhandisi na Ufundi wa China (CCECC) kwa kazi ambazo hazikufanyika na kiasi cha Sh.4,001,851,250 kirejeshwe na kampuni ya Uhandisi na Ufundi ya China (CCECC). | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 5 | 12.3.2.3 | Kazi ambazo hazijatekelezwa Licha ya Kuthibitishwa kulipwa na Mhandisi Mshauri - Sh.582,864,029 | Kwa hali hii, ninapendekeza Shirika la Uhandisi na Ufundi la China (CCECC) kurejesha kiasi cha Sh.582,864,029 kilicholipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa. Pia, hatua za kinadhamu zichukuliwe dhidi ya Mhandisi Mshauri (Cons Africa Limited) na Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji (AQRB) Ujenzi kwa uzembe uliosababishwa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 6 | 12.3.2.4 | Mkataba wa pango baina ya TFC na CRDB kwenye Jengo la Ushirika ulisainiwa bila ya kumhusisha Msajili wa Vyama vya Ushirika kama inavyotakiwa na Sheria za Vyama vya Ushirika ya mwaka 2004 na kodi ya zuio ya Sh. 288,162,453.02 haikulipwa na CRDB kwa Mamlaka ya Mapato | Ni maoni yangu kwamba CRDB kuacha kusajili makubaliano ya kukodisha pango kwa Msajili wa ardhi kunaweza kusababisha upotevu wa haki ya kumiliki pango iwapo kutatokea mgogoro wa kisheria. Pia, nina maoni kwamba Serikali imepoteza Sh. 288,162,453.02 kwa sababu benki ya CRDB haikulipa kodi ya zuio | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | Tanzania (TRA) | iliyoshikilia. Kwa kuzingatia hayo hapo juu, napendekeza uongozi wa CRDB kulipa kodi ya zuio ya Sh. 288,162,453.02 iliyoishikilia kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). | |
| | 12.3.3 | **Ukaguzi Maalumu kuhusu tuhuma zinazohusiana na matumizi mabaya ya fedha za Mfuko wa Ustawi wa watumishi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji** | | |
| 7 | 12.3.3.1 | Maofisa wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji walifanya ubadhirifu wa fedha za mafunzo zilizotolewa na NMB kwenye Mfuko wa Ustawi wa Utumishi- Sh. 66,000,000 | Nina mashaka juu ya matukio ya kula njama yaliyofanywa na Mhasibu Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Mhasibu wa Mkoa (Ilala). Vitendo vyao vimehujumu Sh.66,000,000 zilizopokelewa kutoka NMB kwa ajili ya mafunzo ya uhamasishaji zimamoto na kusababisha upotezaji mkubwa katika mfuko wa ustawi wa watumishi wa Jeshi la zimamoto na uokoaji. Katika muktadha huu, ninapendekeza hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe dhidi ya maafisa wa zimamoto na uokoaji waliohusika. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 8 | 12.3.3.2 | Fedha za ustawi zimehujumiwa na maafisa wa Zimamoto na Uokoaji kwa msingi wa Udanganyifu kwamba Wateja wameweka fedha za mafunzo kwenye akaunti ya benki ya mfuko ustawi na huku hakuna fedha zilizowekwa - Sh. 14,200,000 | Ni maoni yangu kwamba Kamishna wa fedha na utawala wa Jeshi la zimamoto na uokoaji, Mhasibu Mkuu, na Mhasibu wa Mkoa (Ilala) wamefanya mpango huu na kuiba Sh. 14,200,000 kutoka Mfuko wa Ustawi wa Kikosi cha zimamoto na uokoaji na kuathari uhai wa mfuko. Kwa msingi wa udanganyifu hapo juu, napendekeza hatua za kisheria na kinidhamu zilichukuliwe dhidi ya maafisa wote ambao wamehujumu mfuko wa ustawi kwa makusudi. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.3.4 | **Ukaguzi Maalumu kuhusu Vibali vya Kazi za Muda Mfupi vilivyotolewa kwa wageni na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu, Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere** | | |
| 9 | 12.3.4.1 | Hasara ambayo Serikali imepata kwa sababu ya Utoaji wa vibali vya kazi za muda mfupi kwa wageni (CTA) visivyo halali, na Kutofanyika kwa Maombi ya vibali maalumu na vibali vya kuishi nchini - Dola za Marekani 1,732,450 | Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza hatua za kisheria na nidhamu kuchukuliwa kwa Maafisa wote wa Uhamiaji waliohusika. Aidha, Kampuni ya Saruji ya Dangote inapaswa kufidia upotevu wa mapato ya Serikali ya jumla ya Dola za Marekani 1,666,850 kwa kushindwa kufanya maombi ya vibali maalumu na vibali vya ukaazi. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.3.5 | **Ukaguzi Maalumu kuhusu ujenzi wa bweni na ukumbi wa mihadhara** | | |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | | **kwenye Chuo cha Misitu cha Olmotonyi Arusha** | | |
| 10 | 12.3.5.1 | Malipo kwa Mkandarasi yalifanywa bila ya Upimaji Kazi halisi zilizofanyika Sh. 1,903,974,600 | Kwenye suala hili, ninapendekeza Mkandarasi (United Builders) arudishe jumla ya Sh.11,697,900 kwa kazi ambazo hazikufanywa. Pamoja na hilo, napendekeza pia Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Ujenzi (AQRB) kuchukua hatua stahiki za kinidhamu kwa Mhandisi Mshauri (Kapwani Architects) kwa kutofanya kazi kitaalamu hasa katika kuishauri Taasisi ya Mafunzo ya Misitu ya Olmotonyi, wakati wa ugawanyaji wa kazi za ujenzi kwa uwiano wa 52:48 na kwa kutoidhinisha malipo ya Sh. 1,903,974,600 kulingana na kazi halisi zilizofanywa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.3.6 | **Ukaguzi Maalumu kuhusu Mradi wa Ubia kati ya TGGA na Jafferji Developers Limited kuanzia mwaka 2010 hadi 2018** | | |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 11 | 12.3.6.1 | Mapungufu yaliyobainika kwenye Usimamizi wa Mradi wa Ubia | Kwa muktadha huu, ninapendekeza Bodi ya Wadhamini wa TGGA kumwajiri Meneja mpya wa Mradi ili kupunguza mgogoro wa maslahi uliopo kwenye usimamizi wa mradi wa ubia. Pamoja na hayo, ninapendekeza kufanyika kwa tathmini ya Mradi wa ubia ili kutambua gharama halisi ya mradi pamoja kufanya marejeo ya mkataba wa ubia ili kuweka muda wa umiliki wa mradi (concessional period). | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.3.7 | **Ukaguzi Maalumu kuhusu Matumizi ya Sh. 8,000,000 yaliyofanyika kwenye Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kipindi cha Kuanzia tarehe 1 Julai 2019 hadi tarehe 4 Novemba 2019** | | |
| 12 | 12.3.7.1 | Matumizi Mabaya ya fedha za walipakodi kwa udanganyifu kuwa gari imeharibika na kuna uhitaji wa posho ya ziada Sh. 5,380,000 | Ni maoni yangu kuwa jumla ya Sh. 5,380,000 ambayo haikurejeshwa na Afisa aliyetajwa ilitumiwa vibaya, kwani hakukuwa na maombi rasmi ya Sh.8,000,000 ambayo yalithibitishwa wakati wa ukaguzi wangu. Katika suala hili, ninapendekeza hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya Afisa aliyetajwa, na jumla ya Sh. 5,380,000 iliyotumiwa vibaya irejeshwe. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 13 | 12.3.7.2 | Mapungufu yaliyojitokeza kwenye matumizi yaliyofanyika wakati wa ziara maalumu ya Naibu Waziri kwenye Mikoa ya Mwanza na Simiyu - Sh.43,856,000 | Katika muktadha huu, ninapendekeza mifumo ya udhibiti wa ndani iliopo Ofisi ya Rais menejimenti ya utumushi wa umma (POPSM) kuboreshwa. Pamoja na hilo, ninapendekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa madereva wanne (4) kwa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kusimamia mafuta, na afisa aliyetajwa anapaswa kurudisha jumla ya sh.1,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vipeperushi ambavyo havikununuliwa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 14 | 12.3.7.3 | Mapungufu Yaliyobainka kwenye Malipo yaliyolipwa kutoka kwenye fedha za matumizi ya kawaida (OC) kuanzia Julai 2019 hadi Novemba 2019 | Ni maoni yangu kwamba, mifumo ya udhibiti wa ndani katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (POPSM) ni dhaifu. Kwa hivyo, kuna hatari ya fedha za walipakodi kutumiwa vibaya kila mara. Katika hali hii, ninapendekeza maboresho makubwa ya mifumo ya udhibiti wa ndani katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (POPSM). Sanjari na hii, ninapendekeza hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya Kaimu Mhasibu Mkuu, na kiasi cha Sh.4,300,000 ambacho hakikutumika kinastahili kurejeshwa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 12.3.8 | **Ukaguzi Maalumu uliofanyika kwa Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2018** | | |
| 15 | 12.3.8.1 | Mapungufu yaliyobainika wakati wa Usimamizi wa Matumizi, Mapato, Ununuzi na Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2018 | Katika suala hili, ninapendekeza mapitio makubwa ya mifumo ya udhibiti wa ndani katika Ofisi ya Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA). Pamoja na hayo, ninapendekeza kurejeshwa kwa Sh.16,990,300 na maafisa wanne (4) waliotajwa ambao hawakuhudhuria mafunzo nchini Uganda. Uchunguzi unapaswa kuanzishwa kwa wafanyakazi waliopoteza vitabu vya mapato kumi na viwili (12) na kusababisha Ofisi ya Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) kutokusanya mapato iliyotarajia | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| **Mwaka 2017/18** | | | | |
| | 12.2.1 | **Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Mfumo wa Kidijitali wa Kusajili Wapiga Kura (BVR) uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)** | | |
| 16 | 12.2.1.1 | Mfumo wa kidijitali wa kusajili Wapiga kura (BVR) wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Haukuunganishwa na BVR za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) na Malipo | Kuhusiana na suala hili, naishauri Serikali kuongeza usimamizi wa mikataba kwa ukaribu ili kupunguza matatizo yatokanayo na ubadhirifu na matumizi mabaya ya rasimali za umma. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | yasiyokuwa na tija ya manunuzi ya leseni za windows na biometric algorithms kiasi cha Sh.862,085,100 | | |
| 17 | 12.2.1.2 | Malipo zaidi kwa Mzabuni ya jumla ya Dola za Marekani 148,243.73 | Nashauri fedha zaidi zilizolipwa kwa Mzabuni zirejeshwe, na hatua kali za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa Maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) walioshirikiana na Mzabuni kupora Mali za Umma. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 18 | 12.2.1.3 | Malipo ya Mafunzo ambayo hayakufanyika ya Jumla ya Dola za Marekani 358,650 | Kuhusiana na hili, nashauri Mzabuni arejeshe kiasi tajwa. Aidha, hatua za Kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa Maafisa wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) waliohusika kufanya malipo bila mafunzo kufanyika. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.2.2 | **Ukaguzi Maalum Kuhusu ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS ) uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania** | | |
| 19 | 12.2.2.1 | Vigezo vya Kiufundi zilivyoandaliwa na Mtumiaji Mfumo wa utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) Havikuzingatiwa wakati wa Tathmini ya Zabuni | Kuhusiana na suala hili, nashauri manunuzi mapya yote kufuata mahitaji kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu 39(1)(b)-(d) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 ili kuweza kupata thamani halisi ya fedha. Pia, nasisitiza mamlaka husika zichukue hatua stahiki kwa maofisa wote waliohusika. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20 | 12.2.2.2 | Vifaa vya aina Moja vyenye Sifa na Uwezo unaolingana vilitozwa Bei Tofauti na Kusababisha Mzabuni Kulipwa zaidi ya Sh.556,647,610 | Nashauri hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa maafisa wote wa Jeshi la Polisi waliosababishia Serikali hasara ya jumla ya Sh.556,647,610. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 21 | 12.2.2.3 | Zabuni yenye Kumb Na. ME.014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 kwa ajili ya Ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) ilitolewa kwa Mzabuni Asiyekuwa na Sifa. | Kwa mantiki hii, nashauri vigezo vilivyowekwa kwenye Zabuni vitumike wakati wote wa tathmini, uidhinishaji na utoaji wa Zabuni kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2013. Nasisitiza wajumbe wa Kamati za Tathmini za Zabuni kuwa huru na kutumia weledi wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yao. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 22 | 12.2.2.4 | Manunuzi ya Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole Hayakuwa Kwenye Bajeti ya Jeshi la Polisi | Kuhusiana na hili, nashauri matumizi yote yatokane na bajeti iliyopitishwa na kuidhinishwa na bunge; na uhamisho wowote ufuate taratibu zilizoainishwa kwenye kifungu Na. 41 cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 23 | 12.2.2.5 | Kutofungwa Kwa Vifaa Vya Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) Vya Gharama Ya Sh.1,736,056,030.45 Kwenye Magereza 35 | Nashauri vifaa hivi kufungwa kwenye Magereza 35 yaliyoainishwa bila kuchelewa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 24 | 12.2.2.6 | Mafunzo kwa Wataalamu 30 wa Mfumo Yaliyogharimu Sh.604,390,244 Hayakufanyika | Kwa mantiki hii, nashauri Mzabuni Lugumi Enterprises Limited ama akamilishe mafunzo ya wataalumu 30 au arudishe gharama za mafunzo alizolipwa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 25 | 12.2.2.7 | "Monitor" 58 Aina ya L2250p zenye ukubwa wa inchi 22 na zenye thamani Ya Sh.159,166,100 Hazikuonekana Wakati wa Ukaguzi | Kuhusiana na suala hili, napendekeza hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa maafisa wote wa Ofisi ya Upelelezi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi walioshindwa kutunza "monitor'' 58 aina ya Dell optiplex modeli L2250P yenye ukubwa wa inchi 22. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 26 | 12.2.2.8 | Malipo ya Huduma ambayo Haikufanyika Sh.3,304,000,000 | Hivyo, nashauri huduma ya matengenezo na uwezeshaji ikamilishwe na Mzabuni Lugumi Enterprises Limited kwenye mikoa yote ishirini na sita (26) kama ilivyoelekezwa kwenye maktaba. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 27 | 12.2.2.9 | Malipo ya Monitor 213 Aina ya Dell yenye Ukubwa wa Inchi 22 (Modeli L2250P 22 Wide Hybrid 0282 TCO-5.0 1680X105075HZ) zenye Gharama ya Sh.431,658,635 ambazo Hazikuletwa | Kuhusiana na suala hili, nashauri Jeshi la Polisi kutopokea Monitors 213 ambazo hazina matumizi yoyote kwenye Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole. Hivyo, Lugumi Enterprises Limited arejeshe kiasi cha Sh.195,221,282 kilicholipwa zaidi. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.2.3 | **Ukaguzi Maalum wa Tuhuma za Ubadhirifu wa Fedha za Umma wakati wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe uliofanywa na Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege (TAA)** | | |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 28 | 12.2.3.1 | Malipo ya Shughuli za Ujenzi ambazo Hazikuidhinishwa na Mhandisi Mshauri ya Sh. 5,482,610,339.86 na Malipo yenye Udanganyifu ya Sh.570,508,125 | Kuhusiana na suala hili, napendekeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kuanzisha uchunguzi kwenye Hati za Malipo Na. 10 na 03 kabla ya kukabidhiwa kwa Mradi na urejeshaji wa pesa zilizoshikiliwa kwa matazamio (Retention money) kwa Mkandarasi. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 29 | 12.2.3.2 | Kutorejeshwa kwa Malipo ya Awali ya Kuanzisha Shughuli za Ujenzi Sh.1,528,200,879.98 | Kuhusiana na hili, nashauri mwajiri (TAA) kurejesha kiasi husika kwenye Hati za Madai ambazo Mkandarasi hajalipwa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 30 | 12.2.3.3 | Malipo kwa Mkandarasi ambayo Hakustahili Sh.3,383,387,095 | Kuhusiana na suala hili, nashauri Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD arejeshe kiasi cha jumla ya Sh.3,383,387,095 ambazo hakustahili kulipwa, ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria kwa Maafisa wote wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.2.4 | **Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Sare za Polisi uliofanywa na Jeshi la Polisi** | | |
| 31 | 12.2.4.1 | Maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Hayakuzingatiwa | Hivyo, nashauri Jeshi la Polisi mara zote kufanya manunuzi kwa kuzingatia sheria, ikiwa ni pamoja na kujumuisha maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mara baada ya kuhakiki rasimu za mikataba. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 32 | 12.2.4.2 | Malipo ya Sare za Polisi ambazo Hazikuletwa Kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi Sh.16,660,000,000 | Kuhusu suala hili, nashauri Mzabuni Daissy General Traders arejeshe kiasi alicholipwa kwa kutoleta Sare za Polisi na hatua stahiki za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa Maofisa wote wa Jeshi la Polisi kwa kuisababishia Serikali hasara. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.2.5 | **Ukaguzi Maalum wa Masurufu Katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na.52) na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 98)** | | |
| 33 | 12.2.5.1 | Masurufu ambayo Hayajarejeshwa Sh.245,194,247.8 | Hivyo, napendekeza Maafisa Masuuli wa Wizara zilizotajwa kuhakikisha kuwa masurufu ambayo hayajarejeshwa yakatwe kwenye mishahara ya Watumishi husika kama ilivyoelekezwa na Kanuni 103(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 34 | 12.2.5.2 | Masurufu yalitolewa kwa Shughuli ambazo Hazikuwa kwenye Bajeti Sh. 32,529,895 | Kuhusiana na suala hili, nashauri Afisa Masuuli (Fungu Na. 43) kutoa masurufu kwenye matumizi ambayo yamebajetiwa na kuhakikisha masurufu ya mradi wa ERPP yanarejeshwa | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 35 | 12.2.5.3 | Masurufu ambayo Yameshughulikiwa nje ya Mfumo wa “Epicor Imprest Module” Sh.11,756,128,459.71 | Nashauri Maafisa Masuuli wote kushughulikia masurufu yote ndani ya mfumo wa “Epicor Imprest Module” ili kuwe na thamani halisi ya fedha ya ununuzi wa mfumo wa ‘‘Epicor” | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 36 | 12.2.5.4 | Masurufu yaliyorejeshwa ambayo yana Nyaraka Pungufu au yasiyokuwa na Nyaraka Sh. 3,282,748,190.42 | Kuhusiana na suala hili, nashauri Afisa Masuuli kuwawajibisha Maafisa wote ambao wamerejesha masurufu yenye nyaraka pungufu, na wale ambao wamepoteza nyaraka za masurufu. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| | 12.2.6 | **Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Magari 777 aina ya Ashok Leyland uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania** | | |
| 37 | 12.2.6.1 | Mapugufu yaliyojitokeza kwenye ununuzi wa magari 777 aina ya Ashok Leyland yenye thamani ya Dola za Marekani 29,606,100 | Kwa suala hili, napendekeza magari 22 yenye thamani ya Dola za Marekani 572,506 yaliyopatikana na kasoro na kukataliwa na Jeshi la Polisi yabadilishwe. Magari 280 yenye thamani ya Dola za Marekani 6,759,648 na vipuri vya thamani ya Dola za Marekani 5,510,429 viletwe mara moja ili kuepuka ongezeka la gharama za kujitolea (commitment charges) za mkopo wa Dola za Marekani 13,477,570,30 ambao haujatumika. Ninahimiza Serikali daima kuchambua mikopo yote kwa ufanisi na kuachana na mikopo yenye masharti ya kibiashara ambayo inaonekana kuwa ya gharama kubwa. Zaidi, ninahimiza Kamati za Usimamizi wa Madeni za Kitaifa kufanya kazi kitaalum na kutekeleza taratibu zote kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | mikopo ya Serikali, Dhamana na Ruzuku ya Mwaka 1974 (marekebisho ya mwaka 2003) na Kanuni zake. | |
| | 12.2.7 | **Ukaguzi Maalum Kuhusiana na Tuhuma za Matumizi Mabaya ya Marejesho ya Mikopo Katika Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) Tawi la Morogoro** | | |
| 38 | 12.2.7.1 | Matumizi mabaya ya Fedha Wakati wa Kulipa Marejesho ya Mikopo ya Jumla ya Sh.67,489,000 | Namshauri Katibu Mkuu Kiongozi kuhakikisha kuwa Uongozi wa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) unasimamia kikamilifu urejeshaji wa fedha kiasi cha Sh.67,489,000. Pia, achukue hatua stahiki za kisheria kwa Watumishi husika | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 39 | 12.2.7.2 | Mikopo Iliyotolewa Isiyothibitika Kupokelewa na Walengwa Sh.2,500,000 | Ninapendekeza Menejimenti ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) kupitia mfumo wake wa uendeshaji kwa mtazamo wa kudhibiti uwezekano wa matumizi mabaya ya mikopo. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
| 40 | 12.2.7.3 | Risiti za Malipo ya Marejesho Zilizopatikana kwa Wakopaji Zisizoainishwa Katika Kumbukumbu za Malipo ya Marejesho ya Mfuko wa Rais wa kujitegemea (TPF) Kiasi cha Sh.76,560,550 | Ninapendekeza Katibu Mkuu Kiongozi kuhakikisha kwamba, kiasi hicho kilichotumika isivyostahili kinarudishwa na hatua stahiki zinachukuliwa. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Aya | Kichwa cha habari | Mapendekezo | Hali ya utekelezaji |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| 41 | 12.2.7.4 | Udanganyifu kwa Kutumia Nyaraka za Wanachama wa Kikundi cha Mkopo Katika Maombi ya Mkopo Sh.15,000,000 | Ninapendekeza Katibu Mkuu Kiongozi kuhakikisha kuwa Uongozi wa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) unasimamia urejeshaji wa mkopo wa Sh.20,062,500 na kuchukua hatua stahiki kwa waliohusika katika udanganyifu. | Pendekezo lipo katika hatua ya utekelezaji |
